MAFUNDISHO NA MAAGANO

MAFUNDISHO NA MAAGANO

YA KANISA LA YESU KRISTO LA WATAKATIFU WA SIKU ZA MWISHO

YENYE MAFUNUO YALIYOTOLEWA
KWA NABII, JOSEPH SMITH

PAMOJA NA NYONGEZA ZILIZOTOLEWA
KWA WARITHI WAKE
KATIKA URAIS WA KANISA

YALIYOMO

Utangulizi v
Utaratibu wa Wendo. x
Sehemu 1
Matamko Rasmi 359

UTANGULIZI

Mafundisho na Maagano ni mkusanyiko wa mafunuo matakatifu na maazimio ya kuongozwa na Mungu yaliyotolewa kwa ajili ya kuanzisha na kusimamia ufalme wa Mungu hapa duniani katika siku hizi za mwisho. Ingawa kwa sehemu kubwa yamelengwa kwa waumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, ujumbe, maonyo, na ushawishi ni kwa faida ya wanadamu wote na hufanya mwaliko kwa wanadamu wote kila mahali kuisikiliza sauti ya Bwana Yesu Kristo, ikisema nao kwa ajili ya ustawi wao wa kimwili na wokovu wao usio na mwisho.

Sehemu kubwa ya mafunuo katika mkusanyiko huu yalipokelewa kupitia Joseph Smith Mdogo, nabii wa kwanza, na rais wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Mengine yalitolewa kupitia baadhi ya warithi wake katika Urais (ona vichwa vya habari vya M&M 135, 136, na 138, na Matamko Rasmi 1 na 2).

Kitabu cha Mafundisho na Maagano ni moja ya Vitabu Vitakatifu vya Kanisa kwa pamoja na Biblia Takatifu, Kitabu cha Mormoni, na Lulu ya Thamani Kuu. Hata hivyo, Mafundisho na Maagano ni cha kipekee kwa sababu siyo tafsiri ya waraka wa kale, bali ni cha asili ya kisasa na kimetolewa na Mungu kupitia manabii Wake watende kwa ajili ya urejesho wa kazi Yake takatifu na kwa uanzishaji wa ufalme wa Mungu humu duniani katika siku hizi. Katika mafunuo, mtu husikia sauti ya upole lakini iliyo imara ya Bwana Yesu Kristo; akisema upya katika kipindi cha utimilifu wa nyakati; na kazi ambayo imeanzishwa ndani yake ni matayarisho kwa Ujio Wake wa pili, katika utimilifu na ulinganifu wa maneno ya manabii wote watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu.

Joseph Smith Mdogo alizaliwa 23 Desemba 1805, huko Sharon, Wilaya ya Windsor, Vermont. Wakati wa maisha yake ya mwanzoni, yeye pamoja na familia yake walihamia Manchester, magharibi ya New York kama ijulikanavyo hii leo. Ilikuwa wakati alipokuwa akiishi huko katika majira ya kuchipua ya mwaka 1820, alipokuwa na umri wa miaka kumi na minne, kwamba alipata ono lake la kwanza, katika ono hilo alitembelewa na Mungu, Baba wa Milele, na Mwanawe Yesu Kristo. Alielezwa katika ono hili kwamba Kanisa la kweli la Yesu Kristo ambalo lilianzishwa nyakati za Agano Jipya, na ambalo lilifundisha utimilifu wa injili, halikuwepo tena duniani. Maono mengine matakatifu yalifuata ambamo malaika wengi walimfundisha; ilioneshwa kwake kwamba Mungu alikuwa na kazi muhimu ya yeye kuifanya hapa duniani, na kwamba kupitia yeye Kanisa la Yesu Kristo litarejeshwa duniani.

Baada ya muda, Joseph Smith aliwezeshwa kwa msaada mtakatifu kutafsiri na kuchapisha Kitabu cha Mormoni. Wakati huu yeye na

Oliver Cowdery walitawazwa katika Ukuhani wa Haruni na Yohana Mbatizaji mnamo Mei 1829 (ona M&M 13), na muda mfupi baadaye pia walitawazwa kwenye Ukuhani wa Melkizedeki na Mitume wa zamani Petro, Yakobo, na Yohana (ona M&M 27:12). Kutawazwa kwingine kulifuatia ambako funguo za ukuhani zilitolewa na Musa, Eliya, Elia, na manabii wengi wa kale (ona M&M 110; 128:18, 21). Kutawazwa huku kulikuwa, kwa kweli, ni urejesho wa mamlaka takatifu kwa mwanadamu duniani. Mnamo 6 Aprili 1830, chini ya maelekezo ya mbingu, Nabii Joseph Smith alilianzisha Kanisa, na hivyo Kanisa la kweli la Yesu Kristo kwa mara nyingine tena likifanya kazi kama taasisi miongoni mwa wanadamu, likiwa na mamlaka ya kufundisha injili na kutoa ibada za wokovu. (Ona M&M 20 na Lulu ya Thamani Kuu, Joseph Smith—Historia ya 1.)

Mafunuo haya matakatifu yalikuwa yakipokelewa kama majibu ya sala, wakati wa shida, na zilijitokeza katika hali halisi za maisha zikiwahusisha watu halisi. Nabii na washirika wake walitafuta mwongozo mtakatifu, na funuo hizi zilithibitisha kwamba walipokea. Katika mafunuo, mtu huona urejesho na kufichuliwa kwa injili ya Yesu Kristo na kuingia kwa kipindi cha utimilifu wa nyakati. Kuhama kwa Kanisa kutoka New York na Pennsylvania kwenda Ohio, kwenda Missouri, kwenda Illinois, na hatimaye Bonde Kuu la Marekani ya magharibi na jitihada kubwa za Watakatifu katika kujaribu kujenga Sayuni hapa duniani katika nyakati za kisasa pia hujitokeza katika mafunuo haya.

Sehemu kadhaa za mwanzo zinahusiana na mambo yanayohusu tafsiri na uchapishaji wa Kitabu cha Mormoni (ona sehemu ya 3, 5, 10, 17, na 19). Baadhi ya sehemu za mwishoni zinaonyesha kazi ya Nabii Joseph Smith katika kufanya tafsiri ya Biblia, kipindi ambacho sehemu za mafundisho muhimu zilipokelewa (ona, kwa mfano, sehemu ya 37, 45, 73, 76, 77, 86, 91, na 132, ambazo kila moja ina uhusiano wa moja kwa moja na tafsiri ya Biblia).

Katika mafunuo, mafundisho ya injili yanatangazwa pamoja na maelezo juu ya mambo muhimu kama vile asili ya Uungu, mwanzo wa mwanadamu, ukweli juu ya kuwepo kwa Shetani, madhumuni ya kuishi hapa duniani, umuhimu wa utii, haja ya toba, utendaji kazi wa Roho Mtakatifu, ibada na matendo yanayohusiana na wokovu, hatima ya dunia, hali ya baadaye ya mwanadamu baada ya Ufufuko na Hukumu, umilele wa uhusiano wa ndoa, na asili ya milele ya familia. Vivyo hivyo, kufunuliwa pole pole kwa muundo wa usimamizi wa Kanisa unaonyeshwa kwa njia ya kuitwa kwa maaskofu, Urais wa Kwanza, Baraza la Mitume Kumi na Wawili, na Sabini, na kuanzishwa kwa ofisi simamizi zingine za uongozi na akidi. Mwishoni, ushuhuda ambao unatolewa juu ya Yesu Kristo—uungu Wake, utukufu Wake, ukamilifu Wake, upendo Wake, na uwezo Wake wa kukomboa—hufanya kitabu hiki kuwa cha thamani kubwa kwa familia

ya mwanadamu na kuwa cha "thamani kwa Kanisa kuliko utajiri wa dunia yote" (ona kichwa cha habari kwa M&M 70).

Mafunuo haya awali yaliandikwa na waandishi wa Joseph Smith, na waumini wa Kanisa kwa shauku walishirikiana nakala za kuandikwa kwa mkono. Ili kutengeneza kumbukumbu ya kudumu, waandishi mara moja wakanakili mafunuo haya katika mswada kama kitabu cha kumbukumbu, ambacho viongozi wa Kanisa walikitumia katika kuyatayarisha mafunuo haya ili yapigwe chapa. Joseph Smith na watakatifu wa mwanzoni waliyaangalia mafunuo haya kama vile walivyokuwa wakiliangalia Kanisa: yenye uhai, yenye nguvu, na yanayoweza kuboreshwa kwa nyongeza ya ufunuo. Pia walitambua kwamba makosa yasiyo kusudiwa yawezekana kuwa yametokea katika mchakato wa kunakili mafunuo na kuyatayarishwa kwa uchapishaji. Kwa sababu hiyo, mkutano wa Kanisa ulimwomba Joseph Smith katika mwaka 1831 "kusahihisha upotofu au makosa hayo ambayo yawezekana akayagundua kwa njia ya Roho Mtakatifu".

Baada ya mafunuo haya kufanyiwa marejeo na kusahihishwa, waumini wa Kanisa katika Missouri wakaanza kupiga chapa kitabu kilichoitwa *A Book of Commandments for the Government of the Church of Christ* (Kitabu cha Amri kwa ajili ya Kuongoza Kanisa la Kristo), ambacho kilikuwa na mafunuo mengi ya awali ya Nabii. Hata hivyo, jaribio hili la kwanza la kuchapisha mafunuo lilikwama, wakati kikundi cha wahuni kilipoharibu ofisi ya Watakatifu ya kupiga chapa huko Wilaya ya Jackson mnamo 20 Julai 1833.

Baada ya kusikia juu ya uharibifu wa ofisi ya kupiga chapa huko Missouri, Joseph Smith na viongozi wengine wa Kanisa wakaanza maandalizi ya kuchapisha mafunuo haya huko Kirtland, Ohio. Ili tena kusahihisha makosa, na ufafanuzi wa maneno, na kwa kutambua maendeleo katika Kanisa mafundisho na muundo, Joseph Smith alisimamia kazi ya kuhariri maneno ya baadhi ya mafunuo ili kuyaandaa kwa ajili ya uchapaji katika mwaka wa 1835 kama *Doctrine and Covenants of the Church of the Latter Day Saints* (Mafundisho na Maagano ya Kanisa la Watakatifu wa Siku za Mwisho). Joseph Smith aliidhinisha toleo jingine la Mafundisho na Maagano, ambalo lilichapishwa miezi michache tu baada ya kifo cha kishahidi cha Nabii mwaka 1844.

Watakatifu wa Siku za Mwisho wa mwanzoni kabisa waliyathamini mafunuo haya na kuyatazama kama vile ni ujumbe kutoka kwa Mungu. Katika tukio moja mwishoni mwa mwaka 1831, wazee kadhaa wa Kanisa walitoa ushuhuda wa dhati kwamba Bwana amezishuhudia nafsi zao juu ya ukweli wa mafunuo hayo. Ushuhuda huu ulichapishwa katika toleo la mwaka 1835 la Mafundisho na Maagano kama ushuhuda wa kimaandishi wa Mitume Kumi na Wawili:

USHUHUDA WA MITUME KUMI NA WAWILI JUU YA UKWELI WA KITABU CHA MAFUNDISHO NA MAAGANO

Ushuhuda wa Mashahidi juu ya Kitabu cha Amri za Bwana, amri ambazo alizitoa kwa Kanisa lake kupitia Joseph Smith, Mdogo, ambaye aliteuliwa kwa sauti ya Kanisa kwa dhumuni hili:

Kwa hiyo, sisi, tupo radhi kutoa ushuhuda kwa ulimwengu wa wanadamu wote, kwa kila kiumbe kilicho juu ya uso wa dunia, kwamba Bwana ametushuhudia nafsini mwetu, kupitia Roho Mtakatifu aliyemwagwa juu yetu, kwamba amri hizi zilitolewa kwa maongozi ya Mungu, na ni kwa manufaa ya watu wote na amini ni za kweli.

Sisi tunatoa ushuhuda huu kwa ulimwengu, Bwana akiwa msaidizi wetu; na ni kwa neema za Mungu Baba, na Mwana Wake, Yesu Kristo, kwamba sisi tumeruhusiwa kupata nafasi hii ya kutoa ushuhuda huu kwa ulimwengu, nafasi ambayo tunaifurahia kupita kiasi, tukimwomba Bwana daima kwamba kwa hicho wanadamu waweze kufaidika.

Majina ya Mitume Kumi na Wawili yalikuwa:

Thomas B. Marsh	Orson Hyde	William Smith
David W. Patten	William E. McLellin	Orson Pratt
Brigham Young	Parley P. Pratt	John F. Boynton
Heber C. Kimball	Luke S. Johnson	Lyman E. Johnson

Katika mfululizo wa matoleo ya Mafundisho na Maagano, mafunuo ya nyongeza au mambo mengine muhimu yameongezwa, kama yalivyopokelewa, na kama yalivyo kubaliwa na mikusanyiko au mikutano yenye mamlaka ya Kanisa. Toleo la 1876, lililo tayarishwa na Mzee Orson Pratt chini ya maelekezo ya Bringham Young, akiyapanga mafunuo katika utaratibu wa wendo na kuyapa upya vichwa vya habari pamoja na utangulizi wa kihistoria.

Kuanzia toleo la mwaka 1835, mfululizo wa masomo saba ya teolojia pia yaliingizwa ndani; haya yalipewa jina la *Lectures on Faith* (Mihadhara juu ya Imani). Haya yalikuwa yametayarishwa kwa matumizi katika Shule ya Manabii huko Kirtland, Ohio, kutoka mwaka 1834 hadi 1835. Ingawa ni ya manufaa kwa ajili ya mafundisho na maelekezo, mihadhara hii imeondolewa kutoka kwenye Mafundisho na Maagano tangu toleo la mwaka 1921 kwa sababu hayakuwa yametolewa kama mafunuo kwa Kanisa zima.

Katika toleo la mwaka wa 1981 la Kiingereza la Mafundisho na Maagano, nyaraka tatu ziliingizwa kwa mara ya kwanza. Hizi ni sehemu ya sehemu ya 137 na 138, zikiweka misingi ya wokovu kwa ajili ya wafu; na Tamko Rasmi 2, linalotangaza kwamba waumini

wa Kanisa wanaume wote wenye kustahili wanaweza kutawazwa kwenye ukuhani bila kujali asili au rangi.

Kila toleo jipya la Mafundisho na Maagano limesahihisha makosa yaliyopita na kuongeza taarifa mpya, hususani katika eneo la vichwa vya habari vya sehemu. Toleo la sasa linaboresha zaidi tarehe na majina ya mahali na kufanya masahihisho mengine. Mabadiliko haya yamefanyika ili kuleta taarifa hizi katika ulinganifu na taarifa za kihistoria zilizo sahihi zaidi. Sehemu nyingine muhimu za toleo hili la mwisho ni pamoja na ramani zilizo sahihishwa zikionyesha maeneo muhimu kijiografia ambako mafunuo haya yalipokelewa, pamoja na picha iliyoboreshwa ya picha iliyoboreshwa ya maeneo ya kihistoria katika Kanisa, marejeo, vichwa vya habari vya sehemu, na ufupisho wa mada, yote yakiwa yameundwa ili kumsaidia msomajikuelewa na kufurahia katika ujumbe wa Bwana kama ulivyotolewa katika Mafundisho na Maagano. Taarifa kwa ajili ya vichwa vya habari vya sehemu zimechukuliwa kutoka kwenye Muswada wa Historia ya Kanisa na *History of the Church* (Historia ya Kanisa) iliyochapishwa (kwa pamoja zimeitwa katika vichwa vya habari kama historia ya Joseph Smith) na *Joseph Smith Papers* (Karatasi za Joseph Smith).

UTARATIBU WA WENDO WA YALIYOMO

Tarehe		*Mahali*	*Sehemu*
1823	Septemba	Manchester, New York	2
1828	Julai	Harmony, Pennsylvania	3
1829	Februari	Harmony, Pennsylvania	4
	Machi	Harmony, Pennsylvania	5
	Aprili	Harmony, Pennsylvania	6, 7, 8, 9, 10
	Mei	Harmony, Pennsylvania	11, 12, 13*
	Juni	Fayette, New York	14, 15, 16, 17, 18
	Kiangazi	Manchester, New York	19
1830		Wilaya ya Wayne, New York	74
	Aprili	Fayette, New York	20*, 21
	Aprili	Manchester, New York	22, 23
	Julai	Harmony, Pennsylvania	24, 25, 26
	Agosti	Harmony, Pennsylvania	27
	Septemba	Fayette, New York	28, 29, 30, 31
	Oktoba	Manchester, New York	32
	Oktoba	Fayette, New York	33
	Novemba	Fayette, New York	34
	Desemba	Fayette, New York	35*, 36*, 37*
1831	Januari	Fayette, New York	38, 39, 40
	Februari	Kirtland, Ohio	41, 42, 43, 44
	Machi	Kirtland, Ohio	45, 46, 47, 48
	Mei	Kirtland, Ohio	49, 50
	Mei	Thompson, Ohio	51
	Juni	Kirtland, Ohio	52, 53, 54, 55, 56
	Julai	Sayuni, Wilaya ya Jackson, Missouri	57
	Agosti	Sayuni, Wilaya ya Jackson, Missouri	58, 59
	Agosti	Independence, Missouri	60
	Agosti	Mto Missouri, Missouri	61
	Agosti	Chariton, Missouri	62
	Agosti	Kirtland, Ohio	63
	Septemba	Kirtland, Ohio	64
	Oktoba	Hiram, Ohio	65, 66
	Novemba	Hiram, Ohio	1, 67, 68, 69, 70, 133
	Desemba	Hiram, Ohio	71
	Desemba	Kirtland, Ohio	72
1832	Januari	Hiram, Ohio	73
	Januari	Amherst, Ohio	75
	Februari	Hiram, Ohio	76
	Machi	Hiram, Ohio	77, 79, 80, 81

***Hapo au karibu na mahali palipotajwa**

Tarehe		*Mahali*	*Sehemu*
	Machi	Kirtland, Ohio	78
	Aprili	Independence, Missouri	82, 83
	Agosti	Hiram, Ohio	99
	Septemba	Kirtland, Ohio	84
	Novemba	Kirtland, Ohio	85
	Desemba	Kirtland, Ohio	86, 87*, 88
1833	Februari	Kirtland, Ohio	89
	Machi	Kirtland, Ohio	90, 91, 92
	Mei	Kirtland, Ohio	93
	Juni	Kirtland, Ohio	95, 96
	Agosti	Kirtland, Ohio	94, 97, 98
	Oktoba	Perrysburg, New York	100
	Desemba	Kirtland, Ohio	101
1834	Februari	Kirtland, Ohio	102, 103
	Aprili	Kirtland, Ohio	104*
	Juni	Mto Fishing, Missouri	105
	Novemba	Kirtland, Ohio	106
1835	Aprili	Kirtland, Ohio	107
	Agosti	Kirtland, Ohio	134
	Desemba	Kirtland, Ohio	108
1836	Januari	Kirtland, Ohio	137
	Machi	Kirtland, Ohio	109
	Aprili	Kirtland, Ohio	110
	Agosti	Salem, Massachusetts	111
1837	Julai	Kirtland, Ohio	112
1838	Machi	Far West, Missouri	113*
	Aprili	Far West, Missouri	114, 115
	Mei	Spring Hill, Wilaya ya Daviess, Missouri	116
	Julai	Far West, Missouri	117, 118, 119, 120
1839	Machi	Gereza la Liberty, Wilaya ya Clay, Missouri	121, 122, 123
1841	Januari	Nauvoo, Illinois	124
	Machi	Nauvoo, Illinois	125
	Julai	Nauvoo, Illinois	126
1842	Septemba	Nauvoo, Illinois	127, 128
1843	Februari	Nauvoo, Illinois	129
	Aprili	Ramus, Illinois	130
	Mei	Ramus, Illinois	131
	Julai	Nauvoo, Illinois	132
1844	Juni	Nauvoo, Illinois	135
1847	Januari	Winter Quarters (sasa Nebraska)	136
1890	Oktoba	Jiji la Salt Lake, Utah	Tamko Rasmi 1
1918	Oktoba	Jiji la Salt Lake, Utah	138
1978	Juni	Jiji la Salt Lake, Utah	Tamko Rasmi 2

MAFUNDISHO NA MAAGANO

SEHEMU YA 1

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, 1 Novemba 1831, wakati wa mkutano maalumu wa wazee wa Kanisa, uliofanyika Hiram, Ohio. Mafunuo mengi yalikuwa yamekwisha pokelewa kutoka kwa Bwana kabla ya wakati huu, na ukusanyaji kwa ajili ya uchapishaji katika muundo wa kitabu ni moja ya mambo muhimu yaliyopitishwa katika mkutano huo. Sehemu hii inafanya utangulizi wa Bwana wa mafundisho, maagano, na amri alizozitoa katika kipindi hiki.

1–7, Sauti ya onyo ni kwa watu wote; 8–16, Ukengeufu na uovu utatangulia Ujio wa Pili; 17–23, Joseph Smith ameitwa kurejesha duniani ukweli na uwezo wa Bwana; 24–33, Kitabu cha Mormoni kinafichuliwa na Kanisa la kweli linaanzishwa; 34–36, Amani itaondolewa duniani; 37–39, Zichunguzeni amri hizi.

SIKILIZENI, Enyi watu wa [a]kanisa langu, yasema sauti ya yeye akaaye juu, na ambaye [b]macho yake yako juu ya watu wote; ndiyo, amini ninawaambia: [c]Sikilizeni enyi watu wa kutoka mbali; nanyi mlio juu ya visiwa vya bahari, sikilizeni kwa pamoja.

2 Kwani hakika [a]sauti ya Bwana ni kwa watu wote, na [b]hakuna atakayeepuka; na hakuna jicho ambalo halitaona, wala sikio ambalo halitasikia, wala [c]moyo ambao hautapenywa.

3 Na [a]waasi watachomwa kwa uchungu mwingi; kwani uovu wao [b]utasemwa juu ya paa za nyumba, na matendo yao ya siri yatafichuliwa.

4 Na [a]sauti ya onyo itakuwa kwa watu wote, kwa vinywa vya wanafunzi wangu, ambao nimewachagua katika [b]siku hizi za mwisho.

5 Nao watasonga mbele wala hakuna wa kuwazuia, kwani Mimi Bwana nimewaamuru.

6 Tazama, hii ni [a]mamlaka yangu, na ni mamlaka ya watumishi wangu, na ni utangulizi wa

1 1*a* 3 Ne. 27:3; M&M 20:1. MWM Kanisa la Yesu Kristo.
b M&M 38:7–8. MWM Mungu, Uungu.
c Kum. 32:1.
2*a* M&M 133:16.
b Flp. 2:9–11.
c MWM Moyo.
3*a* MWM Uasi.
b Lk. 8:17; 12:3; 2 Ne. 27:11; Morm. 5:8.
4*a* Eze. 3:17–21; M&M 63:37. MWM Kazi ya kimisionari; Onya, Onyo.
b MWM Siku za Mwisho.
6*a* MWM Yesu Kristo—Mamlaka.

kitabu cha amri zangu, ambazo nimewapa wao [b]kuchapisha kwa ajili yenu, Enyi wakazi wa dunia.

7 Hivyo basi, [a]ogopeni na tetemekeni, Enyi watu, kwani Mimi Bwana niliyoagiza ndani yake [b]yatakamilika.

8 Na amini ninawaambia ninyi, kwamba wao waendeleao mbele, wakitangaza habari hizi kwa wakazi wa dunia, kwao uwezo umetolewa wa [a]kufunga kote duniani na mbinguni, wale wasioamini na [b]waasi;

9 Ndiyo, amini, kuwafungia wao hadi siku ile wakati [a]ghadhabu ya Mungu itakapomwagwa juu ya [b]waovu pasipo kipimo—

10 Hadi [a]siku ile wakati Bwana atakapokuja [b]kumlipa kila mtu kulingana na [c]matendo yake, na [d]kumpimia kila mtu kulingana na kipimo alichowapimia wanadamu wenzake.

11 Kwa hiyo sauti ya Bwana ni hata miisho ya dunia, kwamba wale wote watakaosikia na wasikie:

12 Jitayarisheni, jitayarisheni kwa lile ambalo laja, kwani Bwana yu karibu;

13 Na [a]hasira ya Bwana inawaka, na [b]upanga wake unaoshwa mbinguni, nao utawashukia wakazi wa dunia.

14 Na [a]mkono wa Bwana utafunuliwa; na siku yaja kwamba wale ambao [b]hawataisikia sauti ya Bwana, wala sauti ya watumishi wake, wala [c]kutii maneno ya manabii na mitume, [d]watakatiliwa mbali kutoka miongoni mwa watu;

15 Kwani [a]wamepotoka kutoka kwenye [b]ibada zangu, na [c]wamevunja [d]agano langu lisilo na mwisho;

16 [a]Hawamtakii Bwana kuendeleza haki zake, bali kila mtu huenenda katika [b]njia zake [c]mwenyewe, na akifuata [d]mfano wa mungu wake mwenyewe, ambaye ni mfano wa kitu cha duniani, na wa sanamu ya kuchonga, ambayo mali ghafi yake [e]huzeeka na kuangamia katika [f]Babiloni, hata Babiloni ile kuu, ambayo itaanguka.

17 Hivyo basi, Mimi Bwana, nikijua majanga yajayo juu ya [a]wakazi wa dunia, nimemwita mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na kusema naye kutoka

6 *b* M&M 72:21.
7 *a* Kum. 5:29; Mh. 12:13.
b M&M 1:38.
8 *a* MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
b MWM Uasi.
9 *a* Ufu. 19:15–16; 1 Ne. 22:16–17.
b Mos. 16:2; JS—M 1:31, 55.
10 *a* MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b Eze. 7:4; M&M 56:19. MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.
c Mit. 24:12; Alma 9:28; 41:2–5; M&M 6:33.
d Mt. 7:2.
13 *a* M&M 63:6.
b Eze. 21:3; M&M 35:14.
14 *a* Isa. 53:1.
b 2 Ne. 9:31; Mos. 26:28.
c M&M 11:2.
d Mdo. 3:23; Alma 50:20; M&M 50:8; 56:3.
15 *a* Yos. 23:16; Isa. 24:5.
b MWM Ibada.
c MWM Ukengeufu.
d MWM Agano Jipya na Lisilo na Mwisho.
16 *a* Mt. 6:33.
b Isa. 53:6.
c M&M 82:6.
d Ku. 20:4; 3 Ne. 21:17. MWM Kuabudu sanamu.
e Isa. 50:9.
f M&M 64:24; 133:14. MWM Babeli, Babilonia; Malimwengu.
17 *a* Isa. 24:1–6.

mbinguni, na nikampa yeye amri;

18 Na pia nikawapa amri wengine, kwamba yawalazimu kuyatangaza mambo haya duniani; na haya yote kwamba yapate kukamilika yale yaliyoandikwa na manabii—

19 Mambo [a]dhaifu ya dunia yatakuja kuyavunja yale yaliyo makubwa na yenye nguvu, kwamba mwanadamu asimshauri mwanadamu mwenzake, wala [b]asiutegemee mkono wa mwanadamu—

20 Bali kwamba kila mwanadamu aweze [a]kuongea katika jina la Mungu Bwana, hata Mwokozi wa ulimwengu;

21 Kwamba imani pia ipate kuongezeka katika dunia;

22 Kwamba [a]agano langu lisilo na mwisho liweze kuanzishwa;

23 Kwamba utimilifu wa [a]injili yangu uweze [b]kutangazwa na watu walio [c]dhaifu na wa kawaida hata mwisho wa dunia, na mbele ya wafalme na watawala.

24 Tazama, Mimi ni Mungu; na nimeyasema haya; [a]amri hizi ni zangu, na zilitolewa kwa watumishi wangu katika udhaifu wao, kwa namna ya [b]lugha yao, kwamba wapate [c]kuelewa.

25 Na hata wakikosea iweze kujulikana;

26 Na kadiri watakavyoitafuta [a]hekima waweze kuelekezwa;

27 Na kadiri walivyotenda dhambi waweze [a]kukemewa, ili waweze [b]kutubu;

28 Na kadiri walivyokuwa [a]wanyenyekevu waweze kufanywa imara, na kubarikiwa kutoka juu na kupokea [b]maarifa mara kwa mara.

29 Baada ya kupokea kumbukumbu ya Wanefi, ndiyo, hata, mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, kupata uwezo wa kutafsiri, Kitabu cha Mormoni, kwa rehema ya Mungu, na kwa uwezo wa Mungu, [a]Kitabu cha Mormoni.

30 Na pia kwa wale ambao amri hizi zimetolewa, waweze kupata [a]uwezo wa kuweka msingi wa [b]kanisa hili, na kulitoa kutoka lisikoonekana na kutoka [c]gizani, [d]kanisa pekee la kweli na lililo hai katika uso wa dunia yote, ambalo Mimi, Bwana, [e]napendezwa nalo, nikizungumza na kanisa kwa ujumla na siyo mmoja mmoja—

19 *a* Mdo. 4:13; 1 Kor. 1:27; M&M 35:13; 133:58–59. MWM Pole, Upole.
b 2 Ne. 28:31. MWM Tegemea.
20 *a* MWM Shuhudia.
22 *a* M&M 39:11. MWM Agano; Agano Jipya na Lisilo na Mwisho.
23 *a* MWM Injili.
b MWM Kazi ya kimisionari.
c 1 Kor. 1:26–29.
24 *a* 2 Ne. 33:10–11; Moro. 10:27–28.
b 2 Ne. 31:3; Eth. 12:39.
c M&M 50:12. MWM Ufahamu.
26 *a* Yak. (Bib.) 1:5; M&M 42:68. MWM Hekima.
27 *a* MWM Rudi, Kurudiwa.
b MWM Toba, Tubu.
28 *a* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
b MWM Maarifa.
29 *a* MWM Kitabu cha Mormoni.
30 *a* M&M 1:4–5, 17–18.
b MWM Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho; Urejesho wa Injili.
c MWM Giza, Kiroho.
d Efe. 4:5, 11–14. MWM Kanisa, Ishara za Kanisa la Kweli.
e M&M 38:10.

31 Kwani Mimi Bwana siwezi kuiangalia [a]dhambi na kuivumilia hata kidogo;

32 Hata hivyo, yeye anayetubu na kutimiza amri za Bwana huyo [a]atasamehewa;

33 Na yeye ambaye [a]hatubu, kutoka kwake [b]itachukuliwa hata ile nuru aliyoipokea; kwani [c]Roho yangu [d]haitashindana daima na mwanadamu, asema Bwana wa Majeshi.

34 Na tena, amini ninawaambia, Enyi wakazi wa dunia: Mimi Bwana ni radhi kufanya mambo haya yajulikane kwa watu [a]wote;

35 Kwani [a]siwapendelei watu, na ninataka watu wote waje kwamba [b]siku ile yaja haraka; saa ingali, lakini i karibu, wakati [c]amani itakapoondolewa duniani, na [d]ibilisi atakuwa na uwezo juu ya utawala wake mwenyewe.

36 Na pia Bwana atakuwa na uwezo juu ya [a]watakatifu wake, naye [b]atatawala [c]katikati yao, na atashuka chini kwa [d]hukumu juu ya [e]Idumaya, au ulimwengu.

37 Zichunguzeni [a]amri hizi, kwani ni za kweli na za kuaminika, na unabii na [b]ahadi zilizomo ndani yake zote zitatimilizwa.

38 Kile ambacho Mimi Bwana nimesema, nimekisema, na wala sijutii, na ingawa mbingu na dunia zitapita, [a]neno langu halitapita kamwe, bali [b]litatimia, iwe kwa [c]sauti yangu mwenyewe au kwa sauti ya [d]watumishi wangu, yote ni [e]sawa.

39 Kwani tazama, na lo, Bwana ni Mungu, na [a]Roho hushuhudia, na ushuhuda wake ni wa kweli, na [b]ukweli hudumu milele na milele. Amina.

SEHEMU YA 2

Dondoo kutoka katika historia ya Joseph Smith kuhusiana na maneno ya malaika Moroni kwa Joseph Smith Nabii, wakiwa ndani ya

31 *a* Alma 45:16; M&M 24:2. MWM Dhambi.
32 *a* M&M 58:42–43. MWM Samehe.
33 *a* Mos. 26:32.
b Alma 24:30; M&M 60:2–3.
c MWM Roho Mtakatifu.
d Mwa. 6:3; 2 Ne. 26:11; Morm. 5:16; Eth. 2:15; Moro. 9:4.
34 *a* Mt. 28:19; M&M 1:2; 42:58.
35 *a* Kum. 10:17; Mdo. 10:34; Moro. 8:12; M&M 38:16.
b MWM Siku za Mwisho.
c M&M 87:1–2. MWM Amani; Ishara za Nyakati.
d MWM Ibilisi.
36 *a* MWM Mtakatifu.
b MWM Yesu Kristo—Utawala wa Kristo katika milenia.
c Zek. 2:10–11; M&M 29:11; 84:118–119.
d MWM Amua, Hukumu.
e MWM Ulimwengu.
37 *a* MWM Maandiko.
b M&M 58:31; 62:6; 82:10.
38 *a* 2 Fal. 10:10; Mt. 5:18; 24:35; 2 Ne. 9:16; JS—M 1:35.
b M&M 101:64.
c Kum. 18:18; M&M 18:33–38; 21:5. MWM Sauti; Ufunuo.
d MWM Nabii.
e MWM Kuwakubali Viongozi wa Kanisa; Mamlaka.
39 *a* 1 Yoh. 5:6; M&M 20:27; 42:17.
b MWM Ukweli.

nyumba ya baba yake Nabii huko Manchester, New York, jioni ya 21 Septemba 1823. Moroni alikuwa wa mwisho katika safu ndefu ya wanahistoria ambao walitengeneza kumbukumbu ambayo sasa iko mbele ya ulimwengu kama Kitabu cha Mormoni. (Linganisha na Malaki 4:5–6; pia sehemu ya 27:9; 110:13–16; na 128:18.)

1, Eliya ataufunua ukuhani; 2–3, Ahadi za baba zapandikizwa katika mioyo ya watoto.

Tazama, nitaufunua kwenu Ukuhani, kwa mkono wa [a]Eliya, nabii, kabla ya kuja kwa siku ile [b]kuu na ya kutisha ya Bwana.

2 [a]Naye atapandikiza katika mioyo ya watoto [b]ahadi zilizofanywa kwa baba, na mioyo ya watoto itawageukia baba zao.

3 Kama si hivyo, dunia yote ingeliangamia kabisa wakati wa kuja kwake.

SEHEMU YA 3

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, huko Harmony, Pennsylvania, Julai 1828, kuhusiana na upotevu wa kurasa 116 za muswada ulio tafsiriwa kutoka sehemu ya kwanza ya Kitabu cha Mormoni, ambacho kiliitwa kitabu cha Lehi. Nabii huku akisita aliruhusu kurasa hizi kutoka mikononi mwake na kwenda katika mikono ya Martin Harris, ambaye alitumika kwa kipindi kifupi kama mwandishi katika tafsiri ya Kitabu cha Mormoni. Ufunuo huu ulitolewa kupitia Urimu na Thumimu. (Ona sehemu ya 10.)

1–4, Mwelekeo wa Bwana ni imara milele; 5–15, Joseph Smith lazima atubu au atapoteza kipawa cha kutafsiri; 16–20, Kitabu cha Mormoni kimekuja kwa ajili ya kuokoa uzao wa Lehi.

[a]Kazi, na mipango, na malengo ya Mungu hayawezi kubatilishwa, wala hayawezi kuwa kazi bure.

2 Kwani [a]Mungu haenendi katika njia zisizo nyoofu, wala hageuki mkono wa kulia wala wa kushoto, wala habadilishi kauli kutoka ile aliyosema, hivyo njia zake ni nyoofu, na [b]mwelekeo wake ni imara milele.

3 Kumbuka, kumbuka kwamba siyo [a]kazi ya Mungu ambayo hubatilika, bali ni kazi ya wanadamu;

2 1*a* Mal. 4:5–6; 3 Ne. 25:5–6; M&M 110:13–15; 128:17; JS—H 1:38–39. mwm Eliya; Funguo za Ukuhani.
b M&M 34:6–9; 43:17–26.
2*a* M&M 27:9; 98:16–17.
b mwm Kufunga, Muhuri, Tia; Wokovu kwa ajili ya Wafu.
3 1*a* Zab. 8:3–9; M&M 10:43.
2*a* Alma 7:20. mwm Mungu, Uungu.
b 1 Ne. 10:18–19; M&M 35:1.
3*a* Mdo. 5:38–39; Morm. 8:22; M&M 10:43.

4 Kwani ingawa mwanadamu aweza kupata mafunuo mengi, na kuwa na uwezo wa kufanya matendo mengi na makubwa, lakini kama [a]atajivuna katika nguvu zake, na kupuuza [b]ushauri wa Mungu, na kufuata mwongozo wa matakwa yake mwenyewe na tamaa za [c]kimwili, lazima ataanguka, na kujiletea mwenyewe [d]kisasi cha Mungu wa haki juu yake.

5 Tazama, umeaminiwa juu ya mambo haya, lakini ni kali namna gani amri zako; na kumbuka pia ahadi ambazo zimewekwa kwako, kama hungezivunja.

6 Na tazama, ni mara ngapi [a]umezivunja amri na sheria za Mungu, na ukafuata [b]ushawishi wa wanadamu.

7 Kwani, tazama, haungepaswa [a]kumwogopa mwanadamu zaidi kuliko Mungu. Ingawa wanadamu hudharau ushauri wa Mungu, na [b]kuyapuuza maneno yake—

8 Lakini wewe ungelipaswa kuwa mwaminifu; na yeye angelikunyooshea mkono wake na kukutegemeza dhidi ya [a]mishale ya moto ya [b]adui; na yeye angelikuwa pamoja na wewe katika wakati wote wa [c]matatizo.

9 Tazama, wewe ndiwe Joseph, na wewe uliteuliwa kuifanya kazi ya Bwana, lakini kwa sababu ya uvunjaji wa sheria, kama hautakuwa mwangalifu, na wewe utaanguka.

10 Lakini kumbuka, Mungu ni mwenye rehema; hivyo basi, tubu kwa lile ambalo umelifanya ambalo ni kinyume cha amri ambazo nilikupa, na wewe bado u mteule, na wewe tena umeitwa kuifanya kazi;

11 Usipofanya haya, nawe utatolewa na kuwa kama watu wengine, na usiwe na kipawa zaidi.

12 Na wakati wewe ulipokitoa kile ambacho Mungu alikupa wewe kuona na uwezo wa [a]kutafsiri, wewe ukakitoa kile ambacho kilikuwa kitakatifu na kukiweka katika mikono ya [b]mtu mwovu,

13 Ambaye ameyapuuza mashauri ya Mungu, na kuvunja ahadi takatifu zilizofanywa mbele za Mungu, na yeye akategemea zaidi maamuzi yake binafsi na [a]kujivuna katika hekima yake mwenyewe.

14 Na hii ndiyo sababu ya kwamba wewe umepoteza heshima yako kwa muda—

15 Kwani wewe umeruhusu ushauri wa [a]mkurugenzi wako ukanyagwe kutoka mwanzoni.

4*a* M&M 84:73. MWM Kiburi.
b Yak. (KM) 4:10; Alma 37:37. MWM Amri za Mungu; Ushauri.
c MWM Tamaa za kimwili.
d MWM Kisasi.
6*a* M&M 5:21; JS—H 1:28–29.
b M&M 45:29; 46:7.
7*a* Zab. 27:1; Lk. 9:26; M&M 122:9. MWM Hofu; Ushujaa, enye Ushujaa.
b Law. 26:42–43; 1 Ne. 19:7; Yak. (KM) 4:8–10.
8*a* Efe. 6:16; 1 Ne. 15:24; M&M 27:17.
b MWM Ibilisi.
c Alma 38:5.
12*a* M&M 1:29; 5:4.
b M&M 10:6–8.
13*a* MWM Kiburi.
15*a* MY Bwana.

16 Hata hivyo, kazi yangu itaendelea mbele, kwani kadiri ufahamu wa [a]Mwokozi ulivyokuja duniani, kupitia kwa [b]ushuhuda wa Wayahudi, hivyo ndivyo [c]ufahamu wa Mwokozi utakavyokuja kwa watu wangu—

17 Na kwa [a]Wanefi, na Wayakobo, na Wayusufu, na Wazoramu, kupitia ushuhuda wa baba zao—

18 Na [a]ushuhuda huu utakuja kujulikana kwa [b]Walamani, na Walemueli, na Waishmaeli, ambao [c]walififia katika kutokuamini kwa sababu ya uovu wa baba zao, ambao Bwana alikubali [d]wawaangamize ndugu zao Wanefi, kwa sababu ya maovu yao na machukizo yao.

19 Na ni kwa [a]sababu hii [b]mabamba haya yalihifadhiwa, ambayo yana kumbukumbu hizi—kwamba [c]ahadi za Bwana ziweze kutimilika, ambazo alizifanya kwa watu wake;

20 Na kwamba [a]Walamani waweze kuja katika ufahamu wa baba zao, na kwamba waweze kujua ahadi za Bwana, na kwamba waweze [b]kuamini injili na [c]kutegemea fadhili za Yesu Kristo, na [d]kutukuzwa kwa njia ya imani katika jina lake, na kwamba kwa njia ya toba yao waweze kuokolewa. Amina.

SEHEMU YA 4

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa baba yake Joseph Smith Mkubwa, huko Harmony, Pennsylvania, Februari 1829.

1–4, Utumishi wa kishujaa huwaokoa wahudumu wa Bwana; 5–6, Sifa ya uchamungu huwapasisha wao kwenye huduma; 7, Mambo ya Mungu ni lazima yatafutwe.

Sasa tazama, [a]kazi ya ajabu karibu yaja miongoni mwa wanadamu.

2 Hivyo basi, ninyi nyote ambao mnaingia katika [a]utumishi wa Mungu, angalieni kwamba [b]mnamtumikia yeye kwa [c]moyo wenu wote, uwezo, akili na nguvu zenu zote, kwamba muweze kusimama pasipo [d]lawama mbele za Mungu siku ile ya mwisho.

16 *a* mwm Mwokozi.
b 1 Ne. 13:23–25; 2 Ne. 29:4–6.
c Mos. 3:20.
17 *a* 2 Ne. 5:8–9.
18 *a* mwm Kitabu cha Mormoni.
b 2 Ne. 5:14; Eno. 1:13–18.
c 2 Ne. 26:15–16.
d Morm. 8:2–3.
19 *a* 1 Ne. 9:3, 5.
b mwm Mabamba ya Dhahabu.
c 3 Ne. 5:14–15; M&M 10:46–50.
20 *a* 2 Ne. 30:3–6; M&M 28:8; 49:24.
b Morm. 3:19–21.
c 2 Ne. 31:19; Moro. 6:4.
d Moro. 7:26, 38.
4 1 *a* Isa. 29:14; 1 Ne. 14:7; 22:8; M&M 6:1; 18:44. mwm Urejesho wa Injili.
2 *a* mwm Utumishi.
b Yos. 22:5; 1 Sam. 7:3; M&M 20:19; 76:5.
c mwm Moyo; Nia.
d 1 Kor. 1:8; Yak. (KM) 1:19; 3 Ne. 27:20.

3 Kwa hivyo, kama unayo tamaa ya kumtumikia Mungu wewe [a]umeitwa kwenye kazi hiyo;

4 Kwani tazama [a]shamba ni jeupe tayari kwa [b]mavuno; na lo, yeye aingizaye mundu yake kwa nguvu, ndiye huyo huyo ajiwekeaye [c]ghalani akiba ili asiangamie, bali ajiletee wokovu kwa nafsi yake;

5 Na [a]imani, [b]tumaini, [c]hisani na [d]upendo, na [e]jicho lake likiwa kwenye [f]utukufu wa Mungu pekee, humpasisha mtu huyo katika kazi.

6 Kumbuka imani, [a]wema, maarifa, kiasi, [b]uvumilivu, upendano wa kindugu, uchamungu, hisani, [c]unyenyekevu, [d]jitihada.

7 [a]Omba, nawe utapata; bisha, nawe utafunguliwa. Amina.

SEHEMU YA 5

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Harmony, Pennsylvania, Machi 1829, kwa maombi ya Martin Harris.

1–10, Kizazi hiki kitapokea neno la Bwana kupitia Joseph Smith; 11–18, Mashahidi watatu watakishuhudia Kitabu cha Mormoni; 19–20, Neno la Bwana litadhihirishwa kama katika nyakati zilizopita; 21–35, Martin Harris aweza kutubu na kuwa mmoja wa mashahidi hao.

Tazama, ninakuambia wewe, kwamba kama vile mtumishi wangu [a]Martin Harris alivyotaka ushahidi kutoka kwangu, kwamba wewe, mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, unayo [b]mabamba, ambayo umeyashuhudia na umeshuhudia kwamba umeyapata kwangu;

2 Na sasa, tazama, hili ndilo utakalomwambia yeye—yule aliyesema nawe, alikuambia: Mimi, Bwana, ndiye Mungu, na nimekupa mambo haya wewe, mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na nimekuamuru wewe kwamba usimame kama [a]shahidi wa mambo haya;

3 Na nimekusababisha wewe kwamba uingie katika agano na Mimi, kwamba yakupasa

3*a* M&M 11:4, 15; 36:5; 63:57. MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito.
4*a* Yn. 4:35; Alma 26:3–5; M&M 11:3; 33:3, 7.
b MWM Mavuno.
c 1 Tim. 6:19.
5*a* MWM Amini, Imani.
b MWM Tumaini.
c MWM Hisani.
d MWM Upendo.
e Zab. 141:8; Mt. 6:22; Morm. 8:15.
f MWM Utukufu.
6*a* MWM Wema.
b MWM Subira.
c MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
d MWM Bidii.
7*a* Mt. 7:7–8; 2 Ne. 32:4. MWM Sala.
5 1*a* M&M 5:23–24; JS—H 1:61.
b MWM Mabamba ya Dhahabu.
2*a* MWM Shahidi, Ushahidi.

usiyaonyeshe, ila kwa [a]watu wale tu ambao nimekuamuru, na wala huna [b]uwezo juu yake ila ninapokupa.

4 Na unacho kipawa cha kutafsiri mabamba haya; na hiki ni kipawa cha kwanza nilichokupa; na nimekuamuru kwamba usidai kipawa kingine chochote mpaka makusudi yangu yatakapotimilika katika hili; kwani sitakupatia kipawa kingine mpaka itakapomalizika.

5 Amini, ninakuambia wewe, kwamba huzuni itawajia wakazi wa dunia kama [a]hawatasikiliza maneno yangu;

6 Kwani baada ya hapa [a]utatawazwa na kuanza kuyaeneza [b]maneno yangu kwa wanadamu.

7 Tazama, kama [a]hawatayaamini maneno yangu, hawatakuamini wewe, mtumishi wangu Joseph, hata kama ingewezekana kwamba uwaonyeshe mambo haya yote ambayo nimeyakabidhi kwako.

8 O, hiki kizazi [a]kisichoamini na cha wenye [b]shingo ngumu—hasira yangu inawaka juu yao.

9 Tazama, amini ninakuambia wewe, [a]nimeyahifadhi mambo haya ambayo nimeyaaminisha mikononi mwako, mtumishi wangu Joseph, kwa kusudi la hekima yangu, na itajulikana katika vizazi vijavyo;

10 Lakini kizazi hiki kitapata neno langu kupitia kwako;

11 Na kwa nyongeza juu ya ushuhuda wako, [a]ushuhuda wa watumishi wangu watatu, ambao nitawaita na kuwatawaza, ambao kwa hao nitayaonyesha mambo haya, nao watakwenda na maneno yangu ambayo yatatolewa kupitia kwako.

12 Ndiyo, wao watajua kwa uhakika kwamba mambo haya ni ya kweli, kwani kutoka mbinguni nitawatangazia.

13 Nitawapa wao uwezo kwamba waweze kuyatazama na kuyaona mambo haya kama yalivyo;

14 Na [a]sitatoa uwezo huu kwa mtu mwingine awaye yeyote, kupokea ushuhuda wa aina hii miongoni mwa watu wa kizazi hiki, katika huu mwanzo wa kuinuka na kuchomoza kwa [b]kanisa langu kutoka nyikani—wazi kama [c]mbalamwezi, na angavu kama jua, na la kutisha kama jeshi lenye bendera.

15 Na kwa ushuhuda wa [a]mashahidi watatu nitalieneza neno langu.

16 Na tazama, wale wote

3 *a* 2 Ne. 27:13. Tazama pia "Ushuhuda wan Mashahidi Watatu" na "Ushuhuda wa Mashahidi Wanane" katika kurasa tangulizi za Kitabu cha Mormoni.
b 2 Ne. 3:11.
5 *a* Yer. 26:4–5; Alma 5:37–38; M&M 1:14.
6 *a* M&M 20:2–3. MWM Kutawaza, Kutawazwa.
b 2 Ne. 29:7.
7 *a* Lk. 16:27–31; M&M 63:7–12.
8 *a* MWM Kutoamini.
b Morm. 8:33. MWM Kiburi.
9 *a* Alma 37:18.
11 *a* 2 Ne. 27:12; Eth. 5:3–4; M&M 17:1–5.
14 *a* 2 Ne. 27:13.
b MWM Kanisa la Yesu Kristo; Urejesho wa Injili.
c M&M 105:31; 109:73.
15 *a* M&M 17. MWM Mashahidi wa Kitabu cha Mormoni.

[a]watakaoamini juu ya maneno yangu, hao [b]nitawajia kwa [c]ufunuo wa [d]Roho wangu; nao [e]watazaliwa kwangu, hata kwa maji na kwa Roho—

17 Na lazima usubiri kitambo kidogo, kwani bado [a]haujatawazwa—

18 Na ushuhuda wao pia utaenea kama [a]hukumu kwa kizazi hiki kama wataishupaza mioyo yao dhidi yao;

19 Kwani [a]pigo la ukiwa litapita miongoni mwa wakazi wa ulimwengu, nalo litazidi kuminwa kutoka wakati hadi wakati, kama [b]hawatatubu, mpaka dunia itakuwa [c]tupu, na wakazi wake wameteketezwa na wameangamizwa kabisa kwa mng'aro wa [d]kuja kwangu.

20 Tazama, ninakuambia mambo haya, kama vile [a]nilivyowaambia watu juu ya kuangamia kwa Yerusalemu; na [b]neno langu litadhihirika wakati huu kama lilivyodhihirika hapo awali.

21 Na sasa ninakuamuru wewe, mtumishi wangu Joseph, kutubu na kutembea wima zaidi mbele zangu, na wala usishawishiwe tena na wanadamu;

22 Na ya kwamba uwe imara katika [a]kushika amri ambazo nimekuamuru wewe; na kama utayafanya haya, tazama nitakupa uzima wa milele, hata kama [b]utauawa.

23 Na sasa, tena, ninakuambia wewe, mtumishi wangu Joseph, kuhusu [a]mtu huyo autakaye ushahidi—

24 Tazama, ninamwambia yeye, anajikweza yeye mwenyewe na wala hajinyenyekezi vya kutosha mbele zangu; ila kama atainama mbele yangu, na kujinyenyekeza mwenyewe katika sala ya nguvu na imani, katika dhamira thabiti ya moyo wake, ndipo nitampa yeye [a]kuyaona mambo anayotamani kuyaona.

25 Na ndipo atasema kwa watu wa kizazi hiki: Tazama, nimeyaona mambo ambayo Bwana ameyaonyesha kwa Joseph Smith, Mdogo. Na [a]ninajua kwa hakika kuwa ni ya kweli, kwani nimeyaona, na yameonyeshwa kwangu kwa nguvu za Mungu na wala siyo kwa nguvu za mwanadamu.

26 Na Mimi Bwana, ninamwamuru yeye, mtumishi wangu Martin Harris, kwamba hatasema tena kwao kuhusu mambo haya, bali atasema: Nimeyaona,

16*a* Eth. 4:11.
b 1 Ne. 2:16.
c M&M 8:1–3.
d MWM Roho Mtakatifu.
e MWM Batiza, Ubatizo; Kipawa cha Roho Mtakatifu; Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.

17*a* MWM Kutawaza, Kutawazwa; Mamlaka.

18*a* 1 Ne. 14:7; M&M 20:13–15.

19*a* M&M 29:8; 35:11; 43:17–27. MWM Ishara za Nyakati; Siku za Mwisho.
b MWM Toba, Tubu.
c Isa. 24:1, 5–6.
d Isa. 66:15–16; M&M 133:41. MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.

20*a* 1 Ne. 1:18; 2 Ne. 25:9.
b M&M 1:38.

22*a* MWM Mtiifu, Tii, Utii.
b Alma 60:13; M&M 6:30; 135.

23*a* M&M 5:1.

24*a* Tazama "Ushuhuda wa Mashahidi Watatu" katika kurasa tangulizi za Kitabu cha Mormoni.

25*a* Eth. 5:3.

na kwamba yameonyeshwa kwangu kwa nguvu za Mungu; na haya ndiyo maneno atakayosema.

27 Lakini kama atayakana haya atavunja agano ambalo ameagana na Mimi, na tazama, amelaaniwa.

28 Na sasa, kama hakujinyenyekeza mwenyewe, na kukiri kwangu mambo ambayo ameyafanya siyo sahihi, na kuagana na Mimi kwamba atazishika amri zangu, na kuwa na imani nami, tazama, ninamwambia yeye, hatapata kuyaona, kwani sitampa yeye kuona mambo haya ambayo nimeyazungumza.

29 Na kama hivyo ndivyo ilivyo, ninakuamuru wewe, mtumishi wangu Joseph, kwamba utamwambia yeye, kwamba asifanye zaidi, wala asinisumbue tena juu ya jambo hili.

30 Na kama hivyo ndivyo ilivyo, tazama, ninakuambia wewe Joseph, wakati wewe utakapokuwa umetafsiri kurasa nyingine chache na usimame kwa kipindi, hadi nitakapokuamuru tena; ndipo waweza kutafsiri tena.

31 Na endapo hautafanya haya, tazama, wewe hutakuwa na kipawa tena, na nitachukua kutoka kwako mambo ambayo nimekuaminisha wewe.

32 Na sasa, kwa sababu ninawaotea watu wenye hila wanaovizia kukuangamiza, ndiyo, ninaotea kwamba, kama mtumishi wangu Martin Harris hajinyenyekezi mwenyewe na akapokea ushuhuda kutoka mkononi mwangu, kwamba ataanguka katika uvunjaji wa sheria;

33 Na kuna wengi wanaovizia kwa hila [a]kukuangamiza wewe kutoka katika uso wa dunia; na kwa sababu hiyo, kwamba siku zako zitaongezwa, nimekupa wewe amri hizi.

34 Ndiyo, kwa sababu hii, nimesema: Simama, na ubaki hivyo mpaka nitakapokuamuru, na [a]nitakupa njia ambazo wewe waweza kumalizia mambo haya niliyokuamuru.

35 Na kama wewe utakuwa [a]mwaminifu katika kuzishika amri zangu, na wewe [b]utainuliwa juu siku ile ya mwisho. Amina.

SEHEMU YA 6

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Oliver Cowdery, huko Harmony, Pennsylvania, Aprili 1829. Oliver Cowdery alianza kazi yake ya uandishi katika tafsiri ya Kitabu cha Mormoni, 7 Aprili 1829. Alikuwa tayari amekwisha pokea ufunuo mtakatifu wa ukweli wa ushuhuda wa Nabii kuhusiana na mabamba ambayo juu yake

33 *a* M&M 10:6; 38:13, 28.
34 *a* 1 Ne. 3:7.
35 *a* Ku. 15:26; M&M 11:20.
b Yn. 6:39–40; 1 The. 4:17; 3 Ne. 15:1; M&M 9:14; 17:8; 75:16, 22.

imechorwa kumbukumbu ya Kitabu cha Mormoni. Nabii alimwuliza Bwana kupitia Urimu na Thumimu naye akapata jibu hili.

1–6, Wafanyakazi katika shamba la Bwana hupata wokovu; 7–13, Hakuna zawadi iliyo kubwa zaidi kuliko zawadi ya wokovu; 14–27, Ushuhuda wa ukweli huja kwa uwezo wa Roho; 28–37, Mtegemee Kristo na tenda mema daima.

Kazi kubwa na ya [a]ajabu i karibu kuja kwa wanadamu.

2 Tazama, Mimi ndimi Mungu; litiini [a]neno langu, lililo hai na lenye nguvu, [b]kali kuliko upanga wenye makali pande mbili, kwa kugawanya viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; hivyo basi yatiini maneno yangu.

3 Tazama, [a]shamba ni jeupe tayari kwa mavuno; kwa hiyo, yeyote atakaye kuvuna, na aingize mundu yake kwa nguvu zake, na kuvuna wakati siku ingali, ili aweze kujiwekea akiba kwa ajili ya nafsi yake wokovu usio na mwisho katika ufalme wa Mungu.

4 Ndiyo, yeyote yule [a]atakayeingiza mundu yake na kuvuna, yeye huyo ameitwa na Mungu.

5 Kwa hiyo, kama wewe [a]utaniomba mimi utapata, kama utabisha utafunguliwa.

6 Sasa, kama ulivyoomba, tazama ninakuambia, shika amri zangu, na [a]tafuta kuianzisha na kustawisha kusudi la [b]Sayuni;

7 [a]Usitafute [b]utajiri bali [c]hekima, na tazama, [d]siri za Mungu zitafichuliwa kwako, na ndipo wewe utafanywa tajiri. Tazama, yeye aliye na [e]uzima wa milele ndiye tajiri.

8 Amini, amini, nakuambia, kama unavyotaka kwangu na itakuwa hivyo kwako; na kama unataka, utakuwa chanzo cha kufanya mambo mema mengi katika kizazi hiki.

9 Usiseme lolote bali [a]toba kwa kizazi hiki; shika amri zangu, na saidia kuitenda kazi yangu, kulingana na amri zangu, na wewe utabarikiwa.

10 Tazama nawe unacho kipawa, na umebarikiwa kwa sababu ya kipawa chako. Kumbuka ni [a]kitakatifu na chatoka juu—

11 Na kama wewe [a]utauliza, utapata kujua [b]siri zilizo kubwa na za ajabu; hivyo basi wewe unapaswa kutumia [c]kipawa

6 1*a* Isa. 29:14; M&M 4; 18:44.
2*a* Ebr. 4:12; Ufu. 1:16; M&M 27:1.
b Hel. 3:29; M&M 33:1.
3*a* Yn. 4:35; M&M 31:4; 33:3; 101:64.
4*a* Ufu. 14:15–19; Alma 26:5; M&M 11:3–4, 27.
5*a* Mt. 7:7–8.
6*a* 1 Ne. 13:37.
b MWM Sayuni.
7*a* Alma 39:14; M&M 68:31.
b 1 Fal. 3:10–13; Mt. 19:23; Yak. (KM) 2:18–19. MWM Malimwengu; Ukwasi.
c MWM Hekima.
d M&M 42:61, 65. MWM Siri za Mungu.
e M&M 14:7.
9*a* Alma 29:9; M&M 15:6; 18:14–15; 34:6. MWM Kazi ya kimisionari; Toba, Tubu.
10*a* M&M 63:64.
11*a* M&M 102:23; JS—H 1:18, 26.
b Mt. 11:25; 13:10–11; Alma 12:9.
c MWM Karama; Vipawa vya Roho.

chako, kwamba uweze kuzigundua siri, kwamba uweze kuwaleta wengi kwenye maarifa ya ukweli, ndiyo, [d]kuwashawishi wao juu ya makosa ya njia zao.

12 Usifanye kipawa chako kijulikane kwa yeyote ila kwa wale tu wa imani yako. Usicheze na mambo [a]matakatifu.

13 Kama wewe wataka kutenda mema, ndiyo, na [a]endelea kwa [b]uaminifu hadi [c]mwisho, nawe utaokolewa katika ufalme wa Mungu, ambayo ndiyo zawadi kubwa kuliko zote kwa Mungu; kwani hakuna zawadi kubwa zaidi kuliko zawadi ya [d]wokovu.

14 Amini, amini, nakuambia, umebarikiwa wewe, kwa kile ulichofanya; kwani wewe [a]umeniuliza Mimi, na tazama, kama daima ulivyoniuliza, nawe umepata maelekezo ya Roho wangu. Kama isingelikuwa hivyo, wewe usingelifika mahali ulipo sasa.

15 Tazama, na wewe wajua kwamba uliniuliza Mimi na Mimi nikaiangaza [a]akili yako; na sasa ninakuambia wewe mambo haya kwamba uweze kuelewa kwamba wewe uliangaziwa na Roho wa ukweli;

16 Ndiyo, ninakuambia, ili wewe upate kujua kwamba hapana yeyote ila Mungu ambaye [a]hujua mawazo yako na dhamira ya [b]moyo wako.

17 Ninakuambia mambo haya kama ushahidi kwako—kwamba maneno au kazi ambayo wewe umekuwa ukiandika ni ya [a]kweli.

18 Kwa hivyo fanya [a]bidii; [b]simama pamoja na mtumishi wangu Joseph, kiuaminifu, katika hali yoyote iwayo ngumu atakayoweza kuwa kwa sababu ya neno.

19 Muonye katika makosa yake na pia pokea maonyo yake. Kuwa mvumilivu; mtulivu; mwenye kiasi, uwe na subira, imani, tumaini na hisani.

20 Tazama, wewe ndiwe Oliver, na nimesema nawe kwa sababu ya matakwa yako; kwa hiyo [a]yatunze maneno haya katika moyo wako. Uwe mwaminifu na mwenye juhudi katika kushika amri za Mungu, na mimi nitakuzungushia mikono ya upendo wangu.

21 Tazama, Mimi ndimi Yesu Kristo, [a]Mwana wa Mungu. Mimi ni yule yule ambaye nilikuja kwa walio [b]wangu, na walio wangu hawakunipokea. Mimi ni [c]nuru inayong'aa [d]gizani, nalo giza halikuiweza.

11 *d* Yak. (Bib.) 5:20; Alma 62:45; M&M 18:44.
12 *a* Mt. 7:6.
13 *a* 1 Ne. 15:24.
b Mos. 2:41; Eth. 4:19; M&M 51:19; 63:47.
c MWM Stahimili.
d MWM Wokovu.
14 *a* MWM Sala.
15 *a* MWM Nia.
16 *a* 1 Nya. 28:9; Mt. 12:25; Ebr. 4:12; Mos. 24:12; 3 Ne. 28:6. MWM Kujua yote.
b 1 Fal. 8:39.
17 *a* M&M 18:2.
18 *a* MWM Bidii.
b M&M 124:95–96.
20 *a* Eth. 3:21; M&M 84:85.
21 *a* MWM Yesu Kristo.
b Yn. 1:10–12; Mdo. 3:13–17; 3 Ne. 9:16; M&M 45:8.
c Yn. 1:5; M&M 10:58. MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
d MWM Giza, Kiroho.

22 Amini, amini, ninakuambia, kama wataka ushahidi zaidi, rejesha mawazo yako juu ya usiku ule uliponililia katika moyo wako, kwamba uweze [a]kujua ukweli wa mambo haya.

23 Sikusema [a]amani akilini mwako kuhusiana na jambo hili? Ni [b]ushahidi gani mkubwa zaidi unaoweza kupata kuliko kutoka kwa Mungu?

24 Na sasa, tazama, umepata ushahidi; kwani kama mimi nimekuambia mambo ambayo hakuna mtu ajuaye, je hujapata ushahidi?

25 Na, tazama, ninakupa kipawa, kama wataka kutoka kwangu, cha [a]kutafsiri, hata kama mtumishi wangu Joseph.

26 Amini, amini, ninakuambia, kwamba zipo [a]kumbukumbu ambazo zimechukua kiasi kikubwa cha injili yangu, ambayo ilizuiliwa kwa sababu ya [b]uovu wa watu;

27 Na sasa ninakuamuru, kwamba kama unayo tamaa njema—tamaa ya kujiwekea hazina yako mbinguni—ndipo utasaidia katika kuzileta kwenye nuru, kwa kipawa chako, sehemu zile za [a]maandiko yangu matakatifu ambayo yamefichwa kwa sababu ya uovu.

28 Na sasa, tazama, ninakupa wewe pamoja na mtumishi wangu Joseph funguo za kipawa hiki, ambacho kitaileta nuruni huduma hii; na katika vinywa vya [a]mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike.

29 Amini, amini, ninawaambia, kama wao wanakataa maneno yangu, na sehemu hii ya injili yangu na huduma, mmebarikiwa ninyi, kwani wao hawatafanya zaidi kwenu kuliko walivyonifanyia mimi.

30 Na hata kama [a]watawafanyia ninyi kama walivyonifanyia Mimi, mmebarikiwa ninyi, kwani [b]mtaishi pamoja na mimi katika [c]utukufu.

31 Lakini kama [a]hawataya-kataa maneno yangu, ambayo yataanzishwa kwa [b]ushuhuda ambao utatolewa, wamebarikiwa wao, na ndipo ninyi mtapata shangwe ya matunda ya kazi yenu.

32 Amini, amini, ninawaambia, kama nilivyosema kwa wanafunzi wangu, walipo wawili au watatu [a]waliokusanyika pamoja katika jina langu, wakigusia jambo moja, tazama, mimi nitakuwa [b]katikati yao—hata sasa nipo katikati yenu.

33 [a]Msiogope kufanya mema, wana wangu, kwani chochote [b]unachopanda, ndicho pia

22 *a* MWM Utambuzi, Kipawa cha.
23 *a* MWM Amani.
b 1 Yoh. 5:9; M&M 18:2.
25 *a* Mos. 8:13; M&M 5:4; 9:1–5, 10.
26 *a* M&M 8:1; 9:2. MWM Maandiko—Maandiko yaliyotolewa unabii kwamba yatakuja.
b MWM Ovu, Uovu.
27 *a* M&M 35:20.
28 *a* Kum. 19:15; 2 Kor. 13:1; 2 Ne. 27:12–14; M&M 128:3.
30 *a* M&M 5:22; 135. MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.
b Ufu. 3:21.
c MWM Utukufu.
31 *a* 3 Ne. 16:10–14; M&M 20:8–15.
b MWM Ushuhuda.
32 *a* Mt. 18:19–20. MWM Umoja.
b M&M 29:5; 38:7.
33 *a* MWM Ushujaa, enye Ushujaa.
b Gal. 6:7–8; Mos. 7:30–31; Alma 9:28; M&M 1:10.

wewe utakachokivuna; kwa hiyo kama utapanda mema pia utavuna mema kwa thawabu zenu.

34 Kwa sababu hiyo, msiogope, enyi kundi dogo; tendeni mema; acha dunia na jehanamu ziungane dhidi yenu, kwani kama mmejengwa juu ya [a]mwamba wangu, haziwezi kuwashinda.

35 Tazama, siwahukumu ninyi; nendeni zenu na msitende [a]dhambi tena; fanyeni kwa utaratibu kazi ambayo nimewaamuru.

36 [a]Nitegemeeni katika kila wazo; msitie shaka, msiogope.

37 [a]Tazama majeraha yaliyoko yaliotobolewa ubavuni mwangu, na pia alama za [b]misumari katika mikono na miguu yangu; kuweni waaminifu, zishikeni amri zangu, na [c]mtaurithi [d]ufalme wa mbinguni. Amina.

SEHEMU YA 7

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Oliver Cowdery, huko Harmony, Pennsylvania, Aprili 1829, wakati walipoulizia kupitia Urimu na Thumimu kama ikiwa Yohana, mwanafunzi kipenzi, alikuwa bado yu hai au amekufa. Ufunuo huu ni tafsiri ya masimulizi ya kumbukumbu iliyoandikwa na Yohana kwenye karatasi ya ngozi na kufichwa na yeye mwenyewe.

1–3, Yohana Kipenzi ataishi mpaka Bwana atakapokuja; 4–8, Petro, Yakobo na Yohana wanashikilia funguo za injili.

Na Bwana akaniambia: [a]Yohana mpendwa wangu, [b]wataka nini wewe? Kwani ukiomba kile utakachotaka, utapewa.

2 Na mimi nikamwambia: Bwana, nipe uwezo wa kushinda [a]mauti, ili niweze kuishi na kuzileta nafsi nyingi kwako.

3 Na Bwana akaniambia: Amini, amini, ninakuambia, kwa sababu wewe umetaka hili na wewe [a]utaishi mpaka nitakapokuja katika [b]utukufu wangu, na utatoa [c]unabii kwa mataifa, makabila, lugha na watu.

4 Na kwa sababu hii Bwana akamwambia Petro: Kama ninataka kwamba aishi mpaka

34 *a* Zab. 71:3; Mt. 7:24–25; 1 Kor. 10:1–4; Hel. 5:12; M&M 10:69; 18:4, 17; 33:13; Musa 7:53. MWM Mwamba.
35 *a* Yn. 8:3–11.
36 *a* Isa. 45:22; M&M 43:34.
37 *a* MWM Yesu Kristo—Kuonekana kwa Kristo baada ya kifo.
b MWM Kusulubiwa.
c Mt. 5:3, 10; 3 Ne. 12:3, 10.
d MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
7 1 *a* MWM Yohana, Mwana wa Zebedayo.
b 3 Ne. 28:1–10.
2 *a* Lk. 9:27. MWM Mauti ya Kimwili.
3 *a* Yn. 21:20–23. MWM Viumbe waliobadilishwa.
b MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo; Utukufu.
c Ufu. 10:11.

nitakapokuja, hii ni nini kwako? Kwani anataka kwangu kwamba aweze kuzileta roho nyingi kwangu, lakini wewe watamani uje haraka katika [a]ufalme wangu.

5 Ninakuambia wewe, Petro, hii ilikuwa ni tamaa iliyo njema; lakini mpendwa wangu ametamani kwamba aweze kufanya zaidi, au kazi kubwa zaidi miongoni mwa wanadamu kuliko alivyofanya awali.

6 Ndiyo, amekubali kazi kubwa zaidi; hivyo basi nitamfanya yeye kuwa kama moto unaowaka na malaika [a]mhudumu; atawahudumia wale watakaokuwa [b]warithi wa wokovu waishio [c]duniani.

7 Na nitakufanya wewe kuwa mhudumu wake na kwa ndugu yako Yakobo; na kwenu ninyi watatu nitawapa mamlaka haya na [a]funguo za huduma hii mpaka nitakapokuja.

8 Amini ninawaambia ninyi, mtapata kila mtu kulingana na matakwa yenu, kwani ninyi nyote [a]mnajawa shangwe katika yale mnayoyataka.

SEHEMU YA 8

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Oliver Cowdery, huko Harmony, Pennsylvania, Aprili 1829. Katika mpangilio wa kutafsiri Kitabu cha Mormoni, Oliver, ambaye aliendelea kutumika kama mwandishi, kuandika imla iliyokuwa ikitafsiriwa na Nabii, alitamani kupewa kipawa cha tafsiri. Bwana alijibu maombi yake kwa kumpa ufunuo huu.

1–5, Ufunuo huja kwa uwezo wa Roho Mtakatifu; 6–12, Maarifa ya siri za Mungu na uwezo wa kutafsiri kumbukumbu za kale huja kwa imani.

[a]Oliver Cowdery, amini, amini, ninakuambia, kwamba hakika kama Bwana aishivyo, ambaye ndiye Mungu na Mkombozi wako, hata hivyo hakika waweza nawe kupata [b]maarifa ya chochote kile [c]utakachokiomba kwa imani, na moyo mnyoofu, ukiamini kwamba utapata maarifa kuhusiana na michoro ya [d]kumbukumbu ya zamani, ambayo ni ya kale, ambayo ndani yake mna sehemu zile za andiko langu ambalo limezungumziwa kwa [e]ufunuo wa Roho wangu.

2 Ndiyo, tazama, [a]nitakujulisha wewe akilini mwako na

4 *a* MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
6 *a* M&M 130:5.
b M&M 76:86–88.
c Yn. 10:8–11; M&M 77:14.
7 *a* Mt. 16:19; Mdo. 15:7; JS—H 1:72. MWM Funguo za Ukuhani.
8 *a* MWM Shangwe.
8 1 *a* JS—H 1:66. MWM Cowdery, Oliver.
b MWM Maarifa.
c MWM Sala.
d M&M 6:26–27; 9:2.
e M&M 5:16.
2 *a* M&M 9:7–9. MWM Ufunuo.

katika [b]moyo wako, kwa njia ya [c]Roho Mtakatifu, ambaye atakujia na ambaye atakaa moyoni mwako.

3 Sasa, tazama, hii ndiyo roho ya ufunuo; tazama, huyu ndiye Roho ambaye kwa yeye Musa aliwaongoza wana wa Israeli kupitia [a]Bahari ya Shamu kwenye nchi kavu.

4 Hivyo basi hiki ni kipawa chako; kitumie, na umebarikiwa wewe, kwani kitakukomboa wewe kutoka katika mikono ya adui zako, wakati, kama isingalikuwa hivyo, wangelikuua wewe na kuiweka nafsi yako kwenye uharibifu.

5 O, kumbuka [a]maneno haya, na zishike amri zangu. Kumbuka, hiki ndicho kipawa chako.

6 Sasa hiki sicho kipawa pekee ulichonacho; kwani unacho kipawa kingine, ambacho ni kipawa cha Haruni; tazama, kimekuambia mambo mengi;

7 Tazama, hakuna nguvu nyingine, ila nguvu ya Mungu, ambayo yaweza kusababisha nguvu hii ya Haruni ikawa kwako wewe.

8 Hivyo basi, usitie shaka, kwani ni kipawa cha Mungu; na wewe utakishika katika mikono yako, na kufanya kazi za ajabu; na hakuna nguvu itakayoweza kuipokonya kutoka katika mikono yako, kwani hiyo ni kazi ya Mungu.

9 Na, kwa hiyo, chochote utakachoomba kwangu nikuambie kwa njia hiyo, hicho nitakupa, na utakuwa na maarifa kuhusu hilo.

10 Kumbuka kwamba pasipo [a]imani huwezi kufanya lolote; hivyo basi omba kwa imani. Usicheze na mambo haya; [b]usiombe kitu kile usichopaswa kukiomba.

11 Omba kwamba wewe ujue siri za Mungu, na kwamba uweze [a]kutafsiri na kupokea maarifa kutoka kumbukumbu zile zote za kale ambazo zimefichwa, ambazo ni takatifu; na kulingana na imani yako itakuwa hivyo kwako.

12 Tazama, ni mimi niliyeyasema haya; na ni, Mimi yule yule niliyesema na wewe kutoka mwanzo. Amina.

SEHEMU YA 9

Ufunuo uliotolewa kupitia kwa Joseph Smith Nabii kwa Oliver Cowdery, huko Harmony, Pennsylvania, Aprili 1829. Oliver anaonywa kuwa awe mvumilivu na anahimizwa kuridhika na kazi ya uandishi, kwa wakati huu, kama inavyosemwa na mfasiri, kuliko kujaribu kutafsiri.

2 *b* MWM Moyo.
c MWM Roho Mtakatifu.
3 *a* Ku. 14:13–22; Kum. 11:4; 1 Ne. 4:2; Mos. 7:19. MWM Bahari ya Shamu.
5 *a* Kum. 11:18–19.
10 *a* MWM Amini, Imani.
b M&M 88:63–65.
11 *a* M&M 9:1, 10.

1–6, Kumbukumbu nyingine za kale bado hazijatafsiriwa; 7–14, Kitabu cha Mormoni kinatafsiriwa kwa kuchunguza na kwa uthibitisho wa kiroho.

Tazama, ninakuambia wewe, mwana wangu, kwamba kwa sababu [a]hukutafsiri kama ulivyotaka kutoka kwangu, na hivyo umeanza [b]kuandika tena kwa ajili ya mtumishi wangu, Joseph Smith, Mdogo, hivyo ndivyo nipendavyo kwamba uendelee kuandika hadi utakapomaliza kumbukumbu hii, ambayo nimemkabidhi yeye.

2 Na halafu, tazama, [a]kumbukumbu [b]nyingine ninazo, ambazo nitakupa wewe uwezo ili uweze kusaidia kuzitafsiri.

3 Uwe mvumilivu, mwana wangu, kwani hiyo ni hekima kwangu, na haifai wewe kutafsiri kwa wakati huu.

4 Tazama, kazi ambayo umeitwa kuifanya ni kuandika kwa ajili ya mtumishi wangu Joseph.

5 Na, tazama, nimekunyang'anya heshima hiyo, kwa sababu hukuendelea kuifanya kama vile ulivyoianza kutafsiri.

6 [a]Usinung'unike, mwanangu, kwani hiyo ni hekima kwangu kukutendea namna hiyo.

7 Tazama, wewe hujaelewa; ulidhani ya kuwa Mimi nitakupatia tu wewe, wakati wewe hukutafakari isipokuwa kuniomba Mimi tu.

8 Lakini, tazama, ninakuambia, kwamba unalazimika [a]kulichunguza katika akili yako; ndipo [b]uniulize kama ni sahihi, na kama ni sahihi nitaufanya [c]moyo wako [d]uwake ndani yako; kwa njia hiyo, [e]utahisi kuwa hiyo ni sahihi.

9 Lakini kama siyo sahihi hutapata hisia za namna hiyo, bali [a]mzubao wa mawazo ambayo yatakufanya usahau kitu kile kisicho sahihi; kwa sababu hiyo, huwezi kuandika kile kilicho kitakatifu ila kimetolewa kwako kutoka kwangu.

10 Sasa, kama ungelijua hivi ungeliweza [a]kutafsiri; hata hivyo, haifai kuwa wewe utafsiri sasa.

11 Tazama, ilifaa wakati ulipoanza; lakini [a]ukaogopa, na muda umekwisha pita, na haifai tena sasa;

12 Kwani, huoni kwamba nimempa mtumishi wangu [a]Joseph nguvu za kutosha, ambazo kwa hizo zatosheleza? Na wala hakuna kati yenu niliye mhukumu.

13 Fanya jambo hili ambalo nimekuamuru, na wewe

9 1*a* M&M 8:1, 11.
b JS—H 1:67.
2*a* M&M 6:26; 8:1.
b Dokezo kuhusu shughuli ya nyongeza ya kutafsiri, ikijumuisha Tafsiri ya Joseph Smith ya Biblia na Kitabu cha Ibrahimu ambacho Oliver Cowdery alisadia kama mwandishi. MWM Tafsiri ya Joseph Smith (TJS).
6*a* MWM Manung'uniko.
8*a* MWM Tafakari.
b MWM Sala.
c Lk. 24:32.
d MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi; Ushuhuda.
e M&M 8:2–3.
9*a* M&M 10:2.
10*a* M&M 8:11.
11*a* MWM Hofu.
12*a* M&M 18:8.

utastawi. Uwe mwaminifu, na usijiingize katika [a]majaribu.

14 Simama imara katika [a]kazi ambayo [b]nimekuitia, na wala unywele wa kichwa chako hautapotea, na wewe [c]utainuliwa juu siku ya mwisho. Amina.

SEHEMU YA 10

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, huko Harmony, Pennsylvania, yawezekana kuwa mnamo Aprili 1829, ingawa sehemu yawezekana kuwa zilipokelewa mapema zaidi katika kiangazi cha mwaka 1828. Ambamo ndani yake Bwana anamjulisha Joseph juu ya mabadiliko yaliyofanywa na watu waovu katika kurasa 116 za muswada kutoka kwenye tafsiri ya kitabu cha Lehi, katika kitabu cha Mormoni. Kurasa hizi za muswada ambazo zilipotea kutoka katika miliki ya Martin Harris, ambaye karatasi hizo zilikuwa zimeaminishwa kwake kwa muda. (Ona kichwa cha habari cha sehemu ya 3.) Njama ovu zilikuwa ni kusubiri tafsiri ya pili ya jambo ambalo lilikwisha tafsiriwa katika kurasa zilizoibiwa na ndipo wamwaibishe mfasiri. Kwa kuonyesha tofauti zilizosababishwa na mabadiliko hayo. Kwamba kusudio hili la uovu lilikuwa limetungwa na yule mwovu lilijulikana kwa Bwana hata wakati Mormoni, Mnefi mwanahistoria wa kale, alipokuwa akifanya ufupishaji wa mabamba yaliyokusanywa; imeonyeshwa katika kitabu cha Mormoni (ona Maneno ya Mormoni 1:3–7).

1–26, Shetani huwachochea watu waovu kupinga kazi ya Bwana; 27–33, Yeye hutafuta kuziangamiza roho za wanadamu; 34–52, Injili itaenda kwa Walamani na mataifa yote kupitia Kitabu cha Mormoni; 53–63, Bwana atalianzisha Kanisa Lake na injili Yake miongoni mwa wanadamu; 64–70, Atawakusanya wenye kutubu katika Kanisa Lake na atawaokoa watiifu.

Sasa, tazama, ninakuambia wewe, kwa sababu wewe ulitoa maandiko yale ambayo wewe ulipewa uwezo wa kutafsiri kwa njia ya [a]Urimu na Thumimu, na kuyaweka katika mikono ya mtu [b]mwovu, umeyapoteza.

2 Na pia umepoteza kipawa chako vile vile, na [a]akili yako ikawa giza.

3 Hata hivyo, sasa [a]kimerejeshwa tena kwako; kwa hivyo angalia kwamba uwe mwaminifu na endelea hata kumaliza

13*a* mwm Jaribu, Majaribu.
14*a* 1 Kor. 16:13.
b mwm Ita, Itwa na Mungu, Wito.
c Alma 13:29; M&M 17:8.
10 1*a* mwm Urimu na Thumimu.
b M&M 3:1–15.
2*a* mwm Nia.
3*a* M&M 3:10.

mabaki ya kazi ya kutafsiri kama ulivyoanza.

4 Usikimbie [a]haraka zaidi au kufanya kazi zaidi ya [b]nguvu ulizonazo na nyenzo ulizopewa kukuwezesha wewe kutafsiri; bali uwe mwenye [c]bidii hadi mwisho.

5 [a]Omba daima, kwamba uweze kutoka mshindi; ndiyo, uweze kumshinda Shetani, na kwamba uweze kuiepuka mikono ya watumishi wa Shetani ambao hufanya kazi yake.

6 Tazama, wanatafuta [a]kukuangamiza; ndiyo, hata [b]mtu yule ambaye ulimwamini ametafuta kukuangamiza.

7 Na kwa sababu hii nilisema kwamba yeye ni mtu mwovu, kwani yeye ametaka kuchukua vitu ambavyo wewe umeaminiwa; na pia ametafuta kuangamiza kipawa chako.

8 Na kwa sababu wewe umeyatoa maandiko hayo na kuyaweka mikononi mwake, tazama, watu waovu wameyachukua kutoka kwako.

9 Kwa hivyo, wewe umeyatoa, ndiyo, yale yaliyokuwa matakatifu, kwa waovu.

10 Na, tazama, [a]Shetani ameyaweka katika mioyo yao kuyabadilisha maneno ambayo wewe umeyasababisha kuandikwa, au ambayo umeyatafsiri, ambayo yamekutoka mikononi mwako.

11 Na tazama, ninakuambia, kwamba kwa sababu wao wameyabadilisha maneno, yanasomeka kinyume na yale ambayo ulitafsiri na ukasababisha yaandikwe;

12 Na, kwa jinsi hii, ibilisi ametafuta kuweka mpango wa hila, ili apate kuiharibu kazi hii;

13 Kwani yeye ameweka katika mioyo yao kufanya hili, kwamba kwa kudanganya waweze kusema kwamba [a]wamekukamata wewe katika maneno ambayo wewe mwenyewe umedai kuyatafsiri.

14 Amini, ninakuambia, kwamba sitakubali kwamba Shetani atimilize mpango wake huu mwovu katika jambo hili.

15 Kwani tazama, ameyaweka haya katika mioyo yao kukukamata wewe ili unijaribu Bwana Mungu wako, katika kuomba kuyatafsiri hayo tena.

16 Na halafu, tazama, wanasema na kuwaza mioyoni mwao—Tutaona kama Mungu amempa yeye uwezo wa kutafsiri; kama ndivyo, pia atampa tena yeye uwezo;

17 Na kama Mungu atampa yeye uwezo tena, au atatafsiri tena, au, katika maneno mengine, kama atayaleta maneno haya haya, tazama, sisi tunayo, na tumeyabadilisha;

18 Kwa hiyo hawatakubaliana, na tutasema kwamba amesema uwongo katika maneno yake, na kwamba yeye hana kipawa, na kwamba yeye hana uwezo;

4*a* Mos. 4:27.
b Ku. 18:13–26.
c Mt. 10:22.
MWM Bidii.

5*a* 3 Ne. 18:15–21.
MWM Sala.

6*a* M&M 5:32–33; 38:13.
b M&M 5:1–2.

10*a* MWM Ibilisi.

13*a* Yer. 5:26.

19 Kwa hivyo tutamwangamiza, na pia kazi; na tutafanya haya ili tusije aibika mwishoni, na ili tuweze kupata utukufu wa ulimwengu.

20 Amini, amini, ninakuambia, kwamba Shetani ana mshiko mkubwa katika mioyo yao; yeye [a]huwachochea wao kufanya [b]uovu dhidi ya kile kilicho chema;

21 Na mioyo yao [a]imepotoka, na imejaa [b]uovu na machukizo; na [c]wanapenda [d]giza kuliko nuru, kwa sababu [e]matendo yao ni maovu; kwa hivyo wao hawataniomba Mimi.

22 [a]Shetani huwachochea, ili kwamba aweze [b]kuwaongoza nafsi zao kwenye maangamizo.

23 Na hivyo yeye ametega mpango huu wa ulaghai, akifikiria kuharibu kazi ya Mungu; lakini nitayadai haya kutoka kwao, na itageuka kuwa aibu na hukumu yao katika siku ya [a]hukumu.

24 Ndiyo, huwachochea katika mioyo yao kuikasirikia dhidi ya kazi hii.

25 Ndiyo yeye huwaambia: Danganyeni na mvizieni, ili mpate kumwangamiza; tazama, hii haina madhara. Na hivyo huwalaghai, na kuwaambia kwamba siyo dhambi [a]kudanganya ili kwamba waweze kumkamata mtu katika uongo, ili wapate kumwangamiza.

26 Na hivyo huwalaghai, na [a]kuwaongoza wao, hata kuzikokota roho zao hadi chini [b]jehanamu; na hivyo kusababisha hao kujinasa katika [c]mtego wao wenyewe.

27 Na hivyo ndivyo aendavyo juu na chini, [a]mbele na nyuma katika ulimwengu, akitafuta [b]kuziangamiza roho za wanadamu.

28 Amini, amini, ninakuambia, ole na iwe kwake yeye ambaye husema uongo ili [a]kudanganya kwa sababu yeye adhani kwamba mtu mwingine pia husema uongo ili kudanganya, kwani mtu wa namna hiyo hatasamehewa kutokana na [b]hukumu ya Mungu.

29 Sasa, tazama, wameyabadilisha maneno haya, kwa sababu Shetani amewaambia wao hivyo: Amekudanganyeni ninyi—na hivyo ndivyo yeye anavyowalaghai wao kufanya uovu, ili kuwapateni ninyi ili [a]mumjaribu Bwana Mungu wenu.

30 Tazama, ninakuambia, kwamba usitafsiri tena maneno

20 *a* 2 Ne. 28:20–22.
b MWM Dhambi.
21 *a* M&M 112:23–24.
b MWM Ovu, Uovu.
c Musa 5:13–18.
d Mos. 15:26.
MWM Giza, Kiroho.
e Yn. 3:18–21; M&M 29:45.
22 *a* 2 Ne. 2:17–18.
b MWM Jaribu, Majaribu.
23 *a* Hel. 8:25; M&M 121:23–25.
25 *a* 2 Ne. 2:18; 28:8–9; Alma 10:17; Musa 4:4.
MWM Kusema uongo.
26 *a* MWM Ukengeufu.
b MWM Jehanamu.
c Mit. 29:5–6; 1 Ne. 14:3.
27 *a* Ayu. 1:7.
b 2 Ne. 28:19–23; M&M 76:28–29.
28 *a* MWM Danganya, Kudanganya, Udanganyifu.
b Rum. 2:3.
MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
29 *a* Mt. 4:7.

yale ambayo yamekwishatoka mikononi mwako;

31 Kwani, tazama, hawatatimiza njama zao hizo za uovu katika kudanganya dhidi ya maneno yale. Kwani, tazama, kama wewe utayatoa tena maneno yale yale watasema kwamba umedanganya na ya kwamba unajidai kuwa unatafsiri kumbe umejichanganya mwenyewe.

32 Na, tazama, wao watayachapisha haya, na Shetani itaishupaza mioyo ya watu kwa kuwachochea wakukasirikie wewe, kiasi kwamba hawatayaamini maneno yangu.

33 Na hivyo ndivyo [a]Shetani awazavyo ili kuushinda ushuhuda wako katika kizazi hiki, kwamba kazi hii isije katika kizazi hiki.

34 Lakini tazama, hii ndiyo hekima, na kwa sababu ninakuonyesha wewe [a]hekima, na kukupa amri kuhusu mambo haya, nini yakupasa kufanya, usiyaonyeshe kwa walimwengu mpaka utakapomaliza kazi ya kutafsiri.

35 Usishangae kwamba nimeyasema haya kwako: Hapa ndipo penyehekima,usiyaonyeshekwa walimwengu—kwani nilisema, usiyaonyeshe kwa ulimwengu, kwamba uweze kulindwa.

36 Tazama, mimi sisemi kwamba hutaonyesha kwa wenye haki;

37 Bali, kwa vile huwezi daima kuwahukumu wenye [a]haki, au kama vile wewe usivyoweza daima kuwatambua waovu na wenye haki, kwa hivyo ninakuambia, [b]nyamaza mpaka nitakapoona inafaa kuyafanya mambo yote yajulikane kwa ulimwengu kuhusu jambo hili.

38 Na sasa, amini ninakuambia, kwamba historia ya [a]mambo yale ambayo uliyaandika, ambayo yametoka mikononi mwako, yamechorwa katika [b]mabamba ya Nefi.

39 Ndiyo, na unakumbuka kwamba ilisemwa katika maandiko yale kwamba historia zaidi juu ya mambo haya yametolewa katika mabamba ya Nefi.

40 Na sasa, kwa sababu historia ambayo imechorwa juu ya mabamba ya Nefi ambayo ni sahihi zaidi mambo ambayo, katika hekima yangu, nitayaleta kwenye ufahamu wa watu katika historia hii—

41 Kwa hivyo utatafsiri michoro ambayo ipo juu ya [a]mabamba ya Nefi, kwenda chini mpaka ufike kwenye utawala wa mfalme Benjamini, au hadi ufike kwa yale ambayo umekwisha yatafsiri, ambayo uliyabakisha;

42 Na tazama, utachapisha hiyo kama kumbukumbu ya Nefi; na hivyo nitawashinda wao ambao wameyabadilisha maneno yangu.

43 Sitakubali kwamba waiha-

33 *a* MWM Ibilisi.
34 *a* MWM Hekima.
37 *a* Mt. 23:28.
b Ku. 14:14.
38 *a* Katika dibaji ya toleo la kwanza la Kitabu cha Mormoni, Nabii alieleza kwamba yaliyokuwamo katika kurasa 16 zilizopotea yalifasiriwa kutoka katika "Kitabu cha Lehi."
b MWM Mabamba.
41 *a* M. ya Morm. 1:3–7.

ribu kazi yangu; ndiyo, nitawaonyesha wao kwamba hekima yangu ni kuu kuliko hila ya ibilisi.

44 Tazama, wamepata sehemu tu, au ufupisho wa historia ya Nefi.

45 Tazama, kuna mambo mengi yaliyochorwa juu ya mabamba ya Nefi ambayo huonyesha ufahamu mkubwa wa injili yangu; kwa hivyo, ni hekima kwangu kwamba wewe utafsiri sehemu hii ya kwanza ya michoro ya Nefi, na itokee katika kazi hii.

46 Na tazama, mabaki yote ya [a]kazi hii yanayo sehemu zile zote za [b]injili yangu ambayo manabii wangu watakatifu, ndiyo, na pia wanafunzi wangu, [c]walitamani katika sala zao yaweze kutolewa kwa watu hawa.

47 Na mimi niliwaambia wao, kwamba [a]itakubaliwa kwao kulingana na [b]imani yao katika sala zao;

48 Ndiyo, na hii ndiyo ilikuwa imani yao—kwamba injili yangu, ambayo niliwapa wao kwamba waweze kuihubiri katika siku zao, iweze kuja kwa ndugu zao [a]Walamani, na wale pia wamekuwa Walamani kwa sababu ya mafarakano yao.

49 Sasa, haya siyo yote—imani katika sala zao ilikuwa kwamba injili hii iweze kujulikana pia, kama ingewezekana kwamba mataifa mengine yangekuja kumiliki nchi hii;

50 Na hivyo waliacha baraka juu ya nchi hii katika sala zao, kwamba yeyote atakayeamini katika injili hii katika nchi hii apate uzima wa milele;

51 Ndiyo, kwamba iwe bure kwa wote na wa taifa lolote, kabila, lugha, au watu wowote watakaokuwa.

52 Na sasa, tazama, kulingana na imani yao katika sala zao nitaileta sehemu hii ya injili kwenye ufahamu wa watu wangu. Tazama, siileti kuja kuharibu kile ambacho wamekwisha kipokea, bali kwa kukijenga.

53 Na kwa sababu hiyo mimi nimesema: Kama kizazi hiki hakitaishupaza mioyo yao, nitalianzisha kanisa langu miongoni mwao.

54 Sasa sisemi hili ili kuliangamiza kanisa langu, bali nasema hili ili kulijenga kanisa langu;

55 Kwa hivyo, yeyote aliye wa kanisa langu hahitaji [a]kuogopa, kwani huyo [b]ataurithi [c]ufalme wa mbinguni.

56 Lakini ni wao ambao [a]hawaniogopi Mimi, wala kuzishika amri zangu bali wanajijengea [b]makanisa yao wenyewe ili [c]kujinufaisha, ndiyo, na wale wote ambao hufanya maovu na kujenga ufalme wa ibilisi—ndiyo, amini, amini, ninakuambia, kwamba ndiyo wao ambao

46 *a* MWM Kitabu cha Mormoni.
b MWM Injili.
c Eno. 1:12–18; Morm. 8:24–26; 9:34–37.
47 *a* 3 Ne. 5:13–15; M&M 3:19–20.
b MWM Amini, Imani.
48 *a* Moro. 10:1–5; M&M 109:65–66.
55 *a* MWM Hofu.
b Mt. 5:10.
c MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
56 *a* Mh. 12:13–14.
b MWM Ibilisi—Kanisa la ibilisi.
c 4 Ne. 1:26.

nitawavuruga, na kusababisha watetemeke na kutikisika hadi kitovuni.

57 Tazama, Mimi ni Yesu Kristo, [a]Mwana wa Mungu. Nilikuja kwa walio wangu, na walio wangu hawakunipokea.

58 Mimi ni [a]nuru ing'aayo gizani, na wala giza halikuiweza.

59 Mimi ndiye yule aliyesema—[a]Kondoo [b]wengine ninao ambao si wa zizi hili—kwa wanafunzi wangu, na wengi walikuwepo ambao [c]hawakunielewa.

60 Na nitaonyesha kwa watu hawa kwamba nilikuwa na kondoo wengine, na kwamba walikuwa tawi la [a]nyumba ya Yakobo;

61 Na mimi nitazileta katika nuru kazi zao za ajabu, ambazo walizifanya katika jina langu;

62 Ndiyo, na pia nitaileta katika nuru injili yangu ambayo walihudumiwa wao, na, tazama, wao hawataweza kukikataa kile ambacho wewe umekipokea, bali wao watazijenga, na watazileta nuruni sehemu muhimu za kweli za [a]mafundisho yangu, ndiyo, na fundisho pekee lililoko ndani yangu.

63 Na hii ninafanya ili kwamba niweze kuanzisha injili yangu, ili pasiwepo na ubishi mwingi; ndiyo, [a]Shetani huchochea mioyo ya watu kwenye [b]ubishi kuhusu mambo ya mafundisho yangu; na katika mambo haya wanakosea, kwani [c]wanayapindisha maandiko na wala hawayaelewi.

64 Kwa hivyo, nitafunua kwao siri hii kubwa;

65 Kwani, tazama, [a]nitawakusanya wao kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake chini ya mabawa yake, kama hawataishupaza mioyo yao;

66 Ndiyo, kama wanatakakuja, wao wanaweza, na kunywa [a]maji ya uzima bure.

67 Tazama, hili ni fundisho langu—yeyote atubuye na [a]kuja kwangu, huyo ndiye [b]kanisa langu.

68 Yeyote [a]atangazaye zaidi au pungufu kuliko hili, huyo siye wangu, bali ni [b]adui yangu; kwa hivyo siyo wa kanisa langu.

69 Na sasa, tazama, yeyote aliye wa kanisa langu, na alivumiliaye kanisa langu hadi mwisho, huyo nitamweka juu ya [a]mwamba wangu, na [b]milango ya jehanamu haitamshinda.

70 Na sasa, kumbuka maneno yake yeye aliye uzima na [a]nuru ya ulimwengu, Mkombozi wako, [b]Bwana wako na Mungu wako. Amina.

57 *a* Rum. 1:4.
58 *a* M&M 6:21.
59 *a* MWM Mchungaji Mwema.
b Yn. 10:16.
c 3 Ne. 15:16–18.
60 *a* MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
62 *a* 3 Ne. 11:31–40.
63 *a* MWM Ibilisi.
b MWM Ushindani.
c 2 Pet. 3:16.
65 *a* Lk. 13:34; 3 Ne. 10:4–6; M&M 43:24.
66 *a* MWM Maji ya Uzima.
67 *a* Mt. 11:28–30.
b MWM Kanisa la Yesu Kristo.
68 *a* 3 Ne. 11:40.
b Lk. 11:23.
69 *a* MWM Mwamba.
b Mt. 16:18; 2 Ne. 4:31–32; M&M 17:8; 128:10.
70 *a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
b MWM Yesu Kristo.

SEHEMU YA 11

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa kaka yake Hyrum Smith, huko Harmony, Pennsylvania, Mei 1829. Ufunuo huu ulipokelewa kupitia Urimu na Thumimu katika jibu kwa maombi na maulizo ya Joseph Smith. Historia ya Joseph Smith inapendekeza kwamba ufunuo huu ulipokelewa baada ya urejesho wa Ukuhani wa Haruni.

1–6, Watenda kazi katika shamba la mizabibu watapata wokovu; 7–14, Tafuta hekima, hubiri toba, amini katika Roho; 15–22; Shika amri, na jifunze neno la Bwana; 23–27, Usikatae roho wa ufunuo na wa unabii; 28–30, Wale ambao wanampokea Kristo huwa wana wa Mungu.

Kazi [a]kubwa na ya ajabu i karibu kuja miongoni mwa wanadamu.

2 Tazama, Mimi ndimi Mungu; [a]tiini [b]neno langu, lililo hai na lenye [c]nguvu, [d]kali kuliko upanga wenye makali pande mbili, kwa kugawanya viungo na mafuta yaliyo ndani yake; hivyo basi, litiini neno langu.

3 Tazama, shamba ni [a]jeupe tayari kwa mavuno; kwa hivyo, yeyote atakaye kuvuna na aingize mundu yake kwa nguvu zake, na kuvuna wakati siku ingali, ili aweze kujiwekea [b]hazina ya wokovu [c]usio na mwisho kwa ajili ya nafsi yake katika ufalme wa Mungu.

4 Ndiyo, yeyote yule atakayeingiza [a]mundu yake na kuvuna, yeye huyo ameitwa na Mungu.

5 Kwa hivyo, kama wewe [a]utaniomba Mimi utapata, kama utabisha utafunguliwa.

6 Sasa, kama ulivyoomba, tazama, ninakuambia, shika amri zangu, na tafuta kuanzisha na kustawisha kusudi la [a]Sayuni.

7 Usitafute [a]utajiri bali [b]hekima; na, tazama, siri za Mungu zitafichuliwa kwako, na ndipo wewe utafanywa tajiri. Tazama, yule aliye na uzima wa milele ndiye tajiri.

8 Amini, amini, ninakuambia, kama vile unavyotaka kutoka kwangu na hivyo ndivyo itakavyokuwa kwako; na, kama unataka, utakuwa chanzo cha kufanya mema mengi katika kizazi hiki.

9 [a]Usiseme lolote bali [b]toba kwa kizazi hiki. Shika amri zangu, na saidia kuitenda kazi

11 1*a* Isa. 29:14; M&M 4. MWM Urejesho wa Injili.
2*a* 1 Ne. 15:23–25; M&M 1:14; 84:43–45.
b Ebr. 4:12.
c Alma 4:19; 31:5.
d Hel. 3:29–30; M&M 6:2.
3*a* M&M 12:3.
b Lk. 18:22; Hel. 5:8.
c 1 Tim. 6:19.
4*a* Ufu. 14:15; M&M 14:3–4.
5*a* MWM Sala.
6*a* Isa. 52:7–8; M&M 66:11. MWM Sayuni.
7*a* 1 Fal. 3:11–13; 2 Ne. 26:31; Yak. (KM) 2:17–19; M&M 38:39.
b MWM Hekima.
9*a* M&M 19:21–22.
b MWM Toba, Tubu.

yangu, [c]kulingana na amri zangu, nawe utabarikiwa.

10 Tazama, wewe unacho [a]kipawa, au wewe waweza kuwa na kipawa kama utataka kutoka kwangu kwa imani, pamoja na moyo [b]mwaminifu, ukiamini katika uwezo wa Yesu Kristo, au uwezo wangu mimi niongeaye nawe;

11 Kwani, tazama, ni Mimi niongeaye; tazama, Mimi ndimi [a]nuru ing'arayo gizani, na kwa [b]uwezo wangu nitatoa maneno haya kwako wewe.

12 Na sasa, amini, amini, ninakuambia wewe, weka [a]imani yako katika [b]Roho yule ambaye huongoza kufanya mema—ndiyo, kufanya haki, [c]kutembea kwa [d]unyenyekevu, [e]kuhukumu kwa haki; na huyu ndiyo Roho wangu.

13 Amini, amini ninakuambia, nitakupa Roho wangu, ambaye [a]ataiangaza [b]akili yako, ambayo itaijaza nafsi yako kwa [c]shangwe;

14 Na ndipo utajua, au kwa haya utajua, mambo yote ambayo unahitaji kutoka kwangu, ambayo yanahusika na mambo ya [a]haki, katika imani ukiamini katika mimi kwamba utapokea.

15 Tazama, ninakuamuru kwamba hauhitaji kudhani kwamba wewe umeitwa kuhubiri mpaka [a]utakapoitwa.

16 Subiri kidogo, mpaka utakapopata neno langu, [a]mwamba wangu, kanisa langu, na injili yangu, kwamba uweze kujua uhakika wa mafundisho yangu.

17 Na tena, tazama, kulingana na matakwa yako, ndiyo, hata kulingana na imani yako itafanyika kwako.

18 Zishike amri zangu; kaa kimya; omba kwa Roho wangu;

19 Ndiyo, [a]ambatana nami kwa moyo wako wote, ili uweze kusaidia kuleta kwenye nuru mambo yale ambayo yamesemwa—ndiyo, tafsiri ya kazi yangu; uwe mvumilivu mpaka utakapoikamilisha.

20 Tazama, hii ndiyo kazi yako, [a]kuzishika amri zangu, ndiyo, kwa nguvu zako zote, akili na uwezo.

21 Usitafute kulitangaza neno langu, bali kwanza tafuta [a]kulipata neno langu, na kisha ulimi wako utalegezwa; halafu, kama unataka, utapata Roho wangu na neno langu, ndiyo, nguvu ya Mungu kwa kuwashawishi wanadamu.

22 Lakini sasa kaa kimya; jifunze [a]neno langu ambalo limeanza miongoni mwa wanadamu,

9 *c* M&M 105:5.
10 *a* M&M 46:8–12.
b Lk. 8:15.
11 *a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
b MWM Uwezo.
12 *a* M&M 84:116. MWM Tegemea.
b Rum. 8:1–9; 1 Yoh. 4:1–6.
c MWM Tembea, Tembea na Mungu.
d MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
e Mt. 7:1–5; Alma 41:14–15.
13 *a* M&M 76:12.
b MWM Nia.
c MWM Shangwe.
14 *a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
15 *a* M ya I 1:5. MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito; Mamlaka.
16 *a* M&M 6:34. MWM Mwamba.
19 *a* Yak. (KM) 6:5; M&M 98:11.
20 *a* MWM Mtiifu, Tii, Utii.
21 *a* Alma 17:2–3; M&M 84:85.
22 *a* MY Biblia.

na pia [b]jifunze [c]neno langu ambalo litakuja miongoni mwa wanadamu, au lile ambalo sasa linatafsiriwa, ndiyo, mpaka utakapopata yote ambayo [d]nitawapa wanadamu katika kizazi hiki, na kisha mambo yote yataongezwa juu ya hayo.

23 Tazama wewe ni [a]Hyrum, mwanangu; [b]tafuta ufalme wa Mungu, na mambo yote yataongezwa kulingana na kile kilicho cha haki.

24 [a]Jenga juu ya mwamba wangu, ambao ni [b]injili yangu;

25 Usikatae roho ya [a]ufunuo, wala roho ya [b]unabii, kwani ole wake yule ambaye huyakataa mambo haya;

26 Kwa hivyo, yatunze katika [a]hazina ya moyo wako mpaka wakati ambao ni hekima kwangu mimi kwamba uenende mbele.

27 Tazama, ninasema kwa wale wote walio na matakwa yaliyo mema, na [a]wameingiza mundu zao kuvuna.

28 Tazama, Mimi ndimi [a]Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Mimi ni uzima na [b]nuru ya ulimwengu.

29 Mimi ndimi yule yule niliyekuja kwa walio wangu na walio wangu hawakunipokea;

30 Lakini amini, amini ninawaambia ninyi, kwamba kadiri wengi wanavyonipokea Mimi, wao nitawapa [a]uwezo wa kuwa [b]wana wa Mungu, hata kwa wale ambao wataamini juu ya jina langu. Amina.

SEHEMU YA 12

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Joseph Knight Mkubwa, huko Harmony, Pennsylvania, Mei 1829. Joseph Knight aliamini matamko ya Joseph Smith kuhusiana na kuwa nayo mabamba ya Kitabu cha Mormoni na kazi ya kutafsiri ikiwa inaendelea na mara kadhaa amewahi kutoa msaada wa mali kwa Joseph Smith na mwandishi wake, ambao uliwawezesha wao kuendelea kutafsiri. Kwa maombi ya Joseph Knight, Nabii alimwuliza Bwana na kupata ufunuo huu.

1–6, Wafanya kazi katika shamba la mizabibu watapata wokovu; 7–9, Wale wote wanaotamani na wenye kustahili wanaweza kusaidia katika kazi ya Bwana.

22 *b* MWM Maandiko—Thamani ya maandiko.
c MY Kitabu cha Mormoni.
d Alma 29:8.
23 *a* JS—H 1:4.
b Mt. 6:33.
24 *a* Mt. 7:24–27.
b MWM Injili.
25 *a* MWM Ufunuo.
b Ufu. 19:10.
MWM Toa unabii, Unabii.
26 *a* Kum. 11:18; M&M 6:20; 43:34; JS—M 1:37.
27 *a* MWM Kazi ya kimisionari.
28 *a* MWM Yesu Kristo.
b MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
30 *a* Yn. 1:12.
b MWM Wana na Mabinti za Mungu.

Kazi [a]kubwa na ya ajabu i karibu kuja miongoni mwa wanadamu.

2 Tazama, Mimi ndimi Mungu; tiini neno langu, lililo hai na lenye nguvu, kali kuliko upanga wenye makali pande mbili, kwa kugawanya viungo na mafuta yaliyo ndani ya mifupa; kwa hiyo litiini neno langu.

3 Tazama, shamba ni jeupe tayari kwa mavuno; kwa hiyo, yeyote atakaye kuvuna na aingize ndani mundu yake kwa nguvu zake, na kuvuna wakati siku ingali, ili aweze kujiwekea hazina ya wokovu usio na mwisho kwa ajili ya nafsi yake katika ufalme wa Mungu.

4 Ndiyo, yeyote atakayeingiza mundu wake na kuvuna, yeye huyo ameitwa na Mungu.

5 Kwa hiyo, kama utaniomba mimi utapata; kama utabisha utafunguliwa.

6 Sasa, kama ulivyoomba, tazama, ninakuambia, shika amri zangu, na tafuta kuanzisha na kustawisha kusudi la Sayuni.

7 Tazama, ninasema nawe, na pia kwa wale wote walio na hamu ya kuanzisha na kuendeleza kazi hii;

8 Na hakuna yeyote awezaye kusaidia katika kazi hii isipokuwa yule aliye [a]mnyenyekevu na aliyejaa [b]upendo, akiwa na [c]imani, [d]matumaini na [e]hisani, akiwa na kiasi katika mambo yote, yatakayoaminiwa katika utunzaji wake.

9 Tazama, Mimi ndimi nuru na uzima wa ulimwengu, nisemaye maneno haya, kwa hiyo sikiliza kwa nguvu zako, na kisha wewe umeitwa. Amina.

SEHEMU YA 13

Dondoo kutoka katika historia ya Joseph Smith inayoeleza kutawazwa kwa Nabii na Oliver Cowdery kwenye Ukuhani wa Haruni jirani na Harmony, Pennsylvania, 15 Mei 1829. Kutawazwa huko kulifanywa kwa mikono ya malaika ambaye alijitambulisha kama Yohana, yule yule ambaye anaitwa Yohana Mbatizaji katika Agano Jipya. Malaika alieleza kwamba yeye alikuwa akiyafanya chini ya maelekezo ya Petro, Yakobo na Yohana, Mitume wa kale walioshikilia funguo za ukuhani wa juu zaidi, ambao uliitwa Ukuhani wa Melkizedeki. Ahadi ilitolewa kwa Joseph na Oliver kwamba katika wakati upasao ukuhani huu mkuu utatunukiwa kwao. (Ona sehemu ya 27:7–8, 12.)

Funguo na uwezo wa Ukuhani wa Haruni zinatolewa.

Juu yenu ninyi watumishi wenzangu, katika jina la Masiya

12 1*a* Tazama M&M 11:16 kwa ajili ya rejeo linalofanana na hili.

8*a* mwm Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
b mwm Upendo.
c mwm Amini, Imani.
d mwm Tumaini.
e mwm Hisani.

[a]ninawatunukia [b]Ukuhani wa Haruni, ambao hushikilia funguo za huduma za [c]malaika, na za injili ya [d]toba, na za [e]ubatizo kwa uzamisho kwa ajili ya ondoleo la dhambi; na hizi kamwe hazitaondolewa tena kutoka duniani, mpaka [f]wana wa Lawi watakapotoa tena matoleo kwa Bwana katika [g]haki.

SEHEMU YA 14

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa David Whitmer, huko Fayette, New York, Juni 1829. Familia ya Whitmer ilipata kuvutiwa sana katika kutafsiri Kitabu cha Mormoni. Nabii alianzisha makazi yake katika nyumba ya Peter Whitmer Mkubwa, mahali alipokaa hadi kazi ya tafsiri ilipofika kukamilika na haki miliki ya kitabu kilichotarajiwa ilipopatikana. Kati ya wana watatu wa Whitmer, kila mmoja akiwa amepokea ushuhuda wa ukweli wa kazi hiyo, wakawa wamejihusisha sana juu ya mambo ya wajibu wa kila mmoja. Ufunuo huu na mbili zinazofuatia (sehemu ya 15 na 16) zilitolewa kama jibu la maulizo kupitia Urimu na Thumimu. David Whitmer baadaye alikuja kuwa mmoja kati ya Mashahidi Watatu wa Kitabu cha Mormoni.

1–6, Wafanya kazi katika shamba la mizabibu watapata wokovu; 7–8, Uzima wa milele ni zawadi iliyo kubwa ya Mungu; 9–11, Kristo aliumba mbingu na nchi.

Kazi [a]kubwa na ya ajabu i karibu kuja miongoni mwa wanadamu.

2 Tazama, Mimi ndimi Mungu; litiini neno langu, lililo hai na lenye nguvu, kali kuliko upanga wenye makali pande mbili, kwa kugawanya viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; kwa hivyo litii neno langu.

3 Tazama, shamba ni jeupe tayari kwa mavuno; kwa hiyo, yeyote atakaye kuvuna na aingize ndani mundu yake kwa nguvu zake, na kuvuna wakati siku ingali, ili aweze kujiwekea hazina ya wokovu usio na mwisho kwa ajili ya nafsi yake katika ufalme wa Mungu.

4 Ndiyo, yeyote atakayeingiza mundu yake na kuvuna, yeye huyo ameitwa na Mungu.

13 1*a* JS—H 1:68–75. MWM Kutawaza, Kutawazwa.
b M&M 27:8; 84:18–34. MWM Ukuhani wa Haruni.
c MWM Malaika.
d MWM Toba, Tubu.
e MWM Batiza, Ubatizo.
f Tazama maelezo ya Oliver Cowdery kuhusu urejesho wa Ukuhani wa Haruni mwishoni mwa Historia ya Joseph Smith. Kum. 10:8; 1 Nya. 6:48; M&M 128:24.
g MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.

14 1*a* Tazama M&M 11:1–6 kwa ajili ya rejeo linalofanana na hili.

5 Kwa hivyo, kama utaniomba Mimi utapata; kama utabisha utafunguliwa.

6 Tafuta kuanzisha na kustawisha Sayuni yangu. Shika amri zangu katika mambo yote.

7 Na, kama [a]unashika amri zangu na [b]kuvumilia hadi mwisho utapata [c]uzima wa milele, kipawa ambacho ni kikuu katika vipawa vyote vya Mungu.

8 Na itakuja kutokea, kwamba kama utamwomba Baba katika jina langu, kwa imani ukiamini, utampokea [a]Roho Mtakatifu, ambaye hutoa usemi, ili uweze kusimama kama [b]shahidi wa mambo ambayo [c]utayasikia na kuyaona, na pia uweze kutangaza toba kwa kizazi hiki.

9 Tazama, Mimi ni [a]Yesu Kristo, [b]Mwana wa [c]Mungu aliye hai, ambaye [d]aliumba mbingu na [e]dunia, [f]nuru ambayo haiwezi kufichika [g]gizani;

10 Kwa hiyo, ni lazima niulete mbele [a]utimilifu wa injili yangu kuanzia kwa [b]Wayunani hadi nyumba ya Israeli.

11 Na tazama, wewe ni David, na wewe umeitwa kusaidia; kitu ambacho kama utakifanya, na ukiwa mwaminifu, utabarikiwa vyote kiroho na kimwili, na kubwa itakuwa thawabu yako. Amina.

SEHEMU YA 15

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa John Whitmer, huko Fayette, New York, Juni 1829 (ona kichwa cha habari cha sehemu ya 14). Ujumbe ni wa siri na wa kuvutia kibinafsi ambamo kwamba Bwana anasema juu ya lililojulikana tu kwa John Whitmer na Yeye mwenyewe. John Whitmer baadaye alikuja kuwa mmoja wa Mashahidi Wanane wa Kitabu cha Mormoni.

1–2, Mkono wa Bwana u juu ya ulimwengu wote; 3–6, Kuhubiri injili na kuziokoa nafsi ni jambo la thamani kubwa.

Sikiliza mtumishi wangu John, na sikiliza maneno ya Yesu Kristo, Bwana wako na Mkombozi wako.

7 *a* Law. 26:3–12; Yn. 15:10; Mos. 2:22, 41; M&M 58:2.
b MWM Stahimili.
c 2 Ne. 31:20; M&M 6:13. MWM Uzima wa Milele.
8 *a* MWM Roho Mtakatifu.
b Mos. 18:8–10. MWM Shahidi, Ushahidi.
c Tazama "Ushuhuda wa Mashahidi Watatu" katika kurasa tangulizi za Kitabu cha Mormoni.
9 *a* Mos. 4:2; M&M 76:20–24.
b Rum. 1:4.
c Dan. 6:26; Alma 7:6; M&M 20:19.
d Yn. 1:1–3, 14; 3 Ne. 9:15; M&M 45:1. MWM Umba, Uumbaji.
e Ibr. 4:12, 24–25.
f 2 Sam. 22:29. MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
g MWM Giza, Kiroho.
10 *a* M&M 20:8–9; JS—H 1:34.
b MWM Wayunani.

2 Kwani tazama, ninasema nawe kwa ukali na kwa [a]nguvu, kwani mkono wangu u juu ya ulimwengu wote.

3 Na nitakuambia wewe yale ambayo hakuna mtu ajuaye isipokuwa mimi na wewe pekee—

4 Kwani mara nyingi wewe umetamani kujua kutoka kwangu kwamba ni kipi ambacho kitakuwa na thamani kubwa kwako.

5 Tazama, umebarikiwa wewe kwa jambo hili, na kwa kusema maneno yangu ambayo nimekupa kulingana na amri zangu.

6 Na sasa, tazama, ninakuambia, kwamba jambo ambalo litakuwa la thamani kubwa kwako ni [a]kutangaza toba kwa watu hawa, ili uweze kuzileta nafsi hizo kwangu, na kwamba uweze [b]kupumzika pamoja nao katika [c]ufalme wa [d]Baba yangu. Amina.

SEHEMU YA 16

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Peter Whitmer Mdogo, huko Fayette, New York, Juni 1829. (ona kichwa cha habari cha sehemu ya 14). Peter Whitmer Mdogo baadaye alikuja kuwa mmoja wa Mashahidi Wanane wa Kitabu cha Mormoni.

1–2, Mkono wa Bwana u juu ya ulimwengu wote; 3–6, Kuhubiri injili na kuokoa nafsi ni jambo la thamani kubwa.

[a]Sikiliza, mtumishi wangu Peter, na usikilize maneno ya Yesu Kristo, Bwana wako na Mkombozi wako.

2 Kwani tazama, ninasema nawe kwa ukali na kwa nguvu, kwani mkono wangu u juu ya ulimwengu wote.

3 Na nitakuambia wewe yale ambayo hapana mtu ajuaye isipokuwa mimi na wewe pekee—

4 Kwani mara nyingi umetamani kujua kutoka kwangu kwamba ni kipi ambacho kitakuwa na thamani kubwa kwako.

5 Tazama, umebarikiwa wewe kwa jambo hili, na kwa kusema maneno yangu ambayo nimekupa kulingana na amri zangu.

6 Na sasa, tazama, ninakuambia, kwamba jambo ambalo litakuwa na thamani kubwa kwako ni kutangaza toba kwa watu hawa, ili uweze kuzileta nafsi hizo kwangu, na kwamba uweze kupumzika pamoja nao katika ufalme wa Baba yangu. Amina.

15 2*a* Hel. 3:29–30. MWM Uwezo.
6*a* M&M 18:15–16. MWM Kazi ya kimisionari.
b MWM Pumzika.
c MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
d MWM Baba wa Mbinguni.
16 1*a* Tazama M&M 15 kwa ajili ya rejeo linalofanana na hili.

SEHEMU YA 17

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Oliver Cowdery, David Whitmer, na Martin Harris, huko Fayette, New York, Juni 1829, kabla ya kuona mabamba ya michoro ambayo yalikuwa na kumbukumbu ya Kitabu cha Mormoni, Joseph na mwandishi wake, Oliver Cowdery, walijifunza kutoka kwenye tafsiri ya Kitabu cha Mormoni kwamba mashahidi watatu maalumu watateuliwa (ona Etheri 5:2–4; 2 Nefi 11:3; 27:12). Oliver Cowdery, David Whitmer, na Martin Harris waliongozwa kwa kushawishika kutaka kuwa mashahidi watatu maalumu. Nabii alimwuliza Bwana, na ufunuo huu ulitolewa kama jibu kupitia Urimu na Thumimu.

1–4, Kwa imani Mashahidi Watatu hao watayaona mabamba na vitu vingine vitakatifu; 5–9, Kristo atoa ushuhuda wa utakatifu wa Kitabu cha Mormoni.

Tazama, ninawaambia, kwamba ni lazima ninyi mtegemee maneno yangu, ambayo kama mtafanya kwa dhamira ya moyoni, mtapata [a]kuona [b]mabamba hayo, na pia dera ya kifua, [c]upanga wa Labani, [d]Urimu na Thumimu, ambavyo vilitolewa kwa [e]kaka wa Yaredi juu ya mlima, wakati alipozungumza na Bwana [f]uso kwa uso, na vielekezi vya [g]kimiujiza ambavyo alipewa Lehi akiwa nyikani, mpakani mwa [h]Bahari ya Shamu.

2 Na ni kwa imani yenu kwamba mtapata kuyaona hayo, hata kwa imani ile ambayo ilikuwa kwa manabii wa kale.

3 Na baada ya hapo mmekwishapata imani, na mmeyaona hayo kwa macho yenu, [a]mtayashuhudia hayo, kwa nguvu za Mungu.

4 Na hii ninyi mtafanya ili kwamba mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, asiangamizwe, kwamba niweze kutimiza madhumuni yangu ya haki kwa wanadamu katika kazi hii.

5 Na mtashuhudia kwamba mmeyaona, hata vile mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, alivyoyaona; kwani ni kwa uwezo wangu kwamba ameyaona, na ni kwa sababu alikuwa na imani.

6 Na amekwisha tafsiri [a]kitabu, hata [b]sehemu ile ambayo nilimwamuru, na kama vile

17 1*a* 2 Ne. 27:12; Eth. 5:2–4; M&M 5:15. Tazama pia Ushuhuda wa Mashahidi Watatu katika kurasa za tangulizi za Kitabu cha Mormoni.
b Morm. 6:6; JS—H 1:52. MWM Mabamba.
c 1 Ne. 4:8–9; 2 Ne. 5:14; Yak. (KM) 1:10; Mos. 1:16.
d MWM Urimu na Thumimu.
e Etheri 3.
f Mwa. 32:30; Ku. 33:11; Musa 1:2.
g 1 Ne. 16:10, 16, 26–29; Alma 37:38–47.
h 1 Ne. 2:5.
3*a* MWM Shahidi, Ushahidi; Shuhudia.
6*a* MWM Kitabu cha Mormoni.
b 2 Ne. 27:22; 3 Ne. 26:7–10.

Bwana wenu na Mungu wenu aishivyo ni kweli.

7 Kwa hiyo, ninyi mmepokea uwezo ule ule, na imani ile ile, na kipawa kile kile kama yeye;

8 Na kama mtafanya amri zangu hizi za mwisho, ambazo nimewapa ninyi, [a]milango ya jehanamu haitawashinda; kwani [b]neema yangu inawatosha, na ninyi [c]mtainuliwa siku ya mwisho.

9 Na Mimi, Yesu Kristo, [a]Bwana wenu na Mungu wenu, nimesema hayo kwenu ninyi, ili kwamba niweze kutimiza madhumuni yangu ya haki kwa wanadamu. Amina.

SEHEMU YA 18

Ufunuo kwa Joseph Smith, Nabii, Oliver Cowdery, na David Whitmer, uliotolewa huko Fayette, New York, Juni 1829. Kulingana na Nabii, ufunuo huu uliojulikana kama "kuitwa kwa mitume kumi na wawili katika siku hizi za mwisho, na pia maelekezo yahusuyo kuanzishwa kwa Kanisa."

1–5, Maandiko yanaonyesha namna ya kulijenga Kanisa; 6–8, Ulimwengu unakomaa katika dhambi; 9–16, Thamani ya nafsi ni kuu; 17–25 Ili kupata wokovu, wanadamu yawalazimu kujichukulia juu yao wenyewe jina la Kristo; 26–36, Wito na huduma ya Kumi na Wawili yafunuliwa; 37–39, Oliver Cowdery na David Whitmer wawatafute Kumi na Wawili; 40–47, Ili kupata wokovu, mwanadamu inamlazimu kutubu, kubatizwa na kushika amri.

Sasa, tazama, kwa sababu ya jambo ambalo wewe, mtumishi wangu Oliver Cowdery, umetaka kulijua kwangu, ninakupa maneno haya:

2 Tazama, nimekwisha jidhihirisha kwako, kwa Roho yangu mara nyingi, kwamba mambo ambayo umeyaandika ni ya [a]kweli; kwa hiyo unajua ni ya kweli.

3 Na kama wewe unajua kwamba ni ya kweli, tazama, ninakupa wewe amri, kwamba utegemee mambo ambayo [a]yameandikwa;

4 Kwani katika hayo mambo yote yameandikwa kuhusu msingi wa kanisa langu, [a]injili yangu, na [b]mwamba wangu.

5 Kwa hiyo, kama utalijenga kanisa langu, juu ya msingi wa injili yangu na mwamba wangu, milango ya jehanamu haitakushinda.

6 Tazama, [a]ulimwengu unaiva katika dhambi; na ni lazima

8*a* Mt. 16:18; 3 Ne. 11:39; M&M 10:69.
b MWM Neema.
c 1 Ne. 13:37; 3 Ne. 27:14–15, 22; M&M 9:14.
9*a* MWM Bwana.
18 2*a* M&M 6:15–17.
3*a* M&M 98:11. MWM Maandiko—Thamani ya maandiko.
4*a* MWM Injili.
b MWM Mwamba.
6*a* MWM Ulimwengu.

inahitajika kuwa wanadamu wachochewe katika toba, wote [b]Wayunani na pia wa nyumba ya Israeli.

7 Kwa hiyo, kama [a]ulivyobatizwa kwa mikono ya mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, kulingana na vile nilivyomwamuru, ametimiza jambo ambalo nilimwamuru.

8 Na sasa, usishangae kwamba nimemwita yeye kwa madhumuni yangu, madhumuni ambayo yanajulikana kwangu; kwa hiyo, kama atafanya [a]bidii katika [b]kushika amri zangu [c]atabarikiwa kwa uzima wa milele; na jina lake ni [d]Joseph.

9 Na sasa, Oliver Cowdery, ninasema na wewe, na pia na David Whitmer, kwa njia ya amri; kwani, tazama, ninawaamuru watu wote kila mahali kutubu, na ninasema nanyi, hata kama vile kwa Paulo [a]mtume wangu, kwani mmeitwa kwa wito ule ule ambao yeye aliitwa.

10 Kumbuka [a]thamani ya [b]nafsi ni kubwa mbele za Mungu;

11 Kwani, tazama, Bwana [a]Mkombozi wako aliteseka hadi [b]kifo katika mwili; kwa hiyo [c]aliteseka [d]maumivu ya watu wote, ili kwamba watu wote waweze kutubu na kuja kwake.

12 Na yeye [a]amefufuka tena kutoka kwa wafu, ili kwamba aweze kuwaleta watu wote kwake, kwa masharti ya [b]toba.

13 Na ni [a]shangwe kubwa kiasi gani kwake katika nafsi ambayo hutubu!

14 Kwa hiyo, wewe umeitwa [a]kutangaza toba kwa watu hawa.

15 Na kama itakuwa kwamba utafanya kazi siku zako zote katika kutangaza toba kwa watu hawa, na kuleta, japo iwe [a]nafsi moja kwangu, shangwe yako itakuwa kubwa jinsi gani pamoja naye katika ufalme wa Baba yangu!

16 Na sasa, kama shangwe yako itakuwa kubwa kwa hiyo nafsi moja ambayo umeileta kwangu katika [a]ufalme wa Baba yangu, itakuwa [b]shangwe kubwa namna gani kwako kama [c]utazileta nafsi nyingi kwangu!

17 Tazama, unayo injili yangu mbele yako, na mwamba wangu, na [a]wokovu wangu.

18 [a]Mwombe Baba katika [b]jina langu kwa imani, ukiamini kwamba utapokea, nawe utapata Roho Mtakatifu, ambaye

6 *b* MWM Wayunani.
7 *a* JS—H 1:70–71.
8 *a* MWM Bidii.
b MWM Mtiifu, Tii, Utii.
c MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
d 2 Ne. 3:14–15. MWM Smith, Joseph, Mdogo.
9 *a* Rum. 1:1.
10 *a* MWM Nafsi—Thamani ya nafsi.
b MWM Nafsi.
11 *a* MWM Mkombozi.
b MWM Kusulubiwa.
c MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
d Isa. 53:4–5. MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
12 *a* MWM Ufufuko.
b M&M 19:4–18. MWM Toba, Tubu.
13 *a* Lk. 15:7.
14 *a* Alma 29:1–2; M&M 34:5–6; 63:57.
15 *a* MWM Nafsi—Thamani ya nafsi.
16 *a* MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
b Alma 26:11. MWM Shangwe.
c MWM Kazi ya kimisionari.
17 *a* MWM Wokovu.
18 *a* MWM Sala.
b Yn. 15:16.

hudhihirisha mambo yote yaliyo [c]muhimu kwa wanadamu.

19 Na kama wewe hauna [a]imani, [b]matumaini, na [c]hisani, huwezi kufanya lolote.

20 [a]Usishindane na kanisa lolote, isipokuwa [b]kanisa la ibilisi.

21 Ujichukulie juu yako [a]jina la Kristo, na [b]sema ukweli katika [c]utulivu.

22 Na kadiri wengi wanavyotubu na [a]kubatizwa katika jina langu, ambalo ni Yesu Kristo, na [b]kuvumilia hadi mwisho, hao ndiyo wataokolewa.

23 Tazama, Yesu Kristo ndilo [a]jina ambalo limetolewa na Baba, na hakuna jina lingine lililotolewa ambalo kwa hilo mwanadamu aweza kuokolewa;

24 Kwa hiyo, wanadamu wote yawalazimu kujichukulia juu yao jina ambalo limetolewa na Baba, kwani katika jina hilo wataitwa katika siku ya mwisho;

25 Kwa hiyo, kama wao hawajui [a]jina ambalo wanaitwa, hawawezi kupata nafasi katika [b]ufalme wa Baba yangu.

26 Na sasa, tazama, wapo wengine ambao wameitwa kuihubiri injili yangu, kote kwa [a]Myunani na kwa Myahudi;

27 Ndiyo, hata kumi na wawili; na hao Kumi na Wawili watakuwa wanafunzi wangu, na wao watajichukulia juu yao jina langu; na hao [a]Kumi na Wawili ni wale ambao hutamani kujichukulia juu yao [b]jina langu kwa dhamira ya moyo wao wote.

28 Na kama wao hutamani kujichukulia juu yao jina langu kwa dhamira ya moyo wao wote, hao wameitwa kwenda [a]ulimwenguni kote kuhubiri [b]injili yangu kwa [c]kila kiumbe.

29 Na hao ndiyo wale ambao wametawazwa na Mimi [a]kubatiza katika jina langu, kulingana na yale yaliyoandikwa;

30 Na wewe unayo yale ambayo yameandikwa mbele yako; kwa hiyo basi, ni lazima ufanye kulingana na maneno ambayo yameandikwa.

31 Na sasa ninasema na ninyi, [a]Kumi na Wawili—Tazama, neema yangu inatosha kwenu; lazima mtembee wima mbele zangu na msitende dhambi.

32 Na, tazama, ninyi ndiyo wale ambao wametawazwa na mimi ili [a]kuwatawaza makuhani na walimu; kuitangaza injili yangu, [b]kulingana na uwezo wa Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, na kulingana na [c]miito na

18 *c* M&M 88:63–65.
19 *a* MWM Amini, Imani.
b MWM Tumaini.
c MWM Hisani.
20 *a* 2 Tim. 2:23–24; 3 Ne. 11:29–30.
b MWM Ibilisi—Kanisa la ibilisi.
21 *a* 2 Ne. 31:13; Mos. 5:8; 3 Ne. 27:5; M&M 20:37.
b M&M 100:5–8.
c Rum. 12:3.
22 *a* MWM Batiza, Ubatizo.
b MWM Stahimili.
23 *a* Mal. 1:11; Mdo. 4:12; Mos. 3:17; Hel. 3:28–29.
25 *a* Mos. 5:9–14.
b MWM Utukufu wa Selestia.
26 *a* M&M 90:8–9; 112:4.
27 *a* MWM Mtume.
b M&M 27:12.
28 *a* Mk. 16:15–16.
b MWM Injili.
c M&M 1:2; 42:58.
29 *a* 3 Ne. 11:21–28; M&M 20:72–74.
31 *a* M&M 107:23–35.
32 *a* Moro. 3; M&M 20:60; 107:58. MWM Kutawaza, Kutawazwa.
b 2 Pet. 1:21; M&M 68:3–4.
c M&M 20:27.

vipawa vya Mungu kwa wanadamu;

33 Na mimi, Yesu Kristo, Bwana wenu na Mungu wenu, nimeyasema haya.

34 [a]Maneno haya si ya wanadamu wala mwanadamu, bali ni yangu; kwa sababu hiyo, mtayashuhudia hayo kuwa ni yangu na siyo ya mwanandamu;

35 Kwani ni [a]sauti yangu ambayo huyasema kwenu; kwani yanatolewa kwa Roho yangu kwenu, na kwa uwezo wangu ninyi mnaweza kusomeana; na isingekuwa kwa uwezo wangu msingeweza kuyapata hayo;

36 Kwa hiyo basi, ninyi mnaweza [a]kushuhudia kwamba mmesikia sauti yangu, na mnayajua maneno yangu.

37 Na sasa, tazama, ninatoa kwako wewe, Oliver Cowdery, na pia kwako David Whitmer, kwamba mtawatafuta Kumi na Wawili, ambao watakuwa na matamanio haya ambayo nimeyataja;

38 Na kwa matamanio yao na [a]matendo yao mtawajua.

39 Na mkiisha wapata mtaonyesha mambo haya kwao.

40 Na ninyi mtaanguka chini na [a]kumwabudu Baba katika jina langu.

41 Na ninyi lazima mhubiri kwa ulimwengu, mkisema: Lazima mtubu na mbatizwe, katika jina la Yesu Kristo;

42 Kwani, watu wote lazima watubu na wabatizwe, sio tu wanaume, bali hata wanawake, na watoto ambao wamefikia umri wa [a]wajibikaji.

43 Na sasa, baada ya kuwa ninyi mmepokea haya, ni lazima mzishike [a]amri zangu katika mambo yote;

44 Na kwa mikono yenu nitafanya [a]kazi ya kushangaza miongoni mwa wanadamu, kwa [b]kuwashawishi wengi juu ya dhambi zao, ili waweze kuja kwenye toba, na ili waweze kuja kwenye ufalme wa Baba yangu.

45 Kwa hiyo basi, baraka ambazo ninazitoa kwenu ni [a]juu ya mambo yote.

46 Na baada ya kupokea hii, kama [a]hamtashika amri zangu hamtaweza kuokolewa katika ufalme wa Baba yangu.

47 Tazama, Mimi, Yesu Kristo, Bwana wenu na Mungu wenu, na Mkombozi wenu, kwa uwezo wa Roho yangu nimeyasema haya. Amina.

SEHEMU YA 19

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith, huko Manchester, New

34*a* MWM Maandiko.
35*a* M&M 1:38.
MWM Sauti.
36*a* MWM Shuhudia.
38*a* MWM Matendo.
40*a* MWM Kuabudu.
42*a* M&M 20:71; 29:47; 68:27.
MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
43*a* MWM Amri za Mungu.
44*a* Isa. 29:14; M&M 4:1.
b Alma 36:12–19; 62:45.
45*a* M&M 84:35–38.
46*a* M&M 82:3.

York, yawezekana kabisa ilikuwa katika kiangazi cha 1829. Katika historia yake, Nabii alitambulisha hii kama "amri ya Mungu na siyo ya mwanadamu, kwa Martin Harris, iliyotolewa na yeye aliye wa Milele."

1–3, Kristo anao uwezo wote; 4–5, Watu wote lazima watubu au wateseke; 6–12, Adhabu ya milele ni adhabu ya Mungu; 13–20, Kristo aliteseka kwa ajili ya wote, kwamba wao wasiteseke kama watatubu; 21–28, Hubiri injili ya toba; 29–41, Tangaza habari njema.

Mimi ni [a]Alfa na Omega, [b]Kristo Bwana; ndiyo, Mimi ndiye, mwanzo na mwisho, Mkombozi wa ulimwengu.

2 Mimi, nikiwa nimefanikisha na [a]kutimiza mapenzi yake yeye niliye wake, hata Baba, juu yangu—nikiwa nimefanya hili ili niweze [b]kuvitiisha vitu vyote chini yangu—

3 Nikishikilia [a]nguvu zote, hata ya [b]kumwangamiza Shetani na kazi zake hapo [c]mwisho wa dunia, na siku ile kuu ya hukumu, ambayo nitaipitisha juu ya wakazi wake, [d]nikimhukumu kila mtu kulingana na [e]kazi zake na matendo ambayo ameyafanya.

4 Na ni hakika kila mwanadamu ni lazima [a]atubu au [b]ateseke, kwani Mimi, Mungu, sina [c]mwisho.

5 Kwa hiyo [a]sijafuta hukumu ambayo nitaipitisha, lakini huzuni itajitokeza, kilio, [b]kuomboleza na kusaga meno, ndiyo, kwa wale ambao watapatikana katika mkono wangu wa [c]kushoto.

6 Hata hivyo, [a]haikuandikwa kwamba hapatakuwa na mwisho wa mateso haya, bali imeandikwa [b]*mateso yasiyo na mwisho.*

7 Tena, imeandikwa [a]*laana ya milele;* kwa hiyo hii ni wazi zaidi kuliko maandiko mengine, ili liweze kufanya kazi katika mioyo ya wanadamu, kwa ajili ya utukufu wa jina langu.

8 Kwa hivyo, nitakuelezea wewe siri hii, kwani ni muhimu kwako kujua hata kama mitume wangu.

9 Ninasema kwenu ninyi ambao mmechaguliwa katika jambo hili, kama vile mmoja, ili kwamba muweze kuingia katika [a]pumziko langu.

10 Kwani, tazama, [a]siri ya uchamungu, ni kuu namna gani! Kwani, tazama, Mimi sina mwisho, na adhabu iliyotolewa kutoka mikononi mwangu ni

19 1*a* Ufu. 1:8, 11; 3 Ne. 9:18; M&M 35:1; 61:1.
MWM Alfa na Omega.
b MWM Yesu Kristo.
2*a* Yn. 17:4; 3 Ne. 11:11.
b Flp. 3:21.
3*a* MWM Uwezo.
b Isa. 14:12–17; 1 Yoh. 3:8; 1 Ne. 22:26; M&M 88:111–115.
c MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.
d MWM Hukumu ya mwisho.
e MWM Matendo.
4*a* MWM Toba, Tubu.
b Lk. 13:3; Hel. 14:19.
c Musa 1:3.
5*a* M&M 56:4; 58:32.
b Mt. 13:42.
c Mt. 25:41–43.
6*a* M&M 76:105–106; 138:59.
b M&M 76:33, 44–45.
7*a* Hel. 12:25–26; M&M 29:44.
9*a* MWM Pumzika.
10*a* Yak. (KM) 4:8; M&M 76:114–116.

adhabu isiyo na mwisho, kwani [b]Bila mwisho ndilo jina langu. Kwa hiyo—

11 Adhabu ya [a]milele ni adhabu ya Mungu.

12 Adhabu isiyo na mwisho ni adhabu ya Mungu.

13 Kwa hiyo, ninakuamuru wewe kutubu, na kuzishika [a]amri ambazo umezipokea kwa mkono wa mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, katika jina langu;

14 Na ni kwa uwezo wangu mkuu kwamba mmeyapata hayo;

15 Kwa sababu hii ninakuamuru wewe kutubu—tubu, nisije nikakupiga kwa fimbo ya kinywa changu, na ghadhabu yangu, na kwa hasira yangu, na [a]mateso yako kuwa machungu—machungu namna gani hujui, makali namna gani hujui, ndiyo, namna gani magumu kuyavumilia hujui.

16 Kwani tazama, Mimi, Mungu [a]nimeteseka mambo haya kwa ajili ya wote, ili kwamba [b]wasipate kuteseka kama [c]watatubu;

17 Lakini kama hawatatubu lazima [a]wateseke hata kama Mimi;

18 Mateso ambayo yaliyosababisha Mimi mwenyewe, hata Mungu, mkuu kuliko yote, kutetemeka kwa sababu ya maumivu, na kutoka damu kwenye kila kinyweleo, na kuteseka mwili na roho—na kutamani [a]nisinywe kikombe kichungu, na kusita—

19 Hata hivyo, utukufu na uwe kwa Baba, na Mimi nikachukua na [a]kukamilisha maandalizi yangu kwa wanadamu.

20 Kwa hiyo, ninakuamuru tena kutubu, nisije nikakunyenyekeza wewe kwa uwezo wangu mkuu; na kwamba [a]ukiri dhambi zako, usije ukateseka kwa adhabu hizi ambazo nimezisema, ambazo katika udogo wake, ndiyo, hata katika kiwango kidogo ulionja wakati ule Mimi nilipomwondoa Roho yangu.

21 Na ninakuamuru wewe [a]usihubiri chochote bali toba, na [b]usiyaonyeshe mambo haya kwa ulimwengu mpaka itakapokuwa hekima kwangu.

22 Kwani hao [a]hawaiwezi nyama sasa, bali [b]maziwa lazima wapate; kwa sababu hiyo, wao ni lazima wasiyajue mambo haya, wasije wakaangamia.

23 Jifunze kwangu, na sikiliza maneno yangu; [a]enenda katika [b]unyenyekevu wa Roho yangu, na utapata [c]amani kwangu.

24 Mimi ni [a]Yesu Kristo; nili-

10 *b* Musa 1:3; 7:35. MWM Siyo na mwisho.
11 *a* Mt. 25:46.
13 *a* M&M 5:2; 10:6–7; 17.
15 *a* Alma 36:11–19.
16 *a* Alma 11:40–41. MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
b MWM Rehema, enye Rehema.
c MWM Ondoleo la Dhambi.
17 *a* M&M 29:17.
18 *a* Lk. 22:42–44.
19 *a* Yn. 17:4; 19:30.
20 *a* Hes. 5:6–7; Mos. 26:29; M&M 58:43; 64:7. MWM Kiri, Kukiri.
21 *a* M&M 11:9.
b JS—H 1:42.
22 *a* M&M 78:17–18.
b Ebr. 5:11–14; M&M 50:40.
23 *a* Moro. 7:3–4.
b MWM Pole, Upole.
c MWM Amani.
24 *a* MWM Yesu Kristo.

kuja kwa mapenzi ya Baba, na ninafanya mapenzi yake.

25 Na tena, ninakuamuru wewe, kwamba [a]usitamani [b]mke wa jirani yako; wala kutafuta maisha ya jirani yako.

26 Na tena, ninakuamuru kwamba usitamani mali yako mwenyewe, bali itoe bure kwa uchapishaji wa Kitabu cha Mormoni, ambacho kina [a]ukweli wa neno la Mungu—

27 Ambacho ni neno langu kwa [a]Myunani, kwamba karibu kitaweza kwenda kwa [b]Myahudi, ambao kwao Walamani ni [c]baki, ili waweze kuiamini injili, na wasitazamie kuja kwa [d]Masiya ambaye tayari amekuja.

28 Na tena, ninakuamuru kwamba itakupasa [a]kusali kwa [b]sauti na pia katika moyo wako; ndiyo, mbele ya umati na vile vile sirini, katika hadhara na pia kibinafsi.

29 Na wewe [a]utatangaza habari njema, ndiyo, uitangaze juu ya milima, na juu ya kila mwinuko, na miongoni mwa kila watu ambao utaruhusiwa kuwaona.

30 Na utafanya kwa unyenyekevu wote, [a]ukiamini katika Mimi, usitukane dhidi ya wenye kutukana.

31 Na juu ya [a]imani wewe usizungumzie, bali wewe utatangaza toba na [b]imani juu ya Mwokozi, na [c]ondoleo la dhambi kwa [d]ubatizo, na kwa [e]moto, ndivyo, hata [f]Roho Mtakatifu.

32 Tazama, hii ni kuu na [a]amri ya mwisho ambayo nitakupa wewe kuhusiana na jambo hili; kwani hili litatosha kwa matembezi yako ya kila siku, hata mwisho wa maisha yako.

33 Na mateso utapata kama utapuuza [a]ushauri huu, ndiyo, hata maangamizo yako mwenyewe na mali yako.

34 [a]Toa sehemu ya mali yako, ndiyo, hata sehemu ya ardhi yako, na yote isipokuwa ya kutegemeza familia yako.

35 Lipa [a]deni ambalo [b]ulikubaliana na mchapishaji. Jiondoe mwenyewe kutoka kwenye [c]utumwa.

36 [a]Ondoka nyumbani mwako, isipokuwa wakati wewe utakapotamani kuiona familia yako;

37 Na [a]sema kwa uhuru na wote; ndiyo, hubiri, shawishi, tangaza [b]ukweli, hata kwa sauti kubwa, na kwa sauti ya furaha, paza sauti—Hosana, hosana, libarikiwe jina la Bwana Mungu!

25a MWM Tamani.
b Ku. 20:17; 1 Kor. 7:2–4. MWM Uzinzi.
26a MWM Ukweli.
27a MWM Wayunani.
b MWM Wayahudi.
c Omni 1:14–19; Mos. 25:2–4; Hel. 8:21; 3 Ne. 2:12–16.
d MWM Masiya.
28a 1 Tim. 2:8. MWM Sala.
b M&M 20:47, 51; 23:6.
29a MWM Kazi ya kimisionari.
30a MWM Tegemea.
31a 2 Tim. 2:23–24.
b MWM Amini, Imani.
c MWM Ondoleo la Dhambi.
d MWM Batiza, Ubatizo.
e Mt. 3:11.
f MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
32a M&M 58:26–29.
33a MWM Amri za Mungu.
34a Mdo. 4:34–35.
35a MWM Deni.
b MY kulipia uchapaji wa toleo la kwanza la Kitabu cha Mormoni.
c Mit. 22:7.
36a Mt. 19:29.
37a M&M 58:47; 68:8; 71:7.
b M&M 75:4.

38 [a]Omba daima, na Mimi [b]nitakumwagia Roho yangu juu yako, na baraka kubwa itakuwa juu yako—ndiyo, hata zaidi kuliko kama ungelipata hazina za dunia na uozo uliomo ndani yake.

39 Tazama, unaweza wewe kusoma haya bila kufurahi na kuinua moyo wako kwa furaha?

40 Au waweza wewe kukimbia mwendo mrefu kama kiongozi kipofu?

41 Au waweza wewe kuwa [a]mnyenyekevu na msikivu, na kujiendesha mwenyewe kwa hekima mbele zangu? Ndiyo, [b]uje kwangu Mimi Mwokozi wako. Amina.

SEHEMU YA 20

Ufunuo juu ya mfumo na utawala wa Kanisa, uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko au jirani na Fayette, New York. Sehemu ya ufunuo huu yawezekana kuwa ilikuwa imetolewa mapema zaidi katika kiangazi cha 1829. Ufunuo kamili, uliojulikana nyakati hizo kama Kanuni na Maagano, yawezekana yaliandikwa mara baada ya 6 Aprili 1830 (siku Kanisa lilipoanzishwa) Nabii aliandika, "Tulipata kutoka kwake Yeye [Yesu Kristo] yafuatayo, kwa roho wa unabii na ufunuo; ambayo siyo tu ilitupa sisi taarifa nyingi, lakini pia ilituonyesha siku sahihi ambayo, kulingana na mapenzi Yake na amri, ilitupasa kuendelea kuliunda Kanisa Lake mara nyingine hapa duniani."

1–16, Kitabu cha Mormoni huthibitisha utakatifu wa kazi ya siku za mwisho; 17–28, Mafundisho ya uumbaji, anguko, upatanisho na ubatizo yanathibitishwa; 29–37, Sheria zinazotawala toba, kuhesabiwa haki, na kutakasa, na ubatizo zatolewa; 38–67, Kazi za wazee, makuhani, walimu, na mashemasi zatolewa kwa muhtasari; 68–74, Kazi ya waumini, baraka za watoto, na mtindo wa ubatizo unafunuliwa; 75–84, Sala za Sakramenti na kanuni zinazotawala waumini wa Kanisa zinatolewa.

[a]Kuibuka kwa [b]Kanisa la Kristo katika siku hizi za mwisho, ikiwa ni miaka elfu moja mia nane na thelathini toka kuja kwa Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo katika mwili, likiwa kama kawaida [c]limeundwa na kuanzishwa kulingana na sheria za nchi yetu, kwa mapenzi na amri za Mungu, katika mwezi wa nne, na siku ya sita ya mwezi ambao unaitwa Aprili—

2 Amri ambazo alipewa Joseph Smith, Mdogo, ambaye

38 *a* Lk. 18:1; 2 Ne. 32:9; M&M 10:5.
b Mit. 1:23; Mdo. 2:17.

41 *a* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
b Mt. 11:28–30.

20 1 *a* JS—H 1:2.
b 3 Ne. 27:1–8.
MWM Kanisa, Jina la; Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.
c M&M 21:3.

[a]aliitwa na Mungu, na kutawazwa kuwa [b]mtume wa Yesu Kristo, kuwa [c]mzee wa kwanza wa kanisa hili;

3 Na kwa Oliver Cowdery, ambaye pia aliitwa na Mungu, mtume wa Yesu Kristo, kuwa mzee wa pili wa kanisa hili, na kutawazwa chini ya mikono yake;

4 Na hii ni kulingana na neema ya Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo, utukufu wote na uwe kwake, sasa na hata milele. Amina.

5 Baada ya kuwa imefunuliwa kwake mzee huyu wa kwanza kwamba amepokea ondoleo la dhambi zake, [a]alitatizwa tena na majivuno ya ulimwengu;

6 Lakini baada ya kutubu na kujinyenyekeza mwenyewe kwa moyo, kwa njia ya imani, Mungu alimhudumia kwa njia ya [a]malaika mtakatifu, ambaye [b]uso wake ilikuwa kama radi, na ambaye mavazi yake yalikuwa masafi na meupe kupita weupe wote;

7 Na akampa amri ambazo zilimvutia;

8 Na akampa uwezo kutoka juu, kwa [a]njia ambayo iliandaliwa mapema, ya kutafsiri Kitabu cha Mormoni;

9 Ambacho kina kumbukumbu ya watu walioanguka, na [a]utimilifu wa [b]injili ya Yesu Kristo kwa Wayunani na kwa Wayahudi pia;

10 Ambayo ilitolewa kwa maongozi, na imethibitishwa kwa [a]wengine kwa huduma za malaika, na [b]kuhubiriwa kwa walimwengu na wao—

11 Kuthibitisha kwa ulimwengu kwamba maandiko matakatifu ni ya [a]kweli, na kwamba Mungu [b]huwaongoza watu na kuwaita kwenye kazi yake [c]takatifu katika kipindi na kizazi hiki, kama vile katika vizazi vya kale;

12 Kwa hiyo akionyesha kwamba yeye ni Mungu [a]yeye yule jana, leo, na milele. Amina.

13 Kwa sababu hii, wakiwa mashahidi wakuu, kwa hao ulimwengu utahukumiwa, hata kadiri wengi baadaye watakavyo kuja kujua kazi hii.

14 Na wale ambao wanaipokea katika imani, na wakatenda kwa [a]haki, watapokea [b]taji la uzima wa milele;

15 Lakini wale ambao huishupaza mioyo yao katika [a]kutoamini, na kuikataa, itageuka kuwa laana kwao wenyewe—

16 Kwani Bwana Mungu amesema hivi; na sisi, wazee

2*a* MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito; Mamlaka.
b MWM Mtume.
c MWM Mzee.
5*a* JS—H 1:28–29.
6*a* JS—H 1:30–35. MWM Malaika.
b Mt. 28:2–3.
8*a* MWM Urimu na Thumimu.
9*a* JS—H 1:34.
b MWM Injili.
10*a* Moro. 7:29–32; M&M 5:11.
b Tazama Ushuhuda wa Mashahidi Watatu na Ushuhuda wa Mashahidi Wanane katika kurasa tangulizi za Kitabu cha Mormoni.
11*a* MWM Maandiko—Thamani ya maandiko.
b MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi.
c MWM Takatifu.
12*a* Ebr. 13:8; 1 Ne. 10:18–19; Morm. 9:9–10; M&M 35:1; 38:1–4.
14*a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
b MWM Kuinuliwa; Uzima wa Milele.
15*a* MWM Kutoamini.

wa kanisa, tumesikia na kutoa ushahidi kwa maneno ya mtukufu Mfalme aliye juu, utukufu na uwe kwake milele na milele. Amina.

17 Kwa mambo haya sisi [a]tunajua kwamba yuko [b]Mungu mbinguni, ambaye hana mwisho na wa milele, tangu milele hata milele yule yule Mungu asiyebadilika, aliyezifanya mbingu na dunia, na vitu vyote vilivyomo ndani yake;

18 Na kwamba [a]alimuumba mtu, mwanamume na mwanamke, kwa [b]sura na kwa mfano wake, aliwaumba;

19 Na akawapa wao amri kwamba inawapasa [a]kumpenda na [b]kumtumikia yeye, pekee aliye hai na Mungu wa kweli, na kwamba yapasa awe pekee wanayepaswa [c]kumwabudu.

20 Lakini kwa uvunjaji wa sheria hizi takatifu mwanadamu akawa mwenye [a]tamaa na [b]mwovu na akawa mwanadamu [c]aliyeanguka.

21 Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu akamtoa [a]Mwanawe wa Pekee, kama ilivyoandikwa katika yale maandiko ambayo yametolewa naye.

22 Akakumbwa na [a]majaribio lakini hakuyasikiliza;

23 [a]Akasulubiwa, akafa, na [b]akafufuka tena siku ya tatu;

24 Na [a]akapaa mbinguni, kukaa mkono wa kuume wa [b]Baba, kutawala kwa uwezo mkuu kulingana na mapenzi ya Baba;

25 Kwamba kadiri wengi watakavyo [a]amini na kubatizwa katika jina lake takatifu, na [b]kuvumilia katika imani hadi mwisho, wapate kuokolewa—

26 Siyo tu wale ambao waliamini baada ya kuja kwake [a]wakati wa meridiani, katika mwili, bali wale wote toka mwanzo, hata wengi waliokuwepo kabla ya kuja kwake, ambao waliamini katika maneno ya [b]manabii watakatifu, ambao walinena kama walivyoongozwa kwa [c]kipawa cha Roho Mtakatifu, ambaye hakika [d]alimshuhudia katika mambo yote, waweze kuwa na uzima wa milele,

27 Pia na wale ambao watakuja baadaye, ambao wataamini katika [a]vipawa na miito ya Mungu kwa Roho Mtakatifu, ambao [b]hutoa ushuhuda wa Baba na Mwana;

28 Ambao Baba, Mwana na

17 *a* M&M 76:22–23.
b Yos. 2:11. MWM Mungu, Uungu.
18 *a* MWM Umba, Uumbaji.
b Mwa. 1:26–27; Mos. 7:27; Eth. 3:14–17.
19 *a* Kum. 11:1; Mt. 22:37; Moro. 10:32; M&M 59:5–6.
b Kum. 6:13–15. MWM Utumishi.
c MWM Kuabudu.
20 *a* MWM Kupenda anasa, Matamanio ya anasa.
b MWM Ibilisi.
c MWM Mwanadamu wa Tabia ya Asili.
21 *a* MWM Mzaliwa Pekee.
22 *a* Mt. 4:1–11; 27:40.
23 *a* MWM Kusulubiwa.
b MWM Ufufuko.
24 *a* MWM Kupaa.
b MWM Baba wa Mbinguni; Mungu, Uungu—Mungu Baba.
25 *a* M&M 35:2; 38:4; 45:5, 8; 68:9; 76:51–53.
b MWM Stahimili.
26 *a* M&M 39:1–3.
b Yak. (KM) 4:4; 7:11; Mos. 13:33.
c Musa 5:58. MWM Roho Mtakatifu.
d MWM Yesu Kristo—Unabii juu ya Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo.
27 *a* M&M 18:32.
b M&M 42:17.

Roho Mtakatifu ni [a]Mungu mmoja, asiye na mwisho na wa milele, bila mwisho. Amina.

29 Na sisi tunajua kwamba watu wote lazima [a]watubu na kuamini kwa jina la Yesu Kristo, na kumwabudu Baba katika jina lake, na kuvumilia katika [b]imani kwa jina lake hadi mwisho, au hawawezi [c]kuokolewa katika ufalme wa Mungu.

30 Na tunajua kwamba [a]kuhesabiwa haki kwa njia ya [b]neema ya Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo ni haki na kweli;

31 Na tunajua pia, kwamba [a]utakaso kwa njia ya neema ya Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo ni haki na kweli, kwa wale wote ambao wanampenda na kumtumikia Mungu kwa [b]uwezo, akili na nguvu zao zote.

32 Lakini upo uwezekano kwamba mwanadamu akaweza [a]kuanguka kutoka katika hali ya neema, na kujitenga kutoka kwa Mungu aliye hai;

33 Kwa hiyo kanisa na lichukue tahadhari, na kusali daima, wasije wakaanguka [a]majaribuni;

34 Ndiyo, na hata wale waliotakaswa wachukue tahadhari vile vile.

35 Na tunajua kwamba mambo haya ni ya kweli na kulinganana na mafunuo ya Yohana, bila [a]kuongeza wala kupunguza kutoka katika unabii wa kitabu chake, [b]maandiko matakatifu, au mafunuo ya Mungu ambayo yatakuja hapo baadaye kwa kipawa na nguvu za Roho Mtakatifu, [c]sauti ya Mungu, au huduma za malaika.

36 Na Bwana Mungu amesema hilo; na heshima, nguvu na utukufu, utolewe kwa jina lake takatifu, sasa na milele. Amina.

37 *Na tena, kwa njia ya amri kwa kanisa kuhusiana na jinsi ya ubatizo*—Wale wote wenye kunyenyekea wenyewe mbele za Mungu, na kutamani [a]kubatizwa, na wakija na [b]mioyo iliyovunjika na roho zilizopondeka, na kushuhudia mbele ya kanisa kwamba hakika wametubu dhambi zao zote, na wako radhi kujichukulia juu yao [c]jina la Yesu Kristo, wakiwa na [d]dhamira ya kumtumikia hadi mwisho, na hakika wakithibitisha kwa [e]matendo yao kwamba wamempokea Roho wa Kristo kwa [f]msamaha wa dhambi zao, na wapokelewe kwa ubatizo katika kanisa lake.

38 *Kazi za wazee, makuhani, walimu, mashemasi, na waumini wa kanisa la Kristo*—[a]Mtume ni

28 *a* Yn. 17:20–22; 3 Ne. 11:27, 36. MWM Mungu, Uungu.
29 *a* MWM Toba, Tubu. *b* MWM Amini, Imani. *c* MWM Mpango wa Ukombozi; Wokovu.
30 *a* MWM Hesabu kwa haki, Kuhesabiwa haki. *b* MWM Neema.
31 *a* MWM Utakaso. *b* Kum. 6:5; Moro. 10:32.
32 *a* MWM Uasi; Ukengeufu.
33 *a* MWM Jaribu, Majaribu.
35 *a* Ufu. 22:18–19. *b* MWM Maandiko. *c* M&M 18:33–36.
37 *a* MWM Batiza, Ubatizo. *b* MWM Moyo Uliovunjika. *c* Mos. 5:7–9; 18:8–10. MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu. *d* MWM Stahimili. *e* Yak. (Bib.) 2:18. MWM Matendo. *f* MWM Ondoleo la Dhambi.
38 *a* MWM Mtume.

mzee, na ni wito wake [b]kubatiza;

39 Na [a]kuwatawaza wazee wengine, makuhani, walimu, na mashemasi;

40 Na [a]kuhudumia mkate na divai—ishara ya mwili na damu ya Kristo—

41 Na [a]kuwathibitisha wale wanaobatizwa katika kanisa, kwa kuwawekea [b]mikono kwa ajili ya ubatizo wa moto na [c]Roho Mtakatifu, kulingana na maandiko;

42 Na kufundisha, kuelezea, kushawishi, kubatiza, na kusimamia kanisa;

43 Na kulithibitisha kanisa kwa kuwekea mikono yao, na kutunukia Roho Mtakatifu;

44 Na kuchukua uongozi wa mikutano yote.

45 Wazee [a]wataendesha mikutano kadiri watakavyoongozwa na Roho Mtakatifu, kulingana na amri na mafunuo ya Mungu.

46 Kazi ya [a]kuhani ni kuhubiri, [b]kufundisha, kuelezea, kushawishi, na kubatiza, na kuhudumia sakramenti,

47 Na kutembelea nyumba ya kila muumini, na kuwashawishi [a]kusali kwa [b]sauti na kwa siri na kushiriki kazi zote za [c]familia.

48 Na anaweza pia [a]kuwatawaza makuhani wenzie, walimu, na mashemasi.

49 Na yeye atachukua uongozi wa mikutano endapo hakuna mzee katika mahali hapo;

50 Lakini akiwepo mzee, yeye ni wa kuhubiri tu, kufundisha, kuelezea, kushawishi na kubatiza,

51 Na kutembelea nyumba ya kila muumini, akihimiza kusali kwa sauti na sirini na kushiriki kwa kazi zote za familia.

52 Katika kazi hizi zote kuhani ni wa [a]kumsaida mzee kama itahitajika.

53 Kazi ya [a]mwalimu ni [b]kuliangalia kanisa daima, na kuwa nalo, na kuwaimarisha;

54 Na kuona kwamba hakuna uovu katika kanisa, wala [a]kuzozana baina yao, wala kudanganya, kusengenya, wala kusemana [b]mabaya;

55 Na kuona kwamba kanisa linakutana pamoja mara kwa mara, na pia kuona kwamba waumini wote wanatimiza wajibu wao.

56 Na atachukua uongozi wa mikutano ikiwa mzee na kuhani hawapo—

57 Na atasaidiwa daima, katika kazi zake zote katika kanisa, na [a]mashemasi, kama itahitajika.

58 Lakini, si walimu wala ma-

38 *b* 3 Ne. 11:21–22.
39 *a* Moro. 3; M&M 107:58.
40 *a* MWM Sakramenti.
41 *a* M&M 33:11, 14–15; 55:3.
b MWM Mikono, Kuweka juu ya.
c MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
45 *a* Moro. 6:9; M&M 46:2.
46 *a* M&M 84:111; 107:61. MWM Kuhani, Ukuhani wa Haruni.
b MWM Fundisha, Mwalimu.
47 *a* 1 Tim. 2:8.
b M&M 19:28.
c MWM Familia.
48 *a* MWM Kutawaza, Kutawazwa.
52 *a* M&M 107:14.
53 *a* MWM Mwalimu, Ukuhani wa Haruni.
b MWM Kesha, Walinzi.
54 *a* 1 The. 5:11–13.
b MWM Kusema uovu.
57 *a* MWM Shemasi.

shemasi walio na mamlaka ya kubatiza, kuhudumia Sakramenti, au kumwekelea mikono;

59 Wao, kwa hivyo ni wa kuwaonya, kuelezea, kushawishi, na kufundisha, na kuwakaribisha watu wote kuja kwa Kristo.

60 Kila [a]mzee, kuhani, mwalimu, au shemasi apaswa kutawazwa kufuatana na vipawa na [b]miito aliyopewa na Mungu; na atatawazwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, ambaye yu ndani ya yule mwenye kumtawaza.

61 Wazee kadha wanaounda hili kanisa la Kristo watakutana katika mkutano katika kila miezi mitatu, au mara kwa mara kama mikutano hiyo itakavyoelekeza au kuamuriwa;

62 Na mikutano hiyo iliyosemwa ni ya kufanya kazi yoyote ya kanisa iliyo muhimu kufanyika kwa wakati huo.

63 Wazee wanapaswa kupokea leseni zao kutoka kwa wazee wengine, kwa [a]kura ya kanisa ambako wanatoka, au kutoka kwenye mikutano.

64 Kila kuhani, mwalimu, au shemasi, ambaye ametawazwa na kuhani, anaweza kuchukua hati kutoka kwake wakati huo, [a]hati ambayo, ikitolewa kwa mzee, yaweza kumpa yeye haki ya kupewa leseni, ambayo itampa mamlaka yeye ya kufanya kazi za wito wake, au aweza kuipata kutoka mkutanoni;

65 Hakuna mtu [a]atakayetawazwa katika ofisi yoyote katika kanisa hili, mahali ambapo hakuna tawi la kanisa lililoanzishwa kiutaratibu, bila ya kupigiwa [b]kura na kanisa hilo;

66 Lakini wazee viongozi, maaskofu wanaosafiri, baraza kuu, makuhani wakuu, na wazee, wanaweza kuwa na haki ya kutawaza, mahali ambapo hakuna tawi la kanisa ambapo kura yaweza kuitishwa.

67 Kila rais wa ukuhani mkuu (au mzee kiongozi), [a]askofu, mjumbe wa baraza kuu, na [b]kuhani mkuu, anapaswa kutawazwa kwa maelekezo ya [c]baraza kuu au mkutano mkuu.

68 [a]*Kazi ya waumini baada ya kupokelewa kwa ubatizo*—Wazee au makuhani wanapaswa kuwa na muda wa kutosha wa kuelezea mambo yote kuhusu kanisa la Kristo kwa [b]ufahamu wao, kabla ya kupokea kwao [c]sakramenti na kuwa wamethibitishwa kwa kuwekewa [d]mikono ya wazee, ili kwamba mambo yote yaweze kufanyika katika utaratibu.

69 Na waumini wataonyesha mbele ya kanisa, na pia mbele za wazee, kwa mwenendo wa kiucha mungu na katika mazungumzo, kwamba wanastahili, ili paweze kuwa na [a]kazi na

60*a* MWM Mzee.
b MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito.
63*a* MWM Ridhaa ya Wengi.
64*a* M&M 20:84; 52:41.
65*a* MWM Kutawaza, Kutawazwa.
b M&M 26:2. MWM Ridhaa ya Wengi.
67*a* MWM Askofu.
b MWM Kuhani Mkuu.
c MWM Baraza Kuu.
68*a* MWM Wajibu.
b MWM Ufahamu.
c MWM Sakramenti.
d MWM Mikono, Kuweka juu ya.
69*a* Yak. (Bib.) 2:14–17.

imani inayokubaliana na maandiko matakatifu—wakienenda katika [b]utakatifu mbele za Bwana.

70 Kila muumini wa kanisa la Kristo mwenye watoto anapaswa kuwaleta kwa wazee mbele za kanisa, ambao wataweka mikono juu yao katika jina la Yesu Kristo, na [a]kuwabariki katika jina lake.

71 Hakuna yeyote anayeweza kupokelewa katika kanisa la Kristo isipokuwa amefikia katika umri wa [a]uwajibikaji mbele za Mungu, na mwenye uwezo wa [b]toba.

72 [a]Ubatizo yapaswa kufanyika katika njia ifuatayo kwa wale wote wanaotubu—

73 Mtu aliyeitwa na Mungu na mwenye mamlaka kutoka kwa Yesu Kristo ya kubatiza, ataingia katika maji pamoja na mtu aliyejileta mwenyewe kwa ajili ya ubatizo, naye atasema, akimwita kwa jina lake: Kwa mamlaka niliyopewa na Yesu Kristo, ninakubatiza katika jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

74 Ndipo [a]atamzamisha kabisa mtu huyo katika maji, na kumwinua kutoka majini.

75 Yafaa kwamba kanisa likutane pamoja mara kwa mara [a]kupokea mkate na divai katika [b]ukumbusho wake Bwana Yesu;

76 Na mzee au kuhani atahudumu; na kwa [a]njia hii atafanya—atapiga magoti pamoja na kanisa na kulingana Baba katika sala ya dhati, akisema:

77 Ee Mungu, Baba wa Milele, tunakuomba katika jina la Mwanao, Yesu Kristo, ubariki na utakase [a]mkate huu kwa roho za wale wote watakaoula, ili waweze kuula kwa ukumbusho wa mwili wa Mwanao, na [b]wakushuhudie, Ee Mungu, Baba wa Milele, kwamba wako radhi [c]kujichukulia juu yao jina la Mwanao, na daima kumkumbuka, na [d]kushika amri zake ambazo amewapa; ili daima [e]Roho wake apate kuwa pamoja nao. Amina.

78 [a]Namna ya kuhudumia divai—atachukua [b]kikombe pia, na atasema:

79 Ee Mungu, Baba wa Milele, tunakuomba katika jina la Mwanao, Yesu Kristo, ubariki na utakase [a]divai hii kwa roho za wale wote watakaoinywa, ili waweze kufanya kwa ukumbusho wa damu ya Mwanao, ambayo ilimwagwa kwa ajili yao; kwamba washuhudie kwako, Ee Mungu, Baba wa Milele, kwamba wamkumbuke, ili

69 *b* MWM Utakatifu.
70 *a* MWM Baraka, Bariki, Barikiwa—Baraka za watoto.
71 *a* M&M 18:42; 29:47; 68:25–27. MWM Batiza, Ubatizo—Sifa zinazotakiwa kwa ajili ya ubatizo; Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
b MWM Toba, Tubu.
72 *a* 3 Ne. 11:22–28.
74 *a* MWM Batiza, Ubatizo—Ubatizo kwa kuzamishwa.
75 *a* Mdo. 20:7.
b MWM Sakramenti.
76 *a* Moro. 4.
77 *a* Lk. 22:19.
b Mos. 18:8–10; M&M 20:37.
c Mos. 5:8–12.
d MWM Mtiifu, Tii, Utii.
e Yn. 14:16.
78 *a* Moro. 5.
b Lk. 22:20.
79 *a* M&M 27:2–4.

Roho wake apate kuwa pamoja nao. Amina.

80 Muumini yeyote katika kanisa la Yesu Kristo anayevunja, au kughafilika katika kosa, ashughulikiwe kulingana na maelekezo ya maandiko.

81 Utakuwa wajibu wa makanisa kadhaa, yanayounda kanisa la Kristo, kumpeleka mwalimu mmoja au zaidi kuhudhuria mikutano kadha wa kadha inayohudhuriwa na wazee wa kanisa,

82 Pamoja na orodha ya [a]majina ya waumini kadhaa wakijiunga pamoja na kanisa toka mkutano uliopita; au kupeleka kwa mikono ya kuhani; ili kwamba orodha ya kudumu ya majina yote ya kanisa zima iweze kutunzwa katika kitabu na mmoja wa wazee, yeyote yule ambaye wazee wengine watamchagua kila wakati;

83 Na pia, kama yeyote [a]ameondolewa kutoka katika kanisa, ili kwamba majina yao yaweze kufutwa kwenye kumbukumbu ya majina ya kanisa.

84 Waumini wote wakihama kutoka katika kanisa mahali wanapoishi, na kwenda kwenye kanisa mahali wasipojulikana, wanaweza kuchukua barua ikithibitisha kwamba wao ni waumini na kwamba ni waaminifu, hati ambayo inaweza kusainiwa na mzee yeyote au kuhani kama muumini atakayepokea barua hiyo anafahamiana na mzee au kuhani, au yaweza kusainiwa na walimu au mashemasi wa kanisa.

SEHEMU YA 21

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith, Nabii, huko Fayette, New York, 6 Aprili 1830. Ufunuo huu ulitolewa wakati wa kuanzisha Kanisa, katika tarehe iliyotajwa, katika nyumba ya Peter Whitmer Mkubwa. Wanaume sita, ambao walibatizwa hapo awali, walishiriki. Kwa kura nyingi watu hawa walionyesha kutaka kwao na dhamira ya kulianzisha, kulingana na amri ya Mungu (ona sehemu ya 20). Pia walipiga kura ya kuwakubali na kuwaunga mkono Joseph Smith Mdogo na Oliver Cowdery kama maofisa viongozi wa Kanisa. Kwa njia ya kuwawekea mikono, Joseph akamtawaza Oliver kuwa mzee wa Kanisa, na Oliver naye vile vile akamtawaza Joseph. Baada ya huduma ya Sakramenti, Joseph na Oliver wakawawekea mikono kila mtu aliyeshiriki kwa ajili ya kuwapa Roho Mtakatifu na kwa ajili ya uthibitisho wa kila mmoja kama muumini wa Kanisa.

1–3, Joseph ameitwa kuwa mwonaji, mfasiri, nabii, mtume, na mzee; 4–8, Neno lake litaiongoza kusudi la Sayuni; 9–12, Watakatifu

82*a* Moro. 6:4.
83*a* Ku. 32:33; Alma 5:57; Moro. 6:7.

MWM Kutengwa na Kanisa.

wataamini maneno yake atakavyoongea akiwa anaongozwa na Mfariji.

Tazama, pawepo na [a]kumbukumbu itakayotunzwa miongoni mwenu; ambamo ndani yake utaitwa [b]mwonaji, mfasiri, nabii, [c]mtume wa Yesu Kristo, mzee wa kanisa kwa njia ya mapenzi ya Mungu Baba, na neema ya Bwana wenu Yesu Kristo,

2 Ukiwa [a]unaongozwa na Roho Mtakatifu katika kuweka msingi wake, na kulijenga juu ya imani iliyo takatifu sana.

3 [a]Kanisa ambalo [b]liliundwa na kuanzishwa katika mwaka wa Bwana wenu elfu moja mia nane na thelathini, katika mwezi wa nne, na siku ya sita ya mwezi ambao unaitwa Aprili.

4 Kwa hivyo, nikimaanisha kanisa, nawe utayaangalia [a]maneno yake yote na amri ambazo atazitoa kwenu kadiri atakavyozipokea, mkitembea katika [b]utakatifu mbele zangu;

5 Kwani [a]neno lake mtalipokea, kama vile linatoka kinywani mwangu, katika uvumilivu wote na imani yote.

6 Kwani kwa kufanya mambo haya [a]milango ya jehanamu haitawashinda; ndiyo, na Bwana Mungu atazitawanya nguvu za [b]giza kutoka mbele zako, naye atasababisha mbingu [c]zitetemeke kwa ajili yenu, na kwa [d]utukufu wa jina lake.

7 Kwani hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu: Yeye nimemwongoza kuendesha kusudi la [a]Sayuni katika uwezo mwingi kwa ajili ya mema, na juhudi yake ninaijua, na sala zake nimezisikia.

8 Ndiyo, maombolezo yake kwa ajili ya Sayuni nimeyaona, na Mimi nitasababisha kwamba asiomboleze tena kwa ajili yake; kwani siku zake za kufurahi zimekuja kwa [a]ondoleo la dhambi zake, na kufunua baraka zangu juu ya kazi zake.

9 Kwani, tazama, Mimi [a]nitawabariki wale wote watakaofanya kazi katika [b]shamba langu la mizabibu kwa baraka kuu, na wao watayaamini maneno yake, ambayo yanatolewa kwake kutoka kwangu na [c]Mfariji, ambaye [d]hufunulia kwamba Yesu [e]alisulubishwa na watu wenye [f]dhambi kwa ajili ya dhambi za [g]ulimwengu, ndiyo, kwa ajili ya ondoleo la dhambi na kwa wenye [h]moyo ulioponde ka.

21 1*a* M&M 47:1; 69:3–8; 85:1.
b MWM Mwonaji.
c MWM Mtume.
2*a* MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi.
3*a* MWM Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.
b M&M 20:1.
4*a* MWM Maandiko.
b MWM Utakatifu.
5*a* M&M 1:38. MWM Kuwakubali Viongozi wa Kanisa; Nabii.
6*a* Mt. 16:18; M&M 10:69.
b Kol. 1:12–13.
c M&M 35:24.
d MWM Utukufu.
7*a* MWM Sayuni.
8*a* M&M 20:5–6.
9*a* 1 Ne. 13:37; Yak. (KM) 5:70–76.
b MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
c MWM Mfariji.
d MWM Shuhudia.
e MWM Kusulubiwa.
f MWM Dhambi.
g 1 Yoh. 2:2. MWM Ulimwengu—Watu wasiotii amri.
h MWM Moyo Uliovunjika.

10 Kwa hiyo nimeona ni muhimu kwa yeye [a]kutawazwa na wewe, Oliver Cowdery mtume wangu;

11 Hii ikiwa ni ibada kwako wewe, kwamba wewe u mzee chini ya mkono wake, akiwa wa [a]kwanza mbele yako wewe, kwamba uwe mzee katika kanisa hili la Kristo, lililo na jina langu—

12 Na mhubiri wa kwanza wa kanisa hili kwa ajili ya kanisa, na mbele ya ulimwengu, ndiyo, mbele ya Wayunani; ndiyo, na hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu, lo, lo! na kwa [a]Wayahudi pia. Amina.

SEHEMU YA 22

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Manchester, New York, 16 Aprili 1830. Ufunuo huu ulitolewa kwa Kanisa katika matokeo ya baadhi ya watu waliobatizwa hapo awali wakitamani kuungana na Kanisa bila ya kubatizwa tena.

1, Ubatizo ni agano jipya na lisilo na mwisho; 2–4, Ubatizo wenye mamlaka unahitajika.

Tazama, ninawaambia kwamba maagano yote ya [a]zamani nimeyaondoa katika jambo hili; na hili ni agano [b]jipya na lisilo na mwisho, hata lile lililokuweko tangu mwanzo.

2 Kwa hivyo, hata kama mwanadamu angebatizwa mara mia haitamfaa lolote, kwani hamuwezi kuingia kwa kupitia mlango mwembamba kwa [a]torati ya Musa, wala kwa [b]kazi zenu zisizo na uhai.

3 Kwani ni kwa sababu ya kazi zenu zisizo na uhai kwamba nimefanya agano hili la mwisho na kanisa hili lijengwe kwa ajili yangu, kama ilivyokuwa katika siku za kale.

4 Kwa hivyo, ingieni ninyi katika [a]mlango, kama nilivyoamuru, na wala [b]msitake kumshauri Mungu wenu. Amina.

SEHEMU YA 23

Mfululizo wa mafunuo matano yaliyotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Manchester, New York, Aprili 1830, kwa Oliver

10 *a* MWM Kutawaza, Kutawazwa.
11 *a* M&M 20:2.
12 *a* 1 Ne. 13:42; M&M 19:27; 90:8–9.
22 1 *a* Ebr. 8:13; 3 Ne. 12:46–47.
b M&M 66:2.
MWM Agano; Agano Jipya na Lisilo na Mwisho.
2 *a* Gal. 2:16.
MWM Torati ya Musa.
b Moro. 8:23–26.
4 *a* Mt. 7:13–14; Lk. 13:24; 2 Ne. 9:41; 31:9, 17–18; 3 Ne. 14:13–14.
MWM Batiza, Ubatizo.
b Yak. (KM) 4:10.

Cowdery, Hyrum Smith, Samuel H. Smith, Joseph Smith Mkubwa, na Joseph Knight Mkubwa. Kama matokeo ya matamanio ya dhati ya watu hawa watano waliotajwa ya kutaka kujua wajibu wao, Nabii alimwuliza Bwana na kupokea ufunuo kwa ajili ya kila mtu.

1–7, Wanafunzi hawa wa mwanzo wameitwa kuhubiri, kushawishi, na kuliimarisha Kanisa.

Tazama, ninasema na wewe Oliver, maneno machache. Tazama, wewe umebarikiwa, na huna hatia yoyote. Lakini jihadhari na [a]majivuno, usije ukaingia [b]majaribuni.

2 Fanya wito wako ujulikane kwa kanisa, na pia mbele ya ulimwengu, nao moyo wako utafunguliwa kuhubiri ukweli tangu leo na hata milele. Amina.

3 Tazama, ninasema na wewe, Hyrum, maneno machache; kwani na wewe pia huna hatia yoyote, na moyo wako umefunguliwa, na ulimi wako umelegezwa; na wito wako ni wa kushawishi, na [a]kuliimarisha kanisa daima. Kwa hivyo wajibu wako ni kwa kanisa milele, na hii ni kwa sababu ya familia yako. Amina.

4 Tazama, ninasema na wewe maneno machache, [a]Samuel; kwani na wewe pia huna hatia yoyote, na wito wako ni wa kushawishi, na kuliimarisha kanisa; na wewe bado hujaitwa kuhubiri mbele za ulimwengu. Amina.

5 Tazama, ninasema kwako maneno machache, Joseph; kwani na wewe pia huna hatia yoyote, na wito wako pia ni wa kushawishi, na kuliimarisha kanisa; na huu ndiyo wajibu wako tangu leo hata milele. Amina.

6 Tazama, ninakufunulia wewe, Joseph Knight, kwa maneno haya, kwamba wewe lazima ujitwike [a]msalaba wako, kwamba ni lazima [b]uombe kwa [c]sauti mbele ya ulimwengu na pia sirini, na katika familia yako, na miongoni mwa marafiki zako, na katika mahali pote.

7 Na, tazama, ni wajibu wako [a]kuungana na kanisa la kweli, na utoe lugha yako kwa kushawishi daima, ili kwamba uweze kupokea ujira wa mfanya kazi. Amina.

SEHEMU YA 24

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Oliver Cowdery, huko Harmony, Pennsylvania, Julai 1830. Ijapokuwa si zaidi ya miezi minne kupita toka Kanisa lianzishwe, mateso yamekuwa makali,

23 1*a* mwm Kiburi.
b mwm Jaribu, Majaribu.
3*a* M&M 81:4–5; 108:7.
4*a* JS—H 1:4.
6*a* Mt. 10:38; 3 Ne. 12:30.
b mwm Sala.
c M&M 20:47, 51.
7*a* mwm Batiza, Ubatizo—Muhimu.

na viongozi iliwabidi watafute usalama kwa kujitenga na wengine. Mafunuo matatu yanayofuata yalitolewa kwa wakati huo ili kuwaimarisha, kuwahamasisha, na kuwaelekeza.

1–9, Joseph Smith ameitwa ili kutafsiri, kuhubiri, na kuelekezea maandiko; 10–12, Oliver Cowdery ameitwa ili kuhubiri injili; 13–19, Sheria imefunuliwa kuhusiana na miujiza, laana, kukung'uta mavumbi ya miguu, na kwenda pasipo mfuko wala mkoba.

Tazama, wewe uliitwa na kuteuliwa kuandika Kitabu cha Mormoni, na katika huduma yangu; nami nimekutoa katika dhiki zako, na nimekushauri, nikisema kwamba umeponywa kutoka kwa maadui zako, na wewe umeponywa kutoka katika nguvu za Shetani na za giza!

2 Hata hivyo, wewe huna udhuru katika [a]uvunjaji wako wa sheria; kwa hivyo, enenda zako, wala usitende dhambi tena.

3 [a]Itukuze ofisi iliyo yako; na baada ya kuwa umepanda mashamba yako na kuyalinda, nenda haraka katika kanisa lililoko [b]Colesville, Fayette, na Manchester, na wao [c]watakukimu; na Mimi nitawabariki vyote kiroho na kimwili;

4 Lakini kama hawatakupokea wewe, nitapeleka juu yao laana badala ya baraka.

5 Na wewe utaendelea katika kumlingana Mungu katika jina langu, na kuandika mambo ambayo yatatolewa kwako na [a]Mfariji, na kuelezea maandiko yote kwa kanisa.

6 Na itatolewa kwako saa ile ile [a]utakayosema na kuandika, na wao watayasikia, au nitapeleka juu yao laana badala ya baraka.

7 Kwani wewe utajitolea [a]utumishi wako wote katika Sayuni; na katika hili, utakuwa na nguvu.

8 Kuwa [a]mvumilivu katika [b]mateso, kwani utapata mengi; lakini [c]utayastahimili, kwani, lo, Mimi nipo pamoja nawe, hata [d]mwisho wa siku zako.

9 Na kazi za kimwili wewe hutakuwa na nguvu, kwani, huo siyo wito wako. Tekeleza [a]wito wako ambao unao kwa kuitukuza ofisi uliyo nayo, na kuyaelezea maandiko yote, na kuendelea katika kuwawekea mikono na kuyathibitisha makanisa.

10 Na ndugu yako Oliver ataendelea katika kulichukua jina langu mbele ya ulimwengu, na pia kwa kanisa. Na hapaswi kudhani kwamba ataweza kusema ya kutosha katika kazi

24 2*a* M&M 1:31–32.
3*a* Yak. (KM) 1:19; 2:2.
b M&M 26:1; 37:2.
c M&M 70:12.
5*a* mwm Mfariji.
6*a* Ku. 4:12; Mt. 10:19–20; Lk. 12:11–12; Hel. 5:18–19; M&M 84:85; 100:5–8; Musa 6:32.
7*a* mwm Utumishi.
8*a* mwm Subira.
b mwm Shida.
c mwm Stahimili.
d Mt. 28:20.
9*a* mwm Msimamizi, Usimamizi.

yangu; na lo, Mimi nipo pamoja na yeye hata mwisho.

11 Ndani yangu atapata utukufu, na siyo kutoka kwake mwenyewe, iwe katika udhaifu au katika nguvu, iwe katika utumwa au huru;

12 Na kwa nyakati zote, na katika mahali pote, yeye atafumbua kinywa chake na [a]kutangaza injili yangu kama vile kwa sauti ya [b]baragumu, usiku na mchana. Na nitampa yeye nguvu ambazo hazijawahi kujulikana miongoni mwa wanadamu.

13 Usiombe [a]miujiza, ila [b]nitakapokuamuru, isipokuwa kwa [c]kutoa [d]mapepo, [e]kuwaponya wagonjwa, na dhidi ya nyoka wenye [f]sumu, na dhidi ya sumu zenye kufisha;

14 Na [a]mambo haya usiyafanye, isipokuwa utakapohitajika kufanya na wale wenye kutaka, ili kwamba maandiko yapate kutimia; kwani itakupasa kufanya kulingana na yale yaliyoandikwa.

15 Na katika mahali popote [a]mtakapoingia, na wasipo wakaribisha katika jina langu, mtaacha laana badala ya baraka, kwa kukung'uta [b]vumbi la miguu yenu dhidi yao kama ushuhuda, na kusafisha miguu yenu njiani.

16 Na itakuwa kwamba yeyote atakayeweka mikono yake juu yenu akiwakamata kwa fujo, mtaamuru apigwe katika jina langu, na, tazama nitawapiga kulingana na maneno yako, katika wakati wangu mwenyewe.

17 Na yeyote atakaye wapeleka mbele ya sheria atalaaniwa kwa sheria.

18 Na msichukue [a]mfuko wala mkoba, wala fimbo, wala makoti mawili, kwani kanisa litawapatia katika saa ile ile mtakapohitaji chakula na mavazi, na kwa viatu na kwa fedha, na kwa mkoba.

19 Kwani wewe umeitwa [a]kupogoa shamba langu la mizabibu kwa kupogoa kwenye nguvu, ndiyo, hata kwa mara ya mwisho; ndiyo, na pia kwa wale wote ambao wewe [b]umewatawaza, na watafanya kulingana na utaratibu huu. Amina.

SEHEMU YA 25

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Harmony, Pennsylvania, Julai 1830 (ona kichwa cha habari cha sehemu ya 24).

12 *a* MWM Hubiri.
b M&M 34:6.
13 *a* MWM Ishara; Muujiza.
b 1 Ne. 17:50.
c Mk. 16:17.
d MWM Roho—Pepo wachafu.
e MWM Ponya, Uponyaji.
f Mdo. 28:3–9; M&M 84:71–72; 124:98–99.
14 *a* MWM Huduma kwa Wagonjwa.
15 *a* Mt. 10:11–15.
b Mk. 6:11; Lk. 10:11; M&M 60:15; 75:19–22; 99:4–5.
18 *a* Mt. 10:9–10; Lk. 10:4; M&M 84:78–79.
19 *a* Yak. (KM) 5:61–74; M&M 39:17; 71:4.
b MWM Kutawaza, Kutawazwa.

Ufunuo huu ulionyesha mapenzi ya Bwana kwa Emma Smith, mke wa Nabii.

1–6, Emma Smith, bibi mteule, anaitwa kumsaidia na kumfariji mume wake; 7–11, Yeye pia ameitwa kuandika, kuelezea maandiko, na kuchagua nyimbo; 12–14, Wimbo wa mwenye haki ni sala kwa Bwana; 15–16, Kanuni za Utii katika ufunuo huu inatumika kwa wote.

Sikiliza sauti ya Bwana Mungu wako, wakati ninapoongea na wewe, Emma Smith, binti yangu; kwani amini ninakuambia, wale wote ambao [a]huipokea injili yangu ni wana na mabinti katika [b]ufalme wangu.

2 Ufunuo ninautoa kwako kuhusiana na mapenzi yangu; na endapo wewe utakuwa mwaminifu na [a]kuenenda katika njia za [b]haki mbele zangu, nitayalinda maisha yako, na wewe utapata [c]urithi katika Sayuni.

3 Tazama, [a]dhambi zako zimesamehewa, na wewe u bibi mteule, ambaye [b]nimekuita.

4 Usinung'unike kwa sababu ya vitu ambavyo wewe hujaviona, kwani vimezuiliwa kwako na kwa ulimwengu, ambayo ni hekima kwangu katika wakati ujao.

5 Na ofisi ya wito wako itakuwa kwa [a]faraja ya mtumishi wangu, Joseph Smith, Mdogo, mume wako, katika mateso yake, kwa maneno ya faraja, katika roho wa unyenyekevu.

6 Na wewe utakwenda naye wakati wa kuondoka kwake, na uwe mwandishi wake, wakati pakiwa hakuna mtu wa kuandika kwa ajili yake, ili niweze kumtuma mtumishi wangu, Oliver Cowdery, kokote nipendako.

7 Na wewe [a]utatawazwa chini ya mikono yake kuyaelezea maandiko, na kushawishi kanisa, kadiri Roho wangu atakavyokujalia.

8 Kwani yeye ataweka [a]mikono yake juu yako, nawe utampokea Roho Mtakatifu, na muda wako utatumika katika kuandika, na kujifunza mengi.

9 Nawe hutakiwi kuogopa, kwani mume wako atakusadia katika kanisa; kwani kwao ndiyo [a]wito wake, ili kwamba mambo yote yaweze [b]kufunuliwa kwao, lolote nitakalo kulingana na imani yao.

10 Na amini ninakuambia wewe kwamba uyaweke kando

25 1*a* Yn. 1:12.
mwm Wana na Mabinti za Mungu.
b mwm Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
2*a* mwm Tembea, Tembea na Mungu.
b mwm Wema.
c M&M 52:42; 64:30; 101:18.
mwm Sayuni.
3*a* Mt. 9:2.
b mwm Ita, Itwa na Mungu, Wito.
5*a* mwm Huruma.
7*a* au simika.
mwm Usimikaji.
8*a* mwm Mikono, Kuweka juu ya.
9*a* mwm Ita, Itwa na Mungu, Wito; Nabii.
b mwm Toa unabii, Unabii; Ufunuo.

[a]mambo ya [b]ulimwengu huu, na [c]kuyatafuta mambo ya ulimwengu ulio bora.

11 Na itatolewa kwako, pia, kufanya uchaguzi wa [a]nyimbo takatifu, kama itakavyotolewa kwako, zile zenye kunipendeza Mimi, ili ziimbwe katika kanisa langu.

12 Kwani nafsi yangu hufurahia katika [a]nyimbo za [b]moyoni; ndiyo, wimbo wa mwenye haki ni sala kwangu Mimi, nayo itajibiwa kwa baraka juu ya vichwa vyao.

13 Kwa hiyo, inua moyo wako na ufurahie, na uyashikilie maagano ambayo umeyafanya.

14 Endelea katika roho wa [a]unyenyekevu, na jihadhari na [b]majivuno. Acha nafsi yako ifurahie katika mume wako, na utukufu ule ambao utakuja juu yake.

15 Shika amri zangu daima, na [a]taji la [b]haki utalipokea. Na bila wewe kufanya hivyo, mahali Mimi nilipo wewe [c]hutaweza kuja.

16 Na amini, amini, ninakuambia, kwamba hii ni [a]sauti yangu kwa wote. Amina.

SEHEMU YA 26

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, Oliver Cowdery, na John Whitmer, huko Harmony, Pennsylvania, Julai 1830 (ona kichwa cha habari cha sehemu ya 24).

1, Wameelekezwa kujifunza maandiko na kuhubiri; 2, Sheria ya maoni ya wengi yathibitishwa.

Tazama, ninawaambia kwamba muda wenu na utumike kwa [a]kujifunza maandiko, na kuhubiri, na kwa kuthibitisha kanisa huko [b]Colesville, na kufanya kazi zenu katika nchi, kama vile inavyotakiwa, hadi baada ya kwenda kule magharibi kufanya mkutano ujao; na ndipo itakapojulikana nini mtakachofanya.

2 Na mambo yote yafanyike kwa [a]kauli ya pamoja katika kanisa, kwa sala nyingi na imani, kwani mambo yote mtayapokea kwa imani. Amina.

SEHEMU YA 27

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith, Nabii, huko Harmony,

10*a* mwm Tamani; Ukwasi.
b mwm Malimwengu.
c Eth. 12:4.
11*a* mwm Wimbo.
12*a* 1 Nya. 16:9.
mwm Imba.
b mwm Moyo.
14*a* mwm Pole, Upole.
b mwm Kiburi.
15*a* mwm Kuinuliwa; Taji.
b mwm Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
c Yn. 7:34.
16*a* M&M 1:38.
26 1*a* mwm Maandiko—Thamani ya maandiko.
b M&M 24:3; 37:2.
2*a* 1 Sam. 8:7; Mos. 29:26.
mwm Ridhaa ya Wengi.

Pennsylvania, Agosti 1830. Katika maandalizi ya ibada ambapo sakramenti ya mkate na divai ilikuwa itolewe, Joseph alikuwa akienda kununua divai. Alikutana na mjumbe kutoka mbinguni na akapokea ufunuo huu, ambao sehemu yake iliandikwa wakati huo, na iliyosalia iliandikwa mwezi uliofuata wa Septemba. Maji sasa yanatumika badala ya divai katika ibada ya sakramenti ya Kanisa.

1–4, Ishara zitakazotumika kupokea sakramenti zinaelezwa; 5–14, Kristo na watumishi Wake kutoka nyakati zote wanapokea Sakramenti; 15–18, Vaeni silaha za Mungu.

Sikilizeni sauti ya Yesu Kristo, Bwana wenu, Mungu wenu, na Mkombozi wenu, ambaye neno lake ni la [a]haraka na lenye nguvu.

2 Kwani, tazama, ninawaambia, kwamba si muhimu ni nini utakachokunywa au utakachokula wakati unapopokea [a]sakramenti, ili mradi kwamba unafanya hayo kwa jicho likiwa kwenye [b]utukufu wangu pekee—mkikumbuka kwa Baba mwili wangu uliotolewa kwa ajili yenu, na [c]damu yangu iliyomwangwa kwa [d]ondolea la dhambi zenu.

3 Kwa hiyo, amri ninakupa, kwamba usinunue divai wala kinywaji kikali cha adui zako;

4 Kwa hiyo, msipokee chochote isipokuwa kimetengenezwa upya miongoni mwenu; ndiyo, katika huu ufalme wa Baba yangu ambao utajengwa hapa duniani.

5 Tazama, hii ni hekima kwangu; kwa hiyo, usistaajabie, kwani saa yaja ambayo [a]nitakunywa matunda ya mvinyo pamoja nanyi duniani, na pamoja na [b]Moroni, ambaye nilimtuma kwako kufichua Kitabu cha Mormoni, chenye utimilifu wa injili yangu isiyo na mwisho, ambaye nimemkabidhi funguo za kumbukumbu ya [c]fimbo ya Efraimu;

6 Na pia [a]Elia, ambaye nimemkabidhi funguo za kukamilisha urejesho wa mambo yote yaliyonenwa kwa vinywa vya manabii watakatifu tangu mwanzo wa ulimwengu, kuhusu siku za mwisho;

7 Na pia Yohana mwana wa Zakaria, Zakaria ambaye yeye [a](Elia) alimtembelea na kumpa ahadi kwamba atapata mwana, na jina lake litakuwa [b]Yohana, na yeye atakuwa amejazwa na roho ya Elia;

8 Yohana ambaye nimekwisha mtuma kwenu ninyi, watumishi

27 1*a* Hel. 3:29; M&M 6:2.
2*a* MWM Sakramenti.
b MWM Utukufu.
c MWM Damu.
d MWM Ondoleo la Dhambi.
5*a* Mt. 26:29; Mk. 14:25; Lk. 22:18.
b JS—H 1:30–34.
c Eze. 37:16. MWM Efraimu—Kijiti cha Efraimu au Yusufu.
6*a* MWM Elia.
7*a* Lk. 1:17–19.
b Lk. 1:13; M&M 84:27–28.

wangu Joseph Smith, Mdogo, na Oliver Cowdery, kuwatawaza ninyi katika [a]ukuhani wa kwanza ambao mmeupokea, ili kwamba muwe mmeitwa na [b]kutawazwa kama ilivyokuwa hata kama [c]Haruni.

9 Na pia [a]Eliya, ambaye kwake nimemkabidhi funguo za uwezo wa [b]kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na mioyo ya watoto kwa baba, ili kwamba dunia yote isiweze kupigwa kwa laana.

10 Na pia pamoja na Yusufu na Yakobo, na Isaka, na Ibrahimu, baba zako, ambao hao [a]ahadi zinabakia;

11 Na pia Mikaeli, au [a]Adamu, baba wa wote, mtawala wa wote, mzee wa siku;

12 Na pia pamoja na Petro, na Yakobo, na Yohana, ambao niliwatuma kwako, kwa wao [a]nimekutawazeni ninyi na kuwathibitisha kuwa [b]mitume, na [c]mashahidi maalumu wa jina langu, na kuchukua funguo za huduma yenu, na mambo yale yale niliyowafunulia wao;

13 Kwako wewe [a]nimekukabidhi [b]funguo za ufalme wangu, na [c]kipindi cha [d]injili kwa [e]nyakati za mwisho; na kwa [f]utimilifu wa nyakati, ambao ndani yake nitayakusanya [g]pamoja mambo yote, yaliyoko mbinguni na yaliyoko duniani;

14 Na pia wale wote ambao Baba yangu [a]amenipa mimi nje ya ulimwengu.

15 Kwa hiyo, inua moyo wako na ufurahie, na funga viuno vyako, na jitwalie [a]deraya zangu zote, upate kushindana siku ya uovu, na ukiisha kuyatimiza yote, uweze [b]kusimama.

16 Kwa hiyo, simama, ukiwa [a]umejifunga na [b]ukweli kiunoni, na kuvaa [c]dirii ya [d]haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa injili ya [e]amani, ambayo nimemtuma [f]malaika wangu kuikabidhi kwako;

17 Mkitwaa ngao ya imani ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye [a]moto ya adui;

18 Na chukueni helmeti ya wokovu, na upanga wa Roho yangu, ambayo nitaimwaga juu yenu, na neno langu ambalo ninalifunua kwenu, na mpatane

8 *a* M&M 13. MWM Ukuhani wa Haruni.
b MWM Kutawaza, Kutawazwa.
c Ku. 28:1–3, 41; M&M 107:13.
9 *a* 1 Fal. 17:1–22; 2 Fal. 1–2; M&M 2; 110:13–16; JS—H 1:38–39. MWM Eliya.
b MWM Nasaba.
10 *a* MWM Agano la Ibrahimu.
11 *a* MWM Adamu.
12 *a* JS—H 1:72. MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
b MWM Mtume.
c Mdo. 1:8.
13 *a* Mt. 16:19.
b MWM Funguo za Ukuhani.
c MWM Kipindi.
d MWM Injili.
e Yak. (KM) 5:71; M&M 43:28–30.
f Efe. 1:9–10; M&M 112:30; 124:41.
g M&M 84:100.
14 *a* Yn. 6:37; 17:9, 11; 3 Ne. 15:24; M&M 50:41–42; 84:63.
15 *a* Rum. 13:12; Efe. 6:11–18.
b Mal. 3:2; M&M 87:8.
16 *a* Isa. 11:5.
b MWM Ukweli.
c Isa. 59:17.
d MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
e 2 Ne. 19:6.
f M&M 128:19–21.
17 *a* 1 Ne. 15:24; M&M 3:8.

kuhusiana na jambo lolote mtakaloniomba Mimi, na kuweni waaminifu mpaka nijapo Mimi, na ninyi [a]mtanyakuliwa, ili nilipo Mimi nanyi muwepo [b]pia. Amina.

SEHEMU YA 28

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Oliver Cowdery, huko Fayette, New York, Septemba 1830. Hiram Page, muumini wa Kanisa, alikuwa na jiwe fulani na kudai kuwa kunapokea mafunuo kwa msaada wa jiwe hilo kuhusiana na ujenzi wa Sayuni na taratibu za Kanisa. Waumini kadhaa walikuwa wamedanganyika kwa madai haya, na hata Oliver Cowdery alishawishika vibaya kwa hilo. Muda mfupi kabla ya mkutano, Nabii alimwuliza Bwana kwa bidii kuhusiana na jambo hili, na ufunuo huu ulifuata.

1–7, Joseph Smith hushikilia funguo za siri, na ndiye pekee mwenye kupokea ufunuo kwa Kanisa; 8–10, Oliver Cowdery anapaswa kwenda kuwafundisha Walamani; 11–16, Shetani alimdanganya Hiram Page na kumpa mafunuo ya uongo.

Tazama, ninakuambia wewe, [a]Oliver, kwamba itatolewa kwako kwamba utasikilizwa na kanisa katika mambo yote ambayo wewe [b]utawafundisha kwa uwezo wa [c]Mfariji, kuhusu mafunuo na amri ambazo nimezitoa.

2 Lakini tazama, amini, amini, ninakuambia, [a]hakuna mtu atakayeteuliwa kupokea amri na mafunuo katika kanisa hili isipokuwa mtumishi wangu [b]Joseph Smith, Mdogo, kwani yeye huzipokea kama vile Musa.

3 Na wewe uwe mtiifu kwa mambo ambayo nitampa yeye, kama vile [a]Haruni, kuzitangaza kiuaminifu amri hizi na mafunuo, kwa nguvu na [b]mamlaka kwenyea kanisa.

4 Na endapo wewe utaongozwa kwa wakati wowote na Mfariji [a]kuzungumza au kufundisha, au kwa nyakati zote kwa njia ya amri kwa kanisa, waweza kufanya hivyo.

5 Lakini usiliandike kwa njia ya amri, bali kwa hekima;

6 Na wewe usimwamuru yeyote aliye juu yako, na juu ya kanisa;

7 Kwani Mimi nimempa yeye kuzungumza [a]funguo za [b]siri, na

18*a* 1 Ne. 13:37; M&M 17:8.
b Yn. 14:3.
28 1*a* M&M 20:3.
b mwm Fundisha, Mwalimu—Kufundisha kwa Roho.
c mwm Mfariji.
2*a* M&M 35:17–18; 43:4.
b 2 Ne. 3:14–20. mwm Smith, Joseph, Mdogo.
3*a* mwm Haruni, Kaka wa Musa.
b mwm Mamlaka.
4*a* Ku. 4:12–16; M&M 24:5–6.
7*a* M&M 64:5; 84:19.
b mwm Siri za Mungu.

mafunuo ambayo yamefungwa, hadi hapo nitakapomteua mwingine kwa ajili yao badala yake.

8 Na sasa, tazama, ninakuambia kwamba utakwenda kwa [a]Walamani na kuhubiri [b]injili yangu kwao; na kadiri wao watakavyopokea mafundisho yako na wewe utalifanya kanisa langu kuanzishwa miongoni mwao; na wewe utapata mafunuo, walakini usiyaandike kwa njia ya amri.

9 Na sasa, tazama, ninakuambia kwamba haijafunuliwa bado, na hakuna mtu ajuaye mahali [a]mji wa [b]Sayuni utakapojengwa, lakini itatolewa hapo baadaye. Tazama, ninakuambia kwamba itakuwa mipakani mwa Walamani.

10 Na wewe usiondoke mahali hapa mpaka baada ya mkutano, na mtumishi wangu Joseph Smith atateuliwa kuongoza mkutano huo kwa sauti ya mkutano na atakalolisema kwako na wewe utalisema.

11 Na tena, wewe utamchukua ndugu yako Hiram Page, [a]kati yake na wewe peke yenu, na umwambie kwamba yale mambo aliyoyaandika kutoka kwenye jiwe lile siyo yangu na kwamba [b]Shetani [c]anamdanganya;

12 Kwani, tazama, mambo haya hayakuchaguliwa kwake, wala hakuna lolote lililoteuliwa kwa yeyote katika kanisa hili kinyume na maagano ya kanisa.

13 Kwani mambo yote, lazima yafanyike katika utaratibu, na kwa [a]ridhaa ya wengi katika kanisa, na kwa sala ya imani.

14 Na wewe utasaidia kurekebisha mambo haya yote, kulingana na maagano ya kanisa, kabla ya kufanya safari yako miongoni mwa Walamani.

15 Na [a]itatolewa kwako tangu wakati utakapoondoka, hadi wakati utakaporejea, juu ya nini utakachofanya.

16 Na wewe utafumbua kinywa chako nyakati zote, ukitangaza injili yangu kwa sauti ya kufurahi. Amina.

SEHEMU YA 29

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, mbele ya wazee sita, huko Fayette, New York, Septemba 1830. Ufunuo huu ulitolewa siku kadhaa kabla ya mkutano, kuanzia 26 Septemba 1830.

1–8, Kristo anawakusanya wateule Wake; 9–11, Ujio wake waonyesha kuanza kwa Milenia; 12–13, Mitume Kumi na Wawili watawahukumu wana wa Israeli wote; 14–21, Ishara, mabaa, na ukiwa utautangulia Ujio wa Pili; 22–28, Ufufuo wa mwisho

8 *a* 2 Ne. 3:18–22; M&M 30:5–6; 32:1–3.
b M&M 3:19–20.
9 *a* M&M 57:1–3.
b M&M 52:42–43. MWM Sayuni.
11 *a* Mt. 18:15.
b Ufu. 20:10.
c M&M 43:5–7.
13 *a* MWM Ridhaa ya Wengi.
15 *a* 2 Ne. 32:3, 5.

na hukumu ya mwisho itafuatia Milenia; 29–35, Mambo yote kwa Bwana ni ya kiroho; 36–39, Ibilisi na Majeshi yake walifukuzwa kutoka mbinguni ili wawajaribu wanadamu; 40–45, Anguko na Upatanisho huleta wokovu; 46–50, Watoto wadogo wamekombolewa kupitia Upatanisho.

Sikilizeni sauti ya Yesu Kristo, Mkombozi wenu, [a]Mimi Ndimi Mkuu, ambaye mkono wake wa [b]rehema umefanya [c]upatanisho kwa ajili ya dhambi zenu;

2 Ambaye [a]atawakusanya watu wake kama kuku avikusanyavyo vifaranga vyake chini ya mabawa yake, hata wengi kadiri watakavyoifuata sauti yangu na [b]kujinyenyekeza mbele zangu, na kunilingana kwa sala kuu.

3 Tazama, amini, amini, ninawaambia, kwamba kwa wakati huu dhambi zenu [a]zimesamehewa, kwa sababu hiyo pokeeni mambo haya; lakini kumbukeni msitende dhambi tena, isije hatari kubwa ikaja juu yenu.

4 Amini, ninawaambia kwamba ninyi ni wateule toka ulimwenguni kwa kuitangaza injili yangu kwa shangwe, kama shangwe, kama [a]sauti ya parapanda.

5 Inueni mioyo yenu na furahini, kwani Mimi niko [a]katikati yenu, na ni [b]mtetezi wenu kwa Baba; na ni mapenzi yake kuwapa ule [c]ufalme.

6 Na, kama ilivyoandikwa—Lolote [a]mtakaloomba katika [b]imani, mkiwa [c]mmeungana katika sala mkiamini kulingana na amri yangu, mtapokea.

7 Na ninyi mmeitwa [a]kuwakusanya [b]wateule wangu; kwani wateule wangu [c]huisikia sauti yangu na wala hawaishupazi [d]mioyo yao;

8 Kwa hiyo amri imetoka kwa Baba kwamba [a]wakusanywe mahali pamoja juu ya uso wa nchi hii, ili [b]kuitayarisha mioyo yao na kujitayarisha katika mambo yote dhidi ya siku ile wakati [c]taabu na ukiwa vitakapokuja juu ya waovu.

9 Kwani saa i karibu na siku yaja haraka wakati dunia imekomaa; na wote wenye [a]kiburi na wao ambao hufanya maovu watakuwa kama [b]makapi; na [c]nitawateketeza, asema Bwana

29 1*a* MWM MIMI NIKO.
b MWM Rehema, enye Rehema.
c MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
2*a* Mt. 23:37; 3 Ne. 10:4–6.
b MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
3*a* MWM Samehe.
4*a* Alma 29:1–2; M&M 19:37; 30:9.
5*a* Mt. 18:20; M&M 6:32; 38:7; 88:62–63.
b MWM Mtetezi.
c MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
6*a* Mt. 21:22; Yn. 14:13.
b Mk. 11:24.
c 3 Ne. 27:1–2; M&M 84:1.
7*a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b Mk. 13:20; M&M 84:34.
MWM Teule, Wateule.
c Alma 5:37–41.
d MWM Moyo.
8*a* M&M 45:64–66; 57:1.
b M&M 58:6–9; 78:7.
c M&M 5:19; 43:17–27.
9*a* 2 Ne. 20:33; 3 Ne. 25:1.
MWM Kiburi.
b Nah. 1:10; Mal. 4:1; 1 Ne. 22:15, 23; JS—H 1:37.
c M&M 45:57; 63:34, 54; 64:24; 88:94; 101:23–25; 133:64.
MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia.

wa Majeshi, kwamba uovu hautakuwepo duniani;

10 Kwani saa i karibu, na yale [a]yaliyonenwa na mitume wangu lazima yatatimia; kwani kama vile walivyosema ndivyo itakavyokuwa;

11 Kwani nitajifunua mwenyewe kutoka mbinguni kwa uwezo na utukufu mkuu, pamoja na [a]majeshi yote ya mbinguni, na kukaa katika [b]haki pamoja na wanadamu duniani miaka [c]elfu moja, na waovu hawatastahimili.

12 Na tena, amini, amini, ninawaambia, na imetolewa amri kali, kwa mapenzi yake Baba, kwamba [a]mitume wangu, wale Kumi na Wawili ambao walikuwa nami katika huduma yangu kule Yerusalemu, watasimama mkono wangu wa kuume katika siku ile ya kuja kwangu katika nguzo ya [b]moto, wakiwa wamevikwa joho ya haki, na mataji juu ya vichwa vyao, katika [c]utukufu kama vile Mimi nilivyo, [d]kuihukumu nyumba yote ya Israeli, kadiri ya wengi jinsi walivyonipenda Mimi na kushika amri zangu, na siyo wengineo.

13 Kwani [a]parapanda italia kwa sauti yenye kuendelea na kwa sauti, kama vile juu ya Mlima wa Sinai, na dunia yote itatetemeka, nao [b]watatoka—ndiyo, hata wafu [c]waliokufa katika Mimi, ili kupokea [d]taji la haki, na kuvishwa, [e]kama Mimi, na kuwa pamoja nami, ili tuweze kuwa na umoja.

14 Lakini, tazama, ninawaambia kwamba kabla [a]siku hii kuu haijaja [b]jua litatiwa giza, na mwezi utageuzwa kuwa damu, na nyota zitaanguka kutoka mbinguni, na kutakuwa na [c]ishara kuu katika mbingu juu na nchi chini;

15 Na kutakuwa na kulia na [a]kuomboleza miongoni mwa umati wa watu;

16 Na kutakuwa [a]tufani kuu itakayoletwa ili kuangamiza mazao ya ulimwengu.

17 Na itakuwa kwa sababu ya uovu wa ulimwengu, kwamba nitalipiza [a]kisasi juu ya [b]waovu, kwa kuwa hawatatubu; kwani kikombe cha uchungu wa hasira yangu kimejaa; kwani tazama, [c]damu yangu haitawatakasa kama hawatanisikiliza.

18 Kwa hiyo, Mimi Bwana

10*a* MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
11*a* JS—M 1:37.
b MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
c MWM Milenia; Yesu Kristo—Utawala wa Kristo katika milenia.
12*a* MWM Mtume.
b Isa. 66:15–16; M&M 130:7; 133:41.
c MWM Utukufu; Yesu Kristo—Utukufu wa Yesu Kristo.
d Mt. 19:28; Lk. 22:30; 1 Ne. 12:9; Morm. 3:18–19.
13*a* M&M 43:18; 45:45.
b M&M 76:50.
c M&M 88:97; 133:56.
d MWM Kuinuliwa; Taji.
e M&M 76:94–95; 84:35–39.
14*a* MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b Yoe. 2:10; JS—M 1:33.
c MWM Ishara za Nyakati.
15*a* Mt. 13:42.
16*a* Eze. 38:22; Ufu. 11:19; 16:21.
17*a* Ufu. 16:7–11; 2 Ne. 30:10; JS—M 1:53–55. MWM Kisasi.
b MWM Ovu, Uovu.
c 1 Yoh. 1:7; Alma 11:40–41; M&M 19:16–18.

Mungu nitawaleta inzi juu ya uso wa dunia, ambao watawazidi wakazi wake, nao watakula nyama zao, na kusababisha funza kuingia ndani yao;

19 Na ndimi zao zitazuiliwa kwamba [a]hazitanena dhidi yangu; na nyama ya miili yao itaanguka kutoka kwenye mifupa yao, na macho yao kutoka kwenye matundu yake;

20 Na itakuwa kwamba [a]wanyama wa porini na ndege wa angani watawala.

21 Na kanisa lile kuu na la [a]machukizo, ambalo ni [b]kahaba wa ulimwengu wote, litaangamizwa kwa [c]moto uteketezao, kama ilivyonenwa kwa kinywa cha Ezekieli nabii, ambaye alinena juu ya mambo haya, ambayo bado hayajatokea bali kwa hakika ni [d]lazima, kama vile Mimi niishivyo, kwani machukizo hayawezi kutawala.

22 Na tena, amini, amini, ninawaambia kwamba na hiyo miaka [a]elfu itakapokwisha, na wanadamu wakianza tena kumkataa Mungu wao, ndipo nitakapouachia ulimwengu lakini kwa [b]muda mchache;

23 Na [a]mwisho utakapokuja, na mbingu na dunia zitaangamizwa na [b]kupita, na hapo patakuwa na mbingu mpya na [c]dunia mpya.

24 Na ya kale yote [a]yatapita, na yote yatakuwa mapya, hata mbingu na dunia, na vyote vilivyomo, watu na wanyama, ndege wa angani, na samaki wa baharini;

25 Na hapana hata [a]unywele mmoja, wala chembe moja, itakayopotea, kwani hiyo ni kazi ya mikono yangu.

26 Lakini, tazama, amini ninawaambia, kabla dunia haijapita, [a]Mikaeli, [b]malaika wangu mkuu, atapiga [c]parapanda yake, na ndipo wafu wote [d]wataamka, kwani makaburi yao yatafunguka, nao [e]watatoka—ndiyo, hata wote.

27 Na [a]wenye haki watakusanywa [b]mkono wangu wa kuume kwa uzima wa milele; na waovu mkono wangu wa kushoto ndiyo ambao nitaona aibu kuwamiliki mbele za Baba;

28 Kwa hiyo nitawaambia—[a]Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika [b]moto usio na mwisho, aliowekewa tayari [c]ibilisi na malaika zake,

19 *a* Zek. 14:12.
20 *a* Isa. 18:6; Eze. 39:17; Ufu. 19:17–18.
21 *a* MWM Ibilisi—Kanisa la ibilisi.
b Ufu. 19:2.
c Yoe. 1:19–20; 2:3; M&M 97:25–26. MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia.
d M&M 1:38.
22 *a* MWM Milenia.
b Ufu. 20:3; M&M 43:30–31; 88:110–111.
23 *a* Mt. 24:14. MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.
b Mt. 24:35; JS—M 1:35.
c MWM Dunia—Hali ya mwisho ya dunia.
24 *a* Ufu. 21:1–4.
25 *a* Alma 40:23.
26 *a* MWM Adamu; Mikaeli.
b MWM Malaika mkuu.
c 1 Kor. 15:52–55.
d MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa; Ufufuko.
e Yn. 5:28–29.
27 *a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
b Mt. 25:33. MWM Hukumu ya mwisho.
28 *a* Mt. 25:41; M&M 29:41.
b M&M 43:33.
c MWM Ibilisi.

29 Na sasa, tazama, ninawaambia, kamwe wakati wowote sijawahi kueleza kutoka kinywani mwangu kwamba watarejea, kwani [a]mahali nilipo hawawezi kufika, kwani hawana uwezo huo.

30 Lakini kumbukeni kwamba hukumu zangu zote hazijatolewa kwa wanadamu; na kama vile maneno yalivyotoka kinywani mwangu hivyo alivyo yatakayotimia, kwamba wa [a]kwanza atakuwa wa mwisho na wa mwisho atakuwa wa kwanza katika mambo yote niliyoyaumba kwa amri ya uwezo wangu, ambao ni nguvu ya Roho wangu.

31 Kwani kwa nguvu ya Roho wangu [a]niliviumba; ndiyo, vitu vyote vya [b]kiroho na kimwili—

32 Kwanza [a]kiroho, pili kimwili, ambao ndiyo mwanzo wa kazi yangu; na tena, kwanza kimwili, na pili kiroho, ambao ndiyo mwisho wa kazi yangu—

33 Nikizungumza nanyi ili mpate kuelewa kwa namna ya kawaida; lakini kwangu mimi mwenyewe kazi zangu hazina [a]mwisho, wala mwanzo; lakini imetolewa kwenu ili mpate kuelewa, kwa sababu mmeniomba na kukubaliwa.

34 Kwa hiyo, amini ninawaambia kwamba mambo haya yote kwangu mimi ni ya kiroho, na hata wakati wowote sijatoa sheria kwenu ambayo ni ya kimwili; wala mtu yeyote, wala wanadamu; wala si Adamu, baba yenu, ambaye nilimuumba.

35 Tazama, nilimpa yeye ili apate [a]kujiamulia mwenyewe; na nikampa amri, lakini siyo amri ya kimwili nilimpa yeye, kwani [b]amri zangu ni za kiroho; siyo za kiasili wala kimwili, si tamaa ya kimwili wala si ya kianasa.

36 Na ikawa kwamba Adamu, akijaribiwa na ibilisi—kwani, tazama, [a]ibilisi alikuwako kabla ya Adamu, kwani yeye [b]aliniasi mimi, akisema, Nipe mimi [c]heshima yako, ambayo ndiyo [d]uwezo wangu; na pia [e]theluthi moja ya [f]majeshi ya mbinguni aliyafanya yanigeuke kwa sababu ya [g]haki yao ya kujiamulia;

37 Na wakatupwa chini, na hivyo ndivyo kuja kwa [a]ibilisi na [b]malaika zake;

38 Na, tazama, kuna mahali palipotayarishwa kwa ajili yao kutoka mwanzo, mahali hapo ni [a]jehanamu.

39 Na hapana budi kwamba ibilisi lazima [a]awajaribu wanadamu, vinginevyo hawangewe-

29 *a* Yn. 7:34; M&M 76:112.
30 *a* Mt. 19:30; 1 Ne. 13:42.
31 *a* MWM Umba, Uumbaji.
b Musa 3:4–5.
32 *a* MWM Uumbaji wa Kiroho.
33 *a* Zab. 111:7–8; Musa 1:4.
35 *a* MWM Haki ya uamuzi.
b MWM Amri za Mungu.
36 *a* M&M 76:25–26; Musa 4:1–4.
b MWM Baraza Mbinguni.
c MWM Heshima.
d Isa. 14:12–14; M&M 76:28–29.
e Ufu. 12:3–4.
f M&M 38:1; 45:1. MWM Maisha kabla ya kuzaliwa.
g MWM Haki ya uamuzi.
37 *a* MWM Ibilisi.
b 2 Pet. 2:4; Yuda 1:6; Musa 7:26. MWM Malaika.
38 *a* MWM Jehanamu.
39 *a* Musa 4:3–4. MWM Jaribu, Majaribu.

za kujiamulia wao wenyewe; kwani kama kamwe hawakuonja [b]uchungu wasingeliweza kuijua utamu—

40 Kwa hiyo ikawa kwamba ibilisi akamjaribu Adamu, na yeye akala [a]tunda lililokatazwa, na akaivunja amri, hivyo basi akajiingiza [b]chini ya matakwa ya ibilisi, kwa sababu alikubali majaribu.

41 Kwa hiyo, Mimi, Bwana Mungu, [a]nikamfukuza kutoka katika Bustani ya [b]Edeni, kutoka machoni pangu, kwa sababu ya uvunjaji wake wa sheria, kwa ajili hiyo akawa mfu [c]kiroho, ambacho ni kifo cha kwanza, ambacho ni sawa sawa na [d]kifo cha mwisho, ambacho ni cha kiroho, ambacho kitahukumiwa kwao walio waovu nitakaposema: Ondokeni, ninyi [e]mliolaaniwa.

42 Lakini, tazama, ninawaambia kwamba Mimi, Bwana Mungu, nilitoa kwa Adamu na uzao wake, kwamba [a]wasife kwa kifo cha kimwili, hadi Mimi, Bwana Mungu, nitakapowatuma [b]malaika kutangaza kwao [c]toba na [d]ukombozi, kwa njia ya imani juu ya jina la [e]Mwana Pekee.

43 Na hivyo ndivyo nilivyofanya Mimi, Bwana Mungu, kumteua mtu kama siku zake za [a]majaribio—kwamba kwa kifo chake cha kimwili aweza [b]kuinuliwa katika [c]mwili usiokufa hadi [d]uzima wa milele, hata wengi kadiri watakavyoamini;

44 Na wale wasioamini juu ya [a]laana ya milele; kwani hawawezi kukombolewa kutokana na anguko lao la kiroho, kwa sababu hawatubu;

45 Kwani wao hupenda zaidi giza kuliko nuru, na [a]matendo yao ni maovu, na wao hupokea [b]ujira wao kwa yeye wanayemtii.

46 Lakini tazama, ninawaambia, kuwa [a]watoto wadogo [b]wamekombolewa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu kwa njia ya Mwanangu wa Pekee;

47 Kwa hiyo hawafanyi dhambi, kwani uwezo haujatolewa kwa Shetani wa [a]kuwajaribu watoto wadogo, hadi wanapoanza [b]kuwajibika mbele zangu;

48 Kwani imetolewa kwao hata kama vile nitakavyo Mimi, kulingana na mapenzi yangu,

39 *b* Musa 6:55.
40 *a* Mwa. 3:6; Musa 4:7–13.
b 2 Ne. 10:24; Mos. 16:3–5; Alma 5:41–42.
41 *a* MWM Anguko la Adamu na Hawa.
b MWM Edeni.
c MWM Mauti ya Kiroho.
d Alma 40:26.
e M&M 29:27–28; 76:31–39.
42 *a* 2 Ne. 2:21. MWM Mauti ya Kimwili.
b Alma 12:28–30.
c MWM Toba, Tubu.
d MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
e Musa 5:6–8.
43 *a* Alma 12:24; 42:10.
b MWM Ufufuko.
c Musa 1:39. MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
d MWM Uzima wa Milele.
44 *a* M&M 19:7–12. MWM Hukumu.
45 *a* Yn. 3:18–20; M&M 93:31–32.
b Mos. 2:32–33; Alma 3:26–27; 5:41–42; 30:60.
46 *a* Moro. 8:8, 12; M&M 93:38. MWM Mtoto, Watoto.
b M&M 74:7. MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
47 *a* MWM Jaribu, Majaribu.
b MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.

ili kwamba mambo muhimu yaweze kuhitajika kutoka kwenye mikono ya [a]baba zao.

49 Na, tena, ninawaambia, kwamba yeyote aliye na maarifa, sijamuamuru kutubu?

50 Na yeye ambaye hana [a]ufahamu, hubaki ndani yangu kufanya kama ilivyoandikwa. Na sasa sitasema zaidi kwenu kwa wakati huu. Amina.

SEHEMU YA 30

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa David Whitmer, Peter Whitmer Mdogo, na John Whitmer, huko Fayette, New York, Septemba 1830, baada ya mkutano wa siku tatu huko Fayette, lakini kabla ya wazee wa Kanisa hawajaachana. Mwanzoni ufunuo huu ulichapishwa kama mafunuo matatu; yaliunganishwa pamoja kuwa sehemu moja na Nabii mwenyewe kwa ajili ya toleo la mwaka 1835 la Mafundisho na Maagano.

1–4, David Whitmer anakanywa kwa kushindwa kuhudumu kwa bidii; 5–8, Peter Whitmer Mdogo ataambatana na Oliver Cowdery katika misheni kwa Walamani; 9–11, John Whitmer ameitwa ili kuihubiri injili.

Tazama, ninakuambia, [a]David, kwamba [b]umemwogopa mwanadamu na wala [c]hukunitegemea mimi nikupe nguvu kama ulivyotakiwa kufanya.

2 Bali akili yako imekuwa juu ya mambo ya [a]dunia zaidi kuliko mambo yangu, Muumba wako, na huduma ambayo wewe umeitiwa; na wala hukumfuata Roho wangu, na wale waliowekwa juu yako, lakini ukashawishiwa na wale ambao sikuwaamuru.

3 Kwa hiyo, umeachwa kujiulizia mwenyewe kutoka kwangu, na [a]kuyatafakari mambo ambayo umeyapokea.

4 Na nyumbani kwao kutakuwa katika nyumba ya baba yako, hadi nitakapokupa amri zaidi. Na utatenda [a]huduma yako katika kanisa, na mbele ya ulimwengu, na katika maeneo yanayokuzunguka. Amina.

5 Tazama, ninakuambia, [a]Peter, kwamba utafunga [b]safari yako pamoja na kaka yako Oliver; kwani [c]wakati umewadia unao faa kwangu Mimi kuwa yawapasa kufumbua vinywa vyenu ili kuitangaza injili yangu; kwa hiyo, usiogope, bali [d]tii maneno na ushauri wa kaka yako, ambao atakupa.

48 *a* M&M 68:25.
50 *a* M&M 137:7–10. MWM Ufahamu.

30 1 *a* MWM Whitmer, David.
b Mdo. 5:29.
c 2 Nya. 16:7–9.
2 *a* M&M 25:10.
3 *a* MWM Tafakari.
4 *a* MWM Kuhudumu; Utumishi.
5 *a* MWM Whitmer, Peter, Mdogo.
b M&M 32:1–3.
c M&M 11:15.
d MWM Kuwakubali Viongozi wa Kanisa; Ushauri.

6 Na uteseke katika mateso yake yote, daima ukiinua moyo wako kwangu katika sala na imani, kwa ajili ya ukombozi wake na wako; kwani nimempatia yeye uwezo wa kujenga [a]kanisa langu miongoni mwa [b]Walamani;

7 Na hapana yeyote niliyemteua kuwa mshauri [a]juu yake katika kanisa, kuhusu mambo ya kanisa, isipokuwa kaka yake, Joseph Smith, Mdogo.

8 Kwa hiyo, yatii mambo haya na uwe mwenye bidii katika kushika amri zangu, na utabarikiwa kwa uzima wa milele. Amina.

9 Tazama, ninakuambia, mtumishi wangu John, kwamba utaanza kutoka wakati huu [a]kuitangaza injili yangu, kama vile kwa [b]sauti ya parapanda.

10 Na kazi yako itakuwa huko kwa kaka yako Philip Burroughs, na katika maeneo yaliyo karibu, ndiyo, popote unapoweza kusikika, hadi nitakapokuamuru kuondoka hapa.

11 Na kazi yako yote itakuwa katika Sayuni, kwa moyo wako wote, kutoka sasa na kuendelea; ndiyo, daima utafungua kinywa chako katika kazi yangu, bila [a]kuogopa [b]mwanadamu awezacho kukufanya, kwani Mimi niko [c]pamoja nawe. Amina.

SEHEMU YA 31

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Thomas B. Marsh, Septemba 1830. Tukio hili lilitokea muda mfupi baada ya mkutano wa Kanisa (ona kichwa cha habari cha sehemu ya 30). Thomas B. Marsh alikuwa amebatizwa mwanzoni mwa mwezi huo na kutawazwa kuwa mzee katika Kanisa kabla ya kutolewa kwa ufunuo huu.

1–6, Thomas B. Marsh ameitwa kuihubiri injili na anahakikishiwa ustawi wa familia yake; 7–13, Anashauriwa kuwa mvumilivu, kusali daima, na kumtii Mfariji.

[a]Thomas, mwanangu, umebarikiwa kwa sababu ya imani yako katika kazi yangu.

2 Tazama, umepata mateso mengi kwa sababu ya familia yako; hata hivyo, nitakubariki wewe na familia yako, ndiyo, watoto wako; na siku yaja ambayo wataamini na kujua ukweli na kuwa pamoja na wewe katika kanisa langu.

3 Inua moyo wako na ufurahi, kwani saa ya huduma yako imewadia; na ulimi wako utalegezwa, nawe utatangaza habari

6 *a* MWM Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.
b M&M 3:20; 49:24. MWM Walamani.

7 *a* M&M 20:2–3.
9 *a* M&M 15:6.
b M&M 33:2.
11 *a* MWM Hofu; Ushujaa, enye Ushujaa.
b Isa. 51:7.
c Mt. 28:19–20.

31 1 *a* MWM Marsh, Thomas B.

[a]njema ya shangwe kuu kwa kizazi hiki.

4 [a]Utatangaza mambo yale ambayo yamefunuliwa kwa mtumishi wangu, Joseph Smith, Mdogo. Utaanza kuhubiri kutoka wakati huu, ndiyo, kuvuna katika shamba ambalo ni [b]jeupe lililo tayari kuchomwa.

5 Kwa hiyo, [a]ingiza mundu yako kwa moyo wako wote, na dhambi zako [b]zitasamehewa, na wewe utachukua [c]miganda mgongoni mwako, kwani [d]mtenda kazi amestahili ujira wake. Kwa hivyo, familia yako itaishi.

6 Tazama, amini ninakuambia, enenda kutoka kwao japo kwa wakati mfupi, na utangaze neno langu, na Mimi nitawatayarishia mahali.

7 Ndiyo, [a]nitaifungua mioyo ya watu, nao watakupokea. Nami nitalianzisha kanisa kwa mkono wako;

8 Nawe [a]utawaimarisha na kuwatayarisha kwa ajili ya wakati watakapo kusanyika.

9 Uwe [a]mvumilivu wakati wa [b]mateso, usiwashutumu wenye kukushutumu. Itawale [c]nyumba yako kwa unyenyekevu, na uwe thabiti.

10 Tazama, ninakuambia kwamba utakuwa tabibu kwa kanisa, bali siyo kwa walimwengu, kwani wao hawatakupokea.

11 Nenda zako kokote nitakakokutuma, na utapewa na [a]Mfariji, lile la kufanya na mahali pa kwenda.

12 [a]Omba daima, usije ukaanguka [b]majaribuni na kupoteza thawabu yako.

13 Uwe [a]mwaminifu hata mwisho, na lo, Mimi ni [b]pamoja nawe. Maneno haya siyo ya mwanadamu wala ya wanadamu, bali yangu Mimi, Yesu Kristo, Mkombozi wako, kwa [c]mapenzi ya Baba. Amina.

SEHEMU YA 32

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Parley P. Pratt na Ziba Peterson, huko Manchester, New York, mapema Oktoba 1830. Shauku kubwa na hamu iliwaingia wazee hawa kuhusiana na Walamani, ambao ahadi zao zilikuwa zimetabiriwa na kufundishwa Kanisani kutoka kwenye Kitabu cha Mormoni. Kama matokeo, maombi yalifanywa ili kwamba Bwana aonyeshe mapenzi yake kama

3 *a* Isa. 52:7; Lk. 2:10–11; Mos. 3:3–5.
4 *a* Mos. 18:19; M&M 42:12; 52:36.
b M&M 4:4–6.
5 *a* Ufu. 14:15.
b MWM Samehe.
c M&M 79:3.
d Lk. 10:3–11; M&M 75:24.
7 *a* MWM Mwongofu, Uongofu.
8 *a* M&M 81:5; 108:7.
9 *a* MWM Subira.
b MWM Shida.
c MWM Familia—Wajibu wa wazazi.
11 *a* MWM Mfariji; Roho Mtakatifu.
12 *a* 3 Ne. 18:17–21. MWM Sala.
b MWM Jaribu, Majaribu.
13 *a* MWM Stahimili.
b Mt. 28:20.
c MWM Yesu Kristo—Mamlaka.

wazee watumwe kwa wakati huo kwenda kwa makabila ya Wahindi hao huko Magharibi. Ufunuo huu ulifuata.

1–3, Parley P. Pratt na Ziba Peterson wanaitwa kuhubiri kwa Walamani wakiongozana na Oliver Cowdery na Peter Whitmer Mdogo; 4–5, Wanapaswa kuomba kwa ajili ya kufahamu maandiko.

Na sasa, kuhusu mtumishi wangu [a]Parley P. Pratt, tazama, ninasema naye kwamba kadiri vile mimi niishivyo ninataka kwamba yeye akatangaze injili yangu na [b]kujifunza kutoka kwangu, na kuwa mpole na mnyenyekevu wa moyo.

2 Na lile ambalo nimemchagulia yeye ni [a]kuongozana na watumishi wangu, Oliver Cowdery na Peter Whitmer, Mdogo, kwenda nyikani miongoni mwa [b]Walamani.

3 Na [a]Ziba Peterson pia atakwenda pamoja nao; na Mimi mwenyewe nitakwenda pamoja nao na nitakuwa [b]katikati yao; na [c]mtetezi wenu kwa Baba, na wala hakuna kitakachowashinda.

4 Nao [a]watayafuata yaliyoandikwa, na wala wasijisingizie [b]ufunuo mwingine; nao wataomba daima, na niweze [c]kuwafunulia haya kwa [d]ufahamu wao.

5 Na watayafuata maneno haya na hawatayapuuza. Nami nitawabariki. Amina.

SEHEMU YA 33

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Ezra Thayre na Northrop Sweet, huko Fayette, New York, Oktoba 1830. Katika kuutambulisha ufunuo huu, historia ya Joseph Smith inatilia mkazo kuwa "Bwana . . . daima yuko tayari kuwaelekeza wale wenye kumtafuta kwa bidii na katika imani."

1–4, Wafanyakazi wameitwa kuhubiri injili katika ile saa kumi na moja; 5–6, Kanisa limeanzishwa, na wateule watakusanywa; 7–10, Tubuni, kwani ufalme wa mbingu umekaribia; 11–15, Kanisa limejengwa juu ya mwamba wa injili; 16–18, Jitayarisheni kwa ujio wa Bwana harusi.

Tazama, ninawaambia, watumishi wangu Ezra na Northrop, fungueni masikio yenu, na sikilizeni sauti ya Bwana Mungu wenu, ambaye [a]neno lake li hai na lenye nguvu, tena lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta

32 1*a* MWM Pratt, Parley Parker.
b Mt. 11:28–30.
2*a* M&M 28:8; 30:5.
b M&M 3:18–20.
3*a* M&M 58:60.
b Mt. 18:20; M&M 6:32; 38:7.
c MWM Mtetezi.
4*a* 1 Ne. 15:25; M&M 84:43–44.
b M&M 28:2.
c JS—H 1:74.
d MWM Ufahamu.
33 1*a* Ebr. 4:12; Hel. 3:29–30.

yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na [b]makusudi ya moyo.

2 Kwani amini, amini, ninawaambia, kwamba mmeitwa kuzipaza [a]sauti zenu kama parapanda, mkiitangaza injili yangu kwa kizazi hiki chenye ila na ukaidi.

3 Kwani tazameni, [a]shamba li jeupe tayari kwa mavuno; na ni saa [b]kumi na moja, na ni [c]mara ya mwisho ambayo nitawaita wafanyakazi katika shamba langu la mizabibu.

4 Na [a]shamba langu la mizabibu [b]limeharibiwa kabisa; na hakuna hata mmoja atendaye [c]mema ila wachache tu; na wao [d]hukosea mara nyingi kwa sababu ya [e]makuhani wa uongo, wote wamekuwa na mawazo maovu.

5 Na amini, amini, ninawaambia, kuwa [a]kanisa hili [b]nimelianzisha na kulitoa kutoka nyikani.

6 Na hata hivyo ndivyo [a]nitakavyowakusanya wateule wangu kutoka pande [b]nne za dunia, hata wengi kadiri watakaoniamini Mimi, na kuisikiliza sauti yangu.

7 Ndiyo, amini, amini, ninawaambia, kwamba shamba li jeupe tayari kwa mavuno; kwa sababu hiyo, ingizeni mundu zenu, na mvune kwa nguvu, akili na uwezo wenu wote.

8 [a]Fumbueni vinywa vyenu navyo vitajazwa, nanyi mtakuwa kama [b]Nefi wa kale, aliyesafiri kutoka Yerusalemu katika nyika.

9 Ndiyo, fumbueni vinywa vyenu, na wala msiache, na mtachukua [a]miganda migongoni mwenu, kwani lo Mimi ni pamoja nanyi.

10 Ndiyo, fumbueni vinywa vyenu navyo vitajazwa, mkisema: [a]Tubuni, tubuni na itayarisheni njia ya Bwana, na yanyoosheni mapito yake; kwani ufalme wa mbinguni u karibu;

11 Ndiyo, tubuni na [a]mkabatizwe, kila mmoja wenu, kwa ondoleo la dhambi zenu; ndiyo, mkabatizwe hata kwa maji, na halafu waja ubatizo wa moto na wa Roho Mtakatifu.

12 Tazameni, amini, amini, ninawaambia, hii ndiyo [a]injili yangu; na kumbukeni kwamba wawe na imani katika mimi au vinginevyo hawataokolewa;

13 Na juu ya [a]mwamba huu nitalijenga kanisa langu; ndiyo, juu ya mwamba huu ninyi mmejengwa, na kama mtaendelea,

1 *b* Alma 18:32; M&M 6:16.
2 *a* Isa. 58:1.
3 *a* Yn. 4:35; M&M 4:4; 12:3; 14:3.
b Mt. 20:1–16.
c Yak. (KM) 5:71; M&M 43:28.
4 *a* MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
b 2 Ne. 28:2–14; Morm. 8:28–41.
c Rum. 3:12; M&M 35:12.
d 2 Ne. 28:14.
e MWM Ukuhani wa uongo.
5 *a* MWM Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.
b MWM Urejesho wa Injili.
6 *a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b 1 Ne. 19:15–17.
8 *a* M&M 88:81.
b 2 Ne. 1:26–28.
9 *a* Zab. 126:6; Alma 26:3–5; M&M 75:5.
10 *a* Mt. 3:1–3.
11 *a* MWM Batiza, Ubatizo.
12 *a* 3 Ne. 27:13–22.
13 *a* MWM Mwamba.

[b]milango ya jehanamu haitawashinda.

14 Na ninyi kumbukeni kushika [a]kanuni na maagano ya kanisa.

15 Na yeyote atakayekuwa na imani [a]mtamthibitisha katika kanisa langu, kwa kumwekea [b]mikono, nami nitampa [c]kipawa cha Roho Mtakatifu.

16 Na Kitabu cha Mormoni na [a]maandiko matakatifu yanatolewa na mimi kwa ajili ya [b]maelekezo yenu; na uwezo wa Roho wangu ndiye [c]atiaye uzima vitu vyote.

17 Kwa sababu hiyo, kuweni waaminifu, na mkisali daima, mkitengeneza na kuziwasha taa zenu, mkiwa pamoja na mafuta yake, ili kwamba muweze kuwa tayari [a]Bwana harusi ajapo—

18 Kwani tazameni, amini, amini, ninawaambia, kwamba [a]naja upesi. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 34

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Orson Pratt, huko Fayette, New York, 4 Novemba 1830. Ndugu Pratt alikuwa na umri wa miaka kumi na tisa wakati huo. Alikuwa ameongoka na kubatizwa wakati aliposikia kuhubiriwa kwa injili iliyorejeshwa kwa mara ya kwanza iliyohubiriwa na kaka yake mkubwa, Parley P. Pratt, wiki sita kabla. Ufunuo huu ulipokewa katika nyumba ya Peter Whitmer Mkubwa.

1–4, Waaminifu huwa wana wa Mungu kwa njia ya Upatanisho; 5–9, Kuhubiriwa kwa injili hutengeneza njia kwa Ujio wa Pili; 10–12, Unabii huja kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

Mwanangu [a]Orson, sikiliza na usikie na tazama kile Mimi, Bwana Mungu, nitakachokuambia, hata Yesu Kristo Mkombozi wako;

2 Niliye [a]nuru na uzima wa ulimwengu, nuru ing'aayo gizani wala giza haiitambui;

3 Yeye ambaye [a]aliupenda ulimwengu hata [b]yeye [c]akautoa uhai wake mwenyewe, kwamba wale wote watakaoamini waweze kuwa [d]wana wa Mungu.

13 *b* Mt. 16:16–19; M&M 10:69–70.
14 *a* MF M&M 20 (tazama kichwa cha habari sehemu ya 20). M&M 42:13.
15 *a* M&M 20:41.
b MWM Mikono, Kuweka juu ya.
c MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
16 *a* MWM Maandiko.
b 2 Tim. 3:16.
c Yn. 6:63.
17 *a* Mt. 25:1–13. MWM Bwana Harusi.
18 *a* Ufu. 22:20. MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
34 1 *a* MWM Pratt, Orson.
2 *a* Yn. 1:1–5. MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
3 *a* Yn. 3:16; 15:13. MWM Upendo.
b MWM Mkombozi.
c MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi; Lipia dhambi, Upatanisho.
d Yn. 1:9–12; Rum. 8:14, 16–17; Musa 6:64–68. MWM Wana na Mabinti za Mungu.

Kwa sababu hiyo wewe u mwanangu;

4 Na [a]heri wewe kwa sababu umeamini;

5 Na zaidi umebarikiwa kwa sababu [a]umeitwa na mimi kuihubiri injili yangu—

6 Kwa kupaza sauti yako kama vile kwa sauti ya parapanda yenye kuendelea na kwa sauti, na [a]tangaza toba kwa kizazi hiki chenye hila na ukaidi, ukiitayarisha njia ya Bwana kwa ajili ya [b]ujio wa pili.

7 Kwani tazama, amini, amini, ninakuambia, [a]saa i karibu ambayo nitakuja katika [b]wingu kwa uwezo na utukufu mkuu.

8 Nayo itakuwa [a]siku kubwa wakati wa kuja kwangu, kwani mataifa yote [b]yatatetemeka.

9 Lakini kabla ya kuja kwa siku ile kuu, jua litatiwa giza, na mwezi utageuka damu; na nyota hazitatoa nuru yake, na nyingine zitaanguka, na uharibifu mkubwa wawangojea waovu.

10 Kwa hiyo inua sauti yako na wala [a]usiache, kwani Bwana Mungu amesema hayo; hivyo basi toa unabii, na itatolewa kwa [b]uwezo wa Roho Mtakatifu.

11 Na kama wewe ni mwaminifu, tazama, Mimi ni pamoja nawe hadi nitakapokuja—

12 Na amini, amini, ninakuambia, naja upesi, Mimi ndimi Bwana wako na Mkombozi wako. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 35

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Sidney Rigdon, huko au karibu na Fayette, New York, 7 Desemba 1830. Kwa wakati huu, Nabii alikuwa akijishughulisha karibu kila siku na kufanya tafsiri ya Biblia. Tafsiri hiyo ilianza mapema Juni 1830, na wote Oliver Cowdery na John Whitmer walikuwa wametumika kama waandishi. Kwa vile wote sasa walikuwa wameitwa kwenye majukumu mengine, Sidney Rigdon aliitwa kwa uteuzi ulio mtakatifu kuwa kama mwandishi wa Nabii katika kazi hii (ona aya ya 20). Kama utangulizi katika kumbukumbu yake ya ufunuo huu, Historia ya Joseph Smith inaeleza: "Mnamo Desemba Sidney Rigdon alikuja [kutoka Ohio] ili kumwomba Bwana, na pamoja naye alikuja pia Edward Partridge. . . . Muda mfupi baada ya kuwasili kwao ndugu hawa wawili, na hivi ndivyo alivyosema Bwana."

4*a* Yn. 20:29.
5*a* MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito.
6*a* M&M 6:9.
b MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
7*a* Ufu. 1:3.
b Lk. 21:27.
8*a* Yoe. 2:11; Mal. 4:5; M&M 43:17–26. MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b Isa. 64:2.
10*a* Isa. 58:1.
b 2 Pet. 1:21.

1–2, Ni kwa namna gani watu wanaweza kufanyika wana wa Mungu; 3–7, Sidney Rigdon ameitwa kubatiza na kutoa Roho Mtakatifu; 8–12, Ishara na miujiza hufanyika kwa imani; 13–16, Watumishi wa Bwana watawapura mataifa kwa uwezo wa Roho; 17–19, Joseph Smith anashikilia funguo za siri; 20–21, Wateule watastahimili siku ya ujio wa Bwana; 22–27, Israeli ataokolewa.

Sikilizeni sauti ya [a]Bwana Mungu wenu, hata [b]Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, ambaye [c]uelekeo wake ni imara milele, yeye [d]yule leo kama jana, na hata milele.

2 Mimi ndimi Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, [a]aliyesulubiwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, hata wale wote [b]watakaoliamini jina langu, kwamba waweze kuwa [c]wana wa Mungu, hata [d]wamoja ndani yangu kama Mimi tulivyo [e]wamoja na Baba, vile Baba yu ndani yangu ili tuweze kuwa wamoja.

3 Tazama, amini, amini, ninasema mtumishi wangu Sidney, nimekuangalia wewe na kazi zako. Nimezisikia sala zako, na nimekutayarisha kwa kazi iliyo kuu.

4 Umebarikiwa wewe, kwani utafanya mambo makubwa. Tazama wewe umetumwa, kama vile [a]Yohana, kuitengeneza njia mbele yangu, na mbele ya [b]Eliya ambaye atakuja, na wewe hujui.

5 Na wewe umebatiza kwa maji kwa ajili ya toba, lakini [a]hawakumpokea Roho Mtakatifu;

6 Lakini sasa ninakupa wewe amri, kwamba [a]utawabatiza kwa maji, na watampokea [b]Roho Mtakatifu kwa kuwekewa [c]mikono, kama vile mitume wa kale.

7 Na itakuwa kwamba kutakuwa na kazi kubwa katika nchi, hata miongoni mwa [a]Wayunani, kwani upumbavu wao na machukizo yao yatakuwa dhahiri machoni pa watu wote.

8 Kwani Mimi ni Mungu, na mkono wangu [a]haujafupishwa; na nitaonyesha [b]miujiza, [c]ishara, na maajabu, kwa wale wote [d]waaminio katika jina langu.

9 Na yeyote atakayeomba kwa [a]imani katika jina langu, [b]watawatoa [c]pepo wabaya, [d]watawaponya wagonjwa; watawafanya vipofu kuona, na viziwi kusikia, na mababu kusema, na viwete kutembea.

10 Na saa yaja haraka ambapo

35 1*a* MWM Bwana.
b Ufu. 1:8.
MWM Alfa na Omega.
c 1 Ne. 10:19; M&M 3:2.
d Ebr. 13:8; M&M 38:1–4; 39:1–3.
2*a* MWM Kusulubiwa.
b M&M 20:25; 45:5, 8.
c MWM Wana na Mabinti za Mungu.
d Yn. 17:20–23.
MWM Umoja.
e MWM Mungu, Uungu.
4*a* Mal. 3:1; Mt. 11:10; 1 Ne. 11:27; M&M 84:27–28.
b 3 Ne. 25:5–6; M&M 2:1; 110:13–15.
5*a* Mdo. 19:1–6.
6*a* MWM Batiza, Ubatizo.
b MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
c MWM Mikono, Kuweka juu ya.
7*a* MWM Wayunani.
8*a* Isa. 50:2; 59:1.
b MWM Muujiza.
c MWM Ishara.
d MWM Amini, Imani.
9*a* MWM Amini, Imani.
b Mk. 16:17.
c Mk. 1:21–45.
d MWM Ponya, Uponyaji.

mambo makuu yataonyeshwa kwa wanadamu;

11 Lakini [a]pasipo imani hakuna kitu chochote kitakachoonyeshwa isipokuwa [b]ukiwa juu ya [c]Babilonia, ule ule ambao ulifanya mataifa yote kunywa mvinyo wa ghadhabu ya [d]uasherati wake.

12 Na [a]hakuna yeyote afanyaye yaliyo mema isipokuwa wale walio tayari kupokea utimilifu wa injili yangu, ambayo nimeitoa kwa kizazi hiki.

13 Kwa hiyo, nimewachagua walio [a]wadhaifu wa ulimwengu, wale ambao [b]hawakusoma na waliodharauliwa, ili kuyapura mataifa kwa uwezo wa Roho wangu;

14 Na mkono wao utakuwa mkono wangu, na nitakuwa [a]ngao yao na kigao chao; na nitafunga viuno vyao, watapigana kiume kwa ajili yangu; na [b]maadui zao watakuwa chini ya miguu yao; na Mimi [c]nitaushusha upanga kwa niaba yao, na kwa [d]moto wa hasira yangu nitawalinda.

15 Na [a]maskini na [b]wanyenyekevu watahubiriwa injili, nao [c]watautazamia wakati wa ujio wangu, kwani u [d]karibu—

16 Nao watajifunza mfano wa [a]mtini, kwani hata sasa wakati wa mavuno tayari u karibu.

17 Na nimepeleka [a]utimilifu wa injili yangu kwa mkono wa mtumishi wangu [b]Joseph; na katika unyonge nimembariki;

18 Na nimempa [a]funguo za siri ya mambo [b]yaliyofungwa, hata mambo yaliyokuwepo tangu [c]misingi ya ulimwengu, na mambo yatakayokuja, tangu wakati huu hadi wakati wa ujio wangu, kama atakaa ndani yangu, na kama siyo, mwingine nitampanda mahali pake.

19 Kwa hiyo, utamwangalia yeye kwamba imani yake isitindike, na itatolewa na [a]Mfariji, [b]Roho Mtakatifu, ajuaye mambo yote.

20 Na amri ninakupa wewe—kwamba [a]utaandika kwa ajili yake; na maandiko yatatolewa, kama vile yalivyo moyoni mwangu, kwa wokovu wa [b]wateule wangu;

21 Kwani wataisikia [a]sauti yangu, na kuniona Mimi, na wala hawatakuwa wamelala, nao

11 *a* M&M 63:11–12.
b M&M 5:19–20.
c MWM Babeli, Babilonia.
d Ufu. 18:2–4.
12 *a* Rum. 3:10–12; M&M 33:4; 38:10–11; 84:49.
13 *a* 1 Kor. 1:27; M&M 1:19–23; 124:1.
b Mdo. 4:13.
14 *a* 2 Sam. 22:2–3.
b M&M 98:34–38.
c M&M 1:13–14.
d M&M 128:24.
15 *a* Mt. 11:5.
b MWM Pole, Upole.
c 2 Pet. 3:10–13; M&M 39:23; 45:39; Musa 7:62.
d M&M 63:53.
16 *a* Mt. 24:32; M&M 45:36–38; JS—M 1:38. MWM Ishara za Nyakati.
17 *a* M&M 42:12.
b M&M 135:3.
18 *a* M&M 84:19.
b Dan. 12:9; Mt. 13:35; 2 Ne. 27:10–11; Eth. 4:4–7; JS—H 1:65.
c M&M 128:18.
19 *a* Yn. 14:16, 26; 15:26. MWM Mfariji.
b MWM Roho Mtakatifu.
20 *a* Nabii katika wakati huu alikuwa anashughulika na tafsiri ya kiufunuo ya Biblia, ambamo Sidney Rigdon aliitwa kuwa mwandishi.
b MWM Teule, Wateule.
21 *a* Yoe. 2:11; M&M 43:17–25; 88:90; 133:50–51.

[b]watakaa siku ya [c]ujio wangu; kwani watatakaswa, kama vile mimi [d]nilivyotakasika.

22 Na sasa [a]ninakuambia, kaa pamoja naye, naye atasafiri pamoja na wewe; wala usimwache, na hakika mambo haya yatatimia.

23 Na kwa [a]kuwa huandiki, tazama, itatolewa kwake yeye kutoa unabii; nawe utahubiri injili yangu na kuwataja [b]manabii watakatifu ili kuthibitisha maneno yake, kama yatakavyotolewa naye.

24 [a]Shika amri na maagano yote ambayo kwayo mmefungwa; na Mimi nitazifanya mbingu [b]zitikisike kwa ajili yenu, na [c]Shetani atatetemeka, na Sayuni [d]itafurahi juu ya milima na kustawi;

25 Na [a]Israeli [b]ataokolewa katika wakati wangu mwenyewe utakapofika; na kwa [c]funguo nilizompa wataongozwa, na wala hawatachanganyika tena kamwe.

26 Inueni mioyo yenu na furahini, [a]ukombozi wenu u karibu.

27 Msiogope, enyi kundi dogo, [a]ufalme ni wenu hadi nitakapokuja. Tazama, [b]naja haraka. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 36

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Edward Partridge, huko karibu na Fayette, New York 9 Desemba 1830. (ona kichwa cha habari cha sehemu ya 35). Historia ya Joseph Smith inasema kwamba Edward Partridge "alikuwa mfano wa uchaji na mmoja wa watu wakuu wa Bwana."

1–3, Bwana aweka mkono Wake juu ya Edward Partridge kwa mkono wa Sidney Rigdon; 4–8, Kila mwanaume aipokeaye injili na ukuhani aitwe kwenda kuihubiri.

Hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu, [a]Mwenye Enzi wa Israeli: Tazama, ninakuambia, mtumishi wangu [b]Edward, kwamba umebarikiwa, na dhambi zako zimesamehewa, na umeitwa ili kuitangaza injili yangu kama vile kwa sauti ya parapanda;

2 Na nitaweka [a]mkono wangu juu yako kwa mkono wa mtumishi wangu Sidney Rigdon,

21 *b* Mal. 3:2–3.
c MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
d MWM Safi na Isiyo safi.
22 *a* M&M 100:9–11.
23 *a* MY kila wakati ambapo Sidney Rigdon alikuwa hajishughulishi na kuandika.
b MY maandiko.
24 *a* M&M 103:7.
b M&M 21:6.
c 1 Ne. 22:26.
d MWM Shangwe.
25 *a* MWM Israeli.
b Isa. 45:17; 1 Ne. 19:15–16; 22:12.
c MWM Funguo za Ukuhani.
26 *a* Lk. 21:28.
27 *a* MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
b Ufu. 22:20.
36 1 *a* MWM Yehova; Yesu Kristo.
b M&M 41:9–11.
2 *a* MWM Mikono, Kuweka juu ya.

nawe utampokea Roho wangu, Roho Mtakatifu, hata [b]Mfariji, ambaye atakufundisha mambo ya [c]amani yaliyo ya ufalme;

3 Nawe utatangaza kwa sauti kubwa, ukisema: Hosana, na libarikiwe jina la Mungu Aliye Juu Sana.

4 Na sasa wito huu na amri hii ninakupa wewe kuhusu watu wote—

5 Kwamba wale wote wajao mbele ya watumishi wangu Sidney Rigdon na Joseph Smith, Mdogo, wakiukumbatia wito huu na amri hizi, [a]watatawazwa na [b]kutumwa kuihubiri injili isiyo na mwisho miongoni mwa mataifa—

6 Tangazeni toba, mkisema: [a]Jiokoeni wenyewe na kizazi hiki chenye ukaidi, na jitoeni huko kwenye moto, mkilichukia hata [b]vazi lililotiwa uchafu na mwili.

7 Na amri hii itatolewa kwa wazee wa kanisa langu, kwamba kila mtu ambaye ataikumbatia kwa moyo mmoja aweza kutawazwa na kutumwa, kama vile nilivyosema.

8 Mimi ndimi Yesu Kristo, Mwana wa Mungu; hivyo basi, funga viuno vyako na haraka naja kwenye [a]hekalu langu. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 37

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Sidney Rigdon, karibu na Fayette, New York, Desemba 1830. Katika hii sehemu kumetolewa amri ya kwanza kuhusu kukusanyika katika kipindi hiki.

1–4, Watakatifu wanaitwa kukusanyika huko Ohio.

Tazama, ninawaambia kuwa haina manufaa kwangu mimi kwamba ninyi mwendelee [a]kutafsiri zaidi hadi mtakapokwenda Ohio, na hii ni kwa sababu ya adui na faida yenu ninyi.

2 Na tena, ninawaambia kuwa msiende mpaka mtakapokuwa mmehubiri injili yangu katika sehemu zile, na kuliimarisha kanisa popote linapopatikana, na zaidi katika [a]Colesville; kwani, tazama, wanaomba kwangu katika imani kubwa.

3 Na tena, amri ninaitoa kwa kanisa, kwamba ni kwa manufaa kwangu mimi kuwa yawapasa kukusanyika pamoja huko [a]Ohio, katika wakati ambao mtumishi wangu Oliver Cowdery atakaporejea kwao.

2 *b* MWM Mfariji; Roho Mtakatifu.
c M&M 42:61.
5 *a* M&M 63:57.
MWM Kutawaza, Kutawazwa.
b MWM Hubiri.
6 *a* Mdo. 2:40.
b Yuda 1:23.
8 *a* Mal. 3:1.

37 1 *a* MY tafsiri ya Biblia ilikuwa imeshaanza.
2 *a* M&M 24:3; 26:1.
3 *a* MY jimbo la Ohio. M&M 38:31–32.

4 Tazama, hii ni hekima, na acha kila mtu [a]ajichagulie mwenyewe hadi nitakapokuja. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 38

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Fayette, New York, 2 Januari 1831. Tukio lilikuwa ni mkutano wa Kanisa.

1–6, Kristo aliviumba vitu vyote; 7–8, Yeye yupo katikati ya Watakatifu Wake, ambao hivi karibuni Watamwona; 9–12, Wenye mwili wote wameharibika mbele Zake; 13–22, Ameihifadhi nchi ya ahadi kwa ajili ya Watakatifu Wake sasa na hata milele; 23–27, Watakatifu wameamuriwa kuwa na umoja na wachukuliane kama vile ni ndugu; 28–29, Vita vyatabiriwa; 30–33, Watakatifu watapewa uwezo kutoka juu nao watakwenda miongoni mwa mataifa yote; 34–42, Kanisa limeamriwa kuwajali maskini na wenye shida na kuutafuta utajiri wa milele.

Hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu wenu, hata Yesu Kristo, [a]Mimi Ndimi Mkuu, Alfa na Omega, [b]mwanzo na mwisho, yule yule ambaye aliangalia uwazi mpana wa milele, na [c]majeshi yote ya maserafi wa mbinguni, [d]kabla ya ulimwengu [e]kufanyika;

2 Yeye yule [a]ajuaye vitu vyote, kwani vitu [b]vyote vipo mbele ya macho yangu;

3 Mimi ni yeye yule ambaye alinena, na ulimwengu [a]ukafanyika, na vitu vyote vilikuja kwa njia yangu Mimi.

4 Mimi ni yeye yule niliyechukua [a]Sayuni ya Enoki kifuani mwangu mwenyewe; na amini, ninasema, wengi [b]wameamini katika jina langu, kwani Mimi ndiye Kristo, na katika jina langu mwenyewe, na kwa nguvu za [c]damu yangu ambayo nilimwaga, nimewatetea mbele za Baba.

5 Lakini tazama, mabaki ya [a]uovu nimeyaweka katika [b]minyororo ya giza hadi siku ile kuu ya [c]hukumu, ambayo itakuja mwisho wa dunia;

6 Na hivyo ndivyo nitakavyo acha wafungwe, ili kwamba wasiweze kuisikia sauti yangu ila wataishupaza mioyo yao, ole, ole, ole, hayo ndiyo maangamizi yao.

4*a* MWM Haki ya uamuzi.
38 1*a* MWM MIMI NIKO.
b Ufu. 1:8.
c M&M 45:1.
d MWM Maisha kabla ya kuzaliwa.
e Zab. 90:2.
2*a* M&M 88:41; Musa 1:35. MWM Kujua yote.
b Mit. 5:21; 2 Ne. 9:20.
3*a* Zab. 33:6–9. MWM Umba, Uumbaji.
4*a* TJS Mwa. 14:25–40 (Kiambatisho); M&M 45:11–14; 76:66–67; 84:99–100; Musa 7:18–21. MWM Sayuni.
b M&M 20:25; 35:2; 45:3–5.
c MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
5*a* MWM Kutokuwa Adilifu, Siyo Adilifu.
b 2 Pet. 2:4; Yuda 1:6. MWM Jehanamu.
c MWM Hukumu ya mwisho.

7 Lakini tazama, amini, amini, ninawaambia kuwa [a]macho yangu yanawaangalia. Mimi nipo [b]katikati yenu nanyi hamuwezi kuniona;

8 Lakini siku i karibu kuja ambayo [a]mtaniona, na kujua kuwa Mimi ndimi; kwa kuwa utaji wa giza karibu utaondolewa, na yule ambaye [b]hakutakaswa hataweza [c]kukaa siku hiyo.

9 Kwa hiyo, fungeni viuno vyenu na kuwa tayari. Tazameni, [a]ufalme ni wenu, na wala adui hatawashinda.

10 Amini, ninawaambia, ninyi ni [a]safi, lakini siyo wote; na hapana mwingine [b]ninayependezwa naye;

11 Kwani wenye [a]mwili wote wameharibika mbele zangu; na nguvu za [b]giza zimetapakaa juu ya dunia, miongoni mwa wanadamu, katika uwepo wa majeshi yote ya mbinguni—

12 Ambao husababisha ukimya kutawala, na mbingu yote [a]yaumia, na [b]malaika wanasubiri amri kuu ya [c]kuangamiza dunia, kukusanya [d]magugu ili wapate [e]kuyachoma moto; na, tazama, adui amejikusanya.

13 Na sasa ninawaonyesha siri, kitu ambacho kilikuwa sirini, ambacho kingeleta [a]angamizo lenu katika wakati wake, na ninyi hamkujua hilo;

14 Lakini sasa ninawaambia ninyi, na mmebarikiwa ninyi, siyo kwa sababu ya uovu wenu, wala siyo kwa sababu ya mioyo yenu isiyoamini; kwani hakika baadhi yenu mna hatia mbele zangu, lakini nitawasamehe udhaifu wenu.

15 Kwa sababu hiyo, kuweni [a]imara tangu sasa; [b]msiogope, kwani ufalme ni wenu.

16 Na kwa ajili ya wokovu wenu ninatoa amri hii kwenu, kwani nimesikia sala zenu, na [a]maskini wamelalamika mbele zangu, na [b]matajiri nimewaumba, na viumbe vyote ni vyangu, na mimi sina [c]upendeleo.

17 Na nimeifanya dunia kuwa tajiri, na tazama nayo ni [a]mahali pangu pa kuweka miguu, kwa sababu hiyo, tena nitasimama juu yake.

18 Na Mimi ninatoa na ninataka kuwapa ninyi utajiri mkubwa, hata ile nchi ya ahadi, nchi itiririkayo maziwa na asali, nchi ambayo haitakuwa na laana wakati Bwana ajapo;

19 Nami nitaitoa kwenu kuwa nchi ya urithi wenu, kama

7*a* M&M 1:1.
b M&M 6:32; 29:5.
8*a* Ufu. 22:4–5. MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b MWM Safi na Isiyo safi.
c Mal. 3:2.
9*a* Lk. 6:20. MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
10*a* MWM Safi na Isiyo safi.
b M&M 1:30.
11*a* Isa. 1:3–4; M&M 33:4.
b Mik. 3:6; M&M 112:23; Musa 7:61–62.
12*a* Musa 7:41.
b M&M 86:3–7.
c MWM Mavuno.
d M&M 88:94; 101:65–66.
e Mt. 13:30.
13*a* M&M 5:32–33.
15*a* MWM Ushujaa, enye Ushujaa.
b MWM Hofu—Hofu ya mwanadamu.
16*a* Mos. 4:16–18.
b 1 Sam. 2:7.
c Mdo. 10:34; Moro. 8:11–12; M&M 1:34–35.
17*a* 1 Ne. 17:39; Ibr. 2:7.

mtaitafuta kwa mioyo yenu yote.

20 Na hili litakuwa agano langu na ninyi, mtaipata kama nchi yenu ya urithi, na kwa [a]urithi wa watoto wenu milele, kadiri ya dunia itakavyoendelea kuwepo, na ninyi mtaimiliki tena milele yote, wala siyo ya kupita tena.

21 Lakini, amini ninawaambia kwa wakati hamtakuwa na mfalme wala mtawala, kwa kuwa Mimi nitakuwa [a]mfalme wenu na kuwalinda.

22 Kwa hiyo, isikieni sauti yangu na [a]mnifuate, na mtakuwa watu [b]huru, hamtakuwa na sheria bali sheria zangu wakati nitakapokuja, kwa kuwa Mimi ni [c]mtoaji sheria wenu, na ni kipi kitakachouzuia mkono wangu?

23 Lakini, amini ninawaambia, [a]fundishaneni kulingana na ofisi ambayo nimewateua;

24 Na kila mtu na [a]ampende ndugu yake kama vile ajipendavyo mwenyewe, na kutenda [b]wema na [c]utakatifu mbele zangu.

25 Na tena ninakuambia, kila mtu na ampende ndugu yake kama vile ajipendavyo yeye mwenyewe.

26 Kwani ni mtu gani miongoni mwenu mwenye watoto kumi na wawili, na asiye na upendeleo, na watoto wote wanamtumikia kwa utiifu, na amwambie mmoja wao: Vaa majoho na ukae hapa; na kwa mwingine: Kavae matambara na ukakae pale—naye awaangalie watoto wake na kujisemea kuwa mimi ni mtu wa haki?

27 Tazama, hili nimelitoa kwenu kama mfano, na hivyo ndivyo nilivyo. Ninawaambia, muwe na [a]umoja; na kama hamna umoja ninyi siyo wangu.

28 Na tena, ninawaambia kuwa adui katika vyumba vya siri ayatafuta [a]maisha yenu.

29 Mnasikia juu ya [a]vita katika nchi za mbali, na mnasema kwamba karibu kutakuwa na vita vikali katika nchi za mbali, lakini hamjui mioyo ya watu wa nchi yenu yenyewe.

30 Ninawaambia ninyi haya kwa sababu ya sala zenu; kwa hiyo, [a]ihifadhini [b]hekima katika vifua vyenu, wasije watu waovu wakayafunua mambo haya kwenu kwa uovu wao, katika namna ambayo itasema kwa sauti kubwa masikioni mwenu kuliko ile ambayo itaitikisa dunia; lakini kama mmejitayarisha hamtaogopa.

31 Na hivyo muweze kuiepuka

20 *a* M&M 45:58.
21 *a* Zek. 14:9; 2 Ne. 10:14; Alma 5:50.
22 *a* Yn. 10:27.
b MWM Yesu Kristo—Utawala wa Kristo katika milenia.
c Isa. 33:22; Mik. 4:2; M&M 45:59.
23 *a* M&M 88:77–79, 118, 122. MWM Fundisha, Mwalimu.
24 *a* Kum. 17:20; 1 Kor. 4:6.
b M&M 46:33. MWM Wema.
c MWM Utakatifu.
27 *a* Yn. 17:21–23; 1 Kor. 1:10; Efe. 4:11–14; 3 Ne. 11:28–30; Musa 7:18. MWM Umoja.
28 *a* M&M 5:33; 38:13.
29 *a* M&M 45:26, 63; 87:1–5; 130:12.
30 *a* JS—M 1:37.
b MWM Hekima.

nguvu ya adui, na kukusanyika kwangu watu wenye haki, pasipo [a]mawaa na aibu—

32 Kwa hivyo, kwa sababu hii, niliwapa amri kuwa yawapasa kwenda mto [a]Ohio; na huko nitawapa [b]sheria yangu; na huko [c]mtajaliwa uwezo kutoka juu;

33 Tokea wakati huo, yeyote nitakayemhitaji [a]atakwenda miongoni mwa mataifa yote, nao wataambiwa nini cha kufanya; kwani ninayo kazi kubwa inayosubiriwa, kwani Israeli [b]itaokolewa, na Mimi nitawaongoza kokote nitakako, na hakuna nguvu [c]itakayozuia mkono wangu.

34 Na sasa, ninatoa amri kwa kanisa katika sehemu hizi, kuwa watu fulani miongoni mwao watateuliwa, na wateuliwa kwa [a]sauti ya kanisa;

35 Na watawaangalia maskini na wenye shida, na kuwapatia [a]msaada ili kwamba wasiteseke; na kuwapeleka mahali ambapo nimewaamuru wao;

36 Na hii ndiyo itakuwa kazi yao, kusimamia mambo yahusuyo mali za kanisa hili.

37 Na wale wenye mashamba ambayo hayawezekani kuuzwa, na yaachwe au yakodishwe kama vile wao wanavyoona inafaa.

38 Hakikisheni kwamba vitu hivi vyote vinahifadhiwa; na wakati watu [a]watakapojaliwa uwezo kutoka juu na kutumiwa, vitu hivi vyote vikusanywe kwenye kifua cha kanisa.

39 Na endapo mtatafuta [a]utajiri ambao ni mapenzi ya Baba kuwapeni ninyi, mtakuwa matajiri kuliko watu wote, kwa kuwa mtakuwa na utajiri wa milele; na ni kweli kwamba [b]utajiri wa ulimwengu ni wangu na mimi huutoa; lakini jihadharini na [c]majivuno, msije mkawa kama [d]Wanefi wa kale.

40 Na tena, ninawaambia, amri ninawapa, kwamba kila mtu, mzee, kuhani, mwalimu, na pia muumini, aende kwa nguvu zake, kwa kazi za [a]mikono yake, kutayarisha na kutimiliza mambo ambayo nimeyaamuru.

41 Na [a]mahubiri yenu yawe sauti ya [b]kuonya, kila mtu kwa jirani yake, katika upole na unyenyekevu.

42 Na tokeni [a]huko miongoni mwa waovu. Jiokoeni wenyewe. Kuweni safi ninyi mnaochukua vyombo vya Bwana. Hivyo ndivyo. Amina.

31 *a* 2 Pet. 3:14.
32 *a* M&M 37:3.
b M&M 42.
c Lk. 24:49; M&M 39:15; 95:8; 110:9–10.
33 *a* MWM Kazi ya kimisionari.
b Isa. 45:17; Yer. 30:10; M&M 136:22.
c Dan. 4:35.
34 *a* MWM Ridhaa ya Wengi.
35 *a* MWM Ustawi.
38 *a* MWM Endaomenti.
39 *a* Yak. (KM) 2:17–19; M&M 11:7.
b Hag. 2:8.
c MWM Kiburi.
d Moro. 8:27.
40 *a* 1 Kor. 4:12.
41 *a* MWM Hubiri.
b MWM Onya, Onyo.
42 *a* Isa. 52:11.

SEHEMU YA 39

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa James Covel, huko Fayette, New York, 5 Januari 1831. James Covel ambaye alikuwa mchungaji wa Kimethodisti kwa karibu miaka arobaini, aliagana na Bwana kuwa atatii amri yoyote ambayo Bwana atampa kupitia Joseph Nabii.

1–4, Watakatifu wanao uwezo wa kuwa wana wa Mungu; 5–6, Kuipokea injili ni kumpokea Kristo; 7–14, James Covel anaamriwa kubatizwa na kufanya kazi katika shamba la mizabibu la Bwana; 15–21, Watumishi wa Bwana wataihubiri injili kabla ya Ujio wa Pili; 22–24, Wale ambao huipokea injili watakusanyika wakati huu na hata milele.

Sikiliza na sikia sauti yake yeye aliye wa kutoka [a]milele hadi milele yote; [b]Mimi Ndimi Mkuu, hata Yesu Kristo—

2 [a]Nuru na uzima wa ulimwengu; nuru ing'aayo gizani na hata giza haikuitambua;

3 Yeye yule ambaye alikuja [a]wakati wa meridiani alikuja kwa walio wangu, na walio wangu hawakunipokea;

4 Bali wote walionipokea, niliwapa uwezo wa kufanyika [a]wana wangu; na vivyo hivyo nitawapa wale wote wanipokeao Mimi, uwezo wa kufanyika wana wangu.

5 Na amini, amini ninakuambia, yeye aipokeaye injili yangu [a]anipokea Mimi, na yeye asiyeipokea injili yangu hanipokei Mimi.

6 Na hii ni [a]injili yangu—toba na ubatizo wa maji, na halafu huja [b]ubatizo wa moto na Roho Mtakatifu, hata Mfariji, aonyeshaye mambo yote, na [c]afundishaye mambo ya amani yaliyo ya ufalme.

7 Na sasa, tazama, ninakuambia, mtumishi wangu [a]James, nimeziangalia kazi zako na ninakujua wewe.

8 Na amini, ninakuambia, moyo wako sasa ni mnyoofu mbele zangu kwa wakati huu; na, tazama, nimeweka baraka kubwa juu ya kichwa chako;

9 Hata hivyo, wewe umeona huzuni kuu, kwa kuwa umenikataa mimi mara nyingi kwa sababu ya kiburi na shughuli za [a]ulimwengu.

10 Lakini, tazama, siku za ukombozi wako zimefika, kama utaisikiliza sauti yangu, ambayo yasema kwako wewe: Simama na [a]ubatizwe, na ukaoshe

39 1*a* Ebr. 13:8; M&M 20:12; 35:1; 38:1–4.
b Ku. 3:14. mwm Yehova.
2*a* mwm Nuru, Nuru ya Kristo.
3*a* M&M 20:26; Musa 6:57, 62.
4*a* Yn. 1:12. mwm Wana na Mabinti za Mungu.
5*a* Yn. 13:20.
6*a* mwm Batiza, Ubatizo; Injili; Toba, Tubu.
b mwm Roho Mtakatifu; Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.
c M&M 42:61.
7*a* M&M 40:1.
9*a* Mt. 13:22.
10*a* M&M 40. mwm Batiza, Ubatizo.

dhambi zako, ukilingana jina langu, nawe utampokea Roho wangu, na baraka kubwa namna hii ambayo kamwe hujazijua.

11 Na kama wewe utafanya haya, nimekutayarisha kwa ajili ya kazi kuu. Wewe utahubiri utimilifu wa injili yangu, ambayo nimeileta katika siku hizi za mwisho, agano ambalo nimelileta ili [a]kuwarejesha watu wangu, ambao ni wa nyumba ya Israeli.

12 Na itakuwa kwamba uwezo [a]utakuwa juu yako; utakuwa na imani kubwa, na Mimi nitakuwa pamoja na wewe na nitatangulia mbele ya uso wako.

13 Na umeitwa [a]kufanya kazi katika shamba langu la mizabibu, na kulijenga kanisa langu, na [b]kuistawisha Sayuni, ili kwamba iweze kufurahi juu ya vilima na [c]kustawi.

14 Tazama, amini, amini, ninakuambia, hujaitwa kwenda katika nchi za mashariki, bali umeitwa kwenda Ohio.

15 Na kadiri watu wangu watakavyokusanyika wenyewe kule Ohio, nimeweka katika ghala [a]baraka ambayo haijapata kujulikana miongoni mwa wanadamu, nayo itamiminwa juu ya vichwa vyao. Na kutokea huko watu watakwenda katika [b]mataifa [c]yote.

16 Tazama, amini, amini, ninakuambia, kwamba watu huko Ohio wananilingana katika imani kubwa, wakifikiria kuwa nitauzuia mkono wangu katika hukumu juu ya mataifa, lakini siwezi kulikana neno langu.

17 Kwa hiyo anza kazi kwa nguvu zako zote na waite wafanyakazi waaminifu katika shamba langu la mizabibu, ili liweze [a]kupogolewa kwa mara ya mwisho.

18 Na kadiri watakavyotubu na kupokea utimilifu wa injili yangu, na kutakaswa, nitauzuia mkono wangu katika [a]hukumu.

19 Kwa hivyo, nenda, ukipaza sauti kubwa, ukisema: Ufalme wa mbingu u karibu; paza sauti, ukisema: Hosana! libarikiwe jina la Mungu Aliye Juu Sana.

20 Nenda na ukabatize kwa maji, ukiitengeneza njia mbele ya uso wangu kwa ajili ya wakati wa [a]ujio wangu;

21 Kwani wakati umekaribia; [a]siku wala saa hakuna [b]ajuaye; bali hakika yaja.

22 Na yeye ayapokeaye mambo haya anipokea Mimi; na watakusanyika kwangu sasa na hata milele.

23 Na tena, na itakuwa kwamba juu ya wote utakaowabatiza kwa maji, utawawekea [a]mikono yako, na watapokea [b]kipawa cha Roho Mtakatifu,

11 *a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
12 *a* 2 Kor. 12:9.
13 *a* Mt. 20:1–16.
b Isa. 52:8.
c M&M 117:7.
15 *a* M&M 38:32; 95:8; 110:8–10.
b MWM Kazi ya kimisionari.
c M&M 1:2.
17 *a* Yak. (KM) 5:61–75; M&M 24:19.
18 *a* MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.
20 *a* MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
21 *a* Mt. 24:36.
b JS—M 1:40.
23 *a* MWM Mikono, Kuweka juu ya.
b MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.

na [c]watatazamia ishara za [d]ujio wangu, na watanijua.

24 Tazama, naja haraka. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 40

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Sidney Rigdon, huko Fayette, New York, 6 Januari 1831. Kabla ya kumbu kumbu ya ufunuo huu, Historia ya Nabii inaeleza, "Wakati James Covel alipokataa neno la Bwana, na kurejea kwenye kanuni na watu wake wa awali, Bwana alinipa mimi na Sidney Rigdon ufunuo ufuatao" (sehemu ya 39).

1–3, Woga wa mateso na shughuli za ulimwengu husababisha kukataliwa kwa injili.

Tazama, amini ninawaambia, kwamba moyo wa mtumishi wangu [a]James Covel ulikuwa safi mbele zangu, kwani aliagana nami kuwa atatii neno langu.

2 Na [a]akalipokea neno kwa furaha, na moja kwa moja shetani akamjaribu; na woga na [b]mateso na shughuli za ulimwengu zikamsababisha yeye [c]kulikataa neno.

3 Kwa hiyo basi alivunja agano langu, na imebaki kwangu mimi kufanya kwake nilionalo kuwa ni jema. Amina.

SEHEMU YA 41

Ufunuo uliotolewa kupitia kwa Joseph Smith Nabii kwa Kanisa, huko Kirtland, Ohio, 4 Februari 1832. Ufunuo huu unawaamuru Nabii na wazee wa Kanisa wasali ili kupokea "sheria" ya Bwana (ona sehemu ya 42). Joseph Smith alikuwa ndiyo amewasili tu huko Kirtland akitokea New York, na Leman Copley, muumini wa Kanisa katika jirani ya Thompson, Ohio, "aliomba Ndugu Joseph na Sidney [Rigdon] . . . waishi pamoja naye na kwamba yeye angewapa nyumba na mahitaji yao mengine." Ufunuo ufuatao unaelezea mahali ambapo Joseph na Sidney wangepaswa kuishi na pia unamwita Edward Partridge kuwa askofu wa kwanza wa Kanisa.

1–3, Wazee wataliongoza Kanisa kwa roho wa ufunuo; 4–6, Wanafunzi wa kweli watapokea na kuzishika sheria za Bwana; 7–12, Edward Partridge atajwa kama askofu wa Kanisa.

23 *c* Ufu. 3:3; M&M 35:15; 45:39–44.
d 2 Pet. 3:10–14.

40 1 *a* M&M 39:7–11.
2 *a* Mk. 4:16–19.
b Mt. 13:20–22.

mwm Mateso, Tesa.
c mwm Ukengeufu.

Sikilizeni na mkasikie, Ee enyi watu wangu, asema Bwana na Mungu wenu, ninyi ambao nataka [a]kuwabariki kwa baraka kubwa kuliko baraka zote, ninyi mnaonisikia; na [b]nitawalaani ninyi ambao hamnisikii, ambao [c]mmelikiri jina langu, kwa laana nzito kuliko zote.

2 Sikilizeni, Enyi wazee wa kanisa langu ambao nimewaita, tazameni ninawapa amri kwamba mtakusanyika pamoja ninyi wenyewe ili [a]kukubaliana juu ya neno langu;

3 Na kwa sala ya imani yenu mtapokea [a]sheria yangu, ili muweze kujua jinsi ya kulitawala kanisa langu na mambo yote yawe sawa mbele yangu.

4 Na Mimi nitakuwa [a]mtawala wenu wakati [b]nitakapokuja; na tazama, naja upesi, nanyi mtaangalia kwamba sheria yangu imeshikwa.

5 Yeye ambaye [a]huipokea sheria yangu na [b]kuitenda, huyo ndiye mwanafunzi wangu; na yule asemaye ameipokea na haitendi, huyo siyo mwanafunzi wangu, na [c]ataondolewa kutoka miongoni mwenu;

6 Kwani si vyema kwamba vitu ambavyo ni vya watoto wa ufalme wakapewa wao ambao hawastahili, au kwa [a]mbwa, au [b]lulu kutupwa mbele ya nguruwe.

7 Na tena, ni vyema kwamba mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, ajengewe [a]nyumba, ambamo ataishi na [b]kutafsiri.

8 Na tena, ni vyema kwamba mtumishi wangu Sidney Rigdon aishi kama aonavyo yeye kuwa vyema, ili mradi ashike amri zangu.

9 Na tena, nimemwita mtumishi wangu [a]Edward Partridge; ninatoa amri, kwamba anapaswa kuteuliwa kwa sauti ya kanisa, na kutawazwa kuwa [b]askofu kwa kanisa, kuacha biashara zake na [c]kutumia muda wake wote kwa kazi za kanisa;

10 Kuangalia mambo yote kama itakavyoteuliwa kwake katika sheria zangu katika siku ambayo nitazitoa.

11 Na hii ni kwa sababu moyo wake ni safi mbele zangu, kwani yeye ni kama [a]Nathanieli wa zamani, hamna [b]hila ndani yake.

12 Maneno haya yametolewa kwenu, nayo ni safi mbele zangu; kwa hiyo, angalieni jinsi mnavyoyoyashika, kwani yatajibiwa juu ya nafsi zenu katika siku ya hukumu. Hivyo ndivyo. Amina.

---

41 1*a* MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
b Kum. 11:26–28; 1 Ne. 2:23.
c M&M 56:1–4; 112:24–26.
2*a* MWM Umoja.
3*a* M&M 42.
4*a* Zek. 14:9; M&M 45:59.
MWM Yesu Kristo—Utawala wa Kristo katika milenia.
b MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
5*a* Mt. 7:24.
b Yak. (Bib.) 1:22–25; M&M 42:60.
c M&M 50:8–9.
MWM Kutengwa na Kanisa.
6*a* Mt. 15:26.
b Mt. 7:6.
7*a* M&M 42:71.
b MY kutafsiri Biblia. M&M 45:60–61.
9*a* M&M 36:1.
b M&M 72:9–12; 107:68–75.
MWM Askofu.
c M&M 51.
11*a* Yn. 1:47.
b MWM Hila.

SEHEMU YA 42

Ufunuo uliotolewa katika sehemu mbili kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 9 na 23 Februari 1831. Sehemu ya kwanza, ina aya ya 1 hadi ya 72, ilipokelewa mbele ya wazee kumi na wawili na ni katika kutimiza ahadi ya Bwana aliyoifanya hapo awali kwamba "sheria" ingelitolewa Ohio (ona sehemu ya 38:32). Sehemu ya pili ina aya ya 73 hadi ya 93. Nabii anaelezea kuwa ufunuo huu ni kama "kukubali sheria ya Kanisa."

1–10, Wazee wameitwa kuhubiri injili, kubatiza waongofu, na kulijenga Kanisa; 11–12, Ni lazima waitwe na kutawazwa, na watafundisha kanuni za injili zipatikanazo katika maandiko; 13–17, Wao watafundisha na kutoa unabii kwa uwezo wa Roho; 18–29, Watakatifu wanaamriwa wasiue, wasiibe, wasiseme uongo, wasitamani, wasizini, au wasinene maovu dhidi ya wengine; 30–39, Sheria zinazotawala uwekaji wakfu kwa mali yatolewa; 40–42, Majivuno na uvivu vyalaaniwa; 43–52, Wagonjwa wataponywa kwa njia ya huduma na kwa imani; 53–60, Maandiko yanalitawala Kanisa na yatatangazwa kwa ulimwengu; 61–69, Kiwanja cha Yerusalemu Mpya na siri za ufalme zitafunuliwa; 70–73, Mali zilizowekwa wakfu zitumiwe kusaidia maofisa wa Kanisa; 74–93, Sheria zinazotawala uasherati, uzinzi, kuua, kuiba, na kuungama dhambi zinawekwa.

Sikilizeni, Enyi wazee wa kanisa langu, ambao mmekusanyika pamoja katika jina langu, hata Yesu Kristo Mwana wa Mungu aliye hai, Mwokozi wa ulimwengu; kwa sababu mnaliamini jina langu na kushika amri zangu.

2 Tena ninawaambia, sikilizeni na mkasikie na kuitii [a]sheria ambayo nitawapa.

3 Kwani amini ninasema, kama vile wenyewe mlivyokusanyika pamoja kulingana na [a]amri ambayo niliwaamuru, na [b]kukubaliana juu ya jambo hili moja, na mmemwomba Baba katika jina langu, hata hivyo nanyi mtapokea.

4 Tazama, amini ninawaambia, ninawapa amri hii ya kwanza, kwamba mtakwenda katika jina langu, kila mmoja wenu, isipokuwa watumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na Sidney Rigdon.

5 Na ninawapatia wao amri kwamba waende kwa muda mfupi, na itatolewa kwa uwezo wa [a]Roho lini wao warudi.

6 Nanyi mtaenenda katika nguvu ya Roho wangu, mkihubiri injili yangu, [a]wawili wawili, katika jina langu, mkipaza sauti zenu kama kwa sauti ya tarumbeta, mkilitangaza neno

42 2*a* M&M 58:23. MWM Sheria. 3*a* M&M 38:32. *b* Mt. 18:19. 5*a* MWM Roho Mtakatifu. 6*a* Mk. 6:7. MWM Kazi ya kimisionari.

langu kama vile malaika wa Mungu.

7 Na mtaenda kubatiza kwa maji, mkisema: Tubuni ninyi, tubuni ninyi, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.

8 Na toka mahali hapa mtaenda katika maeneo ya magharibi; na kadiri mtakavyowapata watakaowapokea ninyi mtajenga kanisa langu katika kila eneo—

9 Hadi wakati utakapokuja itakapofunuliwa kwenu kutoka juu, wakati ambao [a]mji wa [b]Yerusalemu Mpya utatayarishwa, ili muweze [c]kukusanyika mahali pamoja, ili muweze kuwa [d]watu wangu na Mimi nitakuwa Mungu wenu.

10 Na tena, ninawaambia, kwamba mtumishi wangu [a]Edward Partridge atasimama katika ofisi ambayo nimemteua. Na itakuwa, kwamba kama atavunja sheria [b]mwingine atateuliwa katika mahali pake. Hivyo ndivyo. Amina.

11 Tena ninawaambia, kwamba haitatolewa kwa yeyote kwenda [a]kuhubiri injili yangu, au kulijenga kanisa langu, isipokuwa [b]ametawazwa na mtu fulani aliye na [c]mamlaka, na ijulikane kwa kanisa kwamba anayo mamlaka na ametawazwa kwa utaratibu na viongozi wa kanisa.

12 Na tena, [a]wazee, makuhani na waalimu wa kanisa hili [b]watafundisha kanuni za injili yangu, ambayo imo katika [c]Biblia na [d]Kitabu cha Mormoni, ambamo umo utimilifu wa [e]injili.

13 Na watayashika [a]maagano na kanuni za kanisa na kuzitenda, na haya yatakuwa mafundisho yao, kama watakavyoelekezwa na Roho.

14 Na Roho atatolewa kwenu kwa [a]sala ya imani; na msipompokea [b]Roho msifundishe.

15 Na hii yote mtaendelea kutenda kama nilivyowaamuru juu ya kufundisha kwenu, hadi utimilifu wa [a]maandiko yangu matakatifu yamejulikana.

16 Na wakati mtakapopaza sauti zenu mkiongozwa na [a]Mfariji, mtanena na kutoa unabii kama nionavyo kuwa vyema;

17 Kwa maana, tazama, Mfariji ajua mambo yote, na humshuhudia Baba na Mwana.

9 *a* M&M 57:1–2.
b Eth. 13:2–11; M&M 45:66–71; 84:2–5; Musa 7:62; M ya I 1:10. MWM Yerusalemu Mpya.
c MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
d Zek. 8:8.
10 *a* M&M 41:9–11; 124:19.
b M&M 64:40.
11 *a* MWM Hubiri.
b MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito; Kutawaza, Kutawazwa.
c MWM Mamlaka; Ukuhani.
12 *a* MWM Mzee.
b Mos. 18:19–20; M&M 52:9, 36. MWM Fundisha, Mwalimu.
c MWM Biblia.
d MWM Kitabu cha Mormoni; Maandiko—Thamani ya maandiko.
e MWM Injili.
13 *a* MF M&M 20 (tazama kichwa cha habari sehemu ya 20).
14 *a* M&M 63:64. MWM Sala.
b MWM Fundisha, Mwalimu—Kufundisha kwa Roho; Roho Mtakatifu.
15 *a* M&M 42:56–58.
16 *a* 1 Kor. 2:10–14; M&M 68:2–4. MWM Mfariji.

18 Na sasa, tazama, nasema kwa kanisa. [a]Usiue; na yule [b]anayeua hatapata msamaha katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao.

19 Na tena, ninasema, usiue, lakini yule anayeua [a]atakufa.

20 [a]Usiibe; kwani na yule aibaye asipotubu atatupwa nje.

21 [a]Usiseme uongo; yule asemaye uongo na asipotubu atatupwa nje.

22 [a]Mpende mke wako kwa moyo wako wote, na [b]utaambatana na yeye tu na siyo mwingine.

23 Na yule amwangaliaye mwanamke kwa [a]kumtamani anaikana imani, na hatakuwa na Roho; na kama hatatubu atatupwa nje.

24 [a]Usizini; na yule afanyaye uzinzi, na hatubu, atatupwa nje;

25 Bali yule ambaye amezini na [a]kutubu kwa moyo wake wote, na kusahau, na asitende tena, [b]mtamsamehe;

26 Lakini akirudia [a]tena, hatasamehewa, bali atatupwa nje.

27 [a]Usimseme jirani yako uovu, wala usimdhuru.

28 Mnajua sheria zangu juu ya mambo haya zimetolewa katika maandiko yangu; yule atendaye dhambi na hatubu [a]atatupwa nje.

29 Kama [a]wanipenda [b]utanitumikia na [c]kushika amri zangu zote.

30 Na tazama, nanyi mtawakumbuka [a]maskini, na [b]kuweka wakfu baadhi ya mali zenu kwa ajili ya [c]kuwasaidia wao, kile mlichonacho kwa kuwasaidia wao, kwa agano na mkataba ambao hauwezi kuvunjwa.

31 Na kadiri [a]mtakavyotoa sehemu ya mali yenu kwa [b]maskini, mmenitendea Mimi; na mtaiweka mbele ya [c]askofu wa kanisa langu na washauri wake, wawili kati ya wazee, au makuhani wakuu, kama vile atakavyowateua na [d]kuwaweka rasmi kwa madhumuni hayo.

32 Na itakuja kutokea, kwamba baada ya kuwa imewekwa mbele ya askofu wa kanisa langu, na baada ya kuwa amepokea shuhuda hizi juu ya [a]kuwekwa wakfu kwa mali ya kanisa langu, kwamba haiwezi kuchukuliwa kutoka kanisani, kulingana na amri zangu,

18*a* Ku. 20:13–17; Mt. 5:21–37; 2 Ne. 9:35; Mos. 13:21–24; 3 Ne. 12:21–37.
b MWM Mauaji.
19*a* MWM Adhabu Kuu.
20*a* MWM Iba, Wizi.
21*a* MWM Kusema uongo; Mwaminifu, Uaminifu.
22*a* MWM Ndoa, Oa, Olewa; Upendo.
b Mwa. 2:23–24; Efe. 5:25, 28–33.
23*a* Mt. 5:28; 3 Ne. 12:28; M&M 63:16. MWM Tamaa mbaya.
24*a* MWM Uzinzi.
25*a* MWM Toba, Tubu.
b Yn. 8:3–11. MWM Samehe.
26*a* 2 Pet. 2:20–22; M&M 82:7.
27*a* MWM Sengenya.
28*a* MWM Kutengwa na Kanisa.
29*a* Yn. 14:15, 21.
b MWM Utumishi.
c MWM Mtiifu, Tii, Utii.
30*a* Mos. 4:16–26; Alma 1:27. MWM Maskini.
b MWM Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.
c MWM Ustawi.
31*a* Mos. 2:17. MWM Sadaka, Utoaji sadaka.
b MWM Maskini.
c MWM Askofu.
d MWM Usimikaji.
32*a* M&M 51:4.

kila mtu atafanywa [b]awajibike kwangu, [c]mtumishi juu ya mali yake mwenyewe, au ile ambayo ameipokea kwa kuweka wakfu, ilimradi ni ya kutosha kwake mwenyewe na kwa [d]familia yake.

33 Na tena, kama kutakuwa na mali katika mikono ya kanisa, au mmoja wa watu wake, zaidi kuliko mahitaji yao baada ya uwekaji wakfu huu wa kwanza, ambayo ni [a]mabaki yatawekwa wakfu kwa askofu, nayo yatatunzwa kwa kuwahudumia wale wasionacho, mara kwa mara, kusudi kila mtu mwenye shida aweze kupewa vya kutosha na kupokea kulingana na mahitaji yake.

34 Kwa hivyo, mabaki yatatunzwa ghala ni mwangu, kwa kuwahudumia maskini na wenye shida, kama itakavyoamriwa na baraza kuu la kanisa, na askofu na baraza lake;

35 Na kwa madhumuni ya ununuzi wa ardhi kwa manufaa ya jumuia ya kanisa langu, na ujenzi wa nyumba za kuabudu, na ujenzi wa [a]Yerusalemu Mpya ambayo itafunuliwa hapo baadaye—

36 Ili watu wangu wa agano waweze kukusanywa mahali pamoja katika siku ile wakati [a]nitakapokuja kwenye [b]hekalu langu. Na hii nitafanya kwa ajili ya wokovu wa watu wangu.

37 Na itakuwa, kwamba yule ambaye hutenda dhambi na hatubu [a]atatupwa nje ya kanisa, na hatapokea tena kile ambacho alikiweka [b]wakfu kwa maskini na wenye shida wa kanisa langu, au kwa maneno mengine, kwangu Mimi—

38 Kwani kadiri [a]mlivyomtendea mmojawapo wa hawa, mmenitendea Mimi.

39 Kwani itakuwa, kwamba kile nilichokinena kwa vinywa vya manabii wangu kitatimizwa; kwa kuwa nitaweka wakfu utajiri wa wale ambao huikumbatia injili yangu miongoni mwa Wayunani kwa maskini wa watu wangu ambao ni wa nyumba ya Israeli.

40 Na tena, nawe usiwe na [a]majivuno katika moyo wako; [b]mavazi yako yawe ya kawaida, na uzuri wao uwe uzuri wa kazi za mikono yako;

41 Na mambo yote yafanyike katika usafi mbele yangu.

42 Usiwe [a]mvivu; kwani yule aliye mvivu hatakula mkate wala kuvaa mavazi ya mfanya kazi.

43 Na yeyote miongoni mwenu aliye [a]mgonjwa, na hana imani ya kuponywa, lakini anaamini, alishwe mboga na

32 *b* M&M 72:3–11. MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
c MWM Msimamizi, Usimamizi.
d M&M 51:3.
33 *a* M&M 42:55; 51:13; 119:1–3.
35 *a* MWM Sayuni; Yerusalemu Mpya.
36 *a* M&M 36:8.
b Mal. 3:1.
37 *a* M&M 41:5; 50:8–9. MWM Kutengwa na Kanisa.
b MWM Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.
38 *a* Mt. 25:34–40. MWM Hisani; Ustawi.
40 *a* Mit. 16:5. MWM Kiburi.
b MWM Staha.
42 *a* M&M 68:30–32. MWM Mvivu, Uvivu.
43 *a* MWM Ugonjwa, Ugua.

chakula laini, na kwamba siyo kwa mkono wa adui.

44 Na wazee wa kanisa, wawili au zaidi, wataitwa, na watamwombea kwa kuweka [a]mikono yao juu yao katika jina langu; na kama [b]watakufa, watakufa kwangu, na kama wataishi, wataishi kwangu.

45 Nawe [a]utaishi pamoja katika [b]upendo, kwa kiasi kwamba [c]utalia kwa upotevu wa wale wanaokufa, na hasa kwa wale ambao hawana [d]tumaini la ufufuko mtukufu.

46 Na itakuwa kwamba wale wanaokufa kwangu hawataonja [a]mauti, kwani itakuwa [b]vyema kwao;

47 Na wale wasiokufa kwangu, ole wao, kwani kifo chao ni kichungu.

48 Na tena, itakuwa kwamba yule aliye na [a]imani kwangu ya [b]kuponywa, na [c]hakuteuliwa kufa, ataponywa.

49 Yule aliye na imani ya kuona ataona.

50 Yule aliye na imani ya kusikia atasikia.

51 Kiwete aliye na imani ya kuruka ataruka.

52 Na wale ambao hawana imani ya kufanya mambo haya, lakini wanayo imani na Mimi, wanao uwezo wa kuwa [a]wana wangu; ilimradi hawavunji sheria zangu wewe [b]utaubeba udhaifu wao.

53 Utasimama katika mahali pa [a]usimamizi wako.

54 Usichukue vazi la ndugu yako; nawe utalipa kwa kile utakachokipokea kutoka kwa ndugu yako.

55 Na kama [a]utapata zaidi kuliko mahitaji yako, utaitoa katika [b]ghala yangu, kwamba yote yaweze kufanyika kulingana na kile nilichosema.

56 Nanyi mtaniomba, na [a]maandiko yangu yatatolewa kama nilivyonena, nayo [b]yatatunzwa katika usalama;

57 Na ni vyema kwamba yawapasa kunyamaza juu yake, na msiyafundishe hadi mtakapoyapokea katika ukamilifu.

58 Na ninatoa kwenu ninyi amri kwamba ndipo mtayafundisha kwa watu wote; kwani yatafundishwa kwa mataifa [a]yote, makabila, lugha na watu.

59 Utayachukua mambo ambayo umeyapokea, ambayo yametolewa kwako katika maandiko yangu kuwa sheria, kuwa sheria ya kulitawala kanisa langu;

60 Na yule ambaye [a]huyatenda

44a MWM Huduma kwa Wagonjwa; Mikono, Kuweka juu ya.
b Rum. 14:8; Ufu. 14:13; M&M 63:49.
45a 1 Yoh. 4:16, 20–21.
b MWM Upendo.
c Alma 28:11–12.
d 1 Kor. 15:19–22. MWM Tumaini.
46a MWM Mauti ya Kimwili.
b Ufu. 14:13.
48a M&M 46:19. MWM Amini, Imani.
b MWM Ponya, Uponyaji.
c Mh. 3:1–2; Mdo. 17:26; Ebr. 9:27; M&M 122:9.
52a MWM Wana na Mabinti za Mungu.
b Rum. 15:1. MWM Ushirika.
53a MWM Msimamizi, Usimamizi.
55a M&M 82:17–19; 119:1–3.
b M&M 42:34; 51:13.
56a M&M 45:60–61.
b MWM Maandiko—Thamani ya maandiko.
58a M&M 1:2.
60a M&M 41:5. MWM Mtiifu, Tii, Utii.

kulingana na mambo haya ataokolewa, na yule ambaye hayatendi [b]atahukumiwa kama ataendelea hivyo.

61 Ikiwa utaomba, nawe utapokea [a]ufunuo juu ya ufunuo, [b]maarifa juu ya maarifa, ili uweze kujua [c]siri na mambo ya [d]amani—yale ambayo huleta [e]shangwe, yale ambayo huleta uzima wa milele.

62 Nawe utaomba, na itafunuliwa kwako kwa wakati wangu mahali ambapo [a]Yerusalemu Mpya itajengwa.

63 Na tazama, itakuwa kwamba watumishi wangu watatumwa mashariki na magharibi, kaskazini na kusini.

64 Na hata sasa, na yule aendaye mashariki awafundishe wale watakaoongoka kukimbilia [a]magharibi, na hii ni katika matokeo ya kile ambacho chaja juu ya ulimwengu, na [b]makundi maovu ya siri.

65 Tazama, nawe utatii mambo haya yote, na thawabu yako itakuwa kubwa; kwani kwako imetolewa kujua siri za ufalme, bali kwa walimwengu haikutolewa kujua.

66 Nanyi mtatii sheria ambazo mmezipokea na kuwa waaminifu.

67 Na hapo baadaye mtapokea [a]maagano ya kanisa, kiasi cha kuwatosha ninyi kuendelea, kote hapa na katika Yerusalemu Mpya.

68 Kwa hivyo, yule ambaye amepungukiwa [a]hekima, na aniombe mimi, na nitampa yeye kwa ukarimu na sitamkemea.

69 Inueni mioyo yenu na mfurahi, kwani kwenu [a]ufalme, au kwa maneno mengine, [b]funguo za kanisa zimetolewa. Hivyo ndivyo. Amina.

70 [a]Makuhani na [b]walimu watapewa [c]usimamizi, hata kama waumini.

71 Na wazee au makuhani wakuu ambao wameteuliwa kumsaidia askofu kama washauri katika mambo yote, familia zao zita saidiwa kwa mali iliyowekwa [a]wakfu kwa askofu, kwa ajili ya maskini, na kwa madhumuni mengineyo, kama ilivyotajwa hapo awali;

72 Au watapokea ujira kwa huduma zao zote, iwe kwa usimamizi au vinginevyo, kama itakavyoonekana vema au kuamuliwa na washauri na askofu.

73 Na askofu pia, atapokea msaada wake, au malipo ya haki kwa huduma zake zote katika kanisa.

74 Tazama, amini ninawaambia, kwamba mtu yeyote

60 *b* Musa 5:15.
MWM Hukumu.
61 *a* MWM Ufunuo.
b Ibr. 1:2.
MWM Maarifa; Ushuhuda.
c M&M 63:23.
MWM Siri za Mungu.
d M&M 39:6.
e MWM Shangwe.
62 *a* M&M 57:1–5.
64 *a* M&M 45:64.
b MWM Makundi maovu ya siri.
67 *a* M&M 82:11–15.
68 *a* Yak. (Bib.) 1:5.
MWM Hekima.
69 *a* MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
b Mt. 16:19; M&M 65:2.
MWM Funguo za Ukuhani.
70 *a* MWM Kuhani, Ukuhani wa Haruni.
b MWM Mwalimu, Ukuhani wa Haruni.
c MWM Msimamizi, Usimamizi.
71 *a* MWM Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.

miongoni mwenu, atakayemwacha mwenzi wake kwa sababu ya [a]uasherati, au kwa maneno mengine, kama watathibitisha mbele yenu kwa unyenyekevu wote wa moyo kwamba hiyo ndiyo sababu, msiwatupe nje kutoka miongoni mwenu;

75 Lakini kama mtapata mtu yeyote amemwacha mwenzi wake kwa ajili ya [a]uzinzi, naye ndiye mkosaji, na wenzi hao wanaishi, [b]watupwe nje kutoka miongoni mwenu.

76 Na tena, ninawaambia, kwamba mtakuwa [a]waangalifu, kwa kuwahoji, ili msimpokee yeyote wa aina hiyo miongoni mwenu kama wameoa au kuolewa;

77 Na kama hawajaoa au kuolewa, watubu dhambi zao zote, au msiwapokee.

78 Na tena, mtu yeyote aliye wa kanisa hili la Kristo, atazishika na kutii amri zote na maagano ya kanisa.

79 Na itakuwa, kwamba kama mtu yeyote miongoni mwenu [a]ataua atolewe na kushughulikiwa kulingana na sheria za nchi; kwani kumbukeni kwamba yeye hana msamaha; na itathibitika kulingana na sheria za nchi.

80 Na kama mwanaume yeyote au mwanamke atazini, ashtakiwe mbele ya wazee wawili wa kanisa, au zaidi, na kila neno litathibitika dhidi yake kwa mashahidi wawili wa kanisa, na si kwa adui; lakini kama kuna zaidi ya wawili ni bora zaidi.

81 Lakini yeye atahukumiwa kwa vinywa vya mashahidi wawili; na wazee wataliweka shauri mbele ya kanisa, na kanisa litanyosha mkono dhidi yake, ili kwamba waweze kushughulikiwa kulingana na sheria ya Mungu.

82 Na kama yawezekana, askofu ni muhimu awepo pia.

83 Na hivi ndivyo mtakavyofanya katika kila shauri litakalokuja mbele yenu.

84 Na kama mwanaume au mwanamke atapora, huyo atolewe kwa sheria ya nchi.

85 Na kama mwanaume au mwanamke [a]ataiba, hivyo atolewe kwa sheria ya nchi.

86 Na kama mwanaume au mwanamke [a]atadanganya, atolewe kwa sheria za nchi.

87 Na mwanaume au mwanamke atafanya aina yoyote ya uovu, huyo atatolewa kwa sheria, hata ile ya Mungu.

88 Na kama [a]kaka au dada yako [b]amekukosea, utamchukua yeye na kati yenu ninyi peke yenu; na kama [c]atakiri mtapaswa kupatana.

89 Na kama hakiri mtoe kwa kanisa, siyo kwa waumini, bali kwa wazee. Na itafanyika katika mkutano, na kwamba siyo mbele ya ulimwengu.

90 Na kama kaka au dada

74*a* MWM Uasherati; Utovu wa maadili ya kujamiiana.
75*a* MWM Uzinzi.
b MWM Kutengwa na Kanisa.
76*a* MWM Kesha, Walinzi.
79*a* MWM Mauaji.
85*a* MWM Iba, Wizi.
86*a* MWM Kusema uongo; Mwaminifu, Uaminifu.
88*a* MWM Dada; Kaka, Ndugu.
b Mt. 18:15–17.
c MWM Kiri, Kukiri.

yako amewakosea wengi, na [a]akavipiwe mbele ya wengi.

91 Na kama mtu yeyote anakosea wazi, na akemewe wazi, ili aweze kuaibika. Na kama hakiri, atolewe kwa sheria ya Mungu.

92 Kama mtu yeyote anakosea kwa siri, akanywe kwa siri, ili aweze kupata nafasi ya kukiri kwa siri kwake yeye aliyemkosea, na kwa Mungu, ili kanisa lisiweze kumfedhehesha.

93 Na hivyo ndivyo mtakavyojiendesha katika mambo yote.

SEHEMU YA 43

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, Februari 1831. Kwa wakati huu baadhi ya waumini wa Kanisa walikuwa wakisumbuliwa na watu waliokuwa wakijifanya wao kuwa ni wafunuzi. Nabii alimwomba Bwana na kupokea mawasiliano haya yaliyoelekezwa kwa wazee wa Kanisa. Sehemu ya kwanza hushughulika na masuala ya utawala wa Kanisa; sehemu ya mwisho ina maonyo ambayo wazee lazima wayatoe kwa mataifa ya ulimwengu.

1–7, Mafunuo na amri huja tu kupitia mteule mmoja; 8–14, Watakatifu wanatakaswa kwa kutenda katika utakatifu wote mbele za Bwana; 15–22, Wazee wanatumwa kuhubiri toba na kuwatayarisha watu kwa ajili ya siku kuu ya Bwana; 23–28, Bwana huwaita watu kwa sauti Yake mwenyewe na kwa nguvu za asili; 29–35, Milenia na kufungwa kwa Shetani vitakuja.

Ee sikilizeni, ninyi wazee wa kanisa langu, na mtege sikio kwa maneno ambayo nitayasema kwenu.

2 Kwani tazama, amini, amini ninawaambia, kwamba mmeipokea amri kama [a]sheria kwa kanisa langu, kupitia yule ambaye nimemteua kwenu kupokea [b]amri na mafunuo kutoka mikononi mwangu.

3 Kwa hakika jueni—kwamba hakuna mwingine yeyote aliyeteuliwa kwenu kupokea amri na mafunuo hadi atakapochukuliwa, kama [a]atakaa ndani yangu.

4 Lakini amini, amini, ninawaambia, kwamba [a]hakuna mwingine yeyote atakayeteuliwa kupokea kipawa hiki isipokuwa iwe kupitia kwake; kwani kama kitachukuliwa kutoka kwake hatakuwa na uwezo isipokuwa kumteua mwingine mahali pake.

5 Na hii itakuwa sheria kwenu, kwamba msipokee mafundisho ya yeyote yatakayokuja mbele yenu kama mafunuo au amri;

90*a* mwm Rudi, Kurudiwa.
43 2*a* M&M 42.
b mwm Amri za Mungu; Ufunuo.
3*a* Yn. 15:4.
4*a* M&M 28:2–3.

6 Na hii ninaitoa kwenu ili msiweze [a]kudanganyika, kwamba muweze kujua kwamba siyo wangu.

7 Kwani amini ninawaambia kwamba yule ambaye [a]ametawazwa na Mimi ataingia [b]mlangoni na atatawazwa kama nilivyowaambia hapo awali, kufundisha mafunuo yale ambayo mmeyapokea na mtakayopokea kupitia kwake yeye niliyemteua.

8 Na sasa, tazama, ninawapa ninyi amri, kwamba wakati mkikusanyika pamoja [a]mtaelekezana na kuinuana ninyi kwa ninyi, ili muweze kujua namna ya kutenda na kulielekeza kanisa langu, namna ya kutenda juu ya mafundisho ya sheria na amri zangu, ambazo nimewapa.

9 Na hivyo ndivyo mtafundishwa katika sheria ya kanisa langu, na [a]mtakaswe kwa kile mlichokipokea, nanyi mtajifunga wenyewe kutenda katika utakatifu wote mbele zangu—

10 Kwamba kadiri mtakavyofanya haya, utukufu [a]utaongezwa kwenye ufalme ambao mmepokea. Kadiri msivyo yafanya haya, [b]kitachukuliwa, hata ambacho mmekipokea.

11 Safisheni [a]uovu ulioko miongoni mwenu; jitakaseni wenyewe mbele yangu;

12 Na kama mnataka utukufu wa ufalme, mkubalini mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na [a]muungeni mkono yeye mbele yangu kwa sala ya imani.

13 Na tena, ninawaambia, kwamba kama mnataka [a]siri za ufalme, mpatieni chakula na mavazi, na vitu vyote ahitajivyo kukamilisha kazi ambayo nimemwamuru;

14 Na kama hamtayafanya atabakia kwao waliompokea, ili niweze kuhifadhia watu walio [a]safi mbele zangu.

15 Tena ninasema, sikilizeni ninyi wazee wa kanisa langu, ambao nimewateua: Hamjatumwa [a]kufundishwa, bali kufundisha wanadamu mambo ambayo nimeyaweka mikononi mwenu kwa uwezo wa [b]Roho wangu;

16 Na [a]mtafundishwa kutoka juu. [b]Jitakaseni na [c]mtajaliwa uwezo, ili muweze kutoa kama nilivyonena.

17 Sikilizeni ninyi, kwani, tazama, [a]siku ile [b]kuu ya Bwana imekaribia.

18 Kwani siku yaja ambayo

6*a* M&M 46:7. MWM Danganya, Kudanganya, Udanganyifu.
7*a* MWM Kutawaza, Kutawazwa.
b Mt. 7:13–14; 2 Ne. 9:41; 31:9, 17–18; 3 Ne. 14:13–14; M&M 22.
8*a* M&M 88:77.
9*a* MWM Utakaso.
10*a* Alma 12:10.
b Mk. 4:25.
11*a* MWM Dhambi.
12*a* MWM Kuwakubali Viongozi wa Kanisa.
13*a* MWM Siri za Mungu.
14*a* MWM Safi na Isiyo safi.
15*a* MWM Kazi ya kimisionari.
b MWM Fundisha, Mwalimu—Kufundisha kwa Roho.
16*a* MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi.
b MWM Utakaso.
c Lk. 24:49; M&M 38:32; 95:8–9; 110:8–10.
17*a* M&M 29:8. MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b Mal. 4:5; M&M 2:1; 34:6–9.

Bwana atatoa [a]sauti yake toka mbinguni; mbingu [b]zitatikisika na nchi [c]itatetemeka, na [d]parapanda ya Mungu italia kwa sauti yenye kuendelea na kwa sauti, na atasema kwa mataifa yaliyolala: ninyi watakatifu [e]amkeni na muishi; ninyi wenye dhambi [f]bakini na [g]mlale hadi nitakapoita tena.

19 Kwa hiyo fungeni viuno vyenu msije kukutwa miongoni mwa waovu.

20 Piga kelele na usiache. Yaiteni mataifa kutubu, wazee kwa vijana, wafungwa na walio huru, mkisema: Jitayarisheni wenyewe kwa siku ile kuu ya Bwana;

21 Kwani kama Mimi, niliye mwanadamu, napiga kelele na kuwaita ninyi kutubu, na mnanichukia, mtasema nini wakati siku ile itakapokuja wakati ngurumo ya [a]radi itakapotoa ngurumo kutoka miisho ya dunia, ikisema kwenye masikio ya wale wote walio hai, ikisema—Tubuni, na jitayarisheni kwa ajili ya siku ile kuu ya Bwana?

22 Ndiyo, na tena, wakati vimulimuli vya radi vitakapomulika kutoka mashariki hadi magharibi, na kutoa sauti zao kwa wale wote waishio, na kufanya masikio ya wote kuwaka ya wale wenye kusikia, zikisema maneno haya—Tubuni ninyi, kwani siku ile kuu ya Bwana imekuja?

23 Na tena, Bwana atatoa sauti yake kutoka mbinguni, akisema: Sikieni, Enyi mataifa ya dunia, na yasikilizeni maneno ya yule Mungu aliyewaumba ninyi.

24 Ee, ninyi mataifa ya dunia, ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja kama vile [a]kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini [b]hamkutaka!

25 Na ni mara ngapi [a]nimewaita ninyi kwa vinywa vya [b]watumishi wangu, na kwa [c]kutembelewa na malaika, na kwa sauti yangu mwenyewe, na kwa sauti ya ngurumo za radi, na kwa sauti ya radi, na kwa sauti za tufani, na kwa sauti za matetemeko ya ardhi, na kwa tufani ya mvua ya mawe, na kwa sauti za [d]njaa, na madhara ya kila aina, na kwa sauti kuu ya parapanda, na kwa sauti ya hukumu, na kwa sauti ya [e]huruma kwa siku nzima, na kwa sauti ya utukufu na heshima na utajiri wa uzima wa milele, na ningewaokoa kwa wokovu [f]usio na mwisho, lakini hamkutaka!

26 Tazama, siku imekuja, wakati kikombe cha ghadhabu ya

18 *a* Yoe. 2:11; M&M 133:50.
b Yoe. 2:10; 3:16; M&M 45:48.
c M&M 88:87.
d M&M 29:13; 45:45.
e MWM Ufufuko.
f M&M 76:85; 88:100–101.
g Morm. 9:13–14.
21 *a* 2 Ne. 27:2; M&M 88:90.
24 *a* Mt. 23:37; 3 Ne. 10:4–6.
b MWM Uasi.
25 *a* Hel. 12:2–4.
b Mt. 23:34. MWM Nabii.
c M&M 7:6; 130:4–5.
d Yer. 24:10; Amo. 4:6; M&M 87:6; JS—M 1:29.
e MWM Rehema, enye Rehema.
f MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa; Uzima wa Milele; Wokovu.

uchungu wa hasira yangu kimejaa.

27 Tazama, amini ninawaambia, kwamba haya ni maneno ya Bwana Mungu wenu.

28 Kwa hivyo, fanyeni kazi, [a]fanyeni kazi katika shamba langu la mizabibu kwa mara ya mwisho—kwa mara ya mwisho waiteni wakazi wa dunia hii.

29 Kwani katika saa yangu mwenyewe [a]nitakuja juu ya dunia katika hukumu, na watu wangu watakombolewa na watatawala pamoja nami duniani.

30 Kwani ile [a]Milenia kuu, ambayo niliinena kwa vinywa vya watumishi wangu itakuja.

31 Kwani [a]Shetani atakuwa [b]amefungwa, na wakati atakapoachiliwa tena atatawala kwa [c]kipindi kifupi tu, na hapo ndipo [d]mwisho wa dunia utakapokuja.

32 Na yule ambaye anaishi katika [a]haki [b]atabadilishwa katika kufumba na kufumbua macho, na dunia itapita kama vile kwa moto.

33 Na waovu watakwenda zao katika [a]moto usiozimika, na mwisho wao hakuna mtu aujuaye hapa duniani, wala kamwe hatajua, hadi watakapokuja mbele yangu katika [b]hukumu.

34 Sikilizeni ninyi maneno haya. Tazama, Mimi ni Yesu Kristo, [a]Mwokozi wa ulimwengu. [b]Yatunzeni mambo haya katika mioyo yenu, na [c]taadhima ya milele [d]iwe [e]akilini mwenu.

35 Kuweni [a]makini. Shikeni amri zangu zote. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 44

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Sidney Rigdon, huko Kirtland, Ohio, mwishoni mwa Februari 1831. Katika kutimiza masharti yaliyowekwa humu, Kanisa lilipanga mkutano ufanyike mapema katika mwezi wa Juni iliyofuata.

1–3, Wazee wakusanyike katika mkutano; 4–6, Wanapaswa kulianzisha kulingana na sheria za nchi na kuwajali maskini.

Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu ninyi watumishi wangu, ni muhimu kwangu kuwa wazee wa kanisa

28 *a* Yak. (KM) 5:71; M&M 33:3. MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
29 *a* MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
30 *a* MWM Milenia.
31 *a* 1 Ne. 22:26. MWM Ibilisi.
b M&M 45:55; 84:100; 88:110.
c Ufu. 20:3; Yak. (KM) 5:77; M&M 29:22.
d MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.
32 *a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
b 1 Kor. 15:51–52; M&M 63:51; 101:31. MWM Ufufuko.
33 *a* Mt. 3:12.
b MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.
34 *a* MWM Mwokozi.
b JS—M 1:37.
c M&M 84:61; 100:7–8.
d MWM Tafakari.
e MWM Nia.
35 *a* Rum. 12:3; M&M 18:21.

langu yawapasa waitwe pamoja, kutoka mashariki na kutoka magharibi, na kutoka kaskazini na kutoka kusini, kwa barua au njia nyinginezo.

2 Na itakuwa kwamba kadiri watakavyokuwa waaminifu, na kutenda imani kwangu, nitaimwaga [a]Roho yangu juu yao katika siku ile watakayokutana pamoja.

3 Na itakuwa kwamba watakwenda kwenye maeneo yaliyowazunguka, na [a]kuhubiri toba kwa watu.

4 Na wengi [a]wataongolewa, kiasi kwamba mtapata nguvu ya kujisimamia wenyewe [b]kulingana na sheria za mwanadamu;

5 Ili kwamba [a]maadui zenu wasiweze kuwa na nguvu juu yenu; ili muweze kulindwa katika mambo yote; ili muwezeshwe kushika sheria zangu; kwamba kila mnyororo uweze kuvunjwa ambao kwa huo adui ataka kuwaangamiza watu wangu.

6 Tazama, ninawaambia, kwamba inawalazimu [a]kuwatembelea wagonjwa na wenye shida na kuwapatia msaada, ili waweze kutunzwa hadi mambo yote yaweze kufanywa kulingana na sheria yangu ambayo mmeipokea. Amina.

SEHEMU YA 45

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Kanisa, huko Kirtland, Ohio, 7 Machi 1831. Kama utangulizi wa kumbu kumbu ya ufunuo huu, Historia ya Joseph Smith inaeleza kwamba "katika umri huu wa Kanisa . . . taarifa nyingi za uongo . . . na hadithi za kijinga, zilichapishwa . . . na kusambazwa, ili kuwazuia watu wasichunguze kazi, au kuikumbatia imani. . . . Lakini kwa shangwe ya Watakatifu, nilipokea yafuatayo."

1–5, Kristo ni mtetezi wetu kwa Baba; 6–10, Injili ni ujumbe wa kuitengeneza njia mbele za Bwana; 11–15, Enoki na nduguze wamepokelewa kwa Bwana Mwenyewe; 16–23, Kristo alifunua ishara za ujio Wake kama zilivyotolewa kwenye Mlima wa Mizeituni; 24–38, Injili itarejeshwa, nyakati za Wayunani zitakapotimia, na maradhi ya ukiwa yatakapoifunika nchi; 39–47, Ishara, maajabu na Ufufuko zitaambatana na Ujio wa Pili; 48–53, Kristo atasimama juu ya Mlima wa Mizeituni, na Wayahudi wataona majeraha katika mikono Yake na miguu; 54–59, Bwana atatawala wakati wa Milenia; 60–62, Nabii anaelekezwa kuanza tafsiri ya Agano Jipya, kupitia hilo taarifa muhimu zitafanywa kujulikana; 63–75,

44 2*a* Mdo. 2:17.
3*a* MWM Hubiri.
4*a* MWM Mwongofu, Uongofu.
b M&M 98:5–7.
5*a* 2 Ne. 4:33.
6*a* Yak. (Bib.) 1:27. MWM Huruma; Ustawi.

Watakatifu wanaamriwa kukusanyika na kujenga Yerusalemu Mpya, ambamo watu kutoka mataifa yote watakuja.

Sikilizeni, Enyi watu wa [a]kanisa langu, ambao kwenu [b]ufalme umetolewa; sikilizeni na mtege sikio kwake yule aliyeweka msingi wa dunia, na [c]aliyefanya mbingu na vyote vilivyomo, na ambaye kwake yeye vitu vyote vilifanyika vinavyoishi, na vinavyokwenda, na kuwa na uhai.

2 Na tena ninasema, sikilizeni sauti yangu, isije [a]mauti ikawapata; katika saa msiyodhani [b]wakati wa majira ya joto yamepita, na [c]mavuno yamekwisha, na nafsi zenu hazijaokolewa.

3 Msikilizeni yeye aliye [a]mtetezi kwa Baba, anayetetea mambo yetu mbele zake—

4 Akisema: Baba, tazama [a]mateso na kifo chake yeye ambaye hakutenda [b]dhambi, ambaye ulipendezwa naye; tazama damu ya mwanao iliyomwagika; damu yake yeye ambaye ulimtoa ili upate [c]kutukuzwa;

5 Kwa hiyo, Baba, wasamehe hawa ndugu zangu ambao [a]wanaamini juu ya neno langu, ili waweze kuja kwangu na kupata [b]uzima usio na mwisho.

6 Sikilizeni, Enyi watu wa kanisa langu, nanyi wazee sikilizeni kwa pamoja, na isikilizeni sauti yangu wakati iitapo [a]leo, na msiishupaze mioyo yenu;

7 Kwani amini ninawaambia kwamba Mimi ni [a]Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, nuru na uzima wa ulimwengu—[b]nuru ile ing'aayo gizani na giza haiitambui.

8 Nilikuja kwa walio wangu, na walio wangu hawakunipokea; bali wote walionipokea niliwapa [a]uwezo wa kufanya [b]miujiza mingi, na kuwa [c]wana wa Mungu; na hata kwa wale wote ambao [d]waliamini juu ya jina langu niliwapa uwezo wa kupata [e]uzima wa milele.

9 Na hata hivyo nimepeleka [a]agano langu [b]lisilo na mwisho ulimwenguni, liwe nuru ya ulimwengu, na itakuwa [c]ishara kwa watu wangu, na kwa [d]Wayunani waitafute, na kuwa [e]ujumbe mbele ya uso wangu atakayeitengeneza njia mbele zangu.

10 Kwa hiyo, njooni, na pamoja naye yule ajaye nitahojiana

45 1*a* mwm Kanisa la Yesu Kristo.
b M&M 50:35.
c Yer. 14:22; 3 Ne. 9:15; M&M 14:9.
mwm Umba, Uumbaji.
2*a* Alma 34:33–35.
b Mt. 24:44.
c Yer. 8:20; M&M 56:16.
mwm Mavuno.
3*a* M&M 62:1.
mwm Mtetezi.
4*a* M&M 19:18–19.
mwm Lipia dhambi, Upatanisho.
b Ebr. 4:15.
c Yn. 12:28.
5*a* M&M 20:25; 35:2; 38:4.
b Yn. 3:16.
6*a* Ebr. 3:13; M&M 64:23–25.
7*a* Ufu. 1:8; 21:6; M&M 19:1.
b Yn. 1:5.
8*a* Mt. 10:1.
mwm Uwezo.
b mwm Muujiza.
c mwm Wana na Mabinti za Mungu.
d mwm Amini, Imani.
e M&M 14:7.
9*a* mwm Agano Jipya na Lisilo na Mwisho.
b Yer. 31:31–34; Morm. 5:20.
c 2 Ne. 29:2.
d Isa. 42:6; 2 Ne. 10:9–18.
e Mal. 3:1.

naye kama vile watu katika siku za kale, na nitawaonyesha ninyi hoja zangu zenye [a]nguvu.

11 Kwa hiyo, sikilizeni ninyi kwa pamoja na acheni niwaonyeshe hata hekima yangu—hekima yake huyo msemaye ni Mungu wa [a]Henoko, na ndugu zake,

12 [a]Waliotengwa kutoka duniani, na kupokelewa kwangu mwenyewe—[b]mji uliohifadhiwa hadi siku ya haki itakapofika—siku ambayo ilitafutwa na watu wote watakatifu, na hawakuipata kwa sababu ya uovu na machukizo;

13 Na wakakiri kwamba walikuwa [a]wageni na wasafiri juu ya dunia;

14 Lakini wakapata [a]ahadi kwamba yawapasa kuitafuta na kuiona wakiwa katika miili yao.

15 Kwa hiyo, sikilizeni na mimi nitahojiana na nanyi, na nitasema kwenu na kutoa unabii, kama kwa watu katika siku za kale.

16 Nami nitaonyesha wazi kama [a]nilivyoonyesha kwa wanafunzi wangu kama nilivyosimama mbele yao katika mwili, na kuwaambia wao, nikisema: Kama mlivyoomba kwangu juu ya [b]ishara za kuja kwangu, katika siku nitakapokuja katika utukufu wangu katika mawingu ya mbinguni, ili kuzitimiza ahadi ambazo nilizifanya kwa babu zenu,

17 Kama mlivyoangalia [a]kutoweka kwa muda mrefu kwa [b]roho zenu kutoka katika miili yenu kuwa hali ya kufungwa, nitaonyesha kwenu jinsi siku ya ukombozi itakavyokuja, na pia [c]urejesho wa Waisraeli [d]waliotawanywa.

18 Na sasa mmeliona hili hekalu lililoko katika Yerusalemu, ambalo mnaliita nyumba ya Mungu, na maadui zenu wanasema kwamba nyumba hii kamwe haitaanguka.

19 Lakini, amini ninawaambia, kwamba ukiwa utakuja juu ya kizazi hiki kama vile mwizi ajavyo usiku, na watu hawa wataangamizwa na kutawanywa miongoni mwa mataifa yote.

20 Na hekalu hili ambalo mnaliona litatupwa chini kwamba halitasalia jiwe juu ya jiwe.

21 Na itakuwa, kwamba kizazi hiki cha Wayahudi hakitapita hadi kila ukiwa ambao nimewaambia juu yao utakapotokea.

22 Ninyi mnasema kwamba mnajua kwamba [a]mwisho wa ulimwengu unakuja; mnasema pia mnajua kwamba mbingu na dunia zitapita;

23 Na katika hii ninyi mnasema

10 *a* Isa. 41:21; M&M 50:10–12.
11 *a* Musa 7:69.
12 *a* TJS Mwa. 14:30–34 (Kiambatisho) M&M 38:4; Musa 7:21.
b Musa 7:62–64. MWM Sayuni.
13 *a* Ebr. 11:13; 1 Pet. 2:11.
14 *a* Ebr. 11:8–13; Musa 7:63.
16 *a* Mt. 24; Lk. 21:7–36; JS—M 1.
b MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
17 *a* M&M 138:50.
b MWM Roho.
c MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
d 1 Ne. 10:12–14. MWM Israeli—Kutawanyika kwa Israeli.
22 *a* MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.

kweli, kwani hivyo ndivyo; lakini mambo haya ambayo nimewaambia ninyi hayatapita hadi yote yatimie.

24 Na hili nimewaambia ninyi juu ya Yerusalemu; na wakati siku ile itakapokuja, baki [a]litatawanywa miongoni mwa mataifa yote;

25 Lakini [a]watakusanywa tena; isipokuwa watabakia hadi nyakati za [b]Wayunani zitakapotimia.

26 Na katika [a]siku ile kutasikika vita na minong'ono ya [b]vita, na ulimwengu wote utakuwa katika ghasia, na watu [c]watavunjika mioyo kwa hofu, na watasema kwamba Kristo [d]anakawia kuja hadi mwisho wa dunia.

27 Na upendo wa wanadamu utapoa, na uovu utaongezeka.

28 Na wakati wa [a]Wayunani ukifika, [b]mwanga utazuka miongoni mwao wakaao gizani, nayo itakuwa utimilifu wa injili yangu;

29 Lakini [a]hawaipokei; kwani hawaioni nuru hii, na wanaigeuza [b]mioyo yao kutoka kwangu kwa sababu ya [c]maagizo ya wanadamu.

30 Na katika kizazi hicho nyakati za Wayunani zitatimizwa.

31 Na kutakuwa na watu waliosimama katika kizazi kile, ambao hawatapita hadi waone [a]pigo lifurikalo; kwani maradhi ya ukiwa yataifunika nchi.

32 Lakini wanafunzi wangu [a]watasimama katika mahali pa takatifu, na wala hawataondoshwa; lakini miongoni mwa waovu, watu watapaza sauti zao na [b]kumlaani Mungu na kufa.

33 Na kutakuwa na [a]matetemeko ya ardhi pia mahali mbali mbali, na ukiwa mwingi; bado watu wataishupaza mioyo yao dhidi yangu, na watashika [b]upanga, mmoja dhidi ya mwingine, na watauana wao kwa wao.

34 Na sasa, wakati Mimi Bwana nilipoyasema maneno haya kwa wanafunzi wangu, walifadhaika.

35 Nami nikawaambia: [a]Msifadhaike, kwani haya yote yatakapokuja kutukia, ili ninyi muweze kujua kwamba ahadi ambazo zimefanywa kwenu zitatimizwa.

36 Na wakati nuru itakapoanza kuzuka, itakuwa kwao kama mfano ambao nitawaonyesha—

37 Angalieni na tazameni [a]mtini, nanyi mnaiona kwa macho yenu, na mnasema wakati inapoanza kuchipua, na majani yake yakiwa bado laini, kwamba kiangazi sasa ki karibu;

24 *a* 2 Ne. 25:15.
25 *a* Neh. 1:9; Isa. 11:12–14; 1 Ne. 22:10–12; 2 Ne. 21:12–14.
b Lk. 21:24.
26 *a* MWM Siku za Mwisho.
b M&M 87; JS—M 1:23.
c Lk. 21:26.
d 2 Pet. 3:3–10.
28 *a* 1 Ne. 15:13.
b MWM Nuru, Nuru ya Kristo; Urejesho wa Injili.
29 *a* Yn. 1:5.
b Mt. 15:8–9.
c M&M 3:6–8; 46:7; JS—H 1:19.
31 *a* M&M 5:19–20; 97:22–25.
32 *a* M&M 101:21–22, 64.
b Ufu. 16:11, 21.
33 *a* M&M 43:18; 88:87–90.
b M&M 63:33.
35 *a* Mt. 24:6.
37 *a* Mk. 13:28; Lk. 21:29–31.

38 Vivyo hivyo itakuwa katika siku ile watakapoona mambo haya yote, ndipo watakapojua kwamba saa i karibu.

39 Na itakuja kutokea kwamba yule ambaye [a]ananiogopa mimi atakuwa [b]akiitazamia [c]siku ile kuu ya Bwana itakapokuja, hata kwa [d]ishara za kuja kwa [e]Mwana wa Mtu.

40 Nao wataona ishara na maajabu, kwani zitaonyeshwa mbinguni juu, na chini ya dunia.

41 Na wataona damu, na [a]moto, na mvuke wa moshi.

42 Na kabla ya kuja kwa siku ya Bwana, [a]jua litatiwa giza, na mwezi utageuka kuwa damu, na nyota zitaanguka kutoka mbinguni.

43 Na baki litakusanywa mahali hapa;

44 Na ndipo watanitafuta, na, tazama, nitakuja; na wataniona katika mawingu ya mbinguni, nimevikwa nguvu na [a]utukufu mkuu; pamoja na malaika wote watakatifu; na yule [b]asiyenitazamia mimi ataondolewa.

45 Lakini kabla mkono wa Bwana haujashuka, malaika atapiga [a]parapanda yake, na watakatifu waliolala [b]watakuja kunilaki [c]mawinguni.

46 Kwa hivyo, kama umelala katika [a]imani umebarikiwa; kwani kama sasa unionavyo na kujua kwamba Mimi ndimi, hata hivyo ndipo [b]utakuja kwangu na roho yako [c]itaishi, na ukombozi wako utakamilishwa; na watakatifu watakuja kutoka pande nne za dunia.

47 Ndipo mkono wa Bwana [a]utashuka juu ya mataifa.

48 Na halafu Bwana atakanyaga mguu wake juu ya [a]mlima huu, nao utapasuka katika pande mbili, na dunia [b]itatetemeka, na kuyumba mbele na nyuma, na mbingu pia [c]zitatetemeka.

49 Na Bwana atatoa sauti yake, na miisho yote ya dunia itaisikia; na mataifa ya ulimwengu [a]yataomboleza, na wale waliocheka wataona makosa yao.

50 Na majanga yatamfunika mwenye kudhihaki, na mwenye dharau atakoma; na wote watazamiao uovu watakatiliwa mbali na kutupwa katika moto.

51 Na ndipo [a]Wayahudi [b]watanitazama mimi na kusema: Je, haya majeraha katika mikono yako na katika miguu yako ni nini?

52 Ndipo watakapojua kuwa Mimi ndimi Bwana; kwani nitawaambia: Majeraha haya

39 *a* M&M 10:55–56. MWM Hofu—Hofu juu ya Mungu; Mtiifu, Tii, Utii.
b 2 Pet. 3:10–13; M&M 35:15–16; Musa 7:62.
c MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
d MWM Ishara za Nyakati.
e MWM Mwana wa Mtu.

41 *a* M&M 29:21; 97:25–26.
42 *a* Yoe. 2:10; Ufu. 6:12; M&M 88:87; 133:49.
44 *a* MWM Yesu Kristo—Utukufu wa Yesu Kristo.
b Mt. 24:43–51; Mk. 13:32–37.
45 *a* M&M 29:13; 43:18.
b M&M 88:96–97. MWM Ufufuko.
c 1 The. 4:16–17.
46 *a* Alma 40:12.
b Isa. 55:3.
c MWM Uzima wa Milele.
47 *a* M&M 1:12–16.
48 *a* Zek. 14:4.
b M&M 43:18; 88:87.
c Yoe. 3:16; M&M 49:23.
49 *a* M&M 87:6.
51 *a* MWM Wayahudi.
b Zek. 12:10.

ni majeraha [a]niliyotiwa katika nyumba ya marafiki zangu. Mimi ndiye yule aliyeinuliwa. Mimi ni Yesu ambaye [b]alisulubiwa. Mimi ni Mwana wa Mungu.

53 Na ndipo [a]watakapolia kwa sababu ya uovu wao; ndipo watakapoomboleza kwa sababu walimtesa [b]mfalme wao.

54 Na ndipo mataifa ya [a]wapagani yatakombolewa, na wale ambao hawakuijua sheria watakapokuwa na sehemu katika [b]ufufuo wa kwanza; na hali yao [c]itastahimiliwa.

55 Na [a]Shetani [b]atafungwa, kwamba hatakuwa na sehemu katika mioyo ya wanadamu.

56 Na [a]siku ile, wakati nitakapokuja katika utukufu wangu, ndipo mfano utakapotimia ambalo nilisema juu ya [b]wanawali kumi.

57 Kwani wale walio na hekima na kupokea [a]ukweli, na kumchukua Roho Mtakatifu kuwa [b]kiongozi wao, na [c]hawajadanganyika—amini ninawaambia, hawatakatiliwa chini na kutupwa katika [d]moto, bali watastahimili siku ile.

58 Na [a]dunia itatolewa kwao kwa [b]urithi; nao wataongezeka na kuwa na nguvu, na watoto wao [c]watakua pasipo dhambi hadi kwenye [d]wokovu.

59 Kwa kuwa Bwana atakuwa [a]katikati yao, na utukufu wake utakuwa juu yao, naye atakuwa mfalme wao na [b]mtoa sheria wao.

60 Na sasa, tazama, ninawaambia, haitatolewa kwenu kujua zaidi juu ya mlango huu, hadi [a]Agano Jipya litakapokuwa limetafsiriwa, na humo mambo haya yote yatafanywa yajulikane;

61 Kwa hivyo ninaitoa kwenu ili ninyi muweze sasa kutafsiri, ili muweze kujitayarisha kwa ajili ya mambo yajayo.

62 Kwani amini ninawaambia, kwamba mambo makubwa yanawasubiri;

63 Mnasikia juu ya [a]vita katika nchi za ng'ambo; lakini, tazameni, ninawaambia, i karibu, milangoni mwenu, na siyo miaka mingi kutoka sasa mtasikia vita katika nchi yenu wenyewe.

64 Kwa hivyo Mimi, Bwana, nimesema, kusanyikeni kutoka [a]nchi za mashariki, jikusanyeni pamoja ninyi wazee wa kanisa langu; enendeni katika nchi za magharibi, watangazieni

52 *a* Zek. 13:6.
b MWM Kusulubiwa.
53 *a* Ufu. 1:7.
b Lk. 23:38; Yn. 19:3, 14–15.
54 *a* Eze. 36:23; 39:21.
b MWM Ufufuko.
c M&M 75:22.
55 *a* MWM Ibilisi.
b Ufu. 20:2; 1 Ne. 22:26; M&M 43:31; 88:110.
56 *a* MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b Mt. 25:1–13; M&M 63:54.
57 *a* MWM Ukweli.
b MWM Roho Mtakatifu.
c JS—M 1:37.
d M&M 29:7–9; 63:34; 64:23–24; 101:22–25.
58 *a* MWM Milenia.
b Mt. 5:5.
c M&M 63:51; 101:29–31.
d MWM Wokovu.
59 *a* M&M 29:11; 104:59.
b Mwa. 49:10; Zek. 14:9; M&M 38:21–22.
60 *a* MWM Tafsiri ya Joseph Smith (TJS). Tazama pia Uteuzi kutoka katika Tafsiri ya Joseph Smith ya Biblia.
63 *a* M&M 38:29; 87:1–5; 130:12.
64 *a* M&M 42:64.

wakazi wake watubu, na kadiri watakavyotubu, yajengeni makanisa kwa ajili yangu.

65 Na kwa moyo mmoja na nia moja, kusanyeni mali yenu ili muweze [a]kununua urithi ambao baadaye utatolewa kwenu.

66 Nayo itaitwa [a]Yerusalemu Mpya, [b]nchi ya [c]amani, mji wa [d]kimbilio, mahali pa usalama kwa watakatifu wa Mungu Aliye Juu Sana;

67 Na [a]utukufu wa Bwana utakuwa hapo, na hofu ya Bwana pia itakuwa hapo, kiasi kwamba waovu hawataufikia, na utaitwa Sayuni.

68 Na itakuwa miongoni mwa waovu, kwamba kila mtu ambaye hatauchukua upanga wake dhidi ya jirani yake itamlazimu kukimbilia Sayuni kwa usalama.

69 Na hapo [a]watakusanyika kutoka kila taifa chini ya mbingu; na watakuwa watu pekee ambao hawatakuwa vitani mmoja dhidi ya mwingine.

70 Na itasemwa miongoni mwa waovu: Na tusiende kupigana na Sayuni, kwani wakazi wa Sayuni ni wa kuogopwa; kwa sababu hiyo hatuwezi kusimama.

71 Na itakuwa kwamba wenye haki watakusanywa kutoka miongoni mwa mataifa yote, nao watakuja Sayuni, wakiimba nyimbo za shangwe isiyo na mwisho.

72 Na sasa ninawaambia, yashikilieni mambo haya yasiende ng'ambo kwa walimwengu hadi itakapokuwa vyema kwangu, ili muweze kukamilisha kazi hii machoni pa watu, na machoni pa adui zenu, ili wao wasiweze kujua kazi zenu hadi mtakapomaliza jambo ambalo nimewaamuru;

73 Ili wakati watakapojua, waweze kuyafikiria mambo haya.

74 Kwani wakati ambao Bwana atajitokeza atakuwa [a]mwenye kuogofya kwao, kwamba hofu yaweza kuwakamata, na wao watasimama mbali na wakitetemeka.

75 Na mataifa yote yataogopa kwa sababu ya hofu ya Bwana, na nguvu zake nyingi. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 46

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Kanisa, huko Kirtland, Ohio, 8 Machi 1831. Katika wakati huu wa mwanzo wa Kanisa, mpangilio wa aina moja wa kuendesha ibada za Kanisa

65 *a* M&M 63:27.
66 *a* Eth. 13:5–6; Musa 7:62; M ya I 1:10. MWM Sayuni; Yerusalemu Mpya.
b M&M 57:1–3.
c MWM Amani.
d Isa. 4:6; M&M 115:6.
67 *a* M&M 64:41–43; 97:15–18. MWM Yesu Kristo—Utukufu wa Yesu Kristo.
69 *a* Kum. 30:3; Yer. 32:37–39; M&M 33:6.
74 *a* Sef. 2:11.
46 1 *a* 2 Tim. 3:16–17.
2 *a* Alma 6:1.

ulikuwa bado hujaanzishwa. Hata hivyo, desturi ya kuwaruhusu waumini pekee na wachunguzi wa dhati wa Kanisa kwenye mikutano ya Sakramenti na mikutano mingine ya Kanisa limekuwa jambo la kawaida. Ufunuo huu unaonyesha mapenzi ya Bwana juu ya kuongoza na kuendesha mikutano na mwongozo Wake juu ya kutafuta na kutambua vipawa vya Roho.

1–2, Wazee wataendesha mikutano kama watakavyoongozwa na Roho Mtakatifu; 3–6, Watafuta ukweli yapaswa wasitengwe kwenye ibada za sakramenti; 7–12, Mwombeni Mungu na tafuteni vipawa vya Roho; 13–26, Hesabu ya baadhi ya vipawa hivyo yatolewa; 27–33, Viongozi wa Kanisa wamepewa uwezo wa kutambua vipawa vya Roho.

Sikilizeni, Enyi watu wa kanisa langu; kwani amini ninawaambia kwamba mambo haya yalizungumzwa kwa [a]manufaa na mafundisho yenu.

2 Lakini licha ya mambo yale ambayo yameandikwa, daima imekuwa ikitolewa kwa [a]wazee wa kanisa langu kutoka mwanzo, na daima itakuwa hivyo, [b]kuendesha mikutano yote kama inavyoelekezwa na kuongozwa na Roho Mtakatifu.

3 Hata hivyo mnaamriwa kamwe [a]msimtupe yeyote nje ya mikutano yenu ya jumuiya, ambayo hufanyika mbele ya walimwengu.

4 Pia mnaamriwa msimtupe yeyote aliye wa [a]kanisa nje ya mikutano yenu ya sakramenti; hata hivyo, kama kuna yeyote aliyekosa, acheni [b]asipokee hadi atakapofanya suluhu.

5 Na tena ninawaambia, hamtamtupa yeyote nje ya mikutano yenu ya sakramenti ambaye anautafuta ufalme kwa dhati—ninalisema hili juu ya wale ambao si wa kanisa.

6 Na tena ninawaambia, juu ya [a]mikutano yenu ya uthibitisho, kwamba endapo kutakuwa na yeyote ambaye si wa kanisa, ambaye huutafuta ufalme kwa dhati, msimtupe nje.

7 Lakini mnaamriwa katika mambo yote [a]kumwomba Mungu, awapaye kwa ukarimu, na kile ambacho Roho hushuhudia kwenu hata hivyo nataka ninyi mkifanye katika [b]utakatifu wote wa moyo, mkitembea wima mbele zangu, [c]mkifikiria mwisho wa wokovu wenu, mkifanya mambo yote kwa sala na [d]shukrani, ili msiweze [e]kudanganywa na pepo wachafu, na mafundisho ya [f]maibilisi, au [g]amri za wanadamu; kwani

b Moro. 6:9; M&M 20:45.
3*a* 3 Ne. 18:22–25. MWM Ushirika.
4*a* MWM Kanisa la Yesu Kristo.
b 3 Ne. 18:26–32. MWM Sakramenti.
6*a* MY kuthibitishwa kwa wale waliobatizwa muda si mrefu.
7*a* Yak. (Bib.) 1:5–6; M&M 88:63.
b MWM Utakatifu.
c MWM Tafakari.
d Zab. 100; Alma 34:38. MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
e 1 Tim. 4:1–4; M&M 43:5–7.
f MWM Ibilisi.
g M&M 3:6–7; 45:29.

baadhi ni za wanadamu na nyingine za mapepo.

8 Kwa hivyo, kuweni waangalifu msije kudanganywa; na ili msidanganywe [a]takeni sana karama zilizo kuu, daima mkikumbuka ni kwa nini zinatolewa;

9 Kwani amini ninawaambia, hutolewa kwa manufaa ya wale ambao hunipenda Mimi na hushika amri zangu zote, na yule atafutaye kufanya haya; ili wote waweze kufaidika wale wanitafutao au kuniomba, kwamba wanaomba na hawaombi kwa [a]ishara ili wapate [b]kuvitumia kwa tamaa zao.

10 Na tena, amini ninawaambia, ningetaka kwamba daima mkumbuke, na daima yawekeni katika [a]akili zenu [b]vipawa hivyo ni vipi, ambavyo hutolewa kwa kanisa.

11 Kwani wote hawapokei vipawa vyote; kwani kuna vipawa vingi, na kwa [a]kila mtu kipawa kimetolewa na Roho wa Mungu.

12 Kwa wengine wamepewa kimoja, na wengine wamepewa kingine, ili wote waweze kufaidika.

13 Kwa wengine kinatolewa na Roho Mtakatifu [a]kujua kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, na kwamba alisulubiwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu.

14 Kwa wengine kimetolewa [a]kuamini juu ya maneno yao, ili hao pia waweze kuwa na uzima wa milele kama wataendelea kuwa waaminifu.

15 Na tena, kwa wengine imetolewa na Roho Mtakatifu kujua [a]tofauti za huduma, kama itakavyo mpendeza Bwana yeye yule, kulingana na matakwa ya Bwana, akilinganisha rehema zake kulingana na hali za wanadamu.

16 Na tena, hutolewa na Roho Mtakatifu kwa wengine kujua tofauti za kutenda kazi, kama ni za Mungu, kwamba mafunuo hayo ya Roho yaweze kutolewa kwa kila mtu kwa faida ya wote.

17 Na tena, amini ninawaambia, kwa mwingine amepewa na Roho wa Mungu, neno la [a]hekima.

18 Kwa mwingine neno la [a]maarifa, ili wote waweze kufundishwa kuwa wenye hekima na kuwa na maarifa.

19 Na tena kwa wengine wamepewa kuwa na [a]imani ya kuponywa;

20 Na wengine wamepewa kuwa na imani ya [a]kuponya.

21 Na tena, kwa wengine wamepewa kufanya [a]miujiza;

22 Na kwa wengine wamepewa [a]kutoa unabii;

23 Na kwa wengine [a]kuzitambua roho.

8a 1 Kor. 12:31.
9a MWM Ishara.
b Yak. (Bib.) 4:3.
10a MWM Nia.
b 1 Kor. 14:12. MWM Vipawa vya Roho.
11a 1 Kor. 12:4–11.
13a MWM Ushuhuda.
14a 3 Ne. 12:2. MWM Amini, Imani.
15a Moro. 10:8.
17a Moro. 10:9. MWM Hekima.
18a MWM Maarifa.
19a M&M 42:48–52. MWM Amini, Imani.
20a MWM Ponya, Uponyaji.
21a MWM Muujiza.
22a MWM Toa unabii, Unabii.
23a Musa 1:13–15.

24 Na tena, wengine wamepewa kunena kwa [a]lugha;

25 Na mwingine amepewa tafsiri ya lugha.

26 Na [a]vipawa hivi vyote hutoka kwa Mungu, kwa manufaa ya [b]watoto wa Mungu.

27 Na kwa [a]askofu wa kanisa, na kwa watu wa aina hiyo ambao Mungu atawateua na kuwatawaza kulisimamia kanisa na kuwa wazee wa kanisa, watapewa [b]kuvitambua vipawa hivyo vyote isije pakawepo mtu miongoni mwenu akitabiri na wala isiwe kutoka kwa Mungu.

28 Na itakuwa kwamba yule aombaye katika [a]Roho atapokea katika Roho;

29 Kwamba baadhi waweza kupewa kuwa na vipawa vyote, ili paweze kuwa na kiongozi, ili kwamba kila muumini aweze kufaidika navyo.

30 Yule ambaye [a]anaomba katika [b]Roho aomba kulingana na [c]mapenzi ya Mungu; kwa sababu hiyo hufanyika kwake kama aombavyo.

31 Na tena, ninawaambia, mambo yote lazima yafanyike katika jina la Kristo, lolote mfanyalo katika Roho;

32 Na ni lazima mtoe [a]shukrani kwa Mungu katika Roho kwa baraka zozote mbarikiwazo.

33 Na ni lazima mtende [a]wema na [b]utakatifu mbele zangu daima. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 47

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith, Nabii, huko Kirtland, Ohio, 8 Machi 1831. John Whitmer, ambaye alikuwa tayari ametumika kama karani kwa Nabii, mwanzoni alisita wakati alipoombwa kutumikia kama mwanahistoria na mtunza kumbukumbu wa Kanisa, akiwa akichukua nafasi ya Oliver Cowdery. Aliandika, "Nisingelitaka kufanya hili lakini natamani kuona mapenzi ya Bwana yatimie, na kama ndivyo anavyotaka, natamani kwamba angenionyesha kupitia kwa Joseph Mwonaji." Baada ya Joseph Smith kupokea ufunuo huu, John Whitmer alikubali na kutumikia katika ofisi aliyoteuliwa.

1–4, John Whitmer ateuliwa kutunza historia ya Kanisa na kuwa mwandishi wa Nabii.

Tazama, ni muhimu kwangu kwamba mtumishi wangu John aandike na atunze [a]historia ya

24*a* MWM Ndimi, Kipawa cha.
26*a* Moro. 10:8–19.
b MWM Wana na Mabinti za Mungu.
27*a* MWM Askofu.
b MWM Utambuzi, Kipawa cha.
28*a* M&M 88:64–65.
30*a* M&M 50:29.
b MWM Roho Mtakatifu.
c 2 Ne. 4:35.
32*a* 1 Nya. 16:8–15; 1 The. 1:2; Alma 37:37; M&M 59:7, 21.
MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
33*a* MWM Wema.
b MWM Utakatifu.
47 1*a* M&M 69:2–8; 85:1–2.

kila siku, na akusaidie wewe, Joseph mtumishi wangu, katika kuandika mambo yote utakayopewa, hadi atakapoitwa kwa kazi nyingine,

2 Tena, amini ninakuambia kuwa aweza kupaza sauti yake katika mikutano, popote itakapofanyika.

3 Na tena, ninawaambia kuwa atateuliwa kuandika kumbukumbu na historia ya kanisa daima; kwani Oliver Cowdery nimemteua katika ofisi nyingine.

4 Kwa hiyo, itatolewa kwake na [a]Mfariji, kuandika mambo haya kadiri yeye atakavyokuwa mwaminifu. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 48

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith, Nabii, huko Kirtland, Ohio, 10 Machi 1831. Nabii alimwuliza Bwana juu ya utaratibu wa kutumia katika kununua ardhi kwa ajili ya makazi ya watakatifu. Hili lilikuwa ni jambo muhimu katika suala la uhamaji wa waumini wa Kanisa kutoka majimbo ya mashariki ya Marekani, katika utii kwa amri ya Bwana kwamba iliwapasa kukusanyika Ohio (ona sehemu ya 37:1–3; 45:64).

1–3, Watakatifu wa Ohio washirikiane ardhi yao pamoja na ndugu zao; 4–6, Watakatifu wanunue ardhi, waujenge mji, na wafuate ushauri wa viongozi wao.

Ni muhimu kwa wakati huu kubaki katika mahali penu mnapoishi, ilimradi kwamba hali hiyo ni vizuri kwenu.

2 Na ikiwa mnayo ardhi, [a]mtaitoa kwa ndugu zenu wa mashariki;

3 Na ikiwa hakuna ardhi na wainunue kwa wakati huu katika maeneo yale yaliyo karibu, kama itakavyowapendeza wao, kwani ni lazima na ni muhimu kwamba wapate mahali pa kuishi kwa wakati huu.

4 Ni muhimu kwenu kujiwekea akiba ya fedha kadiri inavyowezekana, na kuwa jipatieni kila kitu kwa haki, ili wakati ukifika muweze [a]kujinunulia ardhi kwa kujenga mji na Ni muhimu kwenu kujiwekea akiba ya fedha kadiri inavyowezekana, na kuwa jipatieni kila kitu kwa haki, ili wakati ukifika muweze [b]kujinunulia ardhi kwa kujenga mji na hata kwa urithi wenu.

5 Mahali bado hapajafunuliwa; lakini baada ya kuwasili ndugu zenu kutoka mashariki watachaguliwa [a]watu fulani, nao watapewa [b]kujua mahali hapo, au patafunuliwa kwao.

6 Na hao watachaguliwa ili kununua ardhi, na kuweka msi-

4*a* MWM Mfariji; Roho Mtakatifu.
48 2*a* MWM Ustawi.
4*a* M&M 57:4–5.
b M&M 42:35–36; 45:65–67.
5*a* M&M 57:6–8.
b M&M 57:1–3.

ngi wa [a]mji; na ndipo mtaanza kukusanyika pamoja na familia zenu, kila mtu kulingana na [b]familia yake, na kwa kadiri ya hali yake, na kadiri atakavyoelezwa na urais na askofu wa kanisa, kulingana na sheria na amri ambazo mmezipokea, na ambazo mtazipokea baadaye. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 49

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Sidney Rigdon, Parley P. Pratt, na Leman Copley huko Kirtland, Ohio, 7 Mei 1831. Leman Copley alikuwa ameikumbatia injili lakini bado ameshikilia baadhi ya mafundisho ya Shakers (United Society of Believers in Christ's Second Appearing [Muungano wa Jumuiya ya Waumini wa Kuonekana kwa Kristo Mara ya Pili]), madhehebu ambayo alikuwepo awali. Baadhi ya imani za Shakers ilikuwa kwamba Ujio wa Pili wa Yesu Kristo tayari ulikwishatimia na kwamba alionekana katika umbile la mwanamke, Ann Lee; Wao hawakuona kama ubatizo wa maji ulikuwa ni kitu cha lazima. Walikataa ndoa na waliamini katika maisha ya useja. Baadhi ya Shakers pia walikataza ulaji wa nyama. Katika utangulizi wa ufunuo huu, historia ya Joseph Smith inaeleza, "Ili kuweza kupata ufahamu sahihi juu ya jambo hili, nilimwomba Bwana, na kupokea yafuatayo." Ufunuo huu unakanusha baadhi ya imani ya kundi hili la Shakers. Ndugu waliotajwa mwanzoni mwa sehemu hii walichukua nakala ya ufunuo na kuwapelekea jumuiya ya Shakers (karibu na Cleveland, Ohio) na kuwasomea hadi mwisho wa ufunuo, lakini ufunuo ulikataliwa.

1–7, Siku na saa ya ujio wa Kristo zitabaki bila kujulikana hadi Yeye atakapokuja; 8–14, Watu lazima watubu, kuiamini injili, na kuzitii ibada ili kupata wokovu; 15–16, Ndoa imeagizwa na Mungu; 17–21, Ulaji wa nyama umeruhusiwa; 22–28, Sayuni itastawi na Walamani watachanua kama waridi kabla ya Ujio wa Pili.

Sikilizeni maneno yangu, watumishi wangu Sidney, na Parley, na Leman; kwani tazameni, amini ninawaambia, kwamba ninawapa ninyi amri ya kwenda [a]kuhubiri injili yangu ambayo mmeipokea, kama vile mlivyoipokea, kuwahubiria waumini wa Shakers.

2 Tazama, ninawaambia, kwamba wanatamani kujua ukweli kwa kiasi fulani, lakini siyo wote, kwani hawako [a]sahihi mbele zangu na lazima watubu.

3 Kwa hiyo, ninawatuma

6*a* mwm Yerusalemu Mpya.

b M&M 51:3.

49 1*a* mwm Hubiri.

2*a* Mdo. 8:21.

ninyi, watumishi wangu Sidney na Parley, kuwahubiria injili.

4 Na mtumishi wangu Leman atatawazwa kwa kazi hii, ili naye akahojiane na kujenga hoja pamoja nao, siyo kulingana na yale aliyopokea kutoka kwao, bali kulingana na yale [a]atakayofundishwa na watumishi wangu; na kwa kufanya hivyo nitambariki yeye, vinginevyo hatastawi.

5 Hivyo ndivyo asemavyo Bwana; maana Mimi ni Mungu, na [a]nimemtuma Mwana wangu wa Pekee katika ulimwengu kwa ajili ya [b]ukombozi wa ulimwengu, na nimeagiza kwamba yule ampokeaye ataokolewa, na yule asiyempokea [c]atahukumiwa—

6 Na wakamtenda [a]Mwana wa Mtu kama walivyotaka; na amejitwalia uwezo wake [b]mkono wa kuume wa [c]utukufu wake, na sasa anatawala katika mbingu, na atatawala hadi atakaposhuka duniani kuwaweka maadui wote [d]chini ya miguu yake, wakati ambao u karibu—

7 Mimi, Bwana Mungu, nimesema haya, walakini habari ya saa ile na [a]siku ile hakuna mtu ajuaye, hata malaika walio mbinguni, wala hawatajua hadi atakapokuja.

8 Kwa hiyo, ningependa kwamba watu wote watubu, kwani wote wapo chini ya [a]dhambi, isipokuwa wale ambao nimejisazia mwenyewe, watu [b]watakatifu ambao ninyi hamuwajui.

9 Kwa hiyo, ninawaambia kwamba nimelileta kwenu [a]agano langu lisilo na mwisho, hata lile ambalo lilikuwepo tangu mwanzo.

10 Na kwamba nilichokiahidi nimekitimiza, na [a]mataifa ya dunia [b]yataliinamia; na kama siyo kwa hiari yao wenyewe, watashushwa chini, kwani kile ambacho sasa kimejikweza chenyewe [c]kitadhiliwa kiuwezo.

11 Kwa hiyo, ninawapa amri kwamba [a]nendeni miongoni mwa watu hawa, na muwaambie, kama mtume wangu wa zamani, ambaye jina lake lilikuwa Petro:

12 Amini juu ya jina la Bwana Yesu, ambaye alikuwa hapa duniani, na atakuja, aliye mwanzo na mwisho;

13 [a]Tubuni na mkabatizwe katika jina la Yesu Kristo, kulingana na amri takatifu, kwa ondoleo la dhambi;

4a MWM Injili; Ukweli.
5a Yn. 3:16–17; M&M 132:24. MWM Yesu Kristo—Mamlaka.
b MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi; Mkombozi.
c MWM Hukumu.
6a MWM Mwana wa Mtu.
b Mdo. 7:55–56; M&M 76:20–23.
c MWM Yesu Kristo—Utukufu wa Yesu Kristo.
d 1 Kor. 15:25; M&M 76:61.
7a Mt. 24:36; Mk. 13:32–37; Ufu. 16:15; M&M 133:11.
8a Gal. 3:22; Mos. 16:3–5.
b Ebr. 13:2; 3 Ne. 28:25–29.
9a Mwa. 17:7; M&M 66:2. MWM Agano Jipya na Lisilo na Mwisho.
10a Zek. 2:11; M&M 45:66–69; 97:18–21.
b Isa. 60:14.
c Mt. 23:12.
11a MWM Kazi ya kimisionari.
13a 3 Ne. 27:19–20.

14 Na yule afanyaye hivi atapokea [a]kipawa cha Roho Mtakatifu, kwa kuwekewa [b]mikono na wazee wa kanisa.

15 Na tena, amini ninawaambia, kwamba yeyote [a]akatazaye kuoa hakuamriwa na Mungu, kwani [b]ndoa imeamriwa na Mungu kwa mwanadamu.

16 Kwa hiyo, ni sheria kwamba yampasa kuwa na [a]mke mmoja, na wawili watakuwa mwili [b]mmoja, na hii yote ili [c]dunia iweze kujibu madhumuni ya kuumbwa kwake;

17 Na kwamba iweze kujazwa kwa kipimo cha mwanadamu, kulingana na [a]uumbaji wake [b]kabla ya ulimwengu kuumbwa.

18 Na yeyote [a]akatazaye ili kuzuia [b]nyama, kwamba mtu asiile, huyo hakuagizwa na Mungu;

19 Kwani, tazama, [a]wanyama wa porini na ndege wa angani, na kile ambacho hutambaa ardhini, vimetawazwa kwa matumizi ya wanadamu kwa ajili ya chakula na mavazi, na kwamba aweze kuwa navyo vingi.

20 Lakini haikutolewa kwamba mwanadamu [a]amiliki zaidi ya mwingine, kwa sababu hiyo [b]ulimwengu umelala dhambini.

21 Na ole kwa mwanadamu ambaye [a]humwaga damu au auharibuye mwili na wala havihitaji.

22 Na tena, amini ninawaambia, kwamba Mwana wa Mtu [a]aja siyo katika umbile la mwanamke, wala la mwanadamu atembeaye juu ya nchi.

23 Kwa hiyo, [a]msidanganyike, bali endeleeni kwa uthabiti, [b]mkitazamia kutetemeka kwa mbingu, na kutingishika kwa ardhi na kuyumbishwa mbele na nyuma kama mtu mlevi, na kwa [c]mabonde kuinuliwa, na kusawazishwa kwa [d]milima, na mahali pa makorongo kutengenezwa—na haya yote wakati malaika atakapopiga [e]parapanda yake.

24 Lakini kabla ya siku ile kuu ya Bwana itakuwa, [a]Yakobo atastawi nyikani, na Walamani [b]watachanua kama waridi.

25 Sayuni [a]itashamiri juu ya [b]vilima na kufurahia juu ya milima, na watajikusanya pamoja mahali nilipopachagua.

14*a* MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
b MWM Mikono, Kuweka juu ya.
15*a* 1 Tim. 4:1–3.
b Mwa. 2:18, 24; 1 Kor. 11:11. MWM Ndoa, Oa, Olewa.
16*a* Yak. (KM) 2:27–30.
b Mwa. 2:24; Mt. 19:5–6.
c MWM Dunia—Iliumbwa kwa ajili ya mwanadamu.
17*a* Musa 3:4–5. MWM Umba, Uumbaji.
b MWM Maisha kabla ya kuzaliwa.
18*a* MY wameambiwa kuacha.
b Mwa. 9:3; 1 Tim. 4:1–3.
19*a* M&M 89:10–13.
20*a* Mdo. 4:32; M&M 51:3; 70:14; 78:6.
b MWM Malimwengu.
21*a* TJS Mwa. 9:10–15 (Kiambatisho).
22*a* MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
23*a* Mt. 24:4–5.
b 2 Pet. 3:12; M&M 45:39.
c Isa. 40:4; M&M 109:74.
d Mik. 1:3–4.
e Mt. 24:29–31.
24*a* 3 Ne. 5:21–26.
b Isa. 35:1; 2 Ne. 30:5–6; 3 Ne. 21:22–25; M&M 3:20; 109:65.
25*a* M&M 35:24.
b Mwa. 49:26; 2 Ne. 12:2–3.

26 Tazama, ninawaambia, enendeni kama nilivyowaamuru; tubuni dhambi zenu zote; [a]ombeni nanyi mtapokea; bisheni nanyi mtafunguliwa.

27 Tazama, nitakwenda mbele yenu na [a]nitawafuata nyuma; na nitakuwa [b]katikati yenu, na wala [c]hamtaaibika.

28 Tazama, Mimi ni Yesu Kristo, na naja [a]haraka. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 50

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 9 Mei 1831. Historia ya Joseph Smith inaeleza kwamba baadhi ya wazee walikuwa hawaelewi kujitokeza kwa roho tofauti zilizoenea katika nchi na kwamba ufunuo huu ulitolewa kama jibu kwa maulizo yake maalumu juu ya jambo hili. Yaliyokuwa yakiitwa matukio ya kiroho wala hayakuwa mageni miongoni mwa waumini, baadhi yao walikuwa wakidai kupokea maono na mafunuo.

1–5, Roho nyingi za uongo zimeenea katika nchi; 6–9, Ole wao wanafiki na wale waliotengwa na Kanisa; 10–14, Wazee watahubiri injili kwa Roho; 15–22, Wote mhubiri na msikilizaji wanahitaji kuangaziwa na Roho; 23–25, Kile kisichojenga siyo cha Mungu; 26–28, Waaminifu ni wamiliki wa vitu vyote; 29–36, Sala za walio safi hujibiwa; 37–46, Kristo ndiye Mchungaji Mwema na Jiwe la Israeli.

Sikilizeni, Enyi wazee wa kanisa langu, na itegeeni sikio sauti ya Mungu aliye hai; na litilieni maanani neno la hekima ambalo litatolewa kwenu, kulingana na vile mlivyoomba na kukubaliwa juu ya kanisa, na roho ambazo zimeenea katika nchi.

2 Tazama, amini ninawaambia, kwamba kuna roho nyingi ambazo ni [a]roho za uongo, ambazo zimeenea katika nchi, zikiudanganya ulimwengu.

3 Na pia [a]Shetani ametafuta kuwadanganya ninyi, ili aweze kuwapindua.

4 Tazama, Mimi, Bwana, nimewaangalia, na nimeona machukizo katika kanisa ambalo [a]hulikiri jina langu.

5 Lakini wamebarikiwa wale walio waaminifu na wenye [a]subira, ikiwa katika kuishi au katika kifo, kwani wataurithi uzima wa milele.

6 Bali ole wao [a]wadanganyifu na wanafiki, kwani, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, nitawaleta kwenye hukumu.

26*a* M&M 88:63.
27*a* Isa. 52:12.
b 3 Ne. 20:22.
c 1 Pet. 2:6; M&M 84:116.
28*a* M&M 1:12.

50 2*a* M&M 129. MWM Roho—Pepo wachafu.
3*a* Lk. 22:31; 3 Ne. 18:18.
4*a* MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
5*a* MWM Stahimili.
6*a* MWM Danganya, Kudanganya, Udanganyifu.

7 Tazama, amini ninawaambia, kuna [a]wanafiki miongoni mwenu, ambao wamewadanganya baadhi yenu, ambao wamempa [b]nguvu [c]adui; lakini wa [d]aina hiyo wataokolewa;

8 Lakini wanafiki watatambulika na [a]kukatiliwa mbali, iwe katika kuishi au katika kufa, kama vile mimi nitakavyo; na ole wao waliokatiliwa mbali kutoka kwenye kanisa langu, kwani wao ulimwengu umewashinda.

9 Kwa hiyo, acha kila mtu ajihadhari ili asije akafanya kile kisicho cha kweli na haki mbele zangu.

10 Na sasa njooni kwa njia ya Roho, asema Bwana, kwa wazee wa kanisa lake, na [a]tusemezane, ili mpate kuelewa;

11 Na tusemezane kama vile watu wanavyosemezana mmoja kwa mwingine uso kwa uso.

12 Sasa, wakati watu wanaposemezana, huelewana, kwa sababu husemezana kama watu; hivyo ndivyo nitakavyo Mimi, Bwana, kusemezana nanyi ili kwamba muweze [a]kunielewa.

13 Kwa hiyo, Mimi Bwana ninawauliza swali hili—[a]mmetawazwa kwa lipi?

14 Kwa kuhubiri injili yangu kwa njia ya [a]Roho, hata [b]Mfariji aliyetumwa kufundisha ukweli.

15 Nanyi mkapokea [a]roho nyingine ambazo hamkuweza kuzielewa, na mkazipokea kama ni za Mungu; na katika hili ninyi mnajiteteaje?

16 Tazama, mtajibu swali hili ninyi wenyewe; hata hivyo, nitakuwa mwenye huruma kwenu; yule aliye dhaifu miongoni mwenu atafanywa baadaye kuwa [a]mwenye nguvu.

17 Amini ninawaambia, yule aliyetawazwa na mimi na kutumwa kwenda [a]kulihubiri neno la kweli kwa njia ya Mfariji, katika Roho wa kweli, je, afundisha kwa [b]Roho wa kweli au kwa njia nyingine?

18 Na kama itakuwa kwa njia nyingine hatokani na Mungu.

19 Na tena, yule apokeaye neno la kweli, je, hulipokea kwa Roho wa kweli au kwa njia nyingine?

20 Kama ni kwa njia nyingine hatokani na Mungu.

21 Kwa hiyo, kwa nini kwamba hamwezi kuelewa na kujua, kwamba yule ambaye hulipokea neno kwa njia ya Roho wa kweli hulipokea kama vile lifundishwavyo na Roho wa kweli?

22 Kwa sababu hiyo, yule

7a Mt. 23:13–15; Alma 34:28.
b MWM Ibilisi.
c Mos. 27:8–9.
d MY wale waliodanganywa.
8a M&M 1:14; 56:3; 64:35.
MWM Kutengwa na Kanisa.
10a Isa. 1:18; M&M 45:10.
12a M&M 1:24.
13a MWM Kutawaza, Kutawazwa.
14a M&M 43:15.
MWM Fundisha, Mwalimu—Kufundisha kwa Roho.
b MWM Mfariji.
15a MWM Utambuzi, Kipawa cha.
16a Eth. 12:23–27.
17a MWM Hubiri; Kazi ya kimisionari.
b M&M 6:15.
MWM Roho Mtakatifu; Ukweli.

ambaye huhubiri na yule apokeaye, huelewana, na wote [a]hujengana na [b]kufurahi kwa pamoja.

23 Na kile kisichojenga siyo cha Mungu, nacho ni [a]giza.

24 Kile kilicho cha Mungu ni [a]nuru; na yule ambaye huipokea nuru, na [b]kukaa ndani ya Mungu, hupokea [c]nuru zaidi; na nuru hiyo huzidi kung'ara hata mchana mkamilifu.

25 Na tena, amini ninawaambia, na ninalisema ili muweze kujua [a]ukweli, ili muweze kuifukuza giza kutoka miongoni mwenu;

26 Yule aliyetawazwa na Mungu na kutumwa, huyo ndiye ameteuliwa kuwa [a]mkuu, bila kujali kuwa yeye ni mdogo na [b]mtumishi wa wote.

27 Kwa hiyo, yeye ni [a]mmiliki wa vitu vyote; kwani vitu vyote viko chini yake, kote mbinguni na duniani, uzima na nuru, Roho na [b]nguvu, ametumwa kwa mapenzi ya Baba kupitia Mwana wake, Yesu Kristo.

28 Lakini hakuna mwanadamu aliye mmiliki wa vitu vyote isipokuwa yule aliye [a]takaswa na [b]kuoshwa dhambi zote.

29 Na kama umetakaswa na kuoshwa kutokana na dhambi zote, [a]utaomba kitu chochote utakacho katika jina la Yesu nalo litafanyika.

30 Lakini jueni hili, mtafunuliwa nini cha kuomba; na kama vile mlivyoteuliwa [a]kuongoza, roho zitakuwa chini yenu.

31 Kwa hiyo, itakuja kutokea, kwamba kama utaona [a]roho amejitokeza ambaye huwezi kumwelewa, na wewe humpokei roho huyo, utamwuliza Baba katika jina la Yesu; na kama haitoi roho hiyo kwako, ndipo waweza kujua kwamba haitokani na Mungu.

32 Na utatolewa kwako, [a]uwezo juu ya pepo hao; nawe utatangaza dhidi ya pepo huyo kwa sauti kubwa kama hatokani na Mungu—

33 Siyo kwa [a]mashtaka ya kumlaumu, ili asije akakushinda, wala siyo kwa [b]kujisifu wala kufurahia, ili nawe usije ukakamatwa.

34 Yule ambaye hupokea vya Mungu, na avihesabu kuwa ni vya Mungu; na afurahi kwamba Mungu humhesabu kuwa mwenye kustahili kupokea.

35 Na kwa kutilia maanani na kuyatenda mambo haya ambayo mmeyapokea, na yale mtakayoyapokea—na [a]ufalme

22 *a* 1 Kor. 14:26.
b Yn. 4:36.
23 *a* MWM Giza, Kiroho.
24 *a* 1 Yoh. 2:8–11; Moro. 7:14–19; M&M 84:45–47; 88:49. MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
b Yn. 15:4–5, 10.
c 2 Ne. 28:30.
25 *a* Yn. 8:32.
26 *a* Mt. 23:11.
b Mk. 10:42–45. MWM Utumishi.
27 *a* M&M 76:5–10, 53–60; 84:34–41.
b MWM Uwezo.
28 *a* 3 Ne. 19:28–29; M&M 88:74–75. MWM Safi na Isiyo safi; Utakaso.
b 1 Yoh. 1:7–9.
29 *a* Hel. 10:5; M&M 46:30. MWM Sala.
30 *a* MWM Mamlaka.
31 *a* 1 Yoh. 4:1. MWM Roho—Pepo wachafu.
32 *a* Mt. 10:1.
33 *a* Yuda 1:9.
b M&M 84:67, 73.
35 *a* MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.

mliopewa na Baba, na [b]uwezo wa kuvishinda vitu vyote ambavyo yeye hakuvianzisha.

36 Na tazama, amini ninawaambia, mmebarikiwa ninyi ambao sasa mnayasikiliza maneno yangu kutoka kinywa cha mtumishi wangu, kwani ninyi [a]mmesamehewa dhambi zenu.

37 Na mtumishi wangu Joseph Wakefield, ambaye napendezwa naye, na mtumishi wangu [a]Parley P. Pratt waende miongoni mwa makanisa na kuyaimarisha kwa neno la [b]kufaa;

38 Na pia mtumishi wangu John Corrill, au na watumishi wangu wengi wengineo kama walivyotawazwa kwenye ofisi hii, na acheni wafanye kazi katika [a]shamba la mizabibu, na acheni mtu yeyote asiwazuie kufanya kile ambacho nimekiteua kwao—

39 Kwa hiyo, katika hili mtumishi wangu [a]Edward Partridge hasamehewi; isipokuwa atubu na atasamehewa.

40 Tazama, ninyi ni watoto wadogo na hamuwezi [a]kuyastahimili yote hivi sasa; na lazima [b]mkue katika [c]neema na katika ujuzi wa [d]ukweli.

41 [a]Msiogope, ninyi [b]watoto wadogo, kwani ninyi ni wangu, na Mimi [c]nimeushinda ulimwengu, nanyi ndiyo wale ambao Baba [d]alinipa;

42 Na hakuna hata mmoja wao wale ambao baba amenipatia [a]atakayepotea.

43 Na Baba na Mimi tu [a]wamoja. Mimi ni ndani ya Baba na Baba yu ndani yangu; na kadiri ninyi mlivyonipokea Mimi, ninyi mu ndani yangu nami ni ndani yenu,

44 Kwa hivyo, Mimi nipo katikati yenu, na mimi ni [a]mchungaji mwema, na [b]jiwe la Israeli. Yule ajengaye juu ya [c]mwamba huu [d]hataanguka kamwe.

45 Na siku yaja ambayo mtaisikia sauti yangu na [a]kuniona, na kujua kwamba Mimi ndimi.

46 [a]Kesheni basi, ili muweze kuwa [b]tayari. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 51

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii huko Thompson,

35 *b* 1 Yoh. 4:4; M&M 63:20, 47.
36 *a* M&M 58:42–43. MWM Samehe.
37 *a* MWM Pratt, Parley Parker.
b M&M 97:3–5.
38 *a* MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
39 *a* MWM Partridge, Edward.
40 *a* 3 Ne. 17:2–3; M&M 78:17–18.
b 1 Kor. 3:2–3; M&M 19:22–23.
c MWM Neema.
d MWM Ukweli.
41 *a* 1 Yoh. 4:18.
b MWM Wana na Mabinti za Mungu.
c Yn. 16:33.
d Yn. 10:27–29; 17:2; 3 Ne. 15:24; M&M 27:14; 84:63.
42 *a* Yn. 17:12; 3 Ne. 27:30–31.
43 *a* Yn. 17:20–23; 3 Ne. 11:35–36. MWM Mungu, Uungu.
44 *a* Yn. 10:14–15. MWM Mchungaji Mwema.
b Mwa. 49:24; 1 Pet. 2:4–8. MWM Jiwe la pembeni.
c 1 Kor. 10:1–4. MWM Mwamba; Yesu Kristo.
d Hel. 5:12.
45 *a* M&M 67:10–13.
46 *a* MWM Kesha, Walinzi.
b Alma 34:32–33.

Ohio, 20 Mei 1831. Kwa wakati huu watakatifu wanaohamia kutoka mashariki walianza kufikia Ohio, na ilikuja kuwa muhimu kufanya mipango ya makazi yao. Na kazi hii ilikuwa wajibu wa ofisi ya askofu, Askofu Edward Partridge aliomba mwongozo juu ya jambo hili, na hivyo Nabii alimwomba Bwana.

1–8, Edward Partridge ameteuliwa kudhibiti usimamizi na mali; 9–12, Watakatifu lazima wafanyiane haki na kupokea sawa sawa; 13–15, Ni lazima wawe na ghala ya askofu na kupanga mali kulingana na sheria ya Bwana; 16–20, Ohio patakuwa mahali pa kukusanyika kwa muda.

Nisikilizeni Mimi, asema Bwana Mungu wenu, na nitasema naye mtumishi wangu [a]Edward Partridge, na kumpa yeye maelekezo; kwani ni muhimu kwamba apokee maelekezo namna ya kuwasimamia watu hawa.

2 Kwani ni muhimu kwamba wasimamiwe kulingana na [a]sheria zangu; vinginevyo, watakatiliwa mbali.

3 Kwa hivyo, mtumishi wangu Edward Partridge, na wale aliowateua, ambao ninapendezwa nao, wawagawie watu hawa sehemu zao, kila mtu [a]sawa kulingana na familia yake, na kulingana na hali yake na matakwa na [b]shida zake.

4 Na mtumishi wangu Edward Partridge, wakati atakapomgawia mtu sehemu yake, na ampe hati ambayo itahakikisha kuwa ni sehemu yake, kwamba ataishikilia hati hiyo na urithi huu katika kanisa, hadi avunje sheria na kutohesabiwa kustahili kwa sauti ya kanisa, kulingana na sheria na [a]maagano ya kanisa, juu ya ustahiki kanisani.

5 Na kama atavunja sheria na hahesabiwi kuwa mwenye kustahili kuwa katika kanisa, hatakuwa na uwezo wa kudai ile sehemu ambayo aliyoiweka wakfu kwa askofu kwa ajili ya maskini na wenye shida wa kanisa langu; kwa hiyo, hatarejeshewa zawadi hiyo, bali atakuwa na madai tu ya sehemu ile aliyogawiwa yeye.

6 Na hivyo ndivyo mambo yote yatakavyolindwa, [a]kulingana na [b]sheria za nchi.

7 Na hivyo kile kilicho cha watu hawa kigawanywe kwa watu hawa.

8 Na [a]fedha zilizosalia kwa watu hawa—na pateuliwe wakala kwa watu hawa, na kuchukua [b]fedha hizo kwa ajili ya kuleta vyakula na mavazi, kulingana na mahitaji ya watu hawa.

9 Na kila mtu na afanye [a]haki,

51 1*a* mwm Partridge, Edward.
2*a* M&M 42:30–39; 105:5.
mwm Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.
3*a* M&M 49:20.
b Mdo. 2:44–45; 4 Ne. 1:2–3.
4*a* my Sehemu ya 20 inaitwa Katiba na Maagano ya Kanisa la Kristo.
M&M 33:14; 42:13.
mwm Agano.
6*a* 1 Pet. 2:13; M&M 98:5–7.
b M&M 58:21–22.
8*a* M&M 84:104.
b M&M 104:15–18.
9*a* mwm Mwaminifu, Uaminifu.

na kuwa sawa miongoni mwa watu hawa, na kupokea sawa, ili kwamba muweze kuwa na [b]umoja, kama vile nilivyowaamuru.

10 Na kile kilicho cha watu hawa kisichukuliwe na kutolewa kwa wale wa [a]kanisa jingine.

11 Kwa hiyo, kama kanisa jingine watapokea fedha za kanisa hili, na walipe kwa kanisa hili tena kulingana na makubaliano yao;

12 Na hii itafanyika kupitia kwa askofu au wakala, ambaye atateuliwa kwa [a]sauti ya kanisa.

13 Na tena, na askofu ataanzisha [a]ghala kwa kanisa hili; na mambo yote ya fedha na katika vyakula, ambayo ni zaidi ya [b]mahitaji kwa watu hawa, vitunzwe katika mikono ya askofu.

14 Na yeye pia ajiwekee kwa mahitaji yake yeye mwenyewe, na kwa mahitaji ya familia yake, tangu atakapoajiriwa katika kufanya shughuli hii.

15 Na hivyo ndivyo ninavyowapa watu hawa nafasi ya kujisimamia wenyewe kulingana na [a]sheria zangu.

16 Nami ninaiweka wakfu [a]nchi hii kwa ajili yao kwa majira mafupi, hadi Mimi, Bwana, nitakapopanga vinginevyo, na kuwaamuru kwenda kutoka hapa;

17 Na saa wala siku haijatolewa kwao, kwa hiyo wafanye katika nchi hii kana kwamba wapo kwa miaka mingi, na hii itageuka kuwa vyema kwao.

18 Tazama, huu utakuwa ni [a]mfano kwa mtumishi wangu Edward Partridge, katika mahali pengine, katika makanisa yote.

19 Na yeyote atakayepatikana kuwa mwaminifu, mwenye haki, na [a]mtumishi mwenye hekima ataingia katika [b]shangwe ya Bwana wake, na ataurithi uzima wa milele.

20 Amini, ninawaambia, Mimi ndimi Yesu Kristo, [a]naja upesi, katika [b]saa msiyodhani. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 52

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa wazee wa Kanisa, huko Kirtland, Ohio, 6 Juni 1831. Mkutano ulikuwa umefanyika huko Kirtland, kuanzia tarehe 3 na kufungwa tarehe 6 Juni. Katika mkutano huu ibada maalumu ya kutawazwa katika ofisi ya kuhani mkuu ilifanyika kwa mara ya kwanza, na kujitokeza mara

9 *b* MWM Umoja.
10 *a* MY tawi jingine la Kanisa au dhehebu jingine.
12 *a* MWM Ridhaa ya Wengi.
13 *a* M&M 42:55. MWM Ghala.
b M&M 42:33–34, 55; 82:17–19.
15 *a* M&M 51:2.
16 *a* MY Kirtland, eneo la Ohio.
18 *a* MY kielezo.
19 *a* Mt. 24:45–47. MWM Msimamizi, Usimamizi.
b MWM Shangwe.
20 *a* Ufu. 22:6–16.
b Mt. 24:44.

kadhaa kwa roho wa uwongo na wadanganyifu kulitambuliwa na kukemewa.

1–2, Mkutano uliofuata ulipangwa kufanyika huko Missouri; 3–8, Teuzi za wazee maalumu kusafiri kwa pamoja zinafanywa; 9–11, Wazee watafundisha yale ambayo mitume na manabii waliyoandika; 12–21, Wale walioangaziwa na Roho huzaa matunda ya sifa na hekima; 22–44, Wazee mbalimbali wanateuliwa kwenda kuhubiri injili wakati wakisafiri kwenda Missouri kwa ajili ya mkutano.

Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwa wazee ambao [a]amewaita na kuwateua katika siku hizi za mwisho, kwa sauti ya Roho wake—

2 Akisema; Mimi, Bwana, nitafanya yajulikane kwenu yale nitakayo kwamba myafanye kutoka wakati huu hadi mkutano ujao, ambao utafanyika katika Missouri, juu ya [a]nchi ambayo nitaiweka [b]wakfu kwa watu wangu, ambao ni [c]baki la Yakobo, na wale ambao ni warithi kulingana na [d]agano.

3 Kwa hiyo, amini ninawaambia, na watumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na Sidney Rigdon wafanye safari yao haraka kadiri maandalizi yanavyoweza kufanyika ya kuziacha nyumba zao, na kusafiri kwenda nchi ya Missouri.

4 Na kadiri watakavyokuwa waaminifu kwangu, itafanywa ijulikane kwao nini cha kufanya;

5 Na pia, kadiri watakavyokuwa waaminifu, itafanywa ijulikane kwao [a]nchi ya urithi wenu.

6 Na kadiri watakavyokuwa siyo waaminifu, watakatiliwa mbali, hata kama vile nitakavyotaka, kama nitakavyoona kuwa ni vyema.

7 Na tena, amini ninawaambia, na mtumishi wangu Lyman Wight na mtumishi wangu John Corrill wafanye safari yao upesi;

8 Na pia mtumishi wangu John Murdock, na mtumishi wangu Hyrum Smith, wafunge safari yao kwenda sehemu hiyo hiyo kwa njia ya Detroit.

9 Na wasafiri kuanzia hapa wakilihubiri neno njiani, wakisema [a]si kitu kingine isipokuwa yale ambayo [b]manabii na mitume wameyaandika, na yale watakayofundishwa na [c]Mfariji kwa njia ya kusali kwa imani.

10 Na waende [a]wawili wawili, na hivyo ndivyo wafundishe njiani katika kila kusanyiko, wakibatiza kwa [b]maji, na kuwa-

52 1*a* mwm Ita, Itwa na Mungu, Wito.
2*a* M&M 57:1–3.
b M&M 58:57; 84:3–4.
c Zab. 135:4; 3 Ne. 5:21–26.
d Ibr. 2:6–11. mwm Agano la Ibrahimu.
5*a* M&M 57:1–3.
9*a* Mos. 18:19–20.
b M&M 42:12; 52:36. mwm Maandiko.
c mwm Fundisha, Mwalimu—Kufundisha kwa Roho; Mfariji; Roho Mtakatifu.
10*a* Mk. 6:7; M&M 61:35.
b Yn. 1:26.

wekea [c]mikono kando kando ya maji.

11 Kwani hivyo ndivyo asemavyo Bwana, nitaimaliza na kuifupisha kazi yangu katika [a]haki, kwani siku zaja ambazo nitaileta hukumu kwa ushindi.

12 Na mtumishi wangu Lyman Wight ajihadhari, kwani Shetani anataka [a]kumpepeta kama makapi.

13 Na tazama, yule [a]aliye mwaminifu atafanywa kuwa mtawala juu ya vitu vingi.

14 Na tena, nitatoa kwenu utaratibu katika mambo yote, ili msidanganyike; kwani Shetani amezagaa katika nchi, na anaenda akiwadanganya mataifa—

15 Kwa hiyo yule aombaye, akiwa roho yake [a]imepondeka, huyo [b]hukubaliwa nami kama anatii [c]ibada zangu.

16 Yule asemaye, akiwa roho yake imepondeka, na ambaye lugha yake ni ya unyenyekevu na yenye kujenga, huyo ni wa Mungu kama anatii maagizo yangu.

17 Na tena, yule atetemekaye chini ya uwezo wangu atafanywa kuwa [a]imara, naye atazaa matunda ya sifa na [b]hekima, sawa sawa na kweli na mafunuo ambayo nimewapa ninyi.

18 Na tena, yule aliyeshinda na [a]asizae matunda, hata sawa sawa na utaratibu huu, siyo wangu.

19 Kwa hiyo, kwa utaratibu huu [a]mtazijua roho katika hali zote chini ya mbingu.

20 Na siku zimefika [a]itakapofanyika kwa wanadamu sawa sawa na imani yao.

21 Tazama, amri hii imetolewa kwa wazee wote ambao nimewateua.

22 Na tena, amini ninawaambia, mtumishi wangu [a]Thomas B. Marsh na mtumishi wangu Ezra Thayre wafanye safari yao pia, wakilihubiri neno njiani katika nchi hii hii.

23 Na tena, mtumishi wangu Isaac Morley na mtumishi wangu Ezra Booth wafunge safari yao, pia wakilihubiri neno njiani katika nchi hii hii.

24 Na tena, watumishi wangu [a]Edward Partridge na Martin Harris wafunge safari yao pamoja na watumishi wangu Sidney Rigdon na Joseph Smith, Mdogo.

25 Na watumishi wangu David Whitmer na Harvey Whitlock pia wafunge safari yao, na wahubiri njiani, pia katika nchi hii hii.

26 Na watumishi wangu [a]Parley P. Pratt na [b]Orson Pratt wafunge safari yao, na wahubiri njiani, pia katika nchi hii hii.

27 Na watumishi wangu

10 *c* Mdo. 8:14–17.
11 *a* Rum. 9:28.
12 *a* Lk. 22:31; 3 Ne. 18:17–18.
13 *a* Mt. 25:23; M&M 132:53.
15 *a* MWM Moyo Uliovunjika.
b M&M 97:8.
c MWM Ibada.
17 *a* M&M 66:8; 133:58.
b MWM Hekima.
18 *a* Mt. 3:10.
19 *a* MWM Utambuzi, Kipawa cha.
20 *a* Mt. 8:5–13.
22 *a* M&M 56:5. MWM Marsh, Thomas B.
24 *a* MWM Partridge, Edward.
26 *a* MWM Pratt, Parley Parker.
b MWM Pratt, Orson.

Solomon Hancock na Simeon Carter pia wafunge safari yao katika nchi hii hii, na wahubiri njiani.

28 Na watumishi wangu Edson Fuller na Jacob Scott pia wafunge safari yao.

29 Na watumishi wangu Levi W. Hancock na Zebedee Coltrin pia wafunge safari yao.

30 Na watumishi wangu Reynolds Cahoon na Samuel H. Smith pia wafunge safari yao.

31 Na watumishi wangu Wheeler Baldwin na William Carter pia wafunge safari yao.

32 Na watumishi wangu [a]Newel Knight na Selah J. Griffin wote wawili watawazwe, na pia wafunge safari yao.

33 Ndiyo, amini ninaambia, na hawa wote wafunge safari zao kwenda sehemu moja, katika njia zao tofauti, na pasiwepo mtu mmoja kujenga juu ya [a]msingi wa mwingine, wala katika njia ya mwingine.

34 Yule aliye mwaminifu, ndiye atakayetunzwa na kubarikiwa kwa [a]matunda mengi.

35 Na tena, ninawaambia, acha watumishi wangu Joseph Wakefield na Solomon Humphrey wafunge safari yao katika nchi za mashariki;

36 Na wafanye kazi pamoja na familia zao, [a]wasitangaze lolote ila yale ya manabii na mitume, kile ambacho [b]wamekiona na kusikia na kwa hakika zaidi [c]wanachoamini, ili kwamba unabii uweze kutimia.

37 Katika matokeo ya kuvunja sheria, na kile kilichowekwa juu ya Herman Basset [a]kiondolewe kutoka kwake, na kuwekwa juu ya kichwa cha Simonds Ryder.

38 Na tena, amini ninawaambia, Jared Carter [a]atawazwe kuwa kuhani, na pia George James atawazwe kuwa [b]kuhani.

39 Na wazee walio salia [a]wachunge makanisa, na kulitangaza neno katika maeneo yanayo wazunguka; na wafanye kazi kwa mikono yao wenyewe kwamba pasiwepo kufanyika kwa [b]ibada za sanamu wala maovu kutendwa.

40 Na wakumbukeni katika mambo yote [a]maskini na [b]wenye shida, wagonjwa na walioteseka, kwani yule asiyefanya mambo haya, huyu siyo mwanafunzi wangu.

41 Na tena, watumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na Sidney Rigdon na Edward Partridge wachukue [a]hati ya uthibitisho pamoja nao kutoka katika kanisa. Na ipatikane moja pia kwa ajili ya mtumishi wangu Oliver Cowdery.

42 Na hivyo ndivyo, hata kama nilivyosema, kama mtakuwa waaminifu mtajikusanya pamoja ninyi wenyewe kufurahi juu ya nchi ya [a]Missouri,

32*a* M&M 56:6–7.
33*a* Rum. 15:20.
34*a* Yn. 15:16; M&M 18:15–16.
36*a* Mos. 18:19–20; M&M 52:9.
b Yn. 3:11.
c MWM Amini, Imani.
37*a* Mt. 25:25–30.
38*a* M&M 79:1.
b MWM Kuhani, Ukuhani wa Haruni.
39*a* Alma 6:1.
b MWM Kuabudu sanamu.
40*a* M&M 104:15–18. MWM Maskini.
b MWM Ustawi.
41*a* M&M 20:64.
42*a* MWM Sayuni.

ambayo ndiyo nchi ya [b]urithi wenu, ambayo sasa ni nchi ya adui zenu.

43 Lakini, tazama, Mimi, Bwana, nitauhimiza mji katika wakati wake, na nitawavika taji waaminifu kwa [a]shangwe na furaha.

44 Tazama, Mimi ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, nami [a]nitawainua siku ya mwisho. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 53

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Algernon Sidney Gilbert, huko Kirtland, Ohio, 8 Juni 1831. Kwa maombi ya Sidney Gilbert, Nabii alimwuliza Bwana juu ya kazi na wito wa Ndugu Gilbert katika Kanisa.

1–3, Wito na uteule wa Sidney Gilbert katika Kanisa ni kutawazwa kuwa mzee; 4–7, Yeye pia atatumikia kama wakala wa askofu.

Tazama, ninakuambia, mtumishi wangu Sidney Gilbert, kwamba nimesikia sala zako; na umenilingana ili ijulikane kwako, na Bwana Mungu wako, juu ya wito na [a]uteule wako katika kanisa, ambalo Mimi, Bwana nimelianzisha siku hizi za mwisho.

2 Tazama, Mimi, Bwana, ambaye [a]nilisulubiwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, ninakupa amri kwamba yakupasa [b]kuachana na ulimwengu.

3 Jichukulie juu yako utawazo wangu, hata wa uzee wa Kanisa, kuhubiri imani na toba na [a]ondoleo la dhambi, kulingana na neno langu, na kumpokea Roho Mtakatifu kwa kuwekewa [b]mikono;

4 Na pia kuwa [a]wakala kwa kanisa hili katika mahali ambapo utapangiwa na askofu, kulingana na amri ambazo zitatolewa hapo baadaye.

5 Na tena, amini ninakuambia, utafanya safari pamoja na watumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na Sidney Rigdon.

6 Tazama, hizi ni ibada za kwanza ambazo utazipokea; na mabaki yatajulikana wakati ujao, kulingana na utendaji kazi wako katika shamba la mizabibu.

7 Na tena, nataka ujifunze kwamba anaokolewa yule tu [a]astahimiliye hadi mwisho. Hivyo ndivyo. Amina.

42 *b* M&M 25:2; 57:1–3.
43 *a* MWM Shangwe.
44 *a* M&M 88:96–98.

53 1 *a* MWM Teule, Wateule; Uteuzi; Wito na Uteuzi.
2 *a* MWM Kusulubiwa.
b MWM Malimwengu; Ulimwengu.
3 *a* MWM Ondoleo la Dhambi.
b MWM Mikono, Kuweka juu ya.
4 *a* M&M 57:6, 8–10, 14–15; 84:113.
7 *a* MWM Stahimili.

SEHEMU YA 54

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, kwa Newel Knight, huko Kirtland, Ohio, 10 Juni 1831. Waumini wa Kanisa wanaoishi huko Thompson, Ohio, waligawanyika juu ya maswali yahusianayo na kuwekwa wakfu kwa mali. Uchoyo na uroho vilijitokeza. Kufuatia misheni yake kwa Shakers (ona kichwa cha habari cha sehemu ya 49). Leman Copley alivunja agano lake la kuweka wakfu shamba lake kubwa kama mahali pa urithi, kwa Watakatifu waliowasili kutoka Colesville, New York. Kama matokeo, Newel Knight (kiongozi wa waumini walioishi katika Thompson) na wazee wengine walikuwa wamekuja kwa Nabii wakiomba mwongozo namna ya kuendelea. Nabii alimwomba Bwana na akapokea ufunuo huu, ambao unawaamuru waumini katika Thompson kuliacha shamba la Leman Copley na kusafiri kwenda Missouri.

1–6, Watakatifu lazima washike agano la injili ili kupata rehema; 7–10, Lazima wawe na subira katika taabu.

Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, hata [a]Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, hata yule [b]aliyesulubiwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu—

2 Tazama, amini, amini, ninakuambia, mtumishi wangu Newel Knight, simama imara katika ofisi niliyokuteua.

3 Na kama ndugu zako wanataka kuwakwepa adui zao, na watubu dhambi zao zote, na kuwa [a]wanyenyekevu na kweli na wanyoofu mbele zangu.

4 Na kwa kuwa [a]agano ambalo walifanya kwangu limevunjwa, na hata hivyo limekuwa bure na [b]limebatilika.

5 Na ole wake mtu aliletaye jambo la [a]kukosesha, kwani ingekuwa heri kwake kama angetoswa katika kilindi cha bahari.

6 Lakini wana heri wale ambao wameshika agano na kufuata amri, kwani watapata [a]rehema.

7 Kwa hiyo, enendeni sasa na muikimbie nchi hii, wasije adui zenu wakaja juu yenu; na anzeni safari yenu, na mchagueni yule mumtakaye kuwa kiongozi wenu, na kulipa fedha kwa ajili yenu.

8 Na hivyo mtafanya safari yenu katika mikoa ya magharibi, kwenye nchi ya [a]Missouri, kwenye mipaka ya Walamani.

9 Na baada ya kufanya safari, tazama, ninawaambia, tafuteni [a]maisha kama watu wengine,

54 1*a* Ufu. 1:8; M&M 19:1. MWM Alfa na Omega.
b MWM Kusulubiwa.
3*a* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
4*a* M&M 42:30–39. MWM Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.
b M&M 58:32–33.
5*a* Mt. 18:6–7.
6*a* MWM Rehema, enye Rehema.
8*a* M&M 52:42.
9*a* 1 The. 4:11.

hadi nitakapotayarisha mahali kwa ajili yenu.

10 Na tena, kuweni [a]wavumilivu katika taabu hadi [b]nijapo; na tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, na wale ambao [c]wamenitafuta mapema watapata [d]pumziko nafsini mwao. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 55

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa William W. Phelps, huko Kirtland, Ohio, 14 Juni 1831. William W. Phelps, mchapishaji, na familia yake walikuwa wamewasili hivi karibuni huko Kirtland, na Nabii alimwomba Bwana taarifa juu yake.

1–3, William W. Phelps ameitwa na kuteuliwa kubatizwa, kutawazwa kuwa mzee, na kuhubiri injili; 4, Pia ataandika vitabu vya watoto katika shule za Kanisa; 5–6, Yeye atasafiri kwenda Missouri, mahali ambako litakuwa eneo lake la kazi.

Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwako, mtumishi wangu William, ndiyo, hata Bwana wa [a]dunia yote, wewe umeitwa na umeteuliwa; na baada ya kuwa [b]umebatizwa kwa maji, kitu ambacho ukikifanya na jicho lako likiwa kwenye utukufu wangu pekee, utapata ondoleo la dhambi zako, na utampokea Roho Mtakatifu kwa kuwekewa [c]mikono;

2 Na halafu utatawazwa kwa mkono wa mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, kuwa mzee katika kanisa hili, ili kuhubiri toba na [a]ondoleo la dhambi kwa njia ya ubatizo katika jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.

3 Na kwa wale wote utakaowawekea mikono yako, kama watajuta mbele zangu, utakuwa na uwezo wa kuwapa Roho Mtakatifu.

4 Na tena, utatawazwa kumsaidia mtumishi wangu Oliver Cowdery kufanya kazi ya kuchapa, na kuchagua na kuandika [a]vitabu kwa ajili ya shule za kanisa hili, ili kwamba watoto wadogo nao waweze kupokea maelekezo mbele zangu kama inipendezavyo.

5 Na tena, amini ninakuambia, kwa sababu hii utafanya safari yako pamoja na watumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na Sidney Rigdon, ili uweze [a]kuwekwa katika nchi ya urithi wako kwa kufanya kazi hii.

6 Na tena, na mtumishi

10 *a* MWM Subira.
b Ufu. 22:12.
MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
c Mit. 8:17.
MWM Sala.
d Mt. 11:28–30.

MWM Pumzika.

55 1 *a* Kum. 10:14; 1 Ne. 11:6; 2 Ne. 29:7.
b MWM Batiza, Ubatizo.
c MWM Mikono, Kuweka juu ya.

2 *a* MWM Ondoleo la Dhambi.

4 *a* M&M 88:118; 109:7, 14.

5 *a* Amo. 9:15.

wangu Joseph Coe pia ashike safari yake pamoja nao. Mabaki yatafunuliwa baadaye, kadiri nitakavyotaka. Amina.

SEHEMU YA 56

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 15 Juni 1831. Ufunuo huu unamrudi Ezra Thayre kwa kutotii ufunuo wa awali (amri iliyotajwa katika aya ya 8), ambayo Joseph Smith alikuwa amepokea kwa ajili yake, ukimwagiza Thayre kuhusu wajibu wake juu ya shamba la Frederick G. Williams ambamo yeye alikuwa akiishi. Ufunuo ufuatao pia unatengua wito wa Thayre wa kusafiri kwenda Missouri pamoja na Thomas B. Marsh (ona sehemu ya 52:22).

1–2, Watakatifu ni lazima wabebe msalaba wao na kumfuata Bwana ili kupata wokovu; 3–13, Bwana huamuru na hutangua, na wenye kiburi hukatiliwa mbali; 14–17, Ole wake tajiri ambaye hatamsaidia maskini, na ole wao maskini ambao mioyo yao haijapondeka; 18–20, Heri maskini walio safi moyoni, kwani watairithi nchi.

Sikilizeni, Enyi watu [a]mliolikiri jina langu, asema Bwana Mungu wenu; kwani tazama, hasira yangu inawaka dhidi ya waasi, na wataujua mkono wangu na uchungu wa hasira yangu, katika siku ya [b]kujiliwa na ya ghadhabu juu ya mataifa.

2 Na yule asiyeuchukua [a]msalaba wake na [b]kunifuata, na kushika amri zangu, huyo hataokolewa.

3 Tazama, Mimi, Bwana, naamuru; na yule ambaye [a]hatatii [b]atakatiliwa mbali katika wakati wangu mwenyewe, baada ya kuwa nimeamuru na amri imevunjwa.

4 Kwa hiyo Mimi, Bwana, ninaamuru, na [a]kutengua, kama nipendavyo; na hii yote itajibiwa juu ya vichwa vya [b]waasi, asema Bwana.

5 Kwa hiyo, ninateangua amri ambayo ilitolewa kwa watumishi wangu [a]Thomas B. Marsh na Ezra Thayre, na ninatoa amri mpya kwa mtumishi wangu Thomas, kwamba aanze safari yake haraka kwenda nchi ya Missouri, na mtumishi wangu Selah J. Griffin aende pia pamoja naye.

6 Kwani tazama, mimi nitatangua amri ambayo ilitolewa kwa watumishi wangu Selah J. Griffin na Newel Knight, katika

56 1*a* M&M 41:1.
b Isa. 10:3–4; Morm. 9:2; M&M 1:13–14; 124:10.
2*a* Lk. 14:27.
b 1 Pet. 2:21; 2 Ne. 31:10–13; Moro. 7:11.
MWM Yesu Kristo—Mfano wa Yesu Kristo.
3*a* MWM Mtiifu, Tii, Utii.
b M&M 1:14–16; 50:8.
4*a* M&M 58:31–33.
b MWM Uasi.
5*a* MWM Marsh, Thomas B.

matokeo ya kiburi cha watu wangu walioko Thompson, na uasi wao.

7 Kwa hiyo, wacheni mtumishi wangu Newel Knight abaki pamoja nao; na wale wote watakaokwenda na waende, wale walio wanyoofu mbele zangu, na waongozwe naye kwenda kwenye nchi niliyoiteua.

8 Na tena amini ninawaambia, kwamba mtumishi wangu Ezra Thayre ni lazima atubu kwa [a]majivuno, na uchoyo wake, na atii amri zilizopita nilizompa juu ya mahali anapoishi.

9 Na kama atayafanya haya, na pasiwepo na mgawanyo wa ardhi hiyo, bado atateuliwa kwenda katika nchi ya Missouri;

10 Na vinginevyo atarejeshewa fedha alizolipa, na kuondoka mahali hapo, na [a]atakatiliwa mbali kutoka katika kanisa langu, asema Bwana Mungu wa majeshi;

11 Na ingawa mbingu na dunia zitapita, maneno haya [a]hayatapita kamwe, bali yatatimilizwa.

12 Na kama mtumishi wangu, Joseph Smith, Mdogo, itambidi kulipa fedha hizo, tazama, Mimi, Bwana, nitamlipa yeye tena katika nchi ya Missouri, ili kwamba wale ambao atapokea kutoka kwao waweze kupata thawabu tena kulingana na yale wanayofanya;

13 Kwani kulingana na kile ambacho wanakifanya watapokea, hata katika ardhi kwa urithi wao.

14 Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwa watu wangu—mnayo mambo mengi ya kufanya na kuyatubu; kwani tazama, dhambi zenu zimenifikia, na hazisameheki, kwa sababu ninyi [a]mnashauriana katika njia zenu wenyewe.

15 Na mioyo yenu hairidhiki. Na wala haitii ukweli, bali [a]mnafurahia katika dhuluma.

16 Ole wenu ninyi watu [a]matajiri, ambao [b]hamtatoa vitu vyenu kwa [c]maskini, kwani [d]utajiri wenu utaziharibu roho zenu; na huku kutakuwa kuomboleza kwenu katika siku ya kujiliwa, na ya hukumu, na ya hasira ya uchungu: [e]Mavuno yamepita, na kiangazi kimeisha, na nafsi yangu haikuokolewa!

17 Ole wenu ninyi watu [a]maskini, ambao mioyo yenu haijapondeka, ambao roho zenu siyo nyoofu, na ambao matumbo yenu hayatosheki, na ambao mikono yenu haijizuii kuchukua mali ya watu, ambao macho yenu yamejaa [b]uroho, na ambao hamfanyi kazi kwa mikono yenu wenyewe!

18 Lakini heri [a]maskini walio

8*a* MWM Kiburi.
10*a* MWM Kutengwa na Kanisa.
11*a* 2 Ne. 9:16.
14*a* Yak. (KM) 4:10.
15*a* Alma 41:10; 3 Ne. 27:11.
16*a* Yer. 17:11; 2 Ne. 9:30.
b MWM Sadaka, Utoaji sadaka.
c Mit. 14:31; Alma 5:55–56. MWM Maskini.
d Yak. (Bib.) 5:3.
e Yer. 8:20; Alma 34:33–35; M&M 45:2.
17*a* Mos. 4:24–27; M&M 42:42; 68:30–32.
b MWM Tamani.
18*a* Mt. 5:3, 8; Lk. 6:20; 3 Ne. 12:3. MWM Maskini.

safi moyoni, ambao mioyo yao [b]imevunjika, na roho zao zimepondeka, kwa kuwa watauona [c]ufalme wa Mungu ukija katika nguvu na utukufu mwingi kwa ukombozi wao; kwani vinono vya [d]nchi vitakuwa vyao.

19 Kwani tazama, Bwana atakuja, na [a]ujira wake utakuwa pamoja naye, na atamlipa kila mtu, na maskini atafurahi;

20 Na vizazi vyao [a]vitairithi dunia kutoka kizazi hadi kizazi, milele na milele. Na sasa nimefika mwisho wa kusema nanyi. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 57

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Sayuni, katika Wilaya ya Jackson, Missouri, 20 Julai 1831. Katika kutii amri za Bwana ya kusafiri kwenda Missouri, mahali ambapo atafunua "ardhi ya urithi wenu" (sehemu ya 52), wazee walisafiri kutoka Kirtland hadi mpaka wa upande wa magharibi wa Missouri. Joseph Smith alitafakari juu ya hali ya Walamani na akishangaa: "Ni lini nyika itachanua kama waridi? Ni lini Sayuni itajengwa katika utukufu wake, na ni wapi hekalu Lako litasimama, ambako mataifa yote yatakuja katika siku za mwisho?" Baada ya hayo alipokea ufunuo huu.

1–3, Independence, Missouri, ndiyo mahali pa Jiji la Sayuni na pa hekalu; 4–7, Watakatifu watanunua ardhi na kupokea urithi katika eneo lile; 8–16, Sidney Gilbert ataanzisha stoo, William W. Phelps atakuwa mchapaji, na Oliver Cowdery atakariri maandiko kwa ajili ya uchapaji.

Sikilizeni, Enyi wazee wa kanisa langu, asema Bwana Mungu wenu, ninyi mliojikusanya pamoja, kulingana na amri zangu, katika nchi hii, ambayo ni nchi ya [a]Missouri, [b]nchi ambayo nimeiteua na [c]kuiweka wakfu kwa ajili ya [d]kukusanyika watakatifu.

2 Kwa hiyo, hii ni nchi ya ahadi, na [a]mahali pa mji wa [b]Sayuni.

3 Na hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu wenu, kama mnataka hekima hapa ndipo penye hekima. Tazama, mahali ambapo sasa panaitwa Independence ni katikati, na eneo kwa ajili ya [a]hekalu linalala upande wa magharibi, kwenye kiwanja ambacho hakiko mbali na nyumba ya mahakama.

18 *b* MWM Moyo Uliovunjika.
c MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
d MWM Dunia.
19 *a* Ufu. 22:12; M&M 1:10.
20 *a* Mt. 5:5; M&M 45:56–58.
57 1 *a* M&M 52:42.
b M&M 29:7–8; 45:64–66.
c M&M 61:17.
d MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
2 *a* M&M 28:9; 42:9, 62.
b MWM Sayuni.
3 *a* M&M 58:57; 97:15–17.

4 Kwa hiyo, ni hekima ardhi hiyo [a]inununuliwe na watakatifu, na kila ardhi iliyoko upande wa magharibi, hadi kwenye mpaka kati ya [b]Myahudi na Myunani;

5 Na pia kila ardhi inayopakana na mbuga pana, kadiri wanafunzi wangu watakavyowezeshwa [a]kununua ardhi. Tazama, hii ni hekima, kwamba waweze [b]kuipata kwa ajili ya urithi usio na mwisho.

6 Na mtumishi wangu Sidney Gilbert asimame katika ofisi ambayo nilimteua, kupokea fedha, kuwa [a]wakala kwa kanisa, kwa kununua ardhi katika maeneo yote ya karibu, kadiri itakavyoweza kufanyika katika haki, na kama hekima itakavyoelekeza.

7 Na mtumishi wangu [a]Edward Partridge asimame katika ofisi ambayo nimemteua, na [b]agawe kwa watakatifu urithi wao, kama vile nilivyoamuru; na pia wale aliowateua kumsaidia.

8 Na tena, amini ninawaambia, na mtumishi wangu Sidney Gilbert ajipandikize mwenyewe katika mahali hapa, na kuanzisha duka, ili aweze kuuza mali kwa uaminifu, ili aweze kupata fedha za kununua ardhi kwa ajili ya watakatifu, na ili aweze kupata vitu vingine ambavyo wanafunzi watahitaji kupanda katika urithi wao.

9 Na pia mtumishi wangu Sidney Gilbert apate leseni—tazama hapa ndipo penye hekima, na yeyote asomaye na afahamu—ili aweze kutuma mali pia kwa watu, hata kwa amtakaye kumwajiri kama karani katika huduma yake;

10 Na hivyo kuwahudumia watakatifu wangu, ili injili yangu iweze kuhubiriwa kwa wale wakaao [a]gizani na katika maeneo ya [b]uvuli wa mauti.

11 Na tena, amini ninawaambia, na mtumishi wangu [a]William W. Phelps awekwe katika mahali hapa, na afanywe kuwa [b]mchapaji wa kanisa.

12 Na lo, kama ulimwengu utayapokea maandiko yake—tazama hii ndiyo hekima—na apate kila awezacho kupata katika haki, kwa faida ya watakatifu.

13 Na mtumishi wangu [a]Oliver Cowdery amsaidie, hata kama vile nilivyo waamuru, katika mahali popote nitakapopateua kwa ajili yake, kunakili, na kusahihisha, na kuchagua, ili mambo yote yaweze kuwa sahihi mbele zangu, kulingana na Roho atakavyoidhinisha kupitia yeye.

14 Na hivyo basi wale ambao nimewazungumzana wawekwe

4 *a* M&M 48:4.
b MY *Myahudi* hapa inamaanisha Walamani, na *Myunani* inamaanisha walowezi wazungu.
5 *a* M&M 58:49, 51; 101:68–74.
b M&M 56:20.
6 *a* M&M 53.
7 *a* M&M 58:24.
MWM Partridge, Edward.
b M&M 41:9–11; 58:14–18.
10 *a* Isa. 9:2; Mt. 4:16.
MWM Giza, Kiroho.
b Zab. 23:4.
11 *a* MWM Phelps, William W.
b M&M 58:37, 40–41.
13 *a* MWM Cowdery, Oliver.

katika nchi hii ya Sayuni, kwa haraka iwezekanavyo, pamoja na familia zao, kufanya mambo yale kama nilivyoyanena.

15 Na sasa juu ya kukusanyika—Askofu na wakala wafanye matayarisho kwa ajili ya familia zilizoamriwa kuja katika nchi hii, upesi iwezekanavyo, na kuwaweka katika urithi wao.

16 Na kwa mabaki ya wote wazee na waumini maelekezo zaidi yatatolewa hapo baadaye. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 58

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Sayuni, katika Wilaya ya Jackson, Missouri, 1 Agosti 1831. Mapema, siku ya Sabato ya kwanza baada ya kuwasili kwa Nabii na kundi lake Wilayani Jackson, Missouri, ibada ya kanisa ilikuwa imefanyika na waumini wawili walikuwa wamepokelewa kwa ubatizo. Katika wiki hiyo, baadhi ya Watakatifu wa Colesville kutoka Tawi la Thompson na wengine waliwasili (ona sehemu ya 54). Wengi walikuwa na shauku ya kutaka kujua matakwa ya Bwana juu yao katika sehemu mpya ya kukusanyika.

1–5, Wale watakaostahimili taabu watavikwa utukufu; 6–12, Watakatifu wajitayarishe kwa ajili ya harusi ya Mwanakondoo na karamu ya Bwana; 13–18; Maaskofu ndiyo waamuzi katika Israeli; 19–23, Watakatifu watatii sheria za nchi; 24–29, Wanadamu watumie haki yao ya kujiamulia kufanya mema; 30–33, Bwana huamuru na kutengua; 34–43, Ili kutubu, wanadamu lazima wakiri na kuacha dhambi zao; 44–58, Watakatifu wanunue urithi wao na wakusanyike Missouri; 59–65, Injili ni lazima ihubiriwe kwa kila kiumbe.

Sikilizeni, Enyi wazee wa kanisa langu, na yasikilizeni maneno yangu, na mjifunze kwangu ni nini matakwa yangu juu yenu, na pia juu ya [a]nchi hii ambayo nimewaleta.

2 Kwani amini ninawaambia, heri yule [a]ashikaye amri zangu, iwe katika maisha au [b]kifo; na yule aliye [c]mwaminifu katika [d]taabu, thawabu yake ni kubwa katika ufalme wa mbinguni.

3 Hamuwezi kuona kwa macho yenu ya asili, kwa wakati huu, mipango ya [a]Mungu wenu juu ya mambo yale ambayo yatakuja hapo baadaye, na [b]utukufu utakaofuata baada ya taabu kubwa.

4 Kwani baada ya [a]taabu

58 1*a* M&M 57:1–8.
2*a* Mos. 2:22.
b 1 Pet. 4:6.
c 2 The. 1:4.
d MWM Shida.
3*a* MWM Mungu, Uungu.
b MWM Utukufu.
4*a* Zab. 30:5; M&M 101:2–7; 103:11–14; 109:76.

kubwa huja [b]baraka. Kwa hiyo siku yaja ambayo ninyi [c]mtavikwa [d]utukufu mkubwa; saa ingali, lakini i karibu.

5 Kumbukeni hili, ambalo ninawaambia kabla, kwamba muweze [a]kuliweka moyoni, na kupokea lile ambalo litafuata.

6 Tazama, amini ninawaambia, kwa sababu hii nimewatuma ninyi—ili muweze kuwa watiifu, na kwamba mioyo yenu iweze [a]kuandaliwa kutoa [b]ushuhuda wa mambo ambayo yatakuja;

7 Na pia muweze kupewa heshima katika kuweka msingi, na katika kutoa ushuhuda wa nchi ambapo [a]Sayuni ya Mungu itasimama;

8 Na pia kwamba karamu ya vitu vinono iweze kuandaliwa kwa [a]maskini; ndiyo, karamu ya vitu vinono, karamu ya divai iliyokaa juu ya [b]urojorojo wake uliochujwa sana, ili ulimwengu uweze kujua kwamba vinywa vya manabii havitashindwa;

9 Ndiyo, karamu ya nyumba ya Bwana, iliyoandaliwa vyema, ambayo kwayo mataifa yote yataalikwa.

10 Kwanza, matajiri na wasomi, wenye hekima na maarufu;

11 Na baada ya hapo yaja siku ya uwezo wangu, halafu maskini, kiwete, na kipofu, na kiziwi, watakuja katika [a]harusi ya Mwanakondoo, na kula [b]karamu ya Bwana, iliyoandaliwa kwa ajili ya siku ile kuu ijayo.

12 Tazama, Mimi, Bwana, nimenena hili.

13 Na ili [a]ushuhuda upate kwenda kutoka Sayuni, ndiyo, kutoka kinywani mwa mji wa urithi wa Mungu—

14 Ndiyo, kwa dhumuni hili nimekutuma hapa, na nimemchagua mtumishi wangu [a]Edward Partridge, na nimempangia huduma yake katika nchi hii.

15 Lakini kama hatatubu dhambi zake, ambazo ni kutokuamini na upofu wa moyo, na atii asije [a]akaanguka.

16 Tazama huduma yake imetolewa kwake, na hautatolewa tena.

17 Na yeyote asimamaye katika huduma hii ameteuliwa kuwa [a]mwamuzi katika Israeli, kama vile ilivyokuwa katika siku za kale, kugawa ardhi ya urithi wa Mungu kwa [b]watoto wake;

18 Na kuwahukumu watu wake kwa ushuhuda wa haki, na kwa msaada wa wasaidizi wake, kulingana na sheria za ufalme ambazo hutolewa na [a]manabii wa Mungu.

19 Kwani amini ninawaambia,

4 *b* MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
c MWM Kuinuliwa; Taji.
d Rum. 8:17–18; M&M 136:31.
5 *a* Kum. 11:18–19.
6 *a* M&M 29:8.
b MWM Ushuhuda.
7 *a* MWM Sayuni.
8 *a* MWM Maskini.
b Isa. 25:6.
11 *a* Mt. 22:1–14; Ufu. 19:9; M&M 65:3.
b Lk. 14:16–24.
13 *a* Mik. 4:2.
14 *a* MWM Partridge, Edward.
15 *a* 1 Kor. 10:12.
17 *a* M&M 107:72–74. MWM Askofu.
b MWM Wana na Mabinti za Mungu.
18 *a* MWM Nabii.

sheria yangu itashikwa katika nchi hii.

20 Acheni mtu yeyote asijifikirie kuwa yeye ni mtawala; bali mwacheni Mungu amtawale yule anaye hukumu, kulingana na ushauri wa matakwa yake yeye mwenyewe, au, katika maneno mengine, yeye ambaye hushauri au aketiye juu ya kiti cha hukumu.

21 Na mtu yeyote asivunje [a]sheria za nchi, kwani yule ambaye hushika sheria za Mungu hana haja ya kuvunja sheria za nchi.

22 Kwa hiyo, mzitii mamlaka zilizopo, hadi [a]atawalapo mwenye haki ya kutawala, na kuwatiisha maadui wote chini ya miguu yake.

23 Tazama, [a]sheria ambazo mmezipokea kutoka mkononi mwangu ni sheria za kanisa, na katika nuru hii mtazishikilia. Tazama, hapa ndipo penye hekima.

24 Na sasa, kama nilivyosema juu ya mtumishi wangu Edward Partridge, nchi hii ni nchi ya makazi yake, na wale aliowateua kuwa washauri wake; na pia nchi ya makazi ya yule ambaye nimemteua kutunza [a]ghala yangu;

25 Kwa hiyo, waacheni wazilete familia zao katika nchi hii, kama vile watakavyoshauriwa kati yao na Mimi.

26 Kwani tazama, si vyema kwamba niamuru katika mambo yote; kwani yule alazimishwaye katika mambo yote, huyo ni [a]mvivu na siyo mtumishi mwenye busara; kwa hiyo hapokei thawabu yoyote.

27 Amini ninawaambia, wanadamu yawapasa [a]kujishughulisha kwa shauku katika kazi njema, na kufanya mambo mengi kwa hiari yao wenyewe, na kutekeleza haki nyingi;

28 Kwani uwezo upo ndani yao, ambamo wao ni [a]mawakala juu yao wenyewe. Na kadiri wanadamu watakavyofanya mema hawatakosa thawabu zao.

29 Lakini yule asiyefanya lolote mpaka ameamriwa, na kupokea amri kwa moyo wenye mashaka, na kuzishika kwa uvivu, huyo [a]amelaaniwa.

30 Mimi ni nani [a]niliyemuumba mwanadamu, asema Bwana, ambaye sitamshika na hatia yule ambaye hatii amri zangu?

31 Mimi ni nani, asema Bwana, ambaye [a]nimeahidi na nisitimize?

32 Ninaamuru na wanadamu hawatii; [a]ninatengua nao hawapati baraka.

33 Ndipo husema mioyoni mwao: Hii siyo kazi ya Bwana, kwani ahadi zake hazijatimia. Lakini ole wao, kwani thawabu yao ujira wao unawavizia [a]chini, na wala haitoki juu.

21 *a* Lk. 20:22–26; M&M 98:4–10; M ya I 1:12. MWM Utawala.
22 *a* MWM Masiya; Milenia; Yesu Kristo.
23 *a* MWM Sheria.
24 *a* M&M 51:13; 70:7–11.
26 *a* Mt. 24:45–51; M&M 107:99–100.
27 *a* MWM Bidii; Matendo.
28 *a* MWM Haki ya uamuzi.
29 *a* MWM Hukumu.
30 *a* Isa. 45:9–10; Hel. 12:6.
31 *a* M&M 1:37–38; 82:10.
32 *a* M&M 56:3–4.
33 *a* M&M 29:45.

34 Na sasa natoa kwenu maelekezo zaidi kuhusu nchi hii.

35 Ni hekima iliyo ndani yangu kwamba mtumishi wangu Martin Harris yapasa awe mfano kwa kanisa, katika [a]kuweka fedha zake mbele ya askofu wa kanisa.

36 Na pia, hii ni sheria kwa kila mtu ajaye katika nchi hii kupokea urithi; naye atafanya kulingana na maelekezo ya sheria.

37 Na ni hekima pia kwamba pawepo na ardhi iliyonunuliwa katika Independence, kwa ajili ya mahali pa ghala, na pia kwa ajili ya nyumba ya [a]uchapishaji.

38 Na maelekezo mengine juu ya mtumishi wangu Martin Harris yatatolewa kwake kwa njia ya Roho, ili aweze kupokea urithi wake kama aonavyo yeye kuwa vyema;

39 Na atubu dhambi zake, kwa vile yeye hutafuta [a]sifa za ulimwenguni.

40 Na pia mtumishi wangu [a]William W. Phelps asimame katika ofisi niliyomteua, na kupokea urithi wake katika nchi;

41 Naye pia ana haja ya kutubu, kwani Mimi, Bwana, sijapendezwa naye, kwani anatafuta kujikweza, na siyo mnyenyekevu vya kutosha mbele zangu.

42 Tazama, yule ambaye [a]ametubu dhambi zake, huyu [b]anasamehewa, na Mimi, Bwana, [c]sizikumbuki tena.

43 Kwa hili mnaweza kujua kama mtu ametubu dhambi zake—tazama, [a]ataungama na [b]kuziacha.

44 Na sasa, amini, ninasema juu ya mabaki ya wazee wa kanisa langu, wakati haujafika bado, na hautafika kwa miaka mingi, kwa wao kupokea urithi wao katika nchi hii, isipokuwa wametamani kwa njia ya sala ya imani, pekee kama itakavyoteuliwa kwao na Bwana.

45 Kwani, tazama, [a]watawasukuma watu pamoja hata kutoka miisho ya dunia.

46 Kwa hiyo, jikusanyeni pamoja; na wale wasioteuliwa kukaa katika nchi hii, na wahubiri injili katika maeneo ya jirani; na baada ya haya na warejee majumbani kwao.

47 Na wahubiri njiani, na [a]kutoa ushuhuda juu ya ukweli katika mahali pote, wakiwaita matajiri, wakubwa na wadogo, na maskini kutubu.

48 Na wajenge [a]makanisa kadiri wakazi wa dunia watakavyotubu.

49 Na acha pawepo na wakala aliye chaguliwa kwa sauti ya kanisa, kwa kanisa la Ohio, kupokea fedha za kununulia ardhi katika [a]Sayuni.

50 Na ninatoa amri kwa mtumishi wangu Sidney Rigdon, kwamba [a]ataandika maelezo juu ya nchi ya Sayuni, na taarifa

35 *a* M&M 42:30–32.
37 *a* M&M 57:11–12.
39 *a* 2 Ne. 26:29; M&M 121:34–37.
40 *a* MWM Phelps, William W.
42 *a* MWM Toba, Tubu.
b Isa. 1:18. MWM Samehe.
c Isa. 43:25.
43 *a* M&M 19:20; 64:7. MWM Kiri, Kukiri.
b M&M 82:7.
45 *a* Kum. 33:17. MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
47 *a* M&M 68:8.
48 *a* MY matawi ya Kanisa.
49 *a* MWM Sayuni.
50 *a* M&M 63:55–56.

ya mapenzi ya Mungu, kama vile itakavyojulishwa kwake na Roho;

51 Na waraka na hati, itawakilishwa kwa makanisa yote ili kupata fedha, ili ziwekwe katika mikono ya askofu, au katika mikono yake mwenyewe au mikono ya wakala, kama itakavyoonekana kwake kuwa ni vyema au kama atakavyoelekeza, kwa kununulia ardhi kwa ajili ya urithi kwa watoto wa Mungu.

52 Kwani, tazama, amini ninawaambia, Bwana ataka kwamba wanafunzi na wanadamu wafungue mioyo yao, hata kwa kununua eneo la nchi hii yote mapema, kama vile muda utakavyoruhusu.

53 Tazama, hii ndiyo ilipo hekima. Na wafanye hili vinginevyo wasije wakakosa kabisa [a]urithi, isipokuwa kwa umwagaji wa damu.

54 Na tena, kadiri itakavyopatikana ardhi, na wafanya kazi wa kila aina watumwe katika nchi hii, kufanya kazi kwa ajili ya watakatifu wa Mungu.

55 Na mambo haya yote na yafanyike katika utaratibu; na haki ya kuwa na ardhi ijulishwe kila wakati na askofu au wakala wa kanisa.

56 Na kazi ya kukusanyika na isifanywe kwa haraka, wala kwa kukimbia; bali na ifanyike kama itakavyoshauriwa na wazee wa kanisa kwenye mikutano, kulingana na taarifa watakazokuwa wakizipokea mara kwa mara.

57 Na mtumishi wangu Sidney Rigdon atakase na kuweka wakfu kwa Bwana ardhi hii, na eneo la ujenzi wa [a]hekalu.

58 Na mkutano uitishwe; na baada ya hayo, watumishi wangu Sidney na Joseph Smith, Mdogo, warejee, na pia Oliver Cowdery pamoja nao, kumaliza mabaki ya kazi ambayo nimewateua katika nchi yao wenyewe, na zilizosalia kama [a]itakavyoamriwa na mikutano.

59 Na pasiwepo na mtu yeyote atakayerejea kutoka nchi hii bila [a]kutoa ushuhuda njiani, kwa kile akijuacho na kwa uhakika zaidi kile anachokiamini.

60 Na kile kilichowekwa juu ya Ziba Peterson kichukuliwe kutoka kwake; na asimame kama muumini katika kanisa, na afanye kazi kwa mikono yake mwenyewe, pamoja na ndugu zake hadi [a]atakaporudiwa vya kutosha kwa dhambi zake zote; kwani yeye haziungami, na anafikiria kuzificha.

61 Na waliobaki kati ya wazee wa kanisa hili, ambao wanakuja katika nchi hii, ambao baadhi yao wamebarikiwa kupita kiasi, pia wafanye mkutano katika nchi hii.

62 Na mtumishi wangu Edward Partridge aongoze mkutano utakaofanywa na hao.

63 Na wao pia warejee, wakihubiri injili njiani, wakitoa

53 *a* M&M 63:27–31.
57 *a* M&M 57:3; 84:3–5, 31; 97:10–17.
58 *a* MWM Ridhaa ya Wengi.
59 *a* MWM Ushuhuda.
60 *a* MWM Rudi, Kurudiwa.

ushuhuda wa mambo yaliyofunuliwa kwao.

64 Kwani, amini, sauti lazima iende mbele kutoka mahali hapa kwenda katika ulimwengu wote, na hata sehemu za mbali zaidi za ulimwengu—injili lazima [a]ihubiriwe kwa kila kiumbe, na [b]ishara zikiwafuata wenye kuamini.

65 Na tazama Mwana wa Mtu yu [a]aja. Amina.

SEHEMU YA 59

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, katika Sayuni, huko Wilayani Jackson, Missouri, 7 Agosti 1831. Kabla ya ufunuo huu, ardhi ilikuwa imekwisha tengwa kwa ajili ya dini, kama vile Bwana alivyoelekeza, na kiwanja kwa ajili ya hekalu la baadaye kiliwekwa wakfu. Katika siku ambayo ufunuo huu ulipokelewa, Polly Knight mke wa Joseph Knight Mkubwa alifariki, Muumini wa kwanza wa Kanisa kufariki katika Sayuni. Waumini wa mwanzoni waliuita ufunuo huu kama "wenye kuwaelekeza Watakatifu namna ya kuishika Sabato na namna ya kufunga na kusali."

1–4, Watakatifu waaminifu katika Sayuni watabarikiwa; 5–8, Watampenda na kumtumikia Bwana na kushika amri Zake; 9–19, Kwa kushika kitakatifu siku ya Bwana, Watakatifu wanabarikiwa kimwili na kiroho; 20–24, Wenye haki wanaahidiwa amani katika ulimwengu huu na uzima wa milele katika ulimwengu ujao.

Tazama, heri, asema Bwana, wale ambao wamekuja katika nchii hii [a]jicho lao likiwa kwenye utukufu wangu pekee, kulingana na amri zangu.

2 Kwani wale waishio [a]watairithi nchi, na wale [b]wanaokufa watapata kupumzika kutoka kwa kazi zao zote, na matendo yao yatafuatana nao; na watapokea [c]taji katika [d]nyumba ya Baba yangu, ambayo nimeitayarisha kwa ajili yao.

3 Ndiyo, heri wale ambao miguu yao inasimama juu ya ardhi ya Sayuni, ambao wameitii injili yangu; kwani watapokea kama ujira wao mambo mema ya nchi, nayo itawazalia kwa [a]wingi.

4 Nao pia watavikwa taji la baraka kutoka juu, ndiyo, na amri zisizo haba, na pamoja na [a]mafunuo katika wakati wao—wale

64 *a* mwm Hubiri.
b mwm Ishara.
65 *a* mwm Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
59 1 *a* Mt. 6:22–24; M&M 88:67.
2 *a* Mt. 5:5; M&M 63:20, 48–49.
b Ufu. 14:13. mwm Mauti ya Kimwili; Peponi.
c mwm Kuinuliwa; Taji.
d Yn. 14:2; M&M 72:4; 76:111; 81:6; 98:18.
3 *a* Mwa. 4:12; Musa 5:37.
4 *a* M&M 42:61; 76:7; 98:12; 121:26–29. mwm Ufunuo.

walio [b]waaminifu na wenye [c]bidii mbele zangu.

5 Kwa hiyo, ninawapa amri, nikisema: Nawe [a]mpende Bwana Mungu wako kwa [b]moyo wako wote, na kwa uwezo wako wote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote; na katika jina la Yesu Kristo [c]utamtumikia yeye.

6 Nawe mpende [a]jirani yako kama nafsi yako. [b]Usiibe; wala [c]usizini, wala [d]usiue, wala usifanye chochote kinachofanana na hayo.

7 Nawe [a]utamshukuru Bwana Mungu wako katika mambo yote.

8 Nawe utamtolea [a]dhabihu Bwana Mungu wako katika [b]haki, hata ile ya moyo uliovunjika na [c]roho iliyopondeka.

9 Na ili ujilinde na dunia [a]pasipo mawaa, utakwenda kwenye nyumba ya sala na kutoa sakramenti zako katika [b]siku yangu takatifu;

10 Kwani amini hii ndiyo siku iliyoteuliwa kwako kupumzika kutokana na kazi zako, na [a]utoe dhabihu zako za shukrani kwa Aliye Juu Sana;

11 Hata hivyo nadhiri zako zitatolewa katika haki siku zote na kwa nyakati zote;

12 Lakini kumbuka kuwa katika siku hii, siku ya Bwana, utatoa [a]sadaka na sakramenti zako kwa Aliye Juu Sana, [b]ukiungama dhambi zako kwa ndugu zako, na mbele za Bwana.

13 Na katika siku hii hutafanya kitu kingine chochote, isipokuwa chakula chako tu na kitengenezwe kwa moyo mmoja ili [a]kufunga kwako kuweze kukamilika, au, katika maneno mengine, [b]shangwe yako iweze kuwa timilifu.

14 Amini, huku ndiyo kufunga na kusali, au kwa maneno mengine, kufurahi na sala.

15 Na kadiri mtakavyofanya mambo haya kwa [a]shukrani, pamoja na [b]mioyo na nyuso zenye [c]furaha, pasipo na [d]vicheko vingi, kwani hii ni dhambi, bali kwa moyo wenye furaha na uso mchangamfu—

16 Amini ninasema, kwamba kadiri mtakavyofanya hivi, vyote viijazavyo dunia ni mali yenu, wanyama wa mwituni na ndege wa angani, kile kipandacho juu ya miti na kitembeacho juu ya nchi;

4 *b* MWM Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki.
c MWM Bidii.
5 *a* Kum. 11:1; Mt. 22:37; Moro. 10:32; M&M 20:19. MWM Upendo.
b MWM Moyo.
c MWM Utumishi.
6 *a* MWM Ushirika.
b MWM Iba, Wizi.
c MWM Uzinzi.
d MWM Mauaji.
7 *a* Zab. 92:1; Alma 37:37; M&M 46:32. MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
8 *a* MWM Dhabihu.
b MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
c MWM Moyo Uliovunjika.
9 *a* Yak. (Bib.) 1:27.
b MWM Siku ya Sabato.
10 *a* MWM Kuabudu.
12 *a* MY sadaka, iwe ya muda, vipaji, au mali, katika kumtumikia Mungu na mwanadamu mwenzako. MWM Dhabihu.
b MWM Kiri, Kukiri.
13 *a* MWM Funga, Kufunga.
b MWM Shangwe.
15 *a* MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
b Mit. 17:22.
c Ku. 25:2; M&M 64:34.
d M&M 88:69.

17 Ndiyo, na mimea, na vitu vizuri vimeavyo kutoka ardhini, viwe kwa chakula au kwa mavazi, au kwa nyumba, au kwa maghala, au kwa bustani ya miti ya matunda, au kwa bustani ya mbogamboga, au kwa shamba la mizabibu;

18 Ndiyo, vitu vyote vimeavyo kutoka [a]ardhini, katika majira yake, vimefanywa kwa faida na matumuzi ya mwanadamu, kwa kuridhisha jicho na kufurahisha moyo;

19 Ndiyo, kwa ajili ya chakula na mavazi, kwa kuonja na kunusa, ili kuuimarisha mwili na kuchangamsha nafsi.

20 Na imempendeza Mungu kwamba ametoa vitu hivi vyote kwa mwanadamu; kwani ni kwa sababu hii vilifanywa ili vitumiwe, kwa hekima, siyo ufujaji, wala siyo kwa kutumia nguvu.

21 Na katika lolote mwanadamu [a]hamkosei Mungu, au ghadhabu ya Mungu haiwaki kwa yeyote, isipokuwa wale tu [b]wasiokiri mkono wake katika mambo yote, na wasiotii amri zake.

22 Tazama, hii ni kulingana na sheria na manabii; kwa hiyo, usinisumbue tena juu ya jambo hili.

23 Lakini, jifunzeni kwamba yule afanyaye kazi za [a]haki atapokea [b]ujira wake, hata [c]amani katika ulimwengu huu, na [d]uzima wa milele katika ulimwengu ujao.

24 Mimi, Bwana, nimeyasema haya, na Roho anayashuhudia. Amina.

SEHEMU YA 60

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, katika Independence, Wilaya ya Jackson, Missouri, 8 Agosti 1831. Katika tukio hili wazee ambao walisafiri kwenda Wilaya ya Jackson na kushiriki katika uwekaji wakfu wa ardhi na kiwanja cha hekalu walitamani kujua kile walichotakiwa kufanya.

1–9, Wazee wahubiri injili katika mikutano ya waovu; 10–14, Wasiupoteze bure muda wao, wala wasivizike vipaji vyao; 15–17, Wanaweza kusafisha miguu yao kama ushuhuda dhidi ya wale wanaoikataa injili.

Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwa wazee wa kanisa lake, ambao wanalazimika kurejea haraka kwenye nchi walikotoka: Tazama, imenipendeza Mimi, kwamba mje mahali hapa;

2 Lakini kwa wengine sipendezwi nao, kwani hawafungui [a]vinywa vyao, bali [b]wanaficha

18*a* MWM Dunia.
21*a* MWM Kosea.
b Ayu. 1:21.
23*a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
b MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
c Mt. 11:28–30.
MWM Amani.
d M&M 14:7.
60 2*a* Efe. 6:19–20.
b Lk. 8:16, 18.

vipaji ambavyo nimewapa, kwa sababu ya [c]kumwogopa mwanadamu. Ole wao hao, kwani hasira yangu inawaka dhidi yao.

3 Na itakuwa kwamba, kama wasipokuwa waaminifu zaidi juu yangu, [a]kitachukuliwa, hata kile walicho nacho.

4 Kwani Mimi, Bwana, natawala katika mbingu juu, na miongoni mwa [a]majeshi ya duniani; na katika siku ile nitakapowafanya kuwa [b]hazina yangu, watu wote watajua ni nini kinachoonyesha uwezo wa Mungu.

5 Lakini, amini, nitasema nanyi juu ya safari yenu kwenda kwenye nchi mlizotoka. Na jengeni au nunueni mashua, kama muonavyo kuwa ni vyema, siyo muhimu kwangu, fungeni safari yenu upesi kwenda sehemu iitwayo St. Louis.

6 Na kutoka huko watumishi wangu, Sidney Rigdon, Joseph Smith, Mdogo, na Oliver Cowdery, washike safari yao kuelekea Cincinnati;

7 Na katika mahali hapo wapaze sauti zao na kulitangaza neno langu kwa sauti kubwa, bila ghadhabu wala mashaka, huku wakiinua mikono [a]mitakatifu juu yao. Kwani ninaweza kuwatakasa, na [b]mmesamehewa dhambi zenu.

8 Na waliobaki wafanye safari yao kutokea St. Louis, wawili wawili, na wakihubiri neno, bila kuharakisha, miongoni mwa mikutano ya waovu, hadi warejee kwenye makanisa waliyotoka.

9 Na haya yote ni kwa manufaa ya makanisa; kwani ni kwa kusudi hili nimewatuma hao.

10 Na mtumishi wangu [a]Edward Partridge na atoe fedha ambazo nimempa, sehemu kwa wazee wangu ambao nimewaamuru kurudi;

11 Na yule ambaye ana uwezo, na arudishe kwa njia ya wakala; na yule asiye na uwezo, hahitajiki.

12 Na sasa ninasema juu ya waliosalia ambao watakuja katika nchi hii.

13 Tazama, wao wametumwa kuhubiri injili miongoni mwa mikutano ya waovu; kwa hiyo, ninawapa wao amri, kwamba: [a]Usipoteze muda wako bure, wala usizike [b]talanta yako ili isiweze kujulikana.

14 Na baada ya kuja katika nchi ya Sayuni, na kuwa umelitangaza neno langu, utarejea upesi, kulitangaza neno langu miongoni mwa mikutano ya waovu, siyo katika haraka, wala katika [a]ghadhabu wala mabishano.

15 Na kung'uta [a]vumbi la mi-

2c Mt. 25:14–30. MWM Hofu—Hofu ya mwanadamu.
3a Mk. 4:25; M&M 1:33.
4a Alma 43:50.
b Isa. 62:3; Zek. 9:16; Mal. 3:17; M&M 101:3.
7a MWM Utakatifu.
b MWM Samehe.
10a MWM Partridge, Edward.
13a M&M 42:42. MWM Mvivu, Uvivu.
b Mt. 25:24–30; M&M 82:18.
14a Mit. 14:29.
15a Mt. 10:14; Lk. 9:5; Mdo. 13:51; M&M 24:15; 75:20; 84:92.

guu yako dhidi ya wale wasiokupokea, siyo mbele yao, usije ukawaudhi, bali sirini; na uoshe miguu yako, kama ushuhuda dhidi yao katika siku ya hukumu.

16 Tazama, hii inatosha, na ni mapenzi ya yule aliyewatuma.

17 Na kwa kinywa cha mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, itajulikana juu ya Sidney Rigdon na Oliver Cowdery. Yaliyosalia baada ya hii. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 61

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, kwenye kingo ya Mto Missouri, sehemu ya McIlwaine's Bend, 12 Agosti 1831. Katika safari yao ya kurejea Kirtland, Nabii na wazee kumi walisafiri kwa mitumbwi katika Mto Missouri. Mnamo siku ya tatu ya safari yao, waliona hatari nyingi. Mzee William W. Phelps, katika ono la mchana, aliona mharibifu akitembea kwa nguvu juu ya uso wa maji.

1–12, Bwana ametangaza uangamiaji mkubwa juu ya maji; 13–22, Maji yalilaaniwa na Yohana, na mharibifu hutembea juu ya uso wake; 23–29, Wengine wana uwezo wa kuyaamuru maji; 30–35, Wazee wasafiri wawili wawili na kuhubiri injili; 36–39, Wanapaswa kujiandaa kwa ajili ya kuja kwake Mwana wa Mtu.

Tazama, na sikilizeni sauti yake yeye aliye na [a]uwezo wote, aliye tangu milele hata milele, [b]Alfa na Omega, mwanzo na mwisho.

2 Tazama, amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu, Enyi wazee wa kanisa langu, mliokusanyika mahali hapa, ninyi ambao dhambi zenu zimesamehewa sasa, kwani Mimi, Bwana, [a]husamehe dhambi, na ni mwenye [b]huruma kwa wale ambao [c]huziungama dhambi zao kwa moyo mnyenyekevu;

3 Lakini amini ninawaambia, kwamba haifai kwa kundi lote hili la wazee kusafiri kwa haraka juu ya maji, wakati wakazi wa pande zote mbili wanaangamia katika kutoamini.

4 Hata hivyo, niliruhusu ili kwamba muweze kushuhudia; tazama, kuna hatari nyingi juu ya maji, na hasa hapo baadaye;

5 Kwani Mimi, Bwana, nimetangaza katika hasira yangu maangamizi mengi juu ya maji; ndiyo, na hususani juu ya maji haya.

6 Hata hivyo, wenye mwili wako katika mikono yangu, na yule aliye mwaminifu miongoni mwenu hataangamia kwa maji.

7 Kwa hivyo, yafaa kuwa

61 1*a* MWM Uwezo.
b MWM Alfa na Omega.
2*a* Mos. 4:10–11.
MWM Samehe.
b MWM Rehema, enye Rehema.
c MWM Kiri, Kukiri.

mtumishi wangu Sidney Gilbert na mtumishi wangu [a]William W. Phelps wafanye haraka kwenda kwenye kazi yao na huduma yao.

8 Hata hivyo, nisingeliwaacha mtawanyike hadi muwe [a]nimewaadhibu kwa ajili ya dhambi zenu zote, ili mpate kuwa na umoja, ili msiweze kuangamia katika [b]uovu;

9 Lakini sasa, amini ninawaambia, ni muhimu kwangu kwamba yawapasa kutawanyika. Kwa hivyo watumishi wangu Sidney Gilbert na William W. Phelps waende na kundi lao la awali, na wafanye safari yao kwa haraka ili waweze kutimiza huduma yao, na kwa kupitia imani yao watashinda;

10 Na kwa kadiri watakavyokuwa waaminifu watalindwa, na Mimi, Bwana, nitakuwa pamoja nao.

11 Na waliosalia wachukue mavazi wanayohitaji.

12 Na mtumishi wangu Sidney Gilbert achukue yale yasiyohitajika pamoja naye, kama mtakavyokubaliana.

13 Na sasa, tazama, kwa [a]faida yenu nilitoa [b]amri kwenu juu ya mambo haya; na Mimi, Bwana, nitasemezana nanyi kama vile watu wa siku za kale.

14 Tazama, Mimi, Bwana, mwanzoni niliyabariki [a]maji; lakini katika siku za mwisho, kwa kinywa cha mtumishi wangu Yohana, [b]niliyalaani maji.

15 Kwa hiyo, siku zitakuja ambapo hakuna kiumbe kitakachokuwa salama juu ya maji.

16 Na itasemwa katika siku zijazo kwamba hakuna awezaye kwenda katika nchi ya Sayuni juu ya maji, ila yule aliye safi moyoni.

17 Na, kama vile Mimi, Bwana, mwanzoni [a]niliilaani ardhi, hata hivyo katika siku za mwisho nimeibariki, katika wakati wake, kwa ajili ya matumizi ya watakatifu wangu, ili waweze kushiriki unono wake.

18 Na sasa ninatoa kwenu amri kwamba lile nilisemalo kwa mmoja ninalisema kwa wote, kwamba mtawaonya ndugu zenu kuhusu maji haya, ili wasije wakasafiri katika maji haya, na imani yao itindike, nao wakanaswa katika mitego;

19 Mimi, Bwana, nimelitangaza na mwangamizaji anatembea juu ya uso wake, na Mimi sifuti tangazo hilo.

20 Mimi, Bwana, niliwakasirikia jana, lakini leo hasira yangu imegeuka.

21 Kwa hiyo, na wale ambao nimezungumza juu yao, kuwa wafunge safari zao upesi—na tena ninawaambia, wafunge safari zao upesi.

22 Na hii sijali, hata kama itakuwa baada ya kitambo kidogo, ili mradi wametimiza wajibu wao, iwe wamekwenda kwa njia ya maji au nchi kavu; na iwe kama inavyofahamika

7 *a* MWM Phelps, William W.
8 *a* MWM Rudi, Kurudiwa.
b MWM Ovu, Uovu.
13 *a* M&M 21:6.
b MWM Amri za Mungu.
14 *a* Mwa. 1:20.
b Ufu. 8:8–11.
17 *a* Musa 4:23.

kwao kulingana na maamuzi yao hapo baadaye.

23 Na sasa, kuhusu watumishi wangu, Sidney Rigdon, Joseph Smith, Mdogo, na Oliver Cowdery, wasije tena juu ya maji, isipokuwa iwe juu ya mfereji, wakati wakisafiri kwenda majumbani kwao; au katika maneno mengine hawatakuja juu ya maji kwa ajili ya kusafiri, isipokuwa juu ya mfereji.

24 Tazama, Mimi, Bwana, nimeonyesha njia kwa ajili ya kusafiri kwa watakatifu wangu; na tazama, hii ndiyo njia—kwamba baada ya kuondoka kwenye mfereji watasafiri kwa nchi, kadiri ya vile watakavyoamuriwa kusafiri na kuelekea kwenye nchi ya Sayuni;

25 Nao watafanya kama wana wa Israeli, *a*wakipiga mahema yao wakiwa njiani;

26 Na, tazama, amri hii mtaitoa kwa ndugu zenu wote.

27 Hata hivyo, kwa yule ambaye *a*uwezo umetolewa kwake kuyaamuru maji, kwake imetolewa kwa njia ya Roho kuzijua njia zake zote;

28 Kwa hiyo, na afanye vile Roho wa Mungu aliye hai anavyomwamuru, iwe juu ya nchi kavu au juu ya maji, kama ilivyobakia kwangu kufanya hapo baadaye.

29 Na kwenu ninyi imetolewa njia kwa ajili ya watakatifu, au njia kwa ajili ya watakatifu wa jeshi la Bwana, kusafiri.

30 Na tena, amini ninawaambia, watumishi wangu Sidney Rigdon, Joseph Smith, Mdogo, na Oliver Cowdery, hawatafungua vinywa vyao katika makusanyiko ya waovu hadi watakapofika huko Cincinnati;

31 Na katika mahali hapo watapaza sauti zao kwa Mungu dhidi ya watu wale, ndiyo, kwake yeye ambaye hasira yake inawaka dhidi ya uovu wao, watu ambao karibu *a*wameiva kwa angamizo.

32 Na kutoka hapo wasafiri kwenda kwenye mkutano wa ndugu zao, kwani kazi zao hata sasa zatakiwa sana miongoni mwao kuliko miongoni mwa makusanyiko ya waovu.

33 Na sasa, kuhusu waliosalia, nao wasafiri na *a*kulitangaza neno miongoni mwa mikutano ya waovu, kadiri vile itakavyotolewa;

34 Na kadiri watakavyofanya hivi watakuwa *a*wakiyaosha mavazi yao, nao watakuwa hawana waa mbele zangu.

35 Nao wasafiri pamoja, au *a*wawili wawili, kama waonavyo wao kuwa ni vyema, isipokuwa tu mtumishi wangu Reynolds Cahoon, na mtumishi wangu Samuel H. Smith, ambao ninapendezwa nao, wasitenganishwe hadi watakaporudi majumbani kwao, na hii

25*a* Hes. 9:18.
27*a* MWM Ukuhani; Uwezo.
31*a* Alma 37:31; Hel. 13:14; M&M 101:11.
33*a* MWM Hubiri; Shuhudia.
34*a* 2 Ne. 9:44; Yak. (KM) 2:2; Mos. 2:28.
35*a* MWM Kazi ya kimisionari.

ni kwa sababu ya hekima iliyo kwangu.

36 Na sasa, amini ninawaambia, na lile nisemalo kwa mmoja nasema kwa wote, muwe na furaha, [a]watoto wadogo; kwani mimi nipo [b]katikati yenu, na [c]sijawasahau;

37 Na kadiri mnavyojinyenyekeza wenyewe mbele zangu, baraka za [a]ufalme ni zenu.

38 Vifungeni viuno vyenu na muwe [a]waangalifu na kuwa na kiasi, mkitazamia kuja kwa Mwana wa Mtu, kwani yuaja katika saa msiodhania.

39 [a]Ombeni daima ili msije mkaingia [b]majaribuni, ili muweze kustahimili siku ya kuja kwake, iwe katika uzima au katika mauti. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 62

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, kwenye kingo za Mto Missouri huko Chariton, Missouri, 13 Agosti 1831. Siku hiyo, Nabii na kikundi chake, ambao walikuwa njiani wakitoka Independence kwenda Kirtland, walikutana na wazee kadha wa kadha waliokuwa njiani wakielekea zao katika nchi ya Sayuni, na, baada ya salamu za furaha, walipokea ufunuo huu.

1–3, Shuhuda zinaandikwa mbinguni; 4–9, Wazee wasafiri na kuhubiri kulingana na maamuzi yao na wanavyoelekezwa na Roho.

Tazama, na sikilizeni, Enyi wazee wa kanisa langu, asema Bwana Mungu wenu, hata Yesu Kristo, [a]mtetezi wenu, ajuaye udhaifu wa mwanadamu na namna ya [b]kuwasaidia wale [c]wanaojaribiwa.

2 Na amini macho yangu yawaangalia wale ambao bado hawajaenda katika nchi ya Sayuni; kwa sababu hiyo huduma zenu bado hazijatimizwa.

3 Hata hivyo, mmebarikiwa ninyi, kwani [a]shuhuda zenu mlizozitoa [b]zimeandikwa mbinguni ili malaika wazione; nao hufurahi juu yenu, na [c]dhambi zenu zimesamehewa.

4 Na sasa endeleeni na safari yenu. Jikusanyeni wenyewe juu ya nchi ya [a]Sayuni; na pangeni mkutano na kufurahi pamoja, na kutoa sakramenti kwa Aliye Juu Sana.

5 Na halafu mnaweza kurudi na kutoa ushuhuda, ndiyo, hata nyote kwa pamoja, au wawili wawili, kama mtakavyoona kuwa ni vyema, si kitu kwangu;

36*a* Yn. 13:33.
b Mt. 18:20.
c Isa. 41:15–17; 1 Ne. 21:14–15.
37*a* M&M 50:35.
38*a* mwm Kesha, Walinzi.
39*a* mwm Sala.
b mwm Jaribu, Majaribu.
62 1*a* M&M 45:3–4. mwm Mtetezi.
b Ebr. 2:18; Alma 7:12.
c mwm Jaribu, Majaribu.
3*a* Lk. 12:8–9. mwm Ushuhuda.
b mwm Kitabu cha Uzima.
c M&M 84:61.
4*a* M&M 57:1–2.

isipokuwa tu kuweni waaminifu, na [a]tangazeni habari njema kwa wakazi wa dunia, au miongoni mwa makusanyiko ya waovu.

6 Tazama, Mimi, Bwana, nimewaleta ninyi pamoja ili ahadi ipate kutimilika, kwamba waaminifu miongoni mwenu yapaswa walindwe na kufurahi pamoja katika nchi ya Missouri. Mimi, Bwana, huwaahidi waaminifu na siwezi [a]kuwadanganya.

7 Mimi, Bwana, niko radhi, kama mtu yeyote miongoni mwenu anataka kusafiri juu ya farasi, au juu ya nyumbu, au katika magari, atapokea baraka hizi, kama atapokea kutoka mkononi mwa Bwana, kwa moyo wa [a]shukrani katika mambo yote.

8 Mambo haya yanabakia kwenu kufanya sawa sawa na maamuzi yenu na maelekezo ya Roho.

9 Tazama, [a]ufalme ni wenu. Na tazama, na lo, mimi daima nipo [b]pamoja na waaminifu. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 63

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, mwishoni mwa 30 Agosti 1831. Nabii, Sidney Rigdon, na Oliver Cowdery waliwasili Kirtland 27 Agosti kutoka safari yao ya Missouri. Historia ya Joseph Smith inauelezea ufunuo huu: "Katika siku hizi za uchanga wa Kanisa, palikuwa na shauku kubwa ya kupata neno la Bwana juu ya kila jambo ambalo kwa namna yoyote ile lililohusu wokovu wetu; na kwa vile nchi ya Sayuni ilikuwa ndicho kitu kilicho kuwa cha maana zaidi usoni, nilimwomba Bwana taarifa zaidi juu ya kukusanyika kwa Watakatifu, na ya ununuzi wa ardhi, na mambo mengineyo."

1–6, Siku ya ghadhabu itafika juu ya waovu; 7–12, Ishara huja kwa imani; 13–19, Afanyaye uzinzi moyoni ataikana imani na atatupwa katika ziwa la moto; 20, Wale walio waaminifu watapokea wokovu juu ya dunia iliyobadilishwa; 21, Habari kamili ya matukio juu ya Mlima wa Kugeuka Sura bado hayajafunuliwa; 22–23, Watiifu hupokea siri za ufalme; 24–31, Urithi katika Sayuni utanunuliwa; 32–35, Bwana hutangaza vita, na waovu huwaua waovu; 36–48, Watakatifu watakusanyika Sayuni na watatoa fedha za kuijenga; 49–54, Waaminifu wamehakikishiwa baraka katika Ujio wa Pili, katika Ufufuko, na wakati wa Milenia; 55–58, Hii ni siku ya

5 *a* MWM Kazi ya kimisionari.
6 *a* Eth. 3:12.
7 *a* MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
9 *a* M&M 61:37.
b Mt. 28:20.

onyo; 59–66, Jina la Bwana latajwa bure na wale ambao hulitumia bila mamlaka.

Sikilizeni, Enyi watu, na funueni mioyo yenu na tegeni sikio kutoka mbali, na sikieni, ninyi mjiitao watu wa Bwana, na lisikizeni neno la Bwana na mapenzi yake juu yenu.

2 Ndiyo, amini, nawaambia, sikizeni neno lake yeye ambaye hasira yake inawaka dhidi ya waovu na [a]waasi;

3 Yeye apendaye kuwachukuwa hata wale atakao [a]kuwachukua, na kuwabakisha katika uhai wale apendao kuwabakisha;

4 Yeye ajengaye kwa mapenzi na ridhaa yake; na huharibu wakati atakao, na anaweza akaitupa nafsi jehanamu.

5 Tazama, Mimi, Bwana, naitoa sauti yangu, na mtaitii.

6 Kwa hiyo, amini ninasema, acha waovu wasikie, na waasi waogope na kutetemeka; acha wasioamini wafunge midomo yao, kwani [a]siku ya ghadhabu itawafikia kama [b]tufani, na wote wenye mwili [c]watajua kuwa Mimi ndimi Mungu.

7 Na yule atafutaye ishara ataziona [a]ishara, lakini siyo kwa wokovu.

8 Amini, ninawaambia, kuna watu miongoni mwenu ambao wanatafuta ishara, na wamekuwepo wa aina hiyo hata tangu mwanzo;

9 Lakini, tazama, imani haiji kwa ishara, bali ishara huwafuata wote wenye kuamini.

10 Ndiyo, ishara huja kwa [a]imani, siyo kwa matakwa ya wanadamu, wala siyo kama wapendavyo, bali kwa mapenzi ya Mungu.

11 Ndiyo, ishara huja kwa imani, kwa matendo makuu, kwani pasipo [a]imani hakuna mwanadamu awezaye kumpendeza Mungu; na kwa yule ambaye Mungu amemkasirikia hapendezwi naye; kwa hivyo, kwa watu wa aina hiyo haonyeshi ishara, isipokuwa katika [b]ghadhabu kwa [c]maangamizo yao.

12 Kwa hiyo, Mimi, Bwana, sijapendezwa na wale miongoni mwenu ambao walitafuta ishara na maajabu kwa ajili ya imani, na siyo kwa faida ya wanadamu kwa utukufu wangu.

13 Hata hivyo, nimetoa amri, na wengi wamegeuka kutoka kwenye amri zangu na hawakuzishika.

14 Palikuwa na [a]wazinzi miongoni mwenu; baadhi yao wamegeuka, na wengine wamebaki pamoja nanyi, ambao baada ya hapa watajulikana.

15 Wa aina hiyo wajihadhari na watubu upesi, hukumu isije ikawajia kama mtego, na upumbavu wao utafanywa dhahiri, na kazi za mikono yao zitawafuata machoni pa watu.

16 Na amini ninawaaambia,

63 2*a* mwm Uasi.
3*a* mwm Mauti ya Kimwili.
6*a* mwm Haki, Uadilifu, enye Uadilifu; Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b Yer. 30:23.
c Isa. 49:26.
7*a* M&M 46:9.
mwm Ishara.
10*a* Moro. 7:37.
mwm Amini, Imani.
11*a* Ebr. 11:6.
b M&M 35:11.
c M&M 88:65.
14*a* M&M 42:24–25.

kama nilivyosema hapo awali, mtu [a]amtazamaye mwanamke kwa [b]kumtamani, au kama wale watakaofanya [c]uzinzi mioyoni mwao, hawatakuwa na Roho, bali wataikana imani na wataogopa.

17 Kwa hiyo, Mimi, Bwana, nimesema kuwa [a]waoga, na wasioamini, na [b]waongo wote, na yeyote apendaye uongo na [c]kuufanya, na wazinzi, na wachawi, watakuwa na sehemu yao katika [d]ziwa lile liwakalo moto na kiberiti ambacho ni [e]kifo cha pili.

18 Amini ninasena, kwamba hawatakuwa na sehemu katika [a]ufufuko wa kwanza.

19 Na sasa tazama, Mimi, Bwana, ninawaambia kwamba [a]hamjahesabiwa haki, kwani mambo haya yapo miongoni mwenu.

20 Hata hivyo, yule [a]astahimiliye katika imani na kutimiza mapenzi yangu, huyo atashinda, na kupokea [b]urithi juu ya dunia wakati siku ya kugeuka sura itakapofika;

21 Wakati [a]dunia [b]itakapogeuzwa sura, hata sawasawa na utaratibu ulioonyeshwa kwa mitume wangu juu ya [c]mlima; habari ambazo utimilifu wake hamjapokea.

22 Na sasa, amini ninawaambia, kama nilivyosema kuwa nitawajulisha matakwa yangu, tazama nitawajulisha, siyo kwa njia ya amri, kwa kuwa wapo wengi wasiojali kuzishika amri zangu.

23 Lakini kwake yeye ashikaye amri zangu nitampa [a]siri za ufalme wangu, na ndani yake patakuwa na chemchemi ya [b]maji ya uzima, [c]yakibubujikia kwenye uzima usio na mwisho.

24 Na sasa, tazama, haya ndiyo mapenzi ya Bwana Mungu wenu kuhusu watakatifu wake, kwamba wanapaswa kujikusanya pamoja katika nchi ya Sayuni, siyo katika haraka, pasije kuwa na mchafuko, uletao mateso.

25 Tazama, nchi ya [a]Sayuni—Mimi, Bwana, ninaishika katika mikono yangu;

26 Hata hivyo, Mimi, Bwana, hutoa kwa [a]Kaisari vitu vilivyo vya Kaisari.

27 Kwa hivyo, Mimi, Bwana, ninataka kuwa mnunue ardhi, ili muweze kuyashinda ya ulimwengu, ili muweze kuwa na haki kwa walimwengu, ili wasichochewe kwa hasira.

16*a* Mt. 5:27–28; M&M 42:23–26.
b MWM Tamaa mbaya.
c MWM Uzinzi.
17*a* Ufu. 21:8.
b MWM Kusema uongo.
c Ufu. 22:15; M&M 76:103.
d Ufu. 19:20; 2 Ne. 9:8–19, 26; 28:23; Yak. (KM) 6:10; Alma 12:16–18; M&M 76:36.
MWM Jehanamu.
e MWM Mauti ya Kiroho.
18*a* Ufu. 20:6.
19*a* MWM Hesabu kwa haki, Kuhesabiwa haki.
20*a* M&M 101:35.
b Mt. 5:5; M&M 59:2; 88:25–26.
21*a* MWM Dunia—Hali ya mwisho ya dunia.
b MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.
c Mt. 17:1–3.
23*a* Alma 12:9–11; M&M 42:61; 84:19; 107:18–19.
b MWM Maji ya Uzima.
c Yn. 4:14.
25*a* MWM Sayuni.
26*a* Lk. 20:25; M&M 58:21–23.
MWM Utawala.

28 Kwani [a]Shetani huiweka katika mioyo yao ili wakasirike dhidi yenu, kiasi cha umwagaji damu.

29 Kwa hivyo, nchi ya Sayuni haitapatikana ila kwa kununua au kwa damu, vinginevyo hakuna urithi wowote kwa ajili yenu.

30 Na kama ni kwa kununua, tazama mmebarikiwa;

31 Na kama ni kwa damu, ninyi mmezuiliwa kumwaga damu, lo, adui zenu wapo juu yenu, na mtafukuzwa kutoka mji hadi mji, na kutoka sinagogi hadi sinagogi, na ni wachache tu watakaosimama na kupokea urithi.

32 Mimi, Bwana, ninakasirishwa na waovu; ninaizuia Roho yangu kwa wakazi wa dunia.

33 Nimeapa katika ghadhabu yangu, na kutangaza [a]vita juu ya uso wa dunia, na waovu watachinja waovu, na woga utakuja juu ya kila mwanadamu;

34 Na [a]watakatifu pia kwa shida wataepuka; hata hivyo, Mimi, Bwana, niko pamoja nao, nami [b]nitashuka kutoka mbinguni kwenye uwepo wa Baba yangu na [c]kuwaangamiza waovu kwa [d]moto usiozimika.

35 Na tazama, hili bado, lakini li karibu.

36 Kwa hiyo, kwa kuona hivyo, Mimi, Bwana, nikatangaza mambo haya yote juu ya uso wa dunia, ninataka kwamba watakatifu wangu wakusanyike katika nchi ya Sayuni;

37 Na kwamba kila mtu ajichukulie [a]haki katika mikono yake na uaminifu viunoni mwake, na kupaza [b]sauti ya kuonya kwa wakazi wa dunia; na kutangaza kwa maneno na kwa kukimbia kwamba [c]ukiwa utawapata waovu.

38 Kwa hiyo, na wanafunzi wangu katika Kirtland wapange mambo yao ya maisha, wale waishio kwenye shamba hili.

39 Na mtumishi wangu Titus Billings, ambaye ni msimamizi wake, aitoe ardhi, ili aweze kujiandaa katika majira ya kuchipua yajayo kwa kuanza safari yake kuja katika nchi ya Sayuni, pamoja na wale wakaao hapo, isipokuwa wale nitakaowabakisha kwa makusudi yangu, ambao hawatakwenda hadi nitakapowaamuru.

40 Na fedha zote zinazoweza kutunzwa, wala sitajali kama zitakuwa nyingi au kidogo zipelekwe katika nchi ya Sayuni, kwao wale niliowateua kuzipokea.

41 Tazama, Mimi, Bwana, nitatoa kwa mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, uwezo ambao utamwezesha [a]kutambua kwa uwezo wa Roho wale watakaokwenda katika nchi ya Sayuni, na wale wanafunzi wangu ambao watabaki.

28 *a* MWM Ibilisi.
33 *a* MWM Vita.
34 *a* MWM Mtakatifu.
b MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
c Mt. 3:12; 2 Ne. 26:6; M&M 45:57; 64:24; 101:23–25, 66.
d MWM Moto.
37 *a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
b M&M 1:4.
c Isa. 47:11.
41 *a* MWM Utambuzi, Kipawa cha.

42 Na mtumishi wangu Newel K. Knight abaki na stoo yake, au kwa maneno mengine, duka, kwa muda mfupi ujao.

43 Hata hivyo, naye atoe fedha zote ambazo anaweza kutoa, ili zipelekwe katika nchi ya Sayuni.

44 Tazama, mambo haya yapo mikononi mwake mwenyewe, na afanye kulingana na hekima.

45 Amini ninawaambia, na atawazwe kama wakala kwa wanafunzi wangu wale watakaobaki na atawazwe katika uwezo huu;

46 Na sasa upesi ukayatembelee makanisa, ukayaelezea mambo haya kwao, pamoja na mtumishi wangu Oliver Cowdery. Tazama, hilo ndilo penzi langu, kupata fedha hata kama vile nilivyoelezea.

47 Yule aliye [a]mwaminifu na mwenye kustahimili ataushinda ulimwengu.

48 Yule ambaye hupeleka hazina katika nchi ya Sayuni atapokea [a]urithi katika ulimwengu huu, na matendo yake yatamfuata, na pia thawabu katika ulimwengu ujao.

49 Ndiyo, na heri wafu [a]wafao katika Bwana, tangu sasa, wakati Bwana atakapokuja, na mambo ya zamani [b]yatapita, na mambo yote yamekuwa mapya, [c]watafufuka kutoka kwa wafu na [d]hawatakufa tena, na watapokea urithi mbele za Bwana, katika mji mtakatifu.

50 Na yule atakayekuwa hai wakati Bwana atakapokuja, na akiwa ameishika imani, [a]amebarikiwa; hata hivyo, imepangwa kwake [b]kufa katika umri wa mwanadamu.

51 Kwa hiyo, watoto [a]watakua hadi wamekuwa wazee; na wazee watakufa, bali hawatalala katika mavumbi, bali [b]watageuzwa katika muda wa kufumba na kufumbua jicho.

52 Kwa hiyo, kwa sababu hii mitume walihubiri kwa walimwengu juu ya ufufuko wa wafu.

53 Mambo hayo ni mambo ambayo ni lazima myatazamie; na, nikisema kulingana na njia ya Bwana, sasa yapo [a]karibu, na katika wakati ujao, hata katika siku ya kuja kwa Mwana wa Mtu.

54 Na hadi saa hiyo patakuwa na [a]wanawali wajinga miongoni mwa wenye hekima; na katika saa hiyo waja utengano mkamilifu wa wenye haki na waovu; na katika siku hiyo nitawatuma malaika wangu [b]kuwaondoa waovu na kuwatupa katika moto usiozimika.

55 Na sasa tazama, amini

47 *a* Mos. 2:41; M&M 6:13.
48 *a* M&M 101:18.
49 *a* Ufu. 14:13; M&M 42:44–47.
b 2 Kor. 5:17.
c MWM Ufufuko.
d Ufu. 21:4; Alma 11:45; M&M 88:116.
MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
50 *a* MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
b MWM Mauti ya Kimwili.
51 *a* Isa. 65:20–22; M&M 45:58; 101:29–31.
MWM Milenia.
b 1 Kor. 15:51–52; M&M 43:32.
53 *a* M&M 35:15.
54 *a* Mt. 25:1–13; M&M 45:56–59.
b Mos. 16:2.

ninawaambia, Mimi, Bwana, sijapendezwa na mtumishi wangu [a]Sidney Rigdon; [b]amejiinua mwenyewe moyoni mwake, na hakupokea ushauri, bali amemhuzunisha Roho;

56 Kwa hiyo [a]maandishi yake hayakubaliki kwa Bwana, na atafanya mengine; na ikiwa Bwana hatayapokea, tazama yeye hatasimama katika ofisi ambayo nimemteua.

57 Na tena, amini ninawaambia, [a]wale watamanio katika mioyo yao, kwa unyenyekevu, [b]kuwaonya wenye dhambi ili watubu, na watawazwe katika uwezo huo.

58 Kwani hii ni siku ya kuonya, na siyo siku ya maneno mengi. Kwani Mimi, Bwana siyo wa kudhihakiwa katika siku ya mwisho.

59 Tazama, Mimi ni wa juu, na uwezo wangu uko hata chini yake. Mimi ni juu ya vyote, na katika yote, na ndani ya yote na [a]yatafuteni mambo yote, na siku yaja ambayo mambo yote yatafanywa kuwa chini yangu.

60 Tazama, Mimi ni [a]Alfa na Omega, hata Yesu Kristo.

61 Kwa hiyo, na watu wote wajihadhari namna walichukuavyo [a]jina langu katika midomo yao—

62 Kwani tazama, amini ninasema, kuwa wapo wengi chini ya hatia hii, ambao hulitaja jina la Bwana, na hulitaja bure, bila mamlaka.

63 Kwa hiyo, na kanisa litubu dhambi zake, na Mimi, Bwana, nitawamiliki; vinginevyo, watakatiliwa mbali.

64 Kumbukeni kwamba kile ambacho huja kutoka juu ni [a]kitakatifu, na ni lazima [b]kitamkwe kwa uangalifu, na kwa ridhaa ya Roho; na katika hili hakuna hatia, nanyi mnampokea Roho kwa [c]njia ya sala; kwa hiyo, bila hivyo hubakia hatia.

65 Na watumishi wangu, Joseph Smith, Mdogo, na Sidney Rigdon, wajitafutie nyumba, kama watakavyofundishwa na Roho kwa njia ya [a]sala.

66 Mambo haya mtayashinda kwa njia ya uvumilivu, ili watakaoshinda waweze kupokea [a]utukufu wa milele [b]uzidio kuwa mwingi sana, vinginevyo, hukumu kuu. Amina.

SEHEMU YA 64

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa wazee wa Kanisa, huko Kirtland, Ohio, 11 Septemba 1831. Nabii alikuwa akijiandaa kwenda Hiram, Ohio, kuanza tena kazi yake ya kutafsiri

55 *a* MWM Rigdon, Sidney.
b MWM Kiburi.
56 *a* M&M 58:50.
57 *a* M&M 4:3–6.
b M&M 18:14–15.
MWM Kazi ya kimisionari; Onya, Onyo.
59 *a* 1 Kor. 2:10.
60 *a* MWM Alfa na Omega.
61 *a* MWM Lugha chafu.
64 *a* MWM Takatifu.
b MWM Uchaji.
c M&M 42:14.
65 *a* MWM Sala.
66 *a* Rum. 8:18; M&M 58:4; 136:31.
b 2 Kor. 4:17.

Biblia, ambayo iliwekwa pembeni wakati alipokuwa Missouri. Kikundi cha ndugu ambao walikuwa wameamriwa kusafiri kwenda Sayuni (Missouri) walikuwa wamejishughulisha katika kufanya maandalizi ya kuhama mwezi wa Oktoba. Katika wakati huu wa shughuli nyingi, ufunuo huu ulipokelewa.

1–11, Watakatifu wanaamriwa kusameheana, isije dhambi kubwa ikabaki kwao; 12–22, Wasiotubu wataletwa mbele ya Kanisa; 23–25, Yule ambaye amelipa zaka hataunguzwa wakati Bwana ajapo; 26–32, Watakatifu waonywa kuepuka madeni; 33–36, Waasi watatupwa nje ya Sayuni; 37–40, Kanisa litayahukumu mataifa; 41–43, Sayuni itastawi.

Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu wenu kwenu, Enyi wazee wa kanisa langu, sikilizeni na sikieni, na yapokeeni mapenzi yangu juu yenu.

2 Kwani amini ninawaambia, kuwa nataka kwamba [a]muushinde ulimwengu; kwa hiyo nitakuwa na [b]huruma juu yenu.

3 Wapo watu miongoni mwenu ambao wametenda dhambi; lakini amini ninawaambia, kwa mara hii moja, kwa ajili ya [a]utukufu wangu mwenyewe, na kwa ajili ya wokovu wa nafsi, [b]nimewasamehe dhambi zenu.

4 Nitakuwa mwenye huruma kwenu, kwani nimewapa ufalme.

5 Na [a]funguo za siri za ufalme hazitachukuliwa kutoka kwa mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, kwa njia niliyoteua, wakati akiwa hai, kadiri yeye atakavyotii [b]ibada zangu.

6 Kuna wale ambao wametafuta kupata sababu za kumshtaki bila sababu;

7 Hata hivyo, yeye ametenda dhambi; lakini amini ninawaambia, Mimi, Bwana, [a]husamehe dhambi kwa wale wenye [b]kuungama dhambi zao mbele zangu na kuomba msamaha, wale ambao hawakutenda dhambi ya [c]mauti.

8 Wanafunzi wangu, katika siku za kale, walitafuta [a]makosa kati yao na wala hawakusameheana katika mioyo yao; na kwa uovu huu walipata mateso na [b]kuadhibiwa vikali.

9 Kwa hiyo, ninawaambia, kwamba mnapaswa [a]kusameheana ninyi kwa ninyi; kwani yule [b]asiyemsamehe ndugu yake makosa yake husimama na hatia mbele za Bwana; kwa kuwa ndani yake imebaki dhambi kubwa.

10 Mimi, Bwana, [a]nitamsamehe yule nitakaye kumsamehe,

64 2*a* 1 Yoh. 5:4.
b mwm Huruma.
3*a* Musa 1:39.
b Isa. 43:25.
5*a* M&M 28:7; 84:19.
mwm Funguo za Ukuhani.
b mwm Ibada.
7*a* mwm Ondoleo la Dhambi; Samehe.
b Hes. 5:6–7; M&M 19:20; 58:43.
mwm Kiri, Kukiri.
c M&M 76:31–37.
8*a* mwm Ushindani.
b mwm Rudi, Kurudiwa.
9*a* Mk. 11:25–26; M&M 82:1.
b Mt. 6:14–15; Efe. 4:32.
10*a* Ku. 33:19; Alma 39:6; M&M 56:14.

lakini ninyi mnatakiwa [b]kuwasamehe watu wote.

11 Nanyi mnapaswa kusema mioyoni mwenu—Mungu na [a]ahukumu kati ya mimi na wewe, na akulipe sawasawa na [b]matendo yako.

12 Na yule asiyetubu dhambi zake, na hazikiri, mtamleta mbele ya [a]kanisa, na mtamfanya kama maandiko yanavyowaambia iwe kwa amri au kwa ufunuo.

13 Na hili mtalifanya ili Mungu aweze kutukuzwa—siyo kwa sababu ninyi hamsamehi, hamna huruma, bali kwamba ninyi msiwe na hatia machoni pa sheria, ili msimkosee yeye ambaye ni mtunga sheria wenu—

14 Amini ninasema, kwa sababu hii mtafanya mambo haya.

15 Tazama, Mimi, Bwana, nilikasirishwa na yule aliyekuwa mtumishi wangu Ezra Booth, na pia mtumishi wangu Isaac Morley, kwa kuwa hawakuishika sheria, wala amri;

16 Walitafuta ubaya katika mioyo yao, na Mimi, Bwana, nilimzuia Roho wangu. [a]Walishutumu kwa uovu jambo ambalo ndani yake hapakuwa na uovu; hata hivyo nimemsamehe mtumishi wangu Isaac Morley.

17 Na pia mtumishi wangu [a]Edward Partridge, tazama, ametenda dhambi, na [b]Shetani anatafuta kuangamiza roho yake; lakini wakati mambo haya yatakapokuwa yamejulikana kwao, nao wakatubu uovu wao, watasamehewa.

18 Na sasa, amini ninasema kwamba ninaona ni muhimu kuwa mtumishi wangu Sidney Gilbert, baada ya wiki chache, arejee katika shughuli zake, na kwenye uwakala wake katika nchi ya Sayuni;

19 Na kile alichokiona na kusikia anaweza kuwajulisha wanafunzi wangu, ili wasiangamie. Na ni kwa sababu hii nimeyasema mambo haya.

20 Na tena, ninawaambia, kuwa mtumishi wangu Isaac Morley [a]asijaribiwe kupita awezavyo, na kutoa ushauri potofu utakaowaumiza, nilitoa amri kuwa shamba lake liuzwe.

21 Sitaki mtumishi wangu Frederick G. Williams auze shamba lake, kwani Mimi, Bwana, ninataka kupaimarisha mahali hapa katika nchi ya Kirtland, kwa kipindi cha miaka mitano, kipindi ambacho sitawaangusha waovu, ili kwamba kwa njia hii niweze kuwakomboa baadhi yao.

22 Na baada ya siku hiyo, Mimi, Bwana, sitamshika na [a]hatia yeyote ambaye atakwenda na moyo uliofunguka katika nchi ya Sayuni; kwa kuwa Mimi, Bwana, ninaitaka [b]mioyo ya wanadamu.

10 *b* Mos. 26:29–31.
11 *a* 1 Sam. 24:12.
b 2 Tim. 4:14.
12 *a* M&M 42:80–93.
16 *a* 2 Ne. 15:20; M&M 121:16.
17 *a* MWM Partridge, Edward.
b MWM Ibilisi.
20 *a* MWM Jaribu, Majaribu.
22 *a* MWM Hatia.
b Ku. 35:5; M&M 59:15; 64:34.

23 Tazama, sasa inaitwa [a]leo hadi [b]kuja kwa Mwana wa Mtu, na hakika ni siku ya [c]kujitoa dhabihu, na siku ya watu wangu kulipa zaka; kwani yule ambaye [d]analipa zaka [e]hataunguzwa moto wakati wa kuja kwake.

24 Kwani baada ya leo kwaja [a]kuungua—hii nikiongea kwa jinsi ya Bwana—kwani amini ninasema, kesho wote wenye [b]kiburi na wote watendao uovu watakuwa makapi; na Mimi nitawachoma, kwani Mimi ndimi Bwana wa Majeshi; na sitamwacha yeyote ambaye atabaki katika [c]Babilonia.

25 Kwa hiyo, kama mnaniamini Mimi, mtafanya kazi wakati ingali inaitwa leo.

26 Na siyo vyema kwamba watumishi wangu [a]Newel K. Whitney na Sidney Gilbert, wauze [b]maduka yao na mali zao hapa; kwa kuwa hiyo siyo hekima hadi mabaki ya kanisa, ambayo yamebakia mahali hapa, watakapokwenda katika nchi ya Sayuni.

27 Tazama, inasemekana katika sheria zangu, au umekatazwa, kujiingiza katika [a]deni kwa maadui zako;

28 Lakini tazama, haijasemwa wakati wowote kwamba Bwana hatachukua wakati atakao, na kulipa wakati aonavyo yeye kuwa ni vyema.

29 Kwa hiyo, ninyi mkiwa kama mawakala, mpo katika utumishi wa Bwana; na lolote mfanyalo sawasawa na mapenzi ya Bwana ni kazi ya Bwana.

30 Na amewaweka ninyi kuwahudumia watakatifu wake katika siku hizi za mwisho, ili waweze kujipatia [a]urithi katika nchi ya Sayuni.

31 Na tazama, Mimi, Bwana, ninawatangazia, na [a]maneno yangu ni hakika na hayatakuwa [b]bure, kwamba watapata.

32 Lakini mambo yote lazima yatakuja kutimia katika wakati wake.

33 Kwa hiyo, [a]msichoke kutenda mema, kwa kuwa mnaijenga misingi ya kazi kubwa. Na kutokana na [b]mambo madogo huja yale yaliyo makuu.

34 Tazama, Bwana [a]anahitaji [b]moyo na akili yenye kukubali, na wenye kukubali na [c]kutii watakula mema ya Sayuni katika siku za mwisho.

35 Na [a]waasi [b]watakatiliwa mbali kutoka nchi ya Sayuni, na

23 *a* M&M 45:6; 64:24–25.
b MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
c MWM Dhabihu.
d Mal. 3:10–11.
MWM Lipa zaka, Zaka.
e Mal. 4:1; 3 Ne. 25:1; JS—H 1:37.
24 *a* Isa. 66:15–16.
MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia; Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.
b Mal. 3:15; 2 Ne. 12:12; 23:11.
MWM Kiburi.
c M&M 1:16.
MWM Babeli, Babilonia.
26 *a* MWM Whitney, Newel K.
b M&M 57:8.
27 *a* MWM Deni.
30 *a* M&M 63:48.
31 *a* Mk. 13:31; 2 Ne. 31:15; M&M 1:37–38.
b M&M 76:3.
33 *a* Gal. 6:9.
b M&M 123:16.
34 *a* Mik. 6:8.
b Kum. 32:46; Yos. 22:5; Morm. 9:27.
MWM Moyo.
c Isa. 1:19.
MWM Mtiifu, Tii, Utii.
35 *a* MWM Uasi.
b M&M 41:5; 50:8–9; 56:3.
MWM Kutengwa na Kanisa.

watapelekwa mbali na hawatairithi nchi.

36 Kwani, amini ninawaambia, kwamba waasi siyo wa damu ya [a]Efraimu, kwa hiyo wataondoshwa.

37 Tazama, Mimi, Bwana, nimelifanya kanisa langu katika siku hizi za mwisho kuwa kama mwamuzi aliyekaa juu ya mlima, au katika mahali pa juu, kuwahukumu mataifa.

38 Kwani itakuwa kwamba wakazi wa Sayuni [a]watahukumu mambo yote yahusuyo Sayuni.

39 Na waongo na wanafiki watadhihirishwa na wao, na wale wasio [a]mitume na manabii watajulikana.

40 Na hata [a]askofu, ambaye ni [b]mwamuzi na washauri wake, ikiwa siyo waaminifu katika [c]usimamizi wao watahukumiwa, na [d]wengine watapandwa badala yao.

41 Kwani, tazama, ninawaambia ninyi kwamba [a]Sayuni itastawi, na [b]utukufu wa Bwana utakuwa juu yake;

42 Naye atakuwa [a]bendera kwa watu, na hapo watakuja kutoka kila taifa chini ya mbingu.

43 Na siku itakuja ambayo mataifa ya dunia [a]yatatetemeka kwa sababu yake, na wataogopa kwa sababu ya wingi wao watishao. Bwana amesema hili. Amina.

SEHEMU YA 65

Ufunuo juu ya sala uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Hiram, Ohio, 30 Oktoba 1831.

1–2, Funguo za ufalme wa Mungu zakabidhiwa kwa mwanadamu duniani, na kazi ya injili itashinda; 3–6, Ufalme wa mbinguni wa milenia utakuja na kuungana na ufalme wa Mungu wa duniani.

Sikilizeni, na lo, sauti ya mtu kama aliyetumwa kutoka juu, mwenye uwezo na mwenye nguvu, ambaye kutoka kwake ni hata mwisho wa dunia, ndiyo, ambaye sauti yake yaenda kwa wanadamu—[a]Itengenezeni njia ya Bwana, yanyoosheni mapito yake.

2 [a]Funguo za [b]ufalme wa Mungu zakabidhiwa kwa mwanadamu duniani, na kutoka huko injili itaenea hata miisho ya dunia,

36*a* Kum. 33:16–17.
38*a* Isa. 2:3–4; M&M 133:21.
39*a* Ufu. 2:2. MWM Mtume.
40*a* MWM Askofu.
b M&M 58:17; 107:72–74.
c MWM Msimamizi, Usimamizi.
d M&M 107:99–100.
41*a* MWM Sayuni.
b M&M 45:67; 84:4–5; 97:15–20. MWM Utukufu.
42*a* MWM Bendera.
43*a* Isa. 60:14; M&M 97:19–20.

65 1*a* Isa. 40:3; Mt. 3:3; Yn. 1:23.
2*a* Mt. 16:19; M&M 42:69. MWM Funguo za Ukuhani.
b M&M 90:1–5.

kama vile [c]jiwe lililochongwa mlimani bila kazi ya mikono litabiringika, hadi [d]litaijaza dunia yote.

3 Ndiyo, sauti iliayo—Itengenezeni njia ya Bwana, andaeni [a]karamu ya Mwanakondoo, kuweni tayari kwa ajili ya [b]Bwana Harusi.

4 Ombeni kwa Bwana, mlilingane jina lake takatifu, wajulisheni watu matendo yake ya ajabu.

5 Mlinganeni Bwana, ili ufalme wake uweze kuenea juu ya dunia, ili wakazi wake waweze kuupokea, na kujitayarisha kwa ajili ya siku zijazo, siku ambazo Mwana wa Mtu [a]atashuka kutoka mbinguni, [b]aliyevikwa katika mng'aro wa [c]utukufu wake, kukutana na [d]ufalme wa Mungu ambao umewekwa duniani.

6 Kwa hiyo, na [a]ufalme wa Mungu uenee, ili [b]ufalme wa mbinguni uweze kuja, ili wewe, Ee Mungu uweze kutukuzwa mbinguni hata na duniani, ili adui zako waweze kushindwa; kwa kuwa ukuu ni [c]wako, uwezo na utukufu, milele na milele. Amina.

SEHEMU YA 66

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Hiram, Ohio, 29 Oktoba 1831. William E. McLellin alimwomba Bwana kwa siri kumjulisha kupitia kwa Nabii jibu kwa maswali matano, ambayo hayakuwa yamejulikana kwa Joseph Smith. Kwa ombi la McLellin Nabii alimwuliza Bwana na akapokea ufunuo huu.

1–4, Agano lisilo na mwisho ndiyo utimilifu wa injili; 5–8, Wazee wafundishe, washuhudie, na kusemezana na watu; 9–13, Huduma ya utumishi wa uaminifu humhakikishia urithi wa uzima wa milele.

Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwa mtumishi wangu William E. McLellin—Heri wewe, kwa kuwa umegeuka na kuacha uovu wako, na umepokea ukweli wangu, asema Bwana Mkombozi wako, Mwokozi wa ulimwengu, hata wengi kama [a]wataliamini jina langu.

2 Amini ninakuambia, heri wewe kwa kuwa umepokea [a]agano langu lisilo na mwisho, hata utimilifu wa injili yangu, iliyotolewa kwa wanadamu, ili wawe na [b]uzima na kufanywa kuwa washiriki wa utukufu

2 *c* Dan. 2:34–45.
d Zab. 72:19.
MWM Danieli—Kitabu cha Danieli; Siku za Mwisho.
3 *a* Mt. 22:1–14; Ufu. 19:9; M&M 58:11.
b MWM Bwana Harusi.
5 *a* Mt. 24:30.
b Zab. 93:1.
c MWM Utukufu.
d Dan. 2:44.
6 *a* MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
b Ufu. 11:15.
c 1 Nya. 29:11; Mt. 6:13.
66 1 *a* Yn. 1:12.
MWM Amini, Imani.
2 *a* MWM Agano Jipya na Lisilo na Mwisho.
b Yn. 10:10; 3 Ne. 5:13.

ambao utafunuliwa katika siku za mwisho, kama vile ilivyoandikwa na manabii na mitume katika siku za kale.

3 Amini ninakuambia, mtumishi wangu William, kwamba wewe u safi, lakini siyo kabisa; tubu mambo yale ambayo hayapendezi machoni mwangu, asema Bwana, kwani Bwana [a]atayaonyesha kwako.

4 Na sasa, amini, Mimi, Bwana, nitakuonyesha mapenzi yangu juu yako, au mapenzi yangu ni nini juu yako.

5 Tazama, amini ninakuambia, kuwa ni mapenzi yangu kuwa [a]utangaze injili yangu kutoka nchi hadi nchi, na kutoka mji hadi mji, ndiyo, katika maeneo ya karibu mahali ambako haijatangazwa.

6 Usikae siku nyingi mahali hapa; bado usiende kwenye nchi ya Sayuni; lakini kadiri unavyoweza kutuma, tuma; vinginevyo usiifikirie mali yako.

7 [a]Nenda nchi za mashariki, toa [b]ushuhuda kila mahali, kwa watu wote na katika masinagogi yao, na ukisemezana na watu.

8 Na mtumishi wangu Samuel H. Smith aende pamoja na wewe, na wala usimwache, na umpe maelekezo; na yule aliye mwaminifu atafanywa kuwa [a]imara kila mahali; na Mimi, Bwana, nitakwenda pamoja nawe.

9 Weka [a]mikono yako juu ya wagonjwa, nao [b]watapona. Usirudi hadi Mimi, Bwana, nitakapokutuma. Uwe mvumilivu katika mateso. [c]Omba nawe utapata; bisha, nawe utafunguliwa.

10 Usitafute kujihangaisha. Acha uovu wote. [a]Usizini—jaribu ambalo limekuwa likikutatiza.

11 [a]Shika maneno haya, kwani ni ya kweli na kuaminika; nawe uitukuze huduma iliyo yako, na wasukume watu wengi kwenda [b]Sayuni [c]wakiimba na shangwe isiyo na mwisho itakuwa juu ya vichwa vyao.

12 [a]Uendelee katika mambo haya hata mwisho, nawe utapata [b]taji la uzima wa milele katika mkono wa kuume wa Baba yangu, ambaye amejaa neema na ukweli.

13 Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana [a]Mungu wako, Mkombozi wako, hata Yesu Kristo. Amina.

3 *a* Yak. (KM) 4:7; Eth. 12:27.
5 *a* Mk. 16:15.
7 *a* M&M 75:6.
b MWM Ushuhuda.
8 *a* M&M 52:17; 133:58.
9 *a* MWM Huduma kwa Wagonjwa; Mikono, Kuweka juu ya.
b Mt. 9:18. MWM Ponya, Uponyaji.
c Yak. (Bib.) 1:5.
10 *a* MWM Uzinzi.
11 *a* M&M 35:24.
b M&M 11:6.
c Isa. 35:10; M&M 45:71. MWM Imba.
12 *a* 2 Tim. 3:14–15; 2 Ne. 31:20.
b Isa. 62:3; Mt. 25:21; 1 Pet. 5:4.
13 *a* MWM Mungu, Uungu—Mungu Mwana.

SEHEMU YA 67

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Hiram, Ohio, mapema Novemba 1831. Tukio lilikuwa la mkutano maalumu, na uchapishaji wa mafunuo ambayo yalikuwa tayari yamepokelewa kutoka kwa Bwana kupitia nabii yalijadiliwa na kutendewa kazi (ona kichwa cha habari cha sehemu ya 1). William W. Phelps alikuwa hivi karibuni ameanzisha kiwanda cha kupiga chapa katika Independence, Missouri. Mkutano uliamua kuchapisha mafunuo katika Book of Commandments (Kitabu cha Amri) na kupiga chapa nakala 10,000 (ambazo kwa sababu ya ugumu usio tarajiwa baadae zilipunguzwa na kuwa nakala 3000). Ndugu wengi wanatoa ushuhuda wa dhati kwamba mafunuo hayo ambayo yalikusanywa kwa ajili ya kuchapishwa yalikuwa ya kweli kabisa, kama vile Roho Mtakatifu alivyowashuhudia alipomwagwa juu yao. Historia ya Joseph Smith inaandika kuwa baada ya ufunuo unaojulikana kama sehemu ya 1 kupokelewa, maoni tofauti yalikuwepo kuhusu lugha iliyotumika katika mafunuo hayo. Ufunuo huu ulifuata.

1–3, Bwana husikiliza sala za wazee Wake na kuwaangalia; 4–9, Yeye anatoa changamoto kwa mwenye hekima kutoa japo ufunuo mmoja sawa na ufunuo mmoja mdogo kati ya mafunuo Yake; 10–14, Wazee waaminifu watahuishwa na Roho na watauona uso wa Mungu.

TAZAMA na sikilizeni, Enyi [a]wazee wa kanisa langu, ambao mmejikusanya pamoja, ambao sala zenu nimezisikia, na ambao mioyo yenu ninaijua, na ambao matakwa yenu yamepanda juu mbele zangu.

2 Tazama, na lo, [a]macho yangu yapo juu yenu, na mbingu na dunia zipo mikononi mwangu, na utajiri wa milele ni juu yangu kuutoa.

3 Mlijitahidi kuamini kuwa yawapasa kupokea baraka ambazo zilitolewa kwenu; lakini tazama, amini ninawaambia kuwa kulikuwa na [a]woga katika mioyo yenu, na amini hii ndiyo sababu ya kuwa ninyi hamkupata.

4 Na sasa Mimi, Bwana ninawapa [a]ushuhuda wa ukweli wa amri hizi ambazo zimewekwa mbele yenu.

5 Macho yenu yamekuwa juu ya mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na [a]lugha yake ninyi mnaijua, na udhaifu wake mnaujua; nanyi mmetafuta katika mioyo yenu maarifa ili muweze kuielekeza kupita lugha yake; hii pia mnajua.

6 Sasa, ninyi tafuteni kutoka katika Kitabu cha Amri, hata ile isiyo muhimu miongoni mwao, na mteueni yule aliye na

67 1*a* MWM Mzee.
2*a* Zab. 34:15.
3*a* MWM Hofu.
4*a* MWM Ukweli; Ushuhuda.
5*a* M&M 1:24.

[a]hekima kuliko wote miongoni mwenu;

7 Au, kama kuna yeyote miongoni mwenu ambaye atafanya mmoja kama huo, ndipo mtakuwa na haki katika kusema kuwa hamjui kwamba ni ya kweli;

8 Lakini, kama hamwezi kufanya hata mmoja kama huo, ninyi mna hatia kama [a]hamshuhudii kwamba ni ya kweli.

9 Kwani mnajua kuwa hamna udhalimu ndani yake, na kwamba kile kilicho cha [a]haki hutoka juu, kutoka kwa Baba wa [b]mianga.

10 Na tena amini ninawaambia kuwa hii ni nafasi kwenu, na ahadi ninaitoa kwa wale waliotawazwa kwa huduma hii, kuwa kwa kadiri mtakavyojivua ninyi wenyewe kuondokana na [a]wivu na [b]woga, na [c]mkajinyenyekeza mbele zangu, kwa kuwa hamjawa wanyenyekevu vya kutosha, [d]pazia litapasuka nanyi [e]mtaniona Mimi ndiye—siyo kwa akili ya kimwili wala ya asili, bali ya kiroho.

11 Kwani hakuna [a]mtu aliyemwona Mungu wakati wowote, isipokuwa amehuishwa na Roho wa Mungu.

12 Wala haiwezekani [a]mwanadamu wa asili akastahimili uwepo wa Mungu, wala kwa namna ya akili ya kimwili.

13 Ninyi hamwezi kustahimili uwepo wa Mungu sasa, wala kutumikiwa na malaika; kwa hiyo, endeleeni katika [a]uvumilivu hadi mtakapokuwa [b]mmekamilika.

14 Na akili zenu zisiangalie nyuma; na wakati [a]mtakapostahili, katika wakati wangu mwenyewe, mtaona na kujua kile ambacho kilitolewa juu yenu kwa mikono ya mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo. Amina.

SEHEMU YA 68

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Hiram, Ohio, 1 Novemba 1831, katika jibu la maombi kwamba mapenzi ya Bwana yafahamike kuhusu Orson Hyde, Luke S. Johnson, Lyman E. Johnson, na William E. McLellin. Ingawa sehemu ya ufunuo huu ilielekezwa kwa watu hawa wanne, mengi ya yaliyomo yanalihusu Kanisa zima. Ufunuo huu ulipanuliwa kwa maelekezo ya Joseph

6a 2 Ne. 9:28–29, 42.
8a MWM Shahidi, Ushahidi.
9a Moro. 7:15–18.
b Yak. (Bib.) 1:17; M&M 50:24; 84:45; 88:49.
10a MWM Wivu, enye Wivu.
b MWM Hofu.
c MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
d MWM Pazia.
e M&M 88:68; 93:1; 97:16.
11a TJS Ku. 33:20, 23 (Kiambatisho) Yn. 1:18; 6:46; TJS 1 Yoh. 4:12 (Kiambatisho) M&M 84:19–22; Musa 1:11, 14.
12a Mos. 3:19. MWM Mwanadamu wa Tabia ya Asili.
13a Rum. 2:7. MWM Subira.
b Mt. 5:48; 3 Ne. 12:48.
14a MWM Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki.

Smith wakati ulipochapishwa katika toleo la mwaka 1835 la Mafundisho na Maagano.

1–5, Maneno ya wazee wakati wakiongozwa na Roho Mtakatifu ni maandiko; 6–12, Wazee watahubiri na kubatiza, na ishara zitawafuata waumini wa kweli; 13–24, Mzaliwa wa kwanza miongoni mwa wana wa Haruni aweza kutumika kama Askofu Kiongozi (hii maana yake, anashikilia funguo za urais kama askofu) chini ya maelekezo ya Urais wa Kwanza; 25–28, Wazazi wanaamriwa kuwafundisha injili watoto wao; 29–35, Watakatifu wataishika Sabato, watafanya kazi kwa bidii, na kuomba.

Mtumishi wangu, Orson Hyde, aliitwa kwa kutawazwa kwake kuitangaza injili isiyo na mwisho, kwa [a]Roho wa Mungu aliye hai, kutoka taifa hadi taifa, na kutoka nchi hadi nchi, katika mikutano ya waovu, katika masinagogi yao, akisemezana nao na kuwaelezea maandiko yote.

2 Na, tazama, na lo, huu ni mfano kwa wale wote ambao wametawazwa katika ukuhani huu, wale ambao kazi imekwisha tolewa kwao kwenda—

3 Na huu ni mfano kwao, kwamba [a]watasema kama vile walivyoongozwa na Roho Mtakatifu.

4 Na lolote watakalolisema wakati wanaongozwa na [a]Roho Mtakatifu litakuwa andiko, litakuwa ni mapenzi ya Bwana, litakuwa ni nia ya Bwana, litakuwa ni neno la Bwana, itakuwa ni sauti ya Bwana, na ni [b]uwezo wa Mungu kwa wokovu.

5 Tazama, hii ni ahadi ya Bwana kwenu, Enyi watumishi wangu.

6 Kwa hiyo, changamkeni, na [a]msiogope, kwani Mimi Bwana nipo pamoja nanyi, na nitasimama karibu yenu; nanyi mtanishuhudia, hata Yesu Kristo, kuwa Mimi ndimi Mwana wa Mungu aliye hai, kwamba nilikuwepo, kwamba nipo, na kwamba nitakuja.

7 Hili ndilo neno la Bwana kwenu, mtumishi wangu [a]Orson Hyde, na pia mtumishi wangu Luke Johnson, na kwa mtumishi wangu Lyman Johnson, na kwa mtumishi wangu William E. McLellin, na kwa wazee wote waaminifu wa kanisa langu—

8 [a]Enendeni ulimwenguni mwote, [b]mkaihubiri injili kwa kila [c]kiumbe, mkitenda katika [d]mamlaka ambayo nimewapa, [e]mkibatiza katika jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.

9 Na [a]yule aaminiye na kubatizwa [b]ataokolewa, na yule asiyeamini [c]atalaaniwa.

68 1*a* мwм Roho Mtakatifu.
3*a* 2 Pet. 1:21; M&M 18:32; 42:16; 100:5.
4*a* мwм Roho Mtakatifu; Ufunuo.
b Rum. 1:16.
6*a* Isa. 41:10.
7*a* мwм Hyde, Orson.
8*a* M&M 1:2; 63:37.
b мwм Hubiri; Kazi ya kimisionari.
c Mk. 16:15.
d мwм Mamlaka.
e мwм Batiza, Ubatizo.
9*a* Mk. 16:16; M&M 20:25.
b мwм Wokovu.
c мwм Hukumu.

10 Na yule aliyeamini atabarikiwa kwa [a]ishara kumfuata, hata kama ilivyoandikwa.

11 Nanyi mtapewa kujua [a]ishara za nyakati, na ishara za kuja kwa Mwana wa Mtu;

12 Na kuhusu wale wote kama vile Baba atakavyowashuhudia, ninyi mtapewa uwezo wa [a]kuwafunga katika uzima wa milele. Amina.

13 Na sasa, kuhusu mambo ya nyongeza katika maangano na amri, nayo ni haya—

14 Yanayobaki baada ya hapa, katika wakati wa Bwana ufikapo, [a]maaskofu wengine wateuliwe kwa ajili ya kanisa, kuhudumu hata kama wale wa kwanza;

15 Kwa hiyo, watakuwa [a]makuhani wakuu wenye kustahili, na wateuliwe na [b]Urais wa Kwanza wa Ukuhani wa Melkizedeki, isipokuwa wale walio wazaliwa wa ukoo wa [c]Haruni.

16 Na kama watakuwa wazaliwa halisi wa ukoo wa [a]Haruni wao wanayo haki kisheria ya uaskofu, kama ni wazaliwa wa kwanza miongoni mwa wana wa Haruni;

17 Kwani mzaliwa wa kwanza anashikilia haki ya urais wa Ukuhani huu, na [a]funguo au mamlaka yake.

18 Hakuna mtu aliye na haki kisheria kwenye ofisi hii, kushikilia funguo za ukuhani huu, isipokuwa yule aliye [a]mzaliwa halisi wa ukoo na ni mzaliwa wa kwanza wa Haruni.

19 Lakini, kama [a]kuhani mkuu wa Ukuhani wa Melkizedeki anayo mamlaka ya kutenda katika ofisi zile ndogo anazoweza kuzitenda kazi katika ofisi ya [b]askofu ikiwa hakuna mzaliwa halisi wa ukoo wa Haruni anayeweza kupatikana, ili mradi ameitwa na kutengwa na kutawazwa katika mamlaka haya, chini ya mikono ya Urais wa Kwanza wa Ukuhani wa Melkizedeki.

20 Na mzaliwa halisi wa ukoo wa Haruni, pia, lazima ateuliwe na Urais huu, na aonekane mwenye kustahili, na [a]kupakwa mafuta, na [b]kutawazwa chini ya mikono ya Urais huu, vinginevyo hawajaruhusiwa kisheria kutenda kazi katika ukuhani wao.

21 Lakini, kwa sababu ya kupitia azimio kuhusu haki yao ya ukuhani kutoka kwa baba hadi kwa mwana, wanaweza kudai haki ya kupakwa kwao mafuta kama wakati wowote wanaweza kuthibitisha safu ya mfuatano wa kuzaliwa, au itafanywa kwa kuhakikisha kwa ufunuo kutoka kwa Bwana chini ya mikono ya Urais uliotajwa hapo juu.

10 *a* MWM Ishara.
11 *a* MWM Ishara za Nyakati.
12 *a* M&M 1:8; 132:49. MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
14 *a* MWM Askofu.
15 *a* M&M 72:1.
b MWM Urais wa Kwanza.
c MWM Haruni, Kaka wa Musa.
16 *a* M&M 107:15–17. MWM Ukuhani wa Haruni.
17 *a* MWM Funguo za Ukuhani.
18 *a* Ku. 40:12–15; M&M 84:18; 107:13–16, 70–76.
19 *a* MWM Kuhani Mkuu.
b MWM Askofu.
20 *a* MWM Paka mafuta.
b MWM Kutawaza, Kutawazwa.

22 Na tena, hakuna askofu au kuhani mkuu ambaye atasimikwa kwa ajili ya huduma hii ambaye atashtakiwa au kuhukumiwa kwa jinai yoyote, isipokuwa mbele ya [a]Urais wa Kwanza wa kanisa;

23 Na kadiri atapatikana na hatia mbele ya Urais huu, kwa ushuhuda ambao hauwezi kutuhumiwa, atahukumiwa;

24 Na kama atatubu [a]atasamehewa, kulingana na maagano na amri za kanisa.

25 Na tena, ili mradi [a]wazazi wanao watoto katika Sayuni, au katika [b]kigingi chake chochote ambacho kimeundwa, ambao [c]hawawafundishi wao kuelewa mafundisho ya toba, imani katika Kristo Mwana wa Mungu aliye hai, na ubatizo na kipawa cha Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono, wafikapo [d]miaka minane, [e]dhambi zao zitakuwa juu ya vichwa vya wazazi.

26 Kwani hii itakuwa sheria kwa wakazi wa [a]Sayuni, au katika kila kigingi chake kilichoundwa.

27 Na watoto wao [a]wabatizwe kwa ajili ya [b]ondoleo la dhambi zao wafikishapo umri wa miaka [c]minane na kupokea kuwekwa mikono.

28 Na pia wawafundishe watoto wao [a]kuomba, na kusimama wima mbele za Bwana.

29 Na wakazi wa Sayuni pia waikumbuke siku ya [a]Sabato kuishika kitakatifu.

30 Na wakazi wa Sayuni pia wazikumbuke kazi zao, ili mradi wameteuliwa kufanya kazi, kwa uaminifu wote; kwani mvivu atakumbukwa mbele za Bwana.

31 Sasa, Mimi, Bwana sipendezwi na wakazi wa Sayuni, kwani kuna [a]wavivu miongoni mwao; na watoto wao pia wanakua katika [b]uovu; pia [c]hawatafuti kwa dhati utajiri wa milele, bali macho yao yamejaa tamaa.

32 Mambo haya hayafai kuwa hivyo, na lazima yakomeshwe kutoka miongoni mwao; kwa hiyo, acha mtumishi wangu Oliver Cowdery ayapeleke maneno haya kwenye nchi ya Sayuni.

33 Na amri ninatoa kwao—kwamba yule asiyefanya [a]sala zake mbele za Bwana katika wakati unaostahili, acha [b]akumbukwe mbele za mwamuzi wa watu wangu.

34 Na [a]misemo hii ni ya kweli na ya kuaminika; kwa hiyo, msiivunje, wala [b]kuondoa lolote ndani yake.

35 Tazama, Mimi ni [a]Alfa na Omega, na [b]naja haraka. Amina.

22*a* MWM Urais wa Kwanza.
24*a* MWM Samehe.
25*a* MWM Familia—Wajibu wa wazazi.
b MWM Kigingi.
c MWM Fundisha, Mwalimu.
d M&M 18:42; 20:71.
e Yak. (KM) 1:19; M&M 29:46–48.
26*a* MWM Sayuni.
27*a* MWM Batiza, Ubatizo.
b MWM Ondoleo la Dhambi.
c MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
28*a* MWM Sala.
29*a* M&M 59:9–12. MWM Siku ya Sabato.
31*a* MWM Mvivu, Uvivu.
b MWM Ovu, Uovu.
c M&M 6:7.
33*a* MWM Sala.
b MWM Amua, Hukumu; Rudi, Kurudiwa.
34*a* Ufu. 22:6.
b M&M 20:35; 93:24–25.
35*a* MWM Alfa na Omega.
b M&M 1:12.

SEHEMU YA 69

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii huko Hiram, Ohio, 11 Novemba 1831. Ukusanyaji wa mafunuo ulio kusudiwa kwa uchapishaji wa awali ulikuwa umekwisha pitishwa kwenye mkutano maalum wa 1–2 Novemba. Ilipofika 3 Novemba ufunuo uliopo hapa ndani unaoonekana kama sehemu ya 133, baadae ukaitwa Kiambatisho, uliongezwa. Oliver Cowdery mwanzoni alikuwa ameteuliwa kubeba miswada ya amri na mafunuo yaliyo kusanywa kwenda Independence, Missouri, kwa ajili ya kupiga chapa. Pia alikuwa achukue fedha zilizokuwa zimechangwa kwa ajili ya kulijenga Kanisa huko Missouri. Ufunuo huu unamwelekeza John Whitmer kuongozana na Oliver Cowdery na pia unamwelekeza Whitmer kusafiri na kukusanya taarifa za kihistoria katika wito wake kama mwanahistoria wa Kanisa na mtunza kumbukumbu.

1–2, John Whitmer atafuatana na Oliver Cowdery kwenda Missouri; 3–8, Yeye pia atahubiri na kukusanya, atanakili kumbukumbu, na kuandika habari za kihistoria.

Nisikilizeni, asema Bwana Mungu wenu, kwa ajili ya mtumishi wangu [a]Oliver Cowdery. Siyo hekima kwangu kwamba lazima akabidhiwe amri na fedha ambazo atazibeba kwenda nchi ya Sayuni, isipokuwa mtu mmoja aende pamoja naye mtu ambaye atakuwa mkweli na mwaminifu.

2 Kwa hiyo, Mimi, Bwana, ninapenda kuwa mtumishi wangu, [a]John Whitmer, aende pamoja na mtumishi wangu Oliver Cowdery;

3 Na pia kwamba naye ataendelea katika kuandika na kutengeneza [a]historia ya mambo yote muhimu ambayo atayaona na kuyafahamu yahusuyo kanisa langu;

4 Na pia kwamba atapokea [a]ushauri na msaada kutoka kwa mtumishi wangu Oliver Cowdery na wengineo.

5 Na pia, watumishi wangu walio nchi za ng'ambo yawapasa kutuma taarifa za [a]usimamizi wao katika nchi ya Sayuni;

6 Kwani nchi ya Sayuni itakuwa makao na mahali pa kupokea na kufanya mambo haya yote.

7 Hata hivyo, mtumishi wangu John Whitmer atasafiri mara nyingi kutoka mahali hadi mahali, na kutoka kanisa hadi kanisa, ili aweze kupata maarifa kwa urahisi—

8 Akihubiri na kuelezea, akiandika, kunakili, kuchagua, na kupata mambo yote yatakayokuwa kwa faida ya kanisa, na kwa vizazi vinavyo chipukia

69 1*a* MWM Cowdery, Oliver.
2*a* MWM Whitmer, John.
3*a* M&M 47:1–3; 85:1.
4*a* MWM Ushauri.
5*a* MWM Msimamizi, Usimamizi.

vitakavyokua katika nchi ya [a]Sayuni, kuimiliki kutoka kizazi hata kizazi, milele na milele. Amina.

SEHEMU YA 70

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Hiram, Ohio, 12 Novemba 1831. Historia ya Nabii inaeleza kuwa mikutano minne maalumu ilikuwa imefanyika kutoka tarehe 1 hadi 12 ya Novemba, kwa pamoja. Katika mkutano wa mwisho kati ya mikutano hii, umuhimu mkubwa wa mafunuo ambayo baadae yangekuja kuchapishwa kama Book of Commandments (Kitabu cha Amri) na baadaye Mafundisho na Maagano, ulifikiriwa. Ufunuo huu ulitolewa baada ya mkutano kupiga kura kwamba mafunuo yalikuwa "ya thamani kwa Kanisa kuliko utajiri wote wa Dunia." Historia ya Joseph Smith inayataja mafunuo haya kuwa ni "msingi wa Kanisa katika siku hizi za mwisho, na ni ya manufaa kwa ulimwengu, yakionyesha kwamba funguo za siri za ufalme wa Mwokozi wetu zimekabidhiwa tena kwa mwanadamu."

1–5, Wasimamizi wanateuliwa kuchapisha mafunuo; 6–13, Wale watendao kazi katika mambo ya kiroho wanastahili ujira wao; 14–18, Watakatifu wanapaswa kuwa sawa katika mambo ya kimwili.

Tazama, na sikilizeni, Enyi wakazi wa Sayuni, na watu wote wa kanisa langu mlio mbali, na sikilizeni neno la Bwana ambalo ninalitoa kwa mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na pia kwa mtumishi wangu Martin Harris, na pia kwa mtumishi wangu Oliver Cowdery, na pia kwa mtumishi wangu John Whitmer, na pia kwa mtumishi wangu Sidney Rigdon, na pia kwa mtumishi wangu William W. Phelps, kama amri kwao.

2 Kwani ninatoa kwao amri; kwa hivyo sikilizeni na msikie, kwani hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwao—

3 Mimi, Bwana, nimewateua, na kuwatawaza kuwa [a]wasimamizi wa mafunuo na amri ambazo nimezitoa kwao, na zile ambazo nitazitoa kwao hapo baadaye;

4 Na taarifa ya usimamizi huu nitawadai hao katika siku ya hukumu.

5 Kwa hiyo, mimi nimeikabidhi kwao, na hii ni kazi yao katika kanisa la Mungu, kusimamia na mambo yahusikanayo, ndiyo, na manufaa yake.

6 Kwa hiyo, amri ninaitoa kwao, kwamba hawatayatoa mambo haya kwa kanisa, wala kwa walimwengu;

8*a* MWM Sayuni.

70 3*a* 1 Kor. 4:1; M&M 72:20.

7 Hata hivyo, kadiri watakavyopokea zaidi ya mahitaji kwa mahitaji yao ya lazima na yasiyo ya lazima, wayapeleke katika [a]ghala yangu;

8 Na manufaa hayo yawekwe wakfu kwa ajili ya wakazi wa Sayuni, na kwa vizazi vyao, ilimradi wamekuwa [a]warithi kulingana na sheria za ufalme.

9 Tazama, hili ndilo alitakalo Bwana kwa kila mtu katika [a]usimamizi wake, hata kama vile Mimi, Bwana, nilivyoteua au nitakavyoteua hapo baadaye kwa kila mtu.

10 Na tazama, hakuna aliyesamehewa kutoka sheria hii aliye wa kanisa la Mungu aliye hai;

11 Ndiyo, si askofu, wala [a]wakala ambaye atunzaye ghala ya Bwana, wala yule aliyeteuliwa katika usimamizi juu ya mambo ya kimwili.

12 Yule aliyeteuliwa kusimamia katika mambo ya kiroho, naye [a]anastahili ujira wake, kama vile wale walioteuliwa katika usimamizi wa kuhudumu katika mambo ya kimwili;

13 Ndiyo, hata kwa wingi sana, wingi ambao huzidishwa kwao kwa njia ya mafunuo ya Roho.

14 Hata hivyo, katika mambo ya kimwili mtakuwa [a]sawa, na hii isiwe kwa kinyongo, vinginevyo uwingi wa mafunuo ya Roho yatazuiliwa.

15 Sasa, [a]amri hii nimetoa kwa watumishi wangu kwa faida yao wakati wangali hai, kama ishara ya baraka zangu juu ya vichwa vyao, na kama thawabu ya [b]bidii yao na kwa usalama wao;

16 Kwa chakula na kwa [a]mavazi; kwa urithi; kwa nyumba na kwa ardhi, katika hali yoyote Mimi, Bwana, nitakayowaweka, na mahali popote ambapo Mimi, Bwana, nitawatuma.

17 Kwani wamekuwa waaminifu juu ya [a]mambo mengi, na wamefanya vizuri mradi tu hawakutenda dhambi.

18 Tazama, Mimi, Bwana ni mwenye [a]huruma na nitawabariki, na wataingia katika shangwe ya mambo haya. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 71

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Sidney Rigdon, huko Hiram, Ohio 1 Desemba 1831. Nabii alikuwa anaendelea kutafsiri Biblia akiwa na Sidney Rigdon kama mwandishi wake hadi ufunuo huu ulipopokelewa, wakati ambapo kazi hiyo iliwekwa kando kwa muda ili kuwawezesha kutekeleza maelekezo yaliyotolewa ndani

7 *a* M&M 72:9–10.
8 *a* M&M 38:20.
9 *a* MWM Msimamizi, Usimamizi.
11 *a* M&M 57:6.
12 *a* Lk. 10:7.
14 *a* M&M 49:20. MWM Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.
15 *a* Kum. 10:12–13.
b MWM Bidii.
16 *a* M&M 59:16–20.
17 *a* Mt. 25:21–23.
18 *a* MWM Rehema, enye Rehema.

yake. Viongozi hawa walitakiwa kwenda kuhubiri ili kutuliza hisia zisizo za kirafiki ambazo zilijitokeza dhidi ya Kanisa kama matokeo ya uchapishaji wa barua zilizoandikwa na Ezra Booth, ambaye alikuwa ameasi Kanisa.

1–4, Joseph Smith na Sidney Rigdon wanatumwa kwenda kutangaza injili; 5–11, Maadui wa Watakatifu watashindwa.

Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu watumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na [a]Sidney Rigdon, kwamba amini wakati umekwishafika kwamba ni muhimu na yafaa kwangu kwamba ninyi mfungue vinywa vyenu katika [b]kutangaza injili yangu, mambo ya ufalme, na kuelezea [c]siri zake kutoka katika maandiko, kulingana na sehemu ya Roho na uwezo utakaotolewa kwenu, hata kama nitakavyotaka.

2 Amini ninawaambia, utangazieni ulimwengu katika maeneo ya jirani, na katika kanisa pia, kwa kipindi cha wakati, hata mpaka itakapojulishwa kwenu.

3 Amini kazi hii niwapayo ni ya muda.

4 Kwa hiyo, fanyeni kazi katika shamba langu la mizabibu. Waambieni wakazi wa dunia, na kuwashuhudia, na kutengeneza njia kwa amri na mafunuo ambayo yatakuja.

5 Sasa, tazama, hii ndiyo hekima; yeyote asomaye na [a]afahamu na [b]kupokea pia;

6 Kwani yule apokeaye atazidishiwa [a]tele, hata uwezo.

7 Kwa hiyo, [a]washindeni maadui zenu; waiteni ili [b]wakutane na ninyi hadharani na faraghani; na kadiri mlivyo waaminifu aibu yao itajidhihirisha.

8 Kwa hiyo, na waje na hoja zao zenye nguvu dhidi ya Bwana.

9 Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu—hakuna [a]silaha iliyotengenezwa dhidi yenu itakayofanikiwa;

10 Na kama mtu yeyote atapaza sauti dhidi yenu nitamshinda katika wakati wangu.

11 Kwa hiyo, zishikeni amri zangu; ni za kweli na za kuaminika. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 72

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio 4 Desemba 1832. Wazee kadhaa na waumini wengine walikuwa wamekusanyika ili kujifunza wajibu wao, na ili kuinuliwa zaidi katika mafundisho ya Kanisa. Sehemu hii ni mkusanyiko wa mafunuo

71 1 *a* mwm Rigdon, Sidney.
b mwm Kazi ya kimisionari.
c M&M 42:61, 65.
5 *a* mwm Ufahamu.
b Alma 12:9–11.
6 *a* Mt. 13:12.
7 *a* Musa 7:13–17.
b M&M 63:37; 68:8–9.
9 *a* Isa. 54:17.

matatu yaliyopokelewa siku moja. Aya ya 1 mpaka ya 8 zinajulisha juu ya wito wa Newel K. Whitney kama askofu. Ndipo aliitwa na kutawazwa, baadaye aya ya 9 hadi ya 23 zilipokelewa, zikitoa habari za nyongeza juu ya kazi ya askofu. Baadae aya 24 hadi 26 zilitolewa zikitoa maelekezo kuhusu kukusanyika Sayuni.

1–8, Wazee watatoa taarifa ya usimamizi wao kwa askofu; 9–15, Askofu atatunza ghala na kutunza maskini na wenye shida; 16–26, Maaskofu watathibitisha ustahilifu wa wazee.

Sikilizeni, na mkasikie sauti ya Bwana, Enyi wote mliojikusanya pamoja, mlio [a]makuhani wakuu wa kanisa langu, ambao [b]ufalme na uwezo vimetolewa.

2 Kwani amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana, ni muhimu kwangu kwa [a]askofu kuteuliwa kwenu, au kutoka kwenu, kwa ajili ya kanisa katika sehemu hii ya shamba la mizabibu la Bwana.

3 Na amini katika jambo hili mmefanya kwa busara, kwani yatakiwa na Bwana, kwa mkono wa kila [a]msimamizi, kutoa [b]hesabu ya [c]usimamizi wake, katika wakati huu na milele.

4 Kwani yule aliye mwaminifu na mwenye [a]busara anahesabiwa kuwa mwenye kustahili kurithi [b]makao yaliyoandaliwa na Baba yangu kwa ajili yake.

5 Amini ninawaambia, wazee wa kanisa katika sehemu hii ya [a]shamba langu la mizabibu watatoa hesabu ya usimamizi wao kwa askofu, ambaye nimemteua katika sehemu hii ya shamba langu la mizabibu.

6 Mambo haya yatatunzwa katika kumbukumbu, ili yakabidhiwe kwa askofu katika Sayuni.

7 Na kazi ya [a]askofu itajulikana kwa amri zilizotolewa, na kwa sauti ya mkutano.

8 Na sasa, amini ninawaambia, mtumishi wangu [a]Newel K. Whitney ndiye mtu atakayeteuliwa na kutawazwa katika uwezo huu. Haya ndiyo mapenzi ya Bwana Mungu wenu, na Mkombozi wenu. Hivyo ndivyo. Amina.

9 Neno la Bwana, ambalo ni nyongeza ya sheria zilizotolewa, zikijulisha kazi ya askofu ambaye amekwisha tawazwa kwa kanisa katika sehemu hii ya shamba la mizabibu, ambalo amini hili ndilo—

10 Kuitunza [a]ghala ya Bwana; kupokea fedha za kanisa katika sehemu hii ya shamba la mizabibu;

11 Kupokea taarifa ya wazee kama ilivyoamriwa hapo awali; na [a]kushughulikia mahitaji

72 1*a* M&M 68:14–19.
b MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
2*a* MWM Askofu.
3*a* MWM Msimamizi, Usimamizi.
b M&M 42:32; 104:11–13.
c Lk. 19:11–27.
4*a* Mt. 24:45–47.
b M&M 59:2.
5*a* MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
7*a* M&M 42:31; 46:27; 58:17–18; 107:87–88.
8*a* MWM Whitney, Newel K.
10*a* M&M 70:7–11; 78:3. MWM Ghala.
11*a* M&M 75:24.

yao, wale watakaolipa kwa ajili ya yale wanayopokea, ilimradi wanao uwezo wa kulipa;

12 Ili hii pia iweze kuwekwa wakfu kwa manufaa ya kanisa, kwa maskini na wenye shida.

13 Na kwa yule [a]asiye na uwezo wa kulipa, hesabu yake itachukuliwa na kukabidhiwa kwa askofu wa Sayuni, ambaye atalipa deni kutokana na kile Bwana atakachokiweka mikononi mwake;

14 Na kazi za uaminifu za wafanya kazi katika mambo ya kiroho, katika kusimamia injili na mambo ya ufalme kwa kanisa, na kwa ulimwengu, zitakubaliwa kulipa deni kwa askofu katika Sayuni;

15 Hivyo malipo yatatoka kanisani, kwa kuwa kulingana na [a]sheria kila mtu ambaye huja Sayuni ni lazima aweke vitu vyote mbele ya askofu katika Sayuni.

16 Na sasa, amini ninawaambia, kwamba kwa vile kila mzee katika sehemu hii ya shamba la mizabibu lazima atoe taarifa ya usimamizi wake kwa askofu katika sehemu hii ya shamba la mizabibu—

17 [a]Hati kutoka kwa jaji au askofu katika sehemu hii ya shamba la mizabibu, kwenda kwa askofu katika Sayuni, humfanya kila mtu aweze kukubaliwa, na hujibu mambo yote, kwa ajili ya urithi, na kupokelewa kama [b]msimamizi mwenye busara na mfanyakazi mwaminifu;

18 Vinginevyo hatakubaliwa na askofu wa Sayuni.

19 Na sasa, amini ninawaambia, na kila mzee ambaye atatoa taarifa kwa askofu wa kanisa katika sehemu hii ya shamba la mizabibu athibitishwe na kanisa au makanisa, ambako hutenda kazi, ili aweze kuonyesha mwenyewe na taarifa yake wamethibitishwa katika mambo yote.

20 Na tena, acha watumishi wangu ambao wameteuliwa kuwa kama wasimamizi juu ya mambo yahusuyo [a]maandishi ya kanisa langu wanayo madai kwa ajili ya msaada kutoka kwa askofu au maaskofu katika mambo yote—

21 Ili [a]mafunuo yaweze kuchapishwa, na kuenea hata miisho ya dunia; kwamba nao pia waweze kupata fedha ambazo zitalinufaisha kanisa katika mambo yote;

22 Ili nao pia waweze kuonyesha kuwa wamethibitishwa katika mambo yote, na wahesabiwe kama wasimamizi wenye busara.

23 Na sasa, tazama, huu utakuwa utaratibu kwa matawi yote makubwa ya kanisa, katika nchi yoyote yatakakoanzishwa. Na sasa ninafanya mwisho wa maneno yangu. Amina.

24 Maneno machache ya nyongeza katika sheria ya ufalme, kuhusu waumini wa kanisa—wale ambao [a]wameteuliwa

13*a* MWM Maskini.
15*a* M&M 42:30–31. MWM Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.
17*a* M&M 20:64, 84.
b M&M 42:32.
20*a* M&M 70:3–5.
21*a* MWM Mafundisho na Maagano.
24*a* MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito.

kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kwenda Sayuni, na ambao wamepata nafasi ya kwenda Sayuni—

25 Na wapeleke hati ya uthibitisho kwa askofu kutoka kwa wazee watatu wa kanisa, au hati ya uthibitisho kutoka kwa askofu;

26 Vinginevyo yule atakayekwenda nchi ya Sayuni hatahesabiwa kama msimamizi mwenye busara. Huu pia ni mfano. Amina.

SEHEMU YA 73

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Sidney Rigdon, huko Hiram, Ohio, tarehe 10 10 Januari 1832. Kutoka mwanzoni mwa Desemba iliyotangulia, Nabii na Sidney walikuwa wamejishughulisha katika kuhubiri, na kwa njia hii inamaanisha walikamilisha mengi katika kupunguza hisia zisizo nzuri ambazo zilijitokeza dhidi ya Kanisa (ona kichwa cha habari cha sehemu ya 71).

1–2, Wazee waendelee kuhubiri; 3–6, Joseph Smith na Sidney Rigdon wataendelea kutafsiri Biblia hadi imalizike.

KWANI amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, yafaa kwangu kwamba [a]waendelee kuhubiri injili, na katika kuyashawishi makanisa katika maeneo ya jirani, hadi wakati wa mkutano;

2 Na halafu, tazama, itajulikana kwao, kwa [a]sauti ya mkutano, juu ya kazi zao mbalimbali.

3 Sasa, amini ninawaambia watumishi wangu, Joseph Smith, Mdogo, na Sidney Rigdon, asema Bwana, ni [a]muhimu kwenu [b]kutafsiri tena;

4 Na, ilimradi yawezekana, kuhubiri katika maeneo ya jirani hadi mkutano ujao; na baada ya hapo ni muhimu ninyi kuendelea na kazi ya kutafsiri hadi imalizike.

5 Na huu uwe ni utaratibu kwa wazee hadi itakapojulishwa vinginevyo, hata kama ilivyoandikwa.

6 Sasa sitatoa zaidi kwenu kwa wakati huu. [a]Vifungeni viuno vyenu na kuwa na kiasi. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 74

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, Wilaya ya Wayne, New

73 1*a* MY wengine waliokuwa misioni; tazama M&M 57–68.
2*a* M&M 20:63.
3*a* MY Joseph na Sidney awali waliamriwa kuacha kutafsiri Biblia na kuhuburi injili. M&M 71:2.
b M&M 45:60–61; 76:15. MWM Tafsiri ya Joseph Smith (TJS).
6*a* 1 Pet. 1:13.

York mwaka 1830. Hata kabla ya kuanzishwa kwa Kanisa, maswali yalikuwa yameibuka juu aina sahihi ya ubatizo, maswali ambayo yalimwongoza Nabii kutafuta majibu juu ya mada hii. Historia ya Joseph Smith inaeleza kwamba ufunuo huu ni maelezo juu ya 1 Wakorintho 7:14, andiko ambalo mara nyingi limekuwa likitumika kuhalalisha ubatizo wa watoto wachanga.

1–5, Paulo alishauri Kanisa la siku zake lisizishikilie torati ya Musa; 6–7, Watoto wadogo ni watakatifu na wametakaswa kwa njia ya Upatanisho.

Kwani mume [a]asiye amini anatakaswa na mke, na mke asiye amini anatakaswa na mume; vinginevyo watoto wenu wangelikuwa wachafu, lakini sasa ni watakatifu.

2 Sasa, katika siku za mitume sheria ya tohara ilikuwepo miongoni mwa Wayahudi wote ambao hawakuamini injili ya Yesu Kristo.

3 Na ikawa kwamba kulitokea [a]ugomvi mkubwa miongoni mwa watu kuhusu sheria ya [b]tohara, kwani mume asiye amini alitaka watoto wake watahiriwe na kuwa chini ya [c]torati ya Musa, torati ambayo ilikwisha timilizwa.

4 Na ikawa kwamba watoto wale, ambao walilelewa chini ya torati ya Musa, walifuata [a]mapokeo ya Baba zao na hawakuamini injili ya Yesu Kristo, kwa njia hii hawakuwa watakatifu.

5 Kwa hiyo, kwa sababu hii, mtume aliliandikia kanisa, akiwapa amri, siyo ya Bwana, bali yake yeye mwenyewe, kwamba mwenye kuamini hapaswi [a]kuungana na asiye amini; isipokuwa [b]torati ya Musa imekoma miongoni mwao,

6 Ili watoto wao waweze kubaki bila tohara; na ili mapokeo yaweze kukoma, ambayo husema watoto wadogo siyo watakatifu; kwani imekuwepo miongoni mwa Wayahudi;

7 Lakini [a]watoto wadogo ni [b]watakatifu, wakiwa [c]wametakaswa kwa njia ya [d]upatanisho wa Yesu Kristo; na hiki ndicho maandiko yanachomaanisha.

SEHEMU YA 75

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Amherst, Ohio, 25 Januari 1832. Sehemu hii ina mafunuo mawili tofauti (wa kwanza

74 1*a* 1 Kor. 7:14–19.
3*a* Mdo. 15:1–35; Gal. 2:1–5.
b mwm Tohara.
c mwm Torati ya Musa.
4*a* mwm Mapokeo.
5*a* mwm Ndoa, Oa, Olewa—Ndoa ya imani mbili.
b 2 Ne. 25:24–27.
7*a* Moro. 8:8–15; M&M 29:46–47; 137:10.
b mwm Takatifu.
c mwm Wokovu—Wokovu wa watoto.
d mwm Lipia dhambi, Upatanisho.

ni katika aya ya 1 hadi ya 22 na wa pili ni katika aya ya 23 hadi 36) yalitolewa siku hiyo hiyo, Tukio lilikuwa la mkutano ambapo Joseph Smith alikubaliwa na kutawazwa kuwa Rais wa Ukuhani Mkuu. Wazee kadhaa walitamani kujua zaidi juu ya kazi zao kwa wakati huo. Mafunuo haya yalifuata.

1–5, Wazee waaminifu ambao wanaihubiri injili watapata uzima wa milele; 6–12, Ombeni ili muweze kumpokea Mfariji, afundishaye mambo yote; 13–22, Wazee watawahukumu wale walioukataa ujumbe wao; 23–36, Familia za wamisionari zitapata msaada kutoka Kanisani.

Amini, amini, ninawaambia, Mimi nisemaye hata kwa [a]sauti ya Roho wangu, [b]Alfa na Omega, Bwana wenu na Mungu wenu—

2 Sikilizeni, Enyi mliotoa majina yenu kwenda kutangaza injili yangu, na [a]kupogoa [b]shamba langu la mizabibu.

3 Tazama, ninawaambia kuwa ni mapenzi yangu kuwa ninyi mwende na wala msibaki, wala [a]msikae bure pasipo kazi bali fanyeni kazi kwa nguvu zenu—

4 Mkipaza sauti zenu kama tarumbeta, [a]mkitangaza [b]ukweli kulingana na mafunuo na amri ambazo nimewapa.

5 Na hivyo, endapo mtakuwa waaminifu mtabebeshwa [a]miganda mingi, na [b]kuvikwa [c]heshima, na [d]utukufu, na [e]kutokufa, na [f]uzima wa milele.

6 Kwa sababu hiyo, amini ninamwambia mtumishi wangu William E. McLellin, [a]ninaifuta kazi niliyoitoa kwake ya kwenda nchi ya mashariki;

7 Na Mimi naitoa kwake kazi mpya na amri mpya, ambayo kwayo Mimi, Bwana, [a]ninamrudi kwa sababu ya [b]manung'uniko ya moyoni mwake;

8 Na ametenda dhambi; hata hivyo, ninamsamehe na kumwambia tena, Nenda katika nchi za kusini.

9 Na mtumishi wangu Luke Johnson aende pamoja naye, na watangaze mambo ambayo nimewaamuru—

10 Wakililingana jina la Bwana, kwa [a]Mfariji, ambaye atawafundisha mambo yote yaliyo muhimu kwao—

11 [a]Wakisali daima ili wasikate tamaa; kadiri watakavyofanya haya, nitakuwa pamoja nao hata mwisho.

12 Tazama, haya ndiyo mapenzi ya Bwana Mungu wenu juu yenu. Hivyo ndivyo. Amina.

75 1*a* mwm Ufunuo.
b Ufu. 1:8.
mwm Alfa na Omega.
2*a* Yak. (KM) 5:62.
b mwm Shamba la mizabibu la Bwana.
3*a* mwm Mvivu, Uvivu.
4*a* mwm Kazi ya kimisionari.
b M&M 19:37.
5*a* Zab. 126:6; Alma 26:5.
b mwm Taji.
c mwm Heshima.
d mwm Utukufu.
e mwm Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
f mwm Uzima wa Milele.
6*a* M&M 66.
7*a* mwm Rudi, Kurudiwa.
b mwm Manung'uniko; Mawazo.
10*a* Yn. 14:26.
mwm Mfariji.
11*a* 2 Ne. 32:9.

13 Na tena, amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana, na mtumishi wangu [a]Orson Hyde na mtumishi wangu [b]Samuel H. Smith wafanye safari yao katika nchi za mashariki, na kutangaza mambo ambayo nimewaamuru; na ilimradi wao ni waaminifu, lo, Mimi nitakuwa [c]pamoja nao, hata mwisho.

14 Na tena, amini ninamwambia mtumishi wangu Lyman Johnson, na mtumishi wangu [a]Orson Pratt, watafanya safari yao pia katika nchi za mashariki; na tazama, na lo, Mimi niko pamoja nao pia, hata mwisho.

15 Na tena, nasema kwa mtumishi wangu Asa Dodds, na kwa mtumishi wangu Calves Wilson, kwamba nao pia wafunge safari yao kwenda nchi za magharibi, na kutangaza injili yangu, hata kama vile nilivyowaamuru wao.

16 Na yule aliye mwaminifu atashinda mambo yote, na [a]atainuliwa juu siku ile ya mwisho.

17 Na tena, ninasema kwa watumishi wangu Major N. Ashley, na mtumishi wangu Burr Riggs, na wafunge safari yao pia kwenda katika nchi ya kusini.

18 Ndiyo, na wote wafunge safari zao, kama nilivyowaamuru, wakipita toka nyumba hadi nyumba, na kutoka kijiji hadi kijiji, na kutoka mji hadi mji.

19 Na nyumba yoyote mtakayoingia; na wakawakaribisha, iacheni baraka yenu juu ya nyumba hiyo.

20 Na katika nyumba yoyote mtakayoingia na wala hawakuwakaribisha, mtatoka upesi kutoka humo, na [a]yakung'uteni mavumbi ya miguu yenu kuwa ushuhuda juu yao.

21 Nanyi mtakuwa na [a]shangwe na furaha; na fahamuni neno hili, kwamba katika siku ile ya hukumu ninyi mtakuwa [b]mahakimu wa nyumba hiyo, na kuwahukumu;

22 Na itakuwa rahisi kuvumilika kwa mpagani katika siku ya hukumu, kuliko watu wa nyumba hiyo; kwa hiyo, [a]vifungeni viuno vyenu na kuweni waaminifu, nanyi mtayashinda mambo yote, na mtainuliwa juu siku ile ya mwisho. Hivyo ndivyo. Amina.

23 Na tena, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu ninyi, Enyi wazee wa kanisa langu, ambao mmeyatoa majina yenu ili muweze kujua mapenzi yake juu yenu—

24 Tazama, ninawaambia, kuwa ni wajibu wa kanisa kusaidia katika kutunza familia za wale, na pia kutunza familia za wale walioitwa na wale watakaohitajika kutumwa ulimwenguni kuitangaza injili kwa ulimwengu.

25 Kwa hiyo, Mimi, Bwana,

13*a* MWM Hyde, Orson.
b MWM Smith, Samuel H.
c Mt. 28:19–20.
14*a* MWM Pratt, Orson.
16*a* M&M 5:35.
20*a* Mt. 10:14; Lk. 10:11–12; M&M 24:15; 60:15.
21*a* Mt. 5:11–12.
b MWM Amua, Hukumu.
22*a* Efe. 6:14; M&M 27:15–18.

ninatoa amri hii kwenu, kwamba tafuteni mahali kwa familia zenu, ili mradi ndugu zenu wapo tayari kuifungua mioyo yao.

26 Na wale wote wanaoweza kupata mahali kwa ajili ya familia zao, na msaada wa kanisa kwa ajili yao, wasiache kwenda katika ulimwengu, iwe mashariki au magharibi, kaskazini au kusini.

27 Na waombe nao watapata, wabishe nao watafunguliwa, na watajulishwa kutoka juu, hata kwa [a]Mfariji, mahali pa kwenda.

28 Na tena, amini ninawaambia, kwamba kila mtu anaye wajibika [a]kuitunza [b]familia yake mwenyewe, na aitunze, na kwa vyovyote vile hatapoteza taji lake; na afanye kazi katika kanisa.

29 Na kila mtu afanye [a]bidii katika mambo yote. Na [b]mzembe hatakuwa na nafasi katika kanisa, isipokuwa atubu na kurekebisha njia zake.

30 Kwa hiyo, mtumishi wangu Simeon Carter na mtumishi wangu Emer Harris waungane katika huduma;

31 Na pia mtumishi wangu Ezra Thayre na mtumishi wangu [a]Thomas B. Marsh;

32 Pia mtumishi wangu Hyrum Smith na mtumishi wangu Reynolds Cahoon;

33 Na pia mtumishi wangu Daniel Stanton na mtumishi wangu Seymour Brunson;

34 Na pia mtumishi wangu Sylvester Smith na mtumishi wangu Gideon Carter;

35 Na pia mtumishi wangu Ruggles Eames na mtumishi wangu Stephen Burnett;

36 Na pia mtumishi wangu Micah B. Welton na pia mtumishi wangu Eden Smith. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 76

Ono lililotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Sidney Rigdon, huko Hiram, Ohio, 16 Februari 1832. Katika utangulizi wa kumbukumbu ya ono hili, Historia ya Joseph Smith inaeleza: "Baada ya kurejea kutoka kwenye mkutano huko Amherst, nilianza tena tafsiri ya Maandiko. Kutokana na mafunuo mbali mbali ambayo nilikuwa nimekwisha yapokea, ilionekana dhahiri kwamba vipengele vingi muhimu vinavyogusa wokovu wa mwanadamu, vilikuwa vimeondolewa kutoka kwenye Biblia, au vilipotezwa kabla haijatungwa. Ilionekana wazi kutokana na ukweli uliosalia, kwamba kama Mungu alimzawadia kila mtu kulingana na matendo aliyoyafanya katika

27 *a* 2 Ne. 32:5; M&M 8:2. MWM Roho Mtakatifu.
28 *a* 1 Tim. 5:8; M&M 83:2.
b MWM Familia.
29 *a* MWM Bidii.
b MWM Mvivu, Uvivu.
31 *a* MWM Marsh, Thomas B.

mwili neno 'Mbingu,' kama linavyo kusudiwa na Watakatifu kuwa makao ya milele, ni lazima ziwe falme zaidi ya moja. Vivyo hivyo, . . . wakati nikitafsiri injili ya Mt. Yohana, mimi mwenyewe na Mzee Rigdon tuliona ono lifuatalo" Wakati ono hili likitolewa, Nabii alikuwa akitafsiri Yohana 5:29.

1–4, Bwana ndiye Mungu; 5–10, Siri za ufalme zitafunuliwa kwa wote walio waaminifu; 11–17, Wote watafufuka katika ufufuo wa wenye haki au wasio na haki; 18–24, Wakazi wa dunia nyingi ni wana au mabinti wa Mungu kwa njia ya Upatanisho wa Yesu Kristo; 25–29, Malaika wa Mungu alianguka na kuwa ibilisi; 30–49, Wana wa upotevu watateseka kwa dhambi ya milele; wengine wote watapata kiwango fulani cha wokovu; 50–70, Utukufu na tuzo za viumbe walioinuliwa katika ufalme wa selestia unaelezewa; 71–80, Wale watakao urithi ufalme terestria wanaelezwa; 81–113, Hali za wale walio katika fahari za telestia, terestria, na selestia zinafafanuliwa; 114–119, Wanaoamini wanaweza kuona na kuelewa siri za ufalme wa Mungu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

[a]Sikieni, Enyi mbingu, na tega sikio, Ewe nchi, na shangilieni ninyi wakazi wake, kwa kuwa Bwana ndiye [b]Mungu, na zaidi yake yeye [c]hapana [d]Mwokozi.

2 Hekima yake ni [a]kuu, njia zake ni za [b]ajabu, na hakuna awezaye kuona upana wa matendo yake.

3 [a]Makusudi yake hayashindwi, wala hakuna awezaye kuzuia mkono wake.

4 Tangu milele hata milele yeye ni [a]yule yule, na miaka yake [b]haikomi.

5 Kwani hivyo ndivyo asemavyo Bwana—Mimi, Bwana, ni mwenye [a]huruma na neema kwa wale wote [b]wanichao, na napenda kuwaheshimu wale wote ambao [c]hunitumikia katika haki na kweli hata mwisho.

6 Tuzo lao litakuwa kuu na [a]utukufu wao utakuwa wa milele.

7 Na kwao [a]nitafunua [b]siri zote, ndiyo, siri zote za ufalme zilizofichwa tangu siku za kale, na za zama zijazo, nitawafahamisha uradhi wa mapenzi yangu yanayohusu mambo yote ya ufalme wangu.

76 1*a* Isa. 1:2.
b Yer. 10:10. MWM Mungu, Uungu—Mungu Mwana.
c Isa. 43:11; Hos. 13:4.
d MWM Mwokozi.
2*a* 2 Ne. 2:24; M&M 38:1–3.
b Ufu. 15:3.
3*a* 1 Fal. 8:56; M&M 1:38; 64:31.
4*a* Ebr. 13:8; M&M 35:1; 38:1–4; 39:1–3.
b Zab. 102:25–27; Ebr. 1:12.
5*a* Ku. 34:6; Zab. 103:8. MWM Rehema, enye Rehema.
b Kum. 6:13; Yos. 4:23–24. MWM Hofu; Uchaji.
c M&M 4:2.
6*a* MWM Utukufu wa Selestia.
7*a* M&M 42:61; 59:4; 98:12; 121:26–33.
b MWM Siri za Mungu.

8 Ndiyo, hata maajabu ya milele watayajua, na mambo yajayo nitawaonyesha, hata mambo ya vizazi vingi.

9 Na [a]hekima yao itakuwa kuu, na [b]ufahamu wao utafika mbinguni; na mbele zao akili za watu wenye akili [c]zitapotea, na ufahamu wa wenye busara utafichwa.

10 Kwani kwa [a]Roho wangu [b]nitawaangaza, na kwa [c]uwezo wangu nitawajulisha siri za mapenzi yangu—ndiyo, hata mambo yale ambayo [d]jicho halijayaona, wala sikio kusikia, wala hayajaingia katika moyo wa mwanadamu.

11 Sisi, Joseph Smith, Mdogo, na Sidney Rigdon, tukiwa [a]katika Roho tarehe kumi na sita ya Februari, katika mwaka wa Bwana wetu elfu moja mia nane na thelathini na mbili—

12 Kwa uwezo wa [a]Roho [b]macho yetu yalifunguliwa na ufahamu wetu ukatiwa nuru, nasi tukaona na kuyaelewa mambo ya Mungu—

13 Hata mambo yale yaliyokuwa mwanzo kabla ya ulimwengu kuwako, yaliyowekwa na Baba, kupitia Mwanawe wa Pekee, ambaye alikuwa kifuani mwa Baba, hata kutoka [a]mwanzo;

14 Ambaye sisi tunamshuhudia; na ushuhuda tunaoutoa ni utimilifu wa injili ya Yesu Kristo, ambaye ndiye Mwana, tuliyemwona na ndiye [a]tuliyeongea naye katika [b]ono la mbinguni.

15 Kwani wakati tulipokuwa tukifanya kazi ya [a]kutafsiri, ambayo Bwana alitupangia, tulikuja kwenye mstari wa ishirini na tisa wa mlango wa tano wa Yohana, ambayo ilitolewa kama ifuatavyo—

16 Ukizungumzia juu ya ufufuko wa wafu, kuhusu wale watakao [a]isikia sauti ya [b]Mwana wa Mtu:

17 Na watatoka; wale waliofanya [a]mema, kwa [b]ufufuo wa wenye [c]haki; na wale waliotenda uovu, kwa ufufuo wa wasio na haki.

18 Sasa hili lilitufanya sisi tustaajabu, kwa kuwa lilitolewa kwetu na Roho.

19 Na wakati [a]tukitafakari mambo haya, Bwana aligusa macho ya ufahamu wetu nayo yakafunguka, na utukufu wa Bwana ukang'aa pande zote.

20 Nasi tukauona [a]utukufu wa Mwana, akiwa [b]mkono wa kuume wa [c]Baba, na kupokea utimilifu wake;

9a MWM Hekima.
b MWM Ufahamu.
c Isa. 29:14; 2 Ne. 9:28–29.
10a Moro. 10:5.
b MWM Ufunuo; Ushuhuda.
c MWM Uwezo.
d Isa. 64:4; 1 Kor. 2:9; 3 Ne. 17:15–17; M&M 76:114–116.
11a Ufu. 1:10.
12a MWM Kugeuka sura.
b M&M 110:1; 137:1; 138:11, 29.
13a Musa 4:2.
14a M&M 109:57.
b MWM Ono.
15a MWM Tafsiri ya Joseph Smith (TJS).
16a Yn. 5:28.
b MWM Mwana wa Mtu.
17a MWM Matendo.
b MWM Ufufuko.
c Mdo. 24:15.
19a MWM Tafakari.
20a MWM Yesu Kristo—Utukufu wa Yesu Kristo.
b Mdo. 7:56.
c MWM Mungu, Uungu—Mungu Baba.

21 Na tukawaona [a]malaika watakatifu, na wale [b]waliotakaswa mbele ya kiti chake cha enzi, wakimwabudu Mungu, na Mwanakondoo, ambao [c]humwabudu yeye milele na milele.

22 Na sasa, baada ya ushuhuda mwingi uliokwisha kutolewa juu yake, huu ni [a]ushuhuda, wa mwisho wa zote, ambao tunautoa juu yake: Kwamba [b]yu hai!

23 Kwani [a]tulimwona, hata mkono wa kuume wa [b]Mungu; na tukasikia sauti ikitushuhudia kuwa yeye ndiye [c]Mzaliwa Pekee wa Baba—

24 Kwamba kwa [a]yeye, na kwa njia yake, na kutoka kwake, [b]dunia zipo na ziliumbwa, na waliomo ni [c]wana na mabinti wa Mungu.

25 Na hii tuliona pia, na tunalishuhudia, kwamba [a]malaika wa Mungu aliye kuwa mwenye mamlaka katika uwepo wa Mungu, ambaye aliasi dhidi ya Mwana Pekee ambaye Baba alimpenda na ambaye alikuwa katika kifua cha Baba, alitupwa chini kutoka katika uwepo wa Mungu na Mwana,

26 Na aliitwa Mpotevu, kwa kuwa mbingu zililia juu yake—alikuwa [a]Lusiferi, mwana wa asubuhi.

27 Nasi tuliona, na lo, [a]ameanguka! ameanguka, hata yule mwana wa asubuhi!

28 Na wakati tukiwa bado katika Roho, Bwana alituamuru kuwa tuliandike ono hili; kwani tulimwona Shetani, yule [a]nyoka wa zamani, aitwaye [b]ibilisi, ambaye [c]alimwasi Mungu, na anataka kuutoa ufalme wa Mungu wetu na Kristo wake—

29 Kwa hiyo, yeye hufanya [a]vita na watakatifu wa Mungu, na kuwazingira.

30 Na tuliona ono la mateso ya wale ambao alifanya vita nao na kuwashinda, kwani hivi ndivyo sauti ya Bwana ilikuja kwetu:

31 Hivyo ndivyo asemavyo Bwana kuhusu wale wote wanaojua uwezo wangu, na kufanywa washiriki wake, na wakaruhusu uwezo wa ibilisi [a]uwashinde, na kuukana ukweli na kuukataa uwezo wangu—

32 Hao ndiyo walio [a]wana wa [b]upotevu, ambao ndiyo nisemao kuwa ingekuwa heri kwao kama wasingalizaliwa;

33 Kwani wao ni vyombo vya ghadhabu, vilivyohukumiwa

21 *a* Mt. 25:31; M&M 130:6–7; 136:37.
b MWM Utakaso.
c MWM Kuabudu.
22 *a* MWM Ushuhuda.
b M&M 20:17.
23 *a* MWM Yesu Kristo—Kuonekana kwa Kristo baada ya kifo.
b MWM Mungu, Uungu—Mungu Baba.
c Yn. 1:14. MWM Mzaliwa Pekee.
24 *a* Ebr. 1:1–3; 3 Ne. 9:15; M&M 14:9; 93:8–10.
b Musa 1:31–33; 7:30. MWM Umba, Uumbaji.
c Mdo. 17:28, 29; Ebr. 12:9. MWM Wana na Mabinti za Mungu.
25 *a* M&M 29:36–39; Musa 4:1–4. MWM Ibilisi.
26 *a* Isa. 14:12–17. MWM Lusiferi.
27 *a* Lk. 10:18.
28 *a* Ufu. 12:9.
b MWM Ibilisi.
c MWM Vita Mbinguni.
29 *a* Ufu. 13:7; 2 Ne. 2:18; 28:19–23.
31 *a* MWM Ukengeufu.
32 *a* MWM Wana wa Upotevu.
b M&M 76:26; Musa 5:22–26.

kuteseka kwa ghadhabu ya Mungu, pamoja na ibilisi na malaika zake milele;

34 Kuhusu niliyemsema hakuna [a]msamaha katika ulimwengu huu wala katika ulimwengu ujao—

35 Akiwa [a]amemkana Roho Mtakatifu baada ya kumpokea, na kumkana Mwana Pekee wa Baba, kwa kuwa [b]wanamsulubisha kwa nafsi zao na kumfedhehesha kwa dhahiri.

36 Hawa ndiyo wale ambao watakwenda katika [a]ziwa la moto na kiberiti, pamoja na ibilisi na malaika zake—

37 Na hao ndiyo pekee ambao [a]mauti ya pili yatakuwa na uwezo juu yao;

38 Ndiyo, amini, [a]hao ndiyo pekee ambao hawatakombolewa wakati wa Bwana ufikapo, baada ya kuteseka kwa ghadhabu yake.

39 Kwani wote waliobakia [a]watarejeshwa kwa [b]ufufuko wa wafu, kwa ushindi na utukufu wa [c]Mwanakondoo, aliyechinjwa, aliyekuwa katika kifua cha Baba kabla ya dunia hazijaumbwa.

40 Na hii ndiyo [a]injili, habari njema, ambayo sauti kutoka mbinguni ilitushuhudia—

41 Kwamba alikuja duniani, hata Yesu, ili [a]kusulubiwa kwa ajili ya ulimwengu, na [b]kuchukua dhambi za [c]ulimwengu, na [d]kuutakasa ulimwengu, na [e]kusafisha kutokana na udhalimu wote;

42 Ili kupitia kwake yeye wote wapate [a]kuokolewa wale ambao Baba aliwaweka katika uwezo wake na kuumbwa naye;

43 Yule amtukuzaye Baba, na kuokoa kazi zote za mikono yake, isipokuwa wale wana wa upotevu wanaomkana Mwana baada ya Baba kumfunua.

44 Kwa hiyo, yeye huwaokoa wote isipokuwa wao—watakwenda zao kuingia katika adhabu isiyo na mwisho, ambayo ni [a]adhabu [b]bila mwisho, ambayo ni adhabu ya milele, kutawala na [c]ibilisi na malaika wake milele, mahali ambamo [d]funza wao hawafi, wala moto hauzimiki, ambayo ndiyo mateso yao—

45 Na [a]mwisho wake, wala mahali pake, wala mateso yao, hakuna mwanadamu ajuaye;

46 Wala haikufunuliwa, wala

34*a* Mt. 12:31–32. MWM Samehe.
35*a* 2 Pet. 2:20–22; Alma 39:6. MWM Dhambi isiyo sameheka.
b Ebr. 6:4–6; 1 Ne. 19:7; M&M 132:27.
36*a* Ufu. 19:20; 20:10; 21:8; 2 Ne. 9:16; 28:23; Alma 12:16–18; M&M 63:17.
37*a* MWM Mauti ya Kiroho.
38*a* MWM Wana wa Upotevu.
39*a* MY watakombolewa; tazama aya 38. Wote watafufuliwa. Tazama Alma 11:41–45. MWM Huisha.
b MWM Ufufuko.
c MWM Yesu Kristo.
40*a* 3 Ne. 27:13–22. MWM Injili; Mpango wa Ukombozi.
41*a* MWM Kusulubiwa.
b Isa. 53:4–12; Ebr. 9:28.
c 1 Yoh. 2:1–2.
d MWM Utakaso.
e MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
42*a* MWM Wokovu.
44*a* MWM Hukumu.
b M&M 19:6–12.
c MWM Ibilisi.
d Isa. 66:24; Mk. 9:43–48.
45*a* M&M 29:28–29.

haifunuliwi, na wala haitafunuliwa kwa mwanadamu, isipokuwa kwao wao washiriki wake;

47 Hata hivyo, Mimi, Bwana, nawaonyesha wengi kwa ono, lakini nafunga tena mara moja;

48 Kwa hiyo, mwisho, upana, urefu, [a]kina na uchungu wake, hawaufahamu, wala hapana mtu yeyote isipokuwa wale [b]waliotawazwa kwa [c]hukumu hii.

49 Na tulisikia sauti ikisema: Andikeni ono hili, kwani lo, huu ndiyo mwisho wa ono la mateso ya wasiomcha Mungu.

50 Na tena, tunatoa ushuhuda—kuwa tuliona na kusikia, na huu ni [a]ushuhuda wa injili ya Kristo kuhusu wao watakaotokea katika [b]ufufuko wa wenye haki—

51 Hawa ni wale ambao wameupokea ushuhuda wa Yesu, na [a]kuliamini jina lake, na [b]wakabatizwa kwa [c]jinsi ya kuzikwa kwake, kwa [d]kuzikwa majini katika jina lake, na hii ni sawa na amri ambazo amezitoa—

52 Kwa kushika amri waweze [a]kuoshwa na [b]kusafishwa kutokana na dhambi zao zote, na kumpokea Roho Mtakatifu kwa kuwekewa [c]mikono na yule ambaye [d]ametawazwa na kufungwa kwa [e]uwezo huu;

53 Na ambaye hushinda kwa imani, na [a]kutiwa muhuri na [b]Roho Mtakatifu wa ahadi, ambaye Baba humpeleka juu ya wale wote walio haki na kweli.

54 Hawa ndiyo wale walio wa kanisa la [a]Mzaliwa wa Kwanza.

55 Hawa ndiyo wale ambao Baba amewapa vitu [a]vyote mikononi mwao—

56 Hawa ndiyo wale walio [a]makuhani na wafalme, ambao wamepokea utimilifu wake, na utukufu wake;

57 Na ni makuhani wa [a]Aliye Juu Sana, kwa mfano wa Melkizedeki, ambaye alikuwa kwa mfano wa [b]Henoko, ambaye alikuwa kwa [c]mfano wa Mwana Pekee.

58 Kwa hiyo, kama vile ilivyoandikwa, wao ndiyo [a]miungu, hata [b]wana wa [c]Mungu—

48 *a* Ufu. 20:1.
b MY hukumiwa, pelekea.
c Alma 42:22.
50 *a* MWM Ushuhuda.
b MWM Ufufuko.
51 *a* M&M 20:25–27, 37.
b MWM Batiza, Ubatizo.
c M&M 128:13.
d Rum. 6:3–5. MWM Batiza, Ubatizo—Ubatizo kwa kuzamishwa.
52 *a* 2 Ne. 9:23; Moro. 8:25–26.
b MWM Safi na Isiyo safi.
c MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu; Mikono, Kuweka juu ya.
d MWM Kutawaza, Kutawazwa.
e MWM Mamlaka.
53 *a* MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
b Efe. 1:13; M&M 88:3–5. MWM Roho Mtakatifu wa Ahadi.
54 *a* Ebr. 12:23; M&M 93:21–22. MWM Mzaliwa wa Kwanza.
55 *a* 2 Pet. 1:3–4; M&M 50:26–28; 84:35–38.
56 *a* Ku. 19:6; Ufu. 1:5–6; 20:6.
57 *a* MWM Kuhani, Ukuhani wa Melkizedeki.
b Mwa. 5:21–24. MWM Henoko.
c M&M 107:1–4.
58 *a* Zab. 82:1, 6; Yn. 10:34–36. MWM Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, uwezekano wa kuwa kama Baba wa Mbinguni.
b MWM Wana na Mabinti za Mungu.
c M&M 121:32. MWM Mungu, Uungu.

59 Kwa hiyo, vitu [a]vyote ni mali yao, iwe uzima au mauti, au vile vilivyopo, au vile vitakavyo kuwepo, vyote ni vyao nao ni wa Kristo, na Kristo ni wa Mungu.

60 Nao [a]watavishinda vitu vyote.

61 Kwa sababu hii, mtu yeyote na [a]asijisifie mwanadamu, bali na [b]ajisifie katika Mungu, ambaye [c]atawaweka maadui zake wote chini ya miguu yake.

62 Hawa [a]watakaa katika [b]uwepo wa Mungu na Kristo wake milele na milele.

63 Hawa ndiyo [a]wale watakaokuja pamoja naye, wakati [b]akija na mawingu ya mbinguni [c]kutawala dunia na watu wake.

64 Hawa ndiyo wale watakao kuwa na sehemu katika [a]ufufuo wa kwanza.

65 Hawa ndiyo wale watakao toka katika [a]ufufuo wa wenye haki.

66 Hawa ndiyo wale walioufikia [a]Mlima [b]Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, mahali pa mbinguni, patakatifu pa patakatifu.

67 Hawa ndiyo wale ambao wamefikia majeshi ya malaika yasiyo hesabika kwa mkutano mkuu na kanisa la [a]Henoko, na la [b]Mzaliwa wa Kwanza.

68 Hawa ndiyo wale ambao majina yao [a]yameandikwa mbinguni, mahali ambako Mungu na Kristo ni [b]waamuzi wa wote.

69 Hawa ndiyo wale watu [a]wenye haki [b]waliokamilishwa kwa njia ya Yesu aliye mpatanishi wa [c]agano jipya, aliye kamilisha [d]upatanisho huu mkamilifu kwa njia ya umwagikaji wa [e]damu yake yeye mwenyewe.

70 Hawa ndiyo wale ambao miili yao ni ya [a]selestia, ambayo [b]utukufu wake ni ule wa [c]jua, hata utukufu wa Mungu, wa juu kuliko wote, utukufu ambao umeandikwa ukifananishwa kama mwangaza wa jua la angani.

71 Na tena, tuliona ulimwengu wa [a]terestria, na tazama na lo, hawa ndiyo wale ambao

59 *a* Lk. 12:42–44; 3 Ne. 28:10; M&M 84:36–38.
60 *a* Ufu. 3:5; 21:7.
61 *a* Yn. 5:41–44; 1 Kor. 3:21–23.
b 2 Ne. 33:6; Alma 26:11–16. MWM Utukufu.
c M&M 49:6.
62 *a* Zab. 15:1–3; 24:3–4; 1 Ne. 15:33–34; Musa 6:57.
b M&M 130:7. MWM Uzima wa Milele.
63 *a* M&M 88:96–98. MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b Mt. 24:30.
c M&M 58:22. MWM Yesu Kristo—Utawala wa Kristo katika milenia.
64 *a* Ufu. 20:6.
65 *a* MWM Ufufuko.
66 *a* Isa. 24:23; Ebr. 12:22–24; Ufu. 14:1; M&M 84:2; 133:56.
b MWM Sayuni.
67 *a* M&M 45:9–12.
b Ebr. 12:23; M&M 76:53–54. MWM Mzaliwa wa Kwanza.
68 *a* MWM Kitabu cha Uzima.
b MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.
69 *a* M&M 129:3; 138:12.
b Moro. 10:32–33.
c MWM Agano Jipya na Lisilo na Mwisho.
d MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
e MWM Damu.
70 *a* M&M 88:28–29; 131:1–4; 137:7–10. MWM Utukufu wa Selestia.
b M&M 137:1–4.
c Mt. 13:43.
71 *a* M&M 88:30. MWM Utukufu wa Terestria.

ni wa terestria, ambao utukufu wao ni tofauti na wale wa kanisa la Mzaliwa wa Kwanza ambao wameupokea utimilifu wa Baba, hata kama ule wa [b]mwezi unavyo tofautiana na jua la angani.

72 Tazama, hawa ndiyo wale ambao walikufa [a]pasipo na [b]sheria;

73 Na pia ndiyo [a]roho za watu waliowekwa [b]kifungoni, ambao Mwana aliwatembelea, na [c]kuwahubiria [d]injili, ili kwamba wahukumiwe katika mwili kama wahukumiwavyo wanadamu;

74 Na ni wale ambao hawakuupokea [a]ushuhuda wa Yesu katika mwili, lakini baadaye waliupokea.

75 Hawa ndiyo wale ambao ni watu wenye kuheshimiwa duniani, ambao walipofushwa kwa ujanja wa wanadamu.

76 Hawa ndiyo wale ambao hupata utukufu wake, lakini siyo utimilifu wake.

77 Hawa ndiyo wale ambao hupata uwepo wa Mwana, lakini siyo utimilifu wa Baba.

78 Kwa hiyo, wana [a]miili ya terestria, na siyo miili ya selestia, na hutofautiana katika utukufu kama vile mwezi unavyo tofautiana na jua.

79 Hawa ndiyo wale ambao si [a]majasiri katika ushuhuda wa Yesu; kwa hiyo, hawatapokea taji la utukufu wa ufalme wa Mungu wetu.

80 Na sasa huu ndiyo mwisho wa ono ambalo tuliliona la miili ya terestria, ambalo Bwana alituamuru sisi kuandika wakati tulipokuwa bado katika Roho.

81 Na tena, tuliona utukufu wa [a]telestia, ambao ni utukufu ulio mdogo, kama vile utukufu wa nyota unavyo tofautiana na ule utukufu wa mwezi katika anga.

82 Hawa ndiyo wale ambao hawakuipokea injili ya Kristo, wala [a]ushuhuda wa Yesu.

83 Hawa ndiyo wale ambao hawamkatai Roho Mtakatifu.

84 Hawa ndiyo wale watupwao chini [a]jehanamu.

85 Hawa ndiyo wale ambao hawatakombolewa kutoka kwa [a]ibilisi hadi [b]ufufuo wa mwisho, hadi Bwana, hata Kristo [c]Mwanakondoo, atakapomaliza kazi yake.

86 Hawa ndiyo wale ambao hawapokei utimilifu wake katika ulimwengu wa milele, ila wa Roho Mtakatifu kwa njia ya huduma ya terestria;

87 Na wa terestria kwa njia ya [a]huduma ya selestia.

88 Na pia wa telestia hupata kuhudumiwa na malaika

71 *b* 1 Kor. 15:40–41.
72 *a* M&M 137:7, 9.
b MWM Sheria.
73 *a* Alma 40:11–14.
MWM Roho.
b M&M 88:99; 138:8.
MWM Jehanamu; Wokovu kwa ajili ya Wafu.
c 1 Pet. 3:19–20; 4:6; M&M 138:28–37.
d MWM Injili.
74 *a* MWM Ushuhuda.
78 *a* 1 Kor. 15:40–42.
79 *a* M&M 56:16.
81 *a* M&M 88:31.
MWM Utukufu wa Telestia.
82 *a* M&M 138:21.
84 *a* 2 Ne. 9:12; Alma 12:11.
MWM Jehanamu.
85 *a* MWM Ibilisi.
b Alma 11:41; M&M 43:18; 88:100–101.
c MWM Mwanakondoo wa Mungu.
87 *a* M&M 138:37.

ambao wameteuliwa kwa ajili ya kuwahudumia wao, au wale ambao huteuliwa kuwa roho watumikao kwa ajili yao; kwa kuwa watakuwa warithi wa wokovu.

89 Na hivi tuliona, katika ono la mbinguni, utukufu wa telestia, ipitayo akili zote;

90 Na hakuna mtu ajuaye isipokuwa yule ambaye Mungu amemfunulia.

91 Na hivi tuliona utukufu wa terestria iizidiyo katika kila kitu utukufu wa telestia, hata katika utukufu, na katika uwezo, na katika nguvu, na katika utawala.

92 Na hivi tuliona utukufu wa selestia, ukizidi nyingine katika vitu vyote—mahali ambapo Mungu, hata Baba, hutawala juu ya kiti chake cha enzi milele na milele;

93 Ambaye mbele ya kiti chake cha enzi vitu vyote husujudu kwa upole na [a]unyenyekevu, na kumpa yeye utukufu milele na milele.

94 Wale waishio katika [a]uwepo wake ni wa kanisa la [b]Mzaliwa wa Kwanza; nao huona kama wanavyoonekana, na [c]kujua kama wanavyojulikana, wakiwa wamepokea utimilifu wake na [d]neema yake;

95 Naye huwafanya kuwa [a]sawa katika uwezo, na katika nguvu, na katika utawala.

96 Na utukufu wa selestia ni moja, kama vile utukufu wa [a]jua ni mbali.

97 Na utukufu wa terestria ni mmoja, kama vile utukufu wa mwezi ni mbali.

98 Na utukufu wa telestia ni mmoja, kama vile utukufu wa nyota ni moja; maana iko tofauti ya utukufu hata kati ya utukufu wa nyota na nyota katika ulimwengu wa telestia.

99 Kwani hawa ndiyo wale ambao ni wa [a]Paulo, na Apolo, na wa Kefa.

100 Hawa ndiyo wale ambao husema kuna wale wa huyu na wengine wa mwingine—wengine wa Kristo na wengine wa Yohana, na wengine wa Musa, na wengine wa Elia, na wengine wa Esaya, na wengine wa Isaya, na wengine wa Henoko;

101 Lakini hawakuipokea injili, wala ushuhuda wa Yesu, wala manabii, wala [a]agano lisilo na mwisho.

102 Mwisho wa wote, hawa wote ni wale ambao hawatakusanywa pamoja na watakatifu, [a]kulakiwa kwenye [b]kanisa la Mzaliwa wa Kwanza, na kupokelewa mawinguni.

103 Hawa ndiyo [a]wale [b]waongo, na wachawi, na [c]wazinzi, na makahaba, na yeyote apendaye na kufanya uwongo.

104 Hawa ndiyo wale ambao huteseka kwa [a]ghadhabu ya Mungu duniani.

93*a* MWM Uchaji.
94*a* M&M 130:7.
b MWM Mzaliwa wa Kwanza.
c 1 Kor. 13:12.
d MWM Neema.
95*a* M&M 29:13; 78:5–7; 84:38; 88:107; 132:20.
96*a* 1 Kor. 15:40–41.
99*a* 1 Kor. 3:4–7, 22.
101*a* MWM Agano Jipya na Lisilo na Mwisho.
102*a* 1 The. 4:16–17; M&M 88:96–98.
b M&M 78:21.
103*a* Ufu. 21:8; M&M 63:17–18.
b MWM Kusema uongo.
c MWM Uzinzi.
104*a* MWM Hukumu.

105 Hawa ndiyo wale ambao [a]huadhibiwa kwa moto wa milele.

106 Hawa ndiyo wale ambao hutupwa chini [a]jehanamu na [b]kuteseka na ghadhabu ya [c]Mwenyezi Mungu, hadi wakati [d]mtimilifu, wakati Kristo a [e]takapowaweka maadui zake wote chini ya miguu yake, na [f]kukamilisha kazi yake;

107 Wakati atakapoutoa ufalme, na kuukabidhi kwa Baba, pasipo doa, akisema: Nimeshinda na [a]nalikanyaga [b]kinu peke yangu, hata kinu cha kushindikia mvinyo wa ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.

108 Ndipo atakapovikwa taji la utukufu wake, na kukaa juu ya [a]kiti cha enzi ya uwezo wake na kutawala milele na milele.

109 Lakini tazama, na lo, tuliona utukufu na wakazi wa ulimwengu wa telestia, kwamba walikuwa hawahesabiki kama vile nyota katika anga la mbingu, au kama mchanga ulio ufukoni mwa bahari;

110 Na tulisikia sauti ya Bwana ikisema: Hawa wote watapiga magoti, na kila ulimi [a]utakiri kwake aketiye juu ya kiti cha enzi milele na milele;

111 Kwani watahukumiwa kulingana na matendo yao, na kila mtu atapokea kulingana na [a]matendo yake, na utawala wake, katika [b]makao yaliyotayarishwa;

112 Nao watakuwa watumishi wa Aliye Juu Sana; lakini [a]mahali Mungu na Kristo [b]wakaapo hawawezi kuja, milele na milele.

113 Huu ni mwisho wa ono ambalo tuliliona, ambalo tuliamriwa kuliandika wakati tulipokuwa bado katika Roho.

114 Lakini ni [a]makuu na ya ajabu matendo ya Bwana, na [b]siri za ufalme wake ambazo alizionyesha kwetu, ambazo hupita akili zote katika utukufu, na katika nguvu, na katika utawala;

115 Ambayo alituamuru tusiyaandike wakati tulipokuwa tungali katika Roho, na ambayo [a]hajaruhusu mwanadamu ayanene;

116 Wala mwanadamu [a]hawezi kuyafunua, kwani ni ya kuonwa tu na [b]kueleweka kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, ambaye Mungu huwapa wale wampendao, na kuwatakasa mbele zake;

117 Hao huwapa heshima hii ya kuona na kutambua wenyewe;

118 Ili kwa njia ya uwezo na mafunuo ya Roho, wakati wakiwa katika mwili, waweze

105*a* Yuda 1:7.
106*a* MWM Jehanamu.
b M&M 19:3–20.
c M&M 87:6.
d Efe. 1:10.
e 1 Kor. 15:24–28.
f Ebr. 10:14.
107*a* Ufu. 19:15; M&M 88:106; 133:46–53.
b Mwa. 49:10–12; Isa. 63:1–3.
108*a* M&M 137:3.
110*a* Flp. 2:9–11; Mos. 27:31.
111*a* Ufu. 20:12–13. MWM Matendo.
b Yn. 14:2; M&M 59:2; 81:6.
112*a* M&M 29:29.
b Ufu. 21:23–27.
114*a* Ufu. 15:3; Morm. 9:16–18; Musa 1:3–5.
b Yak. (KM) 4:8.
115*a* 2 Kor. 12:4.
116*a* 3 Ne. 17:15–17; 19:32–34.
b 1 Kor. 2:10–12.

kustahili uwepo wake katika ulimwengu wa utukufu.

119 Na utukufu, na heshima, na utawala vina Mungu na Mwanakondoo, milele na milele. Amina.

SEHEMU YA 77

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii huko Hiram, Ohio, kama Machi 1832. Historia ya Joseph Smith inaeleza, "Kuhusiana na tafsiri, ya Maandiko, nilipokea ufafanuzi ufuatao wa Ufunuo wa Mt. Yohana."

1–4, Wanyama wana roho na wataishi katika furaha ya milele juu ya dunia isiyo kufa; 5–7, Dunia hii itaishi kwa muda wa miaka 7000; 8–10, Malaika mbalimbali huirejesha injili na kuhudumu duniani; 11, Waliotiwa muhuri kwa 144,000; 12–14, Kristo atakuja mwanzoni mwa miaka ya elfu saba; 15, Manabii wawili watainuliwa kwa taifa la Israeli.

S. [a]Bahari ya kioo iliyozungumzwa na Yohana, mlango 4 na mstari wa 6 wa Ufunuo ni nini?

J. Ni [b]dunia, katika hali yake ya kutakaswa, isiyokufa, na ya [c]milele.

2 S. Tuelewe nini kwa wanyama wanne, waliozungumzwa katika mstari huo huo?

J. Ni maneno ya [a]ishara, yaliyotumiwa na Mfunuzi, Yohana, katika kueleza [b]mbingu, [c]peponi ya Mungu, [d]furaha ya mwanandamu, na ya wanyama, na ya vitu vitambaavyo, na ya ndege wa angani; na kile kilicho kiumbe cha kiroho katika kufanana na kile kilicho cha kimwili; na kile kiumbe cha kimwili katika kufanana na kile cha kiroho; [e]roho ya mwanadamu katika kufanana na mwili wake, vivyo hivyo pia roho ya [f]mnyama, na kila kiumbe ambacho Mungu amekiumba.

3 S. Je, wanyama wale wanne inamaanisha wanawakilisha wanyama maalumu tu, au wanawakilisha wanyama mbalimbali?

J. Wanawakilisha wanyama maalumu wanne, ambao walionyeshwa kwa Yohana, ili kuwakilisha utukufu wa makundi ya viumbe katika mpangilio wao uliokusudiwa au [a]eneo la uumbaji, katika kufurahia [b]furaha yao ya milele.

4 S. Tuelewe nini kwa macho na mabawa ambayo wanyama wale walikuwa nayo?

J. Macho yao yanawakilisha

77 1*a* M&M 130:6–9.
b M&M 88:17–20, 25–26.
c MWM Dunia—Hali ya mwisho ya dunia; Utukufu wa Selestia.
2*a* MWM Uashiriaji.
b MWM Mbinguni.
c MWM Peponi.
d MWM Shangwe.
e Eth. 3:15–16; Ibr. 5:7–8. MWM Roho.
f Musa 3:19.
3*a* M&M 93:30; Musa 3:9.
b M&M 93:33–34.

nuru na [a]maarifa, maana yake, wamejaa maarifa; na mabawa yao yanawakilisha [b]uwezo, wa kutembea, wa kutenda, na kadhalika.

5 S. Tuelewe nini kwa [a]wazee ishirini na wanne, waliozungumzwa na Yohana?

J. Tuelewe kuwa wazee hawa aliowaona Yohana, walikuwa wazee waliokuwa [b]waaminifu katika kazi ya huduma na walikufa; na walikuwa wa makanisa yale [c]saba, na walikuwa katika peponi ya Mungu.

6 S. Tuelewe nini kwa kitabu ambacho Yohana alikiona, ambacho kilikuwa kimetiwa [a]lakiri nyuma kwa lakiri saba?

J. Tuelewe kuwa inajumuisha mapenzi yaliyofunuliwa, [b]siri, na kazi za Mungu; mambo yake yaliyofichika ya utawala wake kuhusu [c]dunia katika kipindi cha miaka elfu saba cha kudumu kwake, au katika uhai wake.

7 S. Tuelewe nini kwa lakiri saba zilizotiwa?

J. Tuelewe kuwa muhuri wa kwanza ni juu ya mambo ya miaka [a]elfu moja ya kwanza, na wa pili pia ni juu ya miaka elfu ya pili, na kuendelea hadi wa saba.

8 S. Tuelewe nini kwa malaika wanne, waliozungumzwa katika mlango wa 7 na mstari wa 1 wa Ufunuo?

J. Tuelewe kuwa ni malaika wanne waliotumwa kutoka kwa Mungu, ambao wamepewa uwezo juu ya pembe nne za nchi, kuponya uhai au kuangamiza; hawa ndiyo wale wenye [a]injili isiyo na mwisho ya kuhubiri kwa kila taifa, kabila, lugha, na watu; wakiwa na uwezo wa kuzifunga mbingu, kuwafungia maisha, au kuwatupa chini [b]sehemu ya giza.

9 S. Tuelewe nini kwa malaika kushuka kutoka mashariki, Ufunuo mlango wa 7 na mstari wa 2?

J. Tuelewe kuwa malaika ashukaye kutoka mashariki ni yule aliyepewa muhuri wa Mungu aliye hai kwa ajili ya makabila kumi na mawili ya [a]Israeli; kwa hiyo, akilia kwa malaika wanne wenye injili isiyo na mwisho, akisema: Msidhuru nchi, wala bahari, wala miti, hata tutakapo kwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya [b]vipaji vya nyuso zao. Na, ikiwa mtaipokea, huyu ndiye [c]Elia atakayekuja kuyakusanya pamoja makabila ya Israel na [d]kurejesha mambo yote.

10 S. Mambo yaliyozungumzwa katika mlango huu yatamalizika wakati gani?

J. Yatamalizika katika kipindi cha miaka [a]elfu sita, au kufunguliwa kwa lakiri ya sita.

11 S. Tuelewe nini kwa kutiwa muhuri kwa watu [a]mia moja na

4 *a* MWM Maarifa.
b MWM Uwezo.
5 *a* Ufu. 4:4, 10.
b Ufu. 14:4–5.
c Ufu. 1:4.
6 *a* Ufu. 5:1.
b MWM Siri za Mungu.
c MWM Dunia.
7 *a* M&M 88:108–110.
8 *a* Ufu. 14:6–7.
b Mt. 8:11–12; 22:1–14; M&M 133:71–73.
9 *a* Ufu. 7:4–8.
b Eze. 9:4.
c MWM Elia.
d MWM Urejesho wa Injili.
10 *a* Ufu. 6:12–17.
11 *a* Ufu. 14:3–5.

arobaini na nne elfu kutoka makabila yote ya Israeli—kumi na wawili elfu kutoka kila kabila?

J. Tuelewe kuwa wale waliotiwa muhuri ni [b]makuhani wakuu, waliotawazwa katika mpango mtakatifu wa Mungu! kusimamia injili isiyo na mwisho; kwani wao ndiyo waliotawazwa kutoka kila taifa, kabila, lugha, na watu, na malaika ambao walipewa uwezo juu ya mataifa ya dunia, kuwaleta wengi kadiri iwezekanavyo katika kanisa la [c]Mzaliwa wa Kwanza.

12 S. Tuelewe nini kwa kupigwa kwa [a]mabaragumu, yaliyotajwa katika mlango wa 8 wa Ufunuo?

J. Tuelewe kuwa kama vile Mungu alivyoumba ulimwengu katika siku sita, na siku ya saba akamaliza kazi yake, na [b]akaitakasa, na pia akamtengeneza mwanadamu kutoka [c]mavumbi ya dunia, hata hivyo, mwanzoni mwa miaka elfu saba Bwana Mungu [d]ataitakasa dunia, na kukamilisha wokovu wa mwanadamu, na [e]kuvihukumu vitu vyote, na [f]atavikomboa vitu vyote, isipokuwa kile ambacho hakukiweka ndani ya uwezo wake, wakati atakapokuwa amekwisha tia muhuri vitu vyote, hata mwisho wa vitu vyote; na kupigwa kwa parapanda za malaika saba ni kutayarisha na kumalizika kwa kazi yake, mwanzoni mwa miaka ya elfu saba—kutayarisha njia kabla ya wakati wa kuja kwake.

13 S. Ni lini yatatimizwa mambo yaliyoandikwa katika mlango wa 9 wa Ufunuo?

J. Yatatimizwa baada ya kufunguliwa kwa lakiri ya saba, kabla ya kuja kwa Kristo.

14 S. Tuelewe nini kwa kitabu kidogo [a]kilicholiwa na Yohana, kama ilivyotajwa katika mlango wa 10 wa Ufunuo?

J. Tuelewe kuwa ilikuwa ni kazi na ibada, kwake yeye ya [b]kuyakusanya makabila ya Israeli; tazama, huyu ndiye Elia, ambaye, kama ilivyoandikwa, ni lazima atakuja naye [c]atarejesha mambo yote.

15 S. Nini kieleweke kwa [a]mashahidi wawili, katika mlango wa kumi na moja ya Ufunuo?J. Ieleweke kuwa ni manabii wawili ambao watainuliwa kwa [b]taifa la Kiyahudi katika [c]siku za mwisho, wakati wa [d]urejesho, na wa kutoa unabii kwa Wayahudi baada ya kukusanywa na kujenga mji wa Yerusalemu katika [e]nchi ya baba zao.

11 *b* MWM Kuhani Mkuu.
c M&M 76:51–70. MWM Mzaliwa wa Kwanza.
12 *a* Ufu. 8:2.
b Mwa. 2:1–3; Ku. 20:11; 31:12–17; Mos. 13:16–19; Musa 3:1–3; Ibr. 5:1–3.
c Mwa. 2:7.
d M&M 88:17–20.
e MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.
f MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
14 *a* Eze. 2:9–10; 3:1–4; Ufu. 10:10.
b MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
c Mt. 17:11.
15 *a* Ufu. 11:1–14.
b MWM Wayahudi.
c MWM Siku za Mwisho.
d MWM Urejesho wa Injili.
e Amo. 9:14–15.

SEHEMU YA 78

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 1 Machi 1832. Katika siku hiyo, Nabii pamoja na viongozi wengine walikusanyika ili kujadili shughuli ya Kanisa. Ufunuo huu awali ulikuwa ukimwelekeza Nabii, Sidney Rigdon na Newel K. Whitney kusafiri kwenda Missouri na kuanzisha duka la Kanisa na kazi za uchapishaji kwa kuunda "kampuni" ambayo ingesimamia jitihada hizi, ikizalisha fedha kwa ajili ya kuanzisha Sayuni na kwa manufaa ya watu masikini. Kampuni hii, iliyojulikana kama United Firm (Kampuni ya Ushirika) ilianzishwa Aprili 1832 na kuvunjika 1834 (ona sehemu ya 82) Wakati Fulani baada ya kuvunjika kwake, chini ya maelekezo ya Joseph Smith, sentesi kama "shughuli za ghala kwa ajili ya masikini" lilitumika badala ya "duka la bidhaa na kiwanda cha uchapishaji" katika ufunuo, na neno "shirika" lilitumika badala ya neno "kampuni."

1–4, Watakatifu yawapasa kutenngeneza na kuanzisha ghala; 5–12, Matumizi ya busara ya mali zao yatawaelekeza kwenye wokovu; 13–14, Kanisa lazima liwe huru na mamlaka ya kidunia; 15–16, Mikaeli (Adamu) hutumikia chini ya maelekezo ya Mtakatifu (Kristo); 17–22, Heri walio waaminifu, kwa maana watarithi vitu vyote.

BWANA alisema kwa Joseph Smith, Mdogo, akisema: Nisikilizeni, asema Bwana Mungu wenu, ninyi ambao mmetawazwa katika [a]ukuhani mkuu wa kanisa langu, ninyi mliojikusanya wenyewe pamoja;

2 Na sikilizeni [a]ushauri wake [b]aliyewatawaza ninyi kutoka juu, ambaye ataongea katika masikio yenu maneno ya hekima, ili wokovu uweze kuwa kwenu katika jambo lile mlilolileta mbele zangu, asema Bwana Mungu.

3 Kwani amini ninawaambia, wakati umefika, na sasa u karibu; na tazama, na lo, hapana budi kuwe na [a]utaratibu wa watu wangu, katika kurekebisha na kuanzisha mambo ya [b]ghala kwa ajili ya watu wangu walio [c]maskini, kote hapa na katika nchi ya [d]Sayuni—

4 Kwa uanzishaji na kwa utaratibu wa kudumu na usio na mwisho kwa kanisa langu, ili kuendeleza kazi, ambayo mmeahidi wenyewe, kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu, na kwa ajili ya utukufu wa Baba yenu aliye mbinguni;

5 Ili muweze kuwa [a]sawa katika kugawana vitu vya mbinguni, ndiyo, na vitu vya duniani

78 1*a* MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
2*a* MWM Ushauri.
b MWM Kutawaza, Kutawazwa.
3*a* M&M 82:11–12, 15–21.
b M&M 72:9–10; 83:5–6.
c M&M 42:30–31. MWM Ustawi.
d M&M 57:1–2.
5*a* M&M 49:20. MWM Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.

pia, kwa ajili ya kupata vitu vya mbinguni.

6 Kwani msipokuwa sawa katika vitu vya duniani hamwezi kuwa sawa katika kupata vitu vya mbinguni;

7 Kwani kama mnataka kwamba niwape mahali katika ulimwengu wa [a]selestia, lazima [b]mjitayarishe wenyewe kwa [c]kufanya mambo niliyo waamuru na ninayoyataka kutoka kwenu ninyi.

8 Na sasa, amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana, ni muhimu kwamba mambo yote yafanyike kwa [a]utukufu wangu, na ninyi ambao mmeungana pamoja katika [b]utaratibu huu;

9 Au, kwa maneno mengine, acha mtumishi wangu Newel K. Whitney na mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na mtumishi wangu Sidney Rigdon wakae kwenye kikao pamoja na watakatifu walioko katika Sayuni;

10 Vinginevyo [a]Shetani anatafuta kuigeuza mioyo yao mbali na ukweli, ili aweze kuwapofusha na wasielewe mambo yaliyotayarishwa kwa ajili yao.

11 Kwa hiyo, amri ninaitoa kwenu, kutayarisha na kujisimamia wenyewe kwa mkataba, au [a]agano lisilo na mwisho ambalo haliwezi kuvunjwa.

12 Na yule alivunjaye atapoteza ofisi yake na nafasi yake katika kanisa, naye atapelekwa kwa [a]karamu ya Shetani hadi siku ya ukombozi.

13 Tazama, hili ni tayarisho ambalo kwalo ninawatayarisha ninyi, na msingi, na utaratibu ambao ninautoa kwenu, ambao kwa huo muweze kutimiza amri mlizopewa;

14 Ili kwa majaliwa yangu, licha ya [a]taabu itakayoshuka juu yenu, kwamba kanisa liweze kusimama huru juu ya viumbe wengine chini ya ulimwengu wa selestia.

15 Ili muweze kuja kwenye [a]taji lililotayarishwa kwa ajili yenu, na kufanywa [b]watawala juu ya falme nyingi, asema Bwana Mungu, Mtakatifu wa Sayuni, ambaye aliweka misingi ya [c]Adamu-Ondi-Amani;

16 Ambaye alimteua [a]Mikaeli mtawala wenu, na kuisimamisha miguu yake, na kumweka juu, na kutoa kwake funguo za wokovu chini ya ushauri na maelekezo ya Mtakatifu, ambaye hana mwanzo wa siku zake au mwisho wa uhai.

17 Amini, amini, ninawaambia, ninyi ni watoto wadogo, nanyi bado hamjaelewa jinsi baraka kuu Baba alizo nazo katika mikono yake mwenyewe na amezitayarisha kwa ajili yenu;

18 Na hamwezi [a]kustahmili

7 *a* MWM Utukufu wa Selestia.
b M&M 29:8; 132:3.
c M&M 82:10.
8 *a* Musa 1:39.
b M&M 92:1.
10 *a* MWM Ibilisi.
11 *a* MWM Agano.
12 *a* 1 Kor. 5:5; M&M 82:21; 104:8–10.
14 *a* M&M 58:2–4.
15 *a* MWM Kuinuliwa; Taji.
b Ufu. 5:10; M&M 76:56–60; 132:19.
c MWM Adamu-ondi-Amani.
16 *a* M&M 27:11; 107:54–55. MWM Adamu.
18 *a* Yn. 16:12; 3 Ne. 17:2–3; M&M 50:40.

mambo yote kwa sasa; hata hivyo, changamkeni, kwa kuwa [b]nitawaongoza. Ufalme ni wenu na baraka zake ni zenu na utajiri wa [c]milele ni wenu.

19 Na yule apokeaye vitu kwa [a]shukrani atatukuzwa; na vitu vya dunia hii ataongezewa, hata [b]mara mia, ndiyo, na zaidi.

20 Kwa hiyo, fanyeni mambo niliyowaamuru, asema Mkombozi wenu, hata Mwana [a]Amani, atayarishaye vitu vyote kabla ya [b]kuwachukua;

21 Kwani ninyi ni [a]kanisa la Mzaliwa wa Kwanza, naye [b]atawachukua katika wingu, na kumgawia kila mtu sehemu yake.

22 Na yule aliye mwaminifu na [a]msimamizi mwenye [b]busara atarithi vitu [c]vyote. Amina.

SEHEMU YA 79

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Hiram, Ohio, 12 Machi 1832.

1–4, Jared Carter anaitwa kuhubiri injili kwa msaada wa Mfariji.

Amini ninawaambia, kuwa haya ndiyo mapenzi yangu kwamba mtumishi wangu Jared Carter aende tena katika nchi za mashariki, kutoka mahali hadi mahali, na kutoka mji hadi mji, katika uwezo uliotokana na [a]kutawazwa kwake, akitangaza habari njema za shangwe kuu, hata injili isiyo na mwisho.

2 Nami nitamletea [a]Mfariji, atakaye mfundisha ukweli na kumwonyesha njia ya kwenda;

3 Na kadiri atakavyokuwa mwaminifu, nitamtuza tena miganda.

4 Kwa hiyo, moyo wako na ufurahi, mtumishi wangu Jared Carter, na [a]usiogope, asema Bwana wako, hata Yesu Kristo. Amina.

SEHEMU YA 80

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, kwenda kwa Stephen Burnett, Hiram, Ohio, 7 Machi 1832.

18 *b* M&M 112:10.
c mwm Uzima wa Milele.
19 *a* Mos. 2:20–21. mwm Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
b Mt. 19:29.
20 *a* M&M 95:17.
b 1 The. 4:17.
21 *a* M&M 76:53–54.
b M&M 88:96–98.
22 *a* mwm Msimamizi, Usimamizi.
b M&M 72:3–4.
c M&M 84:38.
79 1 *a* M&M 52:38. mwm Kutawaza, Kutawazwa.
2 *a* Yn. 14:26. mwm Mfariji.
4 *a* M&M 68:5–6.

1–5, Stephen Burnett na Eden Smith wanaitwa kuhubiri katika mahali popote watakapochagua.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwako wewe mtumishi wangu Stephen Burnett: Nenda wewe, nenda wewe ulimwenguni na [a]ukahubiri injili kwa kila kiumbe kitakachokuwa chini ya sauti yako.

2 Na kwa vile unataka mwenza, nitakupa mtumishi wangu Eden Smith.

3 Kwa hiyo, nendeni na mkaihubiri injili yangu, iwe kaskazini au kusini, mashariki au magharibi, si kitu, kwani hamwezi kukosea.

4 Kwa sababu hiyo, yatangazeni mambo ambayo mmeyasikia, na hakika kuyaamini, na [a]kujua ni ya kweli.

5 Tazama, haya ndiyo mapenzi yake yeye [a]aliyewaita ninyi, Mkombozi wenu, hata Yesu Kristo. Amina.

SEHEMU YA 81

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Hiram, Ohio, 15 Machi 1832. Frederick G. Williams anaitwa kuwa kuhani mkuu na mshauri katika Urais wa Ukuhani Mkuu. Kumbukumbu za kihistoria zinaonyesha kuwa wakati ufunuo huu ulipopokelewa mnamo Machi 1832, ulimwita Jesse Gause katika ofisi ya ushauri kwa Joseph Smith katika Urais. Hata hivyo, aliposhindwa kuendelea katika mwenendo sahihi sawa na uteuzi huu, wito huu baadaye ulihamishiwa kwa Frederick G. Williams. Ufunuo huu (wa Machi 1832) uchukuliwe kama ni hatua muhimu ya kuelekea kwenye mfumo rasmi wa Urais wa Kwanza, wito maalumu wa ofisi ya mshauri katika baraza hilo na kuelezea heshima ya uteuzi huu. Ndugu Gause alitumikia kwa muda lakini alitengwa na Kanisa Desemba 1832. Ndugu Williams alitawazwa katika ofisi hii 18 Machi 1833.

1–2, Funguo za ufalme daima zinashikiliwa na Urais wa Kwanza; 3–7, Kama Frederick G. Williams ni mwaminifu katika huduma yake, atapata uzima wa milele.

Amini, amini, ninakuambia wewe mtumishi wangu Frederick G. Williams: Sikiliza sauti yake anenaye, neno la Bwana Mungu wako, na usikilize wito ambao umeitiwa, hata kuwa [a]kuhani mkuu katika kanisa langu, na mshauri kwa mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo;

2 Kwake yeye nimetoa [a]funguo za ufalme, ambazo daza Ukuhani.

80 1*a* Mk. 16:15.
4*a* mwm Ushuhuda.
5*a* mwm Ita, Itwa na Mungu, Wito.
81 1*a* mwm Kuhani Mkuu.
2*a* mwm Funguo

ima ni za [b]Urais wa Ukuhani Mkuu.

3 Kwa hiyo, amini ninamtambua na nitambariki yeye, na wewe pia, kadiri wewe utakavyokuwa mwaminifu katika ushauri, katika ofisi ambayo nimekuteua, kwa sala daima, kwa sauti na katika moyo wako, hadharani na faraghani, pia katika huduma yako katika kuitangaza injili katika nchi ya walio hai, na miongoni mwa ndugu zako.

4 Na katika kufanya mambo haya utakuwa umefanya mema makuu kwa wanadamu wenzako, na utakuwa umeukuza [a]utukufu wake aliye Bwana wako.

5 Kwa hiyo, uwe mwaminifu; simama katika ofisi ambayo nimekuteua; [a]wasaidie wadhaifu, inyooshe mikono iliyolegea, na [b]yaimarishe magoti yaliyo [c]dhaifu.

6 Na kama utakuwa mwaminifu hadi mwisho nawe utapata tuzo la [a]mwili usiokufa, na [b]uzima wa milele katika [c]makao ambayo nimeyatayarisha katika nyumba ya Baba yangu.

7 Tazama, na lo, haya ndiyo maneno ya Alfa na Omega, hata Yesu Kristo. Amina.

SEHEMU YA 82

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, katika Independence, Wilaya ya Jackson, Missouri, 26 Aprili 1832. Tukio hili lilikuwa la baraza kuu la makuhani wakuu na wazee wa Kanisa. Katika baraza hili, Joseph Smith alikubalika kama Rais wa Ukuhani Mkuu, ofisi ambayo hapo awali alikuwa ametawazwa katika mkutano wa makuhani wakuu, wazee, na waumini, huko Amherst, Ohio, 25 Januari 1832 (ona kichwa cha habari cha sehemu ya 75). Ufunuo huu ulirudia kusema maelekezo yaliyotolewa katika ufunuo wa awali (sehemu ya 78) wa kuanzisha kampuni—ijulikanayo kama Kampuni ya Ushirika (chini ya maelekezo ya Joseph Smith, neno "shirika" baadae lilikuja kutumika badala ya "kampuni")—ili kutawala duka la bidhaa la Kanisa na kazi za uchapishaji.

1–4, Na kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakiwa vingi; 5–7, Giza latawala katika ulimwengu; 8–13, Bwana analazimika wakati tukifanya asemayo Yeye; 14–18, Sayuni lazima iongezeke katika uzuri na utakatifu; 19–24, Kila mtu yampasa kutafuta ustawi wa jirani yake.

2*b* M&M 107:8–9, 22. MWM Urais wa Kwanza.
4*a* Musa 1:39.
5*a* Mos. 4:15–16.
b M&M 108:7.
c Isa. 35:3.
6*a* MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
b MWM Kuinuliwa; Uzima wa Milele.
c Yn. 14:2–3; M&M 59:2; 106:8.

Amini, amini, ninawaambia, watumishi wangu, kwamba kwa kuwa [a]mmesameheana ninyi kwa ninyi makosa yenu, hata Mimi, Bwana, ninawasamehe.

2 Hata hivyo, kuna watu miongoni mwenu ambao wametenda dhambi kupita kiasi; ndiyo, hata ninyi [a]nyote mmetenda dhambi; lakini amini ninawaambia, jihadharini kutoka sasa, na jiepusheni na dhambi, isije hukumu kali ikashuka juu ya vichwa vyenu.

3 Kwani yule aliyepewa [a]vingi kwake huyo [b]vitatakiwa vingi; na yule [c]aliyetenda dhambi dhidi ya [d]nuru kuu zaidi atapokea hukumu kuu zaidi.

4 Mlilingane jina langu kwa [a]mafunuo, nami nitayatoa kwenu; na kadiri msivyoyashika maneno yangu, ambayo ninawapa, mnakuwa wavunjaji wa sheria; na [b]haki na hukumu ni adhabu zilizowekwa kwa sheria yangu.

5 Kwa hiyo, lile nisemalo kwa mmoja ninalisema kwa wote: [a]Kesheni, kwani [b]adui anaeneza utawala wake, na [c]giza linatawala;

6 Na hasira ya Mungu inawaka dhidi ya wakazi wa dunia; na hakuna mtenda mema, kwani wote [a]wamepotoka.

7 Na sasa, amini ninawaambia, Mimi, Bwana, sitawahesabia [a]dhambi kwa makosa yenu; enendeni zenu na msitende dhambi tena; lakini [b]dhambi za awali zitamrudia yule atakayetenda dhambi tena, asema Bwana Mungu wenu.

8 Na tena, ninawaambia, ninawapa amri [a]mpya, ili muweze kufahamu mapenzi yangu kwenu;

9 Au, kwa maneno mengine, ninatoa kwenu maelekezo jinsi ya kuweza [a]kutenda mbele zangu, ili iweze kugeuka kwenu kwa ajili ya wokovu wenu.

10 Mimi, Bwana, [a]ninalazimika wakati ninyi mnapofanya ninayosema; lakini msipofanya ninayosema, ninyi hamna ahadi.

11 Kwa hiyo, amini ninawaambia, kuwa ni muhimu kwa watumishi wangu Edward Partridge na Newel K. Whitney, A. Sidney Gilbert na Sidney Rigdon, na mtumishi wangu Joseph Smith, na John Whitmer na Oliver Cowdery, na W. W. Phelps na Martin Harris wafungwe [a]pamoja kwa mkataba na agano ambalo haliwezi kuvunjika kwa kuvunja sheria, isipokuwa hukumu imefuata mara moja, katika usimamizi wenu mbalimbali—

82 1 *a* Mt. 6:14–15; M&M 64:9–11.
2 *a* Rum. 3:23.
3 *a* Lk. 12:48; Yak. (Bib.) 4:17. MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
b MWM Msimamizi, Usimamizi.
c MWM Dhambi; Ukengeufu.
d Yn. 15:22–24. MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
4 *a* MWM Ufunuo.
b MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
5 *a* MWM Kesha, Walinzi.
b MWM Ibilisi.
c MWM Giza, Kiroho.
6 *a* Rum. 3:12; M&M 1:16.
7 *a* MWM Dhambi.
b M&M 1:32–33; 58:43.
8 *a* Yn. 13:34.
9 *a* M&M 43:8.
10 *a* Yos. 23:14; 1 Fal. 8:23; M&M 1:38; 130:20–21. MWM Baraka, Bariki, Barikiwa; Mtiifu, Tii, Utii.
11 *a* M&M 78:3–7, 11–15.

12 Kusimamia masuala ya maskini, na mambo yote yahusianayo na uaskofu kote katika nchi ya Sayuni na katika nchi ya Kirtland;

13 Kwani nimeiweka wakfu nchi ya Kirtland katika wakati wangu mwenyewe kwa faida ya watakatifu wa Aliye Juu Sana, na kwa ajili ya [a]kigingi kwa Sayuni.

14 Kwani Sayuni lazima iongezeke katika uzuri, na katika utakatifu; mipaka yake lazima ipanuliwe; na vigingi vyake lazima viimarishwe; ndiyo, amini ninawaambia, [a]Sayuni lazima ichomoze na kuvaa [b]mavazi yake mazuri.

15 Kwa hiyo, ninatoa kwenu amri hii, kuwa jifungeni wenyewe kwa agano hili, na ifanyike kulingana na sheria za Bwana.

16 Tazama, na hii pia ndiyo hekima kwangu kwa faida yenu.

17 Nanyi mnapaswa kuwa [a]sawa, au kwa maneno mengine, mtakuwa na haki sawa juu ya mali, kwa ajili ya kusaidia kusimamia masuala yahusuyo usimamizi wenu, kila mtu kulingana na mahitaji na matakwa yake, ilimradi matakwa yake, ni ya haki—

18 Na hii yote ni kwa manufaa ya kanisa la Mungu aliye hai, ili kila mtu aweze kuongeza talanta yake, ili kila mtu aweze kuongeza [a]talanta zingine, ndiyo, hata mara mia, ambazo zinawekwa katika [b]ghala ya Bwana, na kuwa mali ya jumuiya ya kanisa lote—

19 Kila mtu akitafuta ustawi wa jirani yake, na kufanya mambo yote [a]kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

20 [a]Utaratibu huu nimeuteua ili uwe utaratibu usio na mwisho kwenu ninyi, na kwa warithi wenu, ilimradi kama hamtatenda dhambi.

21 Na mtu atakayetenda dhambi kinyume na agano hili, na kuushupaza moyo wake dhidi ya hilo, alishughulikiwa kulingana na sheria za kanisa langu, atatolewa kwa [a]karamu ya Shetani hadi siku ya ukombozi.

22 Na sasa, amini ninawaambia, na hii ndiyo hekima, jifanyeni marafiki kwa mali ya udhalimu, nao hawatawaangamiza.

23 Niachieni hukumu mimi peke yangu, kwani ni yangu nami [a]nitalipa: Amani na iwe kwenu; baraka zangu zitaendelea kuwa nanyi.

24 Kwani [a]ufalme bado ni wenu, na utakuwa nanyi hata milele, kama hamtaanguka kutoka uimara wenu. Hivyo ndivyo. Amina.

13 *a* Isa. 33:20; 54:2.
MWM Kigingi.
14 *a* MWM Sayuni.
b Isa. 52:1; M&M 113:7–8.
17 *a* M&M 51:3.
MWM Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.
18 *a* Mt. 25:14–30; M&M 60:13.
MWM Karama; Vipawa vya Roho.
b M&M 42:30–34, 55; 119:1–3.
MWM Ghala.
19 *a* M&M 88:67.
MWM Jicho, Macho.
20 *a* MWM Mpango wa Ushirika.
21 *a* M&M 104:8–10.
23 *a* Rum. 12:19; Morm. 3:15.
24 *a* Lk. 12:32; M&M 64:3–5.
MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.

SEHEMU YA 83

Ufunuo uliotolewa kupitia kwa Joseph Smith Nabii, huko Independence, Missouri, 30 Aprili 1832. Ufunuo huu ulipokelewa wakati Nabii alipokuwa amekaa katika baraza pamoja na viongozi wenzake wa kanisa.

1–4, Wanawake na watoto wanayo haki ya kudai matunzo kutoka kwa waume na baba zao; 5–6, Wajane na yatima wanayo haki ya kupata matunzo kutoka katika Kanisa.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, kwa nyongeza kwenye sheria za kanisa kuhusu wanawake na watoto, wale ambao ni wa kanisa, ambao [a]wamewapoteza waume au baba zao:

2 Wanawake wanayo [a]haki ya matunzo kutoka kwa waume wao, hadi waume wao watapochukuliwa; na kama hawakupatikana kuwa wavunjaji wa sheria watapata ushirika katika kanisa.

3 Na kama siyo waaminifu hawatapata ushirika katika kanisa; ingawa wanaweza kubaki juu ya urithi wao kulingana na sheria za nchi.

4 [a]Watoto wote wanayo haki juu ya wazazi wao kwa ajili ya matunzo hadi wafikiapo umri wa kujitegemea.

5 Na baada ya hapo, wanakuwa na haki juu ya kanisa, au katika maneno mengine juu ya [a]ghala ya Bwana, ikiwa wazazi wao hawana chochote cha kuwapa kuwa urithi wao.

6 Na ghala itatunzwa kwa mali iliyowekwa wakfu na kanisa; na [a]wajane na yatima watatunzwa kwa mali hiyo, kama pia [b]maskini. Amina.

SEHEMU YA 84

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, tarehe 22 na 23 Septemba 22 na 23, 1832. Katika kipindi cha mwezi wa Septemba, wazee walikuwa wamekwisha anza kurejea kutoka katika kazi zao za umisionari katika nchi za mashariki na kutoa ripoti ya kazi zao. Ilikuwa wakati walipokuwa pamoja katika majira haya ya shangwe kwamba mawasiliano haya yafuatayo yalipokelewa. Nabii aliyaita kama ufunuo juu ya ukuhani.

1–5, Yerusalemu Mpya na hekalu vitajengwa katika Missouri; 6–17, Safu ya ukuhani yatolewa kutoka Musa mpaka Adamu;

83 1*a* Yak. (Bib.) 1:27.
2*a* 1 Tim. 5:8.
4*a* Mos. 4:14.
5*a* M&M 78:3.
mwm Ghala.
6*a* mwm Mjane.
b Mos. 4:16–26; Hel. 4:11–13; M&M 42:30–39.
mwm Maskini.

18–25, Ukuhani mkuu hushikilia ufunguo wa ufahamu wa Mungu; 26–32, Ukuhani mdogo hushikilia ufunguo wa kuhudumiwa na malaika na wa injili ya matayarisho; 33–44, Wanaume hupata uzima wa milele kwa njia ya kiapo na agano la ukuhani; 45–53, Roho wa Kristo huwaangaza watu, na dunia hukaa katika dhambi; 54–61, Watakatifu ni lazima washuhudie mambo yale waliyoyapokea; 62–76, Wao wataihubiri injili, na ishara zitawafuata; 77–91, Wazee watakwenda pasipo mfuko wala mkoba, na Bwana atawatimizia mahitaji yao; 92–97, Magonjwa na laana zinawasubiri wale wanaoikataa injili; 98–102, Wimbo mpya wa ukombozi wa Sayuni unatolewa; 103–110, Kila mtu na asimame katika ofisi yake mwenyewe na kufanya kazi katika wito wake mwenyewe; 111–120, Watumishi wa Bwana watahubiri chukizo la uharibifu la siku za mwisho.

Ufunuo wa Yesu Kristo kwa mtumishi wake Joseph Smith, Mdogo, na wazee sita, kama vile walivyounganisha mioyo yao na [a]kupaza sauti zao juu.

2 Ndiyo, neno la Bwana kuhusu kanisa lake, lililoanzishwa katika siku hizi za mwisho kwa ajili ya [a]urejesho wa watu wake, kama alivyonena kwa vinywa vya [b]manabii wake, na kwa ajili ya kuwakusanya [c]watakatifu wake ili wasimame juu ya [d]Mlima Sayuni, ambao utakuwa mji wa [e]Yerusalemu Mpya.

3 Mji ambao utajengwa, kuanzia sehemu ya kiwanja cha [a]hekalu, mahali ambapo pameteuliwa kwa kidole cha Bwana, katika mipaka ya Jimbo la Missouri, na kuwekwa wakfu kwa mkono wa Joseph Smith, Mdogo, na wengine ambao Bwana alipendezwa nao sana.

4 Amini hili ndilo neno la Bwana, kwamba mji wa [a]Yerusalemu Mpya utajengwa kwa kukusanyika kwa watakatifu, kuanzia mahali hapa, hata mahali pa [b]hekalu, hekalu ambalo litainuliwa katika kizazi hiki

5 Kwani amini kizazi hiki chote hakitapita hadi nyumba itakapojengwa kwa Bwana, na wingu litatulia juu yake, wingu ambalo litakuwa hata [a]utukufu wa Bwana, ambalo litaijaza nyumba.

6 Na wana wa Musa, kulingana na Ukuhani Mtakatifu ambao aliupokea chini ya [a]mkono wa baba mkwe wake, [b]Yethro;

7 Na Yethro aliupokea chini ya mkono wa Kalebu;

8 Na Kalebu aliupokea chini ya mkono wa Elihu;

84 1*a* MWM Sala.
2*a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b Mdo. 3:19–21.
c MWM Mtakatifu.
d Isa. 2:2–5; Ebr. 12:22; Ufu. 14:1; M&M 76:66; 84:32; 133:18, 56.
e Eth. 13:2–11; M&M 42:8–9; 45:66–67; M ya I 1:10. MWM Yerusalemu Mpya.
3*a* M&M 57:3.
4*a* MWM Yerusalemu Mpya.
b MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.
5*a* M&M 45:67; 64:41–43; 97:15–20; 109:12, 37.
6*a* MWM Mikono, Kuweka juu ya.
b MWM Yethro.

9 Na Elihu chini ya mkono wa Yeremia;

10 Na Yeremia chini ya mkono wa Gadi;

11 Na Gadi chini ya mkono wa Isaya;

12 Na Isaya aliupokea chini ya mkono wa Mungu.

13 Isaya pia aliishi katika siku za Ibrahimu, na akabarikiwa naye,

14 [a]Ibrahimu ambaye aliupokea ukuhani kutoka kwa [b]Melkizedeki, ambaye aliupokea kupitia safu ya baba zake, hata mpaka [c]Nuhu;

15 Na kutoka Nuhu hadi [a]Henoko, kupitia safu ya baba zao;

16 Na kutoka Henoko mpaka [a]Habili, aliyeuawa kwa [b]njama za kaka yake, [c]aliyeupokea ukuhani kwa amri za Mungu, kwa mkono wa baba yake [d]Adamu, aliyekuwa mwanadamu wa kwanza—

17 [a]Ukuhani ambao unaendelea katika kanisa la Mungu katika vizazi vyote, nao hauna mwanzo wa siku au mwisho wa miaka.

18 Na Bwana pia alithibitisha [a]ukuhani pia juu ya [b]Haruni na uzao wake, kupitia vizazi vyake vyote, ukuhani ambao pia hudumu na [c]kukaa milele pamoja na ukuhani ambao ni wa mfano mtakatifu zaidi wa Mungu.

19 Na ukuhani huu mkuu huihudumia injili na hushikilia ufunguo wa [a]siri za ufalme, hata ufunguo wa [b]ufahamu wa Mungu.

20 Kwa hiyo, katika [a]ibada hizo, nguvu za uchamungu hujidhihirisha

21 Na pasipo ibada hizo, na [a]mamlaka ya ukuhani, nguvu za uchamungu haziwezi kujidhihirisha kwa mwanadamu katika mwili;

22 Kwani pasipo hizi hakuna [a]mwanadamu anayeweza kuuona uso wa Mungu, hata Baba, na kuishi.

23 Sasa [a]Musa alilifundisha hili kwa uwazi kabisa kwa wana wa Israeli nyikani, na alitafuta kwa bidii kubwa [b]kuwatakasa watu wake ili waweze [c]kuuona uso wa Mungu;

24 Lakini [a]waliishupaza mioyo yao na kushindwa kustahimili uwepo wake; kwa sababu hii, Bwana katika [b]ghadhabu yake, kwani hasira yake iliwaka dhidi yao, akaapa kuwa [c]hawataingia rahani mwake wakati wakiwa

14 *a* MWM Ibrahimu.
b MWM Melkizedeki.
c MWM Nuhu, Patriaki wa Biblia.
15 *a* MWM Henoko.
16 *a* MWM Habili.
b Musa 5:29–32.
c M&M 107:40–57.
d MWM Adamu.
17 *a* Alma 13:1–19; Ibr. 2:9, 11. MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
18 *a* MWM Ukuhani wa Haruni.
b MWM Haruni, Kaka wa Musa.
c M&M 13.
19 *a* M&M 63:23; 107:18–19. MWM Siri za Mungu.
b Ibr. 1:2.
20 *a* MWM Ibada.
21 *a* MWM Mamlaka; Ukuhani.
22 *a* M&M 67:11.
23 *a* Ku. 19:5–11; 33:11.
b MWM Utakaso.
c Ku. 24:9–11; M&M 93:1.
24 *a* Ku. 20:18–21; 32:8; Kum. 9:23; 1 Ne. 17:30–31, 42.
b Zab. 95:8; Ebr. 3:8–11; Yak. (KM) 1:7–8; Alma 12:36.
c TJS Ku. 34:1–2 (Kiambatisho); Hes. 14:23; Ebr. 4:1–11.

nyikani, raha ambayo ni utimilifu wa utukufu wake.

25 Kwa hiyo, alimchukua [a]Musa kutoka katikati yao, na [b]Ukuhani Mtakatifu pia;

26 Na [a]ukuhani mdogo uliendelea, ukuhani ambao hushikilia [b]ufunguo wa [c]kuhudumiwa na malaika na wa injili ya mataYarisho;

27 Injili hii ambayo ni injili ya [a]toba na ya [b]ubatizo, na [c]ondoleo la dhambi, na [d]sheria ya amri ya [e]kimwili, ambao Bwana katika ghadhabu yake aliifanya iendelee pamoja na nyumba ya Haruni miongoni mwa wana wa Israeli hadi [f]Yohana, ambaye Mungu alimwinua, akiwa [g]amejazwa Roho Mtakatifu tokea tumboni mwa mama yake.

28 Kwani yeye alibatizwa wakati akiwa bado mtoto, na alitawazwa na malaika wa Mungu wakati akiwa na umri wa siku nane katika uwezo huu, kuupindua ufalme wa Wayahudi, na kuyanyoosha mapito ya Bwana mbele ya uso wa watu wake, kwa [a]kuwatayarisha kwa ujio wa Bwana, ambaye mikononi mwake umetolewa [b]uwezo wote.

29 Na tena, ofisi za mzee na askofu, ni [a]viambatanisho muhimu vya ukuhani mkuu.

30 Na tena, ofisi za mwalimu na shemasi ni viambatanisho muhimu vya ukuhani mdogo, ukuhani ambao ulitolewa kwa Haruni na wanawe.

31 Kwa hiyo, kama nilivyosema kuhusu wana wa Musa—kwani wana wa Musa na pia wana wa Haruni watatoa [a]matoleo na dhabihu yaliyokubalika katika nyumba ya Bwana, nyumba ambayo itajengwa kwa ajili ya Bwana katika kizazi hiki, juu ya [b]eneo lilowekwa wakfu kama nilivyolichagua—

32 Na wana wa Musa na wa Haruni watajazwa na [a]utukufu wa Bwana, juu ya [b]Mlima Sayuni katika nyumba ya Bwana, wana ambao ni ninyi; na pia wengi ambao nimewaita na kuwatuma kulijenga [c]kanisa langu.

33 Kwani yeyote [a]aliye mwaminifu katika kupata [b]kuhani hizi mbili ambazo nimezinena, na kutukuza wito wake, [c]hutakaswa na Roho kwa kufanywa upya miili yao.

34 Wanakuwa wana wa Musa na Haruni na [a]uzao wa [b]Ibrahimu,

25 *a* Kum. 34:1–5.
b MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
26 *a* MWM Ukuhani wa Haruni.
b M&M 13.
c M&M 107:20.
27 *a* MWM Toba, Tubu.
b MWM Batiza, Ubatizo.
c MWM Ondoleo la Dhambi.
d MWM Torati ya Musa.
e Ebr. 7:11–16.
f MWM Yohana Mbatizaji.
g Lk. 1:15.
28 *a* Isa. 40:3; Mt. 3:1–3; Yn. 1:23.
b Mt. 28:18; Yn. 17:2; 1 Pet. 3:22; M&M 93:16–17.
29 *a* M&M 107:5.
31 *a* M&M 128:24.
b M&M 57:3.
32 *a* MWM Utukufu.
b Ebr. 12:22; M&M 76:66; 84:2; 133:56.
c MWM Kanisa la Yesu Kristo.
33 *a* MWM Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki.
b MWM Ukuhani.
c MWM Utakaso.
34 *a* Gal. 3:29; Ibr. 2:9–11. MWM Ibrahimu—Uzao wa Ibrahimu.
b M&M 132:30–32. MWM Agano la Ibrahimu.

na kanisa na ufalme, na [c]wateule wa Mungu.

35 Na pia wale wote waupokeao ukuhani huu wananipokea Mimi, asema Bwana;

36 Kwani yule awapokeaye watumishi wangu [a]anipokea Mimi;

37 Na yule [a]anipokeaye mimi ampokea Baba yangu;

38 Na yule ambaye ampokea Baba yangu aupokea ufalme wa Baba yangu; kwa hiyo yale [a]yote Baba yangu aliyonayo atapewa.

39 Na hii ni kulingana na [a]kiapo na agano lihusianalo na ukuhani.

40 Kwa hiyo, wale wote waupokeao ukuhani, hupokea kiapo hiki na agano hili la Baba yangu, ambalo haliwezi kuvunjwa, wala kuondolewa.

41 Lakini yeyote [a]avunjaye agano hili baada ya kulipokea, na kuligeuka kabisa, [b]hatapata msamaha wa dhambi katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.

42 Na ole wao wale wote wasiokuja katika ukuhani huu ambao ninyi mmeupokea, ambao sasa ninauthibitisha juu yenu ninyi mlioko hapa leo, kwa sauti yangu mwenyewe kutoka mbinguni; na hata nimewapa majeshi ya mbinguni na [a]malaika wangu wajibu juu yenu.

43 Na sasa mimi ninatoa kwenu ninyi amri ya kuwa waangalifu juu yenu wenyewe, ili kufanya bidii ya [a]usikivu kwa maneno ya uzima wa milele.

44 Kwani [a]mtaishi kwa kila neno litokalo kinywani mwa Mungu.

45 Kwa kuwa [a]neno la Bwana ni ukweli, na lolote lililo [b]kweli ni nuru, na lolote lililo nuru ni Roho, hata Roho wa Yesu Kristo.

46 Na Roho hutoa [a]nuru kwa [b]kila mtu ajaye katika ulimwengu; na Roho humwangazia kila mtu kote ulimwenguni, yule aisikilizaye sauti ya Roho.

47 Na kila mtu aisikilizaye sauti ya Roho huja kwa Mungu, hata Baba.

48 Na Baba [a]humfundisha [b]agano ambalo amelifanya upya na kulithibitisha juu yenu ninyi, ambalo limethibitishwa juu yenu kwa faida yenu, na siyo kwa faida yenu peke yake, bali kwa faida ya ulimwengu wote.

49 Na [a]dunia yote hukaa katika dhambi, na kuugulia [b]gizani na chini ya utumwa wa dhambi.

50 Na kwa hili muweze kujua wao wako chini ya [a]utumwa wa

34 *c* MWM Teule, Wateule.
36 *a* Mt. 10:40–42; Lk. 10:16; M&M 112:20.
37 *a* Yn. 13:20.
38 *a* Lk. 12:43–44; Rum. 8:32; Ufu. 21:7; 3 Ne. 28:10; M&M 132:18–20. MWM Kuinuliwa.
39 *a* MWM Kiapo na Agano la Ukuhani.
41 *a* MWM Ukengeufu.
b M&M 76:34–38; 132:27.
42 *a* M&M 84:88.
43 *a* 1 Ne. 15:23–25; M&M 1:14.
44 *a* Kum. 8:3; Mt. 4:4; M&M 98:11.
45 *a* Zab. 33:4. MWM Neno la Mungu.
b MWM Ukweli.
46 *a* MWM Dhamiri; Nuru, Nuru ya Kristo.
b Yn. 1:9; M&M 93:2.
48 *a* MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi.
b MWM Agano; Agano Jipya na Lisilo na Mwisho.
49 *a* 1 Yoh. 5:19.
b MWM Giza, Kiroho.
50 *a* Gal. 4:9.

[b]dhambi, kwa sababu hawaji kwangu.

51 Kwani yeyote asiyekuja kwangu yu chini ya utumwa wa dhambi.

52 Na yeyote asiye ipokea sauti yangu hajaizoea [a]sauti yangu, na huyo siyo wangu.

53 Na kwa hili muweze kuwatambua kati ya wema na wabaya, na ya kwamba [a]ulimwengu wote [b]unaugulia [c]dhambini na gizani hata sasa.

54 Na akili zenu katika wakati uliopita zilitiwa giza kwa sababu ya [a]kutokuamini, na kwa sababu ya kuyachukulia bila uzito mambo mliyoyapokea—

55 [a]Kiburi na kutokuamini ambako kumelileta kanisa lote chini ya hatia.

56 Na hatia hii i juu ya watoto wa Sayuni, hata wote.

57 Na watabakia chini ya hatia hii hadi watubu na kukumbuka [a]agano jipya, hata [b]Kitabu cha Mormoni na amri za [c]zamani ambazo niliwapa, siyo tu kwa kusema, bali kwa [d]kuzitenda kulingana na lile nililoliandika—

58 Ili waweze kuzaa matunda kwa ajili ya ufalme wa Baba yao; vinginevyo hapo hubaki mateso na hukumu kumwagwa juu ya watoto wa Sayuni.

59 Je, kwani watoto wa ufalme wataichafua nchi takatifu? Amini, ninawaambia, Hapana.

60 Amini, amini, ninawaambia ambao sasa mnayasikia [a]maneno yangu, ambayo ni sauti yangu, mmebarikiwa ninyi ilimradi mnayapokea mambo haya;

61 Kwani [a]nitawasamehe dhambi zenu kwa amri hii—kwamba ninyi muendelee kuwa thabiti katika mawazo yenu katika [b]taadhima na roho ya sala, katika kutoa ushuhuda kwa walimwengu wote kwa yale mambo yote ambayo yamejulishwa kwenu.

62 Kwa hiyo, [a]enendeni ulimwenguni kote; na mahali popote ambako ninyi hamwezi kwenda mtautuma, ili ushuhuda uweze kwenda kutoka kwenu ninyi hadi ulimwenguni kote kwa kila kiumbe.

63 Na kama vile nilivyosema kwa [a]mitume wangu, vivyo hivyo ninawaambia, kuwa ninyi ni mitume wangu, hata makuhani wakuu wa Mungu; ninyi ndiyo wale ambao baba [b]amenipa; ninyi ni [c]marafiki zangu;

64 Kwa hiyo, kama vile nilivyosema kwa mitume wangu ninawaambia ninyi tena, kuwa kila [a]mtu [b]ayaaminiye maneno

50 *b* MWM Dhambi.
52 *a* Yn. 10:27.
53 *a* MWM Ulimwengu.
b Rum. 8:22; Musa 7:48.
c MWM Malimwengu.
54 *a* MWM Kutoamini.
55 *a* MWM Majivuno, Siofaa.
57 *a* Yer. 31:31–34.
b MWM Kitabu cha Mormoni.
c 1 Ne. 13:40–41.
d Yak. (Bib.) 1:22–25; M&M 42:13–15.
60 *a* M&M 18:34–36.
61 *a* Dan. 9:9.
MWM Samehe.
b M&M 43:34; 88:121; 100:7.
62 *a* Mk. 16:15; M&M 1:2–5.
MWM Kazi ya kimisionari.
63 *a* MWM Mtume.
b 3 Ne. 15:24; M&M 50:41–42.
c Yn. 15:13–15; M&M 93:45.
64 *a* MWM Nafsi.
b Mk. 16:15–16.
MWM Amini, Imani.

yenu, na kubatizwa kwa maji kwa ajili ya [c]ondoleo la dhambi, atampokea [d]Roho Mtakatifu.

65 Na ishara hizi [a]zitawafuata hao wanaoamini—

66 Katika jina langu watafanya [a]miujiza mingi;

67 Katika [a]jina langu watawafukuza pepo wabaya;

68 Katika jina langu [a]watawaponya wagonjwa;

69 Katika jina langu watafungua macho ya vipofu, na kuzibua masikio ya viziwi;

70 Na ulimi wake aliye bubu utasema;

71 Na kama mtu yeyote atawawekea [a]sumu haitawadhuru;

72 Na sumu ya nyoka haitakuwa na uwezo wa kuwadhuru.

73 Lakini amri ninaitoa kwao, kwamba [a]wasijivune wenyewe kwa mambo haya, wala kuyanena mbele za walimwengu; kwani mambo haya yametolewa kwenu kwa faida na wokovu wenu.

74 Amini, amini, ninawaambia, wale wasioamini juu ya maneno yenu, na [a]hawajabatizwa katika maji katika jina langu, kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao, ili waweze kumpokea Roho Mtakatifu, [b]watahukumiwa, na hawatakuja katika ufalme wa Baba yangu mahali ambapo Baba na Mimi tupo.

75 Na ufunuo huu kwenu, na amri hii, vinaanza kutumika saa hii hii juu ya ulimwengu wote, na injili hii ni kwa wale wote ambao hawajaipokea.

76 Lakini, amini ninawaambia wale wote ambao kwao ufalme huu umetolewa—kutoka kwenu lazima ihubiriwe kwao, ili waweze kutubu matendo yao maovu ya zamani; kwani watakemewa kwa ajili ya mioyo yao miovu ya kutokuamini, na ndugu zenu katika Sayuni kwa uasi wao dhidi yenu wakati ule nilipowatuma.

77 Na tena ninawaambia, marafiki zangu, kwani kuanzia sasa nitawaita ninyi marafiki, ni muhimu kwamba niwape amri hii, ili muweze kuwa kama marafiki zangu katika siku zile wakati nilipokuwa pamoja nao, wakisafiri kuhubiri injili kwa uwezo wangu;

78 Kwani sikuwaruhusu kwenda na [a]mfuko au mkoba, wala kanzu mbili.

79 Tazama, ninawatuma ninyi kwenda kuuthibitisha ulimwengu, na mfanyakazi anastahili [a]ujira wake.

80 Na mtu yeyote atakaye kwenda na [a]kuhubiri [b]injili hii ya ufalme, na asishindwe kuendelea kwa uaminifu katika mambo yote, hatachoka akilini,

64 *c* MWM Ondoleo la Dhambi.
d MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
65 *a* Mk. 16:17–18. MWM Ishara.
66 *a* MWM Matendo.
67 *a* Mt. 17:14–21.
68 *a* MWM Ponya, Uponyaji.
71 *a* Mk. 16:18; Mdo. 28:3–9; M&M 24:13; 124:98–100.
73 *a* M&M 105:24. MWM Kiburi.
74 *a* 2 Ne. 9:23; M&M 76:50–52. MWM Batiza, Ubatizo—Muhimu.
b Yn. 3:18.
78 *a* Mt. 10:9–10; M&M 24:18.
79 *a* M&M 31:5.
80 *a* MWM Kazi ya kimisionari.
b MWM Injili.

wala kutiwa giza, wala mwilini, mkononi, au viungo; na hautapotea hata [c]unywele mmoja wa kichwa chake. Na hawatakwenda na njaa, wala kiu.

81 Kwa hiyo, [a]msisumbukie juu ya kesho, kuwa mtakula nini au mtakunywa nini, au mtavaa nini.

82 Kwani, fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo, hayafanyi kazi, wala hayasokoti; na falme za ulimwengu, katika utukufu wao wote, hazijavikwa vizuri kama mojawapo ya haya.

83 Kwani [a]Baba yenu, aliye mbinguni, [b]ajua kwamba mnayo haja ya mambo hayo yote.

84 Kwa hiyo, kesho [a]ijisumbukie yenyewe.

85 Wala msiwaze kabla [a]nini cha kusema; bali [b]yahifadhini katika akili zenu daima maneno ya uzima, nanyi [c]mtapewa saa ile ile mtakayosema sehemu ile ambayo itakayokusudiwa kwa kila mtu.

86 Kwa hiyo, pasiwepo mtu yeyote miongoni mwenu, kwani sheria hii ni kwa [a]waaminifu wote walioitwa na Mungu katika kanisa kwa huduma, kutoka sasa kuchukua mfuko au mkoba, yule aendaye kuitangaza injili hii ya ufalme.

87 Tazama, [a]ninawatuma ninyi kuwakemea walimwengu kwa sababu ya matendo yao yote yasiyo ya haki, na kuwafundisha juu ya hukumu ambayo itakuja.

88 Na yeyote [a]awapokeaye ninyi, hapo nitakuwepo pia, kwani nitakwenda mbele ya uso wenu. Nitakuwa mkono wenu wa kuume na wa kushoto, na Roho wangu atakuwa mioyoni mwenu, na [b]malaika zangu watawazingira, ili kuwabeba juu.

89 Yeyote awapokeaye ninyi ananipokea Mimi; naye atawalisha, na kuwavika, na kuwapa fedha.

90 Na yule awalishaye, au kuwavika, au kuwapa fedha, kwa vyovyote [a]hatapoteza kamwe thawabu yake.

91 Na yule asiyewafanyia mambo haya siyo mwanafunzi wangu; kwa njia hii mtaweza kuwajua [a]wanafunzi wangu.

92 Mtu asiyewapokea, ondokeni kwake ninyi wenyewe, na [a]isafisheni miguu yenu hata kwa maji, maji safi, iwe katika joto au baridi, na toeni ushuhuda wake kwa Baba yenu aliye mbinguni, na msirudi tena kwa mtu huyo.

93 Na katika kijiji chochote au mji muingiao, fanyeni vivyo hivyo.

94 Hata hivyo, tafuteni kwa

80 *c* Lk. 21:18.
81 *a* Mt. 6:25–28.
83 *a* MWM Baba wa Mbinguni.
b Mt. 6:8.
84 *a* Mt. 6:34.
85 *a* Mt. 10:19–20; Lk. 12:11–12; M&M 100:6.
b 2 Ne. 31:20; Alma 17:2–3; M&M 6:20; 11:21–26. MWM Tafakari.
c MWM Fundisha, Mwalimu—Kufundisha kwa Roho.
86 *a* Mt. 24:44–46; M&M 58:26–29; 107:99–100.
87 *a* MWM Kazi ya kimisionari.
88 *a* Mt. 10:40; Yn. 13:20.
b M&M 84:42. MWM Malaika.
90 *a* Mt. 10:42; Mk. 9:41.
91 *a* Yn. 13:35.
92 *a* Mt. 10:14; Lk. 9:5; M&M 60:15.

bidii na msiache; na ole wake nyumba ile, au kijiji kile au mji ule uwakataao ninyi, au maneno yenu, au ushuhuda wenu juu yangu.

95 Ole, nasema tena, kwa nyumba ile, au kijiji kile au mji ule uwakataao ninyi, au maneno yenu, au ushuhuda wenu juu yangu Mimi;

96 Kwani, Mimi, [a]Mwenyezi, nimeweka mikono yangu juu ya mataifa, [b]kuwaadhibu kwa [c]uovu wao.

97 Na magonjwa yataenea, na hayataondolewa duniani hadi nitakapomaliza kazi yangu, ambayo [a]itafupishwa kwa haki—

98 Hadi wote watanijua, wanaobaki, hata kuanzia mdogo wao hata mkubwa wao, nao watajawa na kumjua Bwana, na wataona [a]jicho kwa jicho, na watapaza sauti zao, na kwa sauti [b]wataimba pamoja wimbo huu mpya, wakisema:

99 Bwana ameirejesha tena Sayuni;
Bwana [a]amewakomboa watu wake, [b]Israeli,
Kulingana na [c]uchaguzi wa [d]neema,
Ambao ulitimizwa kwa imani
Na [e]agano la Baba zao.

100 Bwana amewakomboa watu wake;
Na Shetani [a]amefungwa na muda umekwisha.
Bwana amevijumlisha vitu vyote katika [b]kimoja.
Bwana ameishusha [c]Sayuni kutoka juu.
Bwana [d]ameiinua Sayuni kutoka chini.

101 [a]Dunia imepata utungu na kuzaa uwezo wake;
Na kweli imeenea katika tumbo lake;
Na mbingu zimetabasamu juu yake;
Naye amevikwa kwa [b]utukufu wa Mungu wake;
Kwani yeye husimama katikati ya watu wake.

102 Utukufu, na heshima, na uwezo, na nguvu,
Ziwe kwa Mungu wetu; kwa kuwa amejaa [a]rehema,
Haki, neema na kweli, na [b]amani,
Milele na milele. Amina.

103 Na tena, amini, amini, ninawaambia, ni muhimu kwamba kila mtu anayekwenda kuihubiri injili yangu isiyo na mwisho, kwamba ilimradi wao wanazo familia, na wanapokea fedha kama zawadi, yawapasa wazitume kwao au wazitumie kwa manufaa yao, kama vile Bwana atakavyowaelekeza, kwa kuwa hivyo ndivyo nionavyo kuwa ni vema.

96 *a* MWM Mwenyezi.
b M&M 1:13–14.
c MWM Ovu, Uovu.
97 *a* Mt. 24:22.
98 *a* Isa. 52:8.
b Zab. 96:1; Ufu. 15:3; M&M 25:12; 133:56. MWM Imba.
99 *a* Ufu. 5:9; M&M 43:29.
b MWM Israeli.
c MWM Uteuzi.
d MWM Neema.
e MWM Agano la Ibrahimu.
100 *a* Ufu. 20:2–3; M&M 43:31; 45:55; 88:110.
b Efe. 1:10; M&M 27:13.
c M&M 45:11–14; Musa 7:62–64. MWM Sayuni.
d M&M 76:102; 88:96.
101 *a* MWM Dunia.
b MWM Utukufu.
102 *a* MWM Rehema, enye Rehema.
b MWM Amani.

104 Na kwa wale wote wasio na familia, ambao wanapokea [a]fedha, na wazitume kwa askofu katika Sayuni, au kwa askofu katika Ohio, ili ziweze kuwekwa wakfu kwa ajili ya kuleta mafunuo na kupiga chapa, na kwa ustawishaji wa Sayuni.

105 Na kama mtu yeyote atatoa kanzu kwa mtu yeyote kati yenu, au suti, achukue ile ya zamani na kumpa [a]maskini, na nenda zako ukifurahia.

106 Na kama mtu yeyote miongoni mwenu akiwa imara katika Roho, na [a]amchukue yule aliye dhaifu pamoja naye, ili aweze kuelekezwa katika [b]unyenyekevu kamili, ili naye aweze kuwa imara pia.

107 Kwa hiyo, wachukueni pamoja nanyi wale waliotawazwa katika [a]ukuhani mdogo, na kuwatuma mbele yenu kuweka ahadi, na kuitengeneza njia, na kutimiza miadi ambayo ninyi wenyewe hamwezi kuitimiza.

108 Tazama, hii ndiyo njia ambayo mitume wangu, katika siku za zamani, walinijengea kanisa langu.

109 Kwa hiyo, kila mtu na asimame katika nafasi yake mwenyewe, na kutenda kazi katika wito wake mwenyewe; na wala kichwa hakiwezi kuiambia miguu sina haja na wewe; kwani pasipo miguu mwili wawezaje kusimama?

110 Pia mwili unahitaji kila [a]kiungo, ili wote uweze kujengwa kwa pamoja, ili muundo uweze kubaki mkamilifu.

111 Na tazama, [a]makuhani wakuu wanapaswa kusafiri, na pia wazee, na pia [b]makuhani wadogo; lakini [c]mashemasi na [d]walimu yapasa wateuliwe [e]kuliangalia kanisa, kuwa wahudumu wa kudumu kwa kanisa.

112 Na askofu, Newel K. Whitney, pia anapaswa kusafiri maeneo ya jirani na miongoni mwa makanisa yote, akiwatafuta maskini na [a]kuhudumia mahitaji yao kwa [b]kuwanyenyekeza matajiri na wenye majivuno.

113 Yampasa pia kuajiri [a]wakala atakayekuwa akiwajibika na kufanya shughuli zake za kawaida kama yeye atakavyoelekeza.

114 Hata hivyo, askofu na aende katika mji wa New York, pia katika mji wa Albany, na pia mji wa Boston, na kuwaonya watu wa miji hiyo kwa sauti ya injili, kwa sauti kubwa, juu ya [a]maangamizo, na maangamizo makamilifu ambayo yanawasubiri ikiwa wanayakataa mambo haya.

115 Kwani ikiwa wanayakataa mambo haya saa ya hukumu yao i karibu, na nyumba yao [a]itaachwa.

104*a* M&M 51:8–9, 12–13.
105*a* MWM Maskini—Maskini katika mahitaji ya muhimu.
106*a* MWM Ushirika.
b MWM Pole, Upole.
107*a* MWM Ukuhani wa Haruni.
110*a* 1 Kor. 12:12–23.
111*a* MWM Kuhani Mkuu.
b MWM Kuhani, Ukuhani wa Haruni.
c MWM Shemasi.
d MWM Mwalimu, Ukuhani wa Haruni.
e MWM Kesha, Walinzi.
112*a* MWM Ustawi.
b M&M 56:16.
113*a* M&M 90:22.
114*a* M&M 1:13–14.
115*a* Lk. 13:35.

116 Na [a]anitegemee mimi na wala [b]hatashindwa; na hata [c]unywele mmoja wa kichwa chake hautapotea.

117 Na amini ninawaambia, watumishi mliosalia, nendeni kadiri hali zenu zitakavyowaruhusu, katika miito yenu mbalimbali, kwenye miji mikuu na vijiji, mkiukemea ulimwengu katika haki juu ya matendo yao yote yasiyo ya haki na yasiyo ya uchamungu, mkielezea vizuri na kwa kueleweka chukizo la uharibifu katika siku za mwisho.

118 Kwani, pamoja nanyi asema Bwana Mwenyezi, [a]nitaziharibu falme zao; siyo tu [b]nitaitikisa dunia, bali mbingu ya nyota itatikisika.

119 Kwani Mimi, Bwana, nimeunyosha mkono wangu ili kuzitakasa nguvu za mbinguni; hamwezi kuona hili sasa, bado kipindi kifupi nanyi mtaona, na kujua kuwa Mimi ndiye, na kwamba [a]nitakuja na [b]kutawala pamoja na watu wangu.

120 Mimi ni [a]Alfa na Omega, mwanzo na mwisho. Amina.

SEHEMU YA 85

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, tarehe 27 Novemba 1832. Sehemu hii ni dondoo kutoka barua ya Nabii aliyo mwandikia William W. Phelps, ambaye alikuwa akiishi Independence, Missouri. Ilitolewa ili kujibu maswali juu ya wale Watakatifu waliokwisha hamia Sayuni lakini hawakuwa wamefuata amri ya kuweka wakfu mali zao na hivyo hawakupokea urithi wao kulingana na utaratibu uliowekwa katika Kanisa.

1–5, Urithi katika Sayuni utapokelewa kwa njia ya kuwekwa wakfu; 6–12, Mmoja aliye hodari na mwenye nguvu atawapa Watakatifu urithi wao katika Sayuni.

Ni kazi ya karani wa Bwana, aliyemteua, kuhifadhi historia, na [a]kumbukumbu ya jumla ya kanisa ya mambo yote yatendekayo katika Sayuni, na juu ya wale wote ambao huweka mali yao [b]wakfu, na kupokea urithi kisheria kutoka kwa askofu;

2 Na pia namna wanavyoishi, imani yao na matendo yao; na pia waasi wanaoasi baada ya kupokea urithi wao.

3 Ni kinyume cha mapenzi na amri ya Mungu kwamba wale ambao hawapati urithi wao kwa [a]kuwekwa wakfu, kulingana na

116 *a* MWM Tegemea.
b Zab. 22:5; 1 Pet. 2:6.
c Mt. 10:29–31.
118 *a* Dan. 2:44–45.
b Yoe. 2:10; M&M 43:18; 45:33, 48; 88:87, 90.
MWM Ishara za Nyakati; Siku za Mwisho.
119 *a* M&M 1:12, 35–36; 29:9–11; 45:59. MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b MWM Milenia.
120 *a* MWM Alfa na Omega.
85 1 *a* M&M 21:1; 47:1; 69:3–6.
b M&M 42:30–35.
3 *a* MWM Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.

sheria yake, ambayo ametoa, ili aweze [b]kuwalipisha zaka watu wake, ili kuwaandaa wao dhidi ya siku ile ya [c]kisasi na kuchomwa, wawe na majina yao yakiwa yameorodheshwa pamoja na watu wa Mungu.

4 Wala nasaba yao isiwekwe, au isiwepo mahali ambapo itaweza kupatikana katika kumbukumbu yoyote au historia ya kanisa.

5 Majina yao hayatapatikana, wala majina ya baba zao, wala majina ya watoto hayataandikwa katika [a]kitabu cha sheria ya Mungu, asema Bwana wa Majeshi.

6 Ndiyo, hivyo ndivyo yasemavyo [a]sauti ndogo tulivu, ambayo hunong'ona na [b]kupenya vitu vyote, na mara nyingi huifanya mifupa yangu itetemeke wakati ijitokezapo, yakisema:

7 Na itakuwa kwamba Mimi, Bwana Mungu, nitamtuma mmoja hodari na mwenye nguvu, akishika fimbo ya mamlaka katika mkono wake, amejivika nuru kama vazi, ambaye kinywa chake kitanena maneno, maneno ya milele; kwa maana matumbo yake yatakuwa chemichemi ya ukweli, ili kuiweka katika utaratibu nyumba ya Mungu, na kupanga kwa kupiga kura urithi wa watakatifu ambao majina yao yanapatikana, na majina ya baba zao, na ya watoto wao, yameorodheshwa katika kitabu cha sheria ya Mungu;

8 Kwa maana mtu yule, aliyeitwa na Mungu na kuteuliwa, kwamba aunyoshe mkono wake ili kulitegemeza [a]sanduku la Mungu, ataanguka kwa mshale wa mauti, kama vile mti uliopigwa kwa mshale wa radi.

9 Na wale wote ambao hawakuandikwa katika [a]kitabu cha kumbukumbu hawatapata urithi katika siku ile, bali watatengwa, na kuwekewa fungu lao miongoni mwa wasioamini, ndiko kutakuwako na [b]kilio na kusaga meno.

10 Mambo haya siyaneni kwa nafsi yangu tu; kwa hiyo, kama vile Bwana anenavyo, yeye pia atatimiza.

11 Na wale wa Ukuhani Mkuu, ambao majina yao hayapatikani kuwa yameandikwa katika [a]kitabu cha sheria, au ambao wamepatikana kuwa [b]wamekengeuka, au kuwa [c]wametengana na kanisa, vile vile wa ukuhani mdogo, au waumini, katika siku ile hawatapata urithi miongoni mwa watakatifu wa Aliye Juu Sana;

12 Kwa hiyo, itafanyika kwao kama vile kwa watoto wa

3 *b* MWM Lipa zaka, Zaka.
c Mal. 3:10–11, 17; M&M 97:25–26.
5 *a* MWM Kitabu cha Uzima.
6 *a* 1 Fal. 19:11–12; Hel. 5:30–31; 3 Ne. 11:3–7.
b Ebr. 4:12.
8 *a* 2 Sam. 6:6–7; 1 Nya. 13:9–10. MWM Sanduku la Agano.
9 *a* 3 Ne. 24:16; Musa 6:5–6. MWM Kitabu cha Ukumbusho.
b M&M 19:5.
11 *a* MWM Kitabu cha Uzima.
b MWM Ukengeufu.
c MWM Kutengwa na Kanisa.

kuhani, kama itakavyoonekana kuandikwa katika mlango wa pili na mstari wa sitini na moja na sitini na mbili wa Ezra.

SEHEMU YA 86

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 6 Desemba 1832. Ufunuo huu ulipokelewa wakati Nabii alipokuwa akihakiki na kuhariri muswada wa tafsiri ya Biblia.

1–7, Bwana anatoa maana ya mfano wa ngano na magugu; 8–11, Anaelezea baraka za ukuhani kwa wale ambao ni warithi kisheria kwa jinsi ya mwili.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu ninyi watumishi wangu, kuhusu [a]mfano wa ngano na magugu:

2 Tazama, amini ninasema, lile konde ni ulimwengu, na mitume walikuwa ni wapanda mbegu;

3 Na baada ya kuwa wamelala mtesaji mkuu wa kanisa, muasi, kahaba, hata [a]Babilonia, yule ayafanyaye mataifa yote kunywa kikombe chake, ambao katika mioyo yao adui, hata Shetani, hukaa na kutawala—tazama yeye ndiye hupanda magugu; kwa hiyo, magugu huikaba ngano na kulifukuzia [b]kanisa nyikani.

4 Lakini tazama, katika [a]siku za mwisho, hata sasa wakati Bwana anapoanza kulileta neno, na jani linapoanza kumea na likiwa bado changa—

5 Tazama, amini ninawaambia, [a]malaika wanamlilia Bwana usiku na mchana, ambao wako tayari na wanasubiri kutumwa ili [b]kuyakata chini makonde;

6 Lakini Bwana huwaambia, msiyang'oe magugu wakati jani likiwa bado changa (kwani amini imani yenu ni dhaifu), msije mkaharibu na ngano pia.

7 Kwa hiyo, acha ngano na magugu yakue pamoja hadi mavuno yatakapokuwa yameiva kikamilifu; ndipo kwanza mtaikusanya ngano kutoka miongoni mwa magugu, na baada ya kuikusanya ngano, tazama na lo, magugu yamefungwa matita matita, na konde limebaki kwa kuchomwa.

8 Kwa hiyo, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu ninyi, ambao [a]ukuhani umedumu kupitia safu ya uzao wa baba zenu—

9 Kwani ninyi ni [a]warithi kisheria, kwa jinsi ya mwili, na [b]mkafichwa kutoka ulimwe-

86 1*a* Mt. 13:6–43; M&M 101:64–67.
3*a* Ufu. 17:1–9.
MWM Babeli, Babilonia.
b Ufu. 12:6, 14.
4*a* MWM Siku za Mwisho.
5*a* M&M 38:12.
b MWM Mavuno.
8*a* M&M 113:8.
MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
9*a* Ibr. 2:9–11.
MWM Agano la Ibrahimu.
b Isa. 49:2–3.

nguni, pamoja na Kristo katika Mungu—

10 Kwa hiyo maisha yenu na ukuhani vimedumu, na havina budi kudumu kupitia ninyi na safu ya uzao wenu hata zije zama za [a]urejesho wa vitu vyote vilivyonenwa kwa vinywa vya manabii wote watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu.

11 Kwa hiyo, heri ninyi kama mtakaa katika wema wangu, na [a]nuru ya kuwa mwangaza kwa Wayunani, na kupitia ukuhani huu, mwokozi kwa watu wangu, [b]Israeli. Bwana amesema hili. Amina.

SEHEMU YA 87

Ufunuo na unabii juu ya vita, uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii huko, au jirani na Kirtland, Ohio, 25 Desemba 1832. Wakati huu migogoro katika Marekani juu ya utumwa na Carolina ya Kusini kufuta kodi ya serikali kuu ilikuwa imeenea. Historia ya Joseph Smith inaeleza kwamba "mwonekano wa matatizo miongoni mwa mataifa" ilikuwa wazi zaidi kwa Nabii "kuliko hapo awali ilivyokuwa tangu Kanisa lianze safari yake kutoka nyikani."

1–4, Vita vyatabiriwa kati ya Majimbo ya Kaskazini na Majimbo ya Kusini; 5–8, Majanga makubwa yatawaangukia wakazi wote wa dunia.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kuhusu vita ambavyo karibu vitatokea, kuanzia kwenye uasi wa [a]Carolina ya Kusini, ambao hatimaye utaishia katika vifo na huzuni kwa watu wengi;

2 Na wakati utakuja ambao [a]vita vitamwagika juu ya mataifa yote, kuanzia mahali hapa.

3 Kwani tazama, Majimbo ya Kusini yatagawanyika dhidi ya Majimbo ya Kaskazini, na Majimbo ya Kusini yatayaita mataifa mengine, hata taifa la Uingereza, kama linavyoitwa, na pia watayaita mataifa mengine, ili kujilinda wenyewe dhidi ya mataifa mengine; na ndipo [a]vita vitamwagwa juu ya mataifa yote.

4 Na itakuwa, baada ya siku nyingi, [a]watumwa watainuka dhidi ya mabwana wao, ambao wataandaliwa na kufundishwa kwa ajili ya vita.

5 Na itakuwa pia mabaki ya waliosalia katika nchi watajipanga wenyewe, na watakuwa wakali kupita kiasi, na watawaudhi Wayunani kwa maudhi makali.

6 Na hivyo, kwa upanga na kwa umwagaji damu wakazi

10*a* Mdo. 3:19–21. MWM Urejesho wa Injili.
11*a* Isa. 49:6.
b M&M 109:59–67.
87 1*a* M&M 130:12–13.
2*a* Yoe. 3:9–16; Mt. 24:6–7; M&M 45:26, 63; 63:33.
3*a* M&M 45:68–69.
4*a* M&M 134:12.

wa dunia [a]wataomboleza; na kwa [b]njaa, na magonjwa, na matetemeko, na kwa ngurumo ya mbinguni, na radi kali ing'arayo pia, wakazi wa dunia watafanywa waisikie ghadhabu, na uchungu wa hasira, na mkono wa [c]adhabu wa Mwenyezi Mungu, hadi kuangamizwa kuliko kusudiwa [d]kumeyakomesha mataifa yote;

7 Kwamba kilio cha watakatifu, na cha [a]damu ya watakatifu, kitakoma kuja katika masikio ya Bwana wa [b]Sabato, kutoka duniani, kulipiza kisasi kwa adui zao.

8 Kwa hiyo, [a]simameni katika mahali pa takatifu, na wala msiondoshwe, hadi siku ya Bwana itapofika; kwani tazama, yaja [b]haraka, asema Bwana. Amina.

SEHEMU YA 88

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii huko Kirtland, Ohio, 27 na 28 Desemba 1832 na 3 Januari 1833. Nabii aliupa jina na akauita kama "'jani la mzeituni' . . . lililochumwa kutoka katika Mti wa Peponi, ujumbe wa Bwana wa amani kwetu sisi." Ufunuo ulitolewa baada ya makuhani wakuu kwenye mkutano kuomba "mmoja mmoja na kwa sauti kwa Bwana ili afunue mapenzi yake kwao kuhusiana na ujenzi wa Sayuni."

1–5, Watakatifu waaminifu humpokea yule Mfariji, ambaye ni ahadi ya uzima wa milele; 6–13, Vitu vyote vinaongozwa na kutawaliwa kwa Nuru ya Kristo; 14–16, Ufufuko huja kupitia Ukombozi; 17–31, Utii kwa sheria za selestia, terestria au telestia huwatayarisha wanadamu kwa falme na fahari husika; 32–35, Wale wanaotaka kukaa katika dhambi hubakia wachafu; 36–41, Falme zote zinatawaliwa kwa sheria; 42–45, Mungu ametoa sheria kwa vitu vyote; 46–50, Mwanadamu atamjua hata Mungu; 51–61, Ule mfano wa mtu kuwatuma watumishi wake shambani na kuongea nao mmoja mmoja; 62–73, Mkaribieni Bwana, na mtauona uso Wake; 74–80, Jitakaseni wenyewe na kufundishana mafundisho ya ufalme; 81–85, Kila mwanadamu aliyeonywa anapaswa kumwonya jirani yake; 86–94, Ishara, mvurugiko wa vitu vya asili, na malaika wanaitengeneza njia kwa ajili ya kuja kwa Bwana; 95–102, Parapanda ya malaika kuwaita wafu katika utaratibu wao; 103–116, Parapanda ya malaika yatangaza urejesho wa injili, anguko la Babilonia, na pambano la Mungu mkuu; 117–126, Tafuteni kujifunza,

6 *a* M&M 29:14–21; 45:49.
b JS—M 1:29.
c MWM Rudi, Kurudiwa.
d MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.
7 *a* Eth. 8:22–24.
b Yak. (Bib.) 5:4; M&M 88:2; 95:7.
8 *a* Mt. 24:15; M&M 45:32; 101:21–22.
b Ufu. 3:11.

jengeni nyumba ya Mungu (hekalu), na jivikeni ninyi wenyewe kwa kifungo cha hisani; 127–141, Utaratibu wa Shule ya Manabii unawekwa, ikiwa ni pamoja na ibada ya kutawadha miguu.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu mliokusanyika wenyewe pamoja ili kupokea mapenzi yake juu yenu:

2 Tazama, hii inampendeza Bwana wenu, na malaika [a]wanafurahi juu yenu; [b]sadaka za sala zenu zimefika juu katika masikio ya Bwana wa [c]Sabato, na kuandikwa katika [d]kitabu cha majina ya waliotakaswa, hata wale wa ulimwengu wa selestia.

3 Kwa hiyo, sasa ninampeleka kwenu [a]Mfariji mwingine, hata juu yenu ninyi marafiki zangu, ili aweze kukaa katika mioyo yenu, hata [b]Roho Mtakatifu wa ahadi; Mfariji mwingine ambaye ni yule yule niliyewaahidi wanafunzi wangu, kama ilivyoandikwa katika ushuhuda wa Yohana.

4 Mfariji huyu ni ahadi ambayo ninawapa ninyi ya [a]uzima wa milele, hata [b]utukufu wa ufalme wa selestia;

5 Utukufu ambao ni wa kanisa la [a]Mzaliwa wa Kwanza, hata wa Mungu, mtakatifu kupita wote, kupitia Yesu Kristo Mwana wake—

6 [a]Yeye yule aliyepaa juu, vile vile pia [b]alishuka chini ya vitu vyote, kiasi kwamba [c]alielewa vitu vyote, ili aweze kuwa katika vyote na ndani ya vitu vyote, [d]nuru ya ukweli;

7 Ukweli ambao hung'ara. Hii ndiyo [a]nuru ya Kristo. Kama vile pia yu katika jua, na ni nuru ya jua na nguvu yake ambayo kwayo [b]liliumbwa.

8 Kama vile pia yu katika mwezi, na ni nuru ya mwezi, na nguvu yake ambayo kwayo uliumbwa;

9 Kama vile pia ni nuru ya nyota, na nguvu yake ambayo kwayo ziliumbwa;

10 Na dunia pia, na ni nguvu yake, hata dunia hii ambayo juu yake [a]mmesimama.

11 Na nuru ing'arayo, ambayo hukupa mwanga, hutoka kwake yeye ayaangazaye macho yako, ambayo ndiyo nuru hiyo hiyo ambayo huhuisha [a]ufahamu wako;

12 [a]Nuru itokayo kutoka katika uwepo wa Mungu ili [b]kuijaza sehemu kubwa—

13 Nuru iliyo ndani ya vitu

88 2*a* Lk. 15:10.
b Mdo. 10:1–4. MWM Sala.
c Yak. (Bib.) 5:4; M&M 95:7.
d MWM Kitabu cha Uzima.
3*a* Yn. 14:16.
b M&M 76:53. MWM Roho Mtakatifu wa Ahadi.
4*a* M&M 14:7.
b MWM Utukufu wa Selestia.
5*a* MWM Mzaliwa wa Kwanza.
6*a* MWM Yesu Kristo.
b M&M 122:8. MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
c MWM Kujua yote.
d M&M 93:2, 8–39. MWM Nuru, Nuru ya Kristo; Ukweli.
7*a* Moro. 7:15–19; M&M 84:45.
b Mwa. 1:16. MWM Umba, Uumbaji.
10*a* Musa 2:1.
11*a* MWM Ufahamu.
12*a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
b Yer. 23:24.

[a]vyote, ambayo hutoa [b]uhai kwa vitu vyote, ambayo ndiyo [c]sheria ambayo kwayo vitu vyote hutawaliwa, hata uwezo wa Mungu aketiye juu ya kiti chake cha enzi, yeye aliye kifuani pa milele, yeye aliye katikati ya vitu vyote.

14 Sasa, amini ninawaambia, kuwa kwa njia ya [a]ukombozi ambao umefanyika kwa ajili yenu huleta kukamilika kwa ufufuko wa wafu.

15 Na [a]roho na [b]mwili ndiyo [c]nafsi ya mwanadamu.

16 Na [a]ufufuko wa wafu ni ukombozi wa nafsi.

17 Na ukombozi wa nafsi ni kupitia kwake yeye ambaye anavihifadhi hai vitu vyote, ambaye kifuani mwake aliadhimia kuwa [a]maskini na [b]wapole wa [c]dunia watairithi nchi.

18 Kwa hiyo, haina budi kusafishwa udhalimu wote, ili iweze kuandaliwa kwa ajili ya utukufu wa [a]selestia;

19 Kwani baada ya kuwa imetimiza kipimo cha uumbaji wake, itavikwa taji la [a]utukufu, hata na uwepo wa Mungu Baba;

20 Kwamba miili ile iliyo ya ufalme wa selestia [a]itaimiliki milele na milele; kwani, kwa [b]kusudi hili, ilitengenezwa na kuumbwa, na kwa kusudi hili [c]wametakaswa.

21 Na wale ambao hawakutakaswa kwa sheria ambayo nimeitoa kwenu, hata sheria ya Kristo, lazima warithi ufalme mwingine, hata ule ufalme wa terestria, au ule ufalme wa telestia.

22 Kwani yule ambaye hawezi kuishi kwa [a]sheria ya ufalme wa selestia hawezi kustahimili katika utukufu wa selestia.

23 Na yule asiyeweza kuishi kwa sheria ya ufalme wa terestria hawezi kustahimili [a]utukufu wa terestria.

24 Na yule asiyeweza kuishi kwa sheria ya ufalme wa telestia hawezi kustahimili utukufu wa [a]telestia; kwa hiyo hafai kwa ufalme wa utukufu. Kwa hiyo yeye lazima aishi katika ufalme usio na utukufu.

25 Na tena, amini ninawaambia, [a]dunia huishi sheria ya ufalme wa selestia, kwa kuwa inatimiza kipimo cha uumbaji wake, na wala haivunji sheria—

26 Kwa hiyo, [a]itatakaswa;

13*a* Kol. 1:16–17.
b Kum. 30:20; M&M 10:70.
c Ayu. 38; M&M 88:36–38.
MWM Sheria.

14*a* MWM Lipia dhambi, Upatanisho; Mpango wa Ukombozi.

15*a* MWM Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, mtoto wa kiroho wa Baba wa Mbinguni; Roho.
b MWM Mwili.
c Mwa. 2:7.
MWM Nafsi.

16*a* Alma 11:42.
MWM Ufufuko.

17*a* MWM Maskini.
b MWM Pole, Upole.
c MWM Dunia—Hali ya mwisho ya dunia.

18*a* MWM Utukufu wa Selestia.

19*a* M&M 130:7–9.

20*a* M&M 38:20.
b Musa 1:39.

MWM Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, uwezekano wa kuwa kama Baba wa Mbinguni.
c MWM Utakaso.

22*a* M&M 105:5.

23*a* MWM Utukufu wa Terestria.

24*a* MWM Utukufu wa Telestia.

25*a* MWM Dunia.

26*a* MWM Dunia—Hali ya mwisho ya dunia.

ndiyo, ijapokuwa [b]itakufa, itahuishwa tena, na itastahimili nguvu ambayo kwayo ilihuishwa, na [c]wenye haki [d]watairithi.

27 Kwani ijapokuwa wanakufa, pia [a]wataamka tena, na [b]mwili wa kiroho.

28 Wale walio wa roho za selestia watapokea mwili huo huo ambao ulikuwa mwili wa asili; hata ninyi mtapata miili yenu, na [a]utukufu ule ambao kwa huo miili yenu [b]ilihuishwa.

29 Ninyi ambao mnahuishwa kwa sehemu ya utukufu wa [a]selestia halafu ndipo mtapokea huo huo, hata utimilifu.

30 Na wale ambao huhuishwa kwa sehemu ya utukufu wa [a]terestria watapokea huo huo, hata utimilifu wake.

31 Na pia wale ambao huhuishwa kwa sehemu ya utukufu wa [a]telestia watapokea huo huo, hata utimilifu wake.

32 Na wale waliosalia nao pia [a]watahuishwa; hata hivyo, watarejeshwa tena mahali pao, ili kufurahia kile ambacho wako [b]tayari kukipokea, kwa sababu hawakuwa tayari kufurahia kile ambacho wangelikipokea.

33 Kwani itamfaidia mtu nini kama zawadi imewekwa juu yake, na hapati zawadi hiyo? Tazama, hafurahii katika kile ambacho kimetolewa kwake, wala hamfurahii yeye aliyetoa zawadi.

34 Na tena, amini ninawaambia, kile kitawaliwacho kwa sheria pia hulindwa kwa sheria na kukamilishwa na [a]kutakaswa kwa sheria hiyo hiyo.

35 Kile [a]kivunjacho sheria, na hakiishi kwa sheria, lakini chatafuta chenyewe kuwa sheria, na kiko tayari kuishi katika dhambi, na moja kwa moja kinaishi katika dhambi, hakiwezi kutakaswa kwa sheria, si kwa [b]rehema, [c]haki, wala hukumu. Kwa hiyo, lazima wazidi kuwa [d]wachafu.

36 Falme zote zinayo sheria zilizotolewa;

37 Na ziko [a]falme nyingi; kwani hakuna nafasi ambamo ndani yake hakuna ufalme; na hakuna ufalme ambamo ndani yake hakuna nafasi, iwe falme kubwa au ndogo.

38 Na kwa kila ufalme [a]sheria imetolewa; na kwa kila sheria kuna mipaka maalumu pia na taratibu zake.

39 Viumbe wote wasioishi

26 *b* MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.
c 2 Pet. 3:11–14. MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
d Mt. 5:5; M&M 45:58; 59:2; 63:49.
27 *a* MWM Ufufuko.
b 1 Kor. 15:44.
28 *a* MWM Hukumu ya mwisho.
b M&M 43:32; 63:51; 101:31.
29 *a* MWM Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, uwezekano wa kuwa kama Baba wa Mbinguni; Utukufu wa Selestia.
30 *a* MWM Utukufu wa Terestria.
31 *a* MWM Utukufu wa Telestia.
32 *a* Alma 11:41–45.
b MWM Haki ya uamuzi.
34 *a* MWM Utakaso.
35 *a* MWM Uasi.
b MWM Rehema, enye Rehema.
c MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
d Ufu. 22:11; 1 Ne. 15:33–35; 2 Ne. 9:16; Alma 7:21.
37 *a* M&M 78:15.
38 *a* M&M 88:13.

katika [a]taratibu hizo [b]hawahesabiwi haki.

40 Kilicho [a]akili huambatana na akili; [b]hekima hupokea hekima; [c]kweli huikumbatia kweli; [d]wema hupenda wema; [e]nuru huambatana na nuru; rehema huonyesha [f]huruma juu ya rehema na hudai chake; haki huchukua mkondo wake na kudai chake; hukumu huenda mbele ya uso wa yule ambaye huketi juu ya kiti cha enzi na atawalaye na kuviongoza vitu vyote.

41 [a]Ajuaye vitu vyote, na vitu vyote viko mbele yake, na vitu vyote humzunguka yeye; na yeye yu juu ya vitu vyote, na ndani ya vitu vyote, na apita vitu vyote, na amevizunguka vitu vyote; na vitu vyote viko kwake, na ni vyake yeye, hata Mungu, milele na milele.

42 Na tena, amini ninawaambia, yeye ametoa sheria kwa vitu vyote, ambazo kwa hizo vinakwenda katika [a]nyakati zake na majira yake;

43 Na njia zao zimewekwa, hata njia za mbinguni na duniani, ambazo huielewa dunia na sayari zote.

44 Nazo hupeana [a]nuru katika nyakati zao na majira yao, katika dakika zao, katika masaa yao, katika siku zao, katika wiki zao, katika miezi yao, katika miaka yao—hivi vyote ni mwaka [b]mmoja kwa Mungu, lakini siyo kwa mwanadamu.

45 Dunia hubiringika kwa mabawa yake, nalo [a]jua hutoa mwanga wake mchana, nao mwezi hutoa mwangaza wake usiku, nazo nyota pia hutoa mwanga wake, wakiwa wanabingirika juu ya mbawa zao katika utukufu wao, katikati ya [b]uwezo wa Mungu.

46 Nitazilinganisha na nini falme hizi, ili muweze kuelewa?

47 Tazama, hizi zote ni falme, na mtu yeyote aliyoiona yoyote au ndogo ya hizi [a]amemwona Mungu akitembea katika ukuu na uwezo wake.

48 Ninawaambia, huyo amemwona; hata hivyo, yule ambaye alikuja kwa walio [a]wake hakutambuliwa.

49 [a]Nuru yang'ara gizani, na giza haiitambui; hata hivyo, siku itakuja [b]mtakayomjua Mungu, mkiwa mmehuishwa ndani yake na yeye mwenyewe.

50 Ndipo mtajua ya kuwa mmeniona Mimi, kwamba Mimi ndiye, na kwamba Mimi ni nuru ya kweli niko ndani

39 *a* M&M 130:20–21.
b MWM Hesabu kwa haki, Kuhesabiwa haki.
40 *a* MWM Akili, Viumbe-akili-asilia.
b MWM Hekima.
c MWM Ukweli.
d MWM Wema.
e MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
f MWM Huruma.
41 *a* 1 Yoh. 3:20; 1 Ne. 9:6; 2 Ne. 9:20; M&M 38:1–3. MWM Kujua yote.
42 *a* Dan. 2:20–22; Ibr. 3:4–19.
44 *a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
b Zab. 90:4; 2 Pet. 3:8.
45 *a* Mwa. 1:16; Ibr. 4:16.
b M&M 88:7–13.
47 *a* Alma 30:44; Musa 1:27–28; 6:63; Ibr. 3:21.
48 *a* Yn. 1:11; 3 Ne. 9:16; M&M 39:1–4.
49 *a* M&M 6:21; 50:23–24; 84:45–47.
b Yn. 17:3; M&M 93:1, 28.

yenu, na ninyi mu ndani yangu; vinginevyo msingelifanikiwa.

51 Tazama, nitazilinganisha falme hizi na mtu mwenye shamba, na aliwapeleka watumishi wake katika shamba ili kulima.

52 Na akamwambia wa kwanza: Nenda ukafanye kazi shambani, na saa moja nitakuja kwako, nawe utaiona shangwe usoni mwangu.

53 Na akamwambia wa pili: Nenda pia shambani, na mnamo saa mbili nami nitakutembelea nikiwa na shangwe usoni mwangu.

54 Na pia kwa yule wa tatu, akisema: Nitakutembelea;

55 Na kwa wanne, na kuendelea hadi wa kumi na wawili.

56 Na Bwana wa shamba akaenda kwa wa kwanza katika saa ya kwanza, na akakaa naye saa hiyo yote, naye alifanywa mwenye furaha kwa nuru ya uso wa Bwana wake.

57 Na halafu akajitoa kwa yule wa kwanza ili aweze kumtembelea wa pili pia, na wa tatu, na wa nne, na kuendelea hadi wa kumi na wawili.

58 Na hivyo wote walipata nuru ya uso wa bwana wao, kila mtu katika saa yake, na katika wakati wake, na katika majira yake—

59 Akianzia yule wa kwanza, na kuendelea hadi wa [a]mwisho, na kutoka wa mwisho hadi wa kwanza, na kutoka wa kwanza hadi wa mwisho;

60 Kila mtu katika mpangilio wake, hadi saa yake ilipokwisha, hata kulingana na bwana alivyomwamuru, ili bwana wake apate kutukuzwa ndani yake, na yeye ndani ya bwana wake, ili wote waweze kutukuzwa.

61 Kwa hiyo, kwa mfano huu ninazifananisha falme hizi zote, na [a]wakazi wake—kila ufalme katika saa yake, na wakati wake, na katika majira yake, hata kulingana na kiwango ambacho Mungu amekiweka.

62 Na tena, amini ninawaambia, [a]marafiki zangu, ninayaacha maneno haya kwenu ili [b]muyatafakari katika mioyo yenu, pamoja na amri hii ambayo ninaitoa kwenu, kwamba [c]mtanilingana maadamu Mimi nipo karibu—

63 [a]Sogeeni karibu nami na mimi nitasogea karibu na ninyi; [b]nitafuteni kwa bidii nanyi [c]mtanipata; ombeni, nanyi mtapewa; bisheni, nanyi mtafunguliwa.

64 Na lolote [a]muombalo kwa Baba katika jina langu mtapewa, lile lililo [b]muhimu kwenu;

65 Na ikiwa mtaomba kitu chochote ambacho siyo [a]muhimu kwenu, kitageuka kuwa [b]hukumu kwenu.

66 Tazama, kile mkisikiacho ni kama [a]sauti ya mtu aliaye

59 *a* Mt. 20:1–16.
61 *a* M&M 76:24.
62 *a* M&M 84:63; 93:45.
b MWM Tafakari.
c Isa. 55:6; Yak. (Bib.) 1:5; M&M 46:7.
63 *a* Zek. 1:3; Yak. (Bib.) 4:8; Ufu. 3:20.
b 1 Nya. 28:9; Eth. 12:41; M&M 101:38.
c M&M 4:7; 49:26.
64 *a* MWM Sala.
b M&M 18:18; 46:28–30.
65 *a* Yak. (Bib.) 4:3.
b M&M 63:7–11.
66 *a* Isa. 40:3; 1 Ne. 17:13; Alma 5:37–38; M&M 128:20.

nyikani—nyikani, kwa sababu hamwezi kumwona—sauti yangu, kwa sababu sauti yangu ni [b]Roho, Roho yangu ndiyo kweli; [c]kweli hudumu na wala haina mwisho; na kama ikiwa ndani yenu mtafanikiwa.

67 Na kama macho yenu yatakuwa katika [a]utukufu wangu [b]pekee, miili yenu yote itajazwa na nuru, na hakutakuwa na giza ndani yenu; na mwili ule uliojazwa na nuru [c]hufahamu mambo yote.

68 Kwa hiyo, [a]jitakaseni, ili [b]mawazo yenu yawe juu ya Mungu, na siku zitakuja ambazo [c]mtamwona yeye; kwani atauficha uso wake kwenu, nayo itakuwa katika wakati wake mwenyewe, na katika njia yake mwenyewe, na kulingana na mapenzi yake mwenyewe.

69 Ikumbukeni ahadi ile iliyo kuu na ya mwisho niliyoifanya kwenu; yaondoeni mbali mawazo yenu [a]potovu na [b]vicheko vyenu vilivyokithiri.

70 Kaeni, kaeni mahali hapa, na itisheni kusanyiko la kiroho, la wale wote walio wafanyakazi wa kwanza katika ufalme huu wa mwisho.

71 Na wale ambao [a]wameonywa katika safari zao na wamlingane Bwana, na kutafakari onyo hilo walilolipokea mioyoni mwao, kwa kipindi kifupi.

72 Tazama na lo, nitalichunga kundi lenu, na kuwainua wazee na kuwatuma kwao.

73 Tazama, nitaiharakisha kazi yangu katika wakati wake.

74 Na ninatoa kwenu, ninyi mlio [a]wafanyakazi wa kwanza katika ufalme huu wa mwisho, amri kuwa jikusanyeni pamoja, na jipangeni, na jiandaeni, na [b]jitakaseni; ndiyo, itakaseni mioyo yenu, na [c]iosheni mikono na miguu yenu mbele zangu, ili niweze kuwafanya kuwa [d]safi;

75 Ili niweze kushuhudia kwa [a]Baba yenu, na Mungu wenu, na Mungu wangu, kwamba ninyi ni wasafi kutokana na damu ya kizazi hiki kiovu; ili niweze kutimiza ahadi hii, ahadi iliyo kuu na ya mwisho, niliyofanya kwenu, wakati nitakapotaka.

76 Pia, ninatoa amri kwenu ya kuwa endeleeni katika [a]sala na [b]kufunga tangu sasa na kuendelea.

77 Na ninatoa kwenu amri ya

66 *b* MWM Nuru, Nuru ya Kristo; Roho Mtakatifu.
c MWM Ukweli.
67 *a* Yn. 7:18.
b Mt. 6:22; Lk. 11:34–36; M&M 82:19.
c Mit. 28:5; M&M 93:28. MWM Utambuzi, Kipawa cha.
68 *a* MWM Utakaso.
b MWM Nia.
c M&M 67:10–13; 93:1; 97:15–17.
69 *a* Mt. 12:36; Mos. 4:29–30; Alma 12:14.
b M&M 59:15; 88:121.
71 *a* MWM Onya, Onyo.
74 *a* Mt. 20:1, 16.
b Law. 20:7–8; 3 Ne. 19:28–29; M&M 50:28–29; 133:62.
c MWM Safi na Isiyo safi.
d Eth. 12:37.
75 *a* MWM Baba wa Mbinguni; Mungu, Uungu—Mungu Baba; Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, mtoto wa kiroho wa Baba wa Mbinguni.
76 *a* MWM Sala.
b MWM Funga, Kufunga.

kuwa [a]mfundishane [b]mafundisho ya ufalme.

78 Fundishaneni kwa bidii na [a]neema yangu itakuwa pamoja nanyi, ili mpate [b]kuelekezwa kiukamilifu zaidi katika nadharia, katika kanuni, katika mafundisho, katika sheria za injili, katika mambo yale yote yahusuyo ufalme wa Mungu, yale yaliyo muhimu kwenu kuyafahamu;

79 Juu ya mambo kote [a]mbinguni na duniani, na chini ya dunia; mambo yaliyokuwepo, mambo yaliyopo, mambo ambayo hayana budi kutokea upesi; mambo yaliyoko nyumbani, mambo yaliyoko ng'ambo; [b]vita na mifadhaiko ya mataifa, na hukumu zilizoko juu ya nchi; na maarifa pia juu ya nchi na falme—

80 Ili mpate kuandaliwa katika mambo yote wakati nitakapowatuma tena kutukuza wito ambao nimewaitia, na huduma ambayo kwayo nimewapa mamlaka.

81 Tazama, nimewatuma ninyi kwenda [a]kushuhudia na kuwaonya watu, na ni wajibu wa kila mtu ambaye ameonywa [b]amwonye jirani yake.

82 Kwa hiyo, wameachwa pasipo udhuru, na dhambi zao ziko juu ya vichwa vyao wenyewe.

83 Yule [a]anitafutaye [b]mapema ataniona, na wala hatasahaulika.

84 Kwa hiyo, kaeni, na fanyeni kazi kwa bidii, ili mpate kukamilishwa katika huduma yenu ya kwenda miongoni mwa [a]Wayunani kwa mara ya mwisho, wengi kadiri kinywa cha Bwana kitakavyo wataja, ili [b]kuifunga sheria na kutia muhuri ushuhuda, na kuwaandaa watakatifu kwa ajili ya saa ya hukumu ambayo itakuja;

85 Kwamba roho zao ziweze kuepuka ghadhabu ya Mungu, [a]chukizo la uharibifu ambalo linawangoja waovu, kote katika ulimwengu huu na ulimwengu ujao. Amini, ninawaambia, acha wale wazee ambao sio wa kwanza waendelee katika shamba la mizabibu hadi kinywa cha Bwana [b]kitakapowaita, kwani wakati wao bado haujafika; mavazi yao bado hayajawa [c]safi kutokana na damu ya kizazi hiki.

86 Kaeni katika [a]uhuru ambamo humo mmefanywa kuwa [b]huru; wala [c]msinaswe [d]dhambini, bali mikono yenu na iwe [e]safi, hadi Bwana ajapo.

87 Kwani baada ya siku hizi

77 *a* MWM Fundisha, Mwalimu.
b MWM Mafundisho ya Kristo.
78 *a* MWM Neema.
b M&M 88:118; 90:15; 93:53.
79 *a* MWM Mbinguni.
b MWM Vita.
81 *a* MWM Shuhudia.
b M&M 63:58.
MWM Onya, Onyo.
83 *a* Kum. 4:29–31; Yer. 29:12–14; M&M 54:10.
b Alma 37:35.
84 *a* JS—H 1:41.
b Isa. 8:16–17.
85 *a* Mt. 24:15.
b M&M 11:15.
c 1 Ne. 12:10–11; Yak. (KM) 1:19; 2:2; M&M 112:33.
MWM Safi na Isiyo safi.
86 *a* Mos. 5:8.
MWM Huru, Uhuru.
b Yn. 8:36.
MWM Haki ya uamuzi; Huru, Uhuru.
c Gal. 5:1.
d MWM Dhambi.
e Ayu. 17:9; Zab. 24:4; Alma 5:19.

chache na [a]dunia [b]itatetemeka na kulewa lewa kama mlevi; nalo [c]jua litauficha uso wake, na litakataa kutoa mwangaza; nao mwezi utaogeshwa katika [d]damu; nazo [e]nyota zitashikwa na hasira, na kujiangusha chini kama mti wa mtini upukutishavyo mapooza yake.

88 Na baada ya ushuhuda wenu yaja ghadhabu na uchungu kwa watu.

89 Kwani baada ya ushuhuda wenu waja ushuhuda wa [a]matetemeko ya ardhi, ambayo yatasababisha sauti za kuelemewa katikati yake, na watu wataanguka juu ya ardhi na wala hawataweza kusimama.

90 Na pia waja ushuhuda wa [a]sauti ya ngurumo za radi, na sauti za radi, na sauti za tufani, na sauti za mawimbi ya bahari yakipanda na kushuka yenyewe hata nje ya mipaka yake.

91 Na vitu vyote vitakuwa katika [a]vurugu; na hakika, watu watavunjika mioyo; kwa kuwa hofu itakuja juu ya watu wote.

92 Na [a]malaika wataruka katikati ya mbingu, wakilia kwa sauti kuu, wakipiga parapanda ya Mungu, wakisema: Jitayarisheni, jitayarisheni, Enyi wakazi wa dunia; kwani hukumu ya Mungu wetu imefika. Tazama, na lo, [b]Bwana harusi anakuja; nendeni nje kumlaki.

93 Na mara patatokea [a]ishara kuu mbinguni, na watu wote wataiona kwa pamoja.

94 Na malaika mwingine atapiga parapanda yake, akisema: Lile [a]kanisa [b]kuu, [c]mama wa machukizo, aliyeyafanya mataifa yote kunywa mvinyo wa ghadhabu ya [d]uasherati wake, ambaye huwatesa watakatifu wa Mungu, ambaye humwaga damu zao—yeye aketiye juu ya maji mengi, na juu ya visiwa vya bahari—tazama, yeye ndiye [e]magugu ya dunia; amefungwa katika mafungu; kamba zake zimefanywa imara, hakuna mtu awezaye kuzifungua; kwa hiyo, yuko tayari [f]kuchomwa. Naye atapiga parapanda yake nayo itazidi kulia sana, na mataifa yote yataisikia.

95 Na patakuwa na [a]ukimya mbinguni kwa kipindi cha nusu saa; na mara baada ya hapo mapazia ya mbinguni yatafunguliwa, kama [b]ukurasa uliokunjuliwa baada ya kukunjwa, na [c]uso wa Bwana utafunuliwa;

96 Na watakatifu waliopo juu ya dunia, walio hai, watahuishwa na [a]kunyakuliwa

87 *a* Isa. 13:4–13.
b M&M 43:18.
c Yoe. 2:10; M&M 45:42; 133:49.
d Ufu. 6:12.
e Yoe. 3:15.
89 *a* M&M 45:33.
90 *a* Ufu. 8:5; M&M 43:17–25.
91 *a* M&M 45:26.
92 *a* Ufu. 8:13; M&M 133:17.
b Mt. 25:1–13; M&M 33:17; 133:10, 19.
93 *a* Mt. 24:30; Lk. 21:25–27. MWM Ishara za Nyakati.
94 *a* MWM Ibilisi—Kanisa la ibilisi.
b 1 Ne. 13:4–9.
c Ufu. 17:5.
d Ufu. 14:8.
e Mt. 13:38.
f M&M 64:23–24; 101:23–25. MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia.
95 *a* M&M 38:12.
b Ufu. 6:14.
c MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
96 *a* 1 The. 4:16–17.

mawinguni kwenda kumlaki yeye.

97 Na wale waliolala makaburini mwao [a]wataamka, kwani makaburi yao yatafunuliwa; nao pia watanyakuliwa kwenda kumlaki yeye katikati ya nguzo ya mbinguni—

98 Hawa ndiyo walio wa Kristo, [a]malimbuko ya kwanza, hawa ndiyo watakaoshuka pamoja naye kwanza, na wale walioko juu ya dunia na katika makaburi yao, ambao watanyakuliwa kwenda kumlaki yeye; na hii yote ni kwa sauti ya kupigwa parapanda ya malaika wa Mungu.

99 Na baada ya hii malaika mwingine atapiga, ambayo ni parapanda ya pili; na halafu utakuja ukombozi wa wale walio wa Kristo katika ujio wake; wale ambao wamepata sehemu yao katika kile [a]kifungo kilichotayarishwa kwa ajili yao, ili wapate kuipokea injili, na [b]kuhukumiwa kulingana na wanadamu katika mwili.

100 Na tena, parapanda nyingine italia, ambayo ni parapanda ya tatu; na halafu zitakuja [a]roho za watu ambao wanatakiwa kuhukumiwa, nao wanapatikana na [b]hatia;

101 Na hawa ndiyo masalia ya [a]wafu; nao hawakuwa hai tena hadi itimie ile miaka [b]elfu, wala hawataishi tena, hadi mwisho wa dunia.

102 Na parapanda nyingine italia, ambayo ni parapanda ya nne, ikisema: Wamepatikana miongoni mwa wale ambao watasalia hadi siku ile kuu na ya mwisho, hata mwisho, wenye uchafu ambao watazidi kuwa [a]wachafu.

103 Na parapanda nyingine italia, ambayo ni parapanda ya tano, ambayo ni ya malaika wa tano ambaye ataleta [a]injili isiyo na mwisho—akiruka katikati ya mbingu, kwa mataifa yote, makabila, lugha, na watu;

104 Na hii itakuwa sauti ya parapanda yake, ikisema kwa watu wote, kote mbinguni na duniani, na wale walioko chini ya dunia—kwani [a]kila sikio litasikia, na kila goti [b]litapigwa, na kila ulimi utakiri, wakati wasikiapo sauti ya parapanda, ikisema: [c]Mcheni Mungu na kumtukuza yeye aketiye juu ya kiti chake cha enzi, milele na milele; kwani saa ya hukumu yake imefika.

105 Na tena, malaika mwingine atapiga parapanda yake, ambaye ni malaika wa sita, akisema: [a]Ameanguka yule aliyefanya mataifa yote kunywa mvinyo ya ghadhabu ya

97 *a* M&M 29:13; 45:45–46; 133:56. MWM Ufufuko.
98 *a* 1 Kor. 15:23.
99 *a* M&M 76:73; 138:8. MWM Wokovu kwa ajili ya Wafu.
b 1 Pet. 4:6.
100 *a* Ufu. 20:12–13; Alma 11:41; M&M 43:18; 76:85.
b MWM Shutuma, Shutumu.
101 *a* Ufu. 20:5.
b MWM Milenia.
102 *a* MWM Chafu, Uchafu.
103 *a* Ufu. 14:6–7. MWM Urejesho wa Injili.
104 *a* Ufu. 5:13.
b Isa. 45:23; Flp. 2:9–11.
c MWM Hofu—Hofu juu ya Mungu; Uchaji.
105 *a* Ufu. 14:8; M&M 1:16.

uasherati wake; ameanguka, ameanguka!

106 Na tena, malaika mwingine atapiga parapanda yake, ambaye ni malaika wa saba, akisema: Imekwisha; imekwisha! [a]Mwanakondoo wa Mungu [b]ameshinda na [c]amelikanyaga shinikizo pekee yake, hata shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mwenyezi Mungu.

107 Na halafu malaika hawa watavikwa mataji ya utukufu wa uwezo wake, nao [a]watakatifu watajawa na [b]utukufu wake, na kupokea [c]urithi wao na watafanywa kuwa [d]sawa naye.

108 Na halafu malaika wa kwanza atapiga parapanda yake tena katika masikio ya wote walio hai, na [a]kufunua matendo ya siri ya wanadamu, na matendo makuu ya Mungu katika miaka [b]elfu moja ya kwanza.

109 Na halafu malaika wa pili atapiga parapanda yake, na kufichua matendo ya siri ya wanadamu, na mawazo na dhamira za mioyo yao, na matendo makuu ya Mungu katika miaka elfu moja ya pili—

110 Na kuendelea, hadi malaika wa saba atakapopiga parapanda yake; naye atasimama juu ya nchi na juu ya bahari, na kuapa katika jina lake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, ya kwamba hapatakuwa na [a]wakati baada ya haya; na [b]Shetani atafungwa, yule nyoka wa zamani, anayeitwa ibilisi, na hataachiliwa kwa kipindi cha miaka [c]elfu.

111 Na halafu [a]ataachiliwa kwa kipindi kifupi, ili apate kuyakusanya pamoja majeshi yake.

112 Na [a]Mikaeli, yule malaika wa saba, hata malaika mkuu, atayakusanya pamoja majeshi yake, hata majeshi ya mbinguni.

113 Naye ibilisi atayakusanya pamoja majeshi yake; hata majeshi ya jehanamu, na atakuja kupambana dhidi ya Mikaeli na majeshi yake.

114 Na halafu linakuja [a]pambano la Mungu mkuu; na ibilisi na majeshi yake watatupwa mahali pao wenyewe, kiasi kwamba wasipate kabisa uwezo tena juu ya watakatifu.

115 Kwani Mikaeli atapigana mapambano yao, na atamshinda yule [a]atafutaye kiti cha enzi cha yule aketiye juu ya kiti cha enzi, hata Mwanakondoo.

116 Huu ndiyo utukufu wa Mungu, na walio [a]takaswa; nao kamwe hawataona [b]mauti tena.

117 Kwa hiyo, amini ninawaambia, [a]marafiki zangu, itisheni

106 *a* MWM Mwanakondoo wa Mungu.
b 1 Kor. 15:25.
c Isa. 63:3–4; Ufu. 19:15; M&M 76:107; 133:50.
107 *a* MWM Mtakatifu.
b MWM Utukufu wa Selestia.
c MWM Kuinuliwa.
d M&M 76:95.
108 *a* Alma 37:25; M&M 1:3.
b M&M 77:6–7.
110 *a* M&M 84:100.
b Ufu. 20:1–3; 1 Ne. 22:26; M&M 101:28. MWM Ibilisi.
c MWM Milenia.
111 *a* M&M 29:22; 43:30–31.
112 *a* MWM Mikaeli.
114 *a* Ufu. 16:14.
115 *a* Isa. 14:12–17; Musa 4:1–4.
116 *a* MWM Kuinuliwa; Utakaso.
b Ufu. 21:4; Alma 11:45; 12:18; M&M 63:49. MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
117 *a* M&M 109:6.

kusanyiko lenu la kiroho, kama nilivyowaamuru.

118 Na kwa vile wote hamna imani, tafuteni kwa bidii na [a]kufundishana maneno ya [b]hekima; ndiyo, tafuteni kutoka kwenye [c]vitabu vizuri maneno ya hekima; tafuteni maarifa, hata kwa kujifunza na pia kwa imani.

119 Jiandaeni wenyewe; tayarisheni kila kitu kinachohitajika; na ijengeni [a]nyumba, hata nyumba ya sala, nyumba ya kufunga, nyumba ya imani, nyumba ya kujifunza, nyumba ya utukufu, nyumba ya utaratibu, nyumba ya Mungu;

120 Ili kuingia kwenu kuweze kuwa katika jina la Bwana; na kutoka kwenu kuweze kuwa katika jina la Bwana; kwamba salamu zenu zote zipate kuwa katika jina la Bwana, na kuinua mikono kwa Aliye Juu Sana.

121 Kwa hiyo, [a]acheni mazungumzo yenu yasiyo na maana, [b]vicheko na [c]tamaa zenu zote zilizo mbaya, na [d]majivuno na upuuzi wenu wote, na matendo yenu yote yaliyo maovu.

122 Chagueni mwalimu miongoni mwenu, na wote wasiwe wazungumzaji kwa wakati mmoja; bali azungumze mmoja na wengine wote wasikilize maneno yake, ili wote watakapokuwa wamezungumza wote wapate kujengana, na kwamba kila mmoja apate kuwa na nafasi sawa.

123 Jitahidini [a]kupendana; acheni [b]kutamani; jifunzeni kupeana kama injili inavyotaka.

124 Acheni kuwa [a]wavivu; acheni kuwa wachafu; acheni [b]kutafutana makosa; acheni kulala kupita inavyotakiwa; laleni vitandani mwenu mapema, ili msichoke; amkeni mapema, ili miili yenu na akili zenu zipate kutiwa nguvu.

125 Na zaidi ya yote, jivikeni wenyewe kwa kifungo cha [a]hisani, kama vile joho, lililo kifungo cha ukamilifu na [b]amani.

126 [a]Ombeni daima, wala msikate tamaa, hadi [b]nitakapokuja. Tazama, na lo, naja haraka, niwakaribishe kwangu. Amina.

127 Na tena, utaratibu wa nyumba uliotayarishwa kwa ajili ya urais wa [a]shule ya manabii, iliyoanzishwa kwa ajili ya mafundisho yao katika mambo yote yaliyo muhimu kwao, hata kwa [b]maofisa wote wa kanisa, au katika maneno mengine, wale walioitwa kwenye huduma katika kanisa, kuanzia makuhani wakuu, hata chini kwa mashemasi—

128 Na huu ndiyo utakuwa utaratibu wa nyumba ya

118 *a* M&M 88:76–80. MWM Fundisha, Mwalimu. *b* MWM Hekima. *c* M&M 55:4; 109:7, 14.
119 *a* M&M 95:3; 97:10–17; 109:2–9; 115:8. MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.
121 *a* M&M 43:34; 100:7. *b* M&M 59:15; 88:69. *c* MWM Tamaa za kimwili. *d* MWM Kiburi.
123 *a* MWM Upendo. *b* MWM Tamani.
124 *a* MWM Mvivu, Uvivu. *b* M&M 64:7–10. MWM Kusema uovu.
125 *a* MWM Hisani. *b* MWM Amani.
126 *a* MWM Sala. *b* M&M 1:12.
127 *a* MWM Shule ya Manabii. *b* MWM Ofisa, Ofisi.

urais wa shule: Yule aliyeteuliwa kuwa rais, au mwalimu, atasimama katika mahali pake, katika nyumba ambayo itaandaliwa kwa ajili yake.

129 Kwa hiyo, atakuwa mtu wa kwanza katika nyumba ya Mungu, katika mahala ambapo mkutano uliomo ndani ya nyumba utaweza kusikia maneno yake kwa usahihi na ufasaha, pasipo sauti kubwa.

130 Na wakati ajapo ndani ya nyumba ya Mungu, kwa kuwa yampasa kwanza kuwa katika nyumba—tazama, hii ni vizuri ili apate kuwa mfano—

131 Na [a]ajitoe yeye mwenyewe katika sala kwa kupiga magoti mbele za Mungu, katika ishara na kumbukumbu ya agano lisilo na mwisho.

132 Na wakati mtu yeyote atakapoingia baada yake, mwalimu na asimame, na, akiinua mikono mbinguni, ndiyo, hata wima, amsalimu kaka yake au ndugu yake kwa maneno haya:

133 Wewe ni kaka au ndugu? Ninakusalimu katika jina la Bwana Yesu Kristo, katika ishara au kumbukumbu ya agano lisilo na mwisho, agano ambalo kwalo ninakupokea wewe kuwa [a]mshiriki mwenzangu, katika dhamira ambayo ni imara, isiyoondosheka, na isiyobadilika, kuwa rafiki yako na [b]kaka yako kwa neema ya Mungu katika kifungo cha upendo, kutembea katika amri zote za Mungu pasipo doa, na kwa shukrani, milele na milele. Amina.

134 Na yule ambaye atapatikana hastahili salamu hii hatakuwa na nafasi miongoni mwenu; kwani ninyi hamtaruhusu nyumba yangu [a]ichafuliwe na mtu huyo.

135 Na yule aingiaye na kuwa mwaminifu mbele zangu, na ni ndugu, au kama wao wakiwa ndugu zake, watamsalimu rais au mwalimu wakiwa wamenyanyua mikono mbinguni, kwa sala hiyo hiyo moja na agano hilo, au kwa kusema Amina, katika ishara hiyo hiyo.

136 Tazama, amini ninawaambia, huu ndiyo utaratibu kwenu kwa kusalimiana katika nyumba ya Mungu, katika shule ya manabii.

137 Nanyi mmeitwa kufanya hivi kwa sala na kwa shukrani, kama Roho atakavyonena katika shughuli zenu zote katika nyumba ya Bwana, katika shule ya manabii, ili ipate kuwa mahali patakatifu, na hema takatifu ya Roho Mtakatifu kwa [a]kuwajenga ninyi.

138 Na hamtampokea yeyote miongoni mwenu katika shule hii isipokuwa amekuwa safi kutokana na [a]damu ya kizazi hiki;

139 Na atapokelewa kwa ibada ya [a]kutawadha miguu, kwani ni kwa madhumuni haya ibada hii ya kutawadha miguu ilianzishwa.

140 Na tena, ibada ya kuta-

131 *a* MWM Kuabudu.
133 *a* MWM Ushirika.
b MWM Dada; Kaka, Ndugu.
134 *a* M&M 97:15–17; 110:7–8.
137 *a* M&M 50:21–24.
138 *a* M&M 88:74–75, 84–85.
139 *a* MWM Osha, Oshwa, Uoshaji.

wadha miguu itahudumiwa na rais, au mzee kiongozi wa kanisa.

141 Itaanza kwa sala; na baada ya [a]kupokea mkate na divai, atajifunga yeye mwenyewe kulingana na [b]utaratibu uliotolewa katika mlango wa kumi na tatu ya ushuhuda wa Yohana juu yangu mimi. Amina.

SEHEMU YA 89

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 27 Februari 1833. Kama matokeo ya viongozi wa awali kutumia tumbaku katika mikutano yao, Nabii aliongozwa kutafakari juu ya jambo hili; matokeo yake, alimwuliza Bwana kuhusiana na jambo hilo. Ufunuo huu, unaojulikana kama Neno la Hekima, ulikuwa ndiyo jibu.

1–9, Matumizi ya mvinyo, vinywaji vikali, tumbaku, na vinywaji vya moto vinakatazwa; 10–17, Majani, matunda, nyama, na nafaka vimewekwa kwa matumizi ya wanadamu na ya wanyama; 18–21, Utii kwa sheria ya injili, pamoja na Neno la Hekima, huleta baraka za kimwili na kiroho.

[a]Neno la Hekima, kwa manufaa ya baraza la makuhani wakuu, waliokusanyika Kirtland, na kanisa, na pia watakatifu katika Sayuni—

2 Kwa kutuma salamu; siyo kwa amri au kwa lazima, ila kwa ufunuo na neno la hekima, ambalo huonyesha mpango na [a]mapenzi ya Mungu katika wokovu wa kimwili wa watakatifu wote katika siku za mwisho—

3 Limetolewa kwa kanuni yenye [a]ahadi, na kuchukuliwa kwa kiwango cha wadhaifu na wadhaifu zaidi ya [b]watakatifu wote, ambao ni au wanaweza kuitwa watakatifu.

4 Tazama, amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu: Kwa sababu ya [a]uovu na njama ambazo zipo na zitaendelea kuwepo katika mioyo ya watu [b]wenye kula njama katika siku za mwisho, [c]nimewaonya, na ninawaonya mapema, kwa kuwapa ninyi hili neno la hekima kwa ufunuo—

5 Kwamba ikiwa mtu yeyote anakunywa [a]divai au kinywaji kikali miongoni mwenu, tazama hivyo siyo vyema, wala haifai machoni pa Baba yenu, isipokuwa tu katika kukusanyika kwenu pamoja kutoa sakramenti mbele zake.

141 *a* MWM Sakramenti.
b Yn. 13:4–17.
89 1 *a* MWM Neno la Hekima.
2 *a* M&M 29:34.
MWM Amri za Mungu.
3 *a* M&M 89:18–21.
b MWM Mtakatifu.
4 *a* MWM Danganya, Kudanganya, Udanganyifu.
b MWM Makundi maovu ya siri.
c MWM Onya, Onyo.
5 *a* Law. 10:9–11; Isa. 5:11–12; 1 Kor. 6:10.

6 Na, tazama, hii yapasa kuwa divai, ndiyo, [a]divai halisi ya tunda la mizabibu, mliyotengeneza ninyi wenyewe.

7 Na, tena, [a]vinywaji vikali siyo kwa ajili ya tumbo, ila kwa kuosha miili yenu.

8 Na tena, tumbaku siyo kwa ajili ya [a]mwili, wala kwa tumbo, na siyo nzuri kwa mwanadamu, bali ni dawa kwa ajili ya majeraha na ng'ombe wote wagonjwa, itumiwe kwa kipimo na ujuzi.

9 Na tena, vinywaji vya moto siyo kwa ajili ya mwili au tumbo.

10 Na tena, amini ninawaambia, majani yote ya [a]mimea Mungu ameiweka kwa ajili ya maumbile, sura, na kwa matumizi ya mwanadamu—

11 Kila mmea katika majira yake, na kila tunda katika majira yake; vyote hivi vitumiwe kwa busara na kwa [a]shukrani.

12 Ndiyo, pia [a]nyama ya [b]wanyama na ya ndege wa angani, Mimi, Bwana, nimeviweka kwa matumizi ya wanadamu kwa shukrani; hata hivyo vitumike kwa [c]uangalifu;

13 Na yapendeza kwangu ikiwa havitatumiwa, isipokuwa tu nyakati za baridi, au katika baridi, au njaa.

14 [a]Nafaka zote zimewekwa kwa ajili ya matumizi ya mwanadamu na wanyama, kuwa chakula cha kutegemewa, siyo tu kwa mwanadamu bali hata kwa wanyama wa mashambani, na ndege wa angani, na wanyama wote wa porini wale watembeao au watambaao juu ya dunia;

15 Na hivi Mungu amevitengeneza kwa matumizi ya mwanadamu tu katika nyakati za ukame na njaa kali.

16 Nafaka zote ni nzuri kwa chakula cha mwanadamu; pia kama vile uzao wa mizabibu; ule utoao matunda, iwe katika ardhi au juu ya ardhi—

17 Hata hivyo, ngano kwa mwanadamu, na mahindi kwa ng'ombe, na mtama kwa farasi, na uwele kwa ndege na kwa nguruwe, na kwa wanyama wote wa mashamba, na shayiri ni kwa wanyama wote watumikao, na kwa vinywaji laini, kama vile nafaka nyinginezo.

18 Na watakatifu wote ambao wanakumbuka kushika na kutenda maneno haya, wakitembea katika utii kwa amri hizi, watapata [a]afya mwilini mwao na mafuta mifupani mwao;

19 Na watapata [a]hekima na hazina kubwa ya [b]maarifa, hata hazina zilizofichika;

20 Na [a]watakimbia na wasichoke, na watatembea wala hawatazimia.

6 *a* M&M 27:1–4.
7 *a* Mit. 20:1; 23:29–35.
8 *a* 1 Kor. 3:16–17. MWM Mwili.
10 *a* Mwa. 1:29; M&M 59:17–20.
11 *a* MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
12 *a* Mwa. 9:3; Law. 11:1–8. *b* 1 Tim. 4:3–4; M&M 49:18–21. *c* M&M 59:20.
14 *a* Dan. 1:6–20.
18 *a* Mit. 3:8.
19 *a* MWM Hekima. *b* MWM Maarifa; Ushuhuda.
20 *a* Isa. 40:31.

21 Na Mimi, Bwana, ninatoa [a]ahadi kwao, kwamba malaika mwangamizaji [b]atawapita, kama wana wa Israeli, na hatawaua. Amina.

SEHEMU YA 90

Ufunuo kwa Joseph Smith Nabii, uliotolewa huko Kirtland, Ohio, 8 Machi 1833. Ufunuo huu ni hatua ya kuendelea katika kuanzisha Urais wa Kwanza (ona kichwa cha habari cha sehemu ya 81); kama matokeo yake, washauri waliotajwa walitawazwa 18 Machi 1833.

1–5, Funguo za ufalme zimekabidhiwa kwa Joseph Smith na kupitia kwake kwenda Kanisani; 6–7, Sidney Rigdon na Frederick G. Williams watatumikia katika Urais wa Kwanza; 8–11, Injili itahubiriwa kwa mataifa ya Israeli, kwa Wayunani, na kwa Wayahudi, kila mtu akiisikia katika lugha yake mwenyewe, 12–18, Joseph Smith na washauri wake wataliweka Kanisa katika mpangilio unaostahili, 19–37, Watu binafsi mbalimbali wameshauriwa na Bwana kutembea wima na kutumikia katika ufalme Wake.

Hivyo ndivyo asemavyo Bwana, amini, amini ninakuambia mwanangu, dhambi zako [a]zimesamehewa, kulingana na maombi yako, kwani sala zako na sala za ndugu zako zimenijia masikioni mwangu.

2 Kwa hiyo, umebarikiwa wewe kutoka sasa wewe ubebaye [a]funguo za ufalme zilizotolewa kwako; [b]ufalme ambao unakuja kwa mara ya mwisho.

3 Amini ninakuambia, funguo za ufalme hazitaondolewa kutoka kwako, wakati wewe ukiwapo katika ulimwengu, wala katika ulimwengu ujao;

4 Hata hivyo, kupitia kwako [a]mafunuo ya Mungu yatatolewa kwa mwingine, ndiyo, hata kwa kanisa.

5 Na wale wote ambao hupokea mafunuo ya Mungu, na [a]wajihadhari jinsi wanavyoyashikilia wasije wakayahesabu kuwa kitu rahisi, na wakaletwa chini ya hatia kwa njia hii, na wakajikwaa na kuanguka wakati dhoruba ishukapo, na upepo kuvuma, na [b]mvua kushuka, na kupiga juu ya nyumba zao.

6 Na tena, amini ninawaambia ndugu zako, Sidney Rigdon na Frederick G. Williams, dhambi zao zimesamehewa pia, nao wanahesabiwa kuwa sawa na

21 *a* M&M 84:80.
b Ku. 12:23, 29.
90 1 *a* MWM Samehe.
2 *a* M&M 65:2.
MWM Funguo za Ukuhani.
b MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
4 *a* Mdo. 7:38; Rum. 3:2; Ebr. 5:12; M&M 124:39, 126.
MWM Toa unabii, Unabii.
5 *a* M&M 1:14.
b Mt. 7:26–27.

wewe katika kushikilia funguo hizi za ufalme huu wa mwisho;

7 Kama vile kupitia utawala wako [a]funguo za shule ya manabii, ambayo nimeamuru kuanzishwa;

8 Ili hapo waweze kukamilishwa katika huduma yao kwa wokovu wa Sayuni, na wa mataifa ya Israeli, na wa Wayunani, kadiri wengi watakavyoamini;

9 Ili kupitia huduma yako waweze kupokea neno, na kupitia huduma yao neno liweze kuenea hata miisho ya dunia, kwa [a]Wayunani [b]kwanza, na halafu, tazama, na lo, watageuka kwa Wayahudi.

10 Na halafu yaja siku wakati mkono wa Bwana [a]utakapofunuliwa katika uwezo kwa kuyashawishi mataifa, mataifa ya wapagani, nyumba ya [b]Yusufu, juu ya injili ya wokovu wao.

11 Kwani itakuja kutokea katika siku ile, kwamba kila mtu [a]atasikia utimilifu wa injili katika ulimi wake, na katika lugha yake mwenyewe, kupitia wale [b]waliotawazwa kwa [c]uwezo huu, kwa huduma ya [d]Mfariji, aliyemwagwa juu yao kwa ajili ya ufunuo wa Yesu Kristo.

12 Na sasa, amini nina kuambia, ninakupa amri kuwa uende katika [a]huduma na urais.

13 Na utakapokuwa umemaliza kutafsiri ya manabii, utaanza [a]kusimamia shughuli za kanisa na za [b]shule;

14 Na mara kwa mara, kama itakavyofunuliwa na Mfariji, kupokea [a]mafunuo ili kuzifichua [b]siri za ufalme;

15 Na kuyaweka vyema makanisa, na [a]kusoma na [b]kujifunza, na kuvifahamu vitabu vyote vilivyo vizuri, na [c]lugha, ndimi, na watu.

16 Na hii itakuwa shughuli na kazi yenu katika maisha yenu yote, kuongoza katika baraza, na kuweka vyema mambo yote ya kanisa hili na ufalme.

17 [a]Msiaibike, wala kufadhaika; bali nawaonya kuhusu majivuno na [b]kiburi, kwani hivyo huleta mitego juu ya nafsi zenu.

18 Ziwekeni sawa sawa nyumba zenu; [a]uvivu na [b]uchafu viwekeni mbali na ninyi.

19 Sasa, amini ninakuambia, na ipatikane nafasi, haraka itakavyowezekana, kwa ajili ya familia ya mshauri na mwandishi wako, hata Frederick G. Williams.

20 Na mtumishi wangu mzee

7 *a* MWM Shule ya Manabii.
9 *a* 1 Ne. 13:42; M&M 107:33; 133:8.
b Mt. 19:30; Eth. 13:10–12.
10 *a* M&M 43:23–27; 88:84, 87–92.
b Mwa. 49:22–26; 1 Ne. 15:13–14.
11 *a* MWM Kazi ya kimisionari.
b MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito; Kutawaza, Kutawazwa.
c MWM Ukuhani.
d MWM Mfariji.
12 *a* MWM Kuhudumu.
13 *a* M&M 107:91–92.
b MWM Shule ya Manabii.
14 *a* MWM Ufunuo.
b MWM Siri za Mungu.
15 *a* M&M 88:76–80, 118; 93:53.
b M&M 107:99–100; 130:18–19.
c MWM Lugha.
17 *a* Rum. 1:16; 2 Ne. 6:13.
b M&M 88:121. MWM Kiburi.
18 *a* M&M 58:26–29. MWM Mvivu, Uvivu.
b M&M 38:42.

[a]Joseph Smith, Mkubwa aendelee kukaa pamoja na familia yake mahali anapoishi sasa; na isiuzwe hadi kinywa cha Bwana kitakapotamka.

21 Na mshauri wangu, hata [a]Sidney Rigdon, abaki mahali anapoishi sasa hadi kinywa cha Bwana kitakapotamka.

22 Na askofu atafute kwa bidii ili kumpata [a]wakala, na awe mtu aliye na [b]mali ghalani—mtu wa Mungu, na mwenye imani kubwa—

23 Ili kwamba kwa njia hiyo awezeshwe kufuta kila deni; ili ghala ya Bwana isiweze kudharauliwa mbele za macho ya watu.

24 Tafuteni kwa [a]bidii, [b]ombeni daima, na muwe wenye kuamini, na mambo [c]yote yatafanyika kwa pamoja kwa faida yenu, kama ninyi mnatembea wima na kukumbuka [d]agano ambalo mmeagana ninyi kwa ninyi.

25 Na [a]familia zenu ziwe ndogo, hususani ya mtumishi wangu mzee wa umri Joseph Smith, Mkubwa, juu ya wale ambao si wa familia zenu;

26 Ili vitu vile vilivyotolewa kwa ajili yenu, ili kutimiza kazi yangu, visichukuliwe kutoka kwenu na kupewa wale ambao hawastahili—

27 Na kwa njia hiyo mmezuiliwa katika kukamilisha mambo yale ambayo nimewaamuru.

28 Na tena, amini ninawaambia, ni mapenzi yangu kuwa mjakazi wangu Vienna Jaques apate fedha za kulipia gharama zake, na kwenda katika nchi ya Sayuni;

29 Na masalia ya fedha hizo zaweza kuwekwa wakfu kwangu, naye atapewa thawabu yake katika wakati wangu.

30 Amini ninawaambia, hilo ni jema machoni mwangu kwamba yampasa kwenda katika nchi ya Sayuni, na kupokea urithi kutoka mikononi mwa askofu;

31 Ili akaweze kutulia katika amani ilimradi atakuwa mwaminifu, na asiwe mvivu katika siku zake kuanzia sasa na kuendelea.

32 Na tazama, amini ninawaambia, kuwa ninyi mtaandika amri hii, na kuwaambia ndugu zenu katika Sayuni, katika salamu ya upendo, kuwa nimewateua ninyi pia [a]kuisimamia Sayuni katika wakati wangu mwenyewe.

33 Kwa hiyo, waache kunichosha kuhusu jambo hilo.

34 Tazama, ninawaambia kuwa ndugu zenu katika Sayuni wanaanza kutubu, na malaika wanafurahi juu yao.

35 Hata hivyo, mimi sijapendezwa na mambo mengi; na mimi sijapendezwa na mtumishi wangu [a]William E. McLellin, wala mtumishi wangu Sidney Joseph Smith, Mkubwa, aliwatunza.

20 *a* MWM Smith, Joseph, Mkubwa.
21 *a* MWM Rigdon, Sidney.
22 *a* M&M 84:112–113.
b Yak. (KM) 2:17–19.
24 *a* MWM Bidii.
b MWM Sala.
c Ezra 8:22; Rum. 8:28; M&M 100:15; 122:7–8.
d MWM Agano.
25 *a* MY Masikini ambao
32 *a* M&M 107:91–92.
35 *a* M&M 66:1; 75:6–9.

Gilbert; na askofu pia, na wengineo wanayo mambo mengi ya kutubu.

36 Lakini amini ninawaambia, kwamba Mimi, Bwana, [a]nitagombana na Sayuni, na nitawasihi wenye nguvu wake, na [b]kumrudi hadi ashinde na kuwa [c]safi mbele zangu.

37 Kwani hataondoshwa kwenye mahali pake. Mimi, Bwana, nimenena haya. Amina.

SEHEMU YA 91

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 9 Machi 1833. Nabii kwa wakati huu alikuwa anajishughulisha na tafsiri ya Agano la Kale. Akiwa amefikia kwenye sehemu ya maandishi ya Kale yaitwayo Apokrifa, alimwuliza Bwana na kupokea maelezo haya.

1–3, Apokrifa imetafsiriwa kwa usahihi zaidi ila ina mengi yaliyoongezwa kwa mikono ya wanadamu ambayo siyo ya kweli; 4–6, Inawanufaisha wale wenye kuangazwa na Roho.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana ninyi kuhusu [a]Apokrifa—Kuna mambo mengi yaliyomo ndani yake ambayo ni ya kweli, na imetafsiriwa kwa usahihi sana;

2 Kuna mambo mengi ndani yake ambayo siyo ya kweli, ambayo yameongezwa kwa mikono ya wanadamu.

3 Amini, ninawaambia, kwamba siyo lazima Apokrifa itafsiriwe.

4 Kwa hiyo, yeyote aisomaye, na [a]afahamu, kwani Roho hufunulia ukweli;

5 Na yeyote atakayeangazwa na [a]Roho atapata faida kutoka humo;

6 Na yeyote asiyepokea kwa Roho, hawezi kufaidika nayo. Kwa hiyo siyo lazima kwamba kitafsiriwe. Amina.

SEHEMU YA 92

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 15 Machi 1833. Ufunuo unamwelekeza Frederick G. Williams, ambaye hivi karibuni aliteuliwa kuwa mshauri kwa Joseph Smith, juu ya majukumu yake katika Kampuni ya Ushirika (ona vichwa vya habari vya sehemu ya 78 na 82).

36*a* mwm Sayuni.
b mwm Rudi, Kurudiwa.
c mwm Safi na Isiyo safi.

91 1*a* mwm Apokrifa.
4*a* mwm Ufahamu.
5*a* mwm Maongozi ya Mungu, Shawishi; Roho Mtakatifu.

1–2, Bwana hutoa amri juu ya kujiunga na mpango wa ushirika.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, nimetoa kwa [a]mpango wa ushirika, ulioundwa kulingana na amri nilizotoa hapo awali, ufunuo na amri kuhusu mtumishi wangu Frederick G. Williams, kuwa yawapasa kumpokea katika ushirika. Nisemacho kwa mmoja ninasema kwa wote.

2 Na tena, ninakuambia mtumishi wangu Frederick G. Williams, utakuwa mshiriki hai katika ushirika huu; na kadiri utakavyokuwa mwaminifu katika kushika amri zote za zamani nawe utabarikiwa milele. Amina.

SEHEMU YA 93

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 6 Mei 1833.

1–5, Wote walio waaminifu watamwona Bwana; 6–18, Yohana anashuhudia kuwa Mwana wa Mungu alikwenda neema hadi neema mpaka yeye akapokea utimilifu wa utukufu wa Baba; 19–20, Watu waaminifu, wanaokwenda neema hadi neema, pia nao watapata utimilifu Wake; 21–22, Wale walio wazaliwa kupitia Kristo ndiyo Kanisa la Mzaliwa wa Kwanza; 23–28, Kristo alipokea utimilifu wa ukweli wote, na mwanadamu kwa utii anaweza kufanya vivyo hivyo; 29–32, Mwanadamu mwanzoni alikuwa pamoja na Mungu; 33–35, Vitu vya asili ni vya milele, na mwanadamu aweza kupokea utimilifu wa furaha shangwe katika Ufufuko; 36–37, Utukufu wa Mungu ni akili; 38–40, Watoto hawana hatia mbele za Mungu kwa sababu ya ukombozi wa Kristo; 41–53, Ndugu viongozi wanaamriwa kuziweka sawa sawa familia zao.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Itakuwa kwamba kila mtu [a]atakayeziacha dhambi zake na kuja kwangu, na [b]kulilingana jina langu, na [c]kuitii sauti yangu, na kushika amri zangu, [d]atauona [e]uso wangu na kujua kuwa Mimi ndiye;

2 Na kuwa Mimi ni [a]nuru ya kweli imwangazayo kila mtu ajaye ulimwenguni;

3 Na kuwa Mimi ni [a]ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu,

92 1*a* M&M 82:11, 15–21. MWM Mpango wa Ushirika.

93 1*a* MWM Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki; Toba, Tubu.
b Yoe. 2:32.
c MWM Mtiifu, Tii, Utii.
d Ku. 33:11; M&M 38:7–8; 67:10–12; 88:68; 101:23; 130:3. MWM Mfariji.
e TJS 1 Yoh. 4:12 (Kiambatisho).
2*a* Yn. 1:4–9; M&M 14:9; 84:45–47; 88:6–7. MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
3*a* Yn. 10:25–38; 17:20–23; M&M 50:43–45.

na kuwa Baba na Mimi tu wamoja—

4 Baba kwa [a]sababu [b]amenipa Mimi utimilifu wake, na Mwana kwa sababu nilikuwepo ulimwenguni na kufanya [c]mwili kuwa hema takatifu yangu, na kuishi miongoni mwa wanadamu.

5 Nami nilikuwa ulimwenguni na nikapokea ya Baba yangu, na [a]kazi zake zikadhihirika wazi.

6 Na [a]Yohana aliona na kushuhudia utimilifu wa [b]utukufu wangu, na utimilifu wa ushuhuda wa [c]Yohana utafunuliwa hapo baadaye.

7 Na alitoa ushuhuda, akisema: Niliuona utukufu wake, kwamba alikuwepo hapo [a]mwanzo, kabla ya ulimwengu kuwepo;

8 Kwa hiyo, hapo mwanzo [a]Neno alikuwepo, kwani alikuwa Neno, hata mjumbe wa wokovu—

9 [a]Nuru na [b]Mkombozi wa ulimwengu; Roho wa kweli, aliyekuja ulimwenguni, kwa sababu ulimwengu uliumbwa naye, na ndani yake mlikuwa na uzima wa wanadamu na nuru ya wanadamu.

10 Dunia [a]ziliumbwa naye; wanadamu waliumbwa naye; vitu vyote viliumbwa naye, na kwa njia yake, na kutoka kwake.

11 Na mimi, Yohana, ninashuhudia kwamba niliuona utukufu wake, kama utukufu wa Mzaliwa Pekee wa Baba, amejaa neema na kweli, hata Roho wa kweli, ambaye alikuja na akakaa katika mwili, na akakaa miongoni mwetu.

12 Na mimi Yohana, niliona kwamba hakupokea [a]utimilifu mwanzoni, bali alipokea [b]neema juu ya neema;

13 Naye hakupokea utimilifu mwanzoni, bali aliendelea kutoka [a]neema hadi neema, mpaka akapokea utimilifu;

14 Na hivyo akaitwa [a]Mwana wa Mungu, kwa sababu hakuwa amepokea utimilifu mwanzoni.

15 Na mimi, [a]Yohana, ninashuhudia, na lo, mbingu zikafunguka, na [b]Roho Mtakatifu akashuka juu yake katika umbo la [c]njiwa, na akatua juu yake, na hapo ikaja sauti kutoka mbinguni ikisema: Huyu ni [d]Mwanangu Mpendwa.

16 Na mimi, Yohana, ninashuhudia kwamba alipata utimilifu wa utukufu wa Baba;

4*a* Mos. 15:1–7.
b MWM Yesu Kristo—Mamlaka.
c Lk. 1:26–35; 2:4–14; 3 Ne. 1:12–14; Eth. 3:14–16.
5*a* Yn. 5:36; 10:25; 14:10–12.
6*a* Yn. 1:34.
b MWM Yesu Kristo—Utukufu wa Yesu Kristo.
c Yn. 20:30–31.
7*a* Yn. 1:1–3, 14; 17:5; M&M 76:39.
8*a* MWM Yehova; Yesu Kristo.
9*a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
b MWM Mkombozi.
10*a* Ebr. 1:1–3; M&M 76:24; Musa 1:31–33.
12*a* Flp. 2:6–11.
b Yn. 1:16–17.
13*a* Lk. 2:52.
14*a* Lk. 1:31–35; M&M 6:21. MWM Mungu, Uungu—Mungu Mwana.
15*a* Yn. 1:29–34.
b MWM Roho Mtakatifu.
c MWM Njiwa, Ishara ya.
d Mt. 3:16–17.

17 Na akapokea [a]uwezo [b]wote, kote mbinguni na duniani, na utukufu wa [c]Baba ulikuwa pamoja naye, kwa kuwa alikaa ndani yake.

18 Na itakuwa, kwamba kama ni waaminifu mtapokea utimilifu wa ushuhuda wa Yohana.

19 Ninayatoa kwenu ninyi maneno haya ili muweze kufahamu na kujua namna ya [a]kuabudu, na kujua nini mnachokiabudu, ili muweze kuja kwa Baba katika jina langu, na kwa wakati wake mpokee utimilifu wake.

20 Kwani ikiwa mnazishika [a]amri zangu mtaupokea [b]utimilifu wake, na [c]kutukuzwa ndani yangu, kama Mimi ndani ya Baba; kwa hiyo, ninawaambia, mtapokea [d]neema juu ya neema.

21 Na sasa, amini ninawaambia, hapo [a]mwanzo nilikuwepo kwa Baba, na Mimi ndiye [b]Mzaliwa wa Kwanza;

22 Na wale wote walio wazaliwa kupitia mimi ni [a]washiriki wa [b]utukufu huo huo, na ndiyo kanisa la Mzaliwa wa Kwanza.

23 Ninyi pia mlikuwepo mwanzoni [a]pamoja na Baba; kile ambacho ni Roho, hata Roho wa kweli;

24 Na [a]ukweli ni [b]maarifa ya mambo kama yalivyo, na kama yalivyokuwa, na kama yatakavyokuwa;

25 Na chochote kilicho [a]zaidi au pungufu ya hivi ni roho wa yule mwovu ambaye alikuwa [b]muongo kutoka mwanzo.

26 Roho wa [a]kweli huyo ndiye wa Mungu. Mimi ni Roho wa kweli, na Yohana alitoa ushuhuda juu yangu, akisema: Alipokea utimilifu wa kweli, ndiyo, hata kweli yote;

27 Na hakuna mtu apokeaye [a]utimilifu isipokuwa amezishika amri zake.

28 Yule [a]azishikaye amri zake hupokea kweli na [b]nuru, hadi ametukuzwa katika kweli na [c]kujua mambo yote.

29 Mwanadamu pia [a]mwanzoni alikuwa na Mungu. [b]Akili, au nuru ya kweli, haikuumbwa au kutengenezwa, na wala kamwe haiwezekani kuwa.

17*a* MWM Uwezo; Yesu Kristo—Mamlaka.
b Mt. 28:18; Yn. 17:2; 1 Pet. 3:22.
c MWM Mungu, Uungu—Mungu Baba.
19*a* Yn. 4:21–26; 17:3; Mdo. 17:22–25. MWM Kuabudu.
20*a* M&M 50:28.
b Yn. 1:16; M&M 84:36–39.
c Yn. 17:4–5, 22. MWM Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, uwezekano wa kuwa kama Baba wa Mbinguni.
d MWM Neema.
21*a* Yn. 1:1–2; 1 Pet. 1:19–20; Musa 4:2.
b MWM Mzaliwa wa Kwanza.
22*a* 1 Pet. 5:1; M&M 133:57.
b MWM Utukufu wa Selestia.
23*a* MWM Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, mtoto wa kiroho wa Baba wa Mbinguni.
24*a* MWM Ukweli.
b MWM Maarifa.
25*a* M&M 20:35.
b Yn. 8:44; 2 Ne. 2:18; Musa 4:4.
26*a* Yn. 14:6.
27*a* MWM Kamilifu.
28*a* MWM Mtiifu, Tii, Utii.
b M&M 50:24; 84:45. MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
c Yn. 17:3; M&M 88:49, 67.
29*a* Ibr. 3:18. MWM Maisha kabla ya kuzaliwa; Mwanadamu, Wanadamu.
b MWM Akili, Viumbe-akili-asilia.

30 Kweli yote ni huru katika mazingira yale ambayo Mungu ameiweka, ili [a]kujiamulia yenyewe, kama akili yote pia; vinginevyo hakuna maisha.

31 Tazama, hapa ndipo ilipo [a]haki ya kujiamulia ya mwanadamu, na hapa ndipo ilipo hukumu ya mwanadamu; kwa sababu kile kilichokuwepo kutoka mwanzoni kinajitokeza [b]wazi kwao, nao hawaipokei nuru.

32 Na kila mtu ambaye roho yake haiipokei [a]nuru iko chini ya hukumu.

33 Kwani mwanadamu ni [a]roho. [b]Vitu vya asili ni vya milele, na roho na vitu vya asili, ambavyo vimeungana na haviwezi kutenganishwa, hupokea shangwe kamilifu;

34 Na [a]vikitenganishwa, mwanadamu hawezi kupokea [b]shangwe kamilifu.

35 [a]Vitu vya asili ni hema takatifu ya Mungu; ndiyo, mwanadamu ni hema takatifu ya Mungu, mahekalu, hata [b]mahekalu; na lolote likichafuliwa, Mungu ataliharibu hekalu hilo.

36 [a]Utukufu wa Mungu ni [b]akili, au, kwa maneno mengine, [c]nuru na kweli.

37 Nuru na kweli humkataa yule [a]mwovu.

38 Kila roho ya mwanadamu [a]haikuwa na dhambi hapo mwanzoni; na Mungu akiwa amekwisha [b]mkomboa mwanadamu kutokana na [c]anguko, wanadamu wakaja tena, katika hali yao ya uchanga, wakiwa [d]safi mbele za Mungu.

39 Na yule mwovu huja na [a]kuziondoa nuru na kweli, kwa kutotii, kutoka kwa wanadamu, na kwa sababu ya [b]mapokeo ya baba zao.

40 Lakini nimewaamuru ninyi kuwalea [a]watoto wenu katika nuru na kweli.

41 Lakini amini ninakuambia, mtumishi wangu Frederick G. Williams, umekaa katika hatia hii;

42 [a]Hujawafundisha watoto wako nuru na kweli, kulingana na amri; na yule mwovu bado

30 *a* 2 Ne. 2:13–27.
31 *a* MWM Haki ya uamuzi.
b Kum. 30:11–14; M&M 84:23–24.
32 *a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo; Ukweli.
33 *a* M&M 77:2; Ibr. 5:7–8. MWM Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, mtoto wa kiroho wa Baba wa Mbinguni.
b M&M 131:7–8; 138:17. MWM Ufufuko.
34 *a* 2 Ne. 9:8–10.
b MWM Shangwe.
35 *a* M&M 130:22.
b 1 Kor. 3:16–17.
36 *a* MWM Utukufu; Yesu Kristo—Utukufu wa Yesu Kristo.
b M&M 130:18–19; Ibr. 3:19. MWM Akili, Viumbe-akili-asilia.
c M&M 88:6–13.
37 *a* Musa 1:12–16. MWM Ibilisi.
38 *a* MWM Asiye na Hatia, Hali ya Kutojua.
b Mos. 27:24–26; Musa 5:9; M ya I 1:3. MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
c MWM Anguko la Adamu na Hawa.
d Moro. 8:8, 12, 22; M&M 29:46–47. MWM Wokovu—Wokovu wa watoto.
39 *a* Mt. 13:18–19; 2 Kor. 4:3–4; Alma 12:9–11.
b Eze. 20:18–19; Alma 3:8. MWM Mapokeo.
40 *a* MWM Familia—Wajibu wa wazazi.
42 *a* 1 Sam. 3:11–13; M&M 68:25–31.

anazo nguvu juu yako, na hii ndiyo chanzo cha mateso yako.

43 Na sasa amri ninaitoa kwako—kama utakombolewa utaiweka [a]sawa sawa nyumba yako mwenyewe, kwani kuna mambo mengi yasiyo sawa katika nyumba yako.

44 Amini, ninakuambia wewe mtumishi wangu Sidney Rigdon, kuwa katika baadhi ya mambo hajashika amri kuhusiana na watoto wake; kwa hiyo, kwanza uirekebishe nyumba yako.

45 Amini, ninamwambia mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, au katika maneno mengine, nitawaita ninyi [a]marafiki, kwa kuwa ninyi ni marafiki zangu, na mtapata urithi pamoja nami—

46 Niliwaita, ninyi [a]watumishi kwa faida ya ulimwengu, na ninyi ni watumishi wao kwa faida yangu—

47 Na sasa, amini ninamwambia Joseph Smith, Mdogo—Hujashika amri, na inakulazimu [a]ukemewe mbele za Bwana;

48 [a]Familia yako lazima itubu na kuacha baadhi ya mambo, na kuyasikiliza kwa makini maneno yako, au, wataondoshwa kwenye nafasi yao.

49 Nisemacho kwa mmoja ninasema kwa wote; [a]ombeni daima asije yule mwovu akawa na nguvu ndani yenu, na kuwaondosha kwenye nafasi yenu.

50 Pia mtumishi wangu Newel K. Whitney, askofu wa kanisa langu, inafaa akemewe, na kuirekebisha nyumba yake, na kuona kuwa wanakuwa na bidii na wenye kujali nyumbani, na kuomba daima, au vinginevyo wataondoshwa kwenye [a]nafasi yao.

51 Sasa, ninawaambia marafiki zangu, na mtumishi wangu Sidney Rigdon aende safari yake, na afanye haraka, na pia akitangaza mwaka [a]uliokubaliwa wa Bwana, na injili ya wokovu, vile nitakavyompa kunena; na kwa sala yenu ya imani kwa nia moja nitamsaidia.

52 Na watumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na Frederick G. Williams wafanye upesi pia, nao watapewa kulingana na sala ya imani; na kadiri mtakavyoshika maneno yangu hamtashindwa katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao.

53 Na, amini ninawaambia, kwamba ni mapenzi yangu kuwa mfanye upesi [a]kutafsiri maandiko yangu, na [b]kupata [c]maarifa ya historia, na ya mataifa, na ya falme, ya sheria za Mungu na mwanadamu, na hii yote ni kwa ajili ya wokovu wa Sayuni. Amina.

43*a* 1 Tim. 3:4–5.
45*a* M&M 84:63; 88:62.
46*a* Law. 25:55; 1 Ne. 21:3–8. MWM Utumishi.
47*a* M&M 95:1–2.
MWM Rudi, Kurudiwa.
48*a* MWM Familia—Wajibu wa mtoto.
49*a* 3 Ne. 18:15–21.
50*a* M&M 64:40.
51*a* Lk. 4:19.
53*a* MWM Tafsiri ya Joseph Smith (TJS).
b M&M 88:76–80, 118.
c MWM Maarifa.

SEHEMU YA 94

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 2 Agosti 1833. Hyrum Smith, Reynolds Cahoon, na Jared Carter wanateuliwa kama kamati ya Ujenzi wa Kanisa.

1–9, Bwana anatoa amri kuhusu ujenzi wa nyumba kwa ajili ya kazi ya Urais; 10–12, Nyumba ya kupiga chapa ijengwe; 13–17, Urithi kiasi fulani watolewa.

Na tena, amini ninawaambia, [a]marafiki zangu, ninawapa amri, ya kuwa mtaanza kazi ya kuweka na kutayarisha mwanzo na msingi wa mji wa [b]kigingi cha Sayuni, hapa katika ardhi ya Kirtland, kuanzia katika nyumba yangu,

2 Na tazama, ni lazima ifanywe kulingana na [a]mpangilio ambao nimeutoa kwenu.

3 Na kiwanja cha kwanza upande wa kusini kiwekwe wakfu kwangu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya urais, kwa ajili ya kazi ya [a]urais, kwa ajili ya kupokelea mafunuo; na kwa ajili ya kazi ya huduma ya urais, katika mambo yote yahusuyo kanisa na ufalme.

4 Amini ninawaambia, kwamba itajengwa futi hamsini na tano kwa sitini na tano katika upana wake na katika urefu wake, katika ukumbi wa ndani.

5 Na patakuwapo na ukumbi wa chini na ukumbi wa juu, kulingana na mfano ambao utatolewa kwenu hapo baadaye.

6 Na iwekwe wakfu kwa Bwana kuanzia msingi wake, kulingana na mfano wa ukuhani, kulingana na utaratibu ambao utatolewa kwenu hapo baadaye.

7 Na yote itawekwa wakfu kwa Bwana kwa ajili ya kazi ya urais.

8 Na msiruhusu kitu chochote [a]kichafu kuja ndani yake; na [b]utukufu wangu utakuwa humo, na uwepo wangu utakuwa hapo.

9 Lakini kama kitakuja ndani yake kitu chochote kilicho [a]kichafu, utukufu wangu hautakuwa humo; na uwepo wangu hautakuja ndani yake.

10 Na tena, amini ninawaambia, kiwanja cha pili upande wa kusini kitawekwa wakfu kwangu mimi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba yangu, kwa ajili ya kazi ya [a]kupiga chapa ya [b]tafsiri ya maandiko yangu, na mambo yote nitakayo waamuru ninyi.

11 Nayo itakuwa futi hamsini na tano kwa sitini na tano katika upana wake na urefu wake, katika ukumbi wa ndani; na patakuwa na ukumbi wa chini na wa juu.

12 Na nyumba hii yote itawe-

94 1*a* M&M 93:45.
b MWM Kigingi.
2*a* M&M 52:14–15.
3*a* M&M 107:9, 22.
8*a* Lk. 19:45–46; M&M 109:16–20.
b 1 Fal. 8:10–11. MWM Utukufu.
9*a* M&M 97:15–17.
10*a* M&M 104:58–59.
b MWM Tafsiri ya Joseph Smith (TJS).

kwa wakfu kwa Bwana kutoka msingi wake, kwa ajili ya kazi ya upigaji chapa, katika mambo yote yale nitakayowaamuru, iwe takatifu, isiyochafuliwa, kulingana na mfano wake katika mambo yote, kama itakavyotolewa kwenu.

13 Na juu ya kiwanja cha tatu mtumishi wangu Hyrum Smith atapokea urithi wake.

14 Na juu ya kiwanja cha kwanza na cha pili upande wa kaskazini mtumishi wangu Reynolds Cahoon na Jared Carter watapata urithi wao—

15 Ili waweze kufanya kazi nilizowapangia, kuwa kamati ya kujenga nyumba zangu, kulingana na amri, ambazo Mimi, Bwana Mungu, nimezitoa kwenu.

16 Nyumba hizi mbili zisijengwe hadi nitakapowapa amri juu yake.

17 Na sasa sitatoa zaidi kwenu kwa wakati huu. Amina.

SEHEMU YA 95

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 1 Juni 1833. Ufunuo huu ni mfululizo wa maelekezo matakatifu ya kujenga nyumba kwa ajili ya kuabudu na mafundisho nyumba ya Bwana (ona sehemu ya 88:119–136).

1–6, Watakatifu wanakemewa kwa kushindwa kwao kujenga nyumba ya Bwana; 7–10, Bwana anataka kuitumia nyumba Yake kwa kuwapa endaomenti watu Wake kwa uwezo utokao juu; 11–17, Nyumba hiyo iwekwe wakfu kama mahali pa kuabudu na kwa ajili ya shule ya Mitume.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu ninyi ambao ninawapenda, na wale niwapendao pia [a]huwarudi ili dhambi zao ziweze [b]kusamehewa, kwani pamoja na kuwarudi ninawatayarishia njia kwa ajili ya [c]ukombozi wao katika mambo yote yatokanayo na [d]majaribu, na nimewapenda ninyi—

2 Kwa hiyo, ninyi yafaa kuwarudi na kukemewa mbele ya uso wangu;

3 Kwani ninyi mmenitendea dhambi kubwa, kwa sababu hamkuipa umuhimu amri ile iliyo kuu katika mambo yote, ambayo nimeitoa kwenu juu ya ujenzi wa [a]nyumba yangu;

4 Kwa ajili ya matayarisho ambayo ninapanga kuwatayarisha mitume wangu kwa ajili

95 1*a* Kum. 11:1–8; Mit. 13:18; Ebr. 12:5–11; Hel. 15:3; M&M 101:4–5; 105:6.
MWM Rudi, Kurudiwa.
b MWM Samehe.
c 1 Kor. 10:13.
d MWM Jaribu, Majaribu.
3*a* Hag. 1:7–11; M&M 88:119. MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.

ya [a]kupogoa shamba langu la mizabibu kwa mara ya mwisho, ili nipate kulitimiza tendo langu la [b]ajabu, ili niweze [c]kumwaga Roho yangu juu ya watu wote—

5 Lakini tazama, amini ninawaambia, kwamba wako wengi waliotawazwa miongoni mwenu, ambao nimewaita lakini ni wachache kati yao [a]walioteuliwa.

6 Wale ambao hawajateuliwa wametenda dhambi mbaya sana, kwa sababu wanatembea [a]gizani saa sita mchana.

7 Na kwa sababu hii niliwapa ninyi amri ya kwamba yawapasa kuitisha [a]kusanyiko lenu la kiroho, ili [b]kufunga kwenu na kuomboleza kwenu kuweze kupaa juu masikioni mwa Bwana wa [c]Sabato, ambaye kwa tafsiri, ni [d]muumba wa siku ya kwanza, mwanzo na mwisho.

8 Ndiyo, amini ninawaambia, niliwapa amri ya kwamba mjenge nyumba, ambamo ndani ya nyumba hiyo ninapanga kuwapa [a]endaomenti wale ambao nimewateua kwa uwezo utokao juu;

9 Kwani hii ndiyo [a]ahadi ya Baba kwenu ninyi; kwa hiyo ninawaamuru ninyi kaeni humu, hata kama wale mitume wangu wa Yerusalemu.

10 Hata hivyo, watumishi wangu walitenda dhambi kubwa sana; na [a]ushindani ulianza katika [b]shule ya manabii; ambao yalikuwa ya kuhuzunisha kwangu, asema Bwana; kwa sababu hiyo, niliwatoa ili kuwarudi.

11 Amini ninawaambia, ni mapenzi yangu kuwa mjenge nyumba. Kama mtazishika amri zangu mtapata uwezo wa kuijenga.

12 Kama [a]hamtazishika amri zangu, [b]upendo wa Baba hautakuwamo ndani yenu, kwa hiyo mtatembea gizani.

13 Sasa hapa ndipo ilipo hekima, na mapenzi ya Bwana—nyumba na ijengwe, siyo kwa jinsi ya ulimwengu, kwani siwaruhusu ninyi kuishi kwa jinsi ya ulimwengu;

14 Kwa hiyo, na ijengwe kwa jinsi ambayo nitaionyesha kwa watatu kati yenu, ambao mtawachagua na kuwaweka katika mamlaka haya.

15 Na ukubwa wake utakuwa futi hamsini na tano katika upana, na iwe futi sitini na tano katika urefu, katika ukumbi wake wa ndani.

16 Na sehemu ya chini ya ukumbi wa ndani uwekwe wakfu kwangu kwa ajili ya sakramenti na matoleo, na kwa ajili ya

4 *a* Yak. (KM) 5:61–75; M&M 24:19; 33:3–4. MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
b Isa. 28:21; M&M 101:95.
c Mit. 1:23; Yoe. 2:28; M&M 19:38. MWM Roho Mtakatifu; Vipawa vya Roho.

5 *a* Mt. 20:16; M&M 105:35–37; 121:34–40. MWM Uteuzi.

6 *a* MWM Giza, Kiroho.

7 *a* M&M 88:70, 74–82, 117–120.
b MWM Funga, Kufunga.
c MWM Yehova.
d MWM Umba, Uumbaji.

8 *a* M&M 38:32; 39:15; 43:16; 110:9–10. MWM Endaomenti.

9 *a* Lk. 24:49.

10 *a* MWM Ushindani.
b MWM Shule ya Manabii.

12 *a* Yn. 15:10.
b 1 Yoh. 2:10, 15.

kuhubiri kwenu, na kufunga kwenu, na kuomba kwenu, na kwa [a]kunitolea matakwa yenu yaliyo matakatifu sana, asema Bwana wenu.

17 Na sehemu ya juu ya ukumbi wa ndani iwekwe wakfu kwangu kwa ajili ya shule ya mitume wangu, asema Mwana [a]Amani; au, kwa maneno mengine, Alfa, au, kwa maneno mengine, Omega; hata Yesu Kristo [b]Bwana wenu. Amina.

SEHEMU YA 96

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, ukionyesha mpangilio wa mji au kigingi cha Sayuni huko Kirtland, Ohio, 4 Juni 1833, kama mfano kwa Watakatifu hapo Kirtland. Tukio lilikuwa ni la mkutano wa makuhani wakuu, na ajenda kubwa ya kujadili ilikuwa ni ugawaji wa ardhi fulani, iliyojulikana kama shamba la French, lililokuwa likimilikiwa na Kanisa karibu na Kirtland. Kwa vile mkutano haukuweza kuafikiana nani alisimamie shamba hilo, wote walikubaliana kumwomba Bwana juu ya jambo hilo.

1, Kigingi cha Sayuni cha Kirtland kiimarishwe; 2–5, Askofu atagawa urithi huo kwa ajili ya Watakatifu; 6–9, John Johnson atakuwa mshiriki wa mpango wa ushirika.

Tazama, ninawaambia, hapa ndipo ilipo hekima, ambayo mtaweza kujua jinsi ya kutenda jambo hili, kwani ni muhimu kwangu kwamba [a]kigingi hiki ambacho nimekiweka kuwa nguvu ya Sayuni chapaswa kuimarishwa.

2 Kwa hiyo, acha mtumishi wangu Newel K. Whitney asimamie mkuu wa mahali hapo palipotajwa miongoni mwenu, ambapo juu yake ninapanga kujenga nyumba yangu takatifu.

3 Na tena, pagawanywe katika viwanja, kulingana na hekima, kwa faida ya wale watafutao urithi, kama itakavyoamriwa katika baraza miongoni mwenu.

4 Kwa hiyo, hakikisheni mnalitazama jambo hili, na sehemu ile iliyo muhimu kwa manufaa ya [a]ushirika wangu, kwa madhumuni ya kulileta neno langu kwa wanadamu.

5 Kwani tazama, amini ninawaambia, hili ni muhimu sana kwangu, kwamba neno langu lapaswa kuenea kwa wanadamu, kwa madhumuni ya kuilainisha mioyo ya wanadamu kwa faida yenu. Hivyo ndivyo. Amina.

6 Na tena, amini ninawaambia,

16*a* M&M 59:9–14.
17*a* M&M 78:20.
b MWM Bwana.

96 1*a* Isa. 33:20; 54:2.
MWM Kigingi.
4*a* M&M 78:3–4.
MWM Mpango wa Ushirika.

ni hekima na ni muhimu kwangu, kwamba mtumishi wangu John Johnson ambaye matoleo yake nimeyakubali, na ambaye sala zake nimezisikia, ambaye kwake ninatoa ahadi ya uzima wa milele ilimradi kama atazishika amri zangu tokea sasa—

7 Kwani yeye ni mzaliwa wa ukoo wa [a]Yusufu na mshirika wa baraka za ahadi zilizofanywa kwa baba zake—

8 Amini ninawaambia, ni muhimu kwangu kwamba awe mshiriki wa mpango wa ushirika, ili aweze kusaidia katika kulileta neno langu kwa wanadamu.

9 Kwa hiyo mtamtawaza katika baraka hii, naye lazima atafute kwa bidii yote kuyaondoa madeni yaliyopo juu ya nyumba iliyotajwa miongoni mwenu, ili aweze kuishi humo. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 97

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 2 Agosti 1833. Ufunuo huu unashughulika hususani na mambo ya Watakatifu katika Sayuni, Wilaya ya Jackson, Missouri, katika jibu la maombi ya Nabii kwa Bwana juu ya taarifa. Waumini wa Kanisa huko Missouri kwa wakati huu walikuwa chini ya mateso makali na, mnamo tarehe 23 Julai 1833, walikuwa wamelazimishwa kuweka saini makubaliano ya kuhama Wilaya ya Jackson.

1–2, Watakatifu wengi katika Sayuni (Wilaya ya Jackson, Missouri) wanabarikiwa kwa ajili ya uaminifu wao; 3–5, Parley P. Pratt anapongezwa kwa kazi yake ya shule katika Sayuni; 6–9, Wale wanaotunza maagano yao wanakubaliwa na Bwana; 10–17, Nyumba na ijengwe katika Sayuni ambamo ndani yake wale walio safi moyoni watamwona Mungu; 18–21, Sayuni ni walio safi moyoni; 22–28, Sayuni ataepuka adhabu ya Bwana kama atakuwa mwaminifu.

Amini ninawaambia marafiki zangu, ninasema nanyi kwa sauti yangu, hata sauti ya Roho yangu, ili niweze kuonyesha kwenu mapenzi yangu juu ya ndugu zenu katika nchi ya [a]Sayuni, wengi wao ni wanyenyekevu wa kweli na wanatafuta kwa bidii kujifunza hekima na kupata ukweli.

2 Amini, amini ninawaambia, heri hao, kwani watapata; kwa kuwa Mimi, Bwana, huonyesha huruma kwa wote walio [a]wapole, na juu ya wale wote nitakao, ili niweze kuhukumu kwa haki wakati niwaletapo wao kwenye hukumu.

7 *a* MWM Yusufu, Mwana wa Yakobo.

97 1 *a* MWM Sayuni.
2 *a* Mt. 5:5; Mos. 3:19.

3 Tazama, ninawaambia, juu ya shule katika Sayuni, Mimi, Bwana, ninapendezwa kuwa pawepo [a]shule katika Sayuni, na pia pamoja na mtumishi wangu [b]Parley P. Pratt, kwa kuwa yeye hukaa ndani yangu.

4 Na kadiri yeye atakavyoendelea kukaa ndani yangu ataendelea kuisimamia shule katika nchi ya Sayuni hadi nitakapotoa kwake amri nyingine.

5 Nami nitambariki yeye kwa baraka nyingi zaidi, katika kuyaeleza maandiko na siri zote kwa kuijenga shule, na kanisa katika Sayuni.

6 Na kwa mabaki ya shule, Mimi, Bwana, niko radhi kuonyesha huruma; hata hivyo, kuna wale ambao ni lazima [a]kuwarudi, na matendo yao yatafanywa yajulikane.

7 Na [a]shoka limekwisha kuwekwa penye mashina ya miti; basi kila mti usiozaa [b]matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni. Mimi, Bwana, nimesema.

8 Amini ninawaambia, wote miongoni mwao wale ambao wanajua kuwa [a]mioyo yao ni ya [b]uaminifu, na imevunjika, na roho zao zimepondeka, na wako [c]radhi kuyatunza maagano yao kwa [d]dhabihu—ndiyo, kila dhabihu ambayo Mimi, Bwana, nitaamuru—[e]wanakubaliwa kwangu.

9 Kwani, Mimi, Bwana, nitawafanya wazae kama mti uzaao matunda ambao umepandwa katika ardhi nzuri, kando kando ya vijito vya maji, uzaao matunda yaliyo mazuri sana.

10 Amini ninawaambia, kwamba ni mapenzi yangu kuwa [a]nyumba ijengwe kwa ajili yangu katika nchi ya Sayuni, kulingana na [b]vipimo ambavyo nimewapa.

11 Ndiyo, na ijengwe haraka, kwa zaka ya watu wangu.

12 Tazama, hii ndiyo [a]zaka na dhabihu ambayo Mimi, Bwana, nayataka kutoka kwao, ili paweze kujengwa [b]nyumba kwa ajili ya wokovu wa Sayuni—

13 Mahali pa [a]shukrani kwa watakatifu wote, na mahali pa mafundisho kwa wale wote walioitwa kufanya kazi ya huduma katika miito na ofisi zao zote mbalimbali;

14 Ili waweze kukamilishwa katika [a]ufahamu wa huduma zao, katika nadharia, katika kanuni, na katika mafundisho, katika mambo yote yahusuyo [b]ufalme wa Mungu juu ya dunia, ufalme ambao [c]funguo zake zimewekwa juu yenu.

3a MWM Shule ya Manabii.
b MWM Pratt, Parley Parker.
6a MWM Rudi, Kurudiwa.
7a Mt. 3:10.
b Lk. 6:43–45; Alma 5:36, 52; 3 Ne. 14:15–20.
8a MWM Moyo Uliovunjika.
b MWM Mwaminifu, Uaminifu.
c M&M 64:34.
d MWM Dhabihu.
e M&M 52:15; 132:50.
10a M&M 57:3; 88:119; 124:51.
b M&M 115:14–16.
12a MWM Lipa zaka, Zaka.
b MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.
13a MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
14a MWM Ufahamu.
b MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
c MWM Funguo za Ukuhani.

15 Na ilimradi watu wangu wakinijengea nyumba katika jina la Bwana, na ikiwa hawataruhusu kitu chochote [a]kichafu kuingia ndani yake, ili isichafuliwe, [b]utukufu wangu utatulia juu yake;

16 Ndiyo, na [a]uwepo wangu utakuwa ndani yake, kwa kuwa nitakuja ndani yake, na wote walio [b]safi moyoni ambao watakuja ndani yake watamwona Mungu.

17 Lakini kama itachafuliwa sitakuja ndani yake, na utukufu wangu hautakuwa humo; kwa kuwa sitakuja ndani ya mahekalu yasiyo matakatifu.

18 Na, sasa, tazama, kama Sayuni itafanya mambo haya [a]itastawi, na kujipanua na kuwa tukufu sana, kuu sana, na ya kutisha sana.

19 Na [a]mataifa ya dunia yatamheshimu, na yatasema: Hakika [b]Sayuni ni mji wa Mungu wetu, na hakika Sayuni haiwezi kuanguka, wala kuondolewa katika mahali pake, kwa kuwa Mungu yuko pale na mkono wa Bwana uko pale;

20 Na ameapa kwa uwezo wa nguvu zake kuwa wokovu wake na [a]mnara wake mrefu.

21 Kwa hiyo, amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, Sayuni na ifurahi, kwani hii ndiyo [a]Sayuni—WALIO SAFI MOYONI; kwa hiyo, Sayuni na ifurahi, wakati waovu wote wataomboleza.

22 Kwani tazama, na lo, [a]kisasi chaja upesi juu ya wasiomcha Mungu kama kimbunga; na ni nani atakayekiepuka?

23 [a]Adhabu ya Bwana itapita usiku na mchana, na habari yake itawaudhi watu wote; ndiyo, haitazuiliwa hadi ajapo Bwana;

24 Kwani uchungu wa Bwana unawaka dhidi ya machukizo yao na matendo yao yote ya uovu.

25 Hata hivyo, Sayuni [a]ataepuka kama atajitahidi kutenda mambo yote niliyomwamuru yeye.

26 Lakini kama hatajitahidi kufanya chochote nilichomwamuru, [a]nitamtembelea yeye kulingana na matendo yake, kwa mateso makali, kwa [b]tauni, kwa baa, kwa upanga, kwa [c]kisasi, kwa [d]moto uangamizao.

27 Hata hivyo, na isomwe mara hii ya kwanza masikioni mwake, kwamba Mimi, Bwana, nimeyakubali matoleo yake; na kama hatatenda dhambi tena [a]hakuna jambo lolote katika haya litakalo mpata;

28 Na [a]nitambariki kwa bara-

15a M&M 94:9; 109:20–21.
b Hag. 2:7; M&M 84:5.
16a M&M 110:1–10.
b Mt. 5:8; M&M 67:10–13; 88:68. MWM Safi na Isiyo safi.
18a M&M 90:24; 100:15.
19a Isa. 60:14; Zek. 2:10–12; M&M 45:66–70; 49:10.
b MWM Yerusalemu Mpya.
20a 2 Sam. 22:3.
21a Musa 7:18. MWM Safi na Isiyo safi; Sayuni.
22a MWM Kisasi.
23a Isa. 28:14–19; M&M 45:31.
25a 2 Ne. 6:13–18; M&M 63:34; JS—M 1:20.
26a M&M 84:54–59.
b Lk. 21:10–13.
c Mal. 4:1–3; 3 Ne. 21:20–21.
d Yoe. 1:15–20.
27a Eze. 18:27.
28a MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.

ka, na kuongeza wingi wa baraka juu yake, na juu ya vizazi vyake milele na milele, asema Bwana Mungu wenu. Amina.

SEHEMU YA 98

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 6 Agosti 1833. Ufunuo huu ulikuja kufuatia mateso waliyoyapata Watakatifu katika Missouri. Kuongezeka kwa makazi ya waumini wa Kanisa huko Missouri kuliwasumbua baadhi ya wahamiaji wengine, ambao walihisi ni kutishika kwa idadi ya Watakatifu, kwa nguvu ya kisiasa na kiuchumi, na kwa tofauti za kiutamaduni na kidini. Mnamo Julai 1833, kikundi cha wahuni kiliharibu mali za Kanisa, na kuwapaka lami na kuwabandika manyoya waumini wawili wa Kanisa, na kudai kwamba Watakatifu waondoke Wilaya ya Jackson. Ingawa taarifa fulani ya matatizo katika Missouri bila shaka zilikuwa zimemfikia Nabii huko Kirtland (umbali wa maili mia tisa), uzito wa hali hiyo ungeliweza kujulikana tu kwake kwa wakati huu kwa njia ya ufunuo.

1–3, Mateso ya Watakatifu yatakuwa ni kwa faida yao; 4–8, Watakatifu wajenge urafiki na sheria ya kikatiba ya nchi; 9–10, Waaminifu, wenye hekima, na watu wema yapaswa kuungwa mkono katika serikali ya nchi; 11–15, Wale wautoao uhai wao katika kazi ya Bwana watapata uzima wa milele; 16–18, Ikataeni vita na tangazeni amani; 19–22, Watakatifu katika Kirtland wanakemewa na kuamriwa kutubu; 23–32, Bwana anafunua sheria Zake zinazotawala usumbufu na mateso yaliyowekwa juu ya watu Wake; 33–38, Vita inakubalika tu ikiwa Bwana ameamuru; 39–48, Watakatifu watasamehe maadui zao, ambao, kama wakitubu, pia wataepuka kisasi cha Bwana.

Amini ninawaambia marafiki zangu, [a]msiogope, mioyo yenu na ifarijike; ndiyo, furahini siku zote, na toeni [b]shukrani katika kila kitu;

2 [a]Mkimngoja Bwana kwa subira, kwani sala zenu zimeingia masikioni mwa Bwana wa Sabato, na zimeandikwa kwa muhuri na ushuhuda huu—Bwana ameapa na kutangaza kuwa atatoa.

3 Kwa hiyo, yeye hutoa ahadi hii kwenu, kwa ahadi isiyobadilika kwamba zitatimizwa; na mambo yote ambayo kwayo [a]mmeteswa yatafanya kazi kwa pamoja kwa faida yenu, na kwa utukufu wa jina langu, asema Bwana.

4 Na sasa, amini ninawaambia

98 1*a* M&M 68:6.
b MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
2*a* Zab. 27:14; Isa. 30:18–19; M&M 133:45.
3*a* M&M 122:7. MWM Shida.

juu ya sheria za nchi, ni mapenzi yangu kuwa watu wangu wakumbuke kufanya mambo yote ninayowaamuru wao.

5 Na [a]sheria hii ya nchi ambayo ni ya [b]kikatiba, inasaidia ile kanuni kwa kulinda haki na heshima, kwa ajili ya watu wote, na inakubalika mbele zangu.

6 Kwa hiyo, Mimi, Bwana, ninawakubali ninyi, na ndugu zenu wa kanisa langu, kwa kuikubali ile sheria ambayo ni sheria ya nchi kikatiba;

7 Na kuhusiana na sheria ya binadamu, chochote kilicho zaidi au pungufu ya hii, hutoka kwa yule mwovu.

8 Mimi, Bwana Mungu, nawafanya muwe [a]huru, kwa hiyo hakika ninyi ni huru; na sheria pia huwafanya ninyi kuwa huru.

9 Hata hivyo, wakati [a]mwovu atawalapo watu huomboleza.

10 Kwa hiyo, watu [a]waaminifu na wenye hekima yapaswa watafutwe kwa bidii, na watu wema na wenye hekima ni lazima mzingatie kuwaunga mkono; vinginevyo chochote kilicho pungufu ya haya chatoka kwa yule mwovu.

11 Na ninawapa ninyi kwenu amri, ya kuwa muache uovu wote na mshikilie wema wote, ili mpate kuishi kwa kila [a]neno litokalo kinywani mwa Mungu.

12 Kwani yeye [a]atampa aliye mwaminifu amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni; nami [b]nitawajaribu na kuwapima kwa njia hii.

13 Na yeyote [a]autoaye uhai wake katika kazi yangu, kwa ajili ya jina langu, atauona tena, hata uzima wa milele.

14 Kwa hiyo, [a]msiwaogope adui zenu, kwani nimeazimia moyoni mwangu, asema Bwana, kwamba [b]nitawajaribu ninyi katika mambo yote, ikiwa mtakaa katika agano langu, hata mpaka [c]kifo, ili muweze kuwa wenye kustahili.

15 Kwani kama hamtakaa katika agano langu hamnistahili.

16 Kwa hiyo, [a]ikataeni [b]vita na tangazeni [c]amani, na tafuteni kwa bidii [d]kuigeuza mioyo ya watoto kuwaelekea baba zao, na mioyo ya baba iwaelekee watoto wao;

17 Na tena, mioyo ya [a]Wayahudi kwa manabii, na manabii kwa Wayahudi; ili nisije nikaipiga dunia kwa laana, na wenye mwili wote wakateketea mbele zangu.

18 Msifadhaike mioyoni mwenu; kwani nyumbani mwa Baba

5a 1 Pet. 2:13–14; M&M 58:21; 134:5.
b M&M 101:77–80; 109:54.
MWM Huru, Uhuru; Katiba.
8a Yn. 8:32; 2 Kor. 3:17.
MWM Haki ya uamuzi; Huru, Uhuru.
9a Mit. 29:2.
10a MWM Mwaminifu, Uaminifu.
11a Kum. 8:3; Mt. 4:4; M&M 84:43–44.
12a Isa. 28:10; M&M 42:61.
b Ibr. 3:25–26.
13a Lk. 9:24; M&M 101:35–38; 103:27–28.
MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.
14a Neh. 4:14; M&M 122:9.
b M&M 124:55.
c Ufu. 2:10; M&M 136:31, 39.
16a Alma 48:14.
MWM Msuluhishi.
b MWM Vita.
c MWM Amani.
d Mal. 4:5–6; M&M 2:1–2.
17a MWM Wayahudi.

yangu mna [a]makao mengi, na nimeandaa mahali kwa ajili yenu: na mahali alipo Baba na Mimi, hapo ndipo mtakuwepo pia.

19 Tazama, Mimi, Bwana, sijapendezwa na wengi walioko katika kanisa huko Kirtland;

20 Kwa kuwa hawajaacha dhambi zao, na njia zao za uovu, kiburi cha mioyo yao, na tamaa zao, na mambo yao yote ya machukizo, na kuyashika maneno ya hekima na ya uzima wa milele ambayo nimewapa.

21 Amini ninawaambia, kwamba Mimi, Bwana, [a]nitawarudi na nitawafanya lolote nitakalo, kama hawatatubu na kuyashika mambo yote niliyowaambia.

22 Na tena ninawaambia, kama mtayashika na [a]kufanya yale yote ninayowaamuru, Mimi, Bwana, nitageuza ghadhabu na uchungu wangu kwenu, na [b]milango ya jehanamu haitawashinda.

23 Sasa, ninasema nanyi kuhusu familia zenu—kama watu [a]watawapiga ninyi, au familia zenu, mara moja, nanyi mkavumilia na msitukane dhidi yao, wala msitake kulipa kisasi, ninyi mtapata thawabu;

24 Lakini kama hamkuvumilia, [a]itahesabiwa kwenu kuwa ndicho kipimo cha haki.

25 Na tena, ikiwa adui yenu atawapiga kwa mara ya pili, na hamumtukani adui yenu, na kuvumilia kwa upole, thawabu yenu itakuwa mara-mia.

26 Na tena, ikiwa adui yenu atawapiga kwa mara ya tatu, nanyi mkavumilia kwa [a]upole, thawabu yenu itaongezeka mara-nne;

27 Na shuhuda hizi tatu zitasimama dhidi ya adui yenu kama hatatubu, na hazitafutwa.

28 Na sasa, amini ninawaambia, kama adui yule ataepuka kisasi changu, ili asiweze kuletwa katika hukumu mbele zangu, ndipo ninyi mtaangalia kwamba [a]mnamwonya huyo katika jina langu, ili asije tena juu yenu, wala juu ya familia yenu, hata watoto wa watoto wenu hadi kizazi cha tatu na cha nne.

29 Na halafu, kama atakuja juu yenu au watoto wenu, au watoto wa watoto wenu hadi wa kizazi cha tatu na cha nne, nimemtoa huyo adui yenu mikononi mwenu;

30 Na halafu kama wewe wataka kumwachia, utapewa thawabu kwa ajili ya uadilifu wako; na pia watoto wako na watoto wa watoto wako hata kizazi cha tatu na cha nne.

31 Hata hivyo, adui yako yu mikononi mwako; na kama wewe utamlipa kulingana na matendo yake utahesabiwa haki; kama amekuwa akitafuta uhai wako, naye anahatarisha maisha yako, adui yako huyo

18 *a* Yn. 14:2; M&M 59:2; 76:111; 81:6.
21 *a* Mos. 23:21; Hel. 12:3. MWM Rudi, Kurudiwa.
22 *a* MWM Mtiifu, Tii, Utii.
b Mt. 16:17–18; M&M 33:12–13.
23 *a* Lk. 6:29; Alma 43:46–47. MWM Mateso, Tesa.
24 *a* Mt. 7:1–2.
26 *a* MWM Subira.
28 *a* MWM Onya, Onyo.

yu mikononi mwako nawe utahesabiwa haki.

32 Tazama, hii ndiyo sheria niliyoitoa kwa mtumishi wangu Nefi, na [a]baba zenu, Yusufu, na Yakobo, na Isaka, na Ibrahimu, na manabii na mitume wangu wote wa kale.

33 Na tena, hii ndiyo [a]sheria ambayo niliwapa watu wangu wa kale, kwamba wasiingie katika mapambano dhidi ya taifa lolote, kabila, lugha, au watu, isipokuwa Mimi, Bwana, nimewaamuru.

34 Na kama taifa lolote, ndimi au watu watatangaza vita dhidi yao, kwanza yawapasa kuinyanyua bendera ya [a]amani kwa watu hao, taifa, au ndimi;

35 Na kama watu hao hawatakubali toleo la amani, au la pili wala la mara ya tatu, walete shuhuda hizi mbele za Bwana;

36 Ndipo Mimi, Bwana, nitawapa amri, na kuwahesabia wao haki katika kwenda vitani dhidi ya taifa, ndimi, au watu.

37 Na Mimi, Bwana, [a]nitapigana vita vyao, na vita vya watoto wao, na watoto wa watoto wao, hadi wamelipa kisasi juu ya adui zao wote, kwenye kizazi cha tatu na cha nne;

38 Tazama, huu ni utaratibu kwa watu wote, asema Bwana Mungu wenu, ili kuhesabiwa haki mbele zangu.

39 Na tena, amini ninawaambia, ikiwa baada ya adui yenu kuja juu yenu mara ya kwanza, akatubu na kuja kwenu kuwaomba msamaha, nanyi mtamsamehe, na msitumie tena ushuhuda dhidi ya adui yenu—

40 Na kuendelea mara ya pili na ya tatu; na kila wakati adui yenu akitubu makosa ambayo amewakosea, ninyi [a]msameheni, hata sabini mara saba.

41 Na kama akikukosea na hakutubu mara ya kwanza, hata hivyo wewe utamsamehe.

42 Na kama atakukosea tena mara ya pili, na hakutubu, hata hivyo wewe utamsamehe.

43 Na akikukosea tena mara ya tatu, na hakutubu, wewe umsamehe pia.

44 Lakini akikukosea tena mara ya nne wewe usimsamehe, bali utazileta shuhuda hizi mbele ya Bwana; na hazitafutwa hadi atakapotubu na kukulipa wewe mara nne katika mambo yote ambayo amekosa dhidi yako.

45 Na kama atafanya hivi, wewe utamsamehe kwa moyo wako wote; na kama hakufanya hivi, Mimi, Bwana, [a]nitalipa kisasi kwa adui yako mara mia zaidi;

46 Na juu ya watoto wake, na juu ya watoto wa watoto wake wote wanaonichukia, hadi kizazi cha [a]tatu na cha nne.

47 Lakini ikiwa watoto watatubu, au watoto wa watoto

32*a* M&M 27:10.
33*a* Kum. 20:10; Alma 48:14–16.
34*a* M&M 105:38–41.
37*a* Yos. 23:10; Isa. 49:25.
40*a* Mt. 18:21–22; M&M 64:9–11.
MWM Samehe.
45*a* Morm. 8:20.
46*a* Kum. 5:9–10.

wake, na [a]kumgeukia Bwana Mungu wao, kwa moyo wao wote na kwa uwezo, akili, na nguvu zao zote, na kurejesha mara-nne makosa yao yote waliyokukosea, au ambayo baba zao wamekukosea, au baba za baba zao, ndipo uchungu wa hasira yako utakoma;

48 Na [a]kisasi hakitakuja tena juu yao, asema Bwana Mungu wako, na makosa yao hayataletwa tena kama ushuhuda dhidi yao mbele ya Bwana. Amina.

SEHEMU YA 99

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa John Murdock, 29 Agosti 1832, huko Hiram, Ohio. Kwa zaidi ya mwaka mmoja, John Murdock amekuwa akihubiri injili wakati watoto wake—wasio na mama baada ya kifo cha mke wake, Julia Clapp, Aprili 1831—wakikaa na familia nyingine huko Ohio.

1–8, John Murdock anaitwa kutangaza injili, na wale wanaompokea, wanampokea Bwana na watapata rehema.

Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwa mtumishi wangu John Murdock—wewe umeitwa kwenda katika nchi za mashariki kutoka nyumba hadi nyumba, kutoka kijiji hadi kijiji, na kutoka mji hadi mji, kutangaza injili yangu isiyo na mwisho kwa wakazi wake, katikati ya [a]mateso na uovu.

2 Na yule [a]akupokeaye wewe anipokea Mimi; nawe utapata nguvu za kulitangaza neno langu kwa [b]dalili za Roho wangu Mtakatifu.

3 Na yule akupokeaye wewe [a]kama mtoto mdogo, huupokea [b]ufalme wangu; na heri yao, kwa maana watapata [c]rehema.

4 Na yeyote akukataaye wewe [a]atakataliwa na Baba yangu na nyumba yake; nawe utayakung'uta mavumbi ya [b]miguu yako katika mahali pa siri kando ya njia kwa ushuhuda dhidi yao.

5 Na tazama, na lo, [a]naja haraka kwa [b]hukumu, na kuwadhibitishia wote matendo yasiyo ya ucha Mungu juu ya matendo ambayo wametenda dhidi yangu, kama ilivyoandikwa katika gombo la chuo.

6 Na sasa, amini ninakuambia, kuwa haifai kwamba uende sasa hadi watoto wako wapate mahitaji yao, na kuwapeleka kwa askofu wa Sayuni.

7 Na baada ya miaka michache,

47 *a* Mos. 7:33; Morm. 9:6.
48 *a* Eze. 18:19–23.
99 1 *a* MWM Mateso, Tesa.
2 *a* Mt. 10:40.
b 1 Kor. 2:4–5.
3 *a* Mt. 18:1–6.
b MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
c MWM Rehema, enye Rehema.
4 *a* Yn. 12:44–50.
b M&M 75:19–22.
5 *a* M&M 1:11–14.
b Yuda 1:14–15. MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.

kama utanitamani, utaweza pia kwenda katika nchi iliyo nzuri, ili kumiliki urithi wako;

8 Vinginevyo wewe utaendelea kutangaza injili yangu [a]hadi utakapochukuliwa. Amina.

SEHEMU YA 100

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii na Sidney Rigdon, huko Perrysburg, New York, tarehe 12 Oktoba 1833. Ndugu hawa wawili, wakiwa mbali na familia zao kwa siku kadhaa, walipatwa na wasi wasi juu yao.

1–4, Joseph na Sidney watahubiri injili kwa ajili ya wokovu wa wanadamu; 5–8, Watapewa saa ile watakayosema; 9–12, Sidney atakuwa msemaji na Joseph atakuwa mfunuzi na mwenye nguvu katika ushuhuda; 13–17, Bwana atawainua watu safi, na watiifu wataokolewa.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu, marafiki zangu [a]Sidney na [b]Joseph, familia zenu ni njema; wako mikononi mwangu, na nitawafanyia nionavyo kuwa ni vyema; kwani ndani yangu kuna uwezo wote.

2 Kwa hiyo, nifuateni, na sikilizeni ushauri nitakaowapa.

3 Tazama, na lo, ninao watu wengi katika eneo hili, katika maeneo ya jirani; na mlango wenye kuleta matokeo yanayotakiwa wakufaa utafunguliwa katika maeneo ya jirani katika nchi za mashariki.

4 Kwa hiyo, Mimi, Bwana, nimewaruhusu ninyi kuja mahali hapa; hivyo niliona ni muhimu kwa [a]wokovu wa wanadamu.

5 Kwa hiyo, amini ninawaambia, pazeni sauti zenu kwa watu hawa; [a]yasemeni mawazo nitakayoyaweka mioyoni mwenu, na ninyi hamtashindwa mbele za watu;

6 Kwani [a]mtapewa katika saa ile ile, ndiyo, katika wakati ule ule, kile mtakachosema.

7 Lakini amri ninaitoa kwenu, kwamba mtakitangaza kitu chochote [a]mtakachotangaza kwa jina langu, kwa taadhima moyoni, kwa roho ya [b]unyenyekevu, katika mambo yote.

8 Na ninatoa ahadi hii kwenu, ya kuwa ilimradi mtayatenda haya [a]Roho Mtakatifu atamwagwa katika kutoa ushuhuda kwa mambo yote mtakayosema ninyi.

9 Na ni muhimu kwangu kwamba wewe, mtumishi wangu Sidney, uwe [a]msemaji kwa watu hawa; ndiyo, amini, nitakutawaza kwa wito huu, hata

8*a* Mt. 19:29.

100 1*a* MWM Rigdon, Sidney.
b MWM Smith, Joseph, Mdogo.
4*a* MWM Wokovu.
5*a* Hel. 5:18; M&M 68:3–4.
6*a* Mt. 10:19–20; M&M 84:85.
7*a* M&M 84:61.
b MWM Pole, Upole.
8*a* 2 Ne. 33:1–4.
9*a* Ku. 4:14–16; 2 Ne. 3:17–18; M&M 124:103–104.

kuwa msemaji kwa mtumishi wangu Joseph.

10 Nami nitampa yeye uwezo wa kuwa mwenye nguvu katika [a]ushuhuda.

11 Na nitakupa wewe uwezo wa kuwa mwenye [a]nguvu katika kuyaelezea maandiko yote, ili wewe uwe msemaji kwake, naye atakuwa [b]mfunuzi kwako, ili uweze kujua uhakika wa mambo yote yahusuyo mambo ya ufalme hapa duniani.

12 Kwa hiyo, endeleeni na safari yenu na mioyo yenu ifurahi; kwani tazameni, na lo, Mimi nipo pamoja nanyi hadi mwisho.

13 Na sasa ninawapa neno juu ya [a]Sayuni. Sayuni [b]itakombolewa, ingawa yeye anatiwa adabu kwa kipindi kifupi.

14 Ndugu zenu, watumishi wangu [a]Orson Hyde na John Gould, wako mikononi mwangu; na ilimradi wao wanazishika amri zangu wataokolewa.

15 Kwa hiyo, mioyo yenu na ifarijike; kwani mambo [a]yote yatafanya kazi kwa pamoja kwa manufaa yao wale watembeao wima, na kwa utakaso wa kanisa

16 Kwani nitajiinulia watu [a]safi, ambao watanitumikia katika haki.

17 Na wale wote [a]walilingao jina la Bwana, na kuzishika amri zake, wataokolewa. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 101

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 16 na 17 Desemba 1833. Wakati huu Watakatifu waliokuwa wamekusanyika Missouri walikuwa wakiudhiwa kwa mateso makubwa. Makundi ya wahuni yaliwafukuza kutoka majumbani mwao katika Wilaya ya Jackson; na baadhi ya Watakatifu walijaribu kuanzisha makazi yao katika Wilaya za Van Buren, Lafayette, na Ray, lakini usumbufu uliwafuata. Kundi kubwa la Watakatifu kwa wakati huo lilikuwa katika Wilaya ya Clay, Missouri. Vitisho vya mauaji dhidi ya watu wa Kanisa vilikuwa vingi. Watakatifu huko Wilaya ya Jackson walikuwa wamepoteza samani za majumbani, nguo, mifugo, na mali nyingine binafsi; mengi ya mazao yao yalikuwa yameharibiwa.

1–8, Watakatifu wanarudiwa na kuteswa kwa sababu ya uvunjaji wao wa sheria; 9–15, Uchungu wa hasira ya Bwana utaanguka juu

10*a* MWM Shuhudia.
11*a* Alma 17:2–3.
b M&M 124:125.
13*a* MWM Sayuni.
b M&M 84:99; 105:9–10, 31, 37.
14*a* MWM Hyde, Orson.
15*a* Rum. 8:28; M&M 90:24; 105:40.
16*a* MWM Safi na Isiyo safi.
17*a* Yoe. 2:32; Alma 38:4–5.

ya mataifa, lakini watu Wake atawakusanya na kuwafariji; 16–21, Sayuni na vigingi vyake vitaimarishwa; 22–31, Namna ya maisha wakati wa Milenia yaelezwa; 32–42, Watakatifu watabarikiwa na kuzawadiwa wakati huo; 43–62, Mfano juu ya watu maarufu na mizeituni inaelezea ya matatizo na hatimaye ukombozi wa Sayuni; 63–75, Watakatifu waendelee kukusanyika pamoja; 76–80, Bwana aliiweka Katiba ya Marekani; 81–101, Watakatifu lazima waombe kwa ajili ya kufidiwa kwa mambo yasiyo ya haki, kulingana na mfano wa mwanamke na mwamuzi asiye na haki.

Amini ninawaambia, juu ya ndugu zenu ambao wameumizwa, na [a]kuteswa, na [b]kufukuzwa kutoka kwenye nchi ya urithi wao—

2 Mimi, Bwana, nimeruhusu [a]mateso yaje juu yao, ambayo kwayo wameteswa, kama matokeo ya [b]uvunjaji wao wa sheria;

3 Hata hivyo nitawamiliki, nao watakuwa [a]wangu katika siku ile wakati nitakapokuja kuwafanya kuwa hazina yangu.

4 Kwa hiyo, hawana budi [a]kurudiwa na kujaribiwa, hata kama [b]Ibrahimu, ambaye aliamriwa kumtoa mwanawe wa pekee.

5 Kwani wale wote ambao hawatastahimili kurudiwa, bali [a]kunikana Mimi, hawawezi [b]kutakaswa.

6 Tazama, ninawaambia, palikuwa na mafarakano, na [a]mabishano, na [b]wivu, na migongano, na [c]ashiki na tamaa mbaya miongoni mwao; kwa hiyo kwa mambo haya waliuchafua urithi wao.

7 Walikuwa wazito wa [a]kusikiliza sauti ya Bwana Mungu wao; kwa sababu hiyo, Bwana Mungu wao amekuwa mzito wa kusikiliza sala zao, kwa kuwajibu katika siku ya matatizo yao.

8 Katika siku ya amani yao huuchukulia kwa wepesi ushauri wangu; lakini, katika siku ya [a]matatizo yao, wanaona umuhimu wa [b]kunitafuta.

9 Amini ninawaambia, licha ya dhambi zao, moyo wangu umejaa [a]huruma juu yao. [b]Sitawafukuzilia mbali, na katika siku ya [c]ghadhabu nitakumbuka huruma.

10 Nimeapa, na azimio limekwisha toka amri ya zamani ambayo nilitoa kwenu, ya kwamba ningeachia ushuke [a]upanga wa uchungu wa hasira

101 1*a* MWM Mateso, Tesa.
b M&M 103:1–2, 11; 109:47.
2*a* M&M 58:3–4.
b Mos. 7:29–30; M&M 103:4; 105:2–10.
3*a* Isa. 62:3; Mal. 3:17; M&M 60:4.
4*a* M&M 95:1–2; 136:31. MWM Rudi, Kurudiwa.
b Mwa. 22:1–14; Yak. (KM) 4:5. MWM Ibrahimu.
5*a* Mt. 10:32–33; Rum. 1:16; 2 Ne. 31:14.
b MWM Utakaso.
6*a* MWM Ushindani.
b MWM Husuda.
c MWM Tamaa mbaya.
7*a* Isa. 59:2; Mos. 11:22–25; 21:15; Alma 5:38.
8*a* Hel. 12:3.
b Mdo. 17:27; Alma 32:5–16.
9*a* MWM Huruma; Rehema, enye Rehema.
b Yer. 30:11.
c M&M 98:21–22.
10*a* M&M 1:13–14.

yangu kwa niaba ya watu wangu; na kama vile nilivyosema, itakuwa hivyo.

11 Uchungu wa hasira yangu karibu utamwagwa pasipo kipimo juu ya mataifa yote; na hili nitalifanya wakati kikombe cha uovu wao kitakapokuwa [a]kimejaa.

12 Na katika siku ile wote watakaopatikana juu ya [a]mnara wa doria, au kwa maneno mengine, Waisraeli wangu wote, wataokolewa.

13 Na wale waliotawanywa [a]watakusanywa.

14 Na wale wote wenye [a]huzuni watafarijika.

15 Na wale wote walioutoa [a]uhai wao kwa ajili ya jina langu watatuzwa;

16 Kwa hiyo, mioyo yenu na ifarijike juu ya Sayuni; kwa kuwa wenye mwili wote wako [a]mikononi mwangu; tulieni na [b]jueni kuwa Mimi ni Mungu.

17 [a]Sayuni haitaondoshwa kutoka mahali pake, licha ya kuwa watoto wake wametawanywa.

18 Wale wanaobaki, na wako safi moyoni, watarejea, na kuja kwenye [a]urithi wao, wao na watoto wao, kwa [b]nyimbo za shangwe isiyo na mwisho, [c]kujenga mahali palipoharibiwa pa Sayuni—

19 Na haya yote yatakuwa ili unabii wa manabii utimizwe.

20 Na, tazama, hapana [a]mahali pengine palipoteuliwa zaidi ya pale nilipopateua; wala hapatakuwa mahali pengine patakapoteuliwa zaidi ya pale nilipopateua, kwa ajili ya kazi ya kuwakusanya watakatifu wangu—

21 Hadi siku itakapofika wakati itakapoonekana hakuna nafasi zaidi kwa ajili yao; na halafu tena ninazo sehemu nyingine ambazo nitawateulia, nazo zitaitwa [a]vigingi, kwa ajili ya mapazia au nguvu ya Sayuni.

22 Tazama, ni mapenzi yangu, kwamba wale wote walilinganao jina langu, na kuniabudu kulingana na injili yangu isiyo na mwisho, yawapasa [a]kukusanyika pamoja, na [b]kusimama mahali patakatifu;

23 Na kujitayarisha kwa ufunuo ujao, wakati [a]pazia lifunikalo hekalu langu, katika hema takatifu yangu, ambayo huificha dunia, litakapoondolewa, na wote wenye mwili [b]watanione kwa pamoja.

24 Na kila kitu [a]kilichoharibika, iwe mwanadamu, au

11 *a* Hel. 13:14; Eth. 2:9–11.
12 *a* MWM Kesha, Walinzi.
13 *a* Kum. 30:3–6; 1 Ne. 10:14. MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
14 *a* Mt. 5:4.
15 *a* Mt. 10:39. MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.
16 *a* Musa 6:32.
b Ku. 14:13–14; Zab. 46:10.
17 *a* MWM Sayuni.
18 *a* M&M 103:11–14.
b Isa. 35:10; M&M 45:71. MWM Imba.
c Amo. 9:13–15; M&M 84:2–5; 103:11.
20 *a* M&M 57:1–4.
21 *a* M&M 82:13–14; 115:6, 17–18. MWM Kigingi.
22 *a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b Mt. 24:15; M&M 45:32; 115:6.
23 *a* MWM Pazia.
b Isa. 40:5; M&M 38:8; 93:1. MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
24 *a* M&M 29:24.

mnyama wa mwituni, au ndege wa angani, au samaki wa baharini, vile viishivyo juu ya uso wote wa dunia vyote, [b]vitateketezwa;

25 Na pia vile vitu vya asili [a]vitayeyuka kwa joto kali; na vitu vyote vitakuwa [b]vipya, ili ufahamu na [c]utukufu wangu vipate kukaa juu ya dunia yote.

26 Na katika siku hiyo [a]uadui wa mwanadamu, na uadui wa wanyama, ndiyo, uadui wa wote wenye mwili [b]utakoma kutoka mbele ya uso wangu.

27 Na katika siku hiyo lolote ambalo mtu yeyote ataliomba, atapewa.

28 Na katika siku hiyo [a]Shetani hatakuwa na uwezo wa kumjaribu mwanadamu yeyote.

29 Na hapatakuwa na [a]huzuni kwa sababu hapatakuwa na mauti.

30 Katika siku hiyo [a]mtoto mchanga hatakufa hadi amekuwa mzee; na uhai wake utakuwa kama umri wa mti;

31 Na wakati atakapokufa hatalala, kama tusemavyo duniani, bali [a]atabadilishwa kwa dakika moja kufumba na kufumbua jicho, na [b]kunyakuliwa, na pumziko lake litakuwa tukufu.

32 Ndiyo, amini ninawaambia, katika [a]siku hiyo wakati Bwana atakapokuja, [b]atayafunua mambo yote—

33 Mambo yaliyokwishapita, na mambo [a]yaliyofichika ambayo hapana mwanadamu aliyejua, mambo ya dunia, ambayo kwayo iliumbwa, na madhumuni na mwisho wake—

34 Mambo yaliyo muhimu zaidi, mambo yaliyo juu, na mambo yaliyo chini, mambo yaliyo ndani ya dunia, na juu ya dunia, na mbinguni.

35 Na wale wote wasumbukao na [a]mateso kwa ajili ya jina langu, na kustahimili katika imani, ingawa wameitwa kuutoa uhai wao [b]kwa ajili yangu hata hivyo nao watashiriki utukufu huu wote.

36 Kwa hiyo, msiogope hata kwa [a]mauti; kwani katika ulimwengu huu shangwe yenu siyo kamilifu, bali ndani yangu [b]shangwe yenu ni kamilifu.

37 Kwa hiyo, msiujali mwili, wala uzima wa mwili; bali zijalini [a]nafsi, na uzima wa nafsi.

38 Na [a]utafuteni uso wa Bwana daima, ili kwa [b]subira mpate kuziponya nafsi zenu, nanyi mtapata uzima wa milele.

39 Wakati wanadamu wana-

24*b* Sef. 1:2–3; Mal. 4:1; M&M 88:94; JS—H 1:37.
25*a* Amo. 9:5; 2 Pet. 3:10–14. MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia.
b Ufu. 21:5.
c MWM Milenia.
26*a* Isa. 11:6–9. MWM Uadui.
b MWM Amani.
28*a* Ufu. 20:2–3; 1 Ne. 22:26; M&M 88:110.
29*a* Ufu. 21:4.
30*a* Isa. 65:20–22; M&M 63:51.
31*a* 1 Kor. 15:52; M&M 43:32.
b 1 The. 4:16–17.
32*a* M&M 29:11. MWM Milenia.
b M&M 121:26–28.
33*a* MWM Siri za Mungu.
35*a* M&M 63:20. MWM Mateso, Tesa.
b M&M 98:13.
36*a* MWM Mauti ya Kimwili.
b MWM Shangwe.
37*a* MWM Nafsi.
38*a* 2 Nya. 7:14; M&M 93:1.
b MWM Subira.

poitwa kwa [a]injili yangu isiyo na mwisho, na kuahidi kwa agano lisilo na mwisho, wao huhesabika kama [b]chumvi ya dunia na ladha ya wanadamu;

40 Wao huitwa kuwa ladha kwa wanadamu; kwa hiyo, ikiwa chumvi ya dunia itapoteza ladha yake, tazama, haifai tena kwa lolote ila kutupwa nje na kukanyagwa na miguu ya watu.

41 Tazama, hapa ndipo penye hekima kuhusu watoto wa Sayuni, hata wengi, bali siyo wote; walipatikana wavunjaji wa sheria, kwa hiyo hawana budi [a]kurudiwa—

42 Yule [a]ajikwezaye mwenyewe atadhiliwa, naye [b]ajidhiliye mwenyewe atakwezwa.

43 Na sasa, nitawaonyesha mfano, ili mpate kujua mapenzi yangu kuhusu ukombozi wa Sayuni.

44 Mtu mmoja [a]kabaila alikuwa na eneo la ardhi, zuri sana; na akawaambia watumishi wake: Enendeni katika [b]shamba langu la mizabibu, hata juu ya sehemu hii ya kipande kilicho kizuri sana, na mpande miti kumi na miwili ya mizeituni;

45 Na wawekeni [a]walinzi kuizunguka, na kujenga mnara, ili mmoja aweze kutazama kuzunguka shamba lote, ili awepo mlinzi juu ya mnara, ili mizeituni yangu isiweze kuvunjwa wakati adui atakapokuja kuiharibu na kujichukulia tunda la mizabibu wangu.

46 Sasa, watumishi wa yule kabaila walikwenda na kufanya kama bwana wao alivyowaamuru, na wakapanda ile mizeituni, na kujenga ua kuizunguka, nakuweka walinzi, na wakaanza kujenga mnara.

47 Na wakati wakiwa bado wanajenga msingi wake, wakaanza kusemezana wao kwa wao: Na bwana wangu anahaja gani na mnara huu?

48 Na wakasemezana kwa muda mrefu, wakisemezana miongoni mwao: Ni haja gani aliyo nayo bwana wangu kwa mnara huu, mbona huu ni wakati wa amani?

49 Fedha hii ingepaswa kuwekwa kwa watoao riba? Kwani hapana haja ya mambo haya.

50 Na wakati walipokuwa wakitofautiana mmoja na mwingine wakawa wavivu sana, na hawakutii ile amri ya bwana wao.

51 Na adui akaja usiku, na akavunja [a]ua; na watumishi wa kabaila yule walipoamka na wakaogopa, na wakakimbia; na adui akaziharibu kazi zao, na kuivunja mizeituni.

52 Sasa, tazama, kabaila, bwana mwenye shamba la mizabibu, aliwaita watumishi wake, na akawaambia, Kwa nini! nini chanzo cha uovu huu mkubwa?

39 *a* MWM Agano Jipya na Lisilo na Mwisho.
b Mt. 5:13; M&M 103:10.
41 *a* MWM Rudi, Kurudiwa.
42 *a* Oba. 1:3–4; Lk. 14:11; Hel. 4:12–13.
b Lk. 18:14.
MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
44 *a* M&M 103:21–22.
b MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
45 *a* Eze. 33:2, 7; 3 Ne. 16:18.
MWM Kesha, Walinzi.
51 *a* Isa. 5:1–7.

53 Ninyi hamkupaswa kufanya kama nilivyowaamuru, na—baada ya kuwa mmepanda shamba la mizabibu, na kujenga ua kulizunguka, na kuwaweka walinzi juu ya ukuta wake—mjenge mnara pia, na kumweka mlinzi juu ya mnara, na kulinda kwa ajili ya shamba langu la mizabibu, na siyo kulala, asije adui akaja juu yenu?

54 Na tazama, mlinzi juu ya mnara angelimwona adui wakati angali bado yuko mbali; na ndipo ninyi mngejitayarisha kuwa tayari na mngelimzuia adui asivunje ua wake, na hivyo kuokoa shamba langu la mizabibu kutoka mikononi mwa mharibifu.

55 Na bwana wa shamba la mizabibu akamwambia mmoja wa watumishi wake: Nenda na uwakusanye watumishi wangu waliobakia, na uchukue nguvu ya nyumba yangu [a]yote, ambao ni wapiganaji wangu, vijana wangu, na wale ambao ni wa umri wa kati pia miongoni mwa watumishi wangu wote, ambao ndiyo nguvu ya nyumba yangu, isipokuwa wale tu ambao nimewateua kukaa;

56 Na nendeni moja kwa moja kwenye nchi ya shamba langu la mizabibu, na mlikomboe shamba langu la mizabibu; kwani ni langu; nimelinunua kwa fedha.

57 Kwa hiyo, nendeni haraka kwenye nchi yangu; bomoeni kuta za adui zangu; angusheni chini mnara wao, na watawanyeni walinzi wao.

58 Na kadiri watakavyo kusanyika pamoja dhidi yenu, [a]nipatieni haki na adui wangu, ili haraka niweze kuja pamoja na mabaki ya nyumba yangu na kuimiliki nchi.

59 Na yule mtumishi akamwambia bwana wake: Mambo haya yatakuwa lini?

60 Naye akamwambia mtumishi wake: Wakati nitakapotaka; enenda zako haraka, na ukafanye mambo yote niliyokuamuru;

61 Na huu ndiyo utakuwa muhuri wangu na baraka juu yako—wakili mwaminifu na mwenye [a]busara ndani ya nyumba yangu, [b]mtawala katika ufalme wangu.

62 Na watumishi wake wakaenda upesi, na wakafanya mambo yote waliyoamriwa na Bwana wake; na [a]baada ya siku nyingi mambo yote yalitimizwa.

63 Tena, amini ninawaambia, nitawaonyesha nionalo kuwa hekima juu ya makanisa yote, ilimradi wapo tayari kuongozwa katika njia ya haki na iliyo sahihi kwa wokovu wao—

64 Ili kazi ya kuwakusanya pamoja watakatifu wangu ipate kuendelea, ili niweze kuwajenga kwa jina langu juu ya [a]mahali patakatifu; kwani wakati wa [b]mavuno umewadia, na neno langu halina budi [c]kutimizwa.

55 *a* M&M 103:22, 29–30; 105:16, 29–30.
58 *a* M&M 97:22–24; 105:15.
61 *a* M&M 78:22.
b Mt. 25:20–23.
62 *a* M&M 105:37.
64 *a* M&M 87:8.
b M&M 33:3, 7. MWM Mavuno.
c M&M 1:38.

65 Kwa hiyo, ni lazima niwakusanye watu wangu pamoja, kulingana na mfano wa ngano na [a]magugu, ili ngano ipate kuhifadhiwa ghalani ili kumiliki uzima wa milele, na kuvikwa taji la utukufu wa [b]selestia, wakati nitakapokuja katika ufalme wa Baba yangu kumzawadia kila mtu kulingana na matendo yake yatakavyokuwa;

66 Wakati magugu yatafungwa mafungu mafungu, na kamba zake zitakuwa imara, ili yaweze [a]kuchomwa kwa moto usiozimika.

67 Kwa hiyo, amri ninaitoa kwa makanisa yote, kwamba wataendelea kukusanyika pamoja mahali pale ambapo nimepateua.

68 Hata hivyo, kama vile nilivyowaambia ninyi katika amri ya awali, na [a]kukusanyika kwenu kusiwe kwa haraka, wala kwa kuruka; bali acheni mambo yote yawe yameandaliwa kabla yenu.

69 Na ili mambo yote yawe yameandaliwa kabla yenu, zishikeni amri ambazo nimezitoa kwenu juu ya mambo haya—

70 Ambayo husema, au hufundisha, [a]kununua ardhi yote kwa fedha, ile iwezekanayo kununuliwa kwa fedha, katika maeneo ya kando ya nchi ambayo nimeiteua kuwa nchi ya Sayuni, kwa ajili ya kuanzia kukusanya watakatifu wangu;

71 Ardhi yote ambayo inaweza kununuliwa katika wilaya ya Jackson, na wilaya za kando kando, na kuyaacha yaliyosalia mikononi mwangu.

72 Sasa, amini ninawaambia, makanisa yote na yakusanye pamoja fedha zao zote; mambo haya na yafanyike kwa wakati wake, lakini siyo kwa [a]haraka; na kuangalia mambo yote yawe yameandaliwa mapema.

73 Na watu maarufu wateuliwe, hata watu wenye hekima, na watumwe kwenda kununua ardhi hiyo.

74 Na makanisa katika nchi za mashariki, wakati yatakapokuwa yamejengwa, ikiwa yatausikiliza ushauri huu yanaweza kununua ardhi na kukusanyika pamoja juu yake; na kwa njia hii yataweza kuanzisha Sayuni.

75 Imekwisha kuwa tayari ghalani ya kutosha, ndiyo, hata kwa wingi, kuikomboa Sayuni, na kupajenga mahali pake palipoharibiwa, pasitupwe chini tena, iwapo makanisa hayo, ambayo hujiita kwa jina langu, yangekuwa [a]tayari kuisikiliza sauti yangu.

76 Na tena ninawaambia, wale ambao wametawanywa na adui zao, ni mapenzi yangu kwamba yawapasa kuendelea kuililia haki na urejesho, na ukombozi, kwa mikono ya wale waliowekwa kama watawala na walio katika mamlaka juu yenu—

77 Kulingana na sheria na [a]katiba ya watu, ambayo

65*a* Mt. 13:6–43; M&M 86:1–7.
b MWM Utukufu wa Selestia.
66*a* Nah. 1:5; Mt. 3:12; M&M 38:12; 63:33–34.
68*a* M&M 58:56.
70*a* M&M 63:27–29.
72*a* Isa. 52:10–12.
75*a* Alma 5:37–39.
77*a* MWM Utawala.

nimeiruhusu iwekwe, na kulindwa kwa ajili ya [b]haki na ulinzi wa wote wenye mwili, kulingana na kanuni zilizo za haki na takatifu;

78 Ili kila mtu aweze kutenda kulingana na mafundisho na kanuni zihusuzo hali yake ya baadaye, kulingana na [a]haki ya kujiamulia ambayo nimempa, ili kila mtu aweze [b]kuwajibika kutokana na dhambi zake mwenyewe katika siku ya [c]hukumu.

79 Kwa hiyo, siyo sahihi kwamba mtu yeyote awe mtumwa kwa mtu mwingine.

80 Na kwa dhumuni hili nimeiweka [a]Katiba ya nchi hii, kwa mikono ya watu wenye hekima ambao niliwainua hasa kwa dhumuni hili, na kuikomboa nchi kwa [b]kumwaga damu.

81 Sasa, tuwalinganishe na nini watoto wa Sayuni? Nitawalinganisha na [a]mfano wa mwanamke na mwamuzi asiye na haki, kwani wanadamu imewapasa daima [b]kuomba na pasipo kuchoka, ambao husema—

82 Palikuwako katika mji mwamuzi ambaye hakumwogopa Mungu, wala hakumjali mtu.

83 Na palikuwako na mwanamke mjane katika mji ule, naye alimwendea, akisema: Nipatie haki na adui yangu.

84 Naye kwa muda alikataa, lakini baadaye akasema moyoni mwake: Ijapokuwa simwogopi Mungu, wala sijali mtu, lakini kwa sababu mjane huyu ananisumbua nitampatia haki yake, asije akanichosha kwa kunijia daima.

85 Hivyo ndivyo nitakavyo walinganisha watoto wa Sayuni.

86 Na walie chini ya miguu ya mwamuzi;

87 Na ikiwa hatawasikiliza, na walie chini ya miguu ya gavana;

88 Na ikiwa gavana hatawasikiliza, na walie chini ya miguu ya rais;

89 Na kama rais hatawasikiliza, ndipo Bwana atainuka na kutoka mahali pake [a]alipojificha, na katika hasira yake kuu atalitesa taifa;

90 Na katika hasira yake, na katika ghadhabu yake, katika wakati wake, atawakatilia mbali wale waovu, wasio waaminifu, na [a]watumishi wasio na haki, na kuwateulia nafasi yao miongoni mwa wanafiki, na [b]wasioamini;

91 Hata nje gizani, ndiko kuna [a]kilio, na kuomboleza, na kusaga meno.

92 Kwa hiyo, ombeni, kwamba masikio yao yapate kufunguliwa kwa vilio vyenu, ili niweze [a]kuwahurumia, ili mambo haya yasiwafikie juu yao.

93 Niliyoyasema kwenu haya-

77 *b* MWM Huru, Uhuru.
78 *a* MWM Haki ya uamuzi.
b MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
c MWM Hukumu ya mwisho.
80 *a* 2 Ne. 1:7–9; M&M 98:5–6.
MWM Katiba.
b 1 Ne. 13:13–19.
81 *a* Lk. 18:1–8.
b MWM Sala.
89 *a* Isa. 45:15; M&M 121:1, 4; 123:6.
90 *a* MWM Msimamizi, Usimamizi.
b Ufu. 21:8.
MWM Kutoamini.
91 *a* Mt. 25:30; M&M 19:5; 29:15–17; 124:8.
92 *a* MWM Rehema, enye Rehema.

na budi kutukia, ili watu wote wasiwe na [a]udhuru;

94 Ili watu wenye hekima na watawala wapate kusikia na kujua yale ambayo kamwe [a]hawakuyafahamu;

95 Ili nilitimize tendo langu, tendo langu la [a]ajabu, na kufanya kazi yangu, kazi yangu ya ajabu, ili watu wapate [b]kupambanua kati ya wenye haki na waovu, asema Mungu wenu.

96 Na tena, ninawaambia, ni kinyume cha amri na mapenzi yangu kwamba mtumishi wangu Sidney Gilbert kuuza [a]ghala yangu, ambayo nimeikabidhi kwa watu wangu, kuiuza mikononi mwa adui zangu.

97 Msiache kile nilichowakabidhi kichafuliwe kwa mikono ya adui zangu, kwa idhini ya wale [a]wajiitao kwa jina langu;

98 Kwani hii ni dhambi mbaya na kubwa sana dhidi yangu, na dhidi ya watu wangu, kwa sababu ya mambo yale ambayo nimeyatangaza na ambayo karibu yatawaangukia mataifa.

99 Kwa hiyo, ni mapenzi yangu kwamba watu wangu wadai, na washikilie madai yao juu ya kile nilichowagawia, ingawa hawataruhusiwa kuishi juu yake.

100 Hata hivyo, sisemi kwamba hawataishi juu yake; kwani ilimradi wao watazaa matunda na kazi zinazostahili kwa ufalme wangu wataishi juu yake.

101 Watajenga, na mtu mwingine [a]hatairithi; nao wapanda mizabibu, na kula matunda yake. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 102

Kumbukumbu za muundo wa baraza kuu la kwanza la Kanisa, huko Kirtland, Ohio, 17 Februari 1834. Kumbu kumbu halisi ziliandikwa na Wazee Oliver Cowdery na Orson Hyde. Siku mbili baadaye, Nabii alifanya marejeo muhtasari ule siku iliyofuata, siku iliyofuata tena muhtasari ule uliosahihishwa ulikubaliwa kwa kura zote na baraza kuu kama "muundo na katiba ya baraza kuu" la Kanisa. Aya ya 30 hadi 32, inahusika na Baraza la Mitume Kumi na Wawili, iliongezwa mwaka 1835 chini ya maelekezo ya Joseph Smith wakati sehemu hii ikitayarishwa kwa ajili ya kuchapishwa katika Mafundisho na Maagano.

1–8, Baraza kuu limeanzishwa ili kutatua matatizo muhimu yanayojitokeza katika Kanisa; 9–18, Taratibu zinatolewa kwa ajili ya kusikiliza mashauri; 19–23, Rais wa baraza ndiye atoaye uamuzi;

93*a* Rum. 1:18–21.
94*a* Isa. 52:15; 3 Ne. 20:45; 21:8.
95*a* Isa. 28:21; M&M 95:4.
b Mal. 3:18. MWM Utambuzi, Kipawa cha.
96*a* MWM Ghala.
97*a* M&M 103:4; 112:25–26; 125:2.
101*a* Isa. 65:21–22. MWM Milenia.

24–34, Utaratibu wa kukata rufani unaelezwa.

Siku ya leo baraza kuu la makuhani wakuu ishirini na wanne limekusanyika katika nyumba ya Joseph Smith, Mdogo, kwa ufunuo, na kuanza kuunda [a]baraza kuu la kanisa la Kristo, ambalo litaundwa na makuhani wakuu kumi na wawili, na rais mmoja au watatu, kama shauri litakavyohitaji.

2 Baraza kuu liliteuliwa kwa ufunuo kwa madhumuni ya kutatua matatizo muhimu ambayo yangeweza kujitokeza katika kanisa, ambayo hayangeweza kutatuliwa na kanisa au baraza la [a]askofu ili kuziridhisha pande hizi.

3 Joseph Smith, Mdogo, Sidney Rigdon na Frederick G. Williams walikubalika kama marais kwa sauti ya baraza; na Joseph Smith, Mkubwa, John Smith, Joseph Coe, John Johnson, Martin Harris, John S. Carter, Jared Carter, Oliver Cowdery, Samuel H. Smith, Orson Hyde, Sylvester Smith, na Luke Johnson, makuhani wakuu, walichaguliwa kuwa baraza la kudumu kwa kanisa, kwa kura nyingi za baraza.

4 Wajumbe waliotajwa hapo juu waliulizwa kama wanakubali uteuzi wao, na kama watatenda katika ofisi ile kulingana na sheria ya mbinguni, ambapo wote walijibu kwamba wamekubali uteuzi wao, nao watazitumikia ofisi zao kulingana na neema ya Mungu iliyowekwa juu yao.

5 Na idadi iliyounda baraza, ambao walipiga kura katika jina na kwa ajili ya kanisa katika kuchagua majina ya wajumbe waliotajwa hapo juu walikuwa arobaini na watatu, kama ifuatavyo: makuhani wakuu tisa, wazee kumi na saba, makuhani wanne, na waumini wa kanisa kumi na watatu

6 Ilipigwa kura: kwamba baraza kuu halitakuwa na uwezo wa kuamua bila wajumbe saba waliotajwa hapo juu, au wawakilishi wao walioteuliwa rasmi kuwepo.

7 Hawa saba watakuwa na uwezo wa kuwateua makuhani wengine wakuu, ambao watawaona kuwa wanastahili na kuwa wanauwezo wa kutenda katika nafasi za wajumbe wasiokuwepo.

8 Ilipigwa kura: kwamba iwapo nafasi yoyote itatokea kutokana na kifo, kuondolewa kutoka katika nafasi kwa ajili ya kuvunja sheria, au kuondolewa kutoka katika mipaka ya serikali ya kanisa hili, kwa yeyote kati ya wajumbe waliotajwa hapo juu, itajazwa kwa uteuzi wa rais au marais, na kuungwa mkono na sauti ya baraza kuu la makuhani wakuu, litakaloitishwa kwa madhumuni hayo, ya kutenda katika jina la kanisa.

9 Rais wa kanisa, ambaye pia ni rais wa baraza, huteuliwa kwa [a]ufunuo, na [b]kuthibitishwa

102 1*a* mwm Baraza Kuu.
2*a* M&M 107:72–74.
9*a* mwm Ufunuo.
b mwm Kuwakubali

katika utawala wake kwa sauti ya kanisa.

10 Na ni kulingana na heshima ya ofisi yake yampasa kuwa kiongozi wa baraza la kanisa; na ni haki yake kusaidiwa na marais wengine wawili, walioteuliwa kwa jinsi hiyo hiyo ambayo yeye mwenyewe aliteuliwa.

11 Na ikiwa mmoja wapo au wote wawili walioteuliwa kumsaidia hawapo, yeye anao uwezo wa kuliongoza baraza bila ya msaidizi; na iwapo yeye mwenyewe hayupo, marais wengine wanao uwezo wa kuongoza badala yake, iwe wote au mmoja wao.

12 Wakati wowote baraza kuu la kanisa la Kristo likiwa limeanzishwa rasmi, kulingana na utaratibu uliotajwa, itakuwa ni wajibu wa wajumbe kumi na wawili kupiga kura kwa namba, kwa njia hiyo watabainisha nani kati ya hao kumi na wawili atazungumza kwanza, wakianza nambari moja na hivyo kuendelea hadi nambari kumi na mbili.

13 Wakati wowote baraza hili likutanapo kuamua shauri lolote, wajumbe hawa kumi na wawili watatafakari iwapo ni gumu au hapana; kama hapana, wawili tu kati ya wajumbe ndiyo watazungumza juu yake, kulingana na utaratibu ulioandikwa hapo juu.

14 Lakini ikiwa litadhaniwa kuwa gumu, wanne watateuliwa; na kama ni gumu zaidi, sita; lakini katika hali yoyote ile pasiteuliwe wazungumzaji zaidi ya sita.

15 Mshtakiwa, katika mashauri yote, anayo haki ya kutetewa na nusu ya wajumbe wa baraza, ili kuzuia kufedheheshwa au kutotendewa haki.

16 Na wajumbe walioteuliwa kuzungumza mbele ya baraza watalileta shauri, baada ya ushahidi kuchunguzwa, katika nuru yake ya kweli mbele ya baraza; na kila mtu ataongea kulingana na usawa na [a]haki.

17 Wale wajumbe waliookota namba chanya, ambazo ni 2, 4, 6, 8, 10, na 12, ndiyo watu ambao watasimama kwa niaba ya mshtakiwa, na kuzuia fedheha na kutotendewa haki.

18 Katika mashauri yote mshtaki na mshtakiwa watakuwa na haki ya kuzungumza wenyewe mbele ya baraza, baada ya ushahidi kusikilizwa na wajumbe ambao wameteuliwa kuzungumza juu ya shauri hilo kumaliza kutoa maelezo yao.

19 Baada ya ushahidi kusikilizwa, wajumbe, mshtaki na mshtakiwa kuwa wamezungumza, rais atatoa uamuzi kulingana na ufahamu ambao ataupata juu ya kesi hiyo, na atawaomba wajumbe hao kumi na wawili kupitisha uamuzi huo kwa kura zao.

20 Lakini iwapo wajumbe waliobakia, ambao hawakuzungumza, au yeyote kati yao, baada ya kusikiliza ushahidi na maombi vizuri bila kuegemea kokote, wanagundua kosa katika uamuzi wa rais, wanaweza

16*a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.

kulionyesha, na shauri litarudiwa kusikilizwa.

21 Na kama, baada ya marejeo ya usikilizaji wa makini, taarifa yoyote ya nyongeza itaonyeshwa juu ya shauri hilo, uamuzi utarekebishwa mara moja.

22 Lakini iwapo hakuna taarifa ya nyongeza iliyotolewa, uamuzi wa kwanza utasimama, na wingi wa baraza linao uwezo wa kuzingatia uamuzi.

23 Iwapo pana ugumu juu ya [a]mafundisho au kanuni, kama hakuna maandishi ya kutosha kuliweka wazi shauri mawazoni mwa baraza, rais anaweza kuomba na kupata nia ya Bwana kwa [b]ufunuo.

24 Makuhani wakuu, wawapo ng'ambo, wanao uwezo wa kuteua na kuunda baraza kwa jinsi ilivyoelekezwa, ili kutatua matatizo, wakati pande mbili hizi au mmoja kati yao itaomba hivyo.

25 Na baraza lililotajwa hapa la makuhani wakuu litakuwa na uwezo wa kumteua mmoja kati yao wenyewe kuliongoza baraza hilo kwa wakati huo.

26 Utakuwa ni wajibu wa baraza hilo kupeleka, haraka iwezekanavyo, nakala ya yaliyotendeka yenye maelezo kamili ya ushuhuda ulioambatana na uamuzi wao, kwa baraza kuu la kiti cha Urais wa Kwanza wa Kanisa.

27 Iwapo pande zote au moja wapo haikuridhika na uamuzi uliotolewa na baraza husika, wanaweza kukata rufaa kwa baraza kuu la kiti cha Urais wa Kwanza wa Kanisa, na kusikilizwa upya tena, shauri ambalo litaendeshwa, kulingana na utaratibu ulioandikwa, mwanzoni, kama vile uamuzi kama huo haukufanyika.

28 Baraza hili la makuhani wakuu ng'ambo litateuliwa tu wakati wa mashauri [a]magumu sana ya kanisa; na hakuna mashauri ya mara kwa mara au ya kawaida yatakayotosheleza kuitwa kwa baraza la aina hiyo.

29 Makuhani wakuu wasafirio mbali na makao makuu au wale waliowekwa mbali wanao uwezo wa kusema endapo ni muhimu kuteuliwa kwa baraza hilo au hapana.

30 Kuna tofauti kati ya baraza kuu au makuhani wakuu wasafirio mbali na makao, na [a]baraza kuu lisafirilo lenye jumla ya [b]mitume kumi na wawili, katika maamuzi yao.

31 Kutoka kwenye maamuzi ya baraza la kwanza inawezekana kukata rufaa; lakini kutokana na maamuzi ya baraza la pili haiwezekani.

32 La pili linaweza tu kuulizwa na viongozi wakuu wa kanisa katika shauri la kuvunjwa kwa sheria.

33 Imeazimiwa: kwamba rais au marais wa kiti cha Urais wa Kwanza wa Kanisa watakuwa na uwezo wa kuamua iwapo shauri la aina hiyo, kama vile litakavyoweza kukatiwa rufaa, linayo haki ya kusikilizwa upya, baada ya kuchunguza

23 *a* Hes. 9:8.
b MWM Ufunuo.
28 *a* M&M 107:78.
30 *a* M&M 107:23–24, 35–38.
b MWM Mtume.

rufani na ushahidi na maelezo yanayoambatana nayo.

34 Wajumbe hao kumi na wawili ndipo waliendelea kupiga kura au kura ya siri, ili kuamua nani azungumze kwanza, na yafuatayo yalikuwa matokeo yake, kwa majina: 1, Oliver Cowdery; 2, Joseph Coe; 3, Samuel H. Smith; 4, Luke Johnson; 5, John S. Carter; 6, Sylvester Smith; 7, John Johnson; 8, Orson Hyde, 9, Jared Carter; 10, Joseph Smith, Mkubwa; 11, John Smith; 12, Martin Harris.

Baada ya sala mkutano uliahirishwa.

Oliver Cowdery,
Orson Hyde,
Makarani

SEHEMU YA 103

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 24 Februari 1834. Ufunuo huu ulipokelewa baada ya kuwasili huko Kirtland, Ohio, kwa Parley P. Pratt na Lyman Wight, ambao walikuja kutoka Missouri ili kushauriana na Nabii juu ya kuwapelekea msaada na urejesho wa Watakatifu kwenye ardhi yao katika Wilaya ya Jackson.

1–4, Kwa nini Bwana aliruhusu Watakatifu katika Wilaya ya Jackson kuteswa; 5–10, Watakatifu watashinda ikiwa watashika amri; 11–20, Ukombozi wa Sayuni utakuja kwa uwezo, na Bwana atakwenda mbele ya watu Wake; 21–28, Watakatifu watakusanyika katika Sayuni, na wale ambao huutoa uhai wao watauona tena; 29–40, Ndugu kadhaa wanaitwa kuunda Kambi ya Sayuni na kwenda Sayuni; wanaahidiwa ushindi ikiwa watakuwa waaminifu.

Amini ninawaambia, marafiki zangu, tazama, nitawapa ufunuo na amri, ili mpate kujua namna ya [a]kutenda katika kutimiza majukumu yenu juu ya wokovu na [b]ukombozi wa ndugu zenu, ambao wametawanywa juu ya nchi ya Sayuni;

2 Wakiwa [a]wamefukuzwa na kupigwa kwa mikono ya adui zangu, ambao nitawamwagia ghadabu pasipo kipimo katika wakati wangu.

3 Kwani nimewavumilia vya kutosha, ili wapate [a]kujaza kipimo cha uovu wao, ili kikombe chao kipate kujaa;

4 Na ili wale wajiitao wenyewe kwa jina langu wapate [a]kurudiwa kwa kipindi kifupi kwa adhabu iliyo kali na chungu, kwa sababu [b]hawakutii kabisa mausia na amri ambazo niliwapa.

5 Lakini amini ninawaambia, kwamba nimeagiza agizo ambalo watu wangu watalipata,

103 1*a* M&M 43:8.
b M&M 101:43–62.
2*a* M&M 101:1; 109:47.
3*a* Alma 14:10–11; 60:13.
4*a* M&M 95:1.
mwm Rudi, Kurudiwa.
b M&M 101:2; 105:2–6.

ilimradi tu watu wangu watatii kutoka saa hii [a]ushauri ambao Mimi, Bwana Mungu wao, nitautoa kwao.

6 Tazama watashinda, kwani nimeagiza, waanze kushinda dhidi ya adui zangu kutoka saa hii.

7 Na kuwa [a]waangalifu kwa maneno yote ambayo Mimi, Bwana Mungu wao, nitasema kwao, kamwe hawatakoma kushinda hadi [b]falme za ulimwengu ziwekwe chini ya miguu yangu, na dunia [c]itolewe kwa [d]watakatifu, ili [e]kuimiliki milele na milele.

8 Lakini kadiri [a]wasivyozishika amri zangu, na wala hawaangalii kutii maneno yangu yote, falme za ulimwengu zitawashinda.

9 Kwani wao waliwekwa kuwa [a]nuru kwa ulimwengu, na kuwa njia ya wokovu kwa wanadamu;

10 Na ilimradi wao sio njia ya wokovu kwa wanadamu, wao ni sawa sawa na [a]chumvi iliyopoteza ladha yake, na haifai tena kwa lolote ila kutupwa nje na kukanyagwa chini ya miguu ya watu.

11 Lakini amini ninawaambia, nimeazimia kwamba ndugu zenu ambao wametawanywa watarudi katika [a]nchi ya urithi wao, na kujenga mahali palipoharibiwa pa Sayuni.

12 Kwa kuwa baada ya [a]taabu nyingi, kama nilivyosema kwenu katika amri ya zamani, huja baraka.

13 Tazama, hii ndiyo baraka niliyoahidi baada ya masumbuko yenu, na masumbuko ya ndugu zenu—ukombozi wenu, na ukombozi wa ndugu zenu, hata urejesho wao katika nchi ya Sayuni, ili kuwaimarisha, kamwe wasitupwe chini tena.

14 Hata hivyo, endapo watauchafua urithi wao watatupwa chini; kwani sitawahurumia kama watachafua urithi wao.

15 Tazama, ninawaambia, ukombozi wa Sayuni hauna budi kuja kwa uwezo;

16 Kwa hiyo, nitawainulia watu wangu mtu, ambaye atawaongoza kama jinsi [a]Musa alivyowaongoza wana wa Israeli.

17 Kwani ninyi ni wana wa Israeli, na wa [a]uzao wa Ibrahimu, na ninyi hamna budi kuongozwa kutoka utumwani kwa uwezo, na kwa mkono ulionyoshwa.

18 Na kama vile baba zenu walivyoongozwa zamani, hivyo ndivyo ukombozi wa Sayuni utakavyokuwa.

19 Kwa hiyo, msiache mioyo yenu ikate tamaa, kwani siwaambii ninyi kama nilivyowaambia baba zenu: [a]Malaika

5*a* MWM Ushauri.
7*a* M&M 35:24. MWM Mtiifu, Tii, Utii.
b Dan. 2:44.
c Dan. 7:27.
d MWM Mtakatifu.
e M&M 38:20.
8*a* Mos. 1:13; M&M 82:10.
9*a* 1 Ne. 21:6.
10*a* Mt. 5:13–16; M&M 101:39–40.
11*a* M&M 101:18.
12*a* Ufu. 7:13–14; M&M 58:4; 112:13.
16*a* Ku. 3:2–10; M&M 107:91–92. MWM Musa.
17*a* MWM Agano la Ibrahimu; Ibrahimu—Uzao wa Ibrahimu.
19*a* MWM Malaika.

wangu atatangulia mbele yenu, lakini sio [b]uwepo wangu.

20 Lakini ninawaambia: Kuwa [a]malaika wangu watatangulia mbele yenu, na pia uwepo wangu, na hatimaye [b]mtaimiliki nchi iliyo bora.

21 Amini, amini ninawaambia, kwamba mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, ndiye [a]mtu ambaye nilimfananisha na mtumishi ambaye Bwana wa [b]shamba alimzungumzia katika mfano ambao nimewapa.

22 Kwa hiyo acheni mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, aseme na [a]nguvu ya nyumba yangu, vijana wangu wa kiume na walio na umri wa kati—Jikusanyeni pamoja katika nchi ya Sayuni, juu ya nchi ambayo nimeinunua kwa fedha ambayo imewekwa wakfu kwa ajili yangu.

23 Na makanisa yote yawatume watu wao wenye hekima pamoja na fedha, na [a]wanunue ardhi kama nilivyowaamuru.

24 Na kadiri maadui zangu wanavyokuja dhidi yenu ili kuwafukuza kutoka katika [a]ardhi yangu iliyo bora, ambayo nimeiweka wakfu kuwa nchi ya Sayuni, hata nchi yenu wenyewe baada ya shuhuda hizi, ambazo mmeniletea mbele yangu dhidi yao, ninyi mtawalaani.

25 Na yeyote mtakayemlaani, nitamlaani, nanyi mtanipatia haki na adui zangu.

26 Na uwepo wangu utakuwepo kati yenu hata katika [a]kunipatia haki mimi na adui zangu, hata kwa kizazi cha tatu na cha nne cha wale wanichukiao Mimi.

27 Na mtu yeyote asiogope [a]kuutoa uhai wake kwa ajili yangu; kwa kuwa yeyote autoaye uhai wake kwa ajili yangu atauona tena.

28 Na yeyote asiye kuwa tayari kuutoa uhai wake kwa ajili yangu siyo mwanafunzi wangu.

29 Ni mapenzi yangu kuwa mtumishi wangu [a]Sidney Rigdon akainue sauti yake katika mikutano katika nchi za mashariki, katika kuyatayarisha makanisa kushika amri ambazo nimewapa juu ya urejesho na ukombozi wa Sayuni.

30 Ni mapenzi yangu kwamba mtumishi wangu [a]Parley P. Pratt na mtumishi wangu Lyman Wight wasirudi katika nchi ya ndugu zao, hadi wao watakapokuwa wamepata watu wa kuongozana nao kwenda nchi ya Sayuni, kwa makumi, au kwa ishirini, au kwa hamsini, au kwa mamia, hadi watakapokuwa wamepata idadi ya mia tano ya [b]nguvu ya nyumba yangu.

31 Tazama haya ndiyo mapenzi yangu; ombeni nanyi

19 *b* M&M 84:18–24.
20 *a* Ku. 14:19–20.
b M&M 100:13.
21 *a* M&M 101:55–58.
b MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
22 *a* M&M 35:13–14; 105:16, 29–30.
23 *a* M&M 42:35–36; 57:5–7; 58:49–51; 101:68–74.
24 *a* M&M 29:7–8; 45:64–66; 57:1–2.
26 *a* M&M 97:22.
27 *a* Mt. 10:39; Lk. 9:24; M&M 98:13–15; 124:54.
29 *a* MWM Rigdon, Sidney.
30 *a* MWM Pratt, Parley Parker.
b M&M 101:55.

mtapata; lakini wanadamu [a]siyo mara kwa mara hufanya mapenzi yangu.

32 Kwa hiyo, kama hamwezi kuwapata mia tano, tafuteni kwa bidii kwamba pengine mtaweza kuwapata mia tatu.

33 Na kama hamwezi kuwapata mia tatu, tafuteni kwa bidii kwamba pengine mtaweza kuwapata mia moja.

34 Lakini amini ninawaambia, amri ninawapa, ya kwamba msiende katika nchi ya Sayuni hadi ninyi mmewapata watu mia wa nguvu ya nyumba yangu, ili kwenda pamoja nanyi katika nchi ya Sayuni.

35 Kwa hiyo, kama nilivyowaambia, ombeni nanyi mtapewa; ombeni kwa dhati ili pengine mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, apate kwenda pamoja nanyi, na kuongoza katikati ya watu wangu, na kuanzisha ufalme wangu juu ya nchi iliyowekwa [a]wakfu, na kuwaimarisha watoto wa Sayuni juu ya sheria na amri ambazo zilikuwepo na ambazo zitatolewa kwenu.

36 Vyote, ushindi na utukufu vitapatikana kwenu kutokana na [a]bidii yenu, uaminifu, na [b]sala za imani.

37 Na mtumishi wangu Parley P. Pratt asafiri pamoja na mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo.

38 Na mtumishi wangu Lyman Wight asafiri pamoja na mtumishi wangu Sidney Rigdon.

39 Na mtumishi wangu Hyrum Smith asafiri pamoja na mtumishi wangu Frederick G. Williams.

40 Na mtumishi wangu Orson Hyde asafiri pamoja na mtumishi wangu Orson Pratt, kokote ambako mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, atakakowashauri, katika kupata ukamilifu wa amri hizi ambazo nimewapa, na mengine yote yaacheni mikononi mwangu. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 104

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio au jirani na hapo, 23 Aprili 1834, juu ya Kampuni ya Ushirika, (ona vichwa vya habari sehemu ya 78 na 82). Tukio yawezekana lilikuwa lile la mkutano wa wanachama wa Kampuni ya Ushirika, ambao ulijadili mahitaji ya kimwili yaliyokuwa yakilisumbua Kanisa. Mkutano wa awali wa kampuni hiyo uliofanyika 10 Aprili ulikuwa umeazimia kampuni hiyo ivunjwe. Ufunuo huu unaelekeza kwamba kampuni badala yake iundwe upya; na mali zake zigawanywe miongoni mwa wanachama wa kampuni hiyo kama wasimamizi. Chini ya maelekezo

31 *a* M&M 82:10.
35 *a* M&M 84:31.
36 *a* MWM Bidii.
b M&M 104:79–82.

ya Joseph Smith, jina Kampuni ya Ushirika liliachwa na badala yake lilitumika "Mpango wa Ushirika" katika ufunuo huu.

1–10, Watakatifu wanaovunja sheria za mpango wa ushirika watalaaniwa; 11–16, Bwana hutimiza mahitaji ya Watakatifu Wake katika njia Yake mwenyewe; 17–18, Sheria ya injili hutawala uangalizi wa maskini; 19–46, Usimamizi na baraka za ndugu mbali mbali zaonyeshwa; 47–53, Mpango wa ushirika huko Kirtland na mpango wa Sayuni zitatenda kazi tofauti; 54–66, Hazina takatifu ya Bwana imewekwa kwa ajili ya kuchapisha maandiko; 67–77, Hazina kuu ya mpango wa ushirika itatenda kazi juu ya msingi wa makubaliano; 78–86, Wale waliomo katika mpango wa ushirika watalipa madeni yao yote, na Bwana atawakomboa kutoka katika utumwa wa kifedha.

Amini ninawaambia, marafiki zangu, ninawapa ushauri, na amri, kuhusu mali zote ambazo ni za mpango ambao nimeamuru uundwe na kuanzishwa, ili uwe [a]mpango wa ushirika, na mpango usio na mwisho kwa faida ya kanisa langu, na kwa ajili ya wokovu wa wanadamu hadi nitakapokuja—

2 Kwa ahadi isiyogeuka na isiyoweza kubadilika, kwamba kadiri wale ambao niliwaamuru walivyokuwa waaminifu wabarikiwe kwa baraka nyingi;

3 Lakini kadiri walivyokuwa siyo waaminifu walikuwa wamekaribia kwenye laana.

4 Kwa hiyo, kwa vile baadhi ya watumishi wangu hawakuzishika amri, bali wamevunja agano kwa [a]tamaa mbaya, na maneno ya kutunga, mimi nimewalaani kwa laana kali na chungu.

5 Kwani Mimi, Bwana, nimeazimia moyoni mwangu, kwamba kadiri mtu yeyote aliye wa mpango huu atakavyoonekana kuwa mvunjaji wa sheria, au, kwa maneno mengine, atavunja agano ambalo kwalo amefungwa, atalaaniwa maishani mwake, na kukanyagwa na yeyote nitakayemtaka;

6 Kwa kuwa Mimi, Bwana, [a]sidhihakiwi katika mambo haya—

7 Na hii yote ili asiye na hatia miongoni mwenu asipate kuhukumiwa pamoja na wasio na haki; na ili mwenye hatia miongoni mwenu asiweze kukwepa; kwa sababu Mimi, Bwana, nimewaahidi [a]taji la utukufu katika mkono wangu wa kulia.

8 Kwa hiyo, kadiri mlivyoonekana kuwa wenye kuvunja sheria, hamwezi kuepuka ghadhabu yangu katika maisha yenu.

9 Na kadiri [a]mlivyokatiliwa mbali kwa ajili ya uvunjaji

104 1*a* M&M 78:3–15. mwm Mpango wa Ushirika.
4*a* mwm Tamani.
6*a* Gal. 6:7–9.
7*a* Isa. 62:3; M&M 76:56. mwm Utukufu.
9*a* mwm Kutengwa na Kanisa.

wenu wa sheria, hamwezi kuepuka [b]mapigo ya [c]Shetani hadi siku ya ukombozi.

10 Nami sasa ninawapa uwezo kutoka saa hii hii, kama kuna mtu yeyote miongoni mwenu, wa mpango huu, atakayepatikana kuwa mvunjaji wa sheria na wala hatubu uovu huo, kwamba mtoeni aende kwenye mapigo ya Shetani; naye hatakuwa na uwezo wa [a]kuleta uovu juu yenu.

11 Ni hekima kwangu; kwa hiyo, amri ninawapa ya kwamba mtajipanga wenyewe na kumgawia kila mtu [a]usimamizi wake;

12 Ili kila mtu apate kutoa hesabu kwangu ya usimamizi wake aliogawiwa.

13 Kwani ni muhimu kwamba Mimi, Bwana, yanipasa kumfanya kila mtu [a]awajibike, kama [b]msimamizi juu ya baraka za kidunia, ambazo nimezifanya na kuzitayarisha kwa ajili ya viumbe vyangu.

14 Mimi, Bwana, nilizitandaza mbingu, na [a]kuijenga dunia, [b]kazi halisi ya mkono wangu; na vitu vyote vilivyomo ni mali yangu.

15 Na ni madhumuni yangu kuwa niwapatie mahitaji watakatifu wangu, kwani vitu vyote ni mali yangu.

16 Lakini haina budi kufanyika katika [a]njia yangu mwenyewe; na tazama hii ndiyo njia ambayo Mimi, Bwana, nimeazimia kutoa mahitaji ya watakatifu wangu, ili [b]maskini wapate kuinuliwa, na kwa njia hiyo matajiri hushushwa.

17 Kwani [a]dunia imejaa, na viko vya kutosha na kubaki; ndiyo, nilitayarisha vitu vyote, na nikawapa wanadamu kuwa na uwezo wa [b]kujiamulia wenyewe.

18 Kwa hiyo, kama mtu yeyote atajichukulia kutoka kwa hivyo [a]vingi nilivyovitengeneza, na asiigawe hiyo sehemu yake, kulingana na [b]sheria ya injili yangu, kwa [c]maskini na wenye shida, yeye, pamoja na waovu, atainua macho yake e [d]jehanamu, akiwa katika mateso.

19 Na sasa, amini ninawaambia, juu ya mali ya [a]ushirika—

20 Acha mtumishi wangu Sidney Rigdon apewe mahali ambapo anaishi sasa, na mahali pa kiwanja cha kiwanda cha ukaushaji wa ngozi kwa usimamizi wake, ili vimsaidie wakati akifanya kazi katika shamba langu la mizabibu, hata kama nitakavyotaka, wakati nitakapo mwamuru.

21 Na acha mambo yote yatendeke kulingana na maelezo ya

9 *b* M&M 82:21.
c MWM Ibilisi.
10 *a* M&M 109:25–27.
11 *a* M&M 42:32.
MWM Msimamizi, Usimamizi.
13 *a* MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
b M&M 72:3–5, 16–22.
14 *a* Isa. 42:5; 45:12.
MWM Umba, Uumbaji.
b Zab. 19:1; 24:1.
16 *a* M&M 105:5.
MWM Ustawi.
b 1 Sam. 2:7–8; Lk. 1:51–53; M&M 88:17.
17 *a* M&M 59:16–20.
MWM Dunia.
b MWM Haki ya uamuzi.
18 *a* Lk. 3:11; Yak. (Bib.) 2:15–16.
b M&M 42:30.
c Mit. 14:21; Mos. 4:26; M&M 52:40.
d Lk. 16:20–31.
19 *a* MWM Mpango wa Ushirika.

ushirika, na ridhaa ya ushirika au sauti ya ushirika, ambao wanaishi katika nchi ya Kirtland.

22 Na usimamizi huu na baraka hii, Mimi, Bwana ninatoa juu ya mtumishi wangu Sidney Rigdon kama baraka juu yake, na uzao wake baada yake;

23 Nami nitazidisha baraka juu yake, kadiri yeye atakavyokuwa mnyenyekevu mbele zangu.

24 Na tena, acha mtumishi wangu Martin Harris akabidhiwe, kwa ajili ya usimamizi wake, kiwanja cha ardhi ambacho mtumishi wangu John Johnson alikipata kwa kubadilishana na urithi wake wa awali, kwa ajili yake na uzao wake baada yake;

25 Na ilimradi ni mwaminifu, nitamzidishia baraka juu yake na uzao wake baada yake.

26 Na acha mtumishi wangu Martin Harris atoe fedha zake kwa ajili ya kuyatangaza maneno yangu, kulingana na vile mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, atakavyomwelekeza.

27 Na tena, acha mtumishi wangu Frederick G. Williams apate sehemu ambayo sasa anaishi.

28 Na acha mtumishi wangu Oliver Cowdery apate kiwanja ambacho kimejitenga lakini karibu na nyumba, ambayo itakuwa kwa ajili ya ofisi ya uchapishaji, ambacho ni kiwanja nambari moja, na pia kiwanja ambacho juu yake baba yake anakaa.

29 Na acha watumishi wangu Frederick G. Williams na Oliver Cowdery wapate ofisi ya uchapishaji na vitu vyote vihusikanavyo.

30 Na huu utakuwa usimamizi wao watakaokabidhiwa.

31 Na kadiri watakavyokuwa waaminifu, tazama nitawabariki, na kuzidisha baraka juu yao.

32 Na huu ndiyo mwanzo wa usimamizi niliowakabidhi wao, kwa ajili yao na uzao wao baada yao.

33 Na, kadiri watakavyokuwa waaminifu, nitazidisha baraka juu yao na uzao wao baada yao, hata wingi wa baraka.

34 Na tena, acha mtumishi wangu John Johnson achukue nyumba ambayo sasa anaishi, na kwa urithi, na kila kitu isipokuwa ardhi iliyotengwa kwa [a]ujenzi wa nyumba zangu, ambayo ni sehemu ya urithi huo, na viwanja vile ambavyo viliwekwa kwa ajili ya mtumishi wangu Oliver Cowdery.

35 Na kadiri atakavyokuwa mwaminifu, nitazidisha baraka juu yake.

36 Na ni mapenzi yangu kwamba auze viwanja vile vilivyopimwa na kutengwa kwa ajili ya ujenzi wa mji wa watakatifu wangu, kadiri itakavyojulishwa kwake kwa [a]sauti ya Roho, na kulingana na maelekezo ya ushirika, na kwa sauti ya ushirika.

37 Na huu ndiyo mwanzo wa usimamizi ambao nimemkabidhi, kwa ajili ya baraka kwake na uzao wake baada yake.

38 Na kadiri atakavyokuwa mwaminifu, nitazidisha wingi wa baraka juu yake.

34*a* M&M 94:3, 10.

36*a* MWM Ufunuo.

39 Na tena, acheni mtumishi wangu [a]Newel K. Whitney akabidhiwe nyumba na kiwanja ambamo sasa anaishi, na kiwanja na jengo ambamo ndani yake biashara hufanyika, na pia kiwanja kilichoko kwenye kona ya kusini mwa stoo ya biashara, na pia kiwanja ambacho kipo kiwanda cha majivu.

40 Na hii yote nimeikabidhi kwa mtumishi wangu Newel K. Whitney kwa ajili ya usimamizi wake, kama baraka juu yake na uzao wake baada yake, kwa manufaa ya biashara za ushirika wangu ambao nimeuanzisha kwa ajili ya kigingi changu katika nchi ya Kirtland.

41 Ndiyo, amini, huu ndiyo usimamizi nilioukabidhi kwa mtumishi wangu N. K. Whitney, hata hii biashara yote, yeye na [a]wakala wake, na uzao wake baada yake.

42 Na kadiri atakavyokuwa mwaminifu katika kushika amri zangu, ambazo nimezitoa kwake, nitazidisha baraka juu yake na uzao wake baada yake, hata wingi wa baraka.

43 Na tena, acha mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, nimemkabidhi kiwanja ambacho kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba yangu, ambacho ni karibu mita mia mbili urefu na sitini upana, na pia urithi ambao juu yake baba yake anaishi sasa;

44 Na huu ndiyo mwanzo wa usimamizi ambao nimemkabidhi, kama baraka juu yake, na juu ya baba yake.

45 Tazama, nimeutunza urithi kwa ajili ya [a]baba yake, kwa ajili ya kumsaidia; kwa hiyo atatambulika katika nyumba ya mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo.

46 Nami nitazidisha baraka juu ya nyumba hiyo ya mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, kadiri atakavyokuwa mwaminifu, hata wingi wa baraka.

47 Na sasa, amri ninatoa kwenu juu ya Sayuni, kwamba ninyi hamtafungwa kuanzia sasa kama ushirika na ndugu zenu wa Sayuni, isipokuwa tu katika hekima hii—

48 Baada ya kuwa mmejipanga, mtakuwa mkiitwa Mpango wa Ushirika wa [a]Kigingi cha Sayuni, katika Mji wa Kirtland. Na ndugu zenu, baada ya kuwa wamejipanga, watakuwa wakiitwa Mpango wa Ushirika wa Mji wa Sayuni.

49 Na watakuwa wamejipanga katika majina yao wenyewe, na katika majina yao wenyewe; nao watakuwa wakifanya shughuli zao katika jina lao wenyewe, na katika majina yao wenyewe;

50 Nanyi mtafanya shughuli zenu katika jina lenu wenyewe, na katika majina yenu wenyewe.

51 Na hii nimeamuru lifanyike kwa ajili ya wokovu wenu, na pia kwa ajili ya wokovu wao,

39*a* MWM Whitney, Newel K.
41*a* M&M 84:112–113.
45*a* M&M 90:20. MWM Smith, Joseph, Mkubwa.
48*a* M&M 82:13; 94:1; 109:59. MWM Kigingi.

kama matokeo ya [a]kufukuzwa kwao na lile linalokuja.

52 Kuvunjwa kwa [a]maagano kwa njia ya uvunjaji wa sheria, kwa [b]tamaa mbaya na maneno ya kutunga—

53 Kwa hiyo, mmevunjwa kama mpango wa ushirika pamoja na ndugu zenu, kwamba hamjafungwa nao hadi hivi sasa tu, ni katika njia hii tu, kama nilivyosema, kwa mkopo kama itakavyokubalika na ushirika huu katika baraza, kama hali yenu itakavyoruhusu na sauti ya baraza itakavyoelekeza.

54 Na tena, amri ninaitoa kwenu juu ya usimamizi ambao nimewachagulia.

55 Tazama, mali hizo zote ni mali yangu, au vinginevyo imani yenu ni bure, nanyi mtaonekana kuwa ni wanafiki, na maagano mliyoyafanya kwangu yamevunjika;

56 Na kama mali hizo ni zangu, hivyo basi ninyi ni [a]wasimamizi; vinginevyo ninyi si wasimamizi.

57 Lakini, amini ninawaambia, nimewateua ninyi kuwa wasimamizi juu ya nyumba yangu, hata wasimamizi wa kweli.

58 Na kwa dhumuni hili nimewaamuru kujipanga wenyewe, hata kwa kuchapa [a]maneno yangu, utimilifu wa maandiko yangu, mafunuo ambayo nimeyatoa kwenu ninyi, na ambayo nitayatoa, baadaye, kwa nyakati tofauti nitayatoa kwenu—

59 Kwa dhumuni la kulijenga kanisa na ufalme wangu juu ya dunia, na kuwaandaa watu wangu kwa ajili ya [a]wakati nitakapokuja [b]kukaa pamoja nao, wakati ambao u karibu.

60 Na mtajitayarishia wenyewe mahali kwa ajili ya hazina, na kupaweka wakfu kwa jina langu.

61 Na mtateua mmoja miongoni mwenu kuitunza hazina hiyo, naye atawazwe kwa baraka hii.

62 Na pawepo lakiri juu ya hazina, na vitu vyote vitakatifu vitawekwa katika hazina; na hakuna mtu miongoni mwenu atakayeiita mali yake mwenyewe, au sehemu yoyote ya hazina hiyo, kwa kuwa itakuwa ni mali yenu ninyi nyote kwa pamoja.

63 Na ninaitoa kwenu ninyi kutoka hivi sasa; na sasa angalieni, kwamba mnaenda na kufanya matumizi ya usimamizi wenu ambao nimewachagulia, isipokuwa kwa mambo matakatifu, kwa ajili ya dhumuni la uchapishaji wa mambo haya matakatifu kama nilivyosema.

64 Na [a]mapato yatokanayo na mambo haya matakatifu yawekwe katika hazina, na lakiri iwe juu yake; na haitatumika au kutolewa nje ya hazina na yeyote, wala lakiri yake itakayowekwa juu yake isilegezwe, isipokuwa tu kwa sauti ya ushirika, au kwa amri.

51 *a* M&M 109:47.
52 *a* MWM Agano.
b MWM Tamani.
56 *a* MWM Msimamizi, Usimamizi.
58 *a* MWM Tafsiri ya Joseph Smith (TJS).
59 *a* MWM Milenia.
b M&M 1:35–36; 29:9–11.
64 *a* MY faida, au mapato.

65 Na hivyo ndivyo mtavyotunza mapato ya mambo matakatifu katika hazina, kwa ajili ya madhumuni yaliyo matakatifu.

66 Na hii itaitwa hazina takatifu ya Bwana; na lakiri itawekwa juu yake ili iweze kuwa takatifu na kuwekwa wakfu kwa Bwana.

67 Na tena, itatayarishwa hazina nyingine, na mtunza hazina ateuliwe wa kutunza hazina, na lakiri itawekwa juu yake;

68 Na fedha zote ambazo mnazipokea katika usimamizi wenu, kwa kuboresha mali ambazo nimewakabidhi, katika majumba, au katika ardhi, au katika ng'ombe, au katika vitu vyote isipokuwa katika maandiko matakatifu na yaliyo ya Mungu, ambayo nimeyaacha kwangu mimi mwenyewe kwa ajili ya madhumuni yaliyo matakatifu, zitawekwa ndani ya hazina haraka mara upokeapo fedha hizo, kwa mamia, au kwa hamsini hamsini, au kwa ishirini ishirini, au kwa makumi, au kwa tano tano.

69 Au katika maneno mengine, kama mtu yeyote miongoni mwenu anapata dola tano na acheni aziweke katika hazina, au kama akipata dola kumi, au ishirini, au hamsini, au mia moja, acha afanye vivyo hivyo;

70 Na acheni pasiwe na yeyote miongoni mwenu atakayesema kwamba ni yake mwenyewe; kwa kuwa haitaitwa yake, wala hata sehemu yake.

71 Na isitumiwe sehemu yake yoyote, au kuchukuliwa kutoka kwenye hazina, isipokuwa tu kwa sauti na ridhaa ya ushirika.

72 Na hii itakuwa sauti na ridhaa ya ushirika—kwamba mtu yeyote miongoni mwenu atamwambia mtunza hazina: Nina shida ya kitu hiki ili kunisaidia katika usimamizi wangu—

73 Kama itakuwa dola tano, au kama itakuwa dola kumi, au ishirini, au hamsini, au mia, mtunza hazina atampa yeye kiasi ambacho anakihitaji ili kumsaidia katika usimamizi wake—

74 Hadi atakapopatikana kuwa mvunja sheria, na kudhihirika mbele ya baraza la ushirika kwa uwazi kwamba siyo mwaminifu na mtumishi [a]asiye na hekima.

75 Lakini ilimradi yeye yu katika ushirika mkamilifu, na ni mwaminifu na mwenye hekima katika usimamizi wake, hii ndiyo itakuwa ishara yake kwa mtunza hazina ili mtunza hazina asimnyime.

76 Lakini katika hali ya uvunjaji wa sheria, mtunza hazina atawajibika kwa baraza na sauti ya ushirika.

77 Na ikiwa mtunza hazina ataonekana si mwaminifu na si mtumishi mwenye hekima, atawajibika kwa baraza na sauti ya ushirika, naye ataondolewa kutoka nafasi yake, na [a]mwingine atateuliwa badala yake.

78 Na tena, amini ninawaambia, juu ya madeni yenu—tazama, ni mapenzi yangu kuwa [a]mlipe [b]madeni yenu yote.

74*a* Lk. 16:1–12.
77*a* M&M 107:99–100.
78*a* M&M 42:54.
b MWM Deni.

79 Na ni mapenzi yangu kuwa [a]mtajinyenyekeza wenyewe mbele zangu, na kupata baraka hii kwa [b]juhudi yenu na unyenyekevu na sala ya imani.

80 Na kadiri mtakavyokuwa wenye bidii na wanyenyekevu, na kutumia [a]sala ya imani, tazama, nitailainisha mioyo ya wale wadeni wenu, hadi nitakapowaletea njia kwa ajili ya ukombozi wenu.

81 Kwa hiyo andika haraka kwa New York na andika kulingana na kile [a]Roho atachosema; nami nitailainisha mioyo ya wale wanaowadai, ili iweze kuondolewa kutoka akilini mwao mawazo ya kuleta mateso juu yenu.

82 Na kadiri mtakavyokuwa [a]wanyenyekevu na waaminifu na kulilingana jina langu, tazama, nitawapatia [b]ushindi.

83 Ninatoa kwenu ahadi, kwamba mtakombolewa mara moja hii kutoka utumwani mwenu.

84 Kadiri utakavyopata nafasi ya kukopa fedha kwa mamia, au maelfu, hata hadi utakopa mkopo wa kutosha kujikomboa mwenyewe kutoka utumwani, ni nafasi yako.

85 Na kuweka rehani mali ambazo nimeziweka mikononi mwako, mara hii moja, kwa kutoa majina yenu kwa ridhaa ya wote au vinginevyo, kama itakavyoonekana kuwa vyema kwenu ninyi.

86 Ninatoa kwenu nafasi hii, mara hii moja; na tazama, kama utaenda kufanya mambo ambayo nimeyaweka mbele yenu, kulingana na amri zangu, vitu hivi vyote ni vyangu, nanyi ni watumishi wangu, na bwana hatakubali nyumba yake ivunjwe. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 105

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, kando ya Mto Fishing, Missouri, 22 Juni 1834. Chini ya uongozi wa Nabii, Watakatifu kutoka Ohio na maeneo mengine walitembea kwa miguu kwenda Missouri katika msafara ambao baadae ulijulikana kama Kambi ya Sayuni. Madhumuni yao yakiwa ni kuwasindikiza Watakatifu wa Missouri waliofukuzwa warudi katika ardhi yao huko Wilaya ya Jackson. Wamisouri ambao hapo awali waliwatesa Watakatifu waliogopa ulipaji kisasi kutoka kwa Kambi ya Sayuni na kwa kushtukiza wakawahi kuwashambulia Watakatifu wanaoishi katika Wilaya ya Clay, huko Missouri. Baada ya gavana wa Missouri kufuta ahadi yake ya kuwasaidia Watakatifu, Joseph Smith alipokea ufunuo huu.

79 *a* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
b MWM Bidii.

80 *a* Yak. (Bib.) 5:15.

81 *a* MWM Roho Mtakatifu.

82 *a* Lk. 14:11; M&M 67:10.
b M&M 103:36.

1–5, Sayuni itajengwa kulingana na sheria ya selestia; 6–13, Ukombozi wa Sayuni unacheleweshwa kwa kipindi kifupi; 14–19, Bwana atapigana vita vya Sayuni; 20–26, Watakatifu watakuwa wenye hekima na wala wasijivunie matendo makuu wakati wanapokusanyika; 27–30, Ardhi katika Jackson na wilaya zinazopakana nayo lazima inunuliwe; 31–34, Wazee watapokea endaomenti katika nyumba ya Bwana katika Kirtland; 35–37, Watakatifu ambao wameitwa na kuteuliwa watatakaswa; 38–41, Watakatifu watainua bendera ya amani kwa walimwengu.

Amini ninawaambia mliojikusanya pamoja ili mpate kujifunza mapenzi yangu juu ya [a]ukombozi wa watu wangu walioteseka—

2 Tazama, ninawaambia, kama isingekuwa [a]uvunjaji wa sheria wa watu wangu, nikizungumza juu ya kanisa na siyo mtu mmoja mmoja, wangelikuwa wamekwisha kombolewa hata sasa.

3 Lakini tazama, hawajajifunza kuwa watiifu kwa mambo ambayo ninayataka kutoka kwao, bali wamejaa aina zote za uovu, wala [a]hawagawi mali zao, kama iwapasavyo watakatifu, kwa maskini na walioteseka miongoni mwao;

4 Na hawana [a]ushirikiano kulingana na ushirika unaotakiwa kwa sheria ya ufalme wa selestia;

5 Na [a]Sayuni haiwezi kujengwa [b]isipokuwa kwa kanuni ya [c]sheria ya ufalme wa selestia; vinginevyo siwezi kumpokea kwangu.

6 Na watu wangu hawanabudi [a]kurudiwa hadi wajifunze [b]utii, kama ni lazima, kwa mambo ambayo wanateseka.

7 Mimi sisemi juu ya wale walioteuliwa kuwaongoza watu wangu, ambao ni wazee wa [a]kwanza wa kanisa langu, kwani siyo wote walio chini ya hatia hii;

8 Bali ninazungumzia juu ya makanisa yangu yaliyoko ng'ambo—wako wengi watakaosema: Mungu wao yuko wapi? Tazama, atawaokoa katika wakati wa taabu, vinginevyo hatutakwenda Sayuni, na tutazishikilia fedha zetu.

9 Kwa hiyo, kwa sababu ya [a]uvunjaji wa sheria wa watu wangu, ni muhimu kwangu kwamba wazee wangu lazima wasubiri kwa kipindi kifupi kwa ajili ya ukombozi wa Sayuni—

10 Ili wao wenyewe wapate kujitayarisha, na ili watu wangu wapate kufundishwa kiukamilifu zaidi, na kupata uzoefu, na kujua kiukamilifu [a]wajibu wao, na mambo niyatakayo kutoka kwao.

11 Na hii haiwezi kutimia

105 1*a* M&M 100:13.
2*a* M&M 104:4–5, 52.
3*a* Mdo. 5:1–11; M&M 42:30. mwm Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.
4*a* M&M 78:3–7.
5*a* mwm Sayuni.
b M&M 104:15–16.
c M&M 88:22.
6*a* M&M 95:1–2. mwm Rudi, Kurudiwa.
b mwm Mtiifu, Tii, Utii.
7*a* M&M 20:2–3.
9*a* M&M 103:4.
10*a* mwm Wajibu.

hadi [a]wazee wangu wamepewa [b]endaomenti kutoka juu.

12 Kwani tazama, nimetayarisha endaomenti kubwa na baraka [a]zitakazomwagwa juu yao, kadiri watakavyokuwa waaminifu na kuendelea katika unyenyekevu mbele zangu.

13 Kwa hiyo ni muhimu kwangu kwamba wazee wangu lazima wasubiri kwa kipindi kifupi, kwa ajili ya ukombozi wa Sayuni.

14 Kwani tazama, sihitaji kutoka kwao kupigana vita vya Sayuni; kama nilivyosema katika amri ya zamani, hata hivyo, nitatimiza—[a]nitapigana vita vyenu.

15 Tazama, [a]mwangamizi nimemtuma kuangamiza na kuwaharibu adui zangu; na siyo miaka mingi kutoka sasa hawataachwa kuuchafua urithi wangu, na [b]kulidharau jina langu juu ya nchi ambayo nimeiweka [c]wakfu kwa ajili ya kukusanywa pamoja kwa watakatifu wangu.

16 Tazama, nimemwamuru mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, kusema na [a]nguvu ya nyumba yangu, hata mashujaa wangu, vijana wangu, na walio wa umri wa kati, kujikusanya pamoja kwa ajili ya ukombozi wa watu wangu, na kuitupa chini minara ya adui zangu, na kuwatawanya [b]walinzi wao;

17 Lakini nguvu za nyumba yangu haijatii maneno yangu.

18 Lakini ilimradi wapo wale ambao wameyatii maneno yangu, nimewatayarishia baraka na [a]endaomenti, kama wataendelea kuwa waaminifu.

19 Nimezisikia sala zao, na nitayapokea matoleo yao; na ni muhimu kwangu kwamba lazima wafikishwe mbali hivyo kwa ajili ya kujaribiwa kwa [a]imani yao.

20 Na sasa, amini ninawaambia, amri ninaitoa kwenu, kwamba kama vile wengi walivyokuja hapa, ambao wanaweza kukaa katika maeneo ya jirani, acheni wakae;

21 Na wale wasioweza kukaa, ambao wanazo familia huko mashariki, acheni wakae kwa kipindi kifupi, kadiri mtumishi wangu Joseph Smith atakavyowapangia;

22 Kwani nitamshauri juu ya jambo hili, na mambo yote yale atakayowapangia yatatimizwa.

23 Na acheni watu wangu wote wakaao katika maeneo ya jirani wawe waaminifu sana, na wenye kuomba, na wanyenyekevu mbele zangu, na wasifichue mambo ambayo nimewafunulia wao, hadi itakapokuwa hekima kwangu kwamba wayafichue.

24 Msizungumzie hukumu, wala [a]msijivunie imani wala matendo makuu, bali kusanyikeni

11 *a* MWM Mzee.
b M&M 38:32; 95:8. MWM Endaomenti.
12 *a* M&M 110.
14 *a* Yos. 10:12–14; Isa. 49:25; M&M 98:37.
15 *a* M&M 1:13–14.
b M&M 112:24–26. MWM Kukufuru, Kufuru.
c M&M 84:3–4; 103:35.
16 *a* M&M 101:55; 103:22, 30.
b MWM Kesha, Walinzi.
18 *a* M&M 110:8–10.
19 *a* MWM Amini, Imani.
24 *a* M&M 84:73. MWM Kiburi.

pamoja kwa uangalifu, iwezekanavyo katika eneo moja kadiri itakavyokubalika katika hisia za watu;

25 Na tazama, nitakupeni ninyi fadhili na neema machoni mwao, ili mpate kupumzika katika [a]amani na usalama, wakati mkisema kwa watu hawa: Tufanyieni hukumu na haki kwa ajili yetu kulingana na sheria, na tufidieni kwa mabaya mliyotutendea.

26 Sasa, tazama, ninawaambia, marafiki zangu, kwa njia hii muweze kupata fadhili machoni mwa watu hawa, hadi [a]jeshi la Israeli litakapokuwa kubwa sana.

27 Nami nitailainisha mioyo ya watu hawa, kama nilivyoufanya moyo wa [a]Farao, mara kwa mara, hadi mtumishi wangu Joseph Smith, Mdogo, na wazee wangu, ambao nimewateua, wapate muda wa kuikusanya nguvu ya nyumba yangu,

28 Na kuwatuma watu wenye [a]hekima, kukamilisha yale niliyoamuru juu ya [b]kununua ardhi yote katika wilaya ya Jackson ile iwezekanayo kununuliwa, na katika wilaya zilizopo karibu.

29 Kwani ni mapenzi yangu kwamba ardhi hizi zapaswa kununuliwa; na baada ya kununuliwa kwamba watakatifu wangu wazimiliki kulingana na [a]sheria za uwekaji wakfu ambazo nimewapatia.

30 Na baada ya ardhi hizi kununuliwa, nitayaona [a]majeshi ya Israeli kuwa hayana hatia katika kumiliki ardhi iliyo yao wenyewe, ambayo awali walinunua kwa fedha yao, na kuiangusha chini minara ya adui zangu ambayo yaweza kuwa juu yao, na kuwatawanya walinzi wao, na [b]kunipatia haki mimi na adui zangu hata kwa kizazi cha tatu na cha nne cha wale wanichukiao.

31 Lakini kwanza acheni jeshi langu liwe kubwa sana, na acheni [a]litakaswe mbele yangu, ili lipate kuwa zuri kama jua, na safi kama [b]mwezi, na kwamba bendera zake ziwe za kutisha kwa mataifa yote;

32 Ili falme za ulimwengu huu zipate kulazimishwa kutambua kwamba ufalme wa Sayuni hakika ni [a]ufalme wa Mungu wetu na Kristo wake, kwa hiyo, na [b]tujiweke chini ya sheria zake.

33 Amini ninawaambia, ni muhimu kwangu kwamba wazee wa kwanza wa kanisa langu wapokee [a]endaomenti kutoka juu katika nyumba yangu, ambayo nimeamuru ijengwe katika jina langu katika nchi ya Kirtland.

34 Na amri zile ambazo nime-

25*a* MWM Amani.
26*a* Yoe. 2:11.
27*a* Mwa. 47:1–12.
28*a* M&M 101:73.
b M&M 42:35–36.
29*a* M&M 42:30. MWM Mpango wa Ushirika; Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.
30*a* M&M 35:13–14; 101:55; 103:22, 26.
b M&M 97:22.
31*a* MWM Utakaso.
b Wim. 6:10; M&M 5:14; 109:73.
32*a* Ufu. 11:15. MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
b MWM Utawala.
33*a* M&M 95:8–9. MWM Endaomenti.

wapa juu ya Sayuni na [a]sheria yake zitelekezwe na kutimizwa, baada ya ukombozi wake.

35 Palikuwa na siku ya [a]kuitwa, lakini wakati umefika wa siku ya kuteua; na acha wale watakaoteuliwa wawe wenye [b]kustahili.

36 Na itajulishwa kwa mtumishi wangu, kwa sauti ya Roho, wale [a]walioteuliwa; nao [b]watatakaswa;

37 Na kadiri watakavyofuata [a]ushauri ambao wanaupokea, watakuwa na uwezo baada ya siku nyingi wa kukamilisha mambo yote yahusuyo Sayuni.

38 Na tena ninawaambia, fungueni mashtaka kwa ajili ya amani, siyo tu kwa watu ambao wamewapiga peke yake, bali pia kwa watu wote;

39 Na inueni [a]bendera ya [b]amani, na tengenezeni tangazo la amani hata kwenye miisho ya dunia;

40 Na toeni mapendekezo kwa ajili ya amani kwa wale walio wapiga, kulingana na sauti ya Roho aliye ndani yenu, na mambo [a]yote yatafanya kazi kwa pamoja kwa faida yenu.

41 Kwa hiyo, kuweni waaminifu; na tazama, na lo, [a]Mimi nipo pamoja nanyi hadi mwisho. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 106

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 25 Novemba 1834. Ufunuo huu unaelekezwa kwa Warren A. Cowdery, kaka mkubwa wa Oliver Cowdery.

1–3, Warren A. Cowdery anaitwa kuwa ofisa kiongozi wa eneo analoishi; 4–5, Ujio wa Pili hautawapita watoto wa nuru kama mwizi; 6–8, Baraka kubwa hufuata utumishi wa uaminifu katika Kanisa.

Ni mapenzi yangu kwamba mtumishi wangu Warren A. Cowdery ateuliwe na kutawazwa kuwa kuhani mkuu kiongozi juu ya kanisa langu, katika nchi ya [a]Freedom na maeneo yanayoizunguka;

2 Na ni lazima aihubiri injili yangu isiyo na mwisho, na kupaza sauti yake na kuwaonya watu, siyo tu katika sehemu yake mwenyewe, bali katika wilaya zinazopakana;

3 Na autoe muda wake wote kwa wito huu mtakatifu na wa juu, ambao sasa ninampa,

34 *a* MY M&M 42 inajulikana kama "Sheria."
35 *a* MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito.
b MWM Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki.
36 *a* M&M 95:5.
MWM Alichagua, Chagua, Chaguliwa (kitenzi).
b MWM Utakaso.
37 *a* MWM Ushauri.
39 *a* MWM Bendera.
b MWM Amani.
40 *a* Rum. 8:28; M&M 90:24; 100:15.
41 *a* Mt. 28:19–20.
106 1 *a* MY mji wa Freedom, New York na maeneo yanayoizunguka.

[a]akiutafuta kwa bidii [b]ufalme wa mbinguni na haki zake, na mambo yote ya lazima yataongezwa juu yake; kwani [c]mfanyakazi anastahili ujira wake.

4 Na tena, amini ninawaambia, [a]ujio wa Bwana [b]unakaribia, nao utaupata ulimwengu kama [c]mwivi ajavyo usiku—

5 Kwa hiyo, jifungeni viuno vyenu, ili mpate kuwa watoto wa [a]nuru, na siku ile [b]isiwapate kama mwivi.

6 Na tena, amini ninawaambia, palikuwa na shangwe mbinguni wakati mtumishi wangu Warren aliposujudu kwenye fimbo yangu ya ufalme, na kujitenga na ujanja wa wanadamu;

7 Kwa hiyo, heri mtumishi wangu Warren, kwani nitakuwa na huruma juu yake; na, bila kujali [a]kiburi cha moyoni mwake, nitamwinua juu kadiri yeye atakavyo jinyenyekeza mbele zangu.

8 Nami nitampa [a]neema na uhakika ambao kwayo aweze kusimama; na kama ataendelea kuwa shahidi mwaminifu na nuru kwa kanisa nimeandaa taji kwa ajili yake katika [b]makao ya Baba yangu. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 107

Ufunuo juu ya ukuhani, uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, mnamo Aprili 1835. Ingawa sehemu hii iliandikwa mwaka 1835, kumbu kumbu za kihistoria zinasisitiza kwamba sehemu kubwa za aya ya 60 hadi 100 zinajumuisha ufunuo uliotolewa kupitia kwa Joseph Smith 11 Novemba 1831. Sehemu hii ilihusiana na kuanzishwa kwa Akidi ya Kumi na Wawili katika Februari na Machi 1835. Yaelekea Nabii aliisoma mbele ya wale waliokuwa wakijitayarisha kuondoka 3 Mei 1835, katika misheni yao ya kwanza kama akidi.

1–6, Kuna ukuhani wa aina mbili: wa Melkizedeki na wa Haruni; 7–12, Wale walio na ukuhani wa Melkizedeki wanao uwezo wa kufanya kazi katika ofisi zote katika Kanisa; 13–17, Uaskofu husimamia Ukuhani wa Haruni, ambao huhudumu katika ibada za kimwili; 18–20, Ukuhani wa Melkizedeki hushikilia funguo za baraka zote za kiroho; Ukuhani wa Haruni unashikilia funguo za

3*a* Mt. 6:33.
b MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
c Mt. 10:10; M&M 31:5.
4*a* Yak. (Bib.) 5:8.
b MWM Siku za Mwisho.
c 1 The. 5:2.
5*a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
b Ufu. 16:15.
7*a* MWM Majivuno, Siofaa.
8*a* MWM Neema.
b Yn. 14:2; Eth. 12:32–34; M&M 59:2; 76:111; 81:6; 98:18.

kuhudumiwa na malaika; 21–38, Urais wa Kwanza, Mitume Kumi na Wawili, na Sabini huunda akidi za kuongoza, ambazo maamuzi yake yatafanywa katika umoja na haki; 39–52, Utaratibu wa kipatriaki unaelezwa kutoka Adamu hadi Nuhu; 53–57, Watakatifu wa zamani walikusanyika huko Adamu-ondi-Ahmani, na Bwana akawatokea; 58–67, Mitume Kumi na Wawili watawaweka maofisa wa Kanisa katika mpangilio unaostahili; 68–76, Maaskofu hutumika kama waamuzi wa wote katika Israeli; 77–84, Urais wa Kwanza na Mitume Kumi na Wawili huunda mahakama ya juu katika Kanisa; 85–100, Marais wa Ukuhani hutawala akidi zao husika.

Katika kanisa, zipo aina mbili za Ukuhani, nazo, ni [a]Melkizedeki na [b]Haruni, ukijumuisha na Ukuhani wa Lawi.

2 Kwa nini wa kwanza unaitwa Ukuhani wa [a]Melkizedeki ni kwa sababu Melkizedeki alikuwa kuhani mkubwa sana.

3 Kabla ya siku zake ulikuwa ukiitwa *Ukuhani Mtakatifu, kwa* [a]*Mfano wa Mwana wa Mungu.*

4 Lakini kwa sababu ya heshima au [a]unyenyekevu kwa jina la Kiumbe Mkuu, ili kuepuka kurudiwa mara kwa mara kwa jina lake, wao, kanisa, katika siku za kale, waliuita ukuhani huo Melkizedeki, au Ukuhani wa Melkizedeki.

5 Mamlaka nyingine zote au ofisi zote katika kanisa ni [a]viambatanisho kwenye ukuhani huu.

6 Lakini ziko sehemu kuu au vichwa vikuu viwili—cha kwanza ni ukuhani wa Melkizedeki, na kingine ni Ukuhani wa Haruni au [a]Ukuhani wa Lawi.

7 Ofisi ya [a]mzee huja chini ya ukuhani wa Melkizedeki.

8 Ukuhani wa Melkizedeki unashikilia haki ya Urais, na unao uwezo na [a]mamlaka juu ya ofisi zote katika kanisa katika vipindi vyote vya ulimwengu, kuhudumu katika mambo ya kiroho.

9 [a]Urais wa Ukuhani Mkuu, kwa mfano wa Melkizedeki, unayo haki ya kutenda kazi katika ofisi zote katika kanisa.

10 [a]Makuhani wakuu kwa mfano wa Ukuhani wa Melkizedeki wanayo [b]haki ya kutenda kazi katika nafasi yao wenyewe, chini ya maelekezo ya urais, katika kuhudumu katika mambo ya kiroho, na pia katika ofisi ya mzee, kuhani (wa mfano wa Lawi), mwalimu, shemasi, na muumini.

11 Mzee anayo haki ya kutenda kazi kwa niaba yake wakati kuhani mkuu hayupo.

12 Kuhani mkuu na mzee watahudumu katika mambo ya

107 1*a* mwm Ukuhani wa Melkizedeki.
b mwm Ukuhani wa Haruni.
2*a* tjs Mwa. 14:25–40 (Kiambatisho); M&M 84:14.
mwm Melkizedeki.
3*a* Alma 13:3–19; M&M 76:57.
4*a* mwm Uchaji.
5*a* M&M 84:29; 107:14.
6*a* Kum. 10:8–9.
7*a* mwm Mzee.
8*a* mwm Mamlaka.
9*a* M&M 81:2; 107:22, 65–67, 91–92.
10*a* mwm Kuhani Mkuu.
b M&M 121:34–37.

kiroho, kulingana na maagano na amri za kanisa; na wanayo haki ya kutenda kazi katika ofisi hizi zote za kanisa iwapo hakuna wenye mamlaka ya juu zaidi.

13 Ukuhani wa pili unaitwa [a]Ukuhani wa Haruni, kwa sababu ulitolewa kwa [b]Haruni na uzao wake, katika vizazi vyao vyote.

14 Kwa nini unaitwa ukuhani mdogo ni kwa sababu ni [a]kiambatanisho kwa ule mkubwa, au Ukuhani wa Melkizedeki, na unao uwezo wa kuhudumu katika ibada za nje.

15 [a]Uaskofu ni urais wa ukuhani huu, na unashikilia funguo, au mamlaka hayo.

16 Hakuna mtu aliye na haki kisheria kwenye ofisi hii, kushikilia funguo za ukuhani huu, isipokuwa ni [a]mzaliwa halisi wa ukoo wa Haruni.

17 Lakini kama kuhani mkuu wa Ukuhani wa Melkizedeki anayo mamlaka ya kutenda kazi katika ofisi ndogo zote, anaweza kutenda kazi katika ofisi ya askofu ikiwa hakuna mzaliwa halisi wa ukoo wa Haruni anayeweza kupatikana, ili mradi awe ameitwa na kuwekwa rasmi na [a]kutawazwa katika uwezo huu kwa mikono ya [b]Urais wa Ukuhani wa Melkizedeki.

18 Uwezo na mamlaka ya ule wa juu, au Ukuhani wa Melkizedeki, ni kushikilia [a]funguo za baraka zote za kiroho za kanisa—

19 Kuwa na haki ya kupokea [a]siri za ufalme wa mbinguni, mbingu kufunuliwa kwao, kuwasiliana na baraza [b]kuu na kanisa la Mzaliwa wa Kwanza, na kufurahia ushirikiano wao na uwepo wa Mungu Baba, na Yesu aliye [c]mpatanishi wa agano jipya.

20 Uwezo na mamlaka ya ule mdogo, au Ukuhani wa Haruni, ni kushikilia [a]funguo za huduma ya malaika, na kufanya huduma ya [b]ibada za kimwili, andiko la injili, [c]ubatizo wa toba kwa [d]ondoleo la dhambi, sawa sawa na maagano na amri.

21 Kuna umuhimu wa kuwepo kwa marais, au maofisa viongozi kutoka, au kuteuliwa au kutoka miongoni mwa wale ambao wametawazwa kwenye ofisi mbali mbali katika aina hizi mbili za ukuhani.

22 Wa [a]Ukuhani wa Melkizedeki, [b]Makuhani Wakuu Viongozi watatu, waliochaguliwa na kikundi, kuteuliwa na kutawazwa katika ofisi hiyo, na [c]kuungwa mkono wa kuaminiwa, imani, na sala ya kanisa, hufanya akidi ya Urais wa Kanisa.

13*a* MWM Ukuhani wa Haruni.
b MWM Haruni, Kaka wa Musa.
14*a* M&M 20:52; 107:5.
15*a* MWM Askofu.
16*a* M&M 68:14–21; 107:68–76.
17*a* MWM Kutawaza, Kutawazwa.
b M&M 68:15.
18*a* MWM Funguo za Ukuhani.
19*a* Alma 12:9–11; M&M 63:23; 84:19–22. MWM Siri za Mungu.
b Ebr. 12:22–24.
c MWM Mpatanishi.
20*a* M&M 13; 84:26–27.
b MWM Ibada.
c MWM Batiza, Ubatizo.
d MWM Ondoleo la Dhambi.
22*a* MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
b M&M 90:3, 6; 107:9, 65–67, 78–84, 91–92.
c MWM Kuwakubali Viongozi wa Kanisa.

23 Wajumbe [a]kumi na wawili wasafirio huitwa kuwa [b]Mitume Kumi na Wawili, au mashahidi maalumu wa jina la Kristo ulimwenguni kote—hivyo kuwa tofauti na maofisa wengine katika kanisa katika majukumu ya wito wao.

24 Nao hufanya akidi, sawa sawa katika mamlaka na uwezo na marais wale watatu waliotajwa awali.

25 [a]Sabini pia huitwa kuihubiri injili, na kuwa mashahidi maalumu kwa Wayunani na ulimwenguni kote—hivyo kuwa tofauti na maofisa wengine katika kanisa katika majukumu ya wito wao.

26 Nao wanafanya akidi, sawa sawa katika mamlaka na ile ya mashahidi maalumu Kumi na Wawili au Mitume ambao tumewataja sasa hivi.

27 Na kila uamuzi unaofanywa na akidi yoyote kati ya hizi lazima uwe kwa kura ya wengi wao, maana yake, kila mshiriki katika kila akidi, lazima akubaliane na maamuzi yake, ili kufanya maamuzi yao yawe na uwezo sawa au yawe na uhalali, yakubalike kwa kila mmoja—

28 Wengi wanaweza kuunda akidi ikiwa hali inafanya kutowezekana kuwa vinginevyo—

29 Kama si hivyo, maamuzi yao hayastahili baraka hizo ambazo maamuzi ya akidi ya marais watatu waliyatoa hapo awali, ambao walitawazwa kwa mfano wa Melkizedeki, na walikuwa watu wema na watakatifu.

30 Maamuzi ya akidi hizi, au mojawapo, yanapaswa kufanywa katika [a]haki tupu, katika utakatifu, na kwa unyenyekevu wa moyo, kwa upole, na kwa uvumilivu, na katika imani, na [b]wema, na maarifa, kiasi, saburi, uchamungu, upendo wa kidugu na hisani;

31 Kwa sababu ahadi ni, kama mambo haya yamejaa tele kwao hawatakuwa watu wasio na [a]matunda katika maarifa ya Bwana.

32 Na ikiwa uamuzi wowote wa akidi hizi umefanywa pasipo haki, unaweza kuletwa mbele ya mkutano mkuu wa akidi hizi kadhaa, ambazo zinaundwa na wenye mamlaka za kiroho za kanisa; vinginevyo hapawezi kuwa na rufaa yoyote kutoka kwenye uamuzi wao.

33 Hawa Kumi na Wawili ndiyo Baraza Kuu la Viongozi Wasafirio, ili kutenda kazi katika jina la Bwana, chini ya maelekezo ya Urais wa Kanisa, kulingana na sheria za mbinguni; ili kulijenga kanisa, na kurekebisha masuala yote yalihusuyo katika mataifa yote, kwanza kwa [a]Wayunani na pili kwa Wayahudi.

34 Sabini watatenda kazi katika jina la Bwana, chini ya maelekezo ya [a]Kumi na Wawili au

23 *a* M&M 107:33–35.
b MWM Mtume.
25 *a* MWM Sabini.
30 *a* M&M 121:36.
MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
b M&M 121:41.
MWM Wema.
31 *a* 2 Pet. 1:5–8.
33 *a* 1 Ne. 13:42; 3 Ne. 16:4–13; M&M 90:8–9.
34 *a* M&M 112:21.

baraza kuu lenye kusafiri, katika kulijenga kanisa na kurekebisha mambo yote yalihusuyo katika mataifa yote, kwanza kwa Wayunani na halafu kwa Wayahudi—

35 Kumi na Wawili wakiwa wametumwa nje, wakiwa na funguo, kufungua mlango kwa utangazaji wa injili ya Yesu Kristo, na kwanza kwa Wayunani na halafu kwa Wayahudi.

36 [a]Baraza kuu la kudumu, katika vigingi vya Sayuni, huunda akidi iliyo sawa katika mamlaka katika mambo ya kanisa, katika maamuzi yao yote, na akidi ya urais, au baraza kuu lisafirilo.

37 Baraza kuu katika Sayuni huunda akidi yenye mamlaka sawa katika mambo ya kanisa, katika maamuzi yao yote, na mabaraza ya Kumi na Wawili katika vigingi vya Sayuni.

38 Ni kazi ya baraza kuu lenye kusafiri kuwaita hawa [a]Sabini, wakati wanapohitaji msaada wa kujaza nafasi za miito mbalimbali kwa ajili ya kuhubiri na kusimamia injili, badala ya mwingine yeyote.

39 Ni wajibu wa Kumi na Wawili, katika matawi makubwa yote ya kanisa, kuwatawaza wahudumu [a]wainjilisti, kulingana na wao watakavyo julishwa kwa ufunuo—

40 Mfano wa ukuhani huu ulithibitishwa kutolewa kutoka baba kwenda kwa mwana, na kisheria ni mali ya wazao halisi wa uzao mteule, ambao kwao ahadi zilifanywa.

41 Mfano huu ulianzishwa katika siku za [a]Adamu, na ulikuja chini kwa [b]kurithi katika namna ifuatayo:

42 Kutoka Adamu hadi [a]Sethi, ambaye alitawazwa na Adamu akiwa na umri wa miaka sitini na tisa, na alibarikiwa naye miaka mitatu kabla ya kifo chake (cha Adamu), na kupokea ahadi ya Mungu kupitia baba yake, kwamba uzao wake watakuwa wateule wa Bwana, na kwamba kitahifadhiwa hadi mwisho wa dunia;

43 Kwa sababu yeye (Sethi) alikuwa mtu [a]mkamilifu, na [b]ufanano wake ulikuwa mfano halisi wa baba yake, kiasi kwamba alikuwa akionekana kama baba yake katika mambo yote, na aliweza kutofautiana naye tu kwa umri wake.

44 Enoshi alitawazwa katika umri wa miaka mia moja na thelathini na nne na miezi minne, kwa mkono wa Adamu.

45 Mungu akamtokea Kenani nyikani katika mwaka wa arobaini wa umri wake; naye alikutana na Adamu akisafiri kwenda mahali paitwapo Shedolamak. Alikuwa na miaka themanini na saba wakati alipopata kutawazwa.

46 Mahalaleli alikuwa na umri wa miaka mia nne na tisini na sita na siku saba wakati

36 *a* MWM Baraza Kuu.
38 *a* MWM Sabini.
39 *a* MWM Kipatriaki, Patriaki; Mwinjilisti.
41 *a* MWM Adamu.
b Mwa. 5; M&M 84:6–16; Musa 6:10–25.
42 *a* MWM Seti.
43 *a* MWM Kamilifu.
b Mwa. 5:3.

alipotawazwa kwa mkono wa Adamu, ambaye pia alimbariki.

47 Yaredi alikuwa na umri wa miaka mia mbili wakati alipotawazwa chini ya mkono wa Adamu, ambaye pia alimbariki.

48 [a]Henoko alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano wakati alipotawazwa chini ya mkono wa Adamu; na alikuwa na miaka sitini na tano Adamu alipombariki.

49 Na yeye alimwona Bwana, na alitembea pamoja naye, na daima alikuwa mbele ya uso wake; na [a]alitembea pamoja na Mungu miaka mia tatu na sitini na mitano, ikimfanya kuwa na umri wa miaka mia nne na thelathini wakati [b]alipohamishwa.

50 [a]Methusela alikuwa na umri wa miaka mia moja wakati alipotawazwa chini ya mkono wa Adamu.

51 Lameki alikuwa na umri wa miaka thelathini na mbili wakati alipotawazwa chini ya mkono wa Sethi.

52 [a]Nuhu alikuwa na umri wa miaka kumi wakati alipotawazwa chini ya mkono wa Methusela.

53 Miaka mitatu kabla ya kifo cha Adamu, alimwita Sethi, Enoshi, Kenani, Mahalaleli, Yaredi, Henoko, na Methusela, ambao wote walikuwa [a]makuhani wakuu, pamoja na mabaki ya uzao wake waliokuwa wenye haki, katika bonde la [b]Adamu-ondi-Amani, na huko akawawekea juu yao baraka zake za mwisho.

54 Na Bwana akawatokea, nao wakainuka na kumbariki [a]Adamu, na wakamwita [b]Mikaeli, mtawala, malaika mkuu.

55 Na Bwana akamfariji Adamu, na akamwambia: Nimekuweka wewe kuwa kiongozi; wingi wa mataifa utatoka kwako, na wewe utakuwa [a]mtawala juu yao milele.

56 Na Adamu alisimama katikati ya makutano; na, licha ya kuwa alikuwa amepinda mgongo kwa sababu ya uzee, akiwa amejawa na Roho Mtakatifu, [a]alitabiri yale yote yatakayoupata uzao wake hata kizazi cha mwisho.

57 Mambo haya yote yaliandikwa katika kitabu cha Henoko, nayo yatashuhudiwa kwa wakati wake.

58 Ni kazi ya [a]Mitume Kumi na Wawili, pia, [b]kuwatawaza na kuwapanga viongozi wengine wote wa kanisa, sawa sawa na ufunuo usemao:

59 Kwa kanisa la Kristo katika nchi ya Sayuni, katika nyongeza kwa [a]sheria za kanisa kuhusu shughuli za kanisa—

60 Amini, ninawaambia, asema Bwana wa Majeshi, hapana budi kuwepo na [a]wazee vio-

48*a* MWM Henoko.
49*a* Mwa. 5:22; Ebr. 11:5; Musa 7:69.
b MWM Viumbe waliobadilishwa.
50*a* MWM Methusela.
52*a* MWM Nuhu, Patriaki wa Biblia.
53*a* MWM Kuhani Mkuu.
b M&M 78:15; 116. MWM Adamu-ondi-Amani.
54*a* M&M 128:21. MWM Adamu.
b MWM Mikaeli.
55*a* M&M 78:16.
56*a* Musa 5:10.
58*a* MWM Mtume.
b MWM Kutawaza, Kutawazwa.
59*a* M&M 43:2–9.
60*a* M&M 107:89–90.

ngozi wa kuongoza juu ya wale walio katika ofisi ya mzee;

61 Na pia [a]makuhani kuongoza juu ya wale walio katika ofisi ya kuhani;

62 Na pia walimu [a]kuongoza juu ya wale walio katika ofisi ya mwalimu, vile vile, na pia mashemasi—

63 Kwa hiyo, kutoka shemasi hadi mwalimu, na kutoka mwalimu hadi kuhani, na kutoka kuhani hadi mzee, kila mmoja kama wanavyoteuliwa, kulingana na maagano na amri za kanisa.

64 Halafu unakuja Ukuhani Mkuu, ambao ni mkubwa kuliko wote.

65 Kwa hiyo, ni muhimu kwamba mtu mmoja wa Ukuhani Mkuu ateuliwe kuusimamia Ukuhani, naye ataitwa Rais wa Ukuhani Mkuu wa Kanisa;

66 Au, katika maneno mengine, Kuhani Mkuu [a]Kiongozi wa Ukuhani Mkuu wa Kanisa.

67 Kutoka kwa huyo kunakuja kusimamia ibada na baraka juu ya kanisa, kwa [a]kuwekea mikono.

68 Kwa hiyo, ofisi ya askofu siyo sawa na hii; kwani [a]ofisi ya askofu ni ya kusimamia mambo yote ya kimwili;

69 Hata hivyo, askofu lazima achaguliwe kutoka kwenye [a]Ukuhani Mkuu, isipokuwa ni wa [b]uzao halisi wa Haruni;

70 Kwani kama yeye siyo wa uzao halisi wa Haruni hawezi kushikilia funguo za ukuhani huo.

71 Hata hivyo, kuhani mkuu, ambaye, ni kwa mfano wa Melkizedeki, anaweza kuwekwa rasmi kwa ajili ya kusimamia mambo ya kimwili, akiwa mwenye maarifa juu yake kwa njia ya Roho wa kweli;

72 Na pia kuwa [a]mwamuzi katika Israeli, kufanya shughuli za kanisa, kukaa katika hukumu juu ya wavunja sheria kulingana na ushuhuda kama utakavyo wekwa mbele yake kulingana na sheria, kwa msaada wa washauri wake, ambao amewachagua au atakao wachagua miongoni mwa wazee wa kanisa.

73 Hii ni kazi ya askofu ambaye siyo wa uzao halisi wa Haruni, bali ametawazwa kwenye Ukuhani huu Mkuu kwa mfano wa Melkizedeki.

74 Hivyo ndivyo atakuwa mwamuzi, hata mwamuzi wa wote miongoni mwa wakazi wa Sayuni, au katika vigingi vya Sayuni, au katika tawi lolote la kanisa ambapo atawekwa rasmi kwa huduma hii, hadi mipaka ya Sayuni ipanuliwe na ni muhimu kuwa na maaskofu au waamuzi wengine katika Sayuni au popote kwingineko.

75 Na ilimradi kuna maaskofu wengine walioteuliwa nao watafanya kazi katika ofisi hiyo hiyo.

76 Lakini mzaliwa halisi wa uzao wa Haruni anayo haki ya

61 *a* M&M 107:87.
62 *a* M&M 107:85–86.
66 *a* M&M 107:9, 91–92. MWM Rais.
67 *a* MWM Mikono, Kuweka juu ya.
68 *a* MWM Askofu.
69 *a* MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
b M&M 68:14–24; 84:18; 107:13–17.
72 *a* M&M 58:17–18.

urais wa ukuhani huu, haki ya [a]funguo za huduma hii, kutenda kazi katika ofisi ya askofu pekee yake, bila washauri, isipokuwa katika shauri ambalo Rais wa Ukuhani Mkuu, kwa mfano wa Melkizedeki, anashtakiwa, kuwa kama mwamuzi katika Israeli.

77 Na uamuzi wa baraza lolote kati ya haya, ukubaliane na amri isemayo:

78 Tena, amini, ninawaambia, shughuli ya kanisa iliyo muhimu zaidi, na mashauri ya kanisa, yaliyo [a]magumu zaidi, kama hakuna kuridhika juu ya uamuzi wa askofu au waamuzi, yakabidhiwe na yapelekwe kwa baraza la kanisa, mbele ya [b]Urais wa Ukuhani Mkuu.

79 Na Urais wa baraza la Ukuhani Mkuu utakuwa na uwezo wa kuwaita makuhani wakuu wengine, hata kumi na wawili, kusaidia kama washauri; na hivyo Urais wa Ukuhani Mkuu na washauri wake watakuwa na uwezo wa kuamua juu ya ushuhuda kulingana na sheria za kanisa.

80 Na baada ya uamuzi huu lisiletwe tena kwenye kumbukumbu mbele ya Bwana; kwani hili ndilo baraza la juu kabisa la kanisa la Mungu, na ni uamuzi wa mwisho juu ya mabishano katika mambo ya kiroho.

81 Hakuna mtu yeyote aliye wa kanisa ambaye hahukumiwi na baraza hili la kanisa.

82 Na kadiri Rais wa Ukuhani Mkuu atakavyovunja sheria, ataletwa mbele ya baraza kuu la kanisa, ambalo litasaidiwa na washauri kumi na wawili wa Ukuhani Mkuu;

83 Na uamuzi wao juu ya kichwa chake utakuwa ndiyo mwisho wa mabishano juu yake.

84 Hivyo, hakuna atakaye samehewa kutokana na [a]haki na sheria za Mungu, ili mambo yote yapate kufanyika katika utaratibu na katika ibada mbele zake, kulingana na kweli na haki.

85 Na tena, amini ninawaambia, kazi ya rais wa ofisi ya [a]shemasi ni kuwaongoza mashemasi kumi na wawili, kukaa katika baraza pamoja nao, na [b]kuwafundisha wajibu wao, wakijengana wao kwa wao, kama ilivyotolewa kulingana na maagano.

86 Na pia kazi ya rais juu ya ofisi ya [a]walimu ni kuwaongoza walimu ishirini na wanne, na kukaa katika baraza pamoja nao, kuwafundisha wajibu wa ofisi zao, kama ulivyotolewa katika maagano.

87 Pia kazi ya rais juu ya Ukuhani wa Haruni ni kuwaongoza [a]makuhani arobaini na wanane, na kukaa katika baraza pamoja nao, kuwafundisha wajibu wa ofisi zao, kama ulivyotolewa katika maagano—

88 Rais huyu anapaswa kuwa [a]askofu; kwani hii ni mojawapo ya kazi za ukuhani huu.

76*a* MWM Funguo za Ukuhani.
78*a* M&M 102:13, 28.
b M&M 68:22.
84*a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
85*a* MWM Shemasi.
b M&M 38:23; 88:77–79, 118.
86*a* M&M 20:53–60. MWM Mwalimu, Ukuhani wa Haruni.
87*a* MWM Kuhani, Ukuhani wa Haruni.
88*a* MWM Askofu.

89 Tena, kazi ya rais juu ya ofisi ya [a]wazee ni kuwaongoza wazee tisini na sita, na kukaa katika baraza pamoja nao, na kuwafundisha kulingana na maagano.

90 Urais huu ni tofauti na ule wa sabini, na umedhamiriwa kwa wale ambao [a]hawasafiri ulimwenguni kote.

91 Na tena, kazi ya Rais wa ofisi ya Ukuhani Mkuu ni [a]kuliongoza kanisa lote, na kuwa kama [b]Musa—

92 Tazama, hii ndiyo hekima; ndiyo, kuwa [a]mwonaji, [b]mfunuzi, mfasiri, na [c]nabii, akiwa na [d]vipawa vyote vya Mungu ambavyo huviweka juu ya kiongozi wa kanisa.

93 Na ni kulingana na ono lionyeshalo mpangilio wa [a]Sabini, kwamba wanapaswa kuwa na marais saba wakiwaongoza, walioteuliwa kutoka katika idadi ya hao sabini;

94 Na rais wa saba kati ya marais hawa atawaongoza sita;

95 Na marais hawa saba watawachagua sabini wengine licha ya sabini wa kwanza ambao humo nao wanatoka, na watawaongoza hao;

96 Na pia sabini wengine, hadi saba mara sabini, kama kazi katika shamba la mizabibu litahitaji hivyo.

97 Na hawa sabini watakuwa [a]wahudumu wa kusafiri, kwa Wayunani kwanza na pia kwa Wayahudi.

98 Kinyume chake maofisa wengine wa kanisa, ambao siyo wale Kumi na Wawili, wala Sabini, hawako chini ya wajibu wa kusafiri miongoni mwa mataifa yote, ila watasafiri kadiri hali zao zitakavyowaruhusu, licha ya kwamba wanaweza kuwa wanashikilia nafasi ya juu na ofisi zenye wajibu mkubwa katika kanisa.

99 Kwa sababu hiyo, sasa acha kila mtu na ajifunze [a]wajibu wake, na kutenda kazi katika ofisi ambayo ameteuliwa, kwa [b]bidii yote.

100 Yule aliye [a]mvivu hatahesabika kuwa mwenye [b]kustahili kusimama, na yule asiye jifunza wajibu wake na asiyeweza kujithibitisha yeye mwenyewe hatahesabika kuwa mwenye kustahili kusimama. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 108

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Kirtland, Ohio, 26 Desemba 1835. Sehemu hii ilipokelewa kwa ombi la Lyman

89 *a* MWM Mzee.
90 *a* M&M 124:137.
91 *a* M&M 107:9, 65–67.
b M&M 28:2; 103:16–21.
92 *a* Mos. 8:13–18.
MWM Mwonaji.
b MWM Ufunuo.
c M&M 21:1.
MWM Nabii.
d MWM Vipawa vya Roho.
93 *a* M&M 107:38.
MWM Sabini.
97 *a* M&M 124:138–139.
99 *a* MWM Wajibu.
b MWM Bidii.
100 *a* M&M 58:26–29.
MWM Mvivu, Uvivu.
b MWM Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki.

Sherman, ambaye mwanzoni alikuwa ametawazwa kama sabini, na ambaye alikuja kwa Nabii akiwa na ombi la ufunuo wa kujulishwa wajibu wake.

1–3, Lyman Sherman asamehewa dhambi zake; 4–5, Ahesabiwe pamoja na wazee viongozi wa Kanisa; 6–8, Yeye ameitwa kuihubiri injili na kuwaimarisha ndugu zake.

Amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwako, mtumishi wangu Lyman: Dhambi zako zimesamehewa, kwa sababu umetii sauti yangu kwa kuja hapa asubuhi hii kupokea ushauri wake yeye niliyemteua.

2 Kwa hiyo, nafsi yako na [a]itulie juu ya msimamo wako wa kiroho, na usiikatae tena sauti yangu.

3 Na amka na uwe mwangalifu zaidi kutoka sasa katika kutimiza nadhiri zako, ambazo umezifanya na unazozifanya, nawe utabarikiwa kwa baraka kubwa kupita kiasi.

4 Subiri kwa uvumilivu hadi [a]kusanyiko la kiroho litakapoitishwa la watumishi wangu, ndipo nawe utakumbukwa pamoja na wazee wangu wa kwanza, na kupokea haki kwa kutawazwa na wazee wangu wengine wote ambao nimewateua.

5 Tazama, hii ni [a]ahadi ya Baba kwako kama utaendelea kuwa mwaminifu.

6 Nayo itatimizwa juu yako katika siku ile ili uwe na haki ya [a]kuhubiri injili yangu popote nitakapokutuma, kutoka hapo na kutoka wakati huo.

7 Kwa hiyo, [a]waimarishe ndugu zako katika mazungumzo yako yote, katika sala zako zote, katika kushawishi kwako kote, na katika matendo yako yote.

8 Na tazama, na lo, Mimi ni pamoja nawe ili kukubariki na [a]kukuokoa wewe milele. Amina.

SEHEMU YA 109

Sala iliyotolewa wakati wa kuwekwa wakfu kwa hekalu huko Kirtland, Ohio, 27 Machi 1836. Kulingana na maelezo yaliyoandikwa na Nabii, sala hii ilitolewa kwake kwa ufunuo.

1–5, Hekalu la Kirtland lilijengwa kama mahali ambapo Mwana wa Mtu atatembelea; 6–21, Itakuwa ni nyumba ya sala, kufunga, imani, kujifunza, utukufu, na utaratibu, na nyumba ya Mungu; 22–33, Na wasiotubu na ambao huwapiga watu wa Bwana nawashindwe; 34–42, Na Watakatifu waendelee katika uwezo kuwakusanya wenye haki katika Sayuni; 43–53, Na Watakatifu waokolewe kutokana

108 2*a* mwm Pumzika.
4*a* M&M 109:6–10.
5*a* M&M 82:10.
6*a* mwm Kazi ya kimisionari.
7*a* Lk. 22:31–32.
8*a* 2 Ne. 9:19.

na mambo mabaya yatakayomiminwa juu ya waovu katika siku za mwisho; 54–58, Na mataifa na watu na makanisa yatayarishwe kwa ajili ya injili; 59–67, Na Wayahudi, na Walamani, na Waisraeli wote wakombolewe; 68–80, Na Watakatifu wavikwe taji la utukufu na heshima, na wapate wokovu wa milele.

[a]Shukrani ziwe kwa jina lako, Ee Bwana Mungu wa Israeli, mwenye kuyashika [b]maagano na kuonyesha rehema kwa watumishi wako watembeao wima mbele zako, kwa moyo wao wote—

2 Wewe uliyewaamuru watumishi wako [a]kuijenga nyumba kwa jina lako katika mahali hapa [Kirtland].

3 Na sasa nawe waona, Ee Bwana, kwamba watumishi wako wamefanya kulingana na amri yako.

4 Na sasa twakuomba, Baba Mtakatifu, katika jina la Yesu Kristo, Mwana aliye kifuani mwako, ambaye katika jina lake pekee wokovu waweza kuhudumiwa kwa wanadamu, twakuomba, Ee Bwana, uikubali [a]nyumba hii, kazi ya [b]ustadi wa mikono yetu sisi, watumishi wako, ambao ulituamuru kuijenga.

5 Kwani wewe wajua kwamba tumeifanya kazi hii katika taabu kuu; na kutoka katika ufukara wetu tumetoa tulichokuwa nacho ili kuijenga [a]nyumba kwa jina lako, ili Mwana wa Mtu apate mahali pa kujionyesha mwenyewe kwa watu wake.

6 Na kama ulivyosema katika [a]ufunuo, uliotolewa kwetu sisi, ukituita marafiki zako, ukisema—Fanyeni kusanyiko lenu la kiroho, kama nilivyowaamuru;

7 Na kwa vile wote hawana imani, tafuteni kwa bidii na kufundishana maneno ya hekima; ndiyo, tafuteni kutoka kwenye vitabu vizuri maneno ya hekima, tafuteni maarifa hata kwa kujifunza na pia kwa imani;

8 Jipangeni wenyewe; tayarisheni kila kitu kilicho muhimu, na jengeni nyumba, hata nyumba ya sala, nyumba ya mfungo, nyumba ya imani, nyumba ya mafundisho, nyumba ya utukufu, nyumba ya utaratibu, nyumba ya Mungu;

9 Kwamba kuingia kwenu kupate kuwa katika jina la Bwana, kwamba kutoka kwenu kupate kuwa katika jina la Bwana, kwamba maamkizi yenu yote yapate kuwa katika jina la Bwana, mkiinua mikono kwake yeye Aliye Juu Sana—

10 Na sasa, Baba Mtakatifu, twakuomba utusaidie sisi, watu wako, kwa neema yako, kwa kuita kusanyiko letu la kiroho, ili lipate kufanyika kwa heshima yako na ukubali wako mtakatifu;

109 1*a* Alma 37:37; M&M 46:32.
MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
b Dan. 9:4.
MWM Agano.
2*a* M&M 88:119.
4*a* 1 Fal. 9:3.
MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.
b 2 Ne. 5:16.
5*a* M&M 124:27–28.
6*a* M&M 88:117–120.

11 Na katika namna ambayo tutaweza kuonekana wenye kustahili, machoni mwako, ili tupate utimilifu wa [a]ahadi ambazo umezifanya kwetu sisi, watu wako, katika mafunuo uliyotupatia;

12 Ili [a]utukufu wako upate kutua juu ya watu wako, na juu ya nyumba yako hii, ambayo sasa tunakutunukia wewe, ili ipate kutakaswa na kuwekwa wakfu kuwa takatifu, na ili uwepo wako mtakatifu, upate daima kuwa ndani ya nyumba hii;

13 Na kwamba watu wote watakaoingia mlangoni mwa nyumba ya Bwana wapate kuhisi uwezo wako, na walazimike kutambua kwamba wewe umeitakasa, na kwamba ni nyumba yako, mahali pa utakatifu wako.

14 Na uwajalie, Baba Mtakatifu, kwamba wale wote watakaoabudu katika nyumba hii wapate kufundishwa maneno ya hekima kutoka katika vitabu vilivyo bora, na kwamba wapate kutafuta maarifa hata kwa kujifunza, na pia kwa imani, kama wewe ulivyotuambia;

15 Na kwamba waweze kukua ndani yako, na kuupokea utimilifu wa Roho Mtakatifu, na kusimamiwa kulingana na sheria zako, na kujitayarisha kupokea kila jambo linalohitajika;

16 Na kwamba nyumba hii iwe nyumba ya sala, nyumba ya mfungo, nyumba ya imani, nyumba ya utukufu na ya Mungu, hata nyumba yako;

17 Kwamba kuingia kote kwa watu wako, ndani ya nyumba hii, kupate kuwa katika jina la Bwana;

18 Kwamba kutoka kwao ndani ya nyumba hii kupate kuwa katika jina la Bwana;

19 Na kwamba maamkizi yao yote yapate kuwa katika jina la Bwana, kwa mikono iliyotakata, iliyoinuliwa kwa Aliye Juu Sana;

20 Na kwamba hakuna kitu kilicho [a]kichafu kitakacho ruhusiwa kuja ndani ya nyumba yako ili kuichafua;

21 Na ikiwa watu wako watavunja sheria, yeyote miongoni mwao, atubu haraka na kurejea kwako, na kuona fadhili machoni pako, na kurejeshwa kwenye baraka ambazo wewe umeziweka ili kuzimwaga juu ya wale [a]watakaokuabudu wewe katika nyumba yako.

22 Na tunakuomba wewe, Baba Mtakatifu, kwamba watumishi wako wapate kwenda katika nyumba hii wakiwa wamevikwa uwezo wako, na kwamba jina lako liweze kuwa juu yao, na utukufu wako uwazingire pande zote, na [a]malaika zako wawalinde;

23 Na kutoka mahali hapa wao wapate kushuhudia habari hizi zilizo kuu na tukufu kupita kiasi, katika ukweli, hadi [a]miisho ya dunia, ili wao wapate kujua kwamba hii ni kazi yako, na kwamba wewe umeunyoosha mkono wako, kutimiza lile

11 *a* M&M 38:32; 105:11–12, 18, 33.
12 *a* MWM Utukufu.
20 *a* M&M 94:8–9; 97:15–17.
21 *a* MWM Uchaji.
22 *a* MWM Malaika.
23 *a* M&M 1:2.

ambalo ulilinena kwa vinywa vya manabii, juu ya siku za mwisho.

24 Tunakuomba, Baba Mtakatifu, kuwastawisha watu ambao watakuabudu, na watakuwa na jina na heshima katika hii nyumba yako, kwa vizazi vyote na yote;

25 Kwamba kila silaha [a]itakayofanyika juu yao isifanikiwe; kwamba achimbaye [b]shimo kwa ajili yao atumbukie mwenyewe;

26 Kwamba hakuna kundi la uovu litakalo kuwa na uwezo wa kuinuka na [a]kuwashinda watu wako ambao juu yao [b]jina lako litawekwa katika nyumba hii;

27 Na kama watu wowote watainuka dhidi ya watu hawa, kwamba hasira yako na iwake dhidi yao;

28 Na kama watawapiga watu hawa na wewe utawapiga; wewe utapigana kwa ajili ya watu wako kama ulivyofanya katika siku ya vita, ili wapate kukombolewa kutoka mikononi mwa adui zao wote.

29 Tunakuomba, Baba Mtakatifu, kuwafadhaisha, na kuwashangaza, na kuwatia aibu na kiwewe, wale wote walioeneza taarifa za uongo kote, ulimwenguni, dhidi ya mtumishi au watumishi wako, kama hawatatubu, wakati injili isiyo na mwisho itakapotangazwa masikioni mwao;

30 Na kwamba kazi zao zote ziwe si kitu, na kufagiliwa mbali kwa [a]mvua ya mawe, na kwa hukumu ambazo utazileta juu yao katika hasira yako, ili uweze kuwa mwisho wa [b]uongo na kashfa dhidi ya watu wako.

31 Kwa kuwa wewe unajua, Ee Bwana, kwamba watumishi wako wamekuwa hawana hatia mbele zako katika kulishuhudia jina lako, kwa sababu hiyo wameteseka mateso haya.

32 Kwa hiyo tunaomba mbele zako ukombozi kamili na mtimilifu kutoka chini ya [a]kongwa hili;

33 Livunje, Ee Bwana; livunje kutoka shingoni mwa watumishi wako, kwa uwezo wako, ili tuweze kuinuka katikati ya kizazi hiki na kufanya kazi yako.

34 Ee Yehova, uwarehemu watu hawa, na kama vile watu wote hutenda [a]dhambi, samehe uvunjaji sheria wa watu wako, na wafutiwe milele.

35 Na [a]mpako wa mafuta wa wahudumu wako na ufungwe juu yao kwa uwezo kutoka juu.

36 Na itimizwe juu yao, kama vile juu ya wale wa siku ya Pentekoste; na vipawa vya [a]ndimi vimwagwe juu ya watu wako, hata ndimi [b]zilizogawanyika kama ndimi za moto, na tafsiri yake.

37 Na nyumba yako na ijazwe, kama kwa uvumi wa upepo wa nguvu uendao kasi, kwa [a]utukufu wako.

25*a* Isa. 54:17.
b Mit. 26:27; 1 Ne. 14:3; 22:14.
26*a* M&M 98:22.
b 1 Fal. 8:29.
30*a* Isa. 28:17; Mos. 12:6; M&M 29:16.
b 3 Ne. 21:19–21.
32*a* MWM Nira.
34*a* Rum. 3:23; 5:12. MWM Dhambi.
35*a* MWM Paka mafuta.
36*a* MWM Ndimi, Kipawa cha.
b Mdo. 2:1–3.
37*a* M&M 84:5; 109:12. MWM Utukufu.

38 Weka juu ya watumishi wako [a]ushuhuda wa agano, ili wakati wakienda nje na kutangaza neno lako wapate [b]kuzifunga sheria, na kuitayarisha mioyo ya watakatifu wako kwa ajili ya hukumu zile zote ambazo u karibu kuzileta, katika ghadhabu yako, juu ya wakazi wa [c]dunia, kwa sababu ya uvunjaji wao wa sheria, ili watu wako wasikate tamaa katika siku ya dhiki.

39 Na katika mji wowote watumishi wako watakaoingia, na watu wa mji huo wakaupokea ushuhuda wao, na amani yako na wokovu wako uwe juu ya mji huo; ili wapate kuwakusanya kutoka mji huo wenye haki, ili waweze kuja [a]Sayuni, au katika vigingi vyake, mahali pa uteuzi wako, kwa nyimbo za shangwe isiyo na mwisho;

40 Na hadi hili litimizwe, usiache hukumu yako ianguke juu ya mji ule.

41 Na mji wowote watumishi wako watakaoingia, na watu wa mji huo wasiupokee ushuhuda wa watumishi wako, na watumishi wako wakawaonya wajiokoe kutoka kizazi hiki chenye ukaidi, na iwe juu ya mji huo kulingana na yale uliyoyanena kwa vinywa vya manabii wako.

42 Lakini waokoe wewe, Ee Yehova, tunakuomba, watumishi wako kutoka mikononi mwao, na kuwaosha kutokana na damu yao.

43 Ee Bwana, hatufurahii katika maangamizo ya wanadamu wenzetu; [a]nafsi zao ni za thamani kubwa mbele zako;

44 Lakini neno lako lazima litimizwe. Wasaidie watumishi wako kusema, wakisaidiwa na [a]neema yako: Mapenzi yako yatimizwe, Ee Bwana, na wala si yetu.

45 Sisi tunajua kwamba umenena kwa vinywa vya manabii wako mambo ya kutisha juu ya waovu, katika [a]siku za mwisho—kwamba utamwaga hukumu zako, pasipo kipimo;

46 Kwa hiyo, Ee Bwana, waokoe watu wako kutokana na majanga ya waovu; wawezeshe watumishi wako kuitia muhuri sheria, na kuufunga ushuhuda, ili waweze kutayarishwa dhidi ya siku ya mchomo.

47 Tunakuomba, Baba Mtakatifu, kuwakumbuka wale waliofukuzwa na wakazi wa wilaya ya Jackson, Missouri, kutoka viwanja vya urithi wao, na livunje, Ee Bwana, kongwa hili la mateso ambalo limewekwa juu yao.

48 Wewe wajua Ee Bwana, kwamba wameonewa na kuteswa sana na watu waovu; na mioyo yetu [a]imetiririka kwa huzuni kwa sababu ya masumbuko yao makali.

49 Ee Bwana, [a]hata lini utawaacha watu hawa kuteseka mateso haya, na vilio vya wasio na hatia kupanda juu masikioni

38*a* MWM Ushuhuda.
b Isa. 8:16; M&M 1:8.
c MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia.
39*a* Isa. 35:10.
43*a* MWM Nafsi.
44*a* MWM Neema.
45*a* MWM Siku za Mwisho.
48*a* MWM Huruma.
49*a* Zab. 13:1–2.

mwako, na [b]damu yao kuja kwako kwa ushuhuda mbele zako, na wala usionyeshe ushuhuda wako kwa niaba yao?

50 Uwe na [a]huruma, Ee Bwana, juu ya kundi la wahuni waovu, ambao wamewafukuza watu wako, ili wapate kukoma kuharibu, ili waweze kutubu dhambi zao kama toba itaonekana;

51 Lakini ikiwa hawatafanya hivi, uweke wazi mkono wako, Ee Bwana, na [a]ukomboe kile ambacho ulikiteua kuwa Sayuni kwa ajili ya watu wako.

52 Na kama haiwezekani kuwa vinginevyo, ili kazi ya watu wako isipate kushindwa mbele zako hasira yako na iwake, na uchungu wa hasira yako uanguke juu yao, ili waharibiwe mbali, vyote shina na tawi, kutoka chini ya mbingu;

53 Lakini kadiri watakavyotubu, wewe ni mwenye neema na huruma, nawe utaigeuza ghadhabu yako wakati uangaliapo juu ya sura ya Mpakwa mafuta wako.

54 Uwe na huruma, Ee Bwana, juu ya mataifa yote ya dunia; uwe na huruma juu ya watawala wa nchi yetu; na kanuni zile ambazo kwa heshima na taadhima zililindwa na mababu zetu, ambazo ndiyo [a]Katiba ya nchi yetu, na idumu milele.

55 Wakumbuke wafalme, watawala, watu mashuhuri, na wakuu wa duniani, na watu wote, na makanisa, maskini wote, na wenye shida, na wanaoteseka duniani;

56 Ili mioyo yao ipate kulainishwa wakati watumishi wako watakapo waendea kutoka nyumbani mwako, Ee Yehova, kulishuhudia jina lako; ili chuki zao zipate kutoa njia mbele ya [a]ukweli, na watu wako wapate kukubalika machoni pa wote;

57 Ili miisho yote ya dunia ipate kujua kwamba sisi, watumishi wako, [a]tumeisikia sauti yako, na kwamba wewe umetutuma sisi;

58 Ili kutoka miongoni mwao wote hawa, watumishi wako, wana wa Yakobo, waweze wawakusanye wenye haki kuujenga mji mtakatifu kwa jina lako, kama wewe ulivyowaamuru.

59 Tunakuomba kuichagulia Sayuni [a]vigingi vingine licha ya hiki ambacho umekiteua, ili [b]kukusanyika kwa watu wako kupate kuendelea katika uwezo mkuu na utukufu, ili kazi yako ipate [c]kufupishwa kwa haki.

60 Sasa maneno haya, Ee Bwana, tumeyanena mbele zako, juu ya mafunuo na amri ambazo umezitoa kwetu sisi, ambao tunashirikishwa na [a]Wayunani.

61 Lakini wewe unajua kwamba unayo mapenzi makubwa kwa watoto wa Yakobo, ambao wametawanywa juu ya milima kwa muda mrefu, katika siku ya mawingu na giza.

49 *b* MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.
50 *a* MWM Rehema, enye Rehema.
51 *a* M&M 100:13; 105:2.
54 *a* 1 Pet. 2:13–15; M&M 98:5–7; 101:77, 80.
MWM Katiba.
56 *a* MWM Ukweli.
57 *a* M&M 20:16; 76:22–24.
59 *a* Isa. 54:2.
b MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
c Mt. 24:22.
60 *a* 1 Ne. 13:1–32; 15:13–18.

62 Sisi kwa hiyo tunakuomba uwe na huruma juu ya watoto wa Yakobo, ili [a]Yerusalemu, kutoka saa hii, iweze kuanza kukombolewa;

63 Na kongwa la utumwa lianze kuvunjwa kutoka nyumba ya [a]Daudi;

64 Na watoto wa [a]Yuda waanze kurejea kwenye [b]viwanja ambavyo wewe ulivitoa kwa Ibrahimu, baba yao.

65 Na fanya kuwa [a]mabaki ya Yakobo, ambao wamelaaniwa na kupigwa kwa sababu ya uvunjaji wao wa sheria, [b]waongolewe kutoka katika hali yao ya unyama na ukatili kuja katika utimilifu wa injili isiyo na mwisho;

66 Ili wapate kuziweka chini silaha zao za umwagaji damu, na kuacha uasi wao.

67 Na mabaki ya [a]Israeli wote waliotawanywa, ambao wamefukuzwa hadi miisho ya dunia, waje katika ufahamu wa ukweli, wamwamini Masiya, na wakombolewe kutokana na kuonewa, na wafurahi mbele zako.

68 Ee Bwana, umkumbuke mtumishi wako, Joseph Smith, Mdogo, na dhiki na mateso yake yote—jinsi [a]alivyoagana na [b]Yehova, na alivyoweka nadhiri kwako, Ewe Mwenyezi Mungu wa Yakobo—na amri ambazo umezitoa kwake, na kwamba kwa moyo wote amejitahidi kuyafanya mapenzi yako.

69 Uwe na huruma, Ee Bwana, juu ya mke na watoto wake, ili wapate kutukuzwa katika uwepo wako, na watunzwe kwa mkono wako wenye kulea.

70 Uwe na huruma juu ya jamaa zao wa karibu, ili chuki zao zipate kuvunjwa na kufagiliwa mbali kama kwa gharika; ili waweze kuongolewa na kukombolewa pamoja na Israeli, na wajue kuwa wewe ndiye Mungu.

71 Wakumbuke, Ee Bwana, marais, hata marais wote wa kanisa lako, ili mkono wako wa kuume upate kuwainua, pamoja na familia zao zote, na jamaa zao wa karibu, ili majina yao yaweze kudumishwa na kuwa katika ukumbusho usiyo na mwisho kutoka kizazi hadi kizazi.

72 Ulikumbuke kanisa lako lote, Ee Bwana, pamoja na familia zao zote, na jamaa zao wote wa karibu, pamoja na wagonjwa na wenye kuteseka wao wote, pamoja na maskini na wanyonge wa dunia wote; ili [a]ufalme, ambao umeuanzisha pasipo mikono, uweze kuwa mlima mkuu na kuijaza dunia yote;

73 Ili kanisa lako liweze

62*a* 3 Ne. 20:29. MWM Yerusalemu.
63*a* MWM Daudi.
64*a* Zek. 12:6–9; Mal. 3:4; M&M 133:13, 35. MWM Yuda.
b Mwa. 17:1–8. MWM Nchi ya Ahadi.
65*a* 2 Ne. 30:3; Alma 46:23–24; 3 Ne. 20:15–21; M&M 19:27.
b 2 Ne. 30:6; 3 Ne. 21:20–22. MWM Mwongofu, Uongofu.
67*a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
68*a* MWM Agano.
b MWM Yehova.
72*a* Dan. 2:44–45; M&M 65:2.

kujitokeza kutoka nyika zenye giza, na kuangaza vizuri kama [a]mwezi, safi kama jua, wakutisha kama jeshi lenye bendera;

74 Na kurembeshwa kama bibi harusi kwa siku ile utakapozifunua mbingu, na kuifanya milima [a]ishushwe mbele ya uwepo wako, na [b]mabonde yainuliwe, mahali palipoparuzwa patalainishwa; ili utukufu wako upate kuijaza nchi;

75 Ili wakati baragumu litakapolia kwa ajili ya wafu, [a]tunyakuliwe mawinguni kukulaki wewe, ili daima tuwe pamoja na Bwana;

76 Ili [a]mavazi yetu yapate kuwa safi, ili tuweze kuvikwa majoho ya haki, tukiwa na matawi ya miti mikononi mwetu, na [b]mataji ya utukufu juu ya vichwa vyetu, na kuvuna [c]shangwe ya milele kwa [d]mateso yetu yote.

77 Ee Bwana Mungu Mwenyezi, utusikilize sisi katika maombi yetu haya, na utujibu kutoka mbinguni, makao yako matakatifu, mahali wewe uketipo katika kiti cha enzi, kwa [a]utukufu, heshima, uwezo, fahari, nguvu, utawala, kweli, haki, hukumu, neema, na utimilifu usio na mwisho, tangu milele hata milele.

78 Ee tusikie, Ee tusikie, Ee tusikie sisi, Ee Bwana! Na ujibu maombi haya, na upokee kuwekwa wakfu kwa nyumba hii kwako, kazi ya mikono yetu, ambayo tumeijenga kwa ajili ya jina lako;

79 Na pia kanisa hili, kuwekwa juu yake jina lako. Na utusaidie sisi kwa uwezo wa Roho wako, ili tuweze kuchanganya sauti zetu pamoja na wale [a]maserafi wazuri na wenye kung'ara kuzunguka kiti chako cha enzi, kwa shangwe za kusifu, tukiimba Hosana kwa Mungu na kwa [b]Mwanakondoo!

80 Na hawa, wapakwa mafuta wako, na [a]wavikwe wokovu, na watakatifu wako wapige kelele kwa sauti kwa ajili ya shangwe. Amina, na Amina.

SEHEMU YA 110

Maono yaliyoonyeshwa kwa Joseph Smith Nabii na Oliver Cowdery katika hekalu huko Kirtland, Ohio, 3 Aprili 1836. Wakati ulikuwa ni ule wa mkutano wa siku ya Sabato. Historia ya Joseph Smith inaeleza: "Wakati wa alasiri, niliwasaidia Marais wengine katika kugawa Chakula cha Bwana kwa Kanisa, baada ya kupokea kutoka kwa Mitume Kumi na Wawili, ambao ilikuwa zamu yao kuongoza

73*a* Wim. 6:10; M&M 5:14; 105:31.
74*a* M&M 133:21–22, 40.
b Isa. 40:4; Lk. 3:5; M&M 49:23.
75*a* 1 The. 4:17.
76*a* Ufu. 7:13–15; 2 Ne. 9:14.
b MWM Kuinuliwa; Taji.
c MWM Shangwe.
d Ebr. 12:1–11; M&M 58:4.
77*a* MWM Utukufu.
79*a* Isa. 6:1–2.
b MWM Mwanakondoo wa Mungu.
80*a* Zab. 132:16.

kwenye meza takatifu kwa siku hii. Baada ya kufanya huduma hii kwa ndugu zangu, nilirejea kwenye mimbari, pazia likiwa limeshushwa, na nikapiga magoti, pamoja na Oliver Cowdery, kwa sala ya unyenyekevu na kimya kimya. Baada ya kumaliza kusali, ono lifuatalo lilifunguliwa kwetu sote wawili."

1–10, Bwana Yehova atokea katika utukufu na kulikubali Hekalu la Kirtland kama nyumba Yake; 11–12, Musa na Elia kila mmoja anatokea na kukabidhi funguo za nyakati zao; 13–16, Eliya anarudi na kukabidhi funguo za kipindi chake kama ilivyoahidiwa na Malaki.

[a]Pazia liliondolewa kutoka akilini mwetu, na [b]macho yetu ya ufahamu yakafunguliwa.

2 Tulimwona Bwana akiwa amesimama kwenye jukwaa la mimbari, mbele yetu; na chini ya miguu yake palikuwa na kama sakafu iliyofanyizwa kwa dhahabu safi, katika rangi kama ya kaharabu.

3 [a]Macho yake yalikuwa kama mwale wa moto; nywele za kichwa chake zilikuwa nyeupe kama theluji safi; [b]uso wake uling'ara kupita mng'aro wa jua; na [c]sauti yake ilikuwa kama sauti ya maji mengi yakimbiayo, hata sauti ya [d]Yehova, akisema:

4 Mimi ni [a]kwanza na mwisho; Mimi ni yeye aliye [b]hai, Mimi ni yule aliyeuawa; Mimi ni [c]mtetezi wenu kwa Baba.

5 Tazama, dhambi zenu [a]zimesamehewa; nanyi ni wasafi mbele zangu; kwa hiyo, inueni vichwa vyenu na kufurahi.

6 Na acha mioyo ya ndugu zenu na ifurahi, na acha mioyo ya watu wangu wote ifurahi, ambao, kwa nguvu zao, [a]wameijenga nyumba hii kwa ajili ya jina langu.

7 Kwani tazama, [a]nimeikubali [b]nyumba hii, na jina langu litakuwa humu; nami nitajionyesha kwa watu wangu kwa rehema katika nyumba hii.

8 Ndiyo, [a]nitajitokeza kwa watumishi wangu, na kusema nao kwa sauti yangu mwenyewe, kama watu wangu watashika amri zangu, na ikiwa [b]hawataichafua [c]nyumba hii takatifu.

9 Ndiyo mioyo ya maelfu na makumi ya elfu itafurahia kwa furaha kuu kwa matokeo ya [a]baraka zitakazomwagwa, na kwa [b]endaomenti ambayo watumishi wangu wamepewa katika nyumba hii.

10 Na umaarufu wa nyumba hii utaenea hadi nchi za kigeni; na huu ni mwanzo wa baraka

110 1*a* MWM Pazia.
b M&M 76:12, 19; 136:32; 138:11.
3*a* Ufu. 1:14.
b Ufu. 1:16; JS—H 1:17.
c Eze. 43:2; Ufu. 1:15; M&M 133:21–22.
d MWM Yehova.
4*a* MWM Mzaliwa wa Kwanza.
b Kum. 5:24.
c MWM Mtetezi.
5*a* MWM Samehe.
6*a* M&M 109:4–5.
7*a* 2 Nya. 7:16.
b MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.
8*a* M&M 50:45.
b M&M 97:15–17.
c MWM Takatifu.
9*a* Mwa. 12:1–3; M&M 39:15; Ibr. 2:8–11.
b M&M 95:8. MWM Endaomenti.

ambazo [a]zitamwagwa juu ya vichwa vya watu wangu. Hivyo ndivyo. Amina.

11 Baada ya [a]ono hili kufungwa, mbingu zilitufungukia tena; na [b]Musa akatokea mbele yetu, na kutukabidhi [c]funguo za [d]kukusanyika kwa Israeli kutoka pande nne za dunia, na kuongozwa kwa makabila kumi kutoka nchi ya [e]kaskazini.

12 Baada ya hili, [a]Elia alitokea, na kutukabidhi [b]kipindi cha [c]injili ya Ibrahimu, akisema kwamba kupitia sisi na uzao wetu vizazi vyote baada yetu sisi vitabarikiwa.

13 Baada ya ono hili kufungwa, ono jingine kubwa na tukufu likatukia juu yetu; kwani [a]Eliya nabii, [b]aliyechukuliwa mbinguni bila ya kuonja mauti, alisimama mbele yetu, na kusema:

14 Tazama, wakati umetimia kikamilifu, ambao ulinenwa kwa kinywa cha Malaki—ukishuhudia kwamba yeye [Eliya] lazima atatumwa, kabla ya kuja kwa siku ile iliyo kuu na ya Bwana—

15 [a]Kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na ya watoto iwaelekee mababu, dunia yote isije ikapigwa kwa laana—

16 Kwa hiyo, funguo za kipindi hiki zimekabidhiwa mikononi mwenu; na kwa hili ninyi mpate kujua kwamba [a]siku ile iliyo kuu na ya kutisha ya Bwana i karibu, hata milangoni.

SEHEMU YA 111

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Salem, Massachusetts, 6 Agosti 1836. Wakati huu viongozi wa Kanisa walikuwa katika deni kubwa kutokana na kazi zao katika huduma. Kwa kuwa walisikia kwamba kiasi kikubwa cha fedha kitapatikana kwao huko Salem, Nabii, Sidney Rigdon, Hyrum Smith, na Oliver Cowdery walisafiri kwenda huko kutoka Kirtland, Ohio, ili kuchunguza dai hili, pamoja na kuhubiri injili. Ndugu hawa walitimiza shughuli kadhaa za Kanisa na kufanya mahubiri. Wakati ilipokuja kujulikana wazi kwamba hapakuwa na fedha yoyote itakayokuja, walirejea Kirtland. Sehemu muhimu kadhaa katika historia hii zimeelezwa katika maneno yaliyotumiwa katika ufunuo huu.

10 *a* M&M 105:12.
11 *a* MWM Ono.
b Mt. 17:3.
c MWM Funguo za Ukuhani.
d Yak. (KM) 6:2; M&M 29:7. MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
e M&M 133:26–32. MWM Israeli—Makabila Kumi ya Israeli yaliyopotea.
12 *a* MWM Elia.
b MWM Kipindi.
c Gal. 3:6–29. MWM Agano la Ibrahimu.
13 *a* MWM Eliya.
b MWM Viumbe waliobadilishwa.
15 *a* JS—H 1:38–39. MWM Nasaba; Wokovu kwa ajili ya Wafu.
16 *a* MWM Siku za Mwisho.

1–5, Bwana huangalia mahitaji ya kimwili ya watumishi Wake; 6–11, Kwa rehema, ataitendea Sayuni na kupanga mambo yote kwa faida ya watumishi Wake.

Mimi, Bwana Mungu wenu, siyo kwamba sijapendezwa na kuja kwenu katika safari hii, licha ya upuuzi wenu.

2 Ninayo hazina kubwa katika mji huu kwa ajili yenu, kwa faida ya Sayuni, na watu wengi katika mji huu, ambao nitawakusanya katika wakati wake kwa faida ya Sayuni, kwa kuwatumia ninyi.

3 Kwa hiyo, ninyi hamna budi kuzoeana na watu wa mji huu, kama vile mtakavyoongozwa, na kama vile mtakavyopewa.

4 Na itakuwa kwamba katika wakati wake nitautoa mji huu mikononi mwenu, kwamba mtakuwa na uwezo juu yake, kiasi kwamba wao hawatagundua siri zenu; na utajiri wake unaohusu dhahabu na fedha utakuwa wenu.

5 Msijisumbue juu ya [a]madeni yenu, kwani nitawapa uwezo wa kuyalipa.

6 Msisumbuke kuhusu Sayuni, kwani nitamrehemu.

7 Kaeni mahali hapa, na katika maeneo ya karibu;

8 Na mahali ambapo nitapenda ninyi mkae, kwani sehemu kubwa, itaonyeshwa kwenu kwa [a]amani na uwezo wa Roho yangu, ambayo itamiminika kwenu.

9 Sehemu hii mtaweza kuipata kwa kuikodi. Na ulizeni kwa bidii juu ya wakazi wa kale zaidi na waanzilishi wa mji huu;

10 Kwani ziko hazina nyingi zaidi ya moja kwa ajili yenu katika mji huu.

11 Basi, muwe na [a]busara kama nyoka lakini pasipo kuwa na dhambi; nami nitayapanga mambo yote kwa [b]faida yenu, haraka kadiri mtakavyoweza kuyapokea. Amina.

SEHEMU YA 112

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii kwa Thomas B. Marsh, huko Kirtland, Ohio, 23 Julai 1837. Ufunuo huu unalo neno la Bwana kwa Thomas B. Marsh juu ya Mitume Kumi na Wawili wa Mwanakondoo. Ufunuo huu ulipokelewa siku ile Wazee Heber C. Kimball na Orson Hyde walipohubiri injili kwa mara ya kwanza huko Uingereza. Thomas B. Marsh kwa wakati huu alikuwa Rais wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili.

1–10, Mitume Kumi na Wawili wataipeleka injili na kupaza sauti ya onyo kwa mataifa yote na watu wote; 11–15, Wao wataubeba

111 5*a* M&M 64:27–29.
8*a* M&M 27:16.
MWM Amani.
11*a* Mt. 10:16.
b Rum. 8:28; M&M 90:24; 100:15.

msalaba wao, kumfuata Yesu, na kulisha kondoo Wake; 16–20, Wale waupokeao Urais wa Kwanza wampokea Bwana; 21–29, Giza limeifunika dunia, na ni wale tu waaminio na kubatizwa wataokolewa; 30–34, Urais wa kwanza na Mitume Kumi na Wawili wanashikilia funguo za kipindi cha utimilifu.

Amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwako wewe mtumishi wangu Thomas: Nimesikia sala zako; na sadaka zako zimefika juu kama [a]ukumbusho mbele zangu, kwa niaba ya wale, ndugu zako, ambao walichaguliwa kutoa ushuhuda wa jina langu na [b]kuupeleka ulimwenguni kote miongoni mwa mataifa yote, makabila, lugha, na watu, na kutawazwa kwa njia ya watumishi wangu.

2 Amini ninakuambia, pamekuwepo na baadhi ya mambo machache moyoni mwako na pamoja nawe ambayo Mimi, Bwana, sikupendezwa nayo.

3 Hata hivyo, kwa vile wewe [a]umejidhili mwenyewe nawe utakwezwa; kwa hiyo, dhambi zako zote zimesamehewa.

4 Acha moyo wako na [a]ufurahi mbele ya uso wangu; nawe utalishuhudia jina langu, siyo tu kwa [b]Wayunani, bali pia kwa [c]Wayahudi; nawe utalipeleka neno langu hata miisho ya dunia.

5 [a]Jitahidi, kwa hiyo, asubuhi hadi asubuhi; na siku hadi siku na acha sauti yako ya [b]kuonya isikike; na usiku uingiapo usiache wakazi wa dunia walale, kwa sababu ya maneno yako.

6 Acha makazi yako yafahamike katika Sayuni, na [a]usiiondoe nyumba yako; kwa kuwa Mimi, Bwana, ninayo kazi kubwa ya kufanywa na wewe, kazi ya kulitangaza jina langu miongoni mwa wanadamu.

7 Kwa hiyo, [a]funga viuno vyako kwa ajili ya kazi hii. Na acha miguu yako ifungiwe pia, kwani wewe umechaguliwa, na njia zako zitakuwa miongoni mwa milima, na miongoni mwa mataifa mengi.

8 Na kwa neno lako wengi walio juu [a]watashushwa chini, na kwa neno lako wengi walio chini watakwezwa.

9 Acha sauti yako iwe karipio kwa wavunja sheria; na kwa kukaripia kwako ulimi wa mzushi na ukome uovu wake.

10 [a]Jinyenyekeze; na Bwana Mungu wako atakuongoza kwa mkono, na kukupa jibu la sala zako.

11 Mimi naujua moyo wako, na nimesikia sala zako juu ya ndugu zako. Usiwe na [a]upendo zaidi kwao kuliko watu wengine wengi, bali acha upendo wako kwao uwe kama ujipendavyo wewe mwenyewe; na acha upendo wako ubaki kwa

112 1*a* Mdo. 10:4.
b M&M 18:28.
3*a* Mt. 23:12; Lk. 14:11.
4*a* Mt. 9:2; Yn. 16:33.
b M&M 18:6; 90:8–9.
c M&M 19:27.
5*a* Yuda 1:3.
b M&M 1:4–5.
6*a* Zab. 125:1.
7*a* Efe. 6:13–17.
8*a* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
10*a* Mit. 18:12.
11*a* Mt. 5:43–48.
MWM Hisani; Upendo.

watu wote, na kwa wote walipendao jina langu.

12 Na uwaombee ndugu zako Kumi na Wawili. Waonye kwa nguvu kwa ajili ya jina langu, na acha waonywe kwa ajili ya dhambi zao zote, na uwe mwaminifu mbele zangu kwa [a]jina langu.

13 Na baada ya [a]majaribu yao, na [b]taabu nyingi, tazama, Mimi, Bwana, nitawatafuta, na kama hawakuishupaza mioyo yao, na kuzikaza shingo zao dhidi yangu, [c]wataongolewa, nami nitawaponya.

14 Sasa, ninakuambia, na hilo nikuambialo, nawaambia wote Kumi na Wawili: Inukeni na vifungeni viuno vyenu, chukua [a]msalaba wako, ukanifuate, na [b]kuwalisha kondoo zangu.

15 Msijikweze wenyewe; [a]msimuasi mtumishi wangu Joseph; kwani amini ninawaambia, Mimi nipo pamoja naye, na mkono wangu utakuwa juu yake; na [b]funguo nilizompa yeye, na pia ninyi, hazitachukuliwa kutoka kwake hadi nitakapokuja.

16 Amini ninakuambia, mtumishi wangu Thomas, wewe ni mtu ambaye nimekuchagua kuzishika funguo za ufalme wangu, zinazowahusu Kumi na Wawili, popote miongoni mwa mataifa yote—

17 Ili upate kuwa mtumishi wangu kwa kufungua mlango wa ufalme mahali pote ambapo mtumishi wangu Joseph, na mtumishi wangu [a]Sidney, na mtumishi wangu [b]Hyrum, hawawezi kufika.

18 Kwani juu yao nimeweka mzigo wa makanisa yote kwa kipindi kifupi.

19 Kwa sababu hiyo, kokote watakakowatuma, nendeni, nami nitakuwa pamoja nanyi; na mahali popote mtakapotangaza jina langu mlango wa matokeo ya [a]kufaa utafunguliwa kwenu, ili wapate kulipokea neno langu.

20 Yeyote [a]alipokeaye neno langu anipokea Mimi, na yeyote anipokeaye Mimi, huwapokea wale, Urais wa Kwanza, ambao nimewatuma, ambao nimewafanya kuwa washauri kwa ajili ya jina langu kwenu.

21 Na tena, ninawaambia, kwamba yeyote mtakayemtuma katika jina langu, kwa sauti ya ndugu zenu, hawa [a]Kumi na Wawili, akiwa amependekezwa na kupewa [b]mamlaka kisheria na ninyi, atakuwa na uwezo wa kufungua mlango wa ufalme wangu kwa taifa lolote ambako ninyi mtawatuma—

22 Ilimradi kama watajinyenyekeza wenyewe mbele zangu,

12 *a* MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
13 *a* MWM Jaribu, Majaribu.
b Yn. 16:33; Ufu. 7:13–14; M&M 58:3–4.
c 3 Ne. 18:32.
14 *a* Mt. 16:24; TJS Mt. 16:25–26 (Kiambatisho); Lk. 9:23.
b Yn. 21:15–17.
15 *a* MWM Uasi.
b M&M 28:7.
MWM Mwongofu, Uongofu.
MWM Funguo za Ukuhani.
17 *a* MWM Rigdon, Sidney.
b MWM Smith, Hyrum.
19 *a* 1 Kor. 16:9; M&M 118:3.
20 *a* M&M 84:35–38.
21 *a* M&M 107:34–35.
b MWM Mamlaka.

na kukaa katika neno langu, na [a]kuisikia sauti ya Roho wangu.

23 Amini, amini, ninawaambia, [a]giza hufunika dunia, na giza kuu huzifunika akili za watu, na wenye mwili wote [b]wameharibika mbele za uso wangu.

24 Tazama, [a]kisasi chaja haraka juu ya wakazi wa dunia, siku ya ghadhabu, siku ya kuteketezwa kwa moto, siku ya ukiwa, ya [b]kulia, ya kilio, na ya maombolezo; na kama tufani itakuja juu ya uso wote wa dunia, asema Bwana.

25 Na juu ya nyumba yangu [a]itaanzia, na kutoka nyumbani mwangu itaenea, asema Bwana;

26 Kwanza miongoni mwa wale walio miongoni mwenu, asema Bwana, ambao [a]wamedai kulijua jina langu na [b]hawakunijua Mimi, nao [c]wamenitukana katikati ya nyumba yangu, asema Bwana.

27 Kwa hiyo, angalieni msijisumbue kuhusu mambo ya kanisa langu mahali hapa, asema Bwana.

28 Bali [a]itakaseni mioyo yenu mbele zangu, na ndipo [b]mwende ulimwenguni kote, na kuihubiri injili yangu kwa kila kiumbe ambacho bado hakijaipokea;

29 Na yule [a]aaminiye na [b]kubatizwa ataokolewa, na yule asiyeamini, na hakubatizwa, [c]atalaaniwa.

30 Kwani kwenu, [a]Kumi na Wawili, na wale, [b]Urais wa Kwanza wa Kwanza, ambao wameteuliwa na ninyi kuwa washauri wenu na viongozi wenu, ndiyo uwezo huu wa ukuhani umetolewa, kwa ajili ya siku za mwisho na kwa mara ya mwisho, ambacho ndicho [c]kipindi cha utimilifu wa nyakati.

31 Uwezo ambao ninyi mnaushikilia, kwa pamoja na wale wote waliopokea kipindi kwa wakati wowote kutoka mwanzo wa uumbaji;

32 Kwani amini ninawaambia, [a]funguo za kipindi, ambazo ninyi mmezipokea, [b]zimekuja chini kutoka kwa mababu, na mwisho wa yote, zimeshushwa kwenu kutoka mbinguni.

33 Amini ninawaambia, tazama wito wenu ni mkubwa kiasi gani. [a]Isafisheni mioyo yenu na mavazi yenu, isije damu ya kizazi hiki [b]ikadaiwa mikononi mwenu.

22*a* MWM Mtiifu, Tii, Utii; Sikiliza.
23*a* Isa. 60:2; Mik. 3:6; M&M 38:11.
MWM Ukengeufu—Ukengeufu wa Kanisa la awali la Kikristo.
b M&M 10:20–23.
24*a* MWM Kisasi.
b M&M 124:8.
25*a* 1 Pet. 4:17–18.
26*a* Mt. 7:21–23; M&M 41:1; 56:1.
b Lk. 6:46; Mos. 26:24–27; 3 Ne. 14:21–23.
c MWM Kukufuru, Kufuru.
28*a* MWM Safi na Isiyo safi.
b Mk. 16:15–16.
29*a* Morm. 9:22–23; M&M 20:25–26.
b MWM Batiza, Ubatizo.
c MWM Hukumu.
30*a* MWM Mtume.
b MWM Urais wa Kwanza.
c Efe. 1:10; M&M 27:13; 124:40–42.
MWM Kipindi.
32*a* M&M 110:11–16.
MWM Funguo za Ukuhani.
b Ibr. 1:2–3.
33*a* Yak. (KM) 1:19.
b M&M 72:3.

34 Kuweni waaminifu hadi nijapo, kwani [a]naja upesi; na ujira wangu u pamoja nami kumlipa kila mtu kulingana na [b]kazi yake itakavyokuwa. Mimi ni Alfa na Omega. Amina.

SEHEMU YA 113

Majibu ya maswali kadha wa kadha juu ya maandiko ya Isaya, yaliyotolewa na Joseph Smith Nabii, huko au jirani na Far West, Missouri, Machi 1838.

1–6, Shina la Yese, chipukizi litokalo ndani yake, na mzizi wa Yese vinaelezewa; 7–10, Mabaki ya watu wa Sayuni waliotawanywa wanayo haki ya ukuhani nao wanaitwa kurejea kwa Bwana.

Shina la [a]Yese anayesemwa katika mstari wa 1, 2, 3, 4 na 5 wa mlango wa 11 wa Isaya ni nani?

2 Amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Ni Kristo.

3 Chipukizi linalosemwa katika mstari wa kwanza wa mlango wa 11 wa Isaya, ambalo litatoka kwenye Shina la Yese ni nini?

4 Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Ni mtumishi katika mikono ya Kristo, ambaye ni wa sehemu ya uzao wa Yese na vile vile ni wa [a]Efraimu, au wa nyumba ya Yusufu, ambaye juu yake umewekwa [b]uwezo mwingi.

5 Mzizi wa Yese unaosemwa katika mstari wa 10 wa mlango wa 11 ni nini?

6 Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, ni mzaliwa wa ukoo wa Yese, vile vile wa Yusuf, ambaye anayo haki ya ukuhani, na [a]funguo za ufalme, kuwa kama [b]bendera, na kwa ajili ya [c]kukusanyika kwa watu wangu katika siku za mwisho.

7 Maswali yaliyoulizwa na Elias Higbee: Kuna maana gani katika amri iliyoko katika Isaya, mlango wa 52, mstari wa 1, ambayo inasema: Jivike nguvu zako, Ee Sayuni—ni watu gani ambao Isaya aliwataja?

8 Alikuwa akiwaelezea watu wale ambao Mungu atawaita katika siku za mwisho, ambao watashikilia uwezo wa ukuhani kuirejesha tena [a]Sayuni, na wa ukombozi wa Israeli; na kujivika [b]nguvu zake ni kujivika mamlaka ya ukuhani, ambayo yeye, Sayuni, anayo [c]haki ya kuzaliwa; pia kurejea kwenye ule uwezo ambao aliupoteza.

9 Tuelewe nini kwa Sayuni kujifungulia vifungo vya shingo yake; mstari wa 2?

34*a* Ufu. 22:7, 12; M&M 49:28; 54:10.
b mwm Matendo.
113 1*a* mwm Yese.
4*a* Mwa. 41:50–52; M&M 133:30–34. mwm Efraimu.
b mwm Uwezo.
6*a* mwm Funguo za Ukuhani.
b M&M 45:9. mwm Bendera.
c mwm Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
8*a* mwm Sayuni.
b M&M 82:14.
c mwm Haki ya Kuzaliwa.

10 Tuelewe kwamba mabaki [a]waliotawanyika wanahimizwa [b]kumrudia Bwana kutoka kule walikoanguka; na wakifanya hivyo, ahadi ya Bwana ni kwamba atanena nao, au atawapa ufunuo. Ona mistari ya 6, 7, na 8. Vifungo vya shingo yake ni laana ya Mungu juu yake, au mabaki ya Israeli katika hali yao ya kutawanywa miongoni mwa Wayunani.

SEHEMU YA 114

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Far West, Missouri, 11 Aprili 1838.

1–2, Nafasi za kanisa zilizoshikiliwa na watu ambao siyo waaminifu zitatolewa kwa watu wengine.

Amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Ni hekima kwa mtumishi wangu David W. Patten, kwamba apange mambo yote ya biashara yake haraka kadiri atakavyoweza, na kugawa bidhaa za biashara yake, ili apate kufanya huduma yangu majira yajayo ya kuchipua, akiambatana na wengine, hata kumi na wawili ikiwa ni pamoja na yeye mwenyewe, ili kulishuhudia jina langu na kutangaza habari njema kwa ulimwengu wote.

2 Kwani amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana, kwamba kwa vile wapo watu miongoni mwenu walikataao jina langu, wengine [a]watapandwa [b]badala yao na kupokea uaskofu wao. Amina.

SEHEMU YA 115

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Far West, Missouri, 26 Aprili 1838, ukijulisha mapenzi ya Mungu juu ya ujenzi wa mahali pale na wa nyumba ya Bwana. Ufunuo huu unaelekezwa kwa maofisa viongozi na waumini wa Kanisa.

1–4, Bwana analiita kanisa Lake Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho; 5–6, Sayuni na vigingi vyake ni mahali pa ngome na makimbilio kwa Watakatifu; 7–16, Watakatifu wanaamriwa kujenga nyumba ya Bwana huko Far West; 17–19, Joseph Smith anashikilia funguo za ufalme wa Mungu duniani.

Amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwako, mtumishi wangu [a]Joseph Smith, Mdogo,

10 *a* MWM Israeli—Kutawanyika kwa Israeli.
b Hos. 3:4–5; 2 Ne. 6:11.
114 2 *a* M&M 118:1, 6.
b M&M 64:40.
115 1 *a* MWM Smith, Joseph, Mdogo.

na pia mtumishi wangu [b]Sidney Rigdon, na pia mtumishi wangu [c]Hyrum Smith, na washauri wenu waliopo na watakaoteuliwa hapo baadaye;

2 Na pia kwako wewe, mtumishi wangu [a]Edward Partridge, na washauri wake;

3 Na pia kwa watumishi wangu waaminifu ambao ni wa baraza kuu la kanisa langu katika Sayuni, kwani hivyo ndivyo litakavyoitwa, na kwa wazee wote na watu wa Kanisa langu la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, waliotawanyika ulimwenguni kote;

4 Kwani hivyo ndivyo [a]kanisa langu litakavyoitwa katika siku za mwisho, hata [b]Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.

5 Amini ninawaambia ninyi nyote: [a]Inukeni na mng'are, ili nuru yenu ipate kuwa [b]bendera kwa ajili ya mataifa;

6 Na ili [a]kukusanyika pamoja juu ya nchi ya [b]Sayuni, na juu ya [c]vigingi vyake, kupata kuwa ngome, na [d]makimbilio wakati wa tufani, na ghadhabu wakati [e]itakapomwagwa pasipo kuchanganywa juu ya dunia yote.

7 Acha mji wa Far West, uwe mji [a]mtakatifu na uliowekwa wakfu kwangu; nao utaitwa mtakatifu sana, kwani ardhi ambayo juu yake umesimama ni takatifu.

8 Kwa hiyo, nakuamuruni [a]kunijengea nyumba, kwa ajili ya kukusanyika pamoja watakatifu wangu, ili wapate [b]kuniabudu.

9 Na acha uwepo mwanzo wa kazi hii, na msingi, na kazi ya maandalizi ya kiangazi hiki kijacho;

10 Na acha mwanzo ufanyike siku ya nne ya Julai ijayo; na tangu wakati ule na kuendelea acha watu wangu wafanye kazi kwa bidii kuijenga nyumba katika jina langu;

11 Na katika mwaka [a]mmoja kutoka siku hii acha waanze kuweka msingi wa [b]nyumba yangu.

12 Hivyo acha kuanzia tangu wakati ule na kuendelea wafanye kazi kwa bidii hadi itakapomalizika, kutoka jiwe lake la kona hadi juu yake, hadi pasiwepo na kitu chochote kitakachobakia bila kumalizika.

13 Amini ninawaambia, msiache mtumishi wangu, Joseph, wala mtumishi wangu Sidney, wala mtumishi wangu Hyrum, waingie tena katika deni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba katika jina langu;

14 Bali acha nyumba ijengwe kwa jina langu kulingana na

1 *b* MWM Rigdon, Sidney.
c MWM Smith, Hyrum.
2 *a* MWM Partridge, Edward.
4 *a* 3 Ne. 27:4–8.
b MWM Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.
5 *a* Isa. 60:1–3.
b Isa. 11:12.
MWM Bendera.
6 *a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b MWM Sayuni.
c M&M 101:21.
MWM Kigingi.
d Isa. 25:1, 4; M&M 45:66–71.
e Ufu. 14:10; M&M 1:13–14.
7 *a* MWM Takatifu.
8 *a* M&M 88:119; 95:8.
b MWM Kuabudu.
11 *a* M&M 118:5.
b M&M 124:45–54.

[a]utaratibu ambao nitauonyesha kwao.

15 Na kama watu wangu hawatajenga kulingana na utaratibu ambao nitauonyesha kwa urais wao, sitaipokea kutoka kutoka kwao.

16 Lakini ikiwa watu wangu wataijenga kulingana na utaratibu ambao nitauonyesha kwa urais wao, hata mtumishi wangu Joseph na washauri wake, ndipo nitaipokea kutoka mikononi mwa watu wangu.

17 Na tena, amini ninawaambia, ni mapenzi yangu kwamba mji wa Far West lazima ujengwe haraka kwa kukusanyika kwa watakatifu wangu;

18 Na pia kwamba mahali pengine pateuliwe kwa ajili ya [a]vigingi katika maeneo ya jirani, kama vile yatakavyofunuliwa kwa mtumishi wangu Joseph, mara kwa mara.

19 Kwani tazama, Mimi nitakuwa pamoja naye, nami nitamtakasa mbele ya hawa watu; kwani yeye nimempa [a]funguo za ufalme huu na huduma hii. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 116

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, karibu na Kivuko cha Wight, mahali paitwapo Spring Hill, Wilaya ya Daviess, Missouri, 19 Mei 1838.

Spring Hill Bwana alipaita [a]Adamu-ondi-Amani, kwa sababu, alisema, ndipo mahali ambapo [b]Adamu atakuja kuwatembelea watu wake, au [c]Mzee wa Siku atakapokaa, kama ilivyonenwa na Danieli nabii.

SEHEMU YA 117

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Far West, Missouri, 8 Julai 1838, juu ya wajibu wa haraka wa William Marks, Newel K. Whitney, na Oliver Granger.

1–9, Watumishi wa Bwana hawapaswi kutamani mambo ya kimwili, kwani "mali ni nini kwa Bwana?"; 10–16, Wao waache udhaifu wa nafsi, na dhabihu zao zitakuwa takatifu kwa Bwana.

Amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwa mtumishi wangu

14 *a* Ebr. 8:5; M&M 97:10.
18 *a* M&M 101:21. mwm Kigingi.
19 *a* mwm Funguo za Ukuhani.
116 1 *a* M&M 78:15. mwm Adamu-ondi-Amani.
b mwm Adamu.
c Dan. 7:13–14, 22.

William Marks, na pia kwa mtumishi wangu Newel K. Whitney, na wapange vizuri biashara zao haraka na wasafiri kutoka nchi ya Kirtland, kabla Mimi, Bwana, sijaipeleka tena theluji juu ya dunia.

2 Na waamke, na kuinuka, na watoke, na wasikae, kwani Mimi, Bwana, ninaamuru.

3 Kwa hiyo, kama watakaa haitakuwa vyema kwao.

4 Na watubu dhambi zao zote, na tamaa zao mbaya zote, mbele zangu, asema Bwana; kwani [a]mali ni nini kwangu? asema Bwana.

5 Acha mali za Kirtland zitolewe kwa ajili ya [a]madeni, asema Bwana. Acha ziende, asema Bwana, na chochote kitakachobakia, acha kibaki mikononi mwenu, asema Bwana.

6 Kwani sina ndege wa angani, na pia samaki baharini, na wanyama milimani? Sijaumba dunia? Je, Mimi sishikilii [a]hatima ya majeshi yote ya mataifa ya dunia?

7 Kwa hiyo, je, sitafanya mahali pa [a]jangwa kuota chipukizi na kuchanua, na kuzaa kwa wingi? Asema Bwana.

8 Je, hakuna nafasi ya kutosha juu ya milima ya [a]Adamu-ondi-Amani, na juu ya mbuga za Olaha [b]Shineha, au [c]nchi ambayo Adamu aliishi, hata ninyi mkatamani kile ambacho ni tone, na kudharau mambo mazito zaidi?

9 Kwa hiyo, njooni huku juu katika nchi ya watu wangu, hata Sayuni.

10 Na mtumishi wangu William Marks awe [a]mwaminifu katika mambo machache, naye atakuwa mtawala juu ya mengi. Na aongoze katikati ya watu wangu katika mji wa Far West, na abarikiwe kwa baraka za watu wangu.

11 Na mtumishi wangu Newel K. Whitney aone aibu kwa kundi la [a]Wanikolai na [b]siri zao zote za machukizo, na udhaifu wote wa nafsi yake mbele zangu, asema Bwana, na aje huku katika nchi ya Adamu-ondi-Amani, na kuwa [c]askofu kwa watu wangu, asema Bwana, siyo kwa maneno bali kwa matendo, asema Bwana.

12 Na tena, ninawaambia, ninamkumbuka mtumishi wangu [a]Oliver Granger; tazama, amini ninamwambia yeye kwamba jina lake litakumbukwa kuwa takatifu kutoka kizazi hadi kizazi, milele na milele, asema Bwana.

13 Kwa hiyo, na apambane kwa dhati kwa ajili ya ukombozi wa Urais wa Kwanza wa Kanisa langu, asema Bwana; na ikiwa ataanguka atainuka tena, kwani [a]dhabihu yake itakuwa takatifu zaidi kwangu Mimi

117 4*a* M&M 104:14.
5*a* M&M 104:78.
6*a* Mdo. 17:26; 1 Ne. 17:36–39.
7*a* Isa. 35:1; M&M 49:24–25.
8*a* M&M 116.
MWM Adamu-ondi-Amani.
b Ibr. 3:13.
c MWM Edeni.
10*a* Mt. 25:23.
11*a* Ufu. 2:6, 15.
b MWM Makundi maovu ya siri.
c MWM Askofu.
12*a* MY wakala aliyeachwa na Nabii ili ashughulikie masuala yake katika Kirtland.
13*a* MWM Dhabihu.

kuliko mafanikio yake, asema Bwana.

14 Kwa hiyo, na aje huku haraka, katika nchi ya Sayuni; na katika wakati ufaao atafanywa kuwa mfanya biashara kwa jina langu, asema Bwana, kwa faida ya watu wangu.

15 Kwa hiyo na mtu yeyote asimdharau mtumishi wangu Oliver Granger, bali na baraka za watu wangu ziwe juu yake milele na milele.

16 Na tena, amini ninawaambia, acha watumishi wangu wote katika nchi ya Kirtland wamkumbuke Bwana Mungu wao, na nyumba yangu pia, kuitunza na kuilinda iwe takatifu, na kuwafukuza wabadili fedha katika wakati wangu Mimi mwenyewe, asema Bwana. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 118

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Far West, Missouri, 8 Julai 1838, kama jibu la ombi, "Tuonyeshe mapenzi yako, Ee Bwana, juu ya Kumi na Wawili."

1–3, Bwana atatoa mahitaji ya familia za Kumi na Wawili; 4–6, Nafasi katika Kumi na Wawili zinajazwa.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Acha mkutano ufanyike haraka; acha Kumi na Wawili wapangwe; na acha watu wateuliwe [a]kujaza nafasi za wale walioanguka.

2 Acha mtumishi wangu [a]Thomas abakie kwa kipindi kifupi katika nchi ya Sayuni, ili kuchapisha neno langu.

3 Acha waliosalia waendelee kuhubiri kutoka sasa, na kama watafanya hivi kwa unyenyekevu wote wa moyo, kwa upole na [a]subira, na [b]uvumilivu, Mimi, Bwana, ninatoa kwao ahadi ya kuwa nitazitunza familia zao; na mlango wenye kuleta matokeo yanayotakiwa utafunguliwa kwa ajili yao, tangu sasa.

4 Na majira ya kuchipua yajayo acha waondoke kwenda kuvuka maji mengi, na huko wakatangaze injili yangu, utimilifu wake, na kulishuhudia jina langu.

5 Acha waondoke kutoka kwa watakatifu wangu katika mji wa Far West, siku ya tarehe ishirini na sita ya Aprili ijayo, kutoka mahali pa kiwanja cha kujenga nyumba yangu, asema Bwana.

6 Acha mtumishi wangu John Taylor, na pia mtumishi wangu John E. Page, na pia mtumishi

118 1*a* Mdo. 1:13, 16–17, 22–26.
2*a* mwm Marsh, Thomas B.
3*a* mwm Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
b mwm Stahimili.

wangu Wilford Woodruff, na pia mtumishi wangu Willard Richards, wateuliwe kujaza nafasi za wale ambao wameanguka, na waarifiwe rasmi juu ya uteuzi wao.

SEHEMU YA 119

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Far West, Missouri, 8 Julai 1838, katika jibu la ombi lake: "Ee Bwana! Onyesha kwa watumishi wako ni kiasi gani cha mali wataka kutoka kwa watu wako kwa ajili ya zaka." Sheria ya zaka, kama inavyofahamika leo, haikuwa imetolewa kwa kanisa kabla ya ufunuo huu. Neno zaka katika sala ambayo imenukuliwa punde na katika mafunuo yaliyopita (64:23; 85:3; 97:11) haikumaanisha tu sehemu moja ya kumi, bali sadaka za hiari, au michango, kwenye mfuko wa Kanisa. Bwana awali alikuwa ametoa sheria kwa Kanisa sheria ya kuweka wakfu na usimamizi wa mali, ambazo waumini (hususani wazee viongozi) waliingia kwa agano ambalo lisingekuwa na mwisho. Kwa sababu ya kushindwa kwa wengi wao kuishi kulingana na agano hili, Bwana aliliondoa kwa muda na badala yake akatoa sheria ya zaka kwa Kanisa lote. Nabii alimwuliza Bwana ni kiasi gani cha mali yao Yeye alikitaka kwa madhumuni yake matakatifu. Jibu lilikuwa ufunuo huu.

1–5, Watakatifu wanapaswa kulipa mali yao ya ziada na halafu kutoa, kama zaka, sehemu moja ya kumi ya mapato yao kila mwaka; 6–7, Utaratibu huu utaitakasa nchi ya Sayuni.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, ninataka mali yao yote ya [a]ziada iwekwe mikononi mwa askofu wa kanisa langu katika Sayuni,

2 Kwa ajili ya ujenzi wa [a]nyumba yangu, na kwa ajili ya kuweka msingi wa Sayuni na kwa ajili ya ukuhani, na kwa ajili ya madeni ya Urais wa Kanisa langu.

3 Na huu ndiyo utakuwa mwanzo wa kulipa [a]zaka kwa watu wangu.

4 Na baada ya hiyo, kwa wale ambao kwa jinsi hiyo wamelipa zaka watalipa sehemu moja ya kumi ya mapato yao ya kila mwaka; na hii itakuwa sheria ya kudumu kwao milele, kwa ajili ya ukuhani wangu mtakatifu, asema Bwana.

5 Amini ninawaambia, itakuwa kwamba wale wote wakusanyikao katika nchi ya [a]Sayuni watalipishwa zaka ya mali zao za ziada, nao watatii sheria hii, au la sivyo wataonekana hawastahili kukaa miongoni mwenu.

119 1*a* M&M 42:33–34, 55; 51:13; 82:17–19.
2*a* M&M 115:8.
3*a* Mal. 3:8–12; M&M 64:23. MWM Lipa zaka, Zaka.
5*a* M&M 57:2–3.

6 Na ninawaambia, kama watu wangu hawatatii sheria hii, kuishika kitakatifu, na kwa sheria hii wakanitakasia nchi ya [a]Sayuni, ili sheria zangu na hukumu zangu zipate kushikwa juu yake, ili ipate kuwa takatifu zaidi, tazama, amini ninawaambia, haitakuwa nchi ya Sayuni kwenu ninyi.

7 Na huu ndiyo utakuwa utaratibu kwa [a]vigingi vyote vya Sayuni. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 120

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Far West, Missouri, 8 Julai 1838, ambao unajulisha juu ya utoaji wa mali zilizotolewa kama zaka kama ilivyotajwa katika ufunuo uliotangulia, sehemu ya 119.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, wakati sasa umefika, ambao [a]itatolewa na baraza, linaloundwa na Urais wa Kwanza wa Kanisa langu, na askofu na baraza lake, na baraza langu kuu; na kwa sauti yangu mwenyewe kwao, asema Bwana. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 121

Sala na unabii ulioandikwa na Joseph Smith Nabii katika waraka wake kwa Kanisa wakati akiwa mfungwa gerezani la Liberty, Missouri, ulioandikwa 20 Machi 1839. Nabii na wenzake kwa miezi kadhaa walikuwa wako gerezani. Msaada wa maombi na rufaa zao zilielekezwa kwa maofisa watendaji na mahakama vilishindwa kuwaletea msaada wowote.

1–6, Nabii amwomba Bwana kwa ajili ya Watakatifu wanaoteseka; 7–10, Bwana amwambia amani; 11–17, Laana i juu ya wale wote waletao vilio vya uongo vya uvunjaji wa sheria dhidi ya watu wa Bwana; 18–25, Hawatakuwa na haki ya kupata ukuhani na watahukumiwa; 26–32, Mafunuo matukufu yameahidiwa kwa wale wastahimilio kwa ujasiri; 33–40, Kwa nini wengi huitwa na wachache huteuliwa; 41–46, Ukuhani unapaswa kutumika tu katika haki.

Ee Mungu, uko wapi? Na ni wapi lilipo hema lifichalo mahali pako pa [a]kujificha?

2 Ni kwa [a]muda gani mkono wako utazuiliwa, na jicho lako, ndiyo, jicho lako lililo safi, lita-

6*a* mwm Sayuni.
7*a* mwm Kigingi.

120 1*a* my zaka.

121 1*a* Zab. 13:1–2; 102:1–2.
2*a* Hab. 1:2.

tazama kutoka katika mbingu za milele maovu ya watu wako na ya watumishi wako, na sikio lako kupenywa kwa vilio vyao?

3 Ndiyo, Ee Bwana, ni kwa [a]muda gani watateseka kwa maovu haya na dhuluma zisizo za kisheria, kabla moyo wako haujalainika kwa ajili yao, na matumbo yako kusikia huruma kwa ajili yao?

4 Ee Bwana Mungu [a]Mwenyezi, muumba wa mbingu, dunia, na bahari, na wa vitu vyote vilivyomo ndani yake, na umtawalaye na kumtiisha ibilisi, na utawala wa giza na usiofahamika wa Sheoli—nyoosha mkono wako; jicho lako na lipenye; hema lako na linyakuliwe; mahali pako pa [b]kujificha na pasifunikwe; sikio lako na litegwe, moyo wako na ulainike, na moyo wako utuonee huruma.

5 Hasira yako na iwake dhidi ya adui zetu; na, katika ghadhabu ya moyo wako, kwa upanga wako [a]tulipie kisasi kwa mabaya tuliyotendewa.

6 Wakumbuke watakatifu wako wanaoteseka, Ee Mungu wetu; na watumishi wako watafurahi katika jina lako milele.

7 Mwanangu, amani iwe katika nafsi yako; [a]taabu yako na mateso yako yatakuwa kwa muda mfupi;

8 Na halafu, kama [a]utastahimili vyema, Mungu atakuinua juu; nawe utawashinda maadui zako wote.

9 [a]Marafiki zako watakuwa waaminifu kwako, nao watakushangilia tena kwa moyo wa upendo na mikono ya urafiki.

10 Wewe bado hujawa kama [a]Ayubu; marafiki zako hawashindani nawe, wala hawatakushtaki kwa uvunjaji wa sheria, kama walivyomfanya Ayubu.

11 Nao wenye kukushtaki kwa uvunjaji wa sheria, matumaini yao yataharibika, na matarajio yao yatayeyukia mbali kama [a]umande uyeyukavyo mbele ya miale iunguzayo ya jua linalochomoza;

12 Na pia kwamba Mungu amepeleka mkono wake na kutia muhuri kubadilisha [a]nyakati na majira, na kupofusha akili zao, ili wasipate kufahamu matendo yake ya ajabu; ili apate kuwajaribu wao pia na kuwachukua wakiwa katika mitego yao wenyewe;

13 Pia kwa sababu mioyo yao imeharibiwa; na mambo ambayo wako tayari kuwaletea wengine, na kupenda kuwaona wengine wakiteseka, na yaje juu yao [a]wenyewe kwa kiwango cha juu kabisa;

14 Ili nao wapate kukatishwa tamaa pia, na matumaini yao yapate kuvunjiliwa mbali;

15 Na siyo miaka mingi kutoka sasa, ili wao na wazao wao wafagiliwe kutoka chini ya mbingu, asema Mungu, ili hata mmoja wao asiachwe hai.

3*a* M&M 109:49.
4*a* MWM Mwenyezi.
b M&M 123:6.
5*a* Lk. 18:7–8.
7*a* MWM Shida.
8*a* 1 Pet. 2:19–23.
MWM Stahimili.
9*a* M&M 122:3.
10*a* MWM Ayubu.
11*a* Ku. 16:14.
12*a* Dan. 2:21.
13*a* Mit. 28:10; 1 Ne. 14:3.

16 Walaaniwe wale wote watakaoinua visigino dhidi ya [a]wapakwa mafuta wangu, asema Bwana, na kulia wametenda [b]dhambi wakati hawajatenda dhambi mbele yangu, asema Bwana, bali wametenda yale yaliyofaa machoni pangu, na yale ambayo niliwaamuru.

17 Lakini wale waliao kuwa uvunjaji wa sheria umetendeka, ndiyo wafanyao kwa sababu wao ni watumwa wa dhambi, nao wenyewe ni [a]wana wa uasi.

18 Na wale waapao kwa uongo dhidi ya watumishi wangu, ili wapate kuwaleta katika utumwa na mauti—

19 Ole wao; kwa sababu [a]wamewakosea wadogo zangu hao watatengwa kwenye [b]ibada za nyumba yangu.

20 [a]Kapu lao halitajaa, nyumba zao na vihenga vyao vitaangamia, na wao wenyewe watadharauliwa na wale walio walaghai.

21 Hawatakuwa na haki ya [a]ukuhani, wala wazao wao baada yao kutoka kizazi hadi kizazi.

22 Ingelikuwa [a]bora kwao kwamba wangefungiwa shingoni jiwe la kusagia, na kutoswa katika kilindi cha bahari.

23 Ole wao wale wote wawasumbuao watu wangu, na kuwafukuza, na kuwaua, na kushuhudia dhidi yao, asema Bwana wa Majeshi; [a]kizazi cha nyoka hakitaepuka hukumu ya jehanamu.

24 Tazama, macho yangu [a]yanaona na kujua matendo yao yote, na nimeiweka tayari [b]hukumu ya haraka katika majira yake, kwa ajili yao wote;

25 Kwani kuna [a]wakati uliopangwa kwa kila mwanadamu, kulingana na [b]matendo yake yatakavyokuwa.

26 Mungu atakupa [a]maarifa kwa njia ya [b]Roho wake Mtakatifu, ndiyo, kwa [c]kipawa chake kisichosemeka cha Roho Mtakatifu, maarifa ambayo hayajafunuliwa tangu ulimwengu kuwepo hadi sasa;

27 Ambayo babu zetu wamekuwa wakiyasubiri kwa shauku kubwa yafunuliwe katika nyakati za mwisho, mababu ambao akili zao zilielekezwa huko na malaika, kama yalivyozuiliwa kwa ajili ya utimilifu wa utukufu wao;

28 Wakati ujao ambamo [a]hakuna kitakachozuiliwa, iwe kuna Mungu mmoja au [b]miungu wengi, watajulikana.

29 Enzi zote na tawala, himaya na nguvu, [a]vitafunuliwa na kuwekwa juu ya wote ambao

16*a* 1 Sam. 26:9; Zab. 105:15.
b 2 Ne. 15:20; Moro. 7:14, 18.
17*a* Efe. 5:6.
19*a* Mt. 18:6. MWM Kosea.
b MWM Ibada.
20*a* Kum. 28:15–20.
21*a* MWM Ukuhani.
22*a* Mt. 18:6; M&M 54:5.
23*a* Mt. 12:34.
24*a* MWM Kujua yote.
b Hel. 8:25. MWM Amua, Hukumu.
25*a* Ayu. 7:1; M&M 122:9.
b MWM Matendo.
26*a* Dan. 2:20–22; M ya I 1:9. MWM Ufunuo.
b M&M 8:2–3.
c MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
28*a* M&M 42:61; 76:7–8; 98:12.
b Zab. 82:1, 6; Yn. 10:34–36; 1 Kor. 8:5–6; M&M 76:58; 132:20; Ibr. 4:1; 5:1–2.
29*a* M&M 101:32.

wamestahimili kwa ujasiri mkubwa kwa ajili ya injili ya Yesu Kristo.

30 Na pia, kama kuna [a]mipaka iliyowekwa kwa mbingu au bahari, au kwa nchi kavu, au kwa jua, mwezi, au nyota—

31 Nyakati za mzunguko wao wote, siku zilizoteuliwa zote, miezi, na miaka, na siku zote za siku zao, miezi, na miaka, na utukufu wao wote, sheria, na nyakati zilizowekwa, zitafunuliwa katika siku za [a]kipindi cha utimilifu wa nyakati—

32 Kulingana na kile ambacho kilitawazwa katikati ya [a]Baraza la [b]Mungu wa Milele, Mungu wa miungu wengine wote kabla ya ulimwengu huu kuwepo, kile ambacho kilipaswa kuhifadhiwa hadi kumalizika na mwisho wake, wakati kila mtu atakapoingia katika [c]uwepo wake wa milele na katika [d]pumziko lake katika mwili usiokufa.

33 Ni kwa muda gani maji yatembeayo yatabaki kuwa machafu? Ni nguvu gani zitazizuia mbingu? Kama vile mwanadamu asivyoweza kunyoosha mkono wake dhaifu kuusimamisha mto Missouri katika mkondo wake uliokusudiwa, au kuugeuza mtiririko wake kwenda juu, vivyo hivyo hawezi kumzuia Mwenyezi kumwaga chini [a]maarifa kutoka mbinguni juu ya vichwa vya Watakatifu wa Siku za Mwisho.

34 Tazama, wengi [a]huitwa, lakini wachache [b]huteuliwa. Na ni kwa nini hawakuteuliwa?

35 Kwa sababu mioyo yao imekuwa juu ya mambo ya [a]ulimwengu huu, na kutafuta kupata [b]heshima kutoka kwa wanadamu, kwamba hawajifunzi somo hili moja—

36 Kwamba [a]haki za ukuhani zimeungana na hazitenganishwi na [b]nguvu za mbinguni, na kwamba nguvu za mbinguni haziwezi kudhibitiwa wala kutawaliwa isipokuwa tu kwa kanuni za [c]haki.

37 Ni kweli, kwamba zinaweza kutunukiwa juu yetu; lakini tutakapojaribu [a]kuficha [b]dhambi zetu, au kuridhisha [c]kiburi chetu, tamaa yetu ya makuu, au kutumia katika udhibiti au utawala au ulazimishaji juu ya nafsi za wanadamu, katika kiwango chochote kisicho cha haki, tazama, mbingu [d]hujitoa zenyewe; Roho wa Bwana husikitika; na mara akijitoa, Amina kwa ukuhani au mamlaka ya mtu yule.

30 *a* Ayu. 26:7–14; Zab. 104:5–9; Mdo. 17:26.
31 *a* MWM Kipindi.
32 *a* MWM Baraza Mbinguni.
b Kum. 10:17.
c MWM Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, uwezekano wa kuwa kama Baba wa Mbinguni.
d MWM Pumzika.
33 *a* M&M 128:19. MWM Maarifa.
34 *a* Mt. 20:16; 22:1–14; M&M 95:5–6. MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito.
b MWM Alichagua, Chagua, Chaguliwa (kitenzi).
35 *a* MWM Malimwengu.
b Mt. 6:2; 2 Ne. 26:29.
36 *a* MWM Mamlaka; Ukuhani.
b MWM Uwezo.
c MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
37 *a* Mit. 28:13.
b MWM Dhambi.
c MWM Kiburi.
d M&M 1:33.

38 Tazama, kabla hajatambua, ameachwa peke yake, [a]kuupiga mateke miiba, [b]kuwatesa watakatifu, na kupigana na Mungu.

39 Tumejifunza kwa uzoefu wa kuhuzunisha kwamba ni [a]kawaida na ni tabia ya karibu wanadamu wote, kwamba mara wapatapo mamlaka kidogo, kama wanavyodhani, huanza mara moja kuyatumia mamlaka hayo bila haki.

40 Kwa sababu hiyo wengi huitwa, lakini wachache huteuliwa.

41 Hakuna nguvu au uwezo unaoweza au upaswao kudumishwa kwa njia ya ukuhani, isipokuwa tu kwa njia ya [a]ushawishi, kwa [b]uvumilivu, kwa upole na unyenyekevu, na kwa upendo usio unafiki;

42 Kwa wema, na maarifa safi, ambayo yataikuza sana nafsi isiyo na [a]unafiki, na isiyo na [b]hila—

43 [a]Kukemea kwa ukali kwa wakati wake, utakapokuwa umeongozwa na Roho Mtakatifu; na halafu baadaye kuonyesha ongezeko la [b]upendo kwa yule uliyemkemea, asije akakudhania wewe kuwa ni adui yake;

44 Ili apate kujua kwamba uaminifu wako ni imara zaidi kuliko kamba za mauti.

45 Na moyo wako pia uwe umejaa hisani kwa wanadamu wote, na kwa jamaa ya waaminio, na [a]wema uyapambe [b]mawazo yako bila kukoma; ndipo kujiamini kwako kutakuwa imara katika uwepo wa Mungu; na mafundisho ya ukuhani yatatonatona juu ya roho yako kama [c]umande utokao mbinguni.

46 [a]Roho Mtakatifu atakuwa mwenzi wako daima, na fimbo yako ya kifalme fimbo isiyobadilika ya haki na ukweli; na [b]utawala wako utakuwa utawala usio na mwisho, na usio wa njia ya kulazimisha utatiririka kwako milele na milele.

SEHEMU YA 122

Neno la Bwana kwa Joseph Smith Nabii, wakati akiwa mfungwa gerezani huko Liberty, Missouri. Sehemu hii ni dondoo kutoka katika waraka kwa Kanisa ulioandikwa 20 Machi 1839 (ona kichwa cha habari kwa sehemu ya 121).

1–4, Miisho ya dunia italiulizia jina la Joseph Smith; 5–7, Hatari na mateso yake yote vitampa uzoefu na yatakuwa kwa faida yake;

38 *a* Mdo. 9:5.
b MWM Mateso, Tesa.
39 *a* MWM Mwanadamu wa Tabia ya Asili.
41 *a* 1 Pet. 5:1–3.
b 2 Kor. 6:4–6.
42 *a* Yak. (Bib.) 3:17.
b MWM Hila.
43 *a* MWM Rudi, Kurudiwa.
b MWM Hisani; Upendo.
45 *a* MWM Wema.
b MWM Mawazo.
c Kum. 32:1–2; M&M 128:19.
46 *a* MWM Roho Mtakatifu.
b Dan. 7:13–14.

8–9, Mwana wa Mtu amejishusha chini yao wote.

Miisho ya dunia italiulizia [a]jina lako, na wapumbavu watakudhihaki, na jehanamu itapigana nawe kwa hasira;

2 Wakati walio safi moyoni, na wenye hekima, na walio maarufu, na walio wema, watautafuta [a]ushauri, na mamlaka, na baraka kutoka chini ya mkono wako daima.

3 Na watu wako kamwe hawatakugeuka kwa ushuhuda wa wasaliti.

4 Na ingawa uwezo wao utakutupa katika matatizo, na gerezani, wewe utaheshimika; na lakini kwa [a]muda mfupi na sauti yako itakuwa ya kutisha sana katikati ya adui zako kuliko [b]simba mkali, kwa sababu ya uadilifu wako; na Mungu wako atakusimamia milele na milele.

5 Kama wewe umeitwa kupita kwenye taabu, kama wewe uko katika hatari miongoni mwa ndugu wa uongo; kama wewe uko katika hatari kati ya wezi; kama wewe ukiwa katika hatari nchi kavu au baharini;

6 Kama wewe utashtakiwa kwa namna zote za shutuma za uongo; kama adui zako watakuwa juu yako; kama watakuondoa wewe kutoka kwenye jumuia ya baba yako na mama na kaka na dada zako; na kama kwa upanga uliotolewa alani mwake adui zako watakuondoa kutoka kifuani mwa mke wako, na kwa wazao wako, na kwa mwana wako wa kwanza, ingawa ni wa umri wa miaka sita tu, atang'ang'ania kwenye mavazi yako, naye atasema, Baba yangu, baba yangu, kwa nini huwezi kukaa na sisi? Ee, baba yangu watu hawa wanakwenda kukufanya nini? na kama hivyo watamwondoa kwako kwa upanga, nawe utaburuzwa kwenda gerezani, na adui zako watakuzungukazunguka kama [a]mbwa mwitu wakitafuta damu ya mwanakondoo;

7 Na kama utatupwa ndani ya shimo, au katika mikono ya wauaji, na hukumu ya kifo ikapitishwa juu yako; kama utatupwa [a]kilindini; kama mawimbi makali yatakula njama dhidi yako; kama upepo mkali utakuja kuwa adui yako; kama mbingu zitakusanya giza, na vitu vyote vya asili vikiungana ili kuzingira njia yako; na juu ya yote, kama mataya yale ya [b]jehanamu yataachama kinywa wazi kwa ajili yako, fahamu wewe, mwanangu, kwamba mambo haya yote yatakupa wewe [c]uzoefu, na yatakuwa kwa faida yako.

8 [a]Mwana wa Mtu [b]amejishusha chini yao wote. Je, wewe u mkuu kuliko yeye?

9 Kwa hiyo, shikilia njia yako, na ukuhani [a]utabakia nawe;

122 1*a* JS—H 1:33.
2*a* mwm Ushauri.
4*a* M&M 121:7–8.
b 3 Ne. 20:16–21; 21:12.
6*a* Lk. 10:3.
7*a* Yon. 2:3–6.
b 2 Sam. 22:5–7; JS—H 1:15–16.
c 2 Kor. 4:17; Ebr. 12:10–11; 2 Ne. 2:11.
8*a* mwm Mwana wa Mtu.
b Ebr. 2:9, 17–18; M&M 76:107; 88:6.
9*a* M&M 90:3.

kwa kuwa [b]mipaka yao imewekwa, hawawezi kuivuka. [c]Siku zako zinafahamika, na miaka yako haitahesabika kuwa michache; kwa hiyo, [d]usiogope mwanadamu awezacho kukutenda, kwani Mungu atakuwa pamoja nawe milele na milele.

SEHEMU YA 123

Wajibu wa Watakatifu kuhusu watesi wao, kama ulivyoandikwa na Joseph Smith Nabii, wakati akiwa mfungwa gerezani huko Liberty, Missouri. Sehemu hii ni nukuu kutoka kwenye waraka kwa Kanisa wa 20 Machi 1839 (ona kichwa cha habari kwa sehemu ya 121).

1–6, Watakatifu wanapaswa kukusanya na kuchapisha historia ya taabu na mateso yao; 7–10, Roho yule yule aliyeanzisha mafundisho ya imani za uongo pia huongoza kuteswa kwa Watakatifu; 11–17, Wengi miongoni mwa madhehebu yote hatimaye wataupokea ukweli.

Na tena, tungelipendekeza ili mpate kufikiria utaratibu wa watakatifu wote kukusanya ukweli wote, juu ya mateso na maonevu yote waliyofanyiwa na watu wa Jimbo hili;

2 Na pia wa mali yote na kiwango cha uharibifu wamefanyiwa, wa sifa na majeraha ya binafsi, vile vile ya mali isiyohamishika;

3 Na pia majina ya watu wote ambao wameshiriki katika unyanyasaji wao, kwa kadiri watakavyoweza kuwapata na kuwagundua.

4 Na pengine kamati yaweza kuteuliwa kuchunguza mambo haya, na kuchukua maelezo na hati za viapo; na pia kukusanya makala za kashfa ambazo zimezagaa;

5 Na yote yaliyomo katika magazeti, na katika ensaiklopidia, na historia zote za kashfa ambazo zimechapishwa, na zinazoandikwa, na ni nani, na kuwakilisha mlolongo mzima wa uhuni wa kiibilisi na uovu na matumizi ya mauaji ambayo yamefanyika kwa watu hawa—

6 Ili tupate si kuchapisha tu kwa walimwengu wote, bali kuzikabidhi kwa viongozi wa serikali katika giza na rangi yao yote ya jehanamu, kama jitihada za mwisho ambazo zimeunganishwa kwetu sisi na Baba yetu wa Mbinguni, kabla hatujaweza kudai kiukamilifu na kwa utimilifu ahadi ile ambayo itamwita yeye kutoka mahali pake pa [a]kujificha; na pia ili taifa lote lipate kuachwa pasipo udhuru kabla yeye hajatuma uwezo wa mkono wake wenye nguvu.

7 Ni kazi muhimu ambayo tunadaiwa na Mungu, na malaika,

9 *b* Mdo. 17:26.
c M&M 121:25.
d Neh. 4:14; Zab. 56:4; 118:6; Mit. 3:5–6; Isa. 51:7; Lk. 12:4–5; 2 Ne. 8:7; M&M 3:7; 98:14.

123 6 *a* M&M 101:89; 121:1, 4.

ambao pamoja nao tutasimamishwa, na pia kwetu sisi wenyewe, kwa wake zetu na watoto, ambao wamefanywa wainame chini kwa huzuni, uchungu, na mashaka, chini ya mkono uliolaaniwa wa uuaji, udhalimu, na ukandamizaji, ukisaidiwa na kuhimizwa na kuungwa mkono na nguvu za yule roho ambaye kwa nguvu sana ameyapiga ribiti mafundisho ya imani ya mababu, ambao wamerithisha uongo, juu ya mioyo ya watoto, na kuujaza ulimwengu kwa machafuko, na amekuwa akikua na kuwa imara na imara, na sasa ndiyo chimbuko kuu la uharibifu wote, na [a]ulimwengu mzima unaugulia chini ya uzito wa uovu wake.

8 Ni [a]nira ya chuma, ni kamba ngumu; wao ndiyo zile pingu za mikono, na minyororo, na vipingamizi, na pingu za miguu za jehanamu.

9 Kwa hiyo ni kazi muhimu tunayodaiwa, siyo tu kwa wake zetu wenyewe na watoto, bali kwa wajane na kwa wasio na baba, ambao waume zao na baba zao [a]wameuawa chini ya mkono wake wa chuma;

10 Ambaye giza na matendo yake meusi yanatosha kuifanya jehanamu yenyewe itetemeke, na kusimama kwa mshangao na woga, na mikono ya ibilisi mwenyewe itetemeke na kupooza.

11 Na pia ni kazi muhimu ambayo tunadaiwa na kizazi chote kinachochipukia, na kwa wote walio safi moyoni—

12 Kwani bado wako wengi duniani miongoni mwa vikundi vyote, vyama, na madhehebu, ambao [a]wanapofushwa na ustadi wa ujanja wa wanadamu, ambao huvizia ili kudanganya, na ambao huzuiliwa kuupata ukweli kwa sababu tu [b]hawajui mahali pa kuupata—

13 Kwa hiyo, kwamba yatupasa kutumia maisha yetu katika kuyaleta kwenye nuru mambo yote ya giza, [a]yaliyofichwa; kadiri tunavyoyajua; nayo hakika yanafunuliwa kutoka mbinguni—

14 Haya ndiyo yanapaswa kushughulikiwa kwa bidii zaidi.

15 Acha mtu yeyote asiyahesabu kama ni mambo madogo madogo; kwani kuna mengine yajayo hapo baadaye, kuhusiana na watakatifu, ambao wanayategemea mambo haya.

16 Mnajua, ndugu, kwamba merikebu kubwa [a]hufaidika kwa kiwango kikubwa sana na usukani mdogo wakati wa dhoruba, kwa kuwekwa katika kutenda kazi dhidi ya upepo na mawimbi.

17 Kwa hiyo, ndugu wapendwa, kwa [a]furaha na tufanye mambo yote yaliyo katika uwezo wetu; na ndipo tusimame imara, kwa uhakika mkubwa, kuuona [b]wokovu wa Mungu, na kwa mkono wake kufunuliwa.

7 *a* Musa 7:48–49.
8 *a* MWM Nira.
9 *a* M&M 98:13; 124:54.
12 *a* Kol. 2:8; M&M 76:75.
b 1 Ne. 8:21–23.
13 *a* 1 Kor. 4:5.
16 *a* Yak. (Bib.) 3:4; Alma 37:6–7; M&M 64:33.
17 *a* M&M 59:15.
b Ku. 14:13.

SEHEMU YA 124

Ufunuo uliotolewa kwa Joseph Smith Nabii, huko Nauvoo, Illinois, 19 Januari 1841. Kwa sababu ya kuongezeka kwa mateso na taratibu zisizo za kisheria dhidi yao kutoka kwa maofisa wa serikali, Watakatifu walilazimika kuhama Missouri. Amri ya kuuawa iliyotolewa na Lilburn W. Boggs, gavana wa Missouri, 27 Oktoba 1838, iliwaacha wasiwe na uchaguzi mbadala. Katika mwaka 1841, wakati ufunuo huu ulipotolewa, mji wa Nauvoo, uliokuwa kiwanja cha kijiji cha zamani cha Commerce, Illinois, ulikuwa umejengwa na Watakatifu, na hapa ndiyo makao makuu ya Kanisa yalipoanzishwa.

1–14, Joseph Smith anaamriwa kutoa tamko la dhati la injili kwa rais wa Marekani, magavana, na watawala wa mataifa yote; 15–21, Hyrum Smith, David W. Patten, Joseph Smith Mkubwa na wengine miongoni mwa walio hai na wafu wamebarikiwa kwa sababu ya uadilifu na wema wao; 22–28, Watakatifu wanaamriwa kujenga nyumba kwa ajili ya kuwakarimu wageni na hekalu katika Nauvoo; 29–36, Ubatizo kwa ajili ya wafu lazima ufanyike hekaluni; 37–44, Watu wa Bwana daima hujenga mahekalu kwa ajili ya kufanya ibada takatifu; 45–55, Watakatifu wanasamehewa kujenga hekalu katika Wilaya ya Jackson kwa sababu ya manyanyaso ya maadui zao; 56–83, Maelekezo yanatolewa kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba ya Nauvoo; 84–96, Hyrum Smith anaitwa kuwa patriaki, ili kupokea funguo, na kusimama mahali pa Oliver Cowdery; 97–122, William Law na wengine wanashauriwa katika kazi zao; 123–145, Viongozi wakuu na wa maeneo watajwa, pamoja na wajibu wao na akidi analoshiriki.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwako, mtumishi wangu Joseph Smith, ninapendezwa na matoleo yako na kukubali kwako, ulikofanya; kwani kwa kusudi hili nilikusimamisha, ili nipate kuonyesha hekima yangu kwa walio [a]wadhaifu wa dunia.

2 Sala zako zinakubalika mbele zangu; na katika kuyajibu ninakuambia kwamba sasa unaitwa haraka kufanya tangazo la dhati la injili yangu, na la [a]kigingi hiki ambacho nimekipanda ili kuwa jiwe la kona la Sayuni, ambalo litanakishiwa kwa kusafishwa mfano wa kasri.

3 Tangazo hili litafanywa kwa [a]wafalme wote wa ulimwengu, kwenye kona zake nne, kwa mheshimiwa rais mteule, na kwa waheshimiwa magavana wa taifa ambamo wewe unaishi, na kwa mataifa yote yaliyotawanyika duniani.

4 Acheni liandikwe katika

124 1*a* 1 Kor. 1:26–28; M&M 1:19; 35:13. 2*a* mwm Kigingi. 3*a* Zab. 119:46; Mt. 10:18; M&M 1:23.

roho ya [a]unyenyekevu na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, ambaye atakuwa ndani yako wakati wa kuliandika hilo;

5 Kwani itatolewa kwako na Roho Mtakatifu kujua mapenzi yangu juu ya wafalme na wenye mamlaka hao, hata yale yatakayowapata wakati ujao.

6 Kwani, tazama, karibu nitawaita waitii nuru na utukufu wa Sayuni, kwani majira yaliyoamriwa yamewadia ya kumpendelea.

7 Waitieni, kwa hiyo, kwa tangazo la sauti kubwa, na kwa ushuhuda wenu, msiwaogope, kwani wao ni kama [a]nyasi, na utukufu wao wote ni kama maua yake ambayo ghafla huanguka, ili nao wapate kuachwa pasipo udhuru—

8 Na ili nipate kuwatembelea siku ya kujiliwa, wakati nitakapofunua uso wa maficho yangu, kuweka fungu la mdhalimu miongoni mwa wanafiki, ndiko kutakuwako na [a]kusaga meno, kama watawakataa watumishi wangu na ushuhuda wangu ambao nimewafunulia.

9 Na tena, nitawajilia na kulainisha mioyo yao, wengi wao kwa faida yenu, ili mpate neema machoni mwao, ili waweze kuja kwenye [a]nuru ya kweli, na Wayunani kwa kuipandisha au kuinuliwa kwa Sayuni.

10 Kwani siku ya kuwajilia yaja haraka, katika [a]saa msiyodhania; na wapi kutakuwa usalama wa watu wangu, na kimbilio kwa wale watakaoachwa nao?

11 Amkeni, enyi wafalme wa dunia! Njooni ninyi, enyi njooni, pamoja na dhahabu na fedha zenu, ili muwasaidie watu wangu, hata kwenye nyumba ya mabinti wa Sayuni.

12 Na tena, amini ninakuambia, acha mtumishi wangu Robert B. Thompson akusaidie kuliandika tangazo hili, kwani Mimi ninapendezwa naye, na kwamba awe pamoja nawe;

13 Acheni yeye, kwa sababu hiyo, atasikiliza ushauri wako, na mimi nitambariki kwa wingi wa baraka; acheni awe mwaminifu na mkweli katika mambo yote tangu sasa na kuendelea, naye atakuwa mkuu machoni pangu;

14 Lakini acheni akumbuke kwamba [a]usimamizi wake nitaudai kutoka kwake.

15 Na tena, amini ninakuambia, amebarikiwa mtumishi wangu [a]Hyrum Smith; kwani Mimi, Bwana, ninampenda kwa sababu ya [b]uadilifu wa moyo wake, na kwa sababu yeye hupenda yaliyo ya haki mbele zangu, asema Bwana.

16 Tena, acha mtumishi wangu John C. Bennett akusaidie katika kazi zako katika kupeleka neno langu kwa wafalme na watu wa dunia, na asimame

4 *a* MWM Pole, Upole.
7 *a* Zab. 103:15–16; Isa. 40:6–8; 1 Pet. 1:24–25.
8 *a* Mt. 8:12; Alma 40:13; M&M 101:91; 112:24.
9 *a* Isa. 60:1–4. MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
10 *a* Mt. 24:44; JS—M 1:48.
14 *a* MWM Msimamizi, Usimamizi.
15 *a* MWM Smith, Hyrum.
b MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.

pamoja nawe, hata wewe mtumishi wangu Joseph Smith, katika saa ya mateso; na thawabu yake haitakosekana kama ataupokea [a]ushauri.

17 Na kwa sababu ya upendo wake atakuwa mkuu, kwani atakuwa wangu kama atafanya hili, asema Bwana. Nimeiona kazi aliyoifanya, ambayo ninaikubali kama ataendelea, na nitamvika taji la baraka na utukufu mkuu.

18 Na tena, ninakuambia kwamba ni mapenzi yangu kuwa mtumishi wangu Lyman Wight aendelee katika kuhubiri kwa ajili ya Sayuni, katika roho ya unyenyekevu, akinikiri mimi mbele ya ulimwengu; nami nitamnyanyua juu kama vile mbawa za [a]tai; naye atajipatia utukufu na heshima kwake yeye mwenyewe na kwa jina langu.

19 Ili atakapomaliza kazi yake nipate kumpokea kwangu, hata kama nilivyomfanya mtumishi wangu [a]David Patten, ambaye yupo pamoja nami hivi sasa, na pia mtumishi wangu [b]Edward Partridge, na pia mtumishi wangu mzee [c]Joseph Smith, Mkubwa, ambaye hukaa [d]pamoja na Ibrahimu mkono wake wa kuume, na yeye yu mtakatifu na mbarikiwa, kwa kuwa yeye ni wangu.

20 Na tena, amini ninawaambia, mtumishi wangu George Miller hana [a]hila; aweza kuaminiwa kwa sababu ya uadilifu wa moyo wake; na kwa mapenzi aliyonayo kwa ushuhuda wangu Mimi, Bwana, ninampenda yeye.

21 Kwa hiyo ninawaambia, ninatia muhuri juu ya kichwa chake ofisi ya [a]uaskofu, kama kwa mtumishi wangu Edward Partridge, ili apate kupokea vilivyowekwa wakfu kwa nyumba yangu, ili apate kutoa baraka juu ya vichwa vya maskini wa watu wangu, asema Bwana. Acheni mtu yeyote asimdharau mtumishi wangu George, kwani yeye ataniheshimu Mimi.

22 Acha mtumishi wangu George, na mtumishi wangu Lyman, na mtumishi wangu John Snider, na wengineo, wajenge [a]nyumba kwa jina langu, kama vile mtumishi wangu Joseph atakavyowaonyesha, juu ya mahali ambapo yeye pia atawaonyesha.

23 Nayo itakuwa kwa ajili ya nyumba ya kuishi, nyumba ambayo wageni wanaweza kuja kutoka mbali na kuishi ndani yake; kwa hiyo acheni iwe nyumba nzuri, yenye kustahili kukubalika kote, ili [a]mgeni aliyechoka aweze kupata afya na usalama wakati atakapokuwa akitafakari neno la Bwana; na [b]jiwe la kona nililolichagua kwa ajili ya Sayuni.

24 Nyumba hii itakuwa maka-

16 *a* MWM Ushauri.
18 *a* Ku. 19:4; Isa. 40:31.
19 *a* M&M 124:130. MWM Patten, David W.
b MWM Partridge, Edward.
c MWM Smith, Joseph, Mkubwa.
d M&M 137:5.
20 *a* MWM Hila.
21 *a* M&M 41:9. MWM Askofu.
22 *a* M&M 124:56–60.
23 *a* Kum. 31:12; Mt. 25:35, 38.
b M&M 124:2.

zi yenye afya ikiwa itajengwa kwa jina langu, na kama gavana ambaye atateuliwa kwa ajili yake hataruhusu uchafu wowote kuja juu yake. Itakuwa takatifu, au kama sivyo Bwana Mungu wenu hatakaa ndani yake.

25 Na tena, amini, ninawaambia, acheni watakatifu wangu wote waje kutoka mbali.

26 Na wapelekeni wajumbe upesi, ndiyo, wajumbe walioteuliwa, na waambieni: Njooni, pamoja na dhahabu zenu zote, na fedha zenu, na mawe yenu ya thamani, na pamoja na vitu vyenu vyote vya kale; na pamoja na wale wote wenye ujuzi wa vitu vya kale, watakao kuja, na waje, na leteni mtidhari, mberoshi, na mteshuri, pamoja na miti yote mizuri ya dunia;

27 Na pamoja na chuma, na shaba nyekundu, na shaba nyeupe, na zinki, pamoja na vitu vyenu vyote vya thamani vya duniani; na jengeni [a]nyumba kwa jina langu, ili Aliye Juu Sana [b]akae ndani yake.

28 Kwani hakuna mahali palipopatikana juu ya dunia ambapo yeye aweza kuja na [a]kurejesha tena kile ambacho kilipotea kwenu, au kile alichokiondolea mbali, hata utimilifu wa ukuhani.

29 Kwani [a]kisima cha ubatizo hakiko juu ya dunia, ili wao, watakatifu wangu, waweze [b]kubatizwa kwa ajili ya wale waliokufa—

30 Kwani ibada hii ni mali ya nyumba yangu, na haiwezi kukubaliwa kwangu, isipokuwa tu katika siku ya ufukara wenu, ambapo hamna uwezo wa kunijengea nyumba.

31 Lakini ninawaamuru ninyi, ninyi watakatifu wangu wote, [a]kunijengea nyumba; na ninatoa kwenu muda wa kutosha kunijengea nyumba; na kwa wakati huo ubatizo wenu nitaukubali.

32 Lakini tazama, muda huu ukiisha ubatizo wenu kwa ajili ya wafu hautakubaliwa kwangu; na kama hamkufanya mambo haya mwishoni mwa muda huu mtakataliwa kama kanisa, pamoja na wafu wenu, asema Bwana Mungu wenu.

33 Kwani amini ninawaambia, kwamba baada ya kupata muda wa kutosha kunijengea nyumba, ambamo ndani yake ibada ya kubatizwa kwa ajili ya wafu itafanyika, na kwa ajili hiyo hii iliwekwa tangu kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu, ubatizo wenu kwa ajili ya wafu wenu hautaweza kukubalika kwangu;

34 Kwani ndani yake [a]funguo za ukuhani mtakatifu zimewekwa, ili mpate kupokea heshima na utukufu.

27 *a* M&M 109:5. MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.
b Ku. 25:8; M&M 97:15–17.
28 *a* MWM Urejesho wa Injili.
29 *a* M&M 128:13.
b 1 Kor. 15:29; M&M 127:6; 138:33. MWM Batiza, Ubatizo—Ubatizo kwa ajili ya wafu; Wokovu kwa ajili ya Wafu.
31 *a* M&M 97:10.
34 *a* M&M 110:14–16. MWM Funguo za Ukuhani.

35 Na baada ya wakati huu, ubatizo wenu kwa ajili ya wafu, kwa wale ambao wametawanyika mbali, hautakubalika kwangu, asema Bwana.

36 Kwani imeamuriwa kwamba katika Sayuni, na katika vigingi vyake, na katika Yerusalemu, sehemu zile ambazo nimeziteua kwa ajili ya [a]kimbilio, zitakuwa ndizo sehemu zenu kwa ajili ya ubatizo wa wafu wenu.

37 Na tena, amini ninawaambia, ni namna gani [a]uoshwaji wenu utakubaliwa kwangu, isipokuwa tu mmeufanya katika nyumba ambayo mmeijenga kwa jina langu?

38 Kwani, kwa ajili hii, nilimwamuru Musa kwamba lazima ajenge [a]hema takatifu, kwamba waibebe pamoja nao huko nyikani, na wajenge [b]nyumba katika nchi ya ahadi, ili ibada zile zipate kufunuliwa zile ambazo zilifichwa kabla ya ulimwengu kuwako.

39 Kwa hiyo, amini ninawaambia, kwamba [a]kupakwa kwenu mafuta, na kuoshwa kwenu, na [b]ubatizo wenu kwa ajili ya wafu, na [c]makusanyiko yenu ya kiroho, na kumbukumbu zenu za [d]dhabihu kwa wana wa Lawi, na kwa ajili ya mafunuo yenu katika [e]mahali penu patakatifu zaidi ambamo ndani yake mnapokea maagizo, na sheria na hukumu zenu, kwa ajili ya kuanza kwa mafunuo na msingi wa Sayuni, na kwa ajili ya utukufu, heshima, na endaomenti kwa manispaa zake zote, zimefanywa kuwa thabiti kwa ibada ya nyumba yangu takatifu, ambayo watu wangu daima wanaamriwa kuijenga kwa jina langu takatifu.

40 Na amini ninawaambia, acheni nyumba hii na ijengwe kwa jina langu, ili nipate kuzifunua ibada zangu ndani yake kwa watu wangu;

41 Kwani nimekubali [a]kulifunulia kanisa langu mambo ambayo [b]yalifichwa tangu kabla ya kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, mambo yale yahusuyo kipindi hiki cha [c]utimilifu wa nyakati.

42 Na [a]Mimi nitamwonyesha mtumishi wangu Joseph mambo yote yahusuyo nyumba hii, na ukuhani wake, na mahali ambapo juu yake itajengwa.

43 Nanyi mtaijenga juu ya mahali ambapo mmefikiria kuijenga, kwani hapo ndipo mahali sahihi nilipowachagulia ninyi kuijenga.

44 Kama mtafanya kazi kwa nguvu zenu zote, nitapaweka wakfu mahali pale ili pafanywe kuwa [a]patakatifu.

45 Na kama watu wangu wa-

36*a* Isa. 4:5–6.
37*a* MWM Osha, Oshwa, Uoshaji.
38*a* Ku. 25:1–9; 33:7. MWM Hema.
b MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.
39*a* Ku. 29:7. MWM Paka mafuta.
b MWM Ibada—Ibada zifanywazo kwa niaba ya wafu.
c M&M 88:117.
d M&M 13; 84:31; 128:24; JS—H 1:69.
e Eze. 41:4; M&M 45:32; 87:8; 101:22.
41*a* M ya I 1:9.
b M&M 121:26–32.
c Efe. 1:9–10; M&M 27:13; 112:30.
42*a* M&M 95:14–17.
44*a* MWM Takatifu.

taisikiliza sauti yangu, na sauti ya [a]watumishi wangu ambao nimewateua kuwaongoza watu wangu, tazama, amini ninawaambia, wao hawataondoshwa kutoka mahali pao.

46 Lakini kama hawataisikiliza sauti yangu, wala sauti ya watu hawa ambao nimewateua, wao hawatabarikiwa, kwa sababu wanachafua ardhi yangu takatifu, na ibada zangu takatifu, na katiba, na maneno yangu matakatifu ambayo nayatoa kwao.

47 Na itakuwa kwamba kama mtaijenga nyumba kwa jina langu, na msifanye mambo yale nisemayo, mimi sitafanya [a]kiapo ambacho ninakifanya kwenu, wala kutimiza ahadi ambazo ninyi mnazitegemea kutoka kwangu, asema Bwana.

48 Kwani [a]badala ya baraka, ninyi, kwa matendo yenu wenyewe, hujiletea laana, ghadhabu, uchungu wa hasira, na hukumu juu ya vichwa vyenu wenyewe, kwa upumbavu wenu, na kwa machukizo yenu yote, ambayo mnayafanya mbele zangu, asema Bwana.

49 Amini, amini, ninawaambia kwamba nitoapo amri kwa wana wa watu wowote kuifanya kazi kwa jina langu, na wana wale wa watu wakienda kwa nguvu zao zote na vile vyote walivyonavyo kuifanya kazi ile, na bila kuacha [a]juhudi yao, na adui zao wakaja juu yao na kuwazuia kufanya kazi ile, tazama, ninakuwa sina budi kuacha [b]kuidai kazi ile kutoka mikononi mwa wanadamu, lakini huyapokea matoleo yao.

50 Na uovu na uvunjaji wa sheria na amri zangu takatifu [a]nitawajilia juu ya vichwa vya wale waliozuia kazi yangu, hadi [b]kizazi cha tatu na cha nne, endapo [c]hawatatubu, na kunichukia mimi, asema Bwana Mungu.

51 Kwa hiyo, kwa sababu hii nimekubali matoleo ya wale ambao niliwaamuru kuujenga mji na [a]nyumba kwa jina langu, katika [b]wilaya ya Jackson, Missouri, na wakazuiliwa na maadui zao, asema Bwana Mungu wenu.

52 Nami nitajibu [a]hukumu, ghadhabu, na uchungu wa hasira, maombolezo, na machungu, na kusaga meno juu ya vichwa vyao, hata kizazi cha tatu na cha nne, ilimradi kama hawatatubu, na hawatanichukia, asema Bwana Mungu wenu.

53 Na hii naifanya mfano kwenu, kwa ajili ya kuwafariji ninyi kuhusu wale wote ambao wameamriwa kufanya kazi na wakazuiliwa kwa mikono ya maadui zao, na kwa ukandamizaji, asema Bwana Mungu wenu.

54 Kwani Mimi ndimi Bwana Mungu wenu, nami nitawaokoa ndugu zenu wale wote ambao wamekuwa [a]wasafi moyoni, na

45 *a* M&M 1:38. MWM Nabii.
47 *a* MWM Kiapo.
48 *a* Kum. 28:15.
49 *a* MWM Bidii.
b M&M 56:4; 137:9.
50 *a* Mos. 12:1.
b Kum. 5:9; M&M 98:46–47.
c MWM Toba, Tubu.
51 *a* M&M 115:11.
b MWM Wilaya ya Jackson, Missouri (Marekani).
52 *a* M&M 121:11–23.
54 *a* MWM Safi na Isiyo safi.

[b]wakauawa katika nchi ya Missouri, asema Bwana.

55 Na tena, amini ninawaambia, ninawaamuru tena kuijenga [a]nyumba kwa jina langu, hata katika mahali hapa, ili mpate [b]kujithibitisha wenyewe kwangu kwamba mu waaminifu katika mambo yote yale nitayowaamuru, ili nipate kuwabariki, na kuwavika kwa heshima, kutokufa, na uzima wa milele.

56 Na sasa ninawaambia, kwa kuhusiana na [a]nyumba yangu ya kuishi ambayo nimewaamuru kuijenga kwa ajili ya kuishi wageni, acheni ijengwe kwa jina langu, na acheni jina langu litajwe juu yake, na mtumishi wangu Joseph na nyumba yake wapate nafasi ndani yake, kutoka kizazi hadi kizazi.

57 Kwani mpako huu wa mafuta nimeuweka juu ya kichwa chake, ili baraka zake pia ziwekwe juu ya uzao wake baada yake.

58 Na kama vile nilivyosema kwa [a]Ibrahimu kuhusu makabila za dunia, hivyo ndivyo ninavyosema kwa mtumishi wangu Joseph: Katika wewe na katika [b]uzao wako kabila zote za dunia zitabarikiwa.

59 Kwa hiyo, acheni mtumishi wangu Joseph na uzao wake baada yake yeye wapate nafasi katika nyumba hiyo, kutoka kizazi hadi kizazi, milele na milele, asema Bwana.

60 Na acheni jina la nyumba hiyo iitwe Nyumba ya Nauvoo; na acheni iwe makazi ya kupendeza kwa mwanadamu, na mahali pa kupumzika kwa msafiri aliyechoka, ili apate kutafakari utukufu wa Sayuni, na utukufu wa hili, jiwe lake la kona;

61 Ili apate pia kupokea ushauri kutoka kwa wale ambao nimewaweka kuwa kama [a]mimea ijulikanayo, na kama [b]walinzi juu ya kuta zake.

62 Tazama, amini ninawaambia, acheni mtumishi wangu George Miller, na mtumishi wangu Lyman Wight, na mtumishi wangu John Snider, na mtumishi wangu Peter Haws, wajipange wenyewe, na kumteua mmoja wao kuwa rais juu ya akidi yao kwa madhumuni ya kuijenga nyumba hiyo.

63 Nao watunge katiba, ambayo kwayo wapate kupokea hisa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hiyo.

64 Nao wasipokee chini ya dola hamsini kama fungu la hisa katika nyumba hiyo, na wataruhusiwa kupokea dola elfu kumi na tano kutoka kwa mtu mmoja kama fungu la hisa katika nyumba hiyo.

65 Lakini hawataruhusiwa kupokea zaidi ya dola elfu kumi na tano kama fungu la ubia kutoka kwa mtu yeyote.

66 Na hawataruhusiwa kupokea chini ya dola hamsini kwa ajili ya fungu la ubia kutoka

54 *b* M&M 98:13; 103:27–28.
55 *a* M&M 127:4.
b Ibr. 3:25.
56 *a* M&M 124:22–24.
58 *a* Mwa. 12:3; 22:18; Ibr. 2:11. MWM Ibrahimu.
b M&M 110:12. MWM Agano la Ibrahimu.
61 *a* Isa. 61:3; Eze. 34:29.
b MWM Kesha, Walinzi.

kwa mtu yeyote katika nyumba hiyo.

67 Na hawataruhusiwa kumpokea mtu yeyote, kama mwenye hisa katika nyumba hii, isipokuwa mtu huyo amelipa hisa yake mikononi mwao wakati anapopata hisa hiyo;

68 Na kwa idadi sawa na kiwango cha hisa anacholipa mikononi mwao atapokea hisa katika nyumba hiyo; lakini kama hakulipa chochote mikononi mwao asipewe hisa yoyote katika nyumba hiyo.

69 Na kama yeyote atalipa hisa mikononi mwao itakuwa kwa ajili ya hisa katika nyumba hiyo, kwa ajili yake, na kwa ajili ya kizazi chake baada yake, kutoka kizazi hadi kizazi, ilimradi tu yeye na warithi wake wataendelea kuishikilia hisa hiyo, na hawaiuzi au kuitoa hisa hiyo kutoka mikononi mwao kwa ridhaa yao wenyewe na kutenda, kama mtafanya mapenzi yangu, asema Bwana Mungu wenu.

70 Na tena, amini ninawaambia, kama mtumishi wangu George Miller, na mtumishi wangu Lyman Wight, na mtumishi wangu John Snider, na mtumishi wangu Peter Haws, watapokea hisa yoyote mikononi mwao, katika fedha, au katika mali ambayo kwayo watapata thamani halisi ya fedha, wasiigawe sehemu yoyote ya hisa hiyo kwa dhumuni jingine lolote, isipokuwa katika nyumba hiyo tu.

71 Na kama wataigawa sehemu yoyote ya hisa hiyo kwenda sehemu nyingine yoyote, isipokuwa katika nyumba hiyo tu, bila ya kauli ya mwenye hisa, na hawalipi mara-nne kwa hisa ambayo waliigawa kokote kwingineko, isipokuwa katika nyumba hiyo, watalaaniwa, nao wataondolewa kutoka katika nafasi zao, asema Bwana Mungu; kwani Mimi, Bwana, ndiye Mungu, na siwezi [a]kudhihakiwa katika mambo haya.

72 Amini ninawaambia, acheni mtumishi wangu Joseph alipe hisa mikononi mwao kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hiyo, kama aonavyo yeye kuwa vyema; lakini mtumishi wangu Joseph hawezi kulipa zaidi ya dola elfu kumi na tano kama hisa katika nyumba hiyo, wala chini ya dola hamsini; wala haiwezekani kwa mtu mwingine yeyote, asema Bwana.

73 Na kuna wengine pia wanaotaka kujua mapenzi yangu juu yao, kwani wameomba kutoka kwangu.

74 Kwa hiyo, ninawaambia juu ya mtumishi wangu Vinson Knight, kama atafanya mapenzi yangu, na aweka hisa ndani ya nyumba hiyo kwa ajili yake mwenyewe, na kwa ajili ya kizazi chake baada yake, kutoka kizazi hadi kizazi.

75 Naye msiache apaze sauti yake kubwa na ndefu, katikati ya watu, ili [a]kuwatetea teto za maskini na wenye shida; na ashindwe, wala moyo wake ukate tamaa; nami [b]nitapokea

71 *a* Gal. 6:7.
75 *a* Mit. 31:9.
b Mwa. 4:4–5; Musa 5:18–28.

matoleo yake, kwani hayatakuwa kwangu kama matoleo ya Kaini, kwani atakuwa wangu, asema Bwana.

76 Acheni familia yake na ifurahi na kuigeuza mioyo yao kutoka kwenye mateso; kwani nimemteua yeye na kumpaka mafuta, naye ataheshimika katikati ya nyumba yake, kwani nitazisamehe dhambi zake zote, asema Bwana. Amina.

77 Amini ninawaambia, acheni mtumishi wangu Hyrum aweke hisa ndani ya nyumba hiyo kama aonavyo yeye kuwa ni vyema, kwa ajili yake na kizazi chake baada yake, kutoka kizazi hadi kizazi.

78 Acheni mtumishi wangu Isaac Galland aweke hisa ndani ya nyumba hiyo; kwani Mimi, Bwana, ninampenda kwa ajili ya kazi alizozifanya, na nitamsamehe dhambi zake zote; kwa hiyo, acheni akumbukwe kuwa alikuwa mwenye hisa katika nyumba hiyo kutoka kizazi hadi kizazi.

79 Acheni mtumishi wangu Isaac Galland ateuliwe miongoni mwenu, na kutawazwa na mtumishi wangu William Marks, na abarikiwe naye, kwenda pamoja na mtumishi wangu Hyrum kumalizia kazi ile ambayo mtumishi wangu Joseph atawaonyesha, nao watabarikiwa sana.

80 Acheni mtumishi wangu William Marks na alipe hisa katika nyumba hiyo, kama aonavyo yeye kuwa vyema, kwa ajili yake mwenyewe na kizazi chake, tangu kizazi hadi kizazi.

81 Acheni mtumishi wangu Henry G. Sherwood na alipe hisa katika nyumba hiyo, kama aonavyo yeye kuwa ni vyema, kwa ajili yake na uzao wake baada yake, tangu, kizazi hadi kizazi.

82 Acheni mtumishi wangu William Law alipe hisa ndani ya nyumba hiyo, kwa ajili yake na uzao wake baada yake, tangu kizazi hadi kizazi.

83 Kama atafanya mapenzi yangu msimwache aichukue familia yake kwenda nchi za mashariki, hata Kirtland; hata hivyo, Mimi, Bwana, nitaijenga Kirtland, lakini Mimi, Bwana, ninalo baa nililolitayarisha kwa ajili ya wakazi wake.

84 Na pamoja na mtumishi wangu Almon Babbit, yapo mambo mengi ambayo sijapendezwa nayo; tazama, anatamani kuweka baraza lake badala ya baraza ambalo nimelitawaza, hata lile la Urais wa Kanisa langu, naye humweka *a*ndama wa dhahabu kwa ajili ya kuabudu watu wangu.

85 Msiache mtu yeyote *a*aende kutoka mahali hapa ambaye amekuja hapa akitafuta kushika amri zangu.

86 Kama wao wanaishi hapa acheni waishi kwangu; na kama watakufa acheni watakufa kwangu; kwani *a*watapumzika kutokana na kazi zao zote za hapa, na wataendelea na kazi zao.

87 Kwa hiyo, acheni mtumishi

84*a* Ku. 32:2–4.
85*a* Lk. 9:62.
86*a* Ufu. 14:13.
мwм Peponi;
Pumzika.

wangu William anitumaini Mimi, na akome kuogopa juu ya familia yake, kwa sababu ya maradhi ya nchi. Kama [a]wanipenda, shika amri zangu; na maradhi ya nchi [b]yatakuletea utukufu wako.

88 Acheni mtumishi wangu William aende na kutangaza injili yangu isiyo na mwisho kwa sauti kubwa, na kwa shangwe kuu, kama vile atakavyoongozwa na [a]Roho wangu, kwa wakazi wa Warsaw, na pia kwa wakazi wa Carthage, na pia kwa wakazi wa Burlington, na pia kwa wakazi wa Madison, na kusubiri kwa uvumilivu na bidii kwa maelekezo zaidi kwenye mkutano wangu mkuu, asema Bwana.

89 Kama atafanya mapenzi yangu mwacheni kutoka sasa na kuendelea asikilize ushauri wa mtumishi wangu Joseph, na kwa faida yake [a]awasaidie maskini, na kuchapisha [b]ile tafsiri mpya ya neno langu takatifu kwa wakazi wa dunia.

90 Na kama atafanya hili [a]nitambariki yeye kwa wingi wa baraka, kwamba yeye hatasahaulika, wala uzao wake hautaonekana [b]ukiomba mkate.

91 Na tena, amini ninawaambia, acheni mtumishi wangu William ateuliwe, atawazwe na kupakwa mafuta, kama mshauri kwa mtumishi wangu Joseph, mahali pa mtumishi wangu Hyrum, ili mtumishi wangu Hyrum apate kuchukua ofisi ya Ukuhani na [a]patriaki, ambayo ilichaguliwa kwake na baba yake, kwa kubarikiwa na pia kwa haki;

92 Ili kutoka sasa yeye atashikilia funguo za baraka za [a]kipatriaki juu ya vichwa vya watu wangu wote;

93 Ili yeyote atakaye mbariki atabarikiwa, na yeyote [a]atakayemlaani atalaaniwa; ili lolote [b]atakalolifunga duniani litakuwa limefungwa mbinguni; na lolote atakalolifungua duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni.

94 Na tangu wakati huu na kuendelea ninamteua yeye aweze kuwa nabii, na [a]mwonaji, na mfunuzi kwa kanisa langu, kama vile mtumishi wangu Joseph;

95 Ili apate kutenda katika umoja pia pamoja na mtumishi wangu Joseph; na kwamba yeye atapokea ushauri kutoka kwa mtumishi wangu Joseph, ambaye atamwonyesha yeye [a]funguo ambazo kwa hizo aweze kuomba na kupokea, na kuvikwa taji la baraka hizo hizo, na utukufu, na heshima, na ukuhani, na vipawa vya ukuhani, ambavyo wakati mmoja

87 *a* Yn. 14:15.
b M&M 121:8; 122:7.
88 *a* MWM Mungu, Uungu—Mungu Roho Mtakatifu.
89 *a* M&M 78:3.
b MY Tafsiri ya Biblia ya Joseph Smith.
90 *a* MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
b Zab. 37:25.
91 *a* M&M 107:39–40.
MWM Kipatriaki, Patriaki.
92 *a* MWM Baraka za Kipatriaki.
93 *a* M&M 132:45–47.
b Mt. 16:19.
MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
94 *a* M&M 107:91–92.
MWM Mwonaji.
95 *a* M&M 6:28.

viliwekwa juu yake yeye aliyekuwa mtumishi wangu [b]Oliver Cowdery;

96 Ili mtumishi wangu Hyrum apate kushuhudia mambo nitakayomwonyesha yeye, ili jina lake lipate kukumbukwa kwa heshima tangu kizazi hadi kizazi, milele na milele.

97 Acheni mtumishi wangu William Law pia apokee funguo ambazo kwa hizo apate kuomba na kupokea baraka; na awe [a]mnyenyekevu mbele zangu, na pasipo [b]hila, naye atampokea Roho wangu, hata [c]Mfariji, ambaye atamwonyesha yeye ukweli wa mambo yote, naye atampa, katika saa ile ile, kile atakachosema.

98 Na [a]ishara hizi zitafuatana naye—[b]atawaponya wagonjwa, atawatoa pepo wabaya, na ataokolewa kutoka kwa wale watakaomywesha sumu;

99 Naye ataongozwa katika njia ambazo nyoka [a]wenye sumu hawatamshika kisigino chake, naye atapaa katika [b]dhana za mawazo yake kama vile juu ya mbawa za tai.

100 Na kama itatokea kwamba nikataka amfufue mtu aliyekufa, msimwache aizue sauti yake.

101 Kwa hiyo, acheni mtumishi wangu William alie kwa sauti na asiache, kwa shangwe na furaha, na pamoja na hosana kwa yeye aketiye juu ya kiti cha enzi milele na milele, asema Bwana Mungu wenu.

102 Tazama, ninawaambia, ninayo huduma niliyoiweka kwa ajili ya mtumishi wangu William, na mtumishi wangu Hyrum, na ni kwao peke yao; na acheni mtumishi wangu Joseph akae nyumbani, kwani yeye anahitajiwa. Wanaobaki nitawaonyesha hapo baadaye. Hivyo ndivyo. Amina.

103 Na tena, ninawaambia, kama mtumishi wangu [a]Sidney atanitumikia mimi na kuwa mshauri kwa mtumishi wangu Joseph, acheni asimame na kuja na kusimama katika ofisi ya wito wake, na kujinyenyekeza mwenyewe mbele zangu.

104 Na kama atanitolea matoleo ya kukubalika, na ya shukrani, na kubaki pamoja na watu wangu, tazama, Mimi, Bwana Mungu wenu, nitamponya ili apate kupona; naye ataipaza sauti yake tena milimani, na kuwa [a]msemaji mbele ya uso wangu.

105 Acheni aje na kuiweka familia yake katika maeneo ya jirani na mtumishi wangu Joseph anapoishi.

106 Na katika safari zake zote acheni apaze sauti yake kama vile sauti ya parapanda, na kuwaonya wakazi wa dunia kuikimbia ghadhabu inayokuja.

107 Acheni amsaidie mtumishi wangu Joseph, na pia acheni mtumishi wangu William Law

95 *b* MWM Cowdery, Oliver.
97 *a* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
b MWM Hila.
c MWM Mfariji.
98 *a* Mk. 16:17–18. MWM Vipawa vya Roho.
b MWM Ponya, Uponyaji.
99 *a* M&M 84:71–73.
b Ku. 19:4; Isa. 40:31.
103 *a* MWM Rigdon, Sidney.
104 *a* Ku. 4:14–16; 2 Ne. 3:17–18; M&M 100:9–11.

na amsaidie mtumishi wangu Joseph, katika kutengeneza *a*tangazo la dhati kwa wafalme wa dunia, hata kama vile nilivyowaambia hapo awali.

108 Kama mtumishi wangu Sidney atafanya mapenzi yangu, msimwache aipeleke familia yake nchi za *a*mashariki, lakini acheni abadilishe makazi yao, hata kama vile nilivyosema.

109 Tazama, siyo mapenzi yangu kwamba atatafuta kupata usalama na kimbilio nje ya mji ambao nimewachagulia, hata mji wa *a*Nauvoo.

110 Amini ninawaambia, hata sasa, kama ataisikiliza sauti yangu, itakuwa vyema kwake yeye. Hivyo ndivyo. Amina.

111 Na tena, amini ninawaambia, acheni mtumishi wangu Amos Davis alipe hisa mikononi mwa wale ambao nimewateua kujenga nyumba ya kuishi, hata Nyumba ya Nauvoo.

112 Acheni afanye hili kama atapata faida; naye acheni asikilize ushauri wa mtumishi wangu Joseph, na kufanya kazi kwa mikono yake mwenyewe ili apate kuaminiwa na watu.

113 Na atakapojithibitisha mwenyewe kwamba ni mwaminifu katika mambo yote yatakayo aminiwa kwake, ndiyo, hata mambo machache, atafanywa *a*mtawala juu ya mengi;

114 Kwa hiyo mwacheni *a*ajidhili mwenyewe ili apate kukwezwa. Hivyo ndivyo. Amina.

115 Na tena, amini ninawaambia, kama mtumishi wangu Robert D. Foster atatii sauti yangu, acheni ajenge nyumba kwa ajili ya mtumishi wangu Joseph, kulingana na mkataba alioufanya naye, kwa vile mlango utafunguliwa kwake mara kwa mara.

116 Naye acheni atubu upumbavu wake wote, na kujivika *a*hisani; na kuacha kutenda uovu, na kuweka kando maneno yake magumu;

117 Na alipe hisa pia mikononi mwa akidi ya Nyumba ya Nauvoo, kwa ajili yake na kwa ajili ya kizazi chake baada yake, tangu kizazi hadi kizazi;

118 Na asikilize ushauri wa watumishi wangu Joseph, na Hyrum, na William Law, na kwa viongozi ambao nimewaita kuweka msingi wa Sayuni; na itakuwa vyema kwake, milele na milele. Hivyo ndivyo. Amina.

119 Na tena, amini ninawaambia, acheni mtu yeyote asilipe hisa kwa akidi ya Nyumba ya Nauvoo isipokuwa amekuwa muumini katika Kitabu cha Mormoni, na mafunuo niliyoyatoa kwenu, asema Bwana Mungu wenu;

120 Kwani kile kilicho *a*zaidi au pungufu kuliko hii chatoka kwa mwovu, nacho kitashughulikiwa kwa laana na siyo baraka, asema Bwana Mungu wenu. Hivyo ndivyo. Amina.

107 *a* M&M 124:2–4.
108 *a* M&M 124:82–83.
109 *a* MWM Nauvoo, Illinois (Marekani).
113 *a* Mt. 25:14–30.
114 *a* Mt. 23:12; M&M 101:42.
116 *a* Kol. 3:14.
MWM Hisani.
120 *a* Mt. 5:37; M&M 98:7.

121 Na tena, amini ninawaambia, acheni akidi ya Nyumba ya Nauvoo walipwe ujira sahihi kwa kazi zao zote wanazozifanya katika kujenga Nyumba ya Nauvoo; na acheni ujira wao uwe kama itakavyokubalika baina yao wenyewe, kulingana na thamani yake.

122 Na acheni kila mtu alipaye hisa abebe sehemu yake ya ujira wao, kama hapana budi, kwa ajili ya kuwasaidia, asema Bwana; vinginevyo, kazi zao zitahesabiwa kama hisa kwao katika nyumba hiyo. Hivyo ndivyo. Amina.

123 Amini ninawaambia, sasa ninatoa kwenu [a]maofisa walio wa Ukuhani wangu, ili ninyi mpate kuzishika [b]funguo zake, hata ukuhani ambao ni kwa mfano wa [c]Melkizedeki, ambao ni kwa mfano wa Mwanangu wa Pekee.

124 Kwanza, ninawapa Hyrum Smith kuwa [a]patriaki kwenu ninyi, kushikilia baraka za [b]kufunga za kanisa langu, hata Roho Mtakatifu wa [c]ahadi, ambaye kwake yeye ninyi [d]mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi, ili msiweze kuanguka licha ya kuwa [e]saa ya majaribu yaweza kuja juu yenu.

125 Ninawapa mtumishi wangu Joseph kuwa mzee kiongozi juu ya kanisa langu lote, kuwa mfasiri, [a]mfunuzi, mwonaji, na nabii.

126 Ninampa yeye kuwa washauri wake mtumishi wangu Sidney Rigdon na mtumishi wangu William Law, ili hawa wapate kuunda akidi na Urais wa Kwanza, kupokea [a]mafunuo kwa ajili ya kanisa zima.

127 Ninawapa ninyi mtumishi wangu [a]Brigham Young kuwa rais juu ya baraza la Kumi na Wawili wasafirio;

128 [a]Kumi na Wawili ambao hushikilia funguo za kufungua mamlaka ya ufalme wangu juu ya pande nne za dunia, na baada ya hiyo [b]kupeleka neno langu kwa kila kiumbe.

129 Wao ni Heber C. Kimball, Parley P. Pratt, Orson Pratt, Orson Hyde, William Smith, John Taylor, John E. Page, Wilford Woodruff, Willard Richards, George A. Smith;

130 [a]David Patten [b]nimemchukua kwangu; tazama, ukuhani wake hakuna mtu auondoaye kutoka kwake; lakini, amini ninawaambia, mwingine aweza kuteuliwa kwa wito huo huo.

131 Na tena, ninawapa [a]baraza kuu, kwa ajili ya jiwe la kona ya Sayuni—

132 Majina yao, Samuel Bent, Henry G. Sherwood, George W.

123 *a* MWM Ofisa, Ofisi.
b MWM Funguo za Ukuhani.
c MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
124 *a* MWM Kipatriaki, Patriaki.
b MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
c M&M 76:53; 88:3–4. MWM Roho Mtakatifu wa Ahadi.
d Efe. 4:30.
e Ufu. 3:10.
125 *a* M&M 21:1. MWM Mwonaji.
126 *a* M&M 90:4–5.
127 *a* MWM Young, Brigham.
128 *a* MWM Mtume.
b Mk. 16:15.
130 *a* MWM Patten, David W.
b M&M 124:19.
131 *a* MWM Baraza Kuu.

Harris, Charles C. Rich, Thomas Grover, Newel Knight, David Dort, Dunbar Wilson—Seymour Brunson nimemchukua kwangu; hakuna mtu aondoaye ukuhani wake, lakini mwingine aweza kuteuliwa katika ukuhani huo huo badala yake; na amini ninawaambia, acheni mtumishi wangu Aaron Johnson atawazwe kwa wito huu badala yake—David Fullmer, Alpheus Cutler, William Huntington.

133 Na tena, ninawapa Don C. Smith kuwa rais juu ya akidi ya makuhani wakuu;

134 Agizo ambalo limewekwa kwa madhumuni ya kuwapasisha wale ambao watateuliwa kuwa marais wasimamizi au watumishi juu ya [a]vigingi mbalimbali vilivyoenea ng'ambo;

135 Nao waweza kusafiri pia kama wanataka, lakini badala yake wametawazwa kuwa marais wasimamizi; hii ndiyo ofisi ya wito wao, asema Bwana Mungu wenu.

136 Ninampa yeye Amasa Lyman na Noah Packard kuwa washauri, ili wapate kuongoza juu ya akidi ya makuhani wakuu wa kanisa langu, asema Bwana.

137 Na tena, ninawaambia, ninawapa John A. Hicks, Samuel Williams, na Jesse Baker, ukuhani ambao ni kuongoza juu ya akidi ya [a]wazee, akidi ambayo kimewekwa kwa ajili ya wahudumu kudumu; hata hivyo hawa wanaweza kusafiri, lakini hawa wametawazwa kuwa wahudumu wa kudumu kwa kanisa langu, asema Bwana.

138 Na tena, ninawapa Joseph Young, Josiah Butterfield, Daniel Miles, Henry Herriman, Zera Pulsipher, Levi Hancock, James Foster, kuongoza juu ya akidi ya [a]sabini;

139 Akidi ambayo kimewekwa kwa ajili ya wazee wasafirio kutoa ushuhuda wa neno langu ulimwenguni kote, popote baraza kuu lisafirilo, mitume wangu, watakapo watuma kuitengeneza njia mbele za uso wangu.

140 Tofauti kati ya akidi hii na akidi ya wazee ni kwamba moja ni ya kusafiri daima, na ingine ni ya kuongoza juu ya kanisa mara kwa mara; moja ina wajibu wa kuongoza mara kwa mara, na ingine haina wajibu wa kuongoza, asema Bwana Mungu wenu.

141 Na tena, ninawaambia, ninakupeni Vinson Knight, Samuel H. Smith, na Shadrach Roundy, kama ataupokea, kusimamia [a]uaskofu; maarifa juu ya uaskofu uliosemwa yametolewa kwenu katika kitabu cha [b]Mafundisho na Maagano.

142 Na tena, ninawaambia, Samuel Rolfe na washauri wake kwa ajili ya makuhani, na rais wa walimu na washauri wake, na pia rais wa mashemasi na washauri wake, na pia rais wa kigingi na washauri wake.

134 *a* MWM Kigingi.
137 *a* M&M 107:11–12, 89–90.
MWM Akidi; Mzee.
138 *a* MWM Sabini.
141 *a* M&M 68:14; 107:15.
b MWM Mafundisho na Maagano.

143 Ofisi zilizoko hapo juu nimezitoa kwenu, na funguo zake, kwa misaada na kwa serikali, kwa kazi ya huduma na [a]kuwakamilisha watakatifu wangu.

144 Na amri ninaitoa kwenu, kwamba lazima mzijaze nafasi hizi zote na [a]kuyathibitisha majina hayo niliyoyataja, au vinginevyo myakatae kwenye mkutano wangu mkuu;

145 Na kwamba tayarisheni vyumba kwa ajili ya ofisi hizi zote katika nyumba yangu wakati mtakapoijenga kwa jina langu, asema Bwana Mungu wenu. Hivyo ndivyo. Amina.

SEHEMU YA 125

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Nauvoo, Illinois, Machi 1841, juu ya Watakatifu katika eneo la Iowa.

1–4, Watakatifu lazima waijenge miji na kukusanyika kwenye vigingi vya Sayuni.

Mapenzi ya Bwana ni yapi juu ya Watakatifu katika eneo la Iowa?

2 Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, ninawaambia, kama wale [a]wajiitao wenyewe kwa jina langu na wanajitahidi kuwa watakatifu wangu, kama watafanya mapenzi yangu na kushika amri zangu juu yao, acheni wajikusanye pamoja mahali ambapo nitawachagulia kwa njia ya mtumishi wangu Joseph, na waijenge miji kwa jina langu, ili wapate kuandaliwa kwa ajili ya kile kilicho wekwa kwa ajili ya wakati ujao.

3 Acheni waujenge mji kwa ajili ya jina langu juu ya ardhi iliyoko upande wa pili wa mji wa Nauvoo, na acheni jina la [a]Zarahemla liitwe juu yake.

4 Na acheni wale wote wanaokuja kutoka mashariki, na magharibi, na kaskazini, na kusini, ambao wanataka kuishi humo, wachukue urithi wao humo humo, na pia katika mji wa [a]Nashville, au katika mji wa Nauvoo, na katika [b]vigingi vyote nilivyoviteua, asema Bwana.

SEHEMU YA 126

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, katika nyumba ya Brigham Young, huko Nauvoo, Illinois, 9 Julai 1841. Kwa wakati

143 *a* Efe. 4:11–14.
144 *a* M&M 26:2. mwm Ridhaa ya Wengi.

125 2 *a* mwm Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
3 *a* mwm Zarahemla.
4 *a* my Nashville katika Wilaya ya Lee, Iowa.
b mwm Kigingi.

huu Brigham Young alikuwa Rais wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili.

1–3, Brigham Young anasifiwa kwa kazi zake na anapumzishwa kusafiri nje ya nchi katika siku zijazo.

Mpenzi na ndugu mpendwa, [a]Brigham Young, amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwako: Mtumishi wangu Brigham, haitakiwi tena mkononi mwako kuiacha familia yako kama siku zilizopita, kwa kuwa sadaka yako imekubaliwa kwangu.

2 Nimeona [a]kazi na sulubu zako katika safari kwa ajili ya jina langu.

3 Kwa hiyo ninakuamuru kulipeleka neno langu nchi za nje, na utaishughulikia vizuri [a]familia yako kutoka sasa, na kuendelea na milele. Amina.

SEHEMU YA 127

Waraka kutoka kwa Joseph Smith Nabii kwa Watakatifu wa Siku za Mwisho huko Nauvoo, Illinois, wenye maelekezo juu ya ubatizo kwa ajili ya wafu, ulioandikwa huko Nauvoo, 1 Septemba 1842.

1–4, Joseph Smith afurahi katika taabu na dhiki; 5–12, Kumbukumbu lazima zitunzwe juu ya ubatizo wa wafu.

Kwa kuwa Bwana amenifunulia kwamba maadui zangu, wote wa Missouri na wa Jimbo hili, walikuwa tena wakinisaka; na kwa vile wananisaka bila [a]sababu, na wala hawana kivuli wala rangi ya kunitendea kisheria au haki kwa upande wao kuhusiana na kuniletea mashtaka yao dhidi yangu; na kwa vile visingizio vyao vyote vinatokana na uongo wa rangi nyeusi, nimefikiri ni muhimu na ni hekima kwangu kuondoka mahali hapa kwa muda mfupi, kwa usalama wangu mwenyewe na kwa usalama wa watu hawa. Ningelisema kwa wale wote wenye shughuli na mimi, kwamba nimeacha mambo yangu kwa mawakala na makarani ambao watashughulikia mambo yote mara moja na ipasavyo, nao wataona kwamba madeni yangu yote yanalipwa kwa wakati wake, kwa kuuza mali, au kwa njia nyingineyo, kadiri itakavyohitajika, au kadiri hali itavyoruhusu. Nitakapojua kwamba dhoruba imemalizika kabisa, ndipo nitarejea kwenu tena.

2 Na juu ya [a]hatari ambazo

126 1*a* mwm Young, Brigham.
2*a* mwm Matendo.
3*a* mwm Familia.
127 1*a* Ayu. 2:3; Mt. 5:10–12; 1 Pet. 2:20–23.
2*a* Zab. 23. mwm Mateso, Tesa.

nimeitwa kuzipitia, yaonekana kuwa jambo dogo kwangu, kama vile [b]wivu na ghadhabu za mwanadamu zimekuwa jambo la kawaida siku zote za maisha yangu; na kwa sababu yake yaonekana kuwa miujiza, isipokuwa kama [c]nilitawazwa kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu kwa ajili ya madhumuni mema, au mabaya, kama mtakavyochagua kuita. Hukumuni ninyi wenyewe. Mungu anajua mambo haya yote, kama ni mazuri au mabaya. Lakini hata hivyo, maji ya kina kirefu nimezoea kuogelea ndani yake. Hii yote imekuwa kawaida ya pili kwangu; na ninajisikia, kama Paulo, kufurahia katika [d]taabu; kwa sababu hadi siku hii Mungu wa baba zangu amenikomboa na haya yote, na atanikomboa kutoka sasa na kuendelea; kwani tazama, na lo, nitawashinda adui zangu wote, kwani Bwana Mungu amesema hayo.

3 Acha watakatifu wote na wafurahi, kwa sababu hiyo, na wawe na furaha tele; kwa kuwa [a]Mungu wa Israeli ndiye Mungu wao, naye atawagawia malipo ya ujira wa haki juu ya vichwa vya watesi wao wote.

4 Na tena, amini hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Acha kazi ya [a]hekalu langu, na kazi zote ambazo nimewapangia, ziendelezwe na zisisimame; na [b]jitihada zenu, na uvumilivu wenu, na ustahimilivu, na kazi zenu zizidishwe mara mbili, nanyi kwa vyovyote vile hamtakosa ujira wenu, asema Bwana wa Majeshi. Na kama [c]wanavyowatesa ninyi, ndivyo walivyowatesa manabii na watu wenye haki waliokuwepo kabla yenu. Kwani kwa haya yote kuna thawabu mbinguni.

5 Na tena, ninatoa kwenu ninyi neno lihusulo [a]ubatizo kwa ajili ya [b]wafu wenu.

6 Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwenu ninyi juu ya wafu wenu: Wakati mmoja wenu [a]abatizwapo kwa ajili ya wafu wenu, acha awepo na [b]mwandishi, naye awe shahidi wa macho wa ubatizo wenu; acha asikie kwa masikio yake, ili apate kuishuhudia kweli, asema Bwana;

7 Ili kumbukumbu zenu zote zipate [a]kuandikwa mbinguni; lolote [b]mtakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lolote mtakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni;

8 Kwani ni karibu [a]kuyarejesha mambo mengi duniani, yahusuyo [b]ukuhani, asema Bwana wa Majeshi.

9 Na tena, acha [a]kumbukumbu

2 *b* MWM Husuda.
c MWM Uteuzi kabla.
d 2 Kor. 6:4–5.
MWM Shida.
3 *a* 3 Ne. 11:12–14.
4 *a* M&M 124:55.
b MWM Bidii.
c MWM Mateso, Tesa.
5 *a* MWM Batiza, Ubatizo—Ubatizo kwa ajili ya wafu.
b MWM Wokovu kwa ajili ya Wafu.
6 *a* 1 Kor. 15:29; M&M 128:13, 18.
b M&M 128:2–4, 7.
7 *a* MWM Kitabu cha Uzima.
b MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
8 *a* MWM Urejesho wa Injili.
b MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
9 *a* M&M 128:24.

zote zitunzwe kwa mpangilio, ili zipate kuwekwa kwenye nyaraka za hekalu langu takatifu, ili ziweze kutunzwa katika ukumbusho toka kizazi hadi kizazi, asema Bwana wa Majeshi.

10 Nitasema kwa watakatifu wote, kwamba nimetamani, kwa tamaa kubwa kupita kiasi, kuwahubiria kutoka jukwaani juu ya jambo la ubatizo kwa ajili ya wafu, siku ya Sabato ijayo. Lakini kwa vile hiyo iko nje ya uwezo wangu kufanya hivyo, nitawaandikia neno la Bwana mara kwa mara, juu ya jambo hilo, na kulituma kwenu kwa njia ya barua, vile vile mambo mengineyo.

11 Sasa ninaifunga barua yangu kwa wakati huu, kwa sababu ya uchache wa muda; kwani adui yuko tayari, na kama Mwokozi alivyosema, yuaja [a]mtawala wa ulimwengu huu, lakini hana kitu kwangu.

12 Tazama, sala yangu kwa Mungu ni kwamba ninyi nyote mpate kuokolewa. Na ninatia saini mimi mwenyewe kama mtumishi wenu katika Bwana, nabii na [a]mwonaji wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.

Joseph Smith.

SEHEMU YA 128

Waraka kutoka kwa Joseph Smith Nabii kwa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, wenye maelekezo zaidi juu ya ubatizo kwa ajili ya wafu, ulioandikwa huko Nauvoo, Illinois, 6 Septemba 1842.

1–5, Waandishi wa maeneo na waandishi wakuu ni lazima wathibitishe ukweli wa ubatizo huo kwa ajili ya wafu; 6–9, Kumbukumbu zao zinafunga na zinaandikwa duniani na mbinguni; 10–14, Kisima cha ubatizo ni mfano wa kaburi; 15–17, Eliya alirejesha uwezo juu ya ubatizo wa wafu; 18–21, Vyote funguo, uwezo, na mamlaka za vipindi vilivyopita vimerejeshwa; 22–25, Habari njema na tukufu zimetangazwa kwa walio hai na wafu.

Kama nilivyoeleza kwenu katika barua yangu kabla ya kuondoka nyumbani kwangu, kwamba nitawaandikia mara kwa mara na kuwapa habari juu ya mambo mengi, sasa ninaanza tena na jambo la [a]ubatizo kwa ajili ya wafu, kwa vile jambo hilo laonekana kutawala akili yangu, na linajisukuma kwenye hisia zangu kwa nguvu, tangu nilipokuwa nikifukuzwa na adui zangu.

2 Niliwaandikia maneno machache ya ufunuo juu ya

11 *a* Yn. 14:30; TJS Yn. 14:30 (Kiambatisho).

MWM Ibilisi.

12 *a* M&M 124:125. MWM Mwonaji.

128 1 *a* MWM Batiza, Ubatizo—Ubatizo kwa ajili ya wafu.

mwandishi. Nimepata kuwa na maoni machache ya nyongeza juu ya jambo hili, ambayo sasa ninayathibitisha. Kwamba ilielezwa katika barua yangu iliyopita kwamba lazima pawepo na [a]mwandishi, ambaye ni lazima awe shahidi wa kuona, na pia kusikia kwa masikio yake, ili apate kumbukumbu ya kweli mbele za Bwana.

3 Sasa, kuhusu jambo hili, itakuwa vigumu sana kwa mwandishi mmoja kuwepo wakati wote, na kufanya shughuli zote. Ili kuepuka tatizo hili, yawezekana kuwa mwandishi ateuliwe katika kila wadi katika mji, ambaye ana uwezo wa kuandika kumbukumbu kwa ufasaha; na acheni awe makini na sahihi katika kuandika matukio yote, akihakikisha katika maandishi yake kwamba aliona kwa macho yake, na kusikia kwa masikio yake, akitoa tarehe, na majina, na kadhalika, na historia ya shughuli yote; akitaja pia majina ya watu watatu waliopo, kama watakuwepo, ambao wanaweza kwa wakati wowote ikiwa wataitwa juu ya kuthibitisha jambo hilo hilo, ili katika vinywa vya [a]mashahidi wawili au watatu kila neno lipate kuthibitishwa.

4 Halafu, acheni awepo mwandishi mkuu, ambaye kwake kumbukumbu hizi zinaweza kupelekwa, zikipelekwa pamoja na hati zenye saini zao wenyewe, zikithibitisha kwamba kumbukumbu ile waliyoyaandika ni ya kweli. Ndipo mwandishi mkuu wa kanisa anaweza kuingiza katika kitabu kikuu cha kanisa, pamoja na hati hizo na majina ya mashahidi wote waliokuwepo, pamoja na maelezo yake mwenyewe kwamba hakika yeye anaamini maelezo yaliyoandikwa hapo juu na anayeandika kuwa ni ya kweli, kutokana na ufahamu wake wa tabia ya jumla na kuteuliwa kwa watu wale na kanisa. Na ikiwa haya yamefanyika kwenye kitabu kikuu cha kanisa, maandiko haya yatakuwa ya haki na matakatifu, na yatafanya ibada hiyo kuwa hivyo hivyo kama vile yeye ameona kwa macho yake na kusikia kwa masikio yake, na kuiandika kumbukumbu hiyo kwenye kitabu kikuu cha kanisa.

5 Ninyi pengine mnaweza kudhani utaratibu huu wa mambo kuwa ni mrefu sana; lakini acha niwaeleze ya kuwa hii ni kujibu tu mapenzi ya Mungu, kwa kufuata maagizo na matayarisho ambayo Bwana ameagiza na kutayarisha kabla ya kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, kwa ajili ya [a]wokovu wa wafu ambao watakufa bila [b]kuifahamu injili.

6 Na zaidi, ninataka ninyi mkumbuke kwamba Yohana Mfunuzi alikuwa akitafakari juu ya jambo hili hili la wafu, wakati alipotangaza, kama mnavyoona imeandikwa katika Ufunuo 20:12—*Na niliwaona wafu, wadogo na wakubwa, wamesimama mbele za Mungu; na vitabu vimefunguliwa; na kitabu*

2*a* M&M 127:6.
3*a* MWM Shahidi, Ushahidi.
5*a* MWM Wokovu kwa ajili ya Wafu.
b 1 Pet. 4:6.

kingine kilifunguliwa, ambacho ni kitabu cha uzima; na wafu walihukumiwa kutokana na mambo yale yaliyoandikwa ndani ya vitabu hivi, kulingana na matendo yao.

7 Mtagundua katika dondoo hii kwamba vitabu vilifunguliwa; na kitabu kingine kilifunguliwa, ambacho kilikuwa ni [a]kitabu cha uzima; lakini wafu walihukumiwa kutokana na mambo yaliyoandikwa ndani ya vitabu hivyo, kulingana na matendo yao; kwa hiyo, vitabu vilivyozungumzwa lazima viwe ni vitabu ambavyo vina kumbukumbu ya matendo yao, na inaonyesha kuwa ni [b]kumbukumbu ambazo zinatunzwa duniani. Na kitabu kilichokuwa kitabu cha uzima ni kumbukumbu inayotunzwa mbinguni; kanuni hii inakubaliana sawa sawa na mafundisho mnayoamriwa ninyi katika ufunuo uliomo katika barua ambayo nimewaandikia kabla sijaondoka nyumbani kwangu—ili katika kumbukumbu zenu zote mwandikazo ziweze kuandikwa mbinguni.

8 Sasa, kiini cha ibada hii kinategemea katika [a]uwezo wa ukuhani, kupitia ufunuo wa Yesu Kristo, ambao ndani yake imetolewa kwamba lolote utakalolifunga duniani litafungwa mbinguni, na lolote [b]utakalolifungua duniani litafunguliwa mbinguni. Au, kwa maneno mengine, mtazamo tofauti wa tafsiri hii, lolote utakaloliandika duniani litaandikwa mbinguni, na lolote usiloliandika duniani halitaandikwa mbinguni; kwani kutoka kwenye vitabu wafu wenu watahukumiwa, kulingana na matendo yao wenyewe, iwe wao wenyewe wametenda [c]ibada hizo wao wenyewe, au kwa njia ya wawakilishi wao, kulingana na agizo ambalo Mungu amelitayarisha kwa ajili ya [d]wokovu wao tangu kabla ya kuwekwa msingi wa dunia, kulingana na kumbukumbu walizoziandika juu ya wafu wao.

9 Yawezekana kwa wengine ikaonekana ni mafundisho yasiyo ya kawaida ambayo tunayazungumzia—uwezo ambao huandika au kufunga duniani na kufungwa mbinguni. Hata hivyo, katika umri wote wa ulimwengu, wakati wowote Bwana alipokuwa ametoa [a]kipindi cha ukuhani kwa mtu yeyote kwa ufunuo halisi, au kwa kundi lolote la wanadamu, uwezo huu daima umekuwa ukitolewa. Kwa sababu hiyo, lolote watu wale walilolifanya katika [b]mamlaka, katika jina la Bwana, na wakalifanya kwa ukweli na kwa uaminifu, na kutunza kwa usahihi na uaminifu kumbukumbu hiyo, ikaja kuwa sheria duniani na mbinguni, na haikuweza kuondolewa, kulingana na maamrisho ya [c]Yehova mkuu. Hili ni neno la kuaminiwa. Ni nani awezaye kulisikia?

7 *a* Ufu. 20:12; M&M 127:6–7. MWM Kitabu cha Uzima.
b M&M 21:1.

8 *a* MWM Ukuhani; Uwezo.
b MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
c MWM Ibada.
d MWM Wokovu kwa ajili ya Wafu.

9 *a* MWM Kipindi.
b MWM Mamlaka.
c MWM Yehova.

10 Na tena, kama mfano mwingine, Mathayo 16:18, 19: *Nami pia nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya jehanamu haitalishinda. Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni: na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lolote utakalolifungua duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni.*

11 Sasa siri kubwa na muhimu ya jambo hili lote, na uzuri mkuu wa juu kabisa juu ya somo lote lililoko mbele yetu, linategemea katika kupata uwezo wa Ukuhani Mtakatifu. Kwake yeye ambaye amepewa [a]funguo hizi hakuna ugumu wa kupata maarifa ya ukweli yahusianayo na [b]wokovu wa wanadamu, wote vile vile kwa ajili ya wafu na walio hai.

12 Katika hili kuna [a]utukufu na [b]heshima, na [c]kutokufa na uzima wa milele—Agizo la ubatizo kwa maji, [d]kuzamishwa ndani yake ili kuwa mfano wa wafu, ili kanuni moja ipate kulingana na nyingine; kuzamishwa majini na kutoka majini ni mfano wa ufufuko wa wafu kutoka makaburini mwao; kwa sababu hiyo, agizo hili liliwekwa ili kufanya uhusiano na agizo la ubatizo kwa ajili ya wafu, ukiwa ni mfano wa wafu.

13 Kwa hiyo, [a]kisima cha maji ya ubatizo kiliwekwa kama [b]mfano wa kaburi, na iliamriwa kiwe chini ya mahali ambapo walio hai wamezoea kukusanyika, ili kuwaonyesha walio hai na wafu, na ili vitu vyote vipate kuwa na mifano yao, na ili vipate kulingana—kile kilicho cha duniani kikubaliane na kile kilicho cha mbinguni, kama vile Paulo alivyotangaza, 1 Wakorintho 15:46, 47, na 48:

14 *Lakini hautangulii ule wa kiroho, bali ule wa kiasili; na baadaye huja ule wa kiroho. Mtu wa kwanza atoka katika nchi, ni wa udongo; mtu wa pili ni Bwana atoka mbinguni. Kama alivyo yeye wa udongo ndivyo walivyo walio wa udongo; na kama alivyo yeye wa mbinguni ndivyo walivyo pia walio wa mbinguni.* Na kama zilivyo kumbukumbu duniani juu ya wafu wenu, ambayo yameandikwa kwa uhakika, pia ndivyo yalivyo maandishi mbinguni. Huu, kwa hiyo, ni uwezo wa [a]kuunganisha na kufunga, kulingana na njia moja ya kulielewa neno, [b]funguo za ufalme, ambazo zinajumuisha funguo za [c]maarifa.

15 Na sasa, wapendwa ndugu na dada zangu, acheni nikuhakikishieni kwamba kanuni hizi zihusianazo na wafu na walio hai kwamba haziwezi kupuuzwa, kwa vile zinahusu wokovu wetu. Kwa kuwa [a]wokovu

11 *a* MWM Funguo za Ukuhani.
b MWM Wokovu.
12 *a* MWM Utukufu.
b MWM Heshima.
c MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
d MWM Batiza, Ubatizo—Ubatizo kwa kuzamishwa.
13 *a* M&M 124:29.
b MWM Uashiriaji.
14 *a* MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
b MWM Funguo za Ukuhani.
c TJS Lk. 11:53 (Kiambatisho).
15 *a* MWM Wokovu kwa ajili ya Wafu.

wao ni wa lazima na ni muhimu kwa wokovu wetu, kama vile Paulo asemavyo juu ya mababu—kwamba wao pasipo sisi [b]hawakamiliki—wala sisi hatuwezi kuwa wakamilifu pasipo wafu wetu.

16 Na sasa, kuhusu ubatizo kwa ajili ya wafu, nitakupeni dondoo nyingine ya Paulo, 1 Wakorintho 15:29: *Au je! Wenye kubatizwa kwa ajili ya wafu watafanyaje, kama wafu hawafufuliwi kamwe? Kwa nini kubatizwa kwa ajili ya wao?*

17 Na tena, sambamba na dondoo hii nitakupeni dondoo kutoka kwa mmoja wa manabii, ambaye macho yake yaliangalia juu ya [a]urejesho wa Ukuhani, utukufu utakaofunuliwa katika siku za mwisho, na kwa jinsi ya pekee jambo hili tukufu juu ya mambo yote yahusuyo injili isiyo na mwisho, nalo ni, ubatizo kwa ajili ya wafu; kwani Malaki anasema, mlango wa mwisho, mstari wa 5 na wa 6: *Tazama, nitamtuma kwenu [b]Eliya nabii kabla ya kuja siku ile iliyo kuu na ya kuogofya ya Bwana: Naye ataigeuza mioyo ya mababu iwaelekee watoto, na mioyo ya watoto iwaelekee mababu zao, nisije nikaja na kuipiga dunia kwa laana.*

18 Ningeweza kufanya tafsiri ya [a]wazi ya hii, lakini ni wazi vya kutosha kukidhi madhumuni yangu kama vile ilivyo. Yatosha kujua, katika jambo hili, kwamba dunia itapigwa kwa laana isipokuwa pamekuwepo na [b]muunganiko wa aina fulani kati ya mababu na watoto, juu ya jambo moja au jingine—na tazama jambo hilo ni lipi? Ni [c]ubatizo kwa ajili ya wafu. Kwani sisi pasipo wao hatuwezi kukamilika; wala wao pasipo sisi hawawezi kukamilika. Si wao wala sisi tunaoweza kukamilika bila wale waliokufa katika injili pia; kwani ni muhimu katika kuingia kwa [d]kipindi cha utimilifu wa nyakati, kipindi ambacho sasa kinaanza kuingia, kwamba muungano wote mzima na ulio mkamilifu, na muunganiko wa pamoja wa vipindi, na funguo, na uwezo, na utukufu yapaswa ufanyike, na kufunuliwa kutoka siku za Adamu hadi wakati huu. Na siyo hili tu, bali mambo yale ambayo kamwe hayajafunuliwa kutoka kuwekwa kwa [e]msingi wa ulimwengu, lakini yamefichwa kwa wenye hekima na akili, yatafunuliwa kwa watoto [f]wachanga na wanyonyao katika hiki, kipindi cha utimilifu wa nyakati.

19 Sasa, tunasikia nini katika injili ambayo tumeipokea? Sauti ya furaha! Sauti ya rehema kutoka mbinguni; na sauti ya [a]ukweli kutoka duniani; habari njema kwa wafu; sauti ya

15 *b* Ebr. 11:40. MWM Kamilifu.
17 *a* MWM Urejesho wa Injili.
b 3 Ne. 25:5–6; M&M 2; 110:13–16. MWM Eliya.
18 *a* JS—H 1:36–39.
b MWM Ibada—Ibada zifanywazo kwa niaba ya wafu; Nasaba.
c M&M 124:28–30; 127:6–7.
d MWM Kipindi.
e M&M 35:18.
f Mt. 11:25; Lk. 10:21; Alma 32:23.
19 *a* Zab. 85:10–11.

furaha kwa walio hai na wafu; [b]habari njema ya shangwe kuu. Jinsi gani ilivyo mizuri juu ya milima [c]miguu ya waletao habari njema ya mambo mema, na wao waiambiao Sayuni: Tazama, Mungu wako anatawala! Kama [d]umande wa Karmeli, hivyo ndivyo maarifa juu ya Mungu yatakavyoshuka juu yao!

20 Na tena, tunasikia nini? Habari njema kutoka [a]Kumora! [b]Moroni, malaika kutoka mbinguni, akitangaza utimilifu wa manabii—[c]kitabu kitafunuliwa. Sauti ya Bwana katika nyika za [d]Fayette, wilaya ya Seneca, ikiwatangazia mashahidi watatu [e]kukishuhudia kitabu hicho! Sauti ya [f]Mikaeli kando kando ya Susquehanna, akimfichua ibilisi wakati alipojitokeza kama malaika wa [g]nuru! Sauti ya [h]Petro, Yakobo, na Yohana nyikani kati ya Harmony, wilaya ya Susquehanna, na Colesville, wilaya ya Broome, kwenye mto Susquehanna waliposema wenyewe kuwa wanashikilia [i]funguo za ufalme, na za kipindi cha utimilifu wa nyakati!

21 Na tena, sauti ya Mungu ndani ya chumba cha [a]Baba mzee Whitmer, huko Fayette, wilaya ya Seneca, na nyakati nyingine mbalimbali, na mahali mbali mbali wakati wa misafara yote na taabu za hili Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho! Na sauti ya Mikaeli, malaika mkuu, sauti ya [b]Gabrieli, na ya [c]Rafaeli, na [d]malaika mbalimbali, kutoka Mikaeli au [e]Adamu kuja chini hadi wakati huu, wote wakitangaza [f]vipindi vyao, haki na utukufu wao, na nguvu za ukuhani wao; wakitoa mstari juu ya mstari, [g]kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na kule kidogo; wakitupa faraja kwa kutangaza kile kitakachokuja, wakithibitisha [h]matumaini yetu!

22 Ndugu, je, si lazima sisi tuendelee katika kazi hii iliyo kuu? Twende mbele na siyo nyuma. Tuweni wajasiri, ndugu; na mbele, mbele kwenye ushindi! Acheni mioyo yenu ifurahi, na kuwa na furaha kupita kiasi. Acheni nchi ipasuke kwa [a]kuimba. Acheni wafu waimbe nyimbo za sifa ya milele kwa Mfalme [b]Imanueli, aliyeagiza, kabla ya ulimwengu kuwepo, kile ambacho kingetuwezesha sisi [c]kuwakomboa kutoka

19 *b* Lk. 2:10.
c Isa. 52:7–10; Mos. 15:13–18; 3 Ne. 20:40.
d Kum. 32:2; M&M 121:45.
20 *a* JS—H 1:51–52. MWM Kumora, Mlima.
b MWM Moroni, Mwana wa Mormoni.
c Isa. 29:4, 11–14; 2 Ne. 27:6–29. MWM Kitabu cha Mormoni.
d MWM Fayette, New York (Marekani).
e M&M 17:1–3.
f M&M 27:11. MWM Adamu.
g 2 Kor. 11:14.
h M&M 27:12.
i MWM Funguo za Ukuhani.
21 *a* MY Peter Whitmer, Mkubwa.
b MWM Gabrieli.
c MWM Rafaeli.
d MWM Malaika.
e M&M 107:53–56.
f MWM Kipindi.
g Isa. 28:10.
h MWM Tumaini.
22 *a* Isa. 49:13.
b Isa. 7:14; Alma 5:50. MWM Imanueli.
c MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.

[d]kifungoni mwao; kwani wafungwa watawekwa huru.

23 Acheni [a]milima ishangilie kwa shangwe, nanyi mabonde yote lieni kwa sauti; nanyi bahari zote na nchi kavu yatajeni maajabu ya Mfalme wenu wa Milele. Nanyi miito, chemichemi, na vijito, miminikeni kwa furaha. Acheni misitu na miti yote ya shamba imsifu Bwana; nanyi [b]miamba lieni kwa shangwe! Na acheni jua, mwezi, na nyota za [c]asubuhi ziimbe kwa pamoja, na watoto wote wa Mungu wapige kelele kwa shangwe! Acheni muumbaji wa milele atangaze jina lake milele na milele! Na tena ninasema, ni tukufu jinsi gani sauti tuisikiayo kutoka mbinguni, ikitangaza masikioni mwetu, utukufu, na wokovu, na heshima, na [d]mwili usiokufa, na [e]uzima wa milele; falme, himaya, na nguvu.

24 Tazama, [a]siku iliyo kuu ya Bwana i karibu; na ni nani atakaye [b]stahimili siku ya kuja kwake, na ni nani atakayesimama wakati atakapoonekana? Kwa maana yeye ni mfano wa moto wa mtu [c]asafishaye, na mfano wa sabuni ya mtu afuaye; naye ataketi kama mtu [d]asafishaye fedha, naye atawasafisha wana wa [e]Lawi, na atawasafisha kama dhahabu na fedha, ili wapate kutoa kwa Bwana [f]dhabihu katika haki. Kwa hiyo, sisi, kama kanisa na watu, na kama Watakatifu wa Siku za Mwisho, tumtolee Bwana dhabihu katika haki; nasi tuonyeshe katika hekalu lake takatifu wakati litakapomalizika, kitabu chenye [g]kumbukumbu za wafu wetu, ambacho kitastahili kukubalika kote.

25 Ndugu zangu, ninayo mambo mengi ya kukuambieni juu ya jambo hili; lakini kwa sasa nitafunga, na kuendelea na jambo hili wakati mwingine. Mimi, daima, mtumishi wenu mnyenyekevu na rafiki asiye tetereka.

Joseph Smith.

SEHEMU YA 129

Mafundisho yaliyotolewa na Joseph Smith Nabii, huko Nauvoo, Illinois, 9 Februari 1843, ambayo yanaelezea funguo kuu tatu ambazo kwa hizo twaweza kutofautisha aina sahihi za malaika na roho wahudumu.

1–3, Mbinguni kuna miili ya waliofufuka na miili ya kiroho; 4–9, Funguo zimetolewa ambazo kwa hizo wajumbe kutoka

22 *d* Isa. 24:22; M&M 76:72–74.
23 *a* Isa. 44:23.
b Lk. 19:40.
c Ayu. 38:7.
d MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
e MWM Uzima wa Milele.
24 *a* MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b Mal. 3:1–3.
c 3 Ne. 24:2–3.
MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia.
d Zek. 13:9.
e Kum. 10:8; M&M 13; 124:39.
f M&M 84:31.
MWM Sadaka, Utoaji sadaka.
g M&M 127:9.
MWM Nasaba.

ng'ambo ya pazia wanaweza kutambulika.

Kuna viumbe wa aina mbili [a]mbinguni, nao ni: [b]Malaika, ambao ni watu [c]waliofufuka, wenye miili ya nyama na mifupa—

2 Kwa mfano, Yesu alisema: *Nishikenishikeni na mwone, kwa kuwa roho haina [a]mwili na mifupa, kama mnavyoniona mimi kuwa nayo.*

3 Ya pili, ni [a]roho za watu wenye [b]haki waliokamilika, wale ambao hawajafufuka, lakini wanarithi utukufu huo huo

4 Wakati mjumbe akija akisema anao ujumbe kutoka kwa Mungu, mpe mkono wako na mwombe mshikane mikono.

5 Kama yeye atakuwa malaika atafanya hivyo, nawe utausikia mkono wake.

6 Kama atakuwa roho ya mtu mwenye haki aliyekamilika yeye atakuja katika utukufu wake; kwa kuwa hiyo ndiyo njia pekee anayoweza kuonekana—

7 Mwombe mshikane mikono, lakini yeye hatafanya lolote, kwa sababu ni kinyume cha utaratibu wa mbinguni kwa mtu mwenye haki kudanganya; lakini yeye bado atatoa ujumbe wake—

8 Lakini ikiwa ni ya [a]ibilisi akiwa kama malaika wa nuru, ukimwomba kushikana mikono naye atakupa mkono wake, na wewe hutasikia chochote; nawe utaweza kumgundua.

9 Hizi ndizo funguo kuu tatu ambazo kwa njia hiyo ninyi mtaweza kujua iwapo huduma yoyote yatoka kwa Mungu.

SEHEMU YA 130

Orodha ya mafundisho yaliyotolewa na Joseph Smith Nabii, huko Ramus, Illinois, 2 Aprili 1843.

1–3, Baba na Mwana wao wenyewe wanaweza kujionyesha kwa mwanadamu; 4–7, Malaika huishi katika mazingira ya selestia; 8–9, Dunia ya kiselestia itakuwa Urimu na Thumimu iliyo kuu; 10–11, Jiwe jeupe linatolewa kwa wote waingiao kwenye ulimwengu wa selestia; 12–17, Wakati wa Ujio wa Pili Nabii amefichwa; 18–19, Akili ipatikanayo katika maisha haya itafufuka pamoja nasi katika Ufufuko; 20–21, Baraka zote huja kwa kutii sheria; 22–23, Baba na Mwana wana miili ya nyama na mifupa.

Wakati Mwokozi [a]atakapojidhihirisha tutamwona kama

129 1 *a* MWM Mbinguni.
b MWM Malaika.
c MWM Ufufuko.
2 *a* Lk. 24:39.
3 *a* MWM Roho.
b Ebr. 12:23; M&M 76:69.
8 *a* 2 Kor. 11:14; 2 Ne. 9:9.
130 1 *a* 1 Yoh. 3:2; Moro. 7:48.
MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.

alivyo. Tutamwona kuwa yeye ni [b]mtu kama sisi wenyewe.

2 Na kwamba uhusiano huu huu uliopo miongoni mwetu hapa utakuwepo miongoni mwetu kule, isipokuwa utazidishiwa [a]utukufu wa milele, utukufu ambao sasa hatuufaidi.

3 Yohana 14:23—Kuonekana kwa [a]Baba na [b]Mwana, katika mstari ule, ni [c]kujidhihirisha binafsi; na wazo la kwamba Baba na Mwana [d]watakaa katika moyo wa mwanadamu ni wazo la zamani la kimadhehebu, na ni uongo.

4 Kama jibu kwa swali—Je, si kweli kwamba jinsi wakati [a]unavyopimwa kwa Mungu, kwa malaika, kwa manabii, na kwa wanadamu, hutegemea na sayari ambayo wao huishi?

5 Najibu, Ndiyo. Lakini hakuna [a]malaika ambao huhudumia dunia hii ila wale ambao ni wa dunia hii, au walikuwa wa dunia hii.

6 Malaika hawaishi katika sayari kama hii dunia;

7 Bali huishi mbele za Mungu, kwenye tufe mfano wa [a]bahari ya kioo na [b]moto, mahali ambapo mambo yote kwa ajili ya utukufu wao huonekana, yaliyopita, yaliyopo, na yajayo, na daima yapo mbele za Bwana.

8 Mahali ambapo Mungu hukaa ni [a]Urimu na Thumimu iliyo kuu.

9 [a]Dunia hii, katika hali yake ya kutakaswa na isiyokufa, itafanywa kuwa mfano wa jiwe angavu kama kioo nayo itakuwa Urimu na Thumimu kwa wakazi wakaao juu yake, humo mambo yote yahusuyo ufalme mdogo, au falme zote za daraja la chini, zitaonekana kwa wale wakaao juu yake; na dunia hii itakuwa ya Kristo.

10 Ndipo jiwe jeupe lililotajwa katika Ufunuo 2:17, litakapokuwa Urimu na Thumimu kwa kila mmoja aliyepokea moja, ambalo kwalo hilo mambo yote yahusuyo falme za daraja la juu zitajulikana;

11 Na [a]jiwe jeupe limetolewa kwa kila mmoja wa wale wanaokuja katika ufalme wa selestia, ambapo juu yake [b]jina jipya limeandikwa, ambalo hakuna mtu ajuaye isipokuwa yeye yule mwenye kulipokea. Jina hilo jipya ni neno la ufunguo.

12 Ninatoa unabii, katika jina la Bwana Mungu, kwamba kuanza kwa [a]matatizo ambayo yatasababisha umwagaji mkubwa wa damu kabla ya kuja kwa Mwana wa Mtu yataanzia [b]Carolina ya Kusini.

13 Huenda ikaanza kutokana na swali la utumwa. Hii sauti

1 *b* Lk. 24:36–40.
2 *a* MWM Utukufu wa Selestia.
3 *a* MWM Mungu, Uungu—Mungu Baba.
b MWM Mungu, Uungu—Mungu Mwana.
c M&M 93:1.
d M&M 130:22. MWM Mungu, Uungu.
4 *a* 2 Pet. 3:8; Ibr. 3:4–10; tazama pia mchoro namba 2 wa Ibr., umbo 1.
5 *a* MWM Malaika.
7 *a* Ufu. 4:6; 15:2.
b Isa. 33:14.
8 *a* MWM Urimu na Thumimu.
9 *a* M&M 77:1. MWM Dunia—Hali ya mwisho ya dunia.
11 *a* Ufu. 2:17.
b Isa. 62:2.
12 *a* M&M 38:29; 45:63.
b M&M 87:1–5.

iliniambia, wakati nilipokuwa nikiomba kwa dhati juu ya jambo hili, Desemba, 25, 1832.

14 Nilikuwa wakati mmoja nikiomba kwa dhati kujua wakati wa [a]kuja kwa Mwana wa Mtu, wakati niliposikia sauti ikirudia yafuatayo:

15 Joseph, mwanangu, kama wewe utaishi mpaka kufikia umri wa miaka themanini na tano, utauona uso wa Mwana wa Mtu; kwa hiyo, acha hiyo yatosha, acha usinisumbue zaidi juu ya jambo hili.

16 Hivyo niliachwa, bila kuweza kuamua kama ujio huu unaozungumziwa ni kuanzia kwa milenia au ni baadhi ya kuonekana kwake kabla, au kama lazima nife na hivyo ndipo niuone uso wake.

17 Ninaamini ujio wa Mwana wa Mtu hautakuwa mapema kabla ya wakati huo.

18 Kanuni yoyote ya [a]akili tuipatayo katika maisha haya, itafufuka pamoja nasi katika [b]ufufuko.

19 Na kama mtu anapata [a]maarifa na akili katika maisha haya kwa njia ya [b]juhudi yake na [c]utii kuliko mwingine, yeye atakuwa na [d]heri ya juu zaidi katika ulimwengu ujao.

20 Kuna [a]sheria, isiyotenguliwa iliyowekwa mbinguni [b]kabla ya misingi ya ulimwengu huu, ambapo juu yake [c]baraka zote hutoka—

21 Na kama tunapata baraka yoyote kutoka kwa Mungu, ni kutokana na utii kwa sheria ile ambayo juu yake hutoka.

22 [a]Baba ana [b]mwili wa nyama na mifupa wenye kushikika kama wa mwanadamu; na Mwana vile vile; lakini [c]Roho Mtakatifu hana mwili wa nyama na mifupa, bali ni mtu wa Kiroho. Kama isingekuwa hivyo, Roho Mtakatifu asingeweza kukaa ndani yetu.

23 Mwanadamu aweza kumpokea [a]Roho Mtakatifu, na anaweza kushukia juu yake na asikae pamoja naye.

SEHEMU YA 131

Mafundisho ya Joseph Smith Nabii, yaliyotolewa huko Ramus, Illinois, 16 na 17 Mei 1843.

1–4, Ndoa ya selestia ni muhimu kwa kuinuliwa katika mbingu ya juu; 5–6, Jinsi watu wanavyotiwa muhuri kwa uzima wa milele inaelezwa; 7–8, Roho zote ni maada.

14 *a* MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
18 *a* MWM Akili, Viumbe-akili-asilia.
b MWM Ufufuko.
19 *a* MWM Maarifa.
b MWM Bidii.
c MWM Mtiifu, Tii, Utii.
d Alma 12:9–11.
20 *a* M&M 82:10.
b MWM Maisha kabla ya kuzaliwa.
c Kum. 11:26–28; M&M 132:5. MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
22 *a* MWM Mungu, Uungu.
b Mdo. 17:29.
c MWM Roho Mtakatifu.
23 *a* MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.

Katika utukufu wa [a]selestia kuna mbingu au daraja tatu;

2 Na ili kupata la [a]juu zaidi, mwanadamu lazima aingie katika utaratibu huu wa ukuhani [ikimaanisha [b]agano jipya na lisilo na mwisho la ndoa];

3 Na kama hakufanya hivyo, hawezi kulipata.

4 Anaweza kuingia katika nyingine, lakini huo ndiyo mwisho wa ufalme wake; hawezi [a]kuongezeka.

5 (17 Mei 1843.) Neno la [a]unabii lililo imara zaidi linamaanisha kujua kwamba mtu [b]ametiwa muhuri kwa [c]uzima wa milele, kwa njia ya ufunuo na roho wa unabii, kwa kupitia uwezo wa Ukuhani Mtakatifu.

6 Haiwezakani kwa mwanadamu [a]kuokolewa katika [b]ujinga.

7 Hakuna kitu kisichoundwa na maada. [a]Roho yote ni maada, lakini ni angavu zaidi au safi, na yaweza kutambuliwa tu kwa macho yaliyo [b]safi zaidi;

8 Hatuwezi kuiona; lakini wakati miili yetu itakaposafishwa tutaona kwamba yote ni maada.

SEHEMU YA 132

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Nauvoo, Illinois, 12 Julai 1843, juu ya agano jipya na lisilo la mwisho, pamoja na umilele wa agano la ndoa na kanuni ya ndoa ya wake wengi. Ingawa ufunuo uliandikwa katika mwaka 1843, ushahidi unaonyesha kwamba baadhi ya kanuni zilizomo ndani ya ufunuo huu zilikuwa zimejulikana kwa nabii mapema tangu mwaka 1831. Tazama Tamko Rasmi 1.

1–6, Kuinuliwa kunapatikana kupitia agano jipya na lisilo na mwisho; 7–14, Masharti na taratibu za agano hilo yaelezwa; 15–20, Ndoa ya selestia na kuendelea kwa kundi la familia kunawawezesha wanadamu kuwa miungu; 21–25, Njia nyembamba na iliyosonga huongoza kwenye uzawa wa milele; 26–27, Sheria yatolewa juu ya kumkufuru Roho Mtakatifu; 28–39, Ahadi ya kuongezeka milele na kuinuliwa zimefanywa kwa manabii na Watakatifu katika nyakati zote; 40–47, Joseph Smith amepewa uwezo wa kufunga na kutia muhuri duniani na mbinguni; 48–50, Bwana anafunga juu yake kuinuliwa kwake; 51–57, Emma Smith anashauriwa kuwa mwaminifu na mkweli; 58–66, Sheria zinazo tawala ndoa ya wake wengi zinawekwa.

131 1*a* M&M 76:70. MWM Utukufu wa Selestia.
2*a* M&M 132:5–21. MWM Kuinuliwa.
b MWM Ndoa, Oa, Olewa—Agano Jipya na la Lisilo na Mwisho la Ndoa.
4*a* M&M 132:16–17.
5*a* 2 Pet. 1:19. MWM Wito na Uteuzi.
b M&M 68:12; 88:4. MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
c MWM Uzima wa Milele.
6*a* MWM Wokovu.
b M&M 107:99–100.
7*a* MWM Roho.
b M&M 76:12; 97:16; Musa 1:11.

Amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana kwako wewe mtumishi wangu Joseph, kwamba kwa kadiri ulivyoniomba kutaka kujua na kufahamu katika nini Mimi, Bwana, niliwahesabia haki watumishi wangu Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, na pia Musa, Daudi na Sulemani, watumishi wangu, juu ya kanuni na mafundisho ya wao kuwa na [a]wake wengi na vimada—

2 Tazama, na lo, Mimi ndimi Bwana Mungu wako, nami nitakujibu juu ya jambo hili.

3 Kwa hiyo, [a]utayarishe moyo wako kupokea na kutii maelekezo ambayo ni karibu kuyatoa kwako; kwa maana wale wote ambao sheria hii ilifunuliwa kwao lazima waitii vile vile.

4 Kwa maana tazama, ninalifunua kwako [a]agano jipya na lisilo na mwisho; na kama hamkutii agano hilo, basi [b]mtahukumiwa; kwa maana hakuna mtu awezaye [c]kulikataa agano hili na kuruhusiwa kuingia katika utukufu wangu.

5 Kwani wote watakaopata [a]baraka kutoka kwangu wataitii [b]sheria iliyowekwa kwa ajili ya baraka hiyo, na masharti yake, kama yalivyowekwa tangu kabla ya kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu.

6 Na kuhusiana na [a]agano jipya na lisilo na mwisho, liliwekwa kwa ajili ya utimilifu wa [b]utukufu wangu; na yule aupokeaye utimilifu wake lazima atii sheria, vinginevyo atahukumiwa, asema Bwana Mungu.

7 Na amini ninawaambia, kwamba [a]masharti ya sheria hii ni haya: Maagano yote, mikataba, mapatano, ahadi, [b]viapo, nadhiri, utendaji, mahusiano, ushirika, au matarajio, ambayo hayakufanyika na kuingizwa ndani na [c]kufungwa na yule [d]Roho Mtakatifu wa ahadi, na yule aliyepakwa mafuta, kwa muda na vile vile kwa milele yote, na lililo takatifu zaidi, kwa [e]ufunuo na amri kwa njia ya mpakwa mafuta wangu, ambaye nimemteua juu ya dunia ili kushikilia uwezo huu (nami nimemteua mtumishi wangu Joseph kushikilia uwezo huu katika siku za mwisho, na hakuna mwingine isipokuwa mmoja tu juu ya dunia kwa wakati mmoja ambaye juu yake uwezo huu na [f]funguo za ukuhani huu hutunukiwa), maagano hayo hayataleta matokeo yanayofaa, uwezo, au nguvu katika ufufuko na baada ya ufufuko kutoka kwa wafu; kwani mikataba yote ile isiyofanywa kwa madhumuni haya inakoma watu wanapokufa.

132 1*a* M&M 132:34, 37–39. MWM Ndoa, Oa, Olewa—Ndoa ya wake wengi.
3*a* M&M 29:8; 58:6; 78:7.
4*a* MWM Agano.
b MWM Hukumu.
c M&M 131:1–4.
5*a* M&M 130:20–21.
b MWM Sheria.
6*a* M&M 66:2. MWM Agano Jipya na Lisilo na Mwisho.
b M&M 76:70, 92–96. MWM Utukufu wa Selestia.
7*a* M&M 88:38–39.
b MWM Kiapo.
c MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
d MWM Roho Mtakatifu wa Ahadi.
e MWM Ufunuo.
f MWM Funguo za Ukuhani.

8 Tazama, nyumba yangu ni nyumba ya utaratibu, asema Bwana Mungu, na siyo nyumba ya vurugu.

9 Je, nitakubali [a]matoleo, asema Bwana, ambayo hayakufanyika katika jina langu?

10 Au je, nitakipokea mikononi mwako kile ambacho [a]sikukiagiza?

11 Na je, nitakuagiza wewe, asema Bwana, isipokuwa iwe kwa sheria, hata kama vile Mimi na Baba yangu [a]tulivyowaagiza, kabla ya ulimwengu kuwako?

12 Mimi ndimi Bwana Mungu wako; na ninatoa kwako amri hii—kwamba mtu [a]haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi au kwa neno langu, ambalo ni sheria yangu, asema Bwana.

13 Na kila kitu kilichoko ulimwenguni, kama kimewekwa na wanadamu, na enzi, au himaya, au nguvu, au vitu vyenye kujulikana, chochote kitakacho kuwa, ambacho hakikuwekwa na Mimi au kwa neno langu, asema Bwana, kitatupwa chini, na [a]hakitabaki baada ya wanadamu kufariki, wala katika ufufuko au baada ya ufufuko, asema Bwana Mungu wenu.

14 Kwani vitu vyote vitakavyosalia vitakuwa vimewekwa na Mimi; na vitu vyovyote ambavyo havikuwekwa na Mimi vitatikiswa na kuangamizwa.

15 Kwa hiyo, kama mtu [a]ataoa mke ulimwenguni, na hamwoi mke kwa njia ya Mimi wala kwa njia ya neno langu, na akaagana naye ilimradi wako ulimwenguni na mke pamoja naye, agano lao na ndoa yao haitakuwa na nguvu wao wakifa, na wao wakiwa nje ya ulimwengu; kwa hiyo, wao hawafungwi na sheria yoyote wakati wakiwa nje ya ulimwengu.

16 Kwa hiyo, wakati wakiwa nje ya ulimwengu wao hawaoi wala [a]hawaolewi; bali huwa [b]malaika waliowekwa mbinguni, malaika ambao ni watumishi wahudumu, ili kuwahudumia wale wenye kustahili utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana.

17 Kwa kuwa malaika hawa hawakutii sheria yangu; kwa sababu hiyo, hawawezi kuongezeka, bali kubaki wametengana mmoja mmoja, pasipo kuinuliwa, katika hali yao ya kuokolewa, milele yote; na kutoka hapo na kuendelea wao siyo miungu, bali malaika wa Mungu milele na milele.

18 Na tena, amini ninawaambia, kama mtu ataoa mke, na kufanya agano pamoja naye kwa muda na kwa milele yote, kama agano hilo halijafanywa kwa njia yangu au kwa njia ya neno langu, ambalo ndilo sheria yangu, na kufungwa na Roho Mtakatifu wa ahadi, kupitia kwake yeye niliyempaka

9 *a* Moro. 7:5–6. MWM Dhabihu.
10 *a* Law. 22:20–25; Musa 5:19–23.
11 *a* M&M 132:5.
12 *a* Yn. 14:6.
13 *a* 3 Ne. 27:10–11.
15 *a* MWM Ndoa, Oa, Olewa.
16 *a* Mt. 22:23–33; Mk. 12:18–25; Lk. 20:27–36.
b MWM Malaika.

mafuta na kumteua kwa uwezo huu, kwa sababu hiyo, siyo halali wala haitakuwa na nguvu wawapo nje ya ulimwengu, kwa sababu hawakuunganishwa na Mimi, asema Bwana, wala kwa neno langu; wawapo nje ya ulimwengu haliwezi kupokelewa huko, kwa sababu ya malaika na miungu waliowekwa huko, ambao hawataweza kuwapita; kwa hiyo, hawawezi kurithi utukufu wangu; kwa maana nyumba yangu ni nyumba ya utaratibu, asema Bwana Mungu.

19 Na tena, amini ninawaambia, kama mtu ataoa mke kwa njia ya neno langu, ambalo ndilo sheria yangu, na kwa [a]agano jipya na lisilo na mwisho, na [b]ikafungwa kwao na Roho Mtakatifu wa [c]ahadi, na yeye aliyepakwa mafuta, na yeye niliyempa uwezo huu na [d]funguo za ukuhani huu; na itasemwa kwao—Mtafufuka katika ufufuko wa kwanza; na kama itakuwa baada ya ufufuko wa kwanza, katika ufufuko unaofuata; na mtarithi [e]enzi, falme, himaya, na nguvu, utawala kwa marefu na vina vyote—ndipo itaandikwa katika [f]Kitabu cha Uzima cha Mwanakondoo, ikiwa hataua, ambako ni kumwaga damu isiyo na hatia, na kama watatii katika agano langu, na hawakuua ambako ni kumwaga damu isiyo na hatia, itafanyika kwao katika mambo yote ambayo mtumishi wangu ameyaweka juu yao, kwa muda, na kwa milele yote; na yatakuwa na nguvu kamili wakati wakiwa nje ya ulimwengu; nao watawapita malaika, na miungu, ambao wamewekwa huko, kwa [g]kuinuliwa kwao na utukufu wao katika mambo yote, kama ilivyofungwa juu ya vichwa vyao, utukufu ambao utakuwa mkamilifu na kuendelea kwa vizazi milele na milele.

20 Kisha wao watakuwa miungu, kwa sababu hawana mwisho; kwa hiyo wao watakuwa tangu milele hadi milele, kwa sababu wanaendelea; kisha wao watakuwa juu ya vyote, kwa sababu vitu vyote vipo chini yao. Kisha watakuwa [a]miungu, kwa sababu wana [b]uwezo wote, na malaika watakuwa chini yao.

21 Amini, amini, ninawaambia, isipokuwa mmetii [a]sheria yangu, hamwezi kuufikia utukufu huu.

22 Kwa maana mlango ni [a]mwembamba, na [b]njia imesonga iongozayo kwenye kuinuliwa na mwendelezo wa [c]uzazi,

19 *a* MWM Ndoa, Oa, Olewa—Agano Jipya na la Lisilo na Mwisho la Ndoa.
b MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
c M&M 76:52–53; 88:3–4.
d MWM Funguo za Ukuhani.
e Ku. 19:5–6; Ufu. 5:10; 20:6; M&M 76:56; 78:15, 18.
f MWM Kitabu cha Uzima.
g MWM Kuinuliwa.
20 *a* Mt. 25:21; M&M 29:12–13; 132:37.
MWM Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, uwezekano wa kuwa kama Baba wa Mbinguni.
b M&M 50:26–29; 76:94–95; 84:35–39.
21 *a* MWM Sheria.
22 *a* Lk. 13:24; 2 Ne. 33:9; Hel. 3:29–30.
b Mt. 7:13–14, 23; 2 Ne. 9:41; 31:17–21.
c M&M 132:30–31.

nao waionayo ni wachache, kwa sababu hamnipokei Mimi ulimwenguni wala hamnijui.

23 Lakini kama mtanipokea Mimi ulimwenguni, basi mtanijua, nanyi mtapokea kuinuliwa kwenu; ili [a]mahali nilipo nanyi muwepo pia.

24 Huu ndiyo [a]uzawa wa milele—kumjua Mungu wa pekee mwenye hekima na kweli, na Yesu Kristo, [b]aliyemtuma. Mimi ndiye. Kwa hiyo ipokeeni, sheria yangu.

25 Mlango ni [a]mpana, na njia ni pana iongozayo [b]mautini; nao ni wengi waingiao kwa mlango huo, kwa sababu [c]hawanipokei Mimi, wala hawakai katika sheria yangu.

26 Amini, amini, ninawaambia, kama mtu ataoa mke kulingana na neno langu, nao wakafungwa na [a]Roho Mtakatifu wa ahadi, kulingana na yale niliyoyaweka, na kama mume au mke akitenda dhambi yoyote au kuvunja agano jipya na lisilo na mwisho, na aina zote za kufuru, na kama [b]hawakuua ambako ni kumwaga damu isiyo na hatia, bado wataamka katika ufufuko wa kwanza, na kuingia katika kuinuliwa kwao; lakini wataangamizwa katika mwili, na [c]watatolewa kwa karamu ya [d]Shetani hadi siku ya ukombozi, asema Bwana Mungu.

27 [a]Kufuru dhidi ya Roho Mtakatifu, ambayo [b]haitasamehewa ulimwenguni wala nje ya ulimwengu, inajumuisha katika mauaji yenu ambako ndiko kumwaga damu isiyo na hatia, na kukubali kifo changu, baada ya kupokea agano langu jipya na lisilo na mwisho, asema Bwana Mungu; na yule asiyetii sheria hii kamwe hawezi kuingia katika utukufu wangu, bali [c]atalaaniwa, asema Bwana.

28 Mimi ndimi Bwana Mungu wenu, na nitawapa sheria ya Ukuhani wangu Mtakatifu, kama ilivyowekwa na Mimi na Baba yangu kabla ya ulimwengu kuwako.

29 [a]Ibrahimu alipokea mambo yote, yoyote aliyapokea, kwa ufunuo na amri, kwa neno langu, asema Bwana, naye ameingia katika kuinuliwa kwake, na ameketi juu ya kiti chake cha enzi.

30 Ibrahimu alipokea [a]ahadi juu ya uzao wake, na juu ya tunda la viuno vyake—ambako katika [b]viuno vyake ninyi mmetoka, kama, mtumishi wangu Joseph—ambayo ilipaswa kuendelea ilimradi wao walikuwepo duniani; na juu ya Ibrahimu

23 *a* Yn. 14:2–3.
24 *a* Yn. 17:3. MWM Uzima wa Milele.
b Yn. 3:16–17; M&M 49:5.
25 *a* Mt. 7:13–14; 3 Ne. 14:13–15.
b MWM Mauti ya Kiroho.
c Yn. 5:43.
26 *a* MWM Roho Mtakatifu wa Ahadi.
b Alma 39:5–6.
c M&M 82:21; 104:9–10.
d MWM Ibilisi.
27 *a* MWM Dhambi isiyo sameheka; Kukufuru, Kufuru.
b Mt. 12:31–32; Ebr. 6:4–6; M&M 76:31–35. MWM Wana wa Upotevu.
c MWM Hukumu.
29 *a* MWM Ibrahimu.
30 *a* Mwa. 12:1–3; 13:16. MWM Agano la Ibrahimu; Ibrahimu—Uzao wa Ibrahimu.
b 2 Ne. 3:6–16.

na uzao wake, nje ya ulimwengu wanapaswa kuendelea; kote ulimwenguni na nje ya ulimwengu yapaswa waendelee kama vile [c]nyota zisizoweza kuhesabika; au, kama ungeliambiwa kuhesabu mchanga wa pwani ya bahari usingeliweza kuuhesabu.

31 Ahadi hii ni yenu pia, kwa sababu ninyi ni wa [a]Ibrahimu, na ahadi ilifanywa kwa Ibrahimu; na kwa sheria hii kazi ya Baba yangu inaendelea, ambamo hujitukuza yeye mwenyewe.

32 Enendeni, kwa hiyo, na mkazifanye [a]kazi za Ibrahimu; ingieni katika sheria yangu nanyi mtaokolewa.

33 Lakini kama hamtaingia katika sheria yangu hamuwezi kupata ahadi za Baba yangu, ambazo alizifanya kwa Ibrahimu.

34 Mungu [a]alimwamuru Ibrahimu, na [b]Sara akamtoa [c]Hajiri kwa Ibrahimu kuwa mke. Na ni kwa nini Sara alifanya hivyo? Kwa sababu hii ilikuwa sheria; na kutoka kwa Hajiri wamechipuka watu wengi. Hii, kwa hiyo, ilikuwa ni kutimiza, miongoni mwa mambo mengine, ahadi ile.

35 Je, Ibrahimu, kwa hiyo, alikuwa na hatia? Amini ninawaambia, Hapana; kwa maana Mimi, Bwana, [a]niliamuru hilo.

36 [a]Ibrahimu aliamriwa kumtoa mwanawe [b]Isaka; hata hivyo, iliandikwa: [c]Usiue. Ibrahimu, hata hivyo, hakukataa, na ilihesabiwa kwake kuwa ni [d]haki.

37 Ibrahimu aliwapokea [a]vimada, nao wakamzalia watoto; na ilihesabiwa kwake kuwa ni haki, kwa sababu walitolewa kwake, naye alitii sheria yangu; kama vile Isaka pia na [b]Yakobo hawakufanya kitu kingine chochote isipokuwa kile walichoamriwa; na kwa sababu hawakufanya kitu kingine zaidi ya kile walichoamriwa, wao wameingia katika [c]kuinuliwa kwao, kulingana na ahadi, na wamekaa juu ya viti vyao vya enzi, na wao siyo malaika bali ni miungu.

38 [a]Daudi pia aliwapokea [b]wake wengi na vimada, na pia Suleimani na Musa watumishi wangu, na pia wengine wengi wa watumishi wangu, tangu mwanzo wa uumbaji hadi sasa; na hawakufanya dhambi katika lolote isipokuwa katika mambo yale ambayo hawakuyapata kutoka kwangu.

39 Wake na vimada wa Daudi [a]aliopewa kutoka kwangu,

30 *c* Mwa. 15:5; 22:17.
31 *a* M&M 86:8–11; 110:12.
32 *a* Yn. 8:39; Alma 5:22–24.
34 *a* Mwa. 16:1–3.
b MWM Sara.
c Mwa. 25:12–18. MWM Hajiri.
35 *a* Yak. (KM) 2:24–30.
36 *a* Mwa. 22:2–12.
b MWM Isaka.
c Ku. 20:13.
d Yak. (KM) 4:5. MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
37 *a* MY wake wengine. Mwa. 25:5–6.
b Mwa. 30:1–4; M&M 133:55. MWM Yakobo, Mwana wa Isaka.
c MWM Kuinuliwa; Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, uwezekano wa kuwa kama Baba wa Mbinguni.
38 *a* MWM Daudi.
b 1 Sam. 25:42–43; 2 Sam. 5:13; 1 Fal. 11:1–3.
39 *a* 2 Sam. 12:7–8.

kwa mkono wa Nathani, mtumishi wangu, na manabii wengine waliokuwa na [b]funguo za uwezo huu; na katika mambo haya hakunitendea dhambi yoyote isipokuwa katika shauri la [c]Uria na mke wake; na, kwa sababu hiyo ameanguka katika kuinuliwa kwake, na amepokea sehemu yake; naye hatawarithi nje ya ulimwengu, kwa kuwa [d]nimewatoa kwa mwingine, asema Bwana.

40 Mimi ndimi Bwana Mungu wako, na nimekupa wewe, mtumishi wangu Joseph, nafasi yenye mamlaka, na [a]urejeshe mambo yote. Omba utakacho, nawe utapewa kulingana na neno langu.

41 Na kwa kuwa umeuliza juu ya uzinzi, amini, amini, ninawaambia, kama mtu atampokea mke katika agano jipya na lisilo na mwisho, na kama mke atakuwa na mwanaume mwingine, na ambaye hakupewa nami kwa mpako mtakatifu wa mafuta, mwanamke huyo amezini na ataangamizwa.

42 Kama mwanamke huyo hatakuwa katika agano jipya na lisilo na mwisho, naye atakutwa na mwanaume mwingine, atakuwa [a]amezini.

43 Na kama mume wake atakuwa na mwanamke mwingine, naye mume yuko chini ya [a]nadhiri, yeye amevunja nadhiri yake na atakuwa amezini.

44 Na kama mke hajafanya uzinzi, bali hana hatia na kwamba hajavunja nadhiri yake, naye anajua hilo, na mimi nikakufunulia wewe, mtumishi wangu Joseph, basi wewe utakuwa na uwezo, kwa uwezo wa Ukuhani wangu Mtakatifu, kumchukua mwanamke huyo na kumpa yeye ambaye hajazini ila amekuwa [a]mwaminifu; kwa maana yeye atafanywa kuwa mtalawa juu ya mengi.

45 Kwa maana nimeweka juu yako [a]funguo na uwezo wa ukuhani, ambamo ndani yake [b]nitarejesha mambo yote, na nitayajulisha kwako mambo yote kwa wakati wake.

46 Na amini, amini, ninakuambia, kwamba lolote [a]utakalolifunga duniani litakuwa limefungwa mbinguni; na lolote utakalolifunga duniani, katika jina langu na kwa neno langu, asema Bwana, litakuwa limefungwa milele mbinguni; na dhambi zozote [b]utakazozisamehe duniani zitakuwa zimesamehewa milele mbinguni; na dhambi zozote mtakazo ziacha pasipo msamaha duniani zitakuwa hazina msamaha mbinguni.

47 Na tena, amini ninakua-

39 *b* MWM Funguo za Ukuhani.
c 2 Sam. 11:4, 27; 12:9; 1 Fal. 15:5.
MWM Mauaji; Uzinzi.
d Yer. 8:10.
40 *a* JS—H 1:33.
MWM Urejesho wa Injili.
42 *a* M&M 42:22–26.
43 *a* MWM Agano; Ndoa, Oa, Olewa.
44 *a* MWM Usafi wa Kimwili.
45 *a* MWM Funguo za Ukuhani.
b Mdo. 3:21; M&M 86:10.
MWM Urejesho wa Injili.
46 *a* MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
b MWM Ondoleo la Dhambi.

mbia, yeyote utakayembariki nitambariki, na yeyote utakaye mlaani [a]nitamlaani, asema Bwana; kwa maana Mimi, Bwana, ndiye Mungu wako.

48 Na tena, amini ninakuambia, mtumishi wangu Joseph, kwamba utakalotoa duniani, na kwa yeyote utakayempa lolote duniani, kwa neno langu na kulingana na sheria yangu, litajiliwa na baraka na siyo laana, na pamoja na uwezo wangu, asema Bwana, nalo halitakuwa na hukumu duniani na mbinguni.

49 Kwa maana Mimi ndimi Bwana Mungu wako, nami nitakuwa pamoja nawe hata [a]mwisho wa ulimwengu, na milele yote; kwa kuwa amini ninatia [b]muhuri juu ya [c]kuinuliwa kwako, na kutengeneza kiti cha enzi kwa ajili yako katika ufalme wa Baba yangu, pamoja na Ibrahimu [d]baba yako.

50 Tazama, nimeona [a]dhabihu zako, nami nitakusamehe dhambi zako zote; nimeona dhabihu zako katika utii kwa kile nilichokuambia. Kwa hiyo, nenda zako, nami nitakufanyia mlango wa kutorokea, kama vile [b]nilivyokubali matoleo ya Ibrahimu ya mwanawe Isaka.

51 Amini, ninakuambia: Amri ninampa mjakazi wangu, Emma Smith, mke wako, ambaye nimekupa, kwamba ajizuie na asipokee kile ambacho nilikuamuru kumpa yeye; kwa kuwa nilifanya vile, asema Bwana, ili kuwajaribu ninyi nyote, kama vile nilivyomjaribu Ibrahimu, na ili nipate kutaka matoleo yangu kutoka mikononi mwenu, kwa agano na dhabihu.

52 Na acha mjakazi wangu, [a]Emma Smith, awapokee wale wote ambao nimempa mtumishi wangu Joseph, na ambao ni wema na wasafi mbele zangu; na wale ambao siyo safi, na wamesema kwamba wao ni wasafi, wataangamizwa, asema Bwana Mungu.

53 Kwa maana Mimi ndimi Bwana Mungu wako, nanyi mtatii sauti yangu; na ninamweka mtumishi wangu Joseph, kwamba atakuwa mtawala juu ya mambo mengi; kwa maana yeye amekuwa [a]mwaminifu juu ya mambo machache, na kutoka sasa na kuendelea nitamuimarisha.

54 Na ninamwamuru mjakazi wangu, Emma Smith, kumtii na kuambatana na mtumishi wangu Joseph, na siyo mwingine. Lakini kama hatatii amri hii ataangamizwa, asema Bwana; kwa maana Mimi ndimi Bwana Mungu wako, nami nitamwangamiza yeye kama hatatii katika sheria yangu.

55 Lakini kama hatatii amri hii, basi mtumishi wangu Joseph atafanya mambo yote kwa ajili yake, hata kama vile alivyosema; nami nitambariki yeye na kumzidisha na kumpa yeye [a]mara mia katika ulimwengu

47 *a* Mwa. 12:1–3; M&M 124:93.
49 *a* Mt. 28:20.
b M&M 68:12.
c M&M 5:22.
MWM Wito na Uteuzi.
d Mwa. 17:1–8; 2 Ne. 8:2.
50 *a* MWM Dhabihu.
b Mwa. 22:10–14; M&M 97:8.
52 *a* MWM Smith, Emma Hale.
53 *a* Mt. 25:21; M&M 52:13.
55 *a* Mk. 10:28–31.

huu, mamia ya baba na mama, kaka na dada, nyumba na ardhi, wake na watoto, na mataji ya [b]vizazi vya milele katika ulimwengu wa milele.

56 Na tena, amini ninasema, acha mjakazi wangu [a]amsamehe mtumishi wangu Joseph makosa yake; na ndipo yeye naye atasamehewa makosa yake, ambayo amenikosea Mimi; na Mimi, Bwana Mungu wako, nitambariki, na kumzidisha, na kuufanya moyo wake ufurahi.

57 Na tena, ninasema, na mtumishi wangu Joseph asitoe mali yake mikononi mwake, asije adui akaja na kumwangamiza; kwani Shetani [a]anatafuta kumwangamiza; kwa maana Mimi ndimi Bwana Mungu wako, na yeye ni mtumishi wangu; na tazama, na lo, Mimi niko pamoja naye, kama nilivyokuwa pamoja na Ibrahimu, baba yako, hata kwenye [b]kuinuliwa kwake na utukufu wake.

58 Sasa, kuhusu sheria ya [a]ukuhani, kuna mambo mengi yanayohusiana nayo.

59 Amini, kama mtu ameitwa na Baba yangu, kama ilivyokuwa kwa [a]Haruni, kwa sauti yangu mwenyewe, na kwa sauti ya yule aliyenituma, nami nikampa yeye endaomenti ya [b]funguo za uwezo wa ukuhani huu, kama atafanya lolote katika jina langu, na kulingana na sheria yangu na kwa neno langu, hatafanya dhambi, nami nitamhesabia haki.

60 Msiache mtu yeyote, kwa hiyo, amshambulie mtumishi wangu Joseph; kwa maana Mimi nitamhesabia haki yeye; kwa maana atafanya dhabihu ambayo ninaitaka kutoka kwake kwa ajili ya uvunjaji wake wa sheria, asema Bwana Mungu wenu.

61 Na tena, kuhusu sheria ya ukuhani—kama mtu yeyote atamposa [a]bikira, na kutamani kuposa [b]mwingine, na wa kwanza akatoa idhini yake, na kama atamposa yule wa pili, nao ni mabikira, nao hawakuweka nadhiri kwa mwanaume mwingine, huyo anahesabiwa haki; hawezi kufanya uzinzi kwa maana wametolewa kwake; kwa kuwa hawezi kufanya uzinzi kwa kile kilicho chake ambacho si cha mwingine yeyote.

62 Na kama anao mabikira kumi aliopewa kwa sheria hii, hawezi kufanya uzinzi, kwani ni mali yake; nao wametolewa kwake; kwa hiyo yeye anahesabiwa haki.

63 Lakini kama mmoja au yeyote wa mabikira hao kumi, baada ya kuposwa, atakuwa na mwanaume mwingine, atakuwa amezini, naye ataangamizwa; kwa maana wao wametolewa kwake ili [a]kuongezeka na

55 *b* MWM Familia—Familia ya milele; Uzima wa Milele.
56 *a* MWM Samehe.
57 *a* Mt. 10:28.
b MWM Kuinuliwa.
58 *a* M&M 84:19–26. MWM Ukuhani.
59 *a* Ebr. 5:4. MWM Haruni, Kaka wa Musa.
b MWM Funguo za Ukuhani.
61 *a* MWM Bikira.
b TR 1. MWM Ndoa, Oa, Olewa—Ndoa ya wake wengi.
63 *a* Mwa. 1:26–28; Yak. (KM) 2:30.

kuijaza nchi, kulingana na amri yangu, na kutimiza ahadi iliyotolewa na Baba yangu kabla ya kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, na kwa ajili ya kuinuliwa kwao katika dunia za milele, ili wapate kuzaa roho za wanadamu; kwani humo ndimo [b]kazi ya Baba yangu huendelezwa, ili apate kutukuzwa.

64 Na tena, amini, amini, ninawaambia, kama mtu yeyote aliye na mke, mtu mwenye kushikilia funguo za uwezo huu, na humfundisha sheria za ukuhani wangu, kuhusu mambo haya, halafu akaamini na amhudumie, la sivyo ataangamizwa, asema Bwana Mungu wenu; kwa maana nitamwangamiza; kwa kuwa nitalitukuza jina langu juu ya wale wote waipokeao na kutii sheria yangu.

65 Kwa hiyo, itakuwa haki kwangu, kama hataipokea sheria hii, kwa yeye kupokea mambo yoyote yale Mimi, Bwana Mungu wake, nitakayompa, kwa sababu yeye mke haamini na hamhudumii kulingana na neno langu; na ndipo yeye mke huwa mvunjaji wa sheria; na yeye mume anasamehewa kutokana na sheria ya Sara, ambaye alimhudumia Ibrahimu kulingana na sheria wakati nilipomwamuru Ibrahimu kumchukua Hajiri kuwa mke.

66 Na sasa, kuhusu sheria hii, amini, amini, ninakuambia wewe, nitakufunulia zaidi, baadaye; kwa hiyo, hii inatosha kwa sasa. Tazama, Mimi ni Alfa na Omega. Amina.

SEHEMU YA 133

Ufunuo uliotolewa kupitia Joseph Smith Nabii, huko Hiram, Ohio, 3 Novemba 1831. Akiandika dibaji ya ufunuo huu Historia ya Joseph Smith inasema, "Kwa wakati huu palikuwa na mambo mengi ambayo Wazee walitaka kujua kuhusiana na kuhubiriwa kwa Injili kwa wakazi wa dunia, na juu ya kukusanyika; na ili kuenenda katika nuru ya kweli, na kufundishwa kutoka juu, mnamo 3 Novemba 1831, mimi nilimwomba Bwana na kupokea ufunuo muhimu ufuatao." Sehemu hii kwanza iliongezwa kwenye kitabu cha Mafundisho na Maagano kama kiambatisho, na mwishowe ikapewa namba kama sehemu.

1–6, Watakatifu wanaamriwa kujitayarisha kwa ajili ya Ujio wa Pili; 7–16, Watu wote wanaamriwa kuikimbia Babilonia, na kuja Sayuni, na kujiandaa kwa ajili ya siku ile iliyo kuu ya Bwana; 17–35, Yeye atasimama juu ya Mlima Sayuni, mabara yatakuwa nchi moja, na makabila yaliyopotea ya Israeli yatarudi; 36–40, Injili ilirejeshwa kupitia Joseph Smith ili kuhubiriwa katika ulimwengu

63 *b* Musa 1:39.

wote; 41–51, Bwana atashuka kulipiza kisasi kwa waovu; 52–56, Utakuwa mwaka wa wakombolewa Wake; 57–74, Injili itapelekwa ili kuwaokoa Watakatifu na kwa ajili ya angamizo la waovu.

Sikilizeni, Enyi watu wa kanisa langu, asema Bwana Mungu wenu, na sikieni neno la Bwana juu yenu—

2 Bwana ambaye [a]atakuja ghafla katika hekalu lake; Bwana ambaye atashuka juu ya ulimwengu wa laana ili [b]kuhukumu; ndiyo, juu ya mataifa yote yenye kumsahau Mungu, na juu ya wote wasio cha Mungu walio miongoni mwenu.

3 Kwani atauweka [a]wazi mkono wake mtakatifu machoni pa mataifa yote, na miisho yote ya dunia yatauona [b]wokovu wa Mungu wao.

4 Kwa hiyo jitengenezeeni, jitengenezeeni, Enyi watu wangu; jitakaseni ninyi wenyewe; kusanyikeni pamoja, Enyi watu wa kanisa langu, juu ya nchi ya Sayuni, ninyi nyote ambao hamkuamriwa kukaa.

5 Tokeni katika [a]Babilonia. Kuweni [b]safi ninyi mnaochukua vyombo vya Bwana.

6 Kuweni na makusanyiko yenu ya kiroho, na [a]msemezane ninyi kwa ninyi mara kwa mara. Na acheni kila mtu alilingane jina la Bwana.

7 Ndiyo, amini ninawaambia tena, wakati umewadia ambapo sauti ya Bwana ipo kwenu ninyi: Tokeni Babilonia; [a]jikusanyeni kutoka miongoni mwa mataifa, kutoka pepo [b]nne, kutoka kona moja ya mbingu hadi nyingine.

8 [a]Wapelekeni wazee wa kanisa langu kwa mataifa yaliyo mbali; kwenye [b]visiwa vya bahari; wapelekeni kwenye nchi za kigeni; yasihini mataifa yote, kwanza juu ya [c]Wayunani, na halafu juu ya [d]Wayahudi.

9 Na tazama, na lo, hiki kitakuwa kilio chao, na sauti ya Bwana kwa watu wote: Enendeni nchi ya Sayuni, ili mipaka ya watu wangu ipate kupanuka, na ili [a]vigingi vyake vipate kuimarishwa, na ili [b]Sayuni ipate kuenea hata maeneo yaliyo karibu.

10 Ndiyo, acheni kilio kiendelee miongoni mwa watu wote: Amkeni na simameni na kwenda kumlaki [a]Bwana harusi; tazama na lo, Bwana harusi yu aja; tokeni mwende kumlaki.

133 2*a* Mal. 3:1; M&M 36:8.
b M&M 1:36.
MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.
3*a* Isa. 52:10.
b Isa. 12:2; 52:10.
MWM Mpango wa Ukombozi; Wokovu.
5*a* Alma 5:57; M&M 1:16.
MWM Babeli, Babilonia; Malimwengu.
b 2 Tim. 2:21; 3 Ne. 20:41; M&M 38:42.
MWM Safi na Isiyo safi.
6*a* Mal. 3:16–18.
7*a* M&M 29:8.
MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b Zek. 2:6–7; Mk. 13:27.
8*a* MWM Kazi ya kimisionari.
b Isa. 11:11; 1 Ne. 22:4; 2 Ne. 10:8, 20.
c MWM Wayunani.
d MWM Wayahudi.
9*a* Isa. 54:2.
MWM Kigingi.
b MWM Sayuni.
10*a* Mt. 25:6; M&M 33:17–18; 45:54–59.
MWM Bwana Harusi.

Jiwekeni tayari kwa ajili ya [b]siku ile iliyo kuu ya Bwana.

11 [a]Kesheni, kwa sababu [b]hamjui siku wala saa.

12 Kwa hiyo, waacheni wao, walio [a]miongoni mwa Wayunani wakimbilie [b]Sayuni.

13 Na acha walio wa [a]Yuda wakimbilie [b]Yerusalemu, katika [c]milima ya [d]nyumba ya Bwana.

14 Tokeni miongoni mwa mataifa, hata kutoka Babilonia, kutoka katikati ya uovu, ambao ni Babeli ya kiroho.

15 Lakini amini, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, acheni kukimbia kwenu kusiwe katika [a]haraka, bali mambo yote yatengenezwe mbele yenu; na yule aendaye, na [b]asiangalie nyuma lisije angamizo la ghafla likaja juu yake.

16 Sikilizeni na msikie, Enyi wakazi wa dunia. [a]Sikieni kwa pamoja, ninyi wazee wa kanisa langu, na msikie sauti ya Bwana; kwani awaita watu wote, naye huwaamuru watu wote kila mahali [b]kutubu.

17 Kwani tazama, Bwana Mungu [a]amemtuma malaika akilia katikati ya mbingu, akisema: Itengenezeni njia ya Bwana, na [b]yanyoosheni mapito yake, kwani saa ya [c]kuja kwake imekaribia—

18 Wakati [a]Mwanakondoo atakaposimama juu ya [b]Mlima Sayuni, na pamoja naye watu [c]mia arobaini na nne elfu, wenye jina la Baba yake limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao.

19 Kwa hiyo, jitayarisheni kwa ajili ya [a]ujio wa [b]Bwana harusi; nendeni, nendeni nje kumlaki.

20 Kwani tazama, [a]atasimama juu ya mlima wa Mizeituni, na juu ya bahari kuu, hata vilindi vikuu, na juu ya visiwa vya bahari, na juu ya nchi ya Sayuni.

21 Naye [a]atatoa sauti yake toka [b]Sayuni, naye atasema kutoka Yerusalemu, na sauti yake itasikika miongoni mwa watu wote;

22 Na itakuwa kama [a]sauti ya maji mengi, na kama sauti ya [b]radi kuu, ambayo [c]itaivunja milima, na mabonde hayataonekana.

23 Ataviamuru vilindi vikuu, navyo vitasukumwa kurudi katika nchi za kaskazini, na [a]visiwa vitakuwa nchi moja;

24 Na nchi ya [a]Yerusalemu na

10 *b* M&M 1:12–14.
11 *a* Mk. 13:32–37; JS—M 1:46, 48.
b M&M 49:7.
12 *a* M&M 38:31, 42.
b MWM Sayuni.
13 *a* MWM Yuda.
b MWM Yerusalemu.
c Isa. 2:1–3; Eze. 38:8.
d Zab. 122.
15 *a* Isa. 52:10–12; M&M 58:56.
b Mwa. 19:17, 26; Lk. 9:62.
16 *a* M&M 1:1–6.
b MWM Toba, Tubu.
17 *a* M&M 13; 27:7–8; 88:92.
b Isa. 40:3–5.
c Mal. 3:1.
18 *a* Ufu. 14:1.
MWM Mwanakondoo wa Mungu.
b M&M 84:2.
c Ufu. 7:1–4.
19 *a* Mt. 25:1–13; M&M 33:17–18; 88:92.
MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b MWM Bwana Harusi.
20 *a* Zek. 14:4; M&M 45:48–53.
21 *a* Yoe. 3:16; Amo. 1:2.
b Isa. 2:2–4.
22 *a* Eze. 43:2; Ufu. 1:15; M&M 110:3.
b Zab. 77:18; Ufu. 14:2.
c Amu. 5:5; Isa. 40:4; 64:1; Ufu. 16:20; M&M 49:23; 109:74.
23 *a* Ufu. 6:14.
24 *a* MWM Yerusalemu.

nchi ya Sayuni zitarudishwa katika mahali pao, na dunia itakuwa kama ilivyokuwa katika siku zile kabla ya [b]kugawanyika.

25 Na Bwana, hata Mwokozi, atasimama katikati ya watu wake, naye [a]atatawala juu ya wote wenye mwili.

26 Nao walioko katika nchi za [a]kaskazini watakumbukwa mbele za Bwana; na manabii wao wataisikia sauti yake, nao hawataweza tena kujizuia; nao wataipiga miamba, na barafu itatiririka mbele ya uwepo wao.

27 Na [a]njia kuu itainuliwa katikati ya vilindi vikuu.

28 Maadui zao watakuwa mawindo kwao,

29 Na katika jangwa [a]kame yatajitokeza mabwawa ya maji ya uzima; na ardhi kavu haitakuwa tena nchi yenye kiu.

30 Nao wataleta hazina za utajiri wao kwa watoto wa [a]Efraimu, mtumishi wangu.

31 Na mipaka ya [a]vilima isiyo na mwisho itatetemeka mbele ya uwepo wao.

32 Na hapo wataanguka chini na kuvikwa taji la utukufu, hata katika Sayuni, kwa mikono ya watumishi wa Bwana, hata watoto wa Efraimu.

33 Nao watajawa na [a]nyimbo za shangwe isiyo na mwisho.

34 Tazama, hii ndiyo baraka ya Mungu asiye na mwisho juu ya [a]makabila ya Israeli, na baraka iliyo kuu juu ya kichwa cha [b]Efraimu na wenzake.

35 Na wao pia wa kabila la [a]Yuda, baada ya machungu yao watatakaswa katika [b]utakatifu mbele za Bwana, ili kukaa mbele za uwepo wake mchana na usiku, milele na milele.

36 Na sasa, amini hivi ndivyo asema Bwana, ili mambo haya yapate kujulikana miongoni mwenu, Enyi wakazi wa dunia, nimemtuma [a]malaika wangu akiruka katikati ya mbingu, mwenye [b]injili isiyo na mwisho, ambaye amewatokea baadhi na kuikabidhi kwa mwanadamu, ambaye ataonekana kwa wengi wale wakaao duniani.

37 Na [a]injili hii [b]itahubiriwa kwa [c]kila taifa, na kabila, na lugha, na watu.

38 Na watumishi wa Mungu watakwenda, wakisema kwa sauti kubwa: Mcheni Mungu na mtukuzeni yeye, kwa maana saa ya hukumu yake imefika;

39 Na [a]mwabuduni yeye aliyezifanya mbingu, na dunia,

24*b* Mwa. 10:25. MWM Dunia—Kugawanywa kwa dunia.
25*a* MWM Yesu Kristo—Utawala wa Kristo katika milenia.
26*a* Yer. 16:14–15; M&M 110:11. MWM Israeli—Makabila Kumi ya Israeli yaliyopotea.
27*a* Isa. 11:15–16; 2 Ne. 21:16.
29*a* Isa. 35:6–7.
30*a* Zek. 10:7–12. MWM Efraimu—Kabila la Efraimu.
31*a* Mwa. 49:26.
33*a* Isa. 35:10; 51:11; M&M 66:11.
34*a* MWM Israeli—Makabila kumi na mawili ya Israeli.
b Mwa. 48:14–20; 1 Nya. 5:1–2; Eth. 13:7–10.
35*a* MWM Yuda—Kabila la Yuda.
b MWM Utakatifu.
36*a* Ufu. 14:6–7; M&M 20:5–12.
b MWM Urejesho wa Injili.
37*a* MWM Injili.
b MWM Hubiri; Kazi ya kimisionari.
c M&M 42:58.
39*a* MWM Kuabudu.

na bahari, na chemi chemi za maji—

40 Mkililingana jina la Bwana mchana na usiku, mkisema: Ee laiti [a]ungepasua mbingu, ili ushuke ili milima ipate kutiririka mbele zako.

41 Na itajibiwa juu ya vichwa vyao; kwa maana uwepo wa Bwana utakuwa kama moto wenye kuyeyuka unaowaka uunguzao, na kama moto ufanyao maji [a]kuchemka.

42 Ee Bwana, utashuka chini ili kuwajulisha adui zako jina lako, na mataifa yote yatatetemeke mbele zako—

43 Unapofanya mambo ya kutisha, mambo wasiyoyatazamia;

44 Ndiyo, ushukapo, na milima kutiririka mbele zako, wewe [a]wamlaki yeye afurahiaye yaliyo ya haki na kuyatenda, wale wakukumbukao katika njia zako.

45 Maana tangu mwanzo wa ulimwengu watu hawakusikia wala kufahamu kwa masikio, wala jicho lolote halikuona, Ee Mungu, zaidi yako wewe, ni mambo gani makuu [a]uliyoyaandaa kwa ajili yake yeye [b]akungojae wewe.

46 Na itasemwa: Ni [a]nani yule [b]ashukaye kutoka kwa Mungu mbinguni mwenye mavazi yaliyotiwa rangi; ndiyo, kutoka sehemu zisizojulikana, aliyevikwa katika mavazi yake matukufu, akitembea katika ukuu wa nguvu zake?

47 Naye atasema: Mimi ndiye niliyenena katika haki, mwenye nguvu ya kuokoa.

48 Naye Bwana atakuwa [a]mwekundu katika mavazi yake, na nguo zake kama za yule akanyagaye katika pipa la mvinyo.

49 Na uwepo wake utakuwa na utukufu mkubwa kiasi kwamba [a]jua litauficha uso wake kwa aibu, na mwezi itaizuia nuru yake, nazo nyota zitaondoshwa kutoka mahali pake.

50 Na sauti yake itasikika: [a]Nalikanyaga shinikizo la mvinyo pekee yangu, na nimeileta hukumu juu ya watu wote; na hakuna hata mmoja aliyekuwa pamoja nami;

51 Na nimewavyoga katika ghadhabu yangu, na nikawakanyaga katika hasira yangu, na damu yao [a]nikainyunyizia kwenye mavazi yangu, nayo imeharibu vazi langu lote; kwani hii ilikuwa siku ya kulipa kisasi kilichokuwa moyoni mwangu.

52 Na sasa mwaka wa waliokombolewa wangu umefika; nao watataja ukarimu wa Bwana wao, na yote ambayo ameyaweka juu yao kulingana na wema wake, na kulingana na ukarimu wake, milele na milele.

40 *a* Isa. 64:1–2.
41 *a* Ayu. 41:31.
44 *a* 1 The. 4:15–18.
45 *a* Isa. 64:4; 1 Kor. 2:9.
b Omb. 3:25; 2 Ne. 6:7, 13.
46 *a* Isa. 63:1–2.
b MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
48 *a* Mwa. 49:11–12; Lk. 22:44; Ufu. 19:11–15; TJS Ufu. 19:15 (Kiambatisho); Mosia 3:7; M&M 19:18.
49 *a* Isa. 13:10; 24:23; M&M 45:42; 88:87.
50 *a* Isa. 63:2–3; M&M 76:107; 88:106.
51 *a* Law. 8:30.

53 Katika [a]mateso yao yote yeye aliteswa. Na malaika wa uwepo wake akawaokoa; na katika [b]upendo wake, na katika huruma yake, [c]akawakomboa, na aliwasaidia, na kuwabeba siku zote za kale;

54 Ndiyo, na [a]Henoko pia, na wale waliokuwa pamoja naye; manabii waliokuwa kabla yake; na [b]Nuhu pia, na wale waliokuwa kabla yake; na [c]Musa pia, na wale waliokuwa kabla yake;

55 Na tangu Musa hadi Eliya, na tangu Eliya hadi Yohana, waliokuwa pamoja na Kristo katika [a]ufufuko wake, na mitume watakatifu, pamoja na Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, watakuwa katika uwepo wa Mwanakondoo.

56 Na [a]makaburi ya [b]watakatifu [c]yatafunguliwa; nao wataamka na kusimama [d]mkono wa kuume wa Mwanakondoo, wakati atakaposimama juu ya [e]Mlima Sayuni, na juu ya mji mtakatifu, [f]Yerusalemu Mpya; nao wataimba [g]wimbo wa [h]Mwanakondoo, mchana na usiku milele na milele.

57 Na kwa sababu hii, ili wanadamu wapate kufanywa washiriki wa [a]utukufu ambao utafunuliwa, Bwana aliupeleka utimilifu wa [b]injili yake, agano lake lisilo na mwisho, wakisemezana kwa uwazi na urahisi—

58 Kuwaandaa walio dhaifu kwa ajili ya mambo yale yajayo duniani, na kwa ajili ya kazi ya Bwana katika siku ile walio [a]wapumbavu watakapo washinda wenye hekima, na [b]mnyonge atakapokuwa taifa hodari, na [c]wawili watawafanya makumi elfu wao kuwakimbia.

59 Na kwa walio wadhaifu wa dunia Bwana [a]atayapura mataifa kwa uwezo wa Roho wake.

60 Na ni kwa ajili hii amri hizi zilitolewa; ziliamriwa kuzuiliwa kuja ulimwenguni katika siku ile zilipotolewa, lakini sasa [a]ziende kwa [b]wote wenye mwili—

61 Na hii ni kulingana na nia na mapenzi ya Bwana, atawalaye juu ya wenye mwili wote.

62 Na kwake yeye [a]atubuye na [b]kujitakasa mwenyewe mbele za Bwana atapewa [c]uzima wa milele.

63 Na juu yao wale [a]wasiosikiliza sauti ya Bwana litatimizwa lile lililoandikwa na nabii

53 *a* Isa. 63:4–9.
b MWM Hisani.
c MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
54 *a* MWM Henoko.
b MWM Nuhu, Patriaki wa Biblia.
c MWM Musa.
55 *a* MWM Ufufuko.
56 *a* M&M 29:13.
b MWM Mtakatifu.
c M&M 45:45–46; 88:96–97.
d Mt. 25:33–34.
e Isa. 24:23; Ufu. 14:1; M&M 76:66; 84:2, 98–102.
f MWM Yerusalemu Mpya.
g Ufu. 15:3; M&M 84:98–102.
h MWM Mwanakondoo wa Mungu.
57 *a* MWM Madaraja ya Utukufu.
b MWM Injili.
58 *a* Mt. 11:25; 1 Kor. 1:27; Alma 32:23; 37:6–7.
b Isa. 60:22.
c Kum. 32:29–30.
59 *a* Mik. 4:11–13.
60 *a* M&M 104:58–59.
b M&M 1:2.
62 *a* MWM Toba, Tubu.
b M&M 88:74. MWM Utakaso.
c MWM Uzima wa Milele.
63 *a* MWM Sikiliza.

Musa, kwamba [b]watakatiliwa mbali kutoka miongoni mwa watu.

64 Na pia lile lililoandikwa na nabii [a]Malaki: Kwa maana, tazameni, siku ile [b]inakuja [c]itakayowaka kama tanuri, na wote wenye kiburi, ndiyo, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa majeshi, hata haitawaachia mzizi wala tawi.

65 Kwa hiyo, hili ndilo litakuwa jibu la Bwana kwao:

66 Katika siku ile nilipokuja kwa walio wangu, hakuna mtu miongoni mwenu [a]aliyenipokea, nanyi mlifukuzwa.

67 Nilipoita tena hapakuwa na yeyote kati yenu wa kunijibu; lakini [a]mkono wangu haukuwa mfupi kwa namna yoyote kwamba nisiweze kukomboa, wala [b]uwezo wangu wa kukomboa.

68 Tazama, kwa kemeo langu [a]ninaikausha bahari. Naifanya mito kuwa jangwa; samaki wao kunuka, na kufa kwa kiu.

69 Nazivika mbingu kwa weusi, nafanya nguo ya gunia kuwa mavazi yake.

70 Na [a]hili mtalipata kutoka mikononi mwangu—mtalala chini kwa huzuni.

71 Tazama, na lo, hakuna wa kuwakomboa ninyi; kwa kuwa hamkutii sauti yangu wakati nilipokuiteni kutoka mbinguni; hamkuwaamini watumishi wangu, na [a]walipoletwa kwenu hamkuwapokea.

72 Kwa hiyo, waliutia [a]muhuri ushuhuda na kuifunga sheria, nanyi mkaachwa gizani.

73 Hawa watakwenda katika giza la nje, ambako kuna [a]kilio, na kuomboleza, na kusaga meno.

74 Tazama Bwana Mungu wenu amenena hilo. Amina.

SEHEMU YA 134

Tamko la imani kuhusu serikali na sheria kwa ujumla, lililokubaliwa kwa kura nyingi kwenye mkutano mkuu wa Kanisa uliofanyika huko Kirtland, Ohio, 17 Agosti 1835. Watakatifu wengi walikusanyika pamoja kutafakari mapendekezo ya maudhui ya toleo la kwanza la Mafundisho na Maagano. Kwa wakati huo, tamko hilo lilipewa dibaji ifuatayo: "Ili imani yetu juu ya serikali za kidunia na sheria kwa ujumla zisipate kutafsiriwa vibaya au kueleweka vibaya, tumefikiri

63*b* Mdo. 3:22–23; 1 Ne. 22:20–21; 3 Ne. 20:23; 21:11; M&M 1:14; JS—H 1:40.
64*a* Mal. 4:1. MWM Malaki.
b JS—H 1:36–37.
c Isa. 66:15–16; 1 Ne. 22:15; 3 Ne. 25:1; M&M 29:9; 64:24. MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia.
66*a* Yn. 1:11.
67*a* 2 Ne. 28:32.
b Isa. 50:2; 2 Ne. 7:2.
68*a* Ku. 14:21; Yos. 3:14–17.
70*a* Isa. 50:11.
71*a* 2 Nya. 36:15–16; Yer. 44:4–5.
72*a* Isa. 8:16–20.
73*a* Mt. 8:11–12; Lk. 13:28; M&M 19:5. MWM Giza, Kiroho; Jehanamu.

ni vyema kutoa, mwishoni mwa kitabu hiki, maoni yetu kuhusiana na jambo hilo."

1–4, Serikali zinapaswa kulinda uhuru wa mawazo na wa kuabudu; 5–8, Watu wote wanapaswa kuziunga mkono serikali zao na kutoa heshima na staha kwa sheria zake; 9–10, Jumuiya za kidini hazipaswi kuwa na mamlaka ya kiserikali; 11–12, Wanadamu wanahalalishwa katika kujitetea wenyewe na mali zao.

Sisi tunaamini kwamba [a]serikali zimewekwa na Mungu kwa manufaa ya mwanadamu; na kwamba [b]anawawajibisha wanadamu kwa matendo yao kuhusiana nazo, katika kutunga sheria na kuzitekeleza, kwa faida na usalama wa jamii.

2 Sisi tunaamini kwamba hakuna serikali inayoweza kudumu katika amani, isipokuwa sheria hizo zimetungwa na kutunzwa bila kuvunjwa ambazo zitamhakikishia kila mtu [a]uhuru wa [b]mawazo, haki na udhibiti wa mali yake, na [c]ulinzi wa maisha yake.

3 Sisi tunaamini kwamba serikali zote zinahitaji kuwa na [a]maofisa wake, na mahakimu ili kuzitekeleza sheria hizo; na ni aina ya maofisa ambao wataitekeleza sheria katika usawa na haki yapaswa watafutwe na kuungwa mkono kwa sauti ya watu kama ni jamhuri, au kwa ridhaa ya wenye nchi.

4 Sisi tunaamini kwamba dini imewekwa na Mungu; na kwamba wanadamu wanawajibika kwake, na ni kwake pekee yake, kwa kuitekeleza, isipokuwa kama dhana za dini yao zinachochea juu ya kuvunja haki na uhuru wa wengine; lakini hatuamini kwamba sheria za kibinadamu zinayo haki ya kuingilia katika kutoa taratibu za jinsi ya [a]kuabudu ili kufunga uhuru wa mawazo ya wanadamu, wala kuweka taratibu kwa ajili ya watu kuabudu hadharani au sirini; kwamba mahakimu wa serikali wanapaswa kuzuia uvunjaji wa sheria, lakini kamwe hawapaswi kuthibiti uhuru wa mawazo; wanapaswa kuwaadhibu wahalifu, lakini kamwe wasikandamize uhuru wa roho.

5 Sisi tunaamini kwamba wanadamu wote wanalazimika kukubali na kuunga mkono serikali zilizopo ambamo ndani yake wanaishi, wakiwa wanalindwa pamoja na haki zao za msingi haki zisizoondoshwa kwa sheria za serikali hizo, na kwamba uchochezi na [a]uasi si sahihi kwa kila raia ambaye kwa njia hiyo hulindwa, na anapaswa kuadhibiwa sawia;

134 1*a* M&M 98:4–7; M ya I 1:12.
b MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
2*a* MWM Haki ya uamuzi.
b MWM Dhamiri.
c M&M 42:18–19.
3*a* M&M 98:8–10.
4*a* Alma 21:21–22; M ya I 1:11. MWM Kuabudu.
5*a* M ya I 1:12. MWM Uasi.

na kwamba serikali zote zinayo haki ya kuzitumia sheria hizo kama ionavyo katika maamuzi yake yenyewe kuwa ni vyema ili kulinda maslahi ya umma; na wakati huo huo, katika hali yoyote, ikishika kitakatifu uhuru wa mawazo.

6 Sisi tunaamini kwamba kila mwanadamu anapaswa kuheshimika katika nafasi yake, kama vile watawala na mahakimu, wakiwa wamewekwa kwa ajili ya ulinzi wa wasio na hatia na kuwaadhibu walio na hatia; na kwamba kwa [a]sheria wanadamu wote wanapaswa kuwapa heshima na staha, kwa vile pasipo wao amani na mapatano vingetawaliwa na vurugu na vitisho; sheria za kibinadamu ziliwekwa hususani kwa madhumuni ya kutawala maslahi yetu kama mtu binafsi na kama taifa, kati ya mtu na mtu; na sheria takatifu zilizotolewa kutoka mbinguni, zikielezea juu ya masuala ya kiroho, kwa ajili ya imani na kuabudu, yote kujibiwa na mwanadamu kwa Muumba wake.

7 Sisi tunaamini kwamba watawala, majimbo, na serikali wanayo haki, na wanalazimika kutekeleza sheria kwa ajili ya kuwalinda wananchi wote katika uhuru wa kutekeleza imani yao ya kidini; lakini hatuamini kwamba wanayo haki kisheria ya kuwanyima wananchi haki yao hii, au kuwakataza wao katika imani yao, ilimradi staha na heshima zinaonyeshwa kwa sheria na imani hiyo ya kidini haitetei uchochezi wala kula njama dhidi ya serikali.

8 Sisi tunaamini kwamba kutendwa kwa uhalifu kunapaswa [a]kuadhibiwa kulingana na aina ya kosa; kwamba mauaji, uhaini, wizi wa kutumia nguvu, wizi, na uvunjaji wa amani kwa ujumla, katika njia yoyote ile, kunapaswa kuadhibiwa kulingana na uzito wa uhalifu wao na mwelekeo wao kwenye uovu miongoni mwa wanadamu, kwa sheria za serikali ile ambamo kosa lile limetendeka; na kwa ajili ya amani na utulivu wa umma watu wote wanapaswa kujitoa na kutumia uwezo wao katika kuwaleta wahalifu mbele ya sheria zilizo nzuri ili kuadhibiwa.

9 Sisi hatuamini kuwa ni haki kuchanganya mvuto wa kidini pamoja na serikali ya kiraia, ambapo jumuiya moja ya kidini itakimiwa na nyingine itakataliwa katika haki zake za kiroho, na haki binafsi za waumini wake, kama wananchi, watanyimwa.

10 Tunaaamini kwamba jumuiya zote za kidini zinayo haki ya kuwashughulikia waumini wake kwa tabia zisizokubalika, kulingana na kanuni na taratibu hizo; ili mradi kushughulika huko ni kwa ajili ya ushirikiano na nia njema; lakini sisi hatuamini kwamba jumuiya yoyote ya kidini inayo mamlaka ya kuwahukumu watu juu ya haki ya mali zao, au uhai wao, kwa kuchukua mali zao za ulimwengu huu, au kuwahatarishia uhai

6*a* M&M 58:21; 88:34. | 8*a* Alma 30:7–11; M&M 42:84–87.

au kiungo, au kutoa adhabu yoyote ya kimwili juu yao. Wanaweza tu [a]kuwatenga kutoka kwenye jumuiya zao, na kuondoa ushirikiano wao.

11 Tunaamini kwamba wanadamu wanapaswa kukata rufaa kwa sheria za nchi kwa ajili ya kufidiwa mabaya na maovu yote, ikiwa mabaya yametendeka kwa mtu au haki ya kumiliki mali au sifa njema imevunjwa, katika mahali ambapo sheria hizi zipo na zitamlinda katika mambo haya; lakini tunaamini kwamba wanadamu wote wanahesabiwa haki katika kujilinda wao wenyewe, marafiki zao, mali, na serikali yao, kutokana na uvamizi usio wa haki na maingiliano ya watu wote nyakati za dharura, wakati ambapo rufaa ya haraka haiwezi kufanyika kwa vyombo vya sheria, na msaada kupatikana.

12 Sisi tunaamini kuwa ni haki [a]kuhubiri injili kwa mataifa yote ya duniani, na kuwaonya wenye haki kujiokoa wenyewe kutokana na uharibifu wa ulimwengu; lakini hatuamini kuwa ni haki kuwaingilia watumwa, wala kuwahubiria injili, wala kuwabatiza kinyume na matakwa na mapenzi ya mabwana wao, wala kuingilia mambo yao au kuwashawishi hata katika kiwango kidogo kuwasababisha wasiridhike na hali yao katika maisha haya, na hivyo kuhatarisha maisha ya watu; kuingilia huko tunaamini kuwa siyo kisheria na siyo haki, na ni hatari kwa amani ya kila serikali inayoruhusu wanadamu kushikiliwa katika utumwa.

SEHEMU YA 135

Tangazo la kifo cha kishahidi cha Joseph Smith Nabii na kaka yake, Hyrum Smith Patriaki, huko Carthage, Illinois, 27 Juni 1844. Hati hii ilijumuishwa mwishoni mwa toleo la 1844 la Mafundisho na Maagano, ambalo ilikuwa linakaribia kuwa tayari kwa uchapishaji wakati Joseph na Hyrum Smith walipouawa.

1–2, Joseph na Hyrum wauawa kifo cha kishahidi katika gereza la Carthage; 3, Nafasi ya juu kabisa ya Nabii yatangazwa kwa shangwe; 4–7, Damu yao isiyo na hatia yashuhudia ukweli na utakatifu wa kazi hii.

Ili kutia muhuri ushuhuda wa kitabu hiki na Kitabu cha Mormoni, tunatangaza [a]mauaji ya kishahidi ya [b]Joseph Smith Nabii, na Hyrum Smith Patriaki. Walipigwa risasi [c]gerezani Carthage, mnamo 27 Juni 1844, kiasi cha saa kumi na moja jioni, na kundi la wahuni wenye

10*a* MWM Kutengwa na Kanisa.
12*a* MWM Hubiri; Kazi ya kimisionari.

135 1*a* M&M 5:22; 6:30. MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.
b MWM Smith, Joseph, Mdogo.
c MWM Gereza la Carthage (Marekani).

silaha—waliojipaka rangi nyeusi—watu wapatao 150 hadi 200. [d]Hyrum alipigwa kwanza na kuanguka kimya kimya, akigutia: *Nimekufa!* Joseph aliruka kutoka dirishani, na alipigwa na kufa alipokuwa akijaribu kuruka, akigutia: *Ee Bwana Mungu wangu!* Wote walipigwa risasi baada ya kuwa wamekufa, katika namna ya kinyama, na wote walipokea risasi nne.

2 [a]John Taylor na Willard Richards, wawili kati ya Kumi na Wawili, walikuwa watu pekee katika chumba kile kwa wakati ule; wa kwanza alijeruhiwa kikatili kwa risasi nne, lakini kwa sasa amepona, wa pili, kwa majaliwa ya Mungu, aliepuka, pasipo hata tundu katika joho lake.

3 Joseph Smith, [a]Nabii na [b]Mwonaji wa Bwana, amefanya mengi, isipokuwa Yesu pekee yake, kwa ajili ya wokovu wa wanadamu katika ulimwengu huu, kuliko mwanadamu mwingine yeyote aliyeishi ndani yake. Katika kipindi kifupi cha miaka ishirini, amekileta Kitabu cha Mormoni, ambacho amekitafsiri kwa kipawa na uwezo wa Mungu, na amekuwa njia ya kukichapisha katika mabara mawili; amepeleka [c]utimilifu wa injili isiyo na mwisho, ambayo imo ndani yake, kwenye robo nne za dunia; ameleta mafunuo na amri ambazo zinaunda kitabu hiki cha Mafundisho na Maagano, na maandishi mengine mengi ya busara na maelekezo kwa manufaa ya wanadamu; kimewakusanya maelfu mengi ya Watakatifu wa Siku za Mwisho, ameanzisha [d]mji mkubwa, na ameacha sifa na jina ambalo haliwezi kuuawa. Aliishi vyema, na amekufa vyema machoni pa Mungu na watu wake; na kama wengi wa wapakwa mafuta wa Bwana katika siku za kale, ametia muhuri huduma yake na kazi zake kwa [e]damu yake yeye mwenyewe; na vivyo hivyo kaka yake Hyrum. Katika maisha hawakugawanyika, na katika mauti hawakutenganishwa!

4 Wakati Joseph alipokwenda Carthage kujitoa mwenyewe kama sheria ilivyodhaniwa kudai, siku mbili au tatu kabla ya mauaji yake, alisema: "Ninakwenda kama [a]kondoo kwa mchinjaji; lakini nimetulia kama asubuhi ya kiangazi; ninayo dhamira isiyo na hatia mbele za Mungu, na mbele za watu wote. MIMI NITAKUFA BILA HATIA, NA BADO ITASEMWA JUU YANGU—ALIUAWA KIKATILI."—Asubuhi hiyo hiyo, baada ya Hyrum kuwa tayari kwenda—tuseme kwa mwuaji? ndiyo, kwani ndivyo ilivyokuwa—alisoma aya ifuatayo, karibuni na mwisho wa mlango wa kumi na mbili wa Etheri, katika Kitabu cha Mormoni, na akaukunja ukurasa ule:

5 *Na ikawa kwamba niliomba kwa Bwana kwamba awape neema*

1 *d* MWM Smith, Hyrum.
2 *a* MWM Taylor, John.
3 *a* MWM Nabii.
b MWM Mwonaji.
c M&M 35:17; 42:12. MWM Urejesho wa Injili.
d MWM Nauvoo, Illinois (Marekani).
e Ebr. 9:16–17; M&M 136:39.
4 *a* Isa. 53:7.

Wayunani, ili wapate kuwa na hisani. Na ikawa kwamba Bwana akasema nami kuwa: Kama hawana hisani haikuhusu wewe, umekuwa mwaminifu; kwa hiyo nguo zako zitafanywa [a]*safi. Na kwa sababu umeuona udhaifu wako, utafanywa kuwa mwenye nguvu, hata kwa kukaa katika mahali ambapo nimepatayarisha katika nyumba ya Baba yangu. Na sasa, mimi . . . ninaaga kwa Wayunani; ndiyo, na pia kwa ndugu zangu ambao ninawapenda, mpaka tutakapokutana mbele ya* [b]*kiti cha hukumu cha Kristo, ambapo watu wote watajua kwamba mavazi yangu hayajawekwa mawaa na damu yenu.* [c]Mashahidi hawa sasa wamekufa, na ushuhuda wao bado una nguvu.

6 Hyrum Smith alikuwa na umri wa miaka arobaini na minne hapo Februari, 1844, na Joseph Smith alikuwa na miaka thelathini na minane hapo Desemba, 1843; na tangu sasa na kuendelea majina yao yataorodheshwa miongoni mwa waliouawa kama mashahidi wa dini; na msomaji katika kila taifa atakumbushwa kwamba Kitabu cha Mormoni, na kitabu hiki cha Mafundisho na Maagano ya kanisa, vimegharimu damu iliyo bora ya karne ya kumi na tisa kuvileta kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu ulio haribiwa; na kwamba kama moto unaweza kuushambulia [a]mti mbichi kwa ajili ya utukufu wa Mungu, ni rahisi namna gani kuunguza miti mikavu kutakasa shamba la mizabibu la uharibifu. Waliishi kwa ajili ya utukufu; walikufa kwa ajili ya utukufu; na utukufu ndiyo thawabu yao ya milele. Kutoka umri mmoja hadi mwingine majina yao yatakwenda chini kwa wazao kama vito kwa ajili ya waliotakaswa.

7 Walikuwa hawana hatia yoyote ya uhalifu, kama mara kwa mara ilivyothibitika kabla, na walikuwa wamezuiliwa tu kifungoni kwa njama za wasaliti na watu waovu; na *damu yao isiyo na hatia* juu ya sakafu ya gereza la Carthage ni muhuri mkubwa uliobandikwa kwenye "Umormoni" ambao hauwezi kukataliwa na mahakama yoyote juu ya dunia, na *damu yao isiyo na hatia* juu ya nembo ya Jimbo la Illinois, pamoja na imani iliyovunjika kwa jimbo kama ilivyonenwa na gavana, ni ushahidi wa ukweli wa injili isiyo na mwisho ambao ulimwengu mzima hauwezi kukamisha; na *damu yao isiyo na hatia* juu ya bendera ya uhuru, na juu ya katiba kuu ya Muungano wa Mataifa ya Marekani ni balozi wa dini ya Yesu Kristo, ambayo itagusa mioyo ya watu waaminifu miongoni mwa mataifa yote; na *damu yao isiyo na hatia,* pamoja na damu isiyo na hatia ya waliouawa kama mashahidi wa dini wote chini ya [a]madhabahu ile ambayo Yohana aliiona, italia kwa Bwana wa Majeshi hadi atakapolipiza kisasi cha damu hiyo juu ya dunia. Amina.

5*a* M&M 88:74–75.
b Eth. 12:36–38.
c Ebr. 9:16–17.
6*a* Lk. 23:31.
7*a* Ufu. 6:9.

SEHEMU YA 136

Neno na mapenzi ya Bwana, yaliyotolewa kupitia Rais Brigham Young huko katika Makazi ya Winter Quarters, ya kambi ya Israeli, Nchi ya Omaha, juu ya kingo za magharibi za Mto Missouri, karibu na Council Bluffs, Iowa.

1–16, Namna kambi ya Israeli inavyopaswa kuundwa kwa ajili ya safari ya kuelekea magharibi yaelezwa; 17–27, Watakatifu wanaamriwa kuishi kulingana na kanuni nyingi za injili; 28–33, Watakatifu yawapasa kuimba, kucheza, kuomba, na kujifunza hekima; 34–42, Manabii wanauawa ili wapate kuheshimiwa na waovu wahukumiwe.

Neno na Mapenzi ya Bwana juu ya Kambi ya Israeli katika safari zao za kwenda Magharibi:

2 Acheni watu wote wa [a]Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, na wale wanaosafiri pamoja nao, wawekwe katika makundi, kwa agano na ahadi ya kuzishika amri zote na sheria za Bwana Mungu wetu.

3 Acheni makundi yaundwe kwa maakida wa [a]mamia, maakida wa hamsini, na maakida wa makumi, pamoja na rais na washauri wake wawili juu ya vichwa vyao, chini ya maelekezo ya [b]Mitume Kumi na Wawili.

4 Na hili litakuwa [a]agano letu—kwamba [b]tutatembea katika [c]maagizo yote ya Bwana.

5 Acheni kila kundi lijitegemee lenyewe kwa mafahari wote, magari ya kukokota mizigo, vyakula, mavazi, na mahitaji mengine muhimu kwa safari, yale wawezayo kupata.

6 Wakati makundi hayo yawapo tayari na waondoke kwa nguvu zao, kuwaandalia wale watakaosalia.

7 Acheni kila kundi, pamoja na maakida wao na marais, waamue ni wangapi wanaweza kwenda wakati wa majira ya kuchipua yajayo; halafu chagueni idadi ya kutosha ya watu wenye nguvu na wataalamu, kuchukua mafahari wa kulima, mbegu, na zana za kulimia, kwenda kama watangulizi wa kutayarisha kwa ajili ya kupanda mazao ya majira ya kuchipua.

8 Acheni kila kikundi kibebe uzito sawa, kulingana na mgawanyo wa mali zao, katika kuwachukua [a]maskini, [b]wajane, [c]wasio na baba, na familia za wale ambao wameenda vitani, ili vilio vya wajane na wasio na baba visije masikioni mwa Bwana dhidi ya watu hawa.

9 Acheni kila kikundi kitengeneze nyumba, na mashamba kwa ajili ya kuotesha nafaka, kwa ajili ya wale ambao watabakia nyuma majira haya; na

136 2*a* MWM Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.
3*a* Ku. 18:21–26.
b MWM Mtume.
4*a* MWM Agano.
b MWM Tembea, Tembea na Mungu.
c MWM Ibada.
8*a* MWM Maskini.
b MWM Mjane.
c Yak. (Bib.) 1:27; 3 Ne. 24:5.

haya ndiyo mapenzi ya Bwana juu ya watu wake.

10 Acheni kila mtu atumie uwezo wake wote na mali yake kuwapeleka watu hawa mahali ambapo Bwana atapachagua kuwa [a]kigingi cha Sayuni.

11 Na kama mtafanya hili kwa moyo safi, katika uaminifu wote, [a]mtabarikiwa; mtabarikiwa katika mifugo yenu, na katika wanyama wenu, na katika mashamba yenu, na katika nyumba zenu, na katika familia zenu.

12 Acheni watumishi wangu Ezra T. Benson na Erastus Snow waunde kikundi.

13 Acheni watumishi wangu Orson Pratt na Wilford Woodruff waunde kikundi.

14 Pia, acheni watumishi wangu Amasa Lyman na George A. Smith waunde kikundi.

15 Na wateueni marais, na maakida wa mamia, na wa hamsini, na wa makumi.

16 Acheni watumishi wangu ambao nimewatuma na waende na kufundisha haya, mapenzi yangu, kwa watakatifu, ili wapate kuwa tayari kwenda kwenye nchi ya amani.

17 Enendeni zenu na mkafanye kama nilivyowaambia, na msiwaogope maadui zenu; kwani hawatakuwa na uwezo wa kuisimamisha kazi yangu.

18 Sayuni [a]itakombolewa katika wakati wangu mwenyewe.

19 Na kama mtu yeyote atatafuta kujijenga mwenyewe, na hatafuti [a]ushauri wangu, hatakuwa na uwezo, na upumbavu wake utadhihirishwa.

20 Tafuteni; na [a]timizeni ahadi zenu wenyewe kwa wenyewe; na [b]usitamani kile kilicho cha ndugu yako.

21 [a]Msifanye uovu kwa kulitamka ovyo jina la Bwana, kwani Mimi ndiye Bwana Mungu wenu, hata [b]Mungu wa baba zenu, Mungu wa Ibrahimu na wa Isaka na wa Yakobo.

22 [a]Mimi ndiye niliye waongoza wana wa Israeli kutoka nchi ya Misri; na mkono wangu umenyooshwa katika siku hizi za mwisho, [b]kuwaokoa watu wangu wa Israeli.

23 Acheni [a]kugombana ninyi kwa ninyi; acheni [b]kuneneana vibaya.

24 Acheni [a]ulevi; na acheni maneno yenu yawe ya [b]kujengana.

25 Kama ukiazima cha jirani yako, wewe utakirejesha kile [a]ulichoazima; na kama huwezi kulipa basi nenda moja kwa moja na kumwambia jirani yako, asije akakuhumu.

26 Kama utakiona kitu cha jirani yako [a]alichokipoteza, wewe

10 *a* MWM Kigingi.
11 *a* Kum. 28:1–14. MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
18 *a* M&M 100:13.
19 *a* MWM Ushauri.
20 *a* MWM Mwaminifu, Uaminifu.
b MWM Tamani.
21 *a* MWM Lugha chafu.
b Ku. 3:6; 1 Ne. 19:10.
22 *a* Ku. 13:18; Yer. 2:5–7; 1 Ne. 5:15; Alma 36:28. MWM Yehova.
b Yer. 30:10; Eze. 20:33–34; M&M 38:33.
23 *a* 3 Ne. 11:29–30. MWM Ushindani.
b M&M 20:54. MWM Kusema uovu.
24 *a* MWM Neno la Hekima.
b M&M 108:7.
25 *a* Zab. 37:21; Mos. 4:28. MWM Deni; Mwaminifu, Uaminifu.
26 *a* Law. 6:4; Kum. 22:3.

fanya bidii ya kumtafuta mwenyewe na kumrudishia tena.

27 Utafanya [a]bidii katika kutunza kile ulichonacho, ili upate kuwa [b]mtumishi mwenye busara; kwani hiyo ni zawadi kutoka kwa Bwana Mungu wako, nawe ni mtumishi wake.

28 Kama mmefurahi, msifuni Bwana kwa [a]kuimba, kwa kinubi, kwa kucheza, na kwa [b]sala ya kusifu na [c]kutoa shukrani.

29 Kama mna [a]huzuni, mlinganeni Bwana Mungu wenu, kwa maombi ya dhati, ili mioyo yenu ipate [b]kufurahi.

30 Msiwaogope maadui zenu, kwa kuwa wapo mikononi mwangu na nitawafanya nipendavyo.

31 Watu wangu ni lazima [a]wajaribiwe katika mambo yote, ili wapate kutayarishwa kupokea [b]utukufu ule nilionao kwa ajili yao, hata utukufu wa Sayuni; naye yule ambaye hatastahimili [c]kurudiwa haustahili ufalme wangu.

32 Acheni yule ambaye hana maarifa ajifunze [a]hekima kwa [b]kujinyenyekeza mwenyewe na kumlingana Bwana Mungu wake, ili macho yake yapate kufunguliwa ili apate kuona, na masikio yake kufunguliwa ili apate kusikia;

33 Kwani [a]Roho yangu imetolewa ulimwenguni kuwaangaza wanyenyekevu na walioponde-ka, na kwa kuwahukumu wasio mcha Mungu.

34 Ndugu zenu wamewakataa ninyi na ushuhuda wenu, hata taifa lile [a]lililowafukuzeni;

35 Na sasa yaja siku ya msiba wao, hata siku za huzuni, kama mwanamke ambaye amechukuliwa katika utungu; na huzuni yao itakuwa kuu isipokuwa watubu haraka, ndiyo, haraka sana.

36 Kwani waliwaua manabii, na wale waliotumwa kwao; nao wamemwaga damu isiyo na hatia, ambayo hulia kutoka ardhini dhidi yao.

37 Kwa hiyo, msishangazwe na mambo haya, kwani ninyi bado hamjawa [a]safi; bado hamwezi kustahimili utukufu wangu; lakini mnaweza kuuona kama mtakuwa waaminifu katika kuyashika maneno yangu ambayo [b]nimeyatoa kwenu, kutoka siku za Adamu hadi Ibrahimu, kutoka Ibrahimu hadi Musa, kutoka Musa hadi Yesu na mitume wake, na kutoka Yesu na mitume wake hadi kwa Joseph Smith, ambaye nilimwita kupitia [c]malaika zangu, watumishi wangu wahudumu,

27 *a* MWM Bidii.
b MWM Msimamizi, Usimamizi.
28 *a* MWM Imba.
b MWM Sala.
c 2 Nya. 5:13; M&M 59:15–16. MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
29 *a* 2 Sam. 22:7.
b MWM Shangwe.
31 *a* M&M 101:4. MWM Shida.
b Rum. 8:18; M&M 58:3–4. MWM Utukufu.
c MWM Rudi, Kurudiwa.
32 *a* MWM Hekima.
b MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
33 *a* MWM Roho Mtakatifu.
34 *a* MWM Mateso, Tesa.
37 *a* MWM Safi na Isiyo safi.
b Hel. 8:18.
c Ufu. 14:6; M&M 110:11–16; 128:19–21; JS—H 1:30–47.

na kwa sauti yangu mimi mwenyewe kutoka mbinguni, kuianzisha kazi yangu;

38 Msingi ambao aliuweka, naye alikuwa mwaminifu; nami nimemchukua kwangu.

39 Wengi wamestaajabu kwa sababu ya kifo chake; lakini ilikuwa muhimu kwamba lazima [a]atie muhuri [b]ushuhuda wake kwa [c]damu yake, ili apate kuheshimiwa na waovu wapate kuhukumiwa.

40 Je, sijawakomboa ninyi kutokana na [a]maadui zenu, katika hilo tu nimeacha ushahidi wa jina langu?

41 Sasa, kwa hiyo, sikilizeni, Enyi watu wa [a]kanisa langu; nanyi wazee sikilizeni kwa pamoja; mmeupokea [b]ufalme wangu.

42 Kuweni na bidii katika kuzishika amri zangu zote, isije hukumu ikaja juu yenu, na imani yenu ikawatindikia, na maadui zenu wakapata ushindi juu yenu. Hivyo hakuna la zaidi kwa sasa. Amina na Amina.

SEHEMU YA 137

Ono lililotolewa kwa Joseph Smith Nabii, ndani ya hekalu huko Kirtland, Ohio, 21 Januari 1836. Tukio lilikuwa la huduma za ibada katika maandalizi kwa ajili ya uwekaji wakfu wa hekalu.

1–6, Nabii anamwona kaka yake Alvin katika ufalme wa selestia; 7–9, Mafundisho ya wokovu kwa ajili ya wafu yanafunuliwa; 10, Watoto wote wameokolewa katika ufalme wa selestia.

[a]Mbingu zikatufunukia, nami nikauona ufalme wa [b]selestia wa Mungu, na utukufu wake, kama nilikuwa katika [c]mwili au nilikuwa nje ya mwili sijui.

2 Niliona uzuri uliopita kiasi wa [a]lango ambalo warithi wa ufalme ule wataingia, ambalo lilikuwa mfano wa [b]miale ya moto yenye kuzunguka;

3 Pia kiti cha enzi cha Mungu chenye [a]kuwaka, juu yake [b]Baba na [c]Mwana wamekaa.

4 Niliona mitaa mizuri ya ufalme ule, ambayo ilionekana kuwa kama umesakafiwa kwa [a]dhahabu.

5 Nilimwona Baba [a]Adamu na [b]Ibrahimu; na [c]baba na

39 *a* Mos. 17:20; M&M 135:3.
b MWM Ushuhuda.
c MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.
40 *a* Ku. 23:22; M&M 8:4; 105:15.
41 *a* MWM Kanisa la Yesu Kristo.
b Dan. 7:27.
137 1 *a* Mdo. 7:55–56; 1 Ne. 1:8; Hel. 5:45–49; JS—H 1:43.
b MWM Utukufu wa Selestia.
c 2 Kor. 12:2–4; 1 Ne. 11:1; Musa 1:11.
2 *a* 2 Ne. 9:41; 31:17.
b Ku. 24:17; Isa. 33:14–15; Hel. 5:23; M&M 130:7.
3 *a* Isa. 6:1; Eze. 1:26–28.
b MWM Mungu, Uungu—Mungu Baba.
c MWM Mungu, Uungu—Mungu Mwana.
4 *a* Ufu. 21:21; M&M 110:2.
5 *a* MWM Adamu.
b M&M 132:29. MWM Ibrahimu.
c M&M 124:19. MWM Smith, Joseph, Mkubwa.

[d]mama yangu; kaka yangu [e]Alvin, ambaye alifariki muda mrefu uliopita.

6 Na nikastaajabu jinsi gani ameweza kupata [a]urithi katika ufalme ule, nilitazama kwamba ameondoka katika maisha haya kabla Bwana hajaweka mkono wake kuwakusanya Israeli mara ya [b]pili, na wala [c]hakubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi.

7 Na hivyo [a]sauti ya Bwana ikanijia ikisema: Wote waliokufa [b]bila kuifahamu injili hii, ambao wangeliipokea kama wangeruhusiwa kuishi, watakuwa [c]warithi wa ufalme wa [d]selestia wa Mungu;

8 Pia wale wote watakaokufa sasa na kuendelea bila kuifahamu, ambao [a]wangeliipokea kwa moyo wao wote, watakuwa warithi wa ufalme huo;

9 Kwani Mimi, Bwana, [a]nitawahukumu watu wote kulingana na [b]matendo yao, kulingana na [c]tamaa za mioyo yao.

10 Nami pia niliona kwamba watoto wote ambao hufa kabla ya kufikia [a]miaka ya uwajibikaji [b]wanaokolewa katika ufalme wa selestia wa mbinguni.

SEHEMU YA 138

Ono, lililotolewa kwa Rais Joseph F. Smith katika Jiji la Salt Lake, Utah, mnamo tarehe 3 Oktoba 1918. Katika hotuba yake ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa 89 wa Nusu Mwaka wa Kanisa, 4 Oktoba 1918, Rais Smith alitangaza kwamba alikuwa amepokea mawasiliano matakatifu kadhaa katika kipindi cha mwezi uliopita. Moja ya haya, ni juu ya Mwokozi kutembea ulimwengu wa wafu wakati mwili wake ulipokuwa kaburini, Rais Smith alikuwa amelipokea siku ya jana yake. Liliandikwa mara moja baada ya kufungwa kwa mkutano. Mnamo tarehe 31 Oktoba 1918, liliwakilishwa kwa washauri katika Urais wa Kwanza, Baraza la Mitume Kumi na Wawili, na Patriaki, nalo walilikubali kwa kauli moja.

1–10, Rais Joseph F. Smith atafakari juu ya maandiko ya Petro na matembezi ya Bwana wetu katika ulimwengu wa kiroho; 11–24,

5 *d* MWM Smith, Lucy Mack.
e JS—H 1:4.
6 *a* MWM Wokovu kwa ajili ya Wafu.
b Isa. 11:11; 1 Ne. 22:10–12; Yak. (KM) 6:2. MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
c Yn. 3:3–5; 2 Ne. 9:23; Eth. 4:18–19; M&M 76:50–52; 84:74. MWM Batiza, Ubatizo.
7 *a* Hel. 5:30. MWM Ufunuo.
b TJS 1 Pet. 4:6 (Kiambatisho); 2 Ne. 9:25–26; Mosia 15:24.
c M&M 76:50–70.
d MWM Utukufu wa Selestia.
8 *a* Alma 18:32; M&M 6:16.
9 *a* Ufu. 20:12–13. MWM Hukumu ya mwisho.
b MWM Matendo.
c M&M 64:34. MWM Moyo.
10 *a* MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
b MWM Wokovu—Wokovu wa watoto.

Rais Smith awaona wafu wenye haki wamekusanyika peponi na huduma ya Kristo miongoni mwao; 25–37, Anaona jinsi kuhubiriwa kwa injili kulivyoanzishwa miongoni mwa roho hizo; 38–52, Anamwona Adamu, Hawa, na wengi wa manabii watakatifu katika ulimwengu wa roho ambao waliitazama hali kabla ya ufufuko wao kama kifungoni; 53–60, Wafu wenye haki wa leo huendelea na kazi zao katika ulimwengu wa kiroho.

Siku ya tatu ya Oktoba, katika mwaka wa elfu moja mia tisa na kumi na nane, nilikaa chumbani mwangu [a]nikitafakari juu ya maandiko;

2 Na nikitazama juu ya dhabihu kuu ya [a]upatanisho ambao ulifanywa na Mwana wa Mungu, kwa ajili ya [b]ukombozi wa ulimwengu;

3 Na [a]upendo mkuu na wa ajabu ulioonyeshwa na Baba na Mwana katika kuja kwa [b]Mkombozi ulimwenguni;

4 Ili kwa njia ya [a]upatanisho wake, na kwa [b]utii kwa kanuni za injili, mwanadamu apate kuokolewa.

5 Wakati nikiwa ninajishughulisha hivyo, akili yangu ilirejea kwenye maandiko ya mtume Petro, kwa [a]watakatifu wa mwanzo waliosambaa sehemu za [b]Ponto, Galatia, Kapadokia, na sehemu nyinginezo za Asia, ambako injili ilikuwa imehubiriwa baada ya kusulubiwa kwa Bwana.

6 Nilifungua Biblia na kusoma mlango wa tatu na wa nne ya waraka wa Petro, na nilivyokuwa nikisoma nilivutiwa sana, kuliko ilivyokuwa kabla yake, na sehemu hizi zifuatazo:

7 "Kwa maana Kristo naye ameteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio na haki, ili atulete kwa Mungu, mwili wake akauawa, bali akahuishwa na Roho:

8 "Ambayo kwa hiyo pia aliwaendea roho waliokaa [a]kifungoni akawahubiria;

9 "Wakati mmoja walikuwa hawatii wakati uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja katika siku za Nuhu, wakati safina ilipokuwa ikitengenezwa, ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane waliokoka kwa maji." (1 Petro 3:18–20.)

10 "Maana kwa ajili hii hata hao waliokufa pia walihubiriwa injili, ili wapate kuhukumiwa kulingana na wanadamu katika mwili, bali waishi kulingana na Mungu katika roho." (1 Petro 4:6.)

11 Nilipokuwa nikitafakari juu ya mambo haya ambayo [a]yameandikwa, [b]macho yangu

138 1*a* MWM Tafakari.
2*a* Mt. 20:28.
MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
b MWM Mpango wa Ukombozi.
3*a* Yn. 3:16.
MWM Upendo.
b MWM Mkombozi.
4*a* M ya I 1:3.
b Mt. 7:21.
MWM Mtiifu, Tii, Utii.
5*a* MY watakatifu wa zamani.
b 1 Pet. 1:1.
8*a* Isa. 61:1; Lk. 4:18; M&M 76:73–74; 88:99.
11*a* MWM Maandiko—Thamani ya maandiko.
b Efe. 1:18; M&M 76:10, 12, 19.

ya ufahamu yakafunguliwa, na Roho wa Bwana [c]akatulia juu yangu, na nikaona jeshi la [d]waliokufa wote, wadogo na wakubwa.

12 Nao walikusanywa pamoja katika mahali pamoja kundi kubwa lisilohesabika la roho za wenye [a]haki, ambao wamekuwa [b]waaminifu katika ushuhuda wa Yesu wakati walipoishi katika mwili wenye kufa;

13 Na ambao walikuwa wametoa [a]dhabihu katika mfano wa dhabihu iliyo kuu ya Mwana wa Mungu, na [b]wakapata taabu katika jina la Mkombozi wao.

14 Hawa wote wameondoka katika mwili wenye kufa, wakiwa imara katika [a]tumaini la [b]ufufuko mtukufu, kupitia [c]neema ya Mungu [d]Baba na [e]Mwanawe wa Pekee, Yesu Kristo.

15 Niliona kwamba walijawa na [a]shangwe na furaha, nao walikuwa wanafurahi kwa pamoja kwa sababu siku ya ukombozi wao ilikuwa imefika.

16 Walikusanyika kusubiri kuja kwa Mwana wa Mungu katika [a]ulimwengu wa roho, kuwatangazia ukombozi wao kutokana na [b]kamba za mauti.

17 Mavumbi yao yaliyolala [a]yangerejeshwa kwenye umbile kamili, [b]mfupa kwa mfupa mwenzie na mafuta na nyama juu yake, [c]roho na mwili kuunganika kamwe isitengane tena, ili wapate kupokea utimilifu wa [d]shangwe.

18 Wakati umati huu mkubwa ulipokuwa ukisubiri na kuongea, wakifurahia katika saa ya ukombozi wao kutokana na minyororo ya mauti, Mwana wa Mungu akatokea, akitangaza [a]uhuru kwa wafungwa waliokuwa waaminifu;

19 Na hapo [a]akawahubiria wao [b]injili isiyo na mwisho, mafundisho ya ufufuko na ukombozi wa mwanadamu kutokana na [c]anguko, na kutokana na dhambi za binafsi kwa masharti ya [d]toba.

20 Lakini kwa [a]waovu hakwenda, na miongoni mwa wasio mcha Mungu na wasiotubu ambao [b]wamejichafua wenyewe wakati wakiwa katika mwili, sauti yake haikusikika;

21 Wala waasi ambao walikataa shuhuda na maonyo ya manabii wa kale hawakuona uwepo wake, wala kuutazama uso wake.

22 Pale walipokuwa hawa,

11 *c* Isa. 11:2.
d MWM Roho.
12 *a* M&M 76:69–70.
b M&M 6:13; 51:19; 76:51–53.
13 *a* MWM Dhabihu.
b Mt. 5:10–12.
14 *a* Eth. 12:4; Moro. 7:3, 40–44. MWM Tumaini.
b MWM Ufufuko.
c MWM Neema.
d MWM Mungu, Uungu—Mungu Baba.
e MWM Mzaliwa Pekee.
15 *a* Isa. 51:11; Alma 40:12.
16 *a* Lk. 23:43; Alma 40:11–12. MWM Peponi.
b Morm. 9:13.
17 *a* 2 Ne. 9:10–13.
b Eze. 37:1–14.
c M&M 93:33–34.
d MWM Shangwe.
18 *a* Isa. 61:1. MWM Wokovu kwa ajili ya Wafu.
19 *a* M&M 76:72–74.
b MWM Injili.
c MWM Anguko la Adamu na Hawa.
d MWM Toba, Tubu.
20 *a* Alma 40:13–14. MWM Jehanamu; Ovu, Uovu.
b 1 Ne. 10:21.

[a]giza lilitawala, lakini miongoni mwa wenye haki kulikuwa na [b]amani;

23 Na watakatifu walifurahia katika [a]ukombozi wao, nao walipiga [b]magoti na kumshukuru Mwana wa Mungu kama Mkombozi na Mwokozi wao kutokana na mauti na [c]minyororo ya jehanamu.

24 Nyuso zao ziling'ara, na [a]nuru kutoka katika uwepo wa Bwana ilitulia juu yao, nao [b]wakaimba nyimbo za sifa kwa jina lake takatifu.

25 Nilistaajabia, kwani nilitambua kwamba Mwokozi alitumia kiasi cha miaka mitatu katika huduma yake miongoni mwa Wayahudi na wale walio nyumba ya Israeli, akijitahidi kuwafundisha wao injili isiyo na mwisho na kuwaita kwenye toba;

26 Na bado, licha ya matendo yake makuu, na miujiza, na tangazo la ukweli, katika [a]uwezo mkubwa na mamlaka, palikuwa na wachache tu walio isikiliza sauti yake, na kufurahia mbele zake, na kupokea wokovu kutoka kwake.

27 Lakini huduma yake miongoni mwa wale walio wafu ilikuwa fupi na ya muda [a]mchache iliyokuwa katikati ya kusulubiwa na kufufuka kwake;

28 Na niliona ajabu kwa maneno ya Petro—ambamo anasema kwamba Mwana wa Mungu alizihubiria roho zilizokuwa kifungoni, ambao wakati fulani hawakuwa watiifu, wakati uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja siku za Nuhu—na ni kwa jinsi gani iliwezekana kwake yeye kuhubiria roho zile na kufanya kazi muhimu miongoni mwao katika kipindi kifupi namna hiyo.

29 Na nilipokuwa nikistaajabu, macho yangu yakafunguliwa, na ufahamu wangu [a]ukahuishwa, nami nikatambua kwamba Bwana hakwenda kifungoni miongoni mwa waovu na wasiokuwa watiifu ambao waliukataa ukweli, kuwafundisha wao;

30 Bali tazama, kutoka miongoni mwa wenye haki, aliunda jeshi lake na akawateua wajumbe, waliovikwa [a]uwezo na mamlaka, na akawapa mamlaka ya kwenda na kupeleka nuru ya injili kwa wao ambao walikuwa [b]gizani, hata kwa roho [c]zote za wanadamu; na hivyo ndivyo injili ilivyohubiriwa kwa wafu.

31 Na wajumbe waliochaguliwa walikwenda kuitangaza siku [a]iliyokubaliwa ya Bwana na kutangaza [b]uhuru kwa wafungwa ambao walifungwa,

22 *a* MWM Giza, Kiroho.
b MWM Amani.
23 *a* MWM Mpango wa Ukombozi.
b Rum. 14:11; Mos. 27:31.
c 2 Ne. 1:13; Alma 12:11.
24 *a* Zab. 104:1–2; Isa. 60:19; Ufu. 22:5; JS—H 1:17. MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
b MWM Imba.
26 *a* 1 Ne. 11:28.
27 *a* Mk. 8:31.
29 *a* M&M 76:12.
30 *a* Lk. 24:49.
b MWM Giza, Kiroho.
c M&M 1:2.
31 *a* Isa. 61:2; Lk. 4:17–19.
b MWM Huru, Uhuru.

hata kwa wote ambao wangetubu dhambi zao na kuipokea injili.

32 Hivyo ndivyo injili ilivyo hubiriwa kwa wale ambao [a]walikufa katika dhambi zao, pasipo [b]ufahamu wa ukweli, au katika uvunjaji wa sheria, wakiwa wamewakataa manabii.

33 Hawa walifundishwa [a]imani kwa Mungu, toba ya dhambi, [b]ubatizo ufanywa kwa niaba ya wafu kwa ajili ya [c]ondoleo la dhambi, [d]kipawa cha Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono;

34 Na kanuni nyingine zote za injili ambazo zilikuwa muhimu kwao kuzijua ili kujithibitishia wenyewe kwamba waweze [a]kuhukumiwa kulingana na wanadamu katika mwili, lakini waishi kulingana na Mungu katika roho.

35 Na hivyo ilijulikana miongoni mwa wafu, wote wadogo na wakubwa, wasio na haki vile vile waaminifu, kwamba ukombozi ulitimizwa kwa njia ya [a]dhabihu ya Mwana wa Mungu juu ya [b]msalaba.

36 Hivyo ndivyo ilivyojulikana kwamba Mkombozi wetu aliutumia muda wake wakati wa kuishi kwake katika ulimwengu wa roho, akifundisha na kuziandaa roho za [a]manabii waaminifu ambao walimshuhudia yeye katika mwili;

37 Ili wao wapate kuupeleka ujumbe wa ukombozi kwa wafu wote, ambao hakuweza kuwaendea yeye mwenyewe, kwa sababu ya [a]uasi wao na uvunjaji wao wa sheria, ili wao kwa njia ya huduma ya watumishi wake wapate pia kuyasikia maneno yake.

38 Miongoni mwa wakuu na wenye nguvu waliokuwa wamekusanyika katika mkutano huu mkuu wa wenye haki walikuwa Baba [a]Adamu, Mzee wa Siku nyingi na baba wa wote,

39 Na mtukufu Mama yetu [a]Hawa, pamoja na mabinti zake wengi waaminifu ambao wameishi katika karne na wakimwabudu Mungu wa kweli na aliye hai.

40 [a]Habili, wa kwanza [b]aliyeuawa kiushahidi wa dini, alikuwepo, na kaka yake [c]Sethi, mmoja kati ya wenye nguvu, ambaye alikuwa katika [d]mfano wa baba yake, Adamu.

41 [a]Nuhu, aliyetoa tahadhari ya gharika; [b]Shemu, [c]kuhani

32 *a* Yn. 8:21–24.
b M&M 128:5. MWM Maarifa.
33 *a* M ya I 1:4. MWM Amini, Imani.
b MWM Batiza, Ubatizo—Ubatizo kwa ajili ya wafu; Ibada—Ibada zifanywazo kwa niaba ya wafu.
c MWM Ondoleo la Dhambi.
d MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
34 *a* MWM Hukumu ya mwisho.
35 *a* Alma 34:9–16. MWM Dhabihu; Lipia dhambi, Upatanisho.
b MWM Kusulubiwa; Msalaba.
36 *a* M&M 138:57.
37 *a* M&M 138:20. MWM Uasi.
38 *a* MWM Adamu.
39 *a* Musa 4:26. MWM Hawa.
40 *a* MWM Habili.
b MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.
c MWM Seti.
d Mwa. 5:3; Musa 6:10.
41 *a* MWM Nuhu, Patriaki wa Biblia.
b MWM Shemu.
c MWM Kuhani Mkuu.

aliye mkuu; [d]Ibrahimu, baba wa walio waaminifu; [e]Isaka, [f]Yakobo, na [g]Musa mtoa-sheria mkuu wa Israeli;

42 Na [a]Isaya, ambaye alitangaza kwa unabii kwamba Mkombozi alipakwa mafuta ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia [b]mateka uhuru wao, na hao waliofungwa [c]kufunguliwa kwao, pia walikuwepo hapo.

43 Zaidi ya hao, [a]Ezekieli, ambaye alionyeshwa ndotoni bonde kuu la [b]mifupa mikavu, ambayo ilikuwa ivikwe mwili, ili kuja tena katika [c]ufufuko wa wafu, kama nafsi hai;

44 [a]Danieli, ambaye aliona na kutabiri juu ya kuanzishwa kwa [b]ufalme wa Mungu katika siku za mwisho, ambao kamwe hautaharibiwa wala kutolewa kwa watu wengine;

45 [a]Elia, aliyekuwa pamoja na Musa juu ya Mlima wa [b]Kugeuka sura;

46 Na [a]Malaki, nabii aliyeshuhudia juu ya kuja kwa [b]Eliya—ambaye pia Moroni alimsema kwa Nabii Joseph Smith, akisema kwamba yeye lazima atakuja kabla ya kuja kwa [c]siku ile iliyo kuu na ya kutisha ya Bwana—pia walikuwepo pale.

47 Nabii Eliya alikuwa apande katika [a]mioyo ya watoto ahadi zilizofanywa kwa baba zao.

48 Ikionyeshwa dalili ya [a]kazi kuu itakayofanyika katika [b]mahekalu ya Bwana katika [c]kipindi cha utimilifu wa nyakati, kwa ajili ya ukombozi wa wafu, na [d]kuwafunga watoto kwa wazazi wao, isije dunia yote ikapigwa kwa laana na kuharibiwa kabisa wakati wa kuja kwake.

49 Wote hawa na wengine zaidi, hata [a]manabii walioishi miongoni mwa Wanefi na wakashuhudia juu ya kuja kwa Mwana wa Mungu, walichanganyika katika kusanyiko hili kuu na wakimsubiri kwa ajili ya ukombozi wao,

50 Kwani wafu waliotazamiwa kwa muda mrefu kutokuwepo kwa [a]roho zao kutoka kwenye miili yao kama ni [b]utumwa.

51 Hizi Bwana alizifundisha, na kuzipa [a]uwezo wa kutoka, baada ya ufufuko wake kutoka kwa wafu, ili kuingia katika ufalme wa Baba yake; ili

41 *d* Mwa. 17:1–8. MWM Ibrahimu.
e Mwa. 21:1–5. MWM Isaka.
f Mwa. 35:9–15. MWM Yakobo, Mwana wa Isaka.
g MWM Musa.
42 *a* MWM Isaya.
b Isa. 61:1–2.
c MWM Jehanamu.
43 *a* MWM Ezekieli.
b Eze. 37:1–14.
c MWM Ufufuko.
44 *a* MWM Danieli.
b Dan. 2:44–45. MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
45 *a* MWM Elia.
b MWM Kugeuka sura.
46 *a* Mal. 4:5–6; JS—H 1:36–39. MWM Malaki.
b M&M 110:13–15. MWM Eliya.
c MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
47 *a* M&M 128:17.
48 *a* MWM Wokovu kwa ajili ya Wafu.
b MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.
c MWM Kipindi.
d MWM Familia—Familia ya milele; Kufunga, Muhuri, Tia.
49 *a* Hel. 8:19–22.
50 *a* MWM Roho.
b M&M 45:17.
51 *a* 1 Kor. 6:14; Alma 40:19–21.

kuvikwa [b]kutokufa na [c]uzima wa milele.

52 Na kuendelea kutoka saa hiyo kufanya kazi zao kama ilivyoahidiwa na Bwana, na kuwa washiriki wa [a]baraka zote ambazo zilishikiliwa kwa akiba kwa ajili yao waliompenda yeye.

53 Nabii Joseph Smith, na baba yangu, Hyrum Smith, Brigham Young, John Taylor, Wilford Woodruff, na roho wengine wateule ambao [a]walihifadhiwa ili kuja katika kipindi cha utimilifu wa nyakati kushiriki katika kuweka [b]misingi ya kazi kuu ya siku za mwisho,

54 Pamoja na ujenzi wa mahekalu na utekelezaji wa ibada zake kwa ajili ya ukombozi wa [a]wafu, walikuwa pia katika ulimwengu wa roho.

55 Niligundua kwamba walikuwako pia miongoni mwa [a]wakuu na watu maarufu [b]waliochaguliwa mwanzoni kuwa watawala katika Kanisa la Mungu.

56 Hata kabla hawajazaliwa, hao, pamoja na wengine wengi, walipokea somo lao la kwanza katika ulimwengu wa roho na [a]waliandaliwa kuja katika [b]wakati ufaao wa Bwana kufanya kazi katika [c]shamba lake la mizabibu kwa ajili ya wokovu wa roho za wanadamu.

57 Niliona kwamba [a]wazee waaminifu wa kipindi hiki, wakati wakiondoka kutoka maisha katika mwili wenye kufa, huendelea na kazi zao katika kuhubiri injili ya toba na ukombozi, kupitia dhabihu ya Mwana Pekee wa Mungu, miongoni mwa wale walio [b]gizani, na chini ya utumwa wa dhambi katika ulimwengu mkuu wa roho za wafu.

58 Wafu wanaotubu [a]watakombolewa, kwa njia ya utii kwa [b]ibada za nyumba ya Mungu.

59 Na baada ya kulipia adhabu ya uvunjaji wao wa sheria, na [a]kuoshwa safi, watapokea thawabu kulingana na [b]matendo yao, kwa kuwa wao ni warithi wa wokovu.

60 Hivyo ndivyo lilivyokuwa ono la ukombozi wa wafu lililofunuliwa kwangu, na ninashuhudia, na ninajua kwamba ushuhuda huu ni wa [a]kweli, kwa njia ya baraka ya Bwana wetu na Mwokozi, Yesu Kristo, hivyo ndivyo. Amina.

51 *b* MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
c M&M 29:43. MWM Uzima wa Milele.
52 *a* Isa. 64:4; 1 Kor. 2:9; M&M 14:7.
53 *a* MWM Uteuzi kabla.
b M&M 64:33.
54 *a* MWM Ibada—Ibada zifanywazo kwa niaba ya wafu.
55 *a* Ibr. 3:22–24.
b MWM Uteuzi kabla.
56 *a* Ayu. 38:4–7; Alma 13:3–7.
b Mdo. 17:24–27.
c Yak. (KM) 6:2–3. MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
57 *a* MWM Mzee.
b MWM Jehanamu.
58 *a* MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
b MWM Ibada.
59 *a* Alma 5:17–22. MWM Samehe.
b MWM Matendo.
60 *a* MWM Ukweli.

TAMKO RASMI 1

Biblia na Kitabu cha Mormoni hufundisha kwamba ndoa kati ya mke au mme mmoja ndiyo kiwango cha ndoa kilichowekwa na Mungu isipokuwa pale Yeye anapotamka vinginevyo (ona 2 Samweli 12:7–8 na Yakobo [KM] 2:27, 30). Kufuatia ufunuo kwa Joseph Smith, kanuni ya ndoa ya wake wengi ilianzishwa miongoni mwa waumini wa Kanisa mapema katika miaka ya 1840 (ona sehemu ya 132). Kuanzia miaka ya 1860 hadi ile ya 1880, serikali ya Marekani ilipitisha sheria ya kuifanya desturi hii ya kidini kuwa kinyume cha sheria. Sheria hizi hatimaye ziliungwa mkono na Mahakama Kuu ya Marekani Baada ya kupokea ufunuo, Rais Wilford Woodruff alitoa Manifesto ifuatayo, ambayo ilikubalika na Kanisa kama mamlaka sahihi na ya kutiiwa mnamo 6 Oktoba 1890. Na hii ilisababisha kukoma kwa desturi ya ndoa za wake wengi katika Kanisa.

Kwa Yeyote Anayehusika:

Taarifa ya habari iliyotumwa kwa madhumuni ya kisiasa, kutoka Jiji la Salt Lake, ambayo imechapishwa sehemu nyingi, ikionyesha kwamba Tume ya Utah, katika taarifa yake ya hivi karibuni kwa Katibu wa Mambo ya Ndani, inadai kwamba ndoa za mitala bado zinafungishwa na kwamba ndoa arobaini au zaidi zimefungwa hapa Utah kutoka Juni iliyopita au wakati wa mwaka jana, pia kwamba katika mahubiri ya hadhara viongozi wa Kanisa wamefundisha, kuchochea na kuhimiza uendelezaji wa tabia ya mitala—

Kwa hiyo, mimi, kama Rais wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, kwa heshima na taadhima, ninatamka kwamba madai haya ni ya uongo. Sisi hatufundishi mitala au ndoa za wake wengi, au kumruhusu mtu yeyote kuingia katika kutenda hayo, na ninakana kwamba ndoa arobaini au idadi yoyote ya ndoa za wake wengi hazijawahi kufungishwa katika Mahekalu yetu kwa kipindi hicho au mahali pengine popote katika Eneo hili.

Jambo moja limearifiwa, ambalo wahusika wanadai kwamba ndoa ilifungwa katika Nyumba ya Endaomenti, katika Jiji la Salt Lake, wakati wa majira ya kuchipua ya 1889, lakini sijaweza kumjua aliyefungisha hiyo; lolote lililofanyika katika jambo hili lilikuwa pasipo kujua kwangu. Kama matokeo ya madai haya Nyumba ya Endaomenti, kwa maelekezo yangu, imebomolewa mara moja.

Kwa vile sheria zimekwishatungwa na Bunge zikikataza ndoa za wake wengi, sheria ambazo zimetangazwa kikatiba na mahakama iliyo kimbilio la mwisho, ninatangaza madhumuni yangu

ya kuwa mtiifu kwa sheria hizo, na kutumia uwezo wangu juu ya waumini wa Kanisa ambao ninawaongoza kufanya hivyo hivyo.

Hakuna lolote katika mafundisho yangu kwa Kanisa au katika yale ya wenzangu, kwa kipindi hicho kilichotajwa, ambayo yanaweza kutafsiriwa kuwa yanafundishwa au kuhimiza mitala; na wakati Mzee yeyote wa Kanisa alipotumia lugha ambayo ilionekana kuelezea mafundisho yoyote ya aina hiyo, amekemewa mara moja. Na sasa ninatangaza hadharani kwamba ushauri wangu kwa Watakatifu wa Siku za Mwisho ni kuacha kufunga ndoa yoyote iliyokatazwa na sheria ya nchi.

Wilford Woodruff
Rais wa Kanisa la Yesu Kristo
la Watakatifu wa Siku za Mwisho.

Rais Lorenzo Snow alisema yafuatayo:

"Ninapendekeza, tukimtambua Wilford Woodruff kama Rais wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, na mtu pekee duniani kwa wakati huu ambaye anashikilia funguo za ibada za kuunganisha, tunatambua kwamba anayo mamlaka kamili kutokana na nafasi yake kutoa Manifesto ambayo imesomwa nasi tumeisikia, na ambayo imetolewa tarehe 24 Septemba 1890, na kwamba kama Kanisa katika Mkutano Mkuu tuliokusanyika, kwamba tunalikubali tamko lake juu ya ndoa ya mke mmoja kuwa ni rasmi na hatuna budi kulitii."

Jiji la Salt Lake, Utah, 6 Oktoba 1890.

DONDOO KUTOKA HOTUBA TATU ZA RAIS WILFORD WOODRUFF JUU YA MANIFESTO

Bwana hataniruhusu mimi au mtu mwingine yoyote asimamaye kama Rais wa Kanisa kuwaongoza ninyi vibaya. Haipo katika mpangilio. Haipo katika mawazo ya Mungu. Kama ningejaribu hilo, Bwana angeniondoa katika nafasi yangu, na hivyo atamfanya mtu yeyote atakaye jaribu kuwaongoza wanadamu nje ya ufunuo wa Mungu na kutoka kwenye wajibu wao. (Mkutano Mkuu wa Nusu Mwaka Sitini na Moja wa Kanisa, Jumatatu, 6 Oktoba 1890, Jiji la Salt Lake, Utah. Ulioripotiwa na *Deseret Evening News,* 11 Oktoba 1890, uk. 2.)

Si muhimu nani anaishi au nani anakufa, au nani anaitwa kuliongoza Kanisa hili, wanalazimika kuliongoza kwa mwongozo wa Mwenyezi Mungu. Kama hawafanyi kwa njia hiyo, hawawezi kufanya kwa njia nyingine yoyote. . . .

Nimepata mafunuo kadhaa hivi karibuni, na ya muhimu sana kwangu, nayo

nitawaambia kile Bwana alichoniambia. Wacha niyarejeshe mawazo yenu katika hiki kitu kinachoitwa Manifesto. . . .

Bwana ameniambia niwaulize Watakatifu wa Siku za Mwisho swali, pia akaniambia kama watasikiliza kile nilichowaambia na kujibu swali lililoulizwa kwao, kwa Roho na kwa uwezo wa Mungu, wote watajibu sawa sawa, na wote wataamini sawa sawa juu ya jambo hili.

Swali ni hili: Njia ipi iliyo ya busara zaidi kwa Watakatifu wa Siku za Mwisho kuifuata—kuendelea kujaribu kufunga ndoa za wake wengi, licha ya sheria za taifa dhidi yake na upinzani wa watu milioni sitini, na kwa gharama ya utaifishaji na upotevu wa Mahekalu yote, na kusimamishwa kwa ibada zake zote, za wote walio hai na wafu, na kufungwa gerezani kwa Urais wa Kwanza na Mitume Kumi na Wawili na viongozi wa familia katika Kanisa, na kutaifishwa kwa mali za watu binafsi (hivi vyote peke yake vinaweza kusimamisha tabia hiyo); au, baada ya kufanya na kuteseka haya tuliyoteseka kupitia kujitoa kwetu kwa kanuni hii kuacha kanuni hii na kutii sheria, na kwa kufanya hivyo tutawaacha Manabii, Mitume na akina baba majumbani, ili waweze kuwafundisha watu na kutimiza wajibu wao kwa Kanisa, na kuyaacha Mahekalu mikononi mwa Watakatifu, ili waweze kutekeleza ibada za injili, wote kwa ajili ya walio hai na wafu?

Bwana alinionyesha kwa ono na ufunuo hasa yatakayotokea kama hatungekomesha desturi hii. Kama hatungeikomesha msingeliweza kuwatumia . . . mtu yeyote katika hekalu hili la Logan; kwani ibada zote zingelikoma nchi yote ya Sayuni. Vurugu ingetawala nchi yote ya Israeli, na watu wengi wangefanywa kuwa wafungwa. Taabu hii ingekuja juu ya Kanisa lote, na tungelilazimika kukomesha desturi hii. Sasa, swali ni hili, je, ikomeshwe kwa jinsi hii, au katika njia ambayo Bwana ameionyesha kwetu, na kuwaacha Manabii wetu na Mitume na akina baba kuwa huru, na mahekalu kuwa mikononi mwa watu, ili wafu wapate kukombolewa. Idadi kubwa tayari imekwisha kukombolewa kutoka kifungoni katika ulimwengu wa roho na watu hawa, na kazi iendelee au isimame? Hili ndilo swali ninaloliweka mbele ya Watakatifu wa Siku za Mwisho. Yawapasa kuamua ninyi wenyewe. Ninakutakeni mjibu wenyewe. Mimi sitajibu; lakini ninakuambieni kwamba hii ndiyo hali halisi ambayo sisi watu tungelikuwa nayo kama tusingechukua hatua tulizochukua.

. . . Nimeona hasa kile ambacho kitakuja kuwa kama pasingefanyika chochote. Nimekuwa na roho hii juu yangu kwa muda mrefu. Lakini nataka kusema hili: Ningeweza kuyaachia mahekalu yote kutoka mikononi mwetu; ningelikwenda gerezani mimi mwenyewe, na kumwacha kila mwanaume kwenda huko, kama Mungu wa mbinguni asingeliniamuru kufanya haya niliyoyafanya; na wakati saa ilipofika ambayo niliamriwa kufanya hilo, yote ilikuwa wazi kwangu. Nilikwenda mbele za Bwana, na nikaandika kile Bwana alichoniambia kuandika. . . .

Ninawaachia hili, kwa ajili ya kulitazama na kutafakari. Bwana yupo kazini pamoja nasi. (Mkutano wa Kigingi cha Cache, Logan, Utah, Jumapili ya 1 Novemba 1891. Iliandikwa katika *Deseret Weekly,* 14 Novemba 1891.)

Sasa nitawaambia kilichofunuliwa kwangu na kile Mwana wa Mungu alichokifanya, katika jambo hili. . . . Mambo haya yote yangelitokea, kama vile Mungu Mwenyezi aishivyo, kama Manifesto ile isingelitolewa. Kwa hiyo, Mwana wa Mungu alielekeza mambo haya yatolewe kwa kanisa na kwa ulimwengu kwa madhumuni yaliyoko akilini mwake. Bwana ameazimia kuistawisha Sayuni. Ameazimia kumalizika kwa hekalu hili. Ameazimia kwamba wokovu wa walio hai na wafu lazima utolewe katika mabonde haya ya milima. Na Mwenyezi Mungu alitangaza kwamba Ibilisi hataizuia. Kama mnaweza kuelewa hilo, huo ndiyo ufunguo wake. (Kutoka katika mafundisho ya kipindi cha sita cha ibada ya

kuwekwa Wakfu kwa Hekalu la Salt Lake, Aprili 1893. Muswada uliopigwa chapa wa Ibada ya kuweka Wakfu. Hifadhi ya Nyaraka, Idara ya Historia ya Kanisa, katika Mji Salt Lake, Utah.)

TAMKO RASMI 2

Kitabu cha Mormoni kinafundisha kwamba "watu wote ni sawa kwa Mungu," ikijumuisha "weusi na weupe, watumwa na huru, wanaume na wanawake" (2 Nefi 26:33). Katika historia yote ya Kanisa, watu wa kila asili na kabila katika nchi nyingi wamebatizwa na wameishi kama waumini waaminifu wa Kanisa. Katika kipindi cha uhai wa Joseph Smith, wanaume weusi wachache waliokuwa waumini wa Kanisa walikuwa wametawazwa katika ukuhani. Mapema katika historia yake, viongozi wa Kanisa walisimamisha kutunuku ukuhani kwa wanaume weusi wenye asili ya Kiafrika. Kumbukumbu hazitoi taarifa kamili juu ya chanzo cha desturi hii. Viongozi wa Kanisa waliamini kwamba ufunuo kutoka kwa Mungu ulihitajika ili kubadilisha desturi hii na kwa maombi walitafuta mwongozo. Ufunuo ulikuja kwa Rais wa Kanisa Spencer W. Kimball na kuthibitishwa na viongozi wengine wa Kanisa katika Hekalu la Salt Lake 1 Juni 1978. Ufunuo uliondoa masharti yoyote yaliyohusishwa na asili ya mtu ambayo wakati fulani yalitumika kwenye ukuhani.

Kwa Yeyote Anayehusika

Mnamo 30 Septemba 1978, wakati wa Mkutano Mkuu wa 148 wa Nusu Mwaka wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, yafuatayo yalitolewa na Rais N. Eldon Tanner, Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza wa Kanisa:

Mwanzoni mwa mwezi Juni ya mwaka huu, Urais wa Kwanza ulitangaza kwamba ufunuo ulikuwa umepokelewa na Rais Spencer W. Kimball wa kutoa ukuhani na baraka za hekaluni kwa wanaume wote walio waumini wa Kanisa. Rais Kimball ameniomba kwamba niueleze mkutano kwamba baada ya kupokea ufunuo huu, ambao ulikuja kwake baada ya tafakari na sala ndani ya vyumba vitakatifu vya hekalu takatifu, aliupeleka kwa washauri wake, ambao waliupokea na kuupitisha. Ndipo baadaye ukafikishwa kwa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, ambao kwa kauli moja waliupitisha, na mwishowe ukapelekwa kwa Viongozi Wakuu wengine wote, ambao nao vile vile waliupitisha kwa kauli moja.

Rais Kimball ameniomba kuwa sasa niisome barua hii:

8 Juni 1978
Kwa viongozi wakuu wote na maofisa wa ukuhani wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho ulimwenguni kote:

Ndugu zangu Wapendwa:

Kama vile tunavyoshuhudia kupanuka kwa kazi ya Bwana duniani, tunashukuru kwamba watu wa mataifa mengi wameitikia ujumbe wa injili ya urejesho, na wamejiunga na Kanisa kwa idadi inayoongezeka daima. Hili, matokeo yake, limetusukuma sisi kuwa na hamu ya kutoa kwa kila muumini mwenye kustahili haki na baraka zote ambazo injili hutoa.

Tukiwa tunafahamu ahadi zilizofanywa na manabii na marais wa Kanisa waliotutangulia sisi kwamba kwa wakati fulani, katika mpango wa milele wa Mungu, ndugu zetu wote wenye kustahili wanaweza kupokea ukuhani, na tukiwa tunashuhudia uaminifu wa wale ambao ukuhani umekataliwa, tumeomba kwa dhati na kwa muda mrefu kwa niaba yao hawa, ndugu zetu waaminifu, tukitumia masaa mengi katika Chumba cha Orofani cha Hekalu tukimwambia Bwana atupe mwongozo mtakatifu.

Amesikia sala zetu, na kwa ufunuo amethibitisha kwamba siku iliyokuwa ikisubiriwa kwa muda mrefu imefika ambapo kila mwanamume, aliye mwaminifu katika Kanisa apate kupokea ukuhani mtakatifu, pamoja na uwezo wa kutumia mamlaka yake matakatifu, na kufurahia pamoja na wapenzi wake kila baraka itiririkayo kutoka huko, pamoja na baraka za hekalu. Kwa hiyo, wanaume wote wenye kustahili walio waumini wa Kanisa wanaweza kutawazwa kwenye ukuhani bila kujali asili au rangi. Viongozi wa ukuhani wanaelekezwa kufuata sera ya kuwatahini kwa uangalifu wote waliopendekezwa kutawazwa au kwenye ukuhani wa Haruni au ukuhani wa Melkizedek ili kuhakikisha kwamba wanatimiza viwango vya ustahili vilivyowekwa.

Tunatamka kwa dhati kwamba Bwana ametujulisha mapenzi yake kwa ajili ya baraka kwa watoto wake wote duniani kote ambao wataisikia sauti ya watumishi wake wenye mamlaka, na kujitayarisha wenyewe kupokea kila baraka ya injili.

Wenu waaminifu,

Spencer W. Kimball
N. Eldon Tanner
Marion G. Romney

Urais wa Kwanza

Kwa kuwa tunamtambua Spencer W. Kimball kama nabii, mwonaji, na mfunuzi, na rais wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, inapendekezwa kwamba sisi kama kusanyiko la kikatiba kuukubali ufunuo huu kama ndilo neno na mapenzi ya Bwana. Wote wanaokubali tafadhali waonyeshe ishara kwa kunyosha mkono wako wa kulia. Yeyote anayepinga kwa ishara hiyo hiyo.

"Kura ya kuunga mkono hoja ilikubaliwa na wote na kwa kauli moja."

Jiji la Salt Lake, Utah, 30 Septemba 1978.